


Ellen G. White Estate

PAMBANO KUU



ELLEN G. WHITE

Pambano Kuu

Ellen G. White

**Copyright © 2021
Ellen G. White Estate, Inc.**

Information about this Book

Overview

This eBook is provided by the [Ellen G. White Estate](#). It is included in the larger free [Online Books](#) collection on the Ellen G. White Estate Web site.

About the Author

Ellen G. White (1827-1915) is considered the most widely translated American author, her works having been published in more than 160 languages. She wrote more than 100,000 pages on a wide variety of spiritual and practical topics. Guided by the Holy Spirit, she exalted Jesus and pointed to the Scriptures as the basis of one's faith.

Further Links

[A Brief Biography of Ellen G. White](#)
[About the Ellen G. White Estate](#)

End User License Agreement

The viewing, printing or downloading of this book grants you only a limited, nonexclusive and nontransferable license for use solely by you for your own personal use. This license does not permit republication, distribution, assignment, sublicense, sale, preparation of derivative works, or other use. Any unauthorized use of this book terminates the license granted hereby. (See [EGW Writings End User License Agreement](#).)

Further Information

For more information about the author, publishers, or how you can support this service, please contact the Ellen G. White Estate

at mail@whiteestate.org. We are thankful for your interest and feedback and wish you God's blessing as you read.

Contents

Information about this Book	i
Kwa Nini Huna Budi Ukisome Kitabu Hiki	12
Utangulizi	14
Kufunua Kifuniko Ili Kuona Mambo Yajayo*	14
1 Utabiri wa Ajali ya Ulimwengu	21
Hekalu Maarufu Kuangamia	23
Uvumilivu Wa Mungu	25
Ishara ya Maangamizo	26
2/Wakristo wa Kwanza Waaminifu wa Kweli	30
Makundi Mawili Kanisani	31
3/Giza la Kiroho Katika Kanisa la Kwanza	35
Jinsi Sabato “Iliyobadilishwa”	36
Siku Za Hatari Kwa Kanisa	38
Jinsi Mafundisho ya Uongo Yalivyoingia	40
4/Waldenses Waitetea Imani	43
Roma Yakutana na Dini ya Biblia	44
Kanuni za Kweli Zilithaminiwa	46
Vijana Walifundishwa Kuwa Wahubiri	47
Wenye Dhambi Kutazamishwa Kwa Kristo	48
Kushambulia Ufalme wa Shetani	49
Rumi Yaazimu Kuwaadhibu Waldenses	50
5/Nuru Yapambazuka Uingereza	52
Mwepesi Kugundua Kosa	53
Alishikwa na Ugonjwa wa Hatari	55
Wycliffe Akataa Kukana Imani	57
Ujumbe wa mwanzo Mpya	58
6/Mashujaa Wawili Wakabili Mauti	61
Picha mbili Zilimvutia Huss	62
Prague Iliwekwa Chini ya Karantini	62
Mlinzi Toka kwa Mfalme	64
Ushindi Unaonekana Kwa Njozi	66
Huss Achomwa Moto Mtini	67
Jerome Asalimu Amri Mahakamani	68
Jerome Atubu na Kuwa na Ujasiri	69

Apangiwa Kufungwa na Kuuawa	70
Walisalitiwa Kijanja	72
7\Luther, Shujaa Kwa Wakati Wake	74
Amani na Mungu	75
Ukweli Juu ya Ngazi ya Pilato.	76
Uuzaji wa Msamaha	77
Kazi ya Luther Yaanza	79
Luther Asimama Na Biblia Tu	80
Kuponyoka Kutoka Augsburg	83
Hatari Kuu	85
8/Jasiri wa Kweli	88
Luther Ashitakiwa Kuwa Mzushi	89
Luther Atakiwa Ahudhurie.	90
Ujasiri wa Mfia Dini	91
Luther Asimama Barazani	93
Luther Mbele ya Baraza Tena	94
Luther Alindwa Hatarini.	97
Juhudi ya Kumpatanisha na Roma	98
Mungu amtumia Frederick Saxony	100
Usalama Huko Wartburg	101
9/Nuru YawashwaUswisi	103
Zwingli Aitwa Kwenda Zurich	105
Uuzaji wa Vyeti Vya Msamaha Huko Uswiss	106
Mabishano Pamoja na Roma	107
10/Maendeleo Katika Ujerumani	110
Matunda ya Mafunzo Yadhihirika	111
Uwezo Wa Neno	112
Maumivu Ya Roho Yaliwekwa Juu ya Luther	113
Mafunzo ya Biblia Po Pote.	115
11/Wakuu Wakataa	117
Jambo Kubwa Hatarini	118
Msimamo Bora wa Wakuu	119
Baraza la Augsburg	120
12/Kwapambazuka Ufaransa	124
Agano Jipya La Kifaransa	126
Berquin Shujaa	127
Berquin Achomwa Moto	128
Mwito wa Calvin.	128

Mashahidi Katika Kuchomwa Moto	129
Utawala wa Hofu Kuu	131
Uchapaji Watangazwa Kuondolewa	132
Forement, Mwalimu	135
Ngurumo za Laana	135
Ushindi wa Matengenezo	136
13/Huko Uholanzi	138
Matengenezo Katika Denmark	140
Maendeleo Katika Swideni	141
14/Ukweli Unaendelea Uingereza	143
Tyndale Atafsiri Agano Jipya Kwa Kiingereza	144
Usahihi Wa Uwezo Wa Maandiko	145
John Knox	145
Maelfu Ya Wachungaji Walifukuzwa	147
Kuhesabiwa Haki Kwa Imani	147
Roho ya Wesley Ilichangamka Kiajabu	149
Wesley Aponyoka Kifo	150
Katika Kuitetea Sheria Ya Mungu	151
Umoja Wa Sheria Na Injili	152
15/Utawala Wa Ufaransa Wa Kitisho: Ukweli Wake	154
Ajabu Ya Utimizo wa Unabii	156
Uadui Dhidi Ya Kristo	156
Maasi Makuu Ya Kutisha.	157
Makufuru ya Ukaidi	159
Mungu Hoja	159
Jinsi Ingalipasa Kuwa	161
Matokeo ya Kuvuna Damuni	162
Kosa Baya Kuliko Yote	164
16/Kutafuta Uhuru Katika Nchi Mpya	167
Mungu Alitawala Mambo	168
Roger Williams	169
Mkataba wa Uhuru.	170
Ukuu wa kweli wa Usalama wa Taifa.	171
17/Ahadi Za Kurudi Kwa Kristo	173
Tetemeko Lililotikisa Ulimwengu	175
Jua Mwezi Kutiwa Giza	176
Mwezi Kama Damu	177
Mwito Wa Kuamka	178

Ujumbe Ulitolewa na Wanyenyekevu	179
18/Nuru Mpya Katika Ulimwengu Mpya.	183
Miller Apata Rafiki	184
Kuja Kwa Kristo Waziwazi	185
Maandiko na utaratibu wa Kuhesabu	186
Kugundua Musa wa Unabii.....	187
Nyakati Mbili Kuanza Pamoja	188
Injili kwa Ulimwengu	188
Mwisho wa Kushangaza	189
“Nenda Uyatangaze Ulimwenguni”	190
Nyota Zaanguka	191
Utabiri Ulitimia	192
Kupendezwa na Kutokuamini	193
Wakaidi na Wasioamini	194
19/Kwa Nini Uchungu Mkuu?	197
Wakati Umetimia	198
Kufa Moyo Hadi Ushindi	200
Ujumbe wa wanafunzi Ulifanana na wa 1844	200
20/Upendo kwa Kurudi Kwake Yesu	203
Mwamko kwa Nchi Mbalimbali Wakati Ule Ule	204
Kinyume cha Tafisi Nyingine	205
Uwezo Kitabuni	205
Ujumbe wa Marejeo Huko Uingereza	206
Aliyofunuliwa Bengel	207
Wahubiri Watoto wa Scandinavia	208
Ujumbe Ulienea.	209
Andiko Rahisi Huleta Uthibitisho	210
Ujumbe Ulipangwa	210
21/Kuvuna Upepo wa Kimbunga	213
Kukataa Nuru kwa Mwanadamu	214
Ujumbe Wa Malaika Wa Kwanza	214
Ujumbe Wa Malaika Wa Pili	216
Uasherati wa Kiroho	216
Umoja wa Ulimwengu	217
Upotovu wa Kwanza Kutoka Katika Ukweli wa Injili	218
22/Unabii Ulitimia	220
Ukakamavu Kidini Waonekana.	222
Makosa Yalisahihishwa.	223

Kilio Cha Usiku Wa Manane	224
Uchungu Tena	225
Ujumbe Ulitolewa Kwa Wakati Hasa.	226
Imani Ilidumishwa	227
23/Kufunua Siri ya Patakatifu	228
Patakatifu Pa Patakatifu Mno.	229
Vyumba Viwili.	230
Siri ya Hema Takatifu Yadhihirika	232
Kutakaswa kwa Patakatifu	232
Siku Kuu ya Upatanisho	233
Ukweli wa Mbinguni	234
Kazi ya Hukumu	235
24/Kristo Anafanya nini Sasa?	237
Nani Atasimama?	238
“Haya Bwana Arusi Yuaja”	238
Kumngojea Bwana Wao.	239
Kufunga kazi Katika Patakatifu	239
25/Sheria ya Mungu Haibadiliki	242
Mwito Kumwabudu Mwumbaji	244
Uthibitisho wa Joka	244
Kuinuka kwa Uwezo Mpya	245
Tofauti ya Ajabu	247
Lakini Sanamu kwa Mnyama Ni Nini? Ilitendekaje?	247
Mnyama na Sanamu Yake	249
Kimya Kabisa Katika Agano Jipya	250
Onyo la Malaika wa Tatu	251
26/Mashujaa wa Kutetea Kweli	253
Sabato ya Kweli Ilishikwa Daima	254
Siyo Mapenzi ya Mungu	255
27/Uamsho wa Kisasa Unafauluje?	257
Sheria ya Uhuru.	259
Thibitisho la Dhambi	260
Utakaso ni Nini?	261
Ni kweli Imani Peke Yake	261
Utakaso wa Biblia	263
28/Kukubalika Kumbukumbu ya Maisha yetu.	266
Makusudi ya Siri	267
Kanuni ya Hukumu	268

Bwana Amkeme Shetani	269
Kufutwa Kabisa kwa Dhambi	270
Kwa Wakati ulioamriwa.	270
Ubinafsi wa Siri Wadhihirika	271
Uombezi wa Kristo	272
Mambo ya Wote Yamekatwa	273
29/Kwa nini Dhambi Iliruhusiwa?	274
Kutoridhika Miongoni Mwa Malaika	276
Kufukuzwa Mbinguni	278
Hoja kwa Ajili ya Mwanadamu	279
30/Shetani na Mwanadamu Vitani	281
Adui Mwangalifu	282
31/Roho Chafu	284
Malaika Walinzi	285
32/Jinsi ya Kumshinda Shetani	288
Ukweli Hutakasa	289
Biblia Nzima ni Kiongozi	290
Kweli Ilikataliwa kwa Kuwa Huhusu Msalaba.	291
Makosa ya hatari	291
Vionyesho Vya Neno	292
Ushahidi Utoshao	292
33/Baada ya Kufa Kuna Nini?	295
Uwongo Mkuu	296
Uzushi Kuhusu Mateso ya Milele.	297
Wokovu wa Jumla Maandiko Hayausemi.	298
Masharti Yamewekwa	299
Hawako Tayari Kuingia Mbinguni	300
Mshahara wa Dhambi	301
Ufufuo wa Kwanza	301
34/Mizimu ni Nani Katika Imani ya Roho	305
Mwito wa Shetani Wenye Akili	306
Mwito Kwa Wapenda Anasa	307
Biblia Huhesabiwa Kama Hadithi	308
35/Uhuru wa Dhamiri Unatishwa	311
Mapatano na Kuridhiana	312
Mfanano wa Kushangaza	313
Mwungano wa Umizimu na Ukristo	314
Badilio katika Uprotestanti	315

Utunzaji wa Jumapili	316
Adhabu Kali	317
Mnyama Mwenye Pembe Mbili Kama Kondoo	318
36/Mapambano Yaliyo Karibu Sana	321
Kuweka Kando Sheria ya Mungu	322
Ulevi umewafumba Wengi	322
37/Usalama Wetu wa Pekee	327
Kutukuza mamlaka ya Kibinadamu	328
Wajibu wa Kwanza wa Mkuu	329
Matokeo ya Kutosoma Biblia na Kuomba.	330
38/Ujumbe wa Mungu wa Mwisho	332
Jaribu Kuu la uaminifu	333
Tufani yakaribia	335
Upinzani Kufikia Kikomo Kipya	335
Mvua ya Masika na Kilio Kikuu	336
39/Wakati wa Taabu	338
Wakati wa Taabu ya Yakobo	339
Uchungu Kwamba Mungu Alaumiwe.	341
Dhambi Zilifutwa	341
Imani Idumuyo	342
Tendo la Kutawazwa	343
Watu wa Mungu hawapotoshwi	344
Makundi ya Malaika Walinzi	346
40/Watu wa Mungu Wakombolewa	349
Siku ya Bwana	351
Mfalme wa Wafalme Atokea	352
Mpaka Mji Mtakatifu.	354
Adamu Wawili Wakutana	355
Waliokombolewa Katika Utukufu	356
41/Dunia Katika Maangamizi	359
Malaika wa Mauti	360
Kifungu cha Shetani	361
42/Amani ya Milele Mwisho wa Mapambano	364
Shambulio la Mwisho Juu ya Mungu	365
Waasi watamkiwa Hukumu	366
Shetani Ashindwa	368
Mwisho Mbaya wa Waovu	369
Ukumbusho wa Kusulubiwa	370

Ushindi wa Pendo la Mungu 372

Kwa Nini Huna Budi Ukisome Kitabu Hiki

Kwa mamilioni ya watu maisha kwao hayana maana yoyote na huonekana kama upuuzi. Elimu ya Sayansi na ya ufundi wote, Elimu ya Filosofia hata ya mambo ya dini imemdhahirisha binadamu kama kiumbe aliyetokea kwa bahati tu. Walakini, kwa kusudi watu wake wanaona kwamba ni vigumu kukubali kuishi maisha ya ubatili. Ujeuri, ukaidi na uasi, kujaribisha madawa haya yote, kwa ujumla huonyesha upumbavu wa watu wanaoshindana na hali ya kutisha ya upotevu. Sawa kama mtoto yatima wanalia katika hali ya kukata tamaa, wakisema Mimi ni nani? Wazazi wangu walikuwa akina nani? Nitawapateje?

Wengi hugeukia Sayansi ili wapate jawabu; hugeukia kwamba huuliza, Je, kuna mtu yeyote huko anayenifahamu ambaye anani-angalia? Lakini Sayansi haina jawabu. Sayansi imewekwa kuuliza tu maswali, chembechembe hufanyikaje? Hutawanyikaje? Mawazo yetu hufanyaje kazi? Ulimwengu umefanyikaje?

Sayansi haiwezi kutueleza sababu za kuwako chembe ndogo, au kwa nini biandamu anaishi, au kwa nini ulimwengu uliumbwa. Wala haiawezi kujibu maswali muhimu ya watu wenye hekima ya dunia.

Kama kuna maana na haki ulilmwnguni kwa nini mwenye haki hutaabika pamoja na mwovu? Je, kuna maisha baada ya kufa? Je, nafsi ya mtu huishi milele? Je, makanisa ya kikristo ya leo kwa kweli humtetea Mungu? Ukweli ni nini?

Hali ya ulimwengu wa baadaye ni nini? Je ulimwengu utakwisha kwa hali ya kitoto kutaabika kupata hewa ya mwisho katika machafuko ya hewa au utamalizwa na kombora kubwa lililotupwa kutoka katika chombo? Au mwanadamu ambaye tangu mwanzo hakuweza kuonesha uwezo wowote wa kujitawala asiwe mtu wa kuacha ubinafsi ghafla atokee kukomesha maovu, vita umaskini na kifo?

[ii] Kitabu hiki kinatoa majibu ya hakika. Maisha yanaumuhimu! Sisi sio peke yetu ulimwenguni. Yuko mtunzaji! Kwa kweli yuko

anayejiishughulisha na mambo ya binadamu, ambaye alijiunga na jamii yetu ili tuweze kupitia kwake na yeye kwetu. Yuko ambaye mkono wake hodari hutunza sayari yetu ambaye ataongoza na kufikisha mahali pa usalama tena karibuni.

Lakini zamani za miaka iliyopita adui mwenye kushawishi alikusudia kuinyakua dunia yetu na kuitawala na kuuharibu mpango bora wa Mungu wa amani na furaha kwa jamaa nzima ya binadamu. Maelezo ya hali ya ulimwengu yameitaja hatari hii isiyoonekana ya uwezo ulio tayari kuuharibu ulimwengu wetu. Katika onekano la kibinadamu ukafiri na hali ya makanisa vimeungana pamoja na kuwa katika hatia.

Kitabu hiki kitaweza kuchapishwa na kutawanywa tu pale palipo na uhuru wa dini, maana kinatoboa wazi makosa katika siku zetu. Kinaeleza sababu zilizofanya matengenezo ya kanisa yakahitajika na kwa nini yalisimamishwa. Kinatoa kisa cha kusikitisha cha makanisa yaliyoanguka, na muungano wa kikatili wenye kutesa watu na kuinua kwa ushirikiano wa kanisa na serikali ambao utafanya sehemu yake ya ukatili kabla ya kumalizika kwa mshindano makuu kati ya uovu na wema. Katika mapambano haya kila mwanadamu atahusika.

Mwandishi anaandika mambo ambayo hayajatukia wakati wa uhai wake, lakini hayana budu kutukia. Anasema kwa hakika mambo ya kustusha. Mambo ya mapambano haya ni mazito mno kiasi cha kutaka mtu ayatangaze ili kuonya watu.

Hakuna msomaji atakayesoma mambo haya bila kushanga na kutaka kuyachunguza zaidi, na kuwa ilikuwa zaidi bahati yake kuyapata.

Watengenezaji.

Utangulizi

Kufunua Kifuniko Ili Kuona Mambo Yajayo*

Kabla dhambi haijaingia ulimwenguni Adamu alifurahia maongezi pamoja na Muumba wake; lakini tangu watu walipojitenga wenyewe na Mungu wao kwa ajili ya uasi wanadamu wamekatwa kabisa na uhusiano wao umevunjika. Walakini kwa njia ya mpango wa wokovu njia imefunguliwa tena ambayo itawarudisha wanadamu katika ushirikiano na mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kawa njia ya Roho Wake, na nuru ya Mungu imetolewa ulimwenguni kwa ajili ya ufunuo kwa watumishi waliochaguliwa: “Watakatifu wa Mungu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu” 2Petro 1:21.

Katika muda wa miaka 2500 ya kwanza ya historia ya wanadamu hapakuwako na maandiko yo yote yaliyofunuliwa. Wale waliofundishwa na Mungu walipitisha elimu hiyo kwa wengine, na ikapitishwa vivyo hivyo toka kwa baba mpaka kwa mwana kufuatana na vizazi. Matayarisho ya kutumia maandiko yalianzia kwa wakati wa Musa. Maandiko matakatifu yaliunganishwa pamoja katika kitabu kitakatifu. Kazi hii iliendelea muda mrefu wa miaka 1600 — tangu Musa aliyeandika historia ya uumbaji na sheria, mpaka Yohana, mwandishi wa kweli tukufu za Injili.

Biblia inamtaja Mungu kuwa mwandishi wake, lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu, na kwa namna mbalimbali katika vitabu vyake huonesha tabia ya waandishi. Ukweli ulioandikwa humo wote una “Pumzi ya Mungu” (2Tim. 3:16) Lakini ukweli wote unaelezwa katika lugha ya kibinadamu, yaani maneno ya watu. Mungu Mwenyenzi kwa njia ya roho Mtakatifu aliwavuvia watumishi wake katika mawazo yao na katika mioyo yao. Aliwapa ndoto na njozi, na mifano na tarakimu, na wote waliopewa mambo hayo waliyakusanya wakayandika kwa kutumia maneno ya lugha ya kibinadamu.

Vitabu vya Biblia vilivyoandikwa nyakati mbalimbali na watu tofauti tofauti hali zote, na kwa kazi mbalimbali, huleta haki pana

sana na aina ya uandishi tofauti lakini ujumbe ule ule. Kwa mtu mzembe ambaye anasoma juu juu tu huonekana kwamba Biblia inajipinga yenyewe, lakini kwa msomaji makini ataona kuwa Biblia haipingani hata kidogo.

Kwa jinsi ilivyoandikwa na waandishi wetu mbalimbali kweli imeletwa kwa aina mbalimbali. Mwandishi mmoja anakazia hasa jambo fulani, hushikilia viini vinavyohusiana na uzoefu wake na mwingine anasisitizia jambo jingine, na kila mmoja kwa kuongozwa na roho mtakatifu ujumbe wao wauletao huwafaa watu wa hali zote.

Mungu anapenda kwamba ukweli wake utangazwe ulimwengu kwa njia ya wanadamu, na yeye Mwenyewe amewawezesha kufanya kazi hii kwa Roho Wake Mtakatifu. Aliwaongoza mawazo yao yapi ya kusema na yapi ya kuandika. Ujumbe wa thamani umekabidhiwa kwa vyombo vya duniani, lakini ni ujumbe wa mbinguni, na kweli iliyofunuliwa huunganishwa na kukamilika ili kufaa mahitaji ya wanadamu katika hali zote za maisha yao. Maneno ya ushuhuda hutolewa katika hali zote za maisha yao. Maneno ya ushuhuda hutolea katika lugha hafifu ya binadamu, lakini ni ushuhuda wa Mungu na wenye kuuamini ataona uwezo wa Mungu ndani yake umejaa neema na kweli. Katika neno lake Mungu ametoa mambo yote ya lazima kwa wokovu wa wanadamu. Maandiko matakatifu budi yapokelewe kama mwongozo halisi wa ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Maandiko Matakatifu ndiyo kipimo kamili cha tabia na mafundisho.

[iv]

“Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” 2Tim. 3:16-17.

Lakini alipokuwa Mungu amemfunulia mwanadamu mapenzi yake kwa njia ya neno lake, si kwamba amekomaa kuwaongoza watu kwa Roho Wake Mtakatifu. Kinyume cha huyo Roho Mtakatifu aliahidiwa ili apate kulitafsiri neno la Mungu kwa watu, ili wapate kuelewa na kushika mafundisho yake. Kwa kuwa roho Mtakatifu ndiye aliyewaongoza waandishi wa Biblia, hivyo haiwezekani kwa Roho Mtakatifu kupingana na hilo Neno.

Roho hakutolewa ili kuchukua nafasi ya Biblia. Kwa maana Maandiko yanasema wazi kwamba, neno la Mungu ndilo kipimo cha kupimia mafundisho yote ya Imani zote. Mtume Yohana asema,

[v] “Msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho kwamba zimetokana na Mungu. Kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duni-ani”. 1 Yohana 4:1 na Isaya naye anasema, “Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawa sawa na neno hili, bila shaka kwa hao hamna asubuhi”. Isaya 8:20.

Shutumumu kubwa limetupwa kwa kazi ya Roho Mtakatifu kwa njia ya au wanaotangatanga huku na huku wakidai kwamba wanaongozwa na Roho Mtakatifu, wakisema kwamba hakuna haja ya kuongozwa na neno la Mungu. Wanatawaliwa na hali ya kujisikia msisimko kwamba hiyo ndiyo sauti ya Roho katika mioyo yao. Lakini hali hiyo inayowatawala siyo Roho wa Mungu. Kule kujisikia msisimko kukifuatwa huishia katika machafuko, udanganyifu na uharibifu. Hali hiyo huendeleza tu kazi ya mwovu. Kwa kuwa kazi ya Roho Mtakatifu ni muhimu sana katika kanisa la Kristo, ni makusudi ya Shetani kubuni mbinu za uongo kwa njia ya wakorofi wanaotangatanga na kujipendekeza kwamba wanaongozwa na Roho ili kuchafua kazi ya Roho na kuwafanya watu wa Mungu wasijali maandiko ambayo ndiyo njia iliyowekwa na Bwana mwenyewe.

Pamoja na neno la Mungu Roho Mtakatifu ataendelea na kazi yake katika muda wote wa ujumbe wa Injili. Wakati ule ambapo Maandiko ya Agano la kale na Agano Jipya yaliyotolewa, Roho Mtakatifu hakuacha kuwasiliana na watu na kuwavuvia, mbali na alivyowaongoza katika kazi ya kuunganisha maandiko matakatifu katika kitabu. Biblia yenyewe inasema, jinsi watu walivyopata maonyo, kemeo mashauri na maongozi katika kazi ya kuunga Biblia kwa njia ya Roho Mtakatifu. Hata manabii kadhaa wametajwa katika vizazi mbalimbali ambao maneno yao hayakuandikwa. Vivyo hivyo baada ya mkusanyo wa maandiko Matakatifu na kuungwa katika kitabu, Roho Mtakatifu aliendelea na kazi yake ya kuwaelimisha, kuwaonya na kuwafaraji watoto wa Mungu.

Yesu aliwaahidi wanafunzi wake. “Msaidizi huyu Roho Mtakatifu ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha, yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia” “. . . . na mambo yajayo atawapasha habari zake, atawaongoza katika kweli yote” Yoh. 14:26; 16:13. Maandiko Matakatifu yanaeleza wazi kwamba ahadi hizi ambazo hazikukomea katika siku za mitume tu, zinaendelea katika kanisa la Kristo katika siku za mitume tu, zinaendelea katika kanisa la Kristo katika vizazi vyote. Mwokozi anawahakikisha wafuasi

wake. “Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dhari” Mathayo 28:20. Na Paulo asema kwamba karama ya maono ya Roho Mtakatifu vitakuwamo kanisani. “Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa Imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo”. Waefeso 4:12-13.

[vi]

Kwa waumini wa Efeso Mtume aliomba, “Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa Utukufu, awape ninyi Roho ya Hekima na ya Ufunuo katika kumjua yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la wito wake. . . . Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadri ya utendaji wa nguvu za uweza wake.” Waefeso 1:17-19. Huduma ya Roho Mtakatifu katika kuelimisha, na kuwajulisha watu mambo ya Mungu kwa njia ya neno lake ndiyo mibaraka ambayo Paulo aliwatakia waumini wa kanisa la Efeso.

Baada ya matokeo ya ajabu ya siku ya pentekoste, Petro aliwasihi watu watubu na kubatizwa kwa jina la Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi. “Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie” Matendo 2:38-39.

Katika kuunganisha na siku kuu ya Mungu, Bwana kwa njia ya nabii Yoeli aliahidi maonyesho ya Roho Mtakatifu. Yoel 2:28. Unabii huu ulitimia sehemu katika siku ya Pentekoste; lakini utatimia kikamilifu wakati wa neema kuu ya Mungu itakayoonekana wakati wa kufunga kazi ya injili.

Mapambano makali baina ya wema na uovu yataendelea na kuzidi mpaka mwisho kabisa. Katika vizazi vyote hasira ya Shetani imeonekana ikipinga Kanisa la Mungu, na Mungu amewapa watu wake neema ili waweze kupingana na maovu hayo. Wakati mitume wa Kristo walipopaswa kueneza ujumbe mahali mahali ulimwenguni Mungu aliwajalia uwezo kwa neema yake, walimwagiwa Roho Mtakatifu na uwezo mwingi. Lakini kadiri kanisa linapokaribia mwisho, ili liokolewe, shetani atajitahidi sana kwa nguvu kulipinga. Ameshuka chini mwenye ghadhabu kuu, kwa kuwa anajua kuwa ana muda mdogo sana. Ufunuo 12:12. Atafanya kazi akitumia ishara

[vii] na ajabu za uongo. 2Thesalonike 2:9. Kwa muda wa miaka 6,000 ibilisi huyu ambaye hapo kwanza alikuwa malaika Mkuu wa Mungu, amejitahidi kudanyanya ulimwengu kwa kila njia ya kuuangamiza. Ujanja wake wote na udanganyifu wa kishetani na ukatili na kila hali vyote vitatumiwa kuwapinga watu wa Mungu katika shindano la mwisho, na wakati huu wa hatari kuu, watu wa Mungu watatoa maonyo ya mwisho katika ulimwengu, kuhusu kuja kwa Yesu mara ya pili. Watu lazima watayarishwe ili kusimama mbele ya Kristo pasipo “mawaa wala kunyanzi”. 2Petro 3:14. Wakati huu neema ya Mungu itakayohitajiwa haitapungua kwa ile iliyotolewa siku ya Pentekoste, siku za mitume.

Mwandishi wa kitabu hiki amefunuliwa mapambano haya baina ya wema na uovu na Roho Mtakatifu. Wakati kwa wakati ameruhusiwa kuona maendeleo ya shindano hili ambalo limeendelea kwa vizazi vyote. Kristo ambaye ni mkuu wa uzima ndiye mwanzilishi wa wokovu wetu. Shetani, ambaye ni mkuu wa giza ndiye mwanzilishi wa dhambi, na ndiye aliyekuwa muasi wa kwanza wa sheria ya Mungu Takatifu. Uadui wa Shetani juu ya Kristo umeonekana dhahiri kwa wafuasi wake. Uadui ule ule uliokuwa wa kupinga kanuni za Mungu, njia ile ile ya udanganyifu ambayo hufanya kosa lionekane kuwa ni kweli, na kufanya sheria za watu kuwa bora kuliko za Mungu, kwa njia hiyo watu wameongozwa kuabudu kiumbe badala ya Mwumbaji, hali hiyo ikifuatiliwa inakwenda katika Historia yetu iliyopita. Juhudi ya shetani ya kumsema Mungu vibaya na kuharibu tabia yake, ili watu wamwelewe Mungu vibaya, wamwone kuwa ni katili wala hana upendo wowote, huwafanya watu wamwogope na kujaribu kuepukana na matakwa yake kadiri iwezekanavyo. Hali hiyo shetani ameitumia katika vizazi vyote. Hali hiyo ilionekana siku za Wazee na Manabii, Mitume na Wafia dini na za Watengenezaji wa kanisa.

Katika pambano kuu la mwisho, shetani atatumia njia zile zile hali ile ile, na namna ile ile ilivyokuwa nyakati za nyuma. Jinsi ilivyokuwa, ndivyo itakavyokuwa, isipokuwa tu shindano la kutisha, ambalo ulimwengu haujaliona. Madanganyo ya shetani yatakuwa ya ujanja mno na werevu mwingi. Mashambulio yake yatakuwa makali sana. Kama ikiwezekana yawapoteze hata wateule. Marko 13:22.

Jinsi Roho wa Mungu alivyonifunulia ukweli mkuu wa neno lake, na mambo yaliyopita na yale yajayo, nimeagizwa kuwajulisha

wengine mambo haya, yaliyofunuliwa kwangu, kufuatilia historia ya mapambano yaliyokuwa hapo katika vizazi vya nyumba na yalivyo sasa na jinsi yakatakvyokuwa wakati ujao. Katika kushughulika na jambo hili nimejitahidi kuchagua na kupanga pamoja matokeo mbalimbali katika historia ya kanisa, ili kuona jinsi ukweli ulivyofunuliwa katika nyakati tofauti, na kutangazwa ulimwenguni, na jinsi ukweli huo ulivyochochea ghadhabu ya Shetani na uadui wa kanisa liupendalo ulimwengu ambao umetangazwa na watu ambao “hawakuthamini maisha yao hata kufa”

[viii]

Katika maandishi haya tutaona kivuli cha mapambano yanayotukabili. Kuhusu mambo haya, katika nuru ya Neno la Mungu na uvuvio wa Roho tutaona jinsi mbinu za mwovu zinavyopangwa, pamoja na hatari, ambazo lazima ziepukwe na wale ambao watakutwa “bila mawaa” wakati wa kurudi kwake Bwana.

Matokeo makuu yaliyokuwa wakati wa matengenezo yamekuwa historia tu iliyopita ambayo inajulikana sana na kukubaliwa na makanisa yote ya kiprotestanti. Kuna ukweli usioweza kukanushwa. Historia hii nimesimulia kifupi tu, katika kitabu ambacho kimefupishwa, ambacho ukweli umefupishwa kwa ufahamu wa matumizi yake. Mahali pengine mtunzi au mwandishi wa historia ametoa maelezo kamili au pengine inapolazimu maneno yake yamenakiliwa, pengine imeachwa tu kama ilivyosimuliwa. Katika kusimulia mambo ya hao watengenezaji wa kanisa katika siku zetu, matumizi yale yale kutoka katika maandiko yao yametajwa.

Siyo kusudi la kitabu hiki kuleta ukweli mpya kuhusu mapambano haya ya zamani, ila kuleta kanuni za kweli kuhusu matokeo yajayo. Lakini kukumbusha sehemu iliyopita huonekana kuna umuhimu, maana humulika hali ya siku za mbele, kwa wale watakaopambana na hali hiyo kama watengeneza dini walivyofanya, kushuhudia na kutetea neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo.

Kitabu hiki hasa kusudi lake ni kufunua pambano kali kati ya kweli na uongo, kuonesha hila za Shetani, na njia ya kufaulu kuzipinga, kuonesha njia ya kutatua tatizo la uovu, kufunua upendo wa Mungu na haki yake jinsi anavyochukuliana na viumbe vyake, na kuonesha sheria ya Mungu isiyobadilika. Ili kwa kukisoma watu waweze kuokolewa kutoka katika nguvu za giza ili washiriki urithi wa watakatifu. Sifa kwake yeye aliyejitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ndiyo sala ya dhati ya mwandishi.

[ix]

E.G.White

1 Utabiri wa Ajali ya Ulimwengu

[1]

Kutoka juu ya kilele cha mlima wa mizeituni, Yesu aliutazama mji wa Yerusalemu. Hekalu lile maarufu lilionekana wazi. Jua la jioni lilitupa miale yake myeupe ya kuta za mawe na marumaru ing' aayo tangu mnara wake wa dhahabu mpaka chini. Mwisraeli ye yote angewezaje kulitazama bila kusifu kwa jinsi iliyvokuwa maarufu! Lakini Yesu alikuwa na mawazo mengine “Alipofika karibu aliuona mji, akaulilia” Luka 19:41.

Machozi ya Yesu hayakuwa kujililia mwenyewe, ingawa mbele yake palikuwa na Getsemane, mahali pa mateso makali yaliomkabili, na Kalwari, mahali pa kusulubishwa pake. Walakini siyo

mambo hayo yaliyomtia huzuni kiasi cha kulia. Aliwalilia maelfu ambao watafikwa na ajali waliomo Yerusalemu.

Historia ya miaka elfu ya watu wa Mungu walio wateule, na jinsi Mungu alivyokuwa akiwaangalia kwa huruma nyingi, ilipita katika macho yake Yerusalemu, mji uliotukuzwa na Mungu kuliko yote duniani mwote. “Bwana ameichagua Sayuni akae ndani yake”. Zab. 132:13. Kwa muda wa vizazi vingi manabii watakatifu walikuwa wakitoa ujumbe wa maonyo. Damu za kondoo zilikuwa zikitolewa kila siku kafara zikielekeza kwa Mwanakondoo wa Mungu.

Kama Israeli angedumisha ushirika wake na mbingu, Yerusalemu ungedumu milele, maana ni mteule wa Mungu. Lakini historia nzima ya watu hawa walipendwa na Mungu imekuwa ya uasi tu. Mungu alikuwa amewahurumia watu wake zaidi ya upendo wa Baba kwa mtoto wake. “Kwa sababu aliwahurumia watu wake, na makao yake” 2Mambo ya Nyakati 36:15. Maonyo na kusihi kote viliposhindwa, aliwatumia kipaji maarufu kabisa cha mbinguni, mwana wa Mungu mwenyewe, ili kushughulikia mji muasi. Kwa muda wa miaka mitatu Bwana na Nuru na utukufu, amekuwa akienda huku na huko kati ya watu wake, “Akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi”. “Kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru

waliosetwa, na kutangaza mwaka uliokubaliwa”. “Vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na maskini wanahubiriwa habari njema” Matendo 10:38; Luka 4:18; Mathayo 11:5.

[2] Aliishi kati yao bila kuwa na makao maalumu ili apate kuwasaidia katika hali zao za kuhurumiwa, akiwasihi ili wapate kukikubali kipawa cha mbinguni, ambacho ni cha uzima. Huruma zake nyingi zilikataliwa na waasi hawa kwa masikitiko makubwa. Lakini Israeli alimkataa rafiki yake mkuu na msaidizi wake wa pekee. Kusihhi kwake kwa upendo mwingi kumedharauliwa na kukataliwa.

Muda wa rehema na msamaha ulikuwa unatoweka. Mkusanyo wa ghadabu kwa ajili ya uasi wao, ambao ni wa muda mrefu, ulikuwa umejaa karibu kupasuka juu yao. Yule ambaye ndiye angeweza kuwaokoa na ajali dhahiri iliyokuwa ikiwakabili, amedharauliwa, amekataliwa na karibu atasulubishwa.

Kristo alipoutazama Yerusalemu na ajali yake ikiukabili, pamoja na taifa zima, aliona maangamizo yake yote kwa ukamilifu. Alimwona Malaika mwenye upanga tayari kuharibu na kuangamiza mji ambao umekuwa makao ya Mungu kwa muda mrefu. Kutokea mahali pale pale alipokuwa akisimama mpaka sehemu yote ya mji ambao baadaye Titus jemadari alisimama pamoja na jeshi lake, alitazama ng'ambo pale hekalu takatifu liliposimama. Machozi yakilengalenga machoni mwake, akiona jinsi kuta za mji zitakavyozungukwa na majeshi ya wageni. Alisikia vishindo vya majeshi vikijipanga kwa vita. Alisikia sauti za akina mama na watoto wao wakililia chakula, wakati mji umezingirwa na majeshi ya adui. Aliona nyumba takatifu ya Mungu ikiteketea katika ndimi za moto, na maangamizo makuu.

Akitazama mbele katika vizazi vingi aliona watu wa agano na Mungu wakitawanyika katika nchi zote, kama “mavunjiko jangwani”. Huruma za Mungu, upendo usio kifani, unaonekana katika maneno ya maombolezo ya Yesu juu yao. “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uuaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale walio-tumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wake, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mbawa yake, lakini hamkutaka” Mathayo 23:37.

Kristo aliona katika Yerusalemu mfano wa ulimwengu ambao ni mgumu kwa kutokuamini na uasi, nao una haraka kuingia

katika hukumu za Mungu. Roho yake ilijaa huzuni kwa ajili ya maangamizo ya nchi. Alitamani kuwaokoa wote. Alikuwa tayari kujitoa kabisa mpaka kifo ili kuwaletea watu wote wokovu.

Mtukufu wa mbinguni analia! Jambo hilo laonesha jinsi ilivyo kazi ngumu mno ya kumwokoa mkosaji na matokeo ya kuvunja sheria ya Mungu. Yesu aliuona ulimwengu umehusika katika uasi sawa na Yerusalemu ulivyoangamizwa kwa uasi ule ule.

Dhambi kuu ya Wayahudi ilikuwa ile ya kumkataa Kristo. Dhambi kuu ya ulimwengu ni ile ya kukataa sheria ya Mungu, ambayo ndio msingi wa utawala wake, mbinguni na duniani. Watu [3] mamilioni waliomo dhambini ambao wataangamia, katika mauti ya pili watakataa kusikia ukweli katika wakati wao wa wokovu.

Hekalu Maarufu Kuangamia.

Siku mbili kabla ya Pasaka Kristo na wanafunzi wake walikwenda tena katika mlima wa mizeituni kuelekea mji. Mara nyingine tena aliliangalia hekalu likiwa katika uzuri wake na mng'ao wake. Sulemani Mfalme wa Israeli, mwenye hekima kuliko wote alijenga hekalu la kwanza. Lilikuwa maarufu kabisa, ambalo ulimwengu haujaona kama hilo. Baada ya kuharibiwa na Nebukadneza, lili-jengwa upya miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Lakini hekalu hili la pili halikulingana na lile la kwanza kwa utukufu. Wingu la utukufu, halikutua juu yake, wala moto kutoka mbinguni haukuja juu ya madhabahu yake. Sanduku, kiti cha rehema, na meza za wonyesho havikuonekana ndani yake. Hakuna sauti kutoka mbinguni iliyosema na makuhani kuwajulisha mapenzi ya Mungu. Hekalu la pili halikujia na utukufu wa Mungu, ila mmoja ambaye ni Mungu halisi alikuwako, yaani Kristo. Mmoja anayetakiwa na mataifa yote, ndiye amekuja katika hekalu lake. Ndiye, ambaye ni mtu wa Nazareti aliyefundisha katika ukumbi wake, na kuponya wagonjwa. Lakini Israeli wametia unajisi karama ya mbinguni. Basi, pamoja na mwalimu huyu mnyenyekevu alipotoka mlangoni mwa hekalu, utukufu uliwaacha milele pamoja na hekalu lao. Maneno ya Mwokozi yalikuwa yametimia tayari. “Nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa” Mathayo 23:38

Wanafunzi walishangaa sana maneno ya Kristo ya kulaani hekalu, nao walitamani sana kufahamu maana yake. Herode Mkuu

alikuwa ametia humo hazina tele ya Warumi na ya Wayahudi. Mawe ya marmar yenye kung'aa yaliyotolewa kutoka Rumi yalijengwa katika hekalu hilo. Kwa hayo wanafunzi walitaka Kristo aangalie na kustaajabia uzuri wake. Walimwambia “Tazama, yalivyo mawe na majengo haya” Marko 13:1.

[4] Yesu akajibu na kusema “Amini nawaambieni, Halitasalia jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa” Mathayo 24:2. Bwana alikuwa amewaambia wanafunzi kuwa atakuja mara ya pili. Hivyo alipotaja hukumu juu ya Yerusalemu mawazo yao yalirudi habari za kuja kwake, kwa hiyo walisema, “Mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako na ya mwisu wa dunia?” Mathayo 24:3. Kristo aliwaeleza wanafunzi mambo ya matokeo makuu yatakayotokea kabla ya mwisho wa ulimwengu. Unabii aliotoa ulikuwa na maana mbili. Wakati ulihusu maangamizo ya Yerusalemu, pia ulihusu matisho ya siku kuu ijayo.

Hukumu zitawaangukia Waisraeli kwa ajili ya kumkataa na kumsulubisha Masihi. “Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu lile lililonenwa na Nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu) ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani” Mathayo 24:15-16 soma pia Luka 21:20-21. Wakati hali ya ukafiri wa Kirumi utakapokuwa ukifanyika katika mahali patakatifu penye kuta za mji mtakatifu, wafuasi wa Kristo itawapasa watafute mahali pengine pa usalama wakakae. Wale watakaookoka itawapasa waharakishe kutoka bila kuchelewa. Kwa ajili ya dhambi za Yerusalemu, zimesababisha hukumu yake. Ukaidi wake na uasi wake umesababisha ajali hiyo. Soma Mika 3:9.

Wenyeji wa Yerusalemu walimlaumu Kristo, kwamba ndiye aliyesababisha maovu yote yaliyowapata, ambayo ni dhambi zao wenyewe. Ingawa walimfahamu kuwa hana dhambi yo yote, walisema kuwa hana budi kufa ili taifa zima lisiangamie. Walikubaliana na uamuzi wa kuhani wao mkuu; kwamba, “inafaa mtu mmoja afe kuliko taifa zima kuangamia.” Yohana 11:47-53.

Wakati walimchinja Mwokozi wao kwa ajili ya kutaja dhambi zao, wao wenyewe walijidai kuwa wana wa Mungu wapendwa, na walitazamia kuwa Mungu angewaokoa kutoka kwa adui zao Warumi!

Uvumilivu Wa Mungu

Mungu alikawiza hukumu yake juu yao kwa muda wa miaka karibuni arobaini. Kulikuwa na Wayahudi wengi ambao hawakuelewa kazi ya Kristo. Tena watoto hawakupata nafasi kama ile ya wazazi wao. Kwa njia ya mahubiri ya mitume nuru ya Injili ingewafikia wote. Wangeona jinsi unabii ulivyotimia, sio kwa kuuliwa kwa Kristo tu, bali kwa kifo na kufufuka kwake pia. Watoto wasingepaswa kupata adhabu kwa ajili ya dhambi za wazazi wao. Lakini walipoikataa nuru iliyowafikia, ndipo wakashiriki dhambi za wazazi wao na kukijaza kikombe cha uovu wao.

Wayahudi kwa ajili ya ukaidi wao na uasi wao walikataa karama yao ya neema ya mwisho waliyopewa. Ndipo Mungu akawaondolea ulinzi wake. Taifa zima likaachwa liongozwe na kiongozi waliyemchagua. Shetani aliwaamshia hali fedhuli kabisa, nyonge na ya udhalimu. Watu walikuwa kama wanyama tu wakitangatanga kama vipofu, wakawa wakatili. Marafiki na watu wa jamaa moja moja walisalitiana tu wao kwa wao. Wazazi waliwaua watoto wao, na watoto wazazi wao. Watawala hawakuweza kujitawala wenyewe, ukali wao ukawafanya kuwa wajeuri sana. Wayahudi walikubali maneno ya ushahidi wa uongo juu ya Kristo hata wakamwua Yule mwenye haki, Mwana wa Mungu, asiye na hatia. Sasa mashitaka yao ya uongo yamefanya maisha yao kuwa ya ovyo. Hofu ya Mungu haikuwa ndani yao tena. Shetani ndiye alikuwa mtawala wao. Viongozi wa upinzani wakaangamizana wao na wapinzani wao bila huruma. Hata mambo matakatifu ya hekaluni hayakuweza kuheshimiwa. Hekalu lilitiwa unajisi kwa maiti zilizokuwa zikitupwa huko ovyo. Hata hivyo matendo ya kinyama ya jinsi hii waliyoyatenda walikuwa wakiona sawa tu na kusema kuwa waliyoyatenda walikuwa wakiona sawa tu na kusema kuwa Yerusalemu hautaharibiwa, maana ni mji wa Mungu! Hata wakati ule Warumi walipozunguka mji wafedhuli hawa walikuwa na tumaini kuwa Mungu angeingilia kati na kuwafukuza Warumi. Lakini Israeli alikuwa ameondolewa ulinzi wake, na sasa yuko wazi bila kinga yoyote.

[5]

Ishara ya Maangamizo

Utabiri wowote Yesu aliotabiri kuhusu uangamizo wa Yerusalemu ulikuwa unatimia moja kwa moja. Ishara na vioja vilionekana. Kwa muda wa miaka saba mtu fulani alikuwa akitembea katika barabara za Yerusalemu huku akitangaza ole utakaoujia mji. Mtu huyu ambaye hajulikani alikotoka aliteswa na kufunga na kutendwa mabaya lakini kwa dharau na jeuri yeye alijibu, “Ole Ole, wa Yerusalemu”. Baadaye aliuawa katika kuuzingira Yerusalemu. Katika maangamizo ya Yerusalemu hakuna hata mkristo mmoja aliyepotea. Baada ya majeshi ya Kirumi chini ya jemadari Cestius kuuzingira mji, ghafla waliondoka bila kutazamiwa, wakati kila jambo lilikuwa tayari kwa mashambulio. Jemadari wa Kirumi aliamuru majeshi yake yaondoke bila sababu maalum. Dalili iliyoahidiwa na Kristo kwa wafuasi wake imefika. Luka 21:20-21.

Mambo yalitayarishwa kabisa ili kuwezesha wakristo kukimbia, ambavyo hayakuwezekana kuzuilika. Wayahudi au Warumi hawakuweza kuyazuia. Wakati majeshi ya jemadari Cestius yalipoondika, Wayahudi nao walitoka kuwafukuza, na wakati walipokuwa katika kupambana, wakristo walipata nafasi ya kukimbilia mahali pa usalama. Walikimbilia mji wa Pella.

[6] Majeshi ya Wayahudi yaliyowafuatia Warumi yalishambulia majeshi ya nyuma. Hivyo Warumi walifaulu kwa shida sana kuendelea. Wayahudi walirudi Yerusalemu wakifurahi, wakiwa na vitu walivyoteka. Ushindi mdogo huu uliwaletea maafa makubwa. Walizidi kuwa wakaidi zaidi wasitake kujisalimisha kwa Warumi, hivyo maafa makubwa yasiyoelezeka, bila kipimo yalifuata baadaye.

Mabaya ya kutisha yaliujia Yerusalemu wakati jemadari Titus aliporudi na kuuzingira mji mara ya pili. Mji ulizingirwa wakati wa Pasaka, wakati Wayahudi kwa mamilioni walikuwa wamekusanyika ndani yake. Maghala ya vyakula yalikuwa yameharibiwa na watu wenye fitina, na sasa hali ya njaa iliwaingilia. Watu walikula ngozi za mishipi yao na viatu vyao. Watu wengi sana walikuwa wakipenya usiku na kutoka nje ya mji kutafuta matunda mwithu. Wengi walikuwa wakikamatwa na kuuawa kikatili. Mara nyingi hata wale waliowahi kurudi salama, walinyanganywa na wenzao kile walichopata huko nje. Waume waliwanyang'anya wake zao

chakula na wake vivyohivyo waliwanyanga'nya waume zao. Watoto walipokonya chakula kutoka vinywani mwa wazee wao.

Viongozi wa majeshi ya Kirumi walikusudia kutoa kipigo kizito kwa Wayahudi ambacho kingewafanya wasalimu amri mara moja. Mateka walipigwa, wakateswa sana na kutundikwa mitini, mbele ya kuta za mji. Kufuata bonde la Yeoshafati na kuendelea mpaka mlima wa Golgota, misalaba mingi sana, ambako watu walikuwa wametundikwa ilijazana tena. Hapakuwako na nafasi ya kupita kati yake. Kwa hiyo matamshi yaliyotamkwa mbele ya kiti cha hukumu cha Pilato kwamba: “Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu” yalikuwa yanatimia. Mathayo 27:25.

Jemadari Titus alijawa na hofu ya mshangao wa kuchukiza alipoona maiti za Wayahudi zimejazana bondeni humo. Alilitazama Hekalu; akaamuru kuwa mtu asiliguse. Aliwasihi viongozi wa Wayahudi wasalimu amri, asije akalazimika kuwaharibu, na kupa-haribu mahali patakatifu kwa kumwaga damu; yaani wasiingize vita hekaluni. Kama Wayahudi wanalipigania mahali pengine, hakuna Mrumi hata mmoja angelithubutu kuharibu hekalu takatifu! Josephus aliwasihi sana wasalimu amri ili wajiokoe, na kuokoa mji wao, pamoja na hekalu lao takatifu. Lakini alijibiwa kwa matusi mabaya na kushambuliwa kwa ghafla. Hivyo ndiyo ilikuwa nafasi yao ya mwisho na Josephus alikuwa mwombezi wao wa mwisho. Titus alijaribu kuliokoa hekalu, lakini ilikuwa kazi bure. Mkuu kuliko yeye alikuwa ametamka kuwa, halitasalia jiwe juu ya jiwe.

Baada ya kuliteketeza hekalu, mji wote ukaangukia mikononi mwa Warumi. Viongozi wa Wayahudi waliziacha ngome zao. Titus alisema kuwa Mungu ndiye amezitia katika mikono yake, maana hakuwa na uwezo wa aina yoyote ile ambao ungaliweza kuzibomoa ngome hizo. Mji na hekalu pia vilibomolewa mpaka na misingi yake yote; na mahali pale hekalu takatifu lilipojengwa palilimwa kwa jembe na kusawazishwa kama shamba. Yeremia 26:18. Watu zaidi ya milioni moja waliangamia, na waliobakia wengine walitekwa na kupelea utumwani; wengine waliuzwa kama watumwa wengine walitawanyika wakaishi mahali pengine katika hali ya ukimbizi na wengine walitupwa katika matundu ya simba na wanyama wakali wakawa sinema ya kutazamwa na watu wakiangamizwa.

Wayahudi walikuwa wamekijaza kikombe chao cha kulipizwa kisasi. Katika misiba iliyowafuata baadaye ilikuwa na mavuno ya

mambo waliyoyapanda kwa mikono yao wenyewe. “Ee Israeli, umejiangamiza mwenyewe; . . . Kwa maana umeanguka kwa sababu ya maovu yako”. Hosea 13:9; 14:1. Taabu yao ilitajwa kila mara kama adhabu iliyoagizwa na Mungu. Kwa njia hii mdanganyaji mkuu hufunika kazi yake na kuitupa kwa Mungu. Wayahudi kwa ajili ya ukaidi wao wa kukataa rehema na upendo wa Mungu walijiondolea ulinzi wa Mungu wakabakia wazi.

Hatujui kiasi gani tunawiwa na Kristo kwa ajili ya amani na ulinzi tulivyo navyo. Mkono wa Mungu wa kuulinda humzuia Shetani asituharibu. Kutotii na kutoshukuru ni deni kubwa tulilo nalo kwa Mungu. Lakini mtu anapovuka mpaka wa Mungu ulinzi wake huondolewa. Mungu hamtetei mtu huyu kama mshitakiwa. Huwaacha hao wakaidi wavune kile walichopanda. Kila cheche ya nuru iliyokataliwa ni mbegu iliyopandwa, nayo italeta mavuno. Roho wa Mungu anayesihi akipingwa daima, mwisho ataondoka.

[8] Ndipo mtu atabaki bila uwezo wa kuzuia tama mbaya kwake, hakuna kinga kwa madanganyo ya mwovu Shetani.

Uharibifu wa Yerusalemu ni onyo kuu kwa watu wote wanaokataa rehema za Mungu. Unabii wa Mwokozi kuhusu hukumu ya Yerusalemu utatimia kwa njia nyingine. Katika ajali ya mji mteule, tunaona msiba utakaowapata walimwengu waliokataa rehema za Mungu na kukanyaga sheria yake takatifu. Huzuni kuu ambayo haijatokea ulimwenguni. Iliwapata watu wapotovu. Kukataa mamlaka ya mbinguni kumekuwa jambo la kutisha sana. Lakini wakati ujao utakuwa wa huzuni kuu zaidi. Wakati roho wa Mungu atakapoondolea kabisa ulimwenguni, hakuna kitu kitakachozuia hali ya kinyama, na hasira za kishetani na udanganyifu wake wa kikatili.

Katika siku hiyo, sawa na ulivyokuwa kwa Yerusalemu, watu wa Mungu wataokolewa. Soma Isaya 4:3; Mathayo 24:30-31. Kristo atakuja mara ya pili ili kuwakusanya watu wake. “Ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni, pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu” Mathayo 24:30-32.

Hebu watu na waangalie sana, wasije wakasahau maneno ya Kristo. Kama vile alivyowaonya wanafunzi wake kuhusu uharibifu wa Yerusalemu, juu ya kukimbia kwao, ndivyo pia ame-

onya ulimwengu kuhusu uharibifu wa mwisho. Wale wapendao wanaweza kukimbia ghadhabu ijayo. “Tena kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa” Luka 21:25. Soma pia Mathayo 24:29; Marko 13:24-26; Ufunuo 6:12-17. Maneno ya Kristo ya maonyo ni kwamba, “Kesheni basi” Marko 13:35. Wale wataojali maonyo hawataachwa wakae gizani.

Sasa ulimwengu hauko tayari kupokea maneno ya ujumbe wa Kristo kwa wakati huu, kuliko Wayahudi walivyopokea maonyo ya Kristo kuhusu uharibifu wa Yerusalemu. Njoo, maadamu ni leo. Siku ya Mungu itawaghafulisha wote, wasiomcha Mungu. Wakati maisha yatakapokuwa yanaendelea kama kawaida; wakati watu watakapozama kabisa katika anasa; katika shughuli, na katika uchumi; wakati waongozi wa dini watakaposifia maendeleo ya ulimwengu na watu wakijitumainisha kuwa na amani na usalama, ndipo, kama vile mwizi aibavyo usiku, ndivyo uharibifu utakavyowajia wote wasiomcha Mungu, “Wala hakika hawataokolewa”. 1Thes. 5:2-5.

Marejeo:

Milman — History of the Jews. Book 13

[9]

2/Wakristo wa Kwanza Waaminifu wa Kweli

Yesu aliwafunulia wanafunzi wake hali ya watu wake jinsi itakavyokuwa tangu siku ile atakayoaacha kwenda zake mbinguni, hata siku atakaporudi mara ya pili kwa nguvu na utukufu mwingi. Alipenyeza macho yake akaona hali ya fujo na mateso itakayowapata wafuasi wake siku za usoni. Soma Mathayo 24:9,21-22. Wafuasi wa Kristo hawana budi kupitia njia ile ile ya dharau na dhihaka na masumbuko, kwa Mwokozi wa ulimwengu, utaonekana kwa wote watakaoliamini jina lake pia.

Umizimu uliona kuwa kama ukristo utafaulu utaondolea mbali mahekalu na madhehebu zote za giza kwa hiyo moto wa mateso ukachochewa. Wakristo walinyang'anywa mali zao, na kufukuziwa mbali kutoka katika miji yao. Watu wenye elimu na wasio na elimu, walichinjwa bila huruma.

Mateso yalianzia wakati wa mfalme Nero yakaendelea kwa karne nyingi. Wakristo walisingiziwa kuwa ndio wameleta njaa, tauni, na tetemeko la nchi. Walisaliti na wachochezi walikuwa tayari kusaliti na kuwasingizia wasio na hatia kwamba ni hatari kwa jamii. Wengi sana walitupwa katika matundu ya wanyama wakali au walichomwa moto; wengine walitundikwa mitini, wengine walivishwa ngozi za wanyama wakatupiwa mbwa na kurarulia nao. Katika mikutano ya hadhara, watu wengi walihudhuria ili kushangilia mateso yao na jinsi walivyokufa kikatili kabisa.

Wafuasi wa Kristo walilazimishwa kutafuta maficho mahali pa ukiwa nyikani. Chini ya milima iliyoko nje ya mji wa Rumi walichimba mifereji mirefu, wakafanya makao katika mapango hayo chini ya miamba. Humo ndimo walimozika wafu wao pia. Hayo yalikuwa makimbilio yao. Wengine walikumbuka maneno ya Bwana, kwa hiyo walipoudhiwa walifurahi tu. “Thawabu yao itakuwa kubwa sana mbinguni, maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yao” Mathayo 5:11-12.

[10]

Nyimbo za ushindi zilisikika kutoka katika miale ya moto wakiziimba kwa furaha. Kwa imani walimwona Kristo na malaika

wakiwazunguka kwa kupendezwa sana kwa ajili ya ushujaa wao. Sauti ilisikika kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu, ikisema: “Uwe mwaminifu mpaka kufa, nami nitakupa taji ya uzima”. Ufunuo 2:10.

Shetani alijitahidi kuliharibu kanisa la Kristo, kwa njia ya mateso, lakini ilikuwa kazi bure. Watendakazi wa Mungu walichinjwa, lakini Injili ilizidi kuenea, na wafuasi kuongezeka. Mkristo mmoja alisema, “Mnatukatakata kama majani, lakini tunazidi kuongezeka; damu ya wakristo ndiyo mbegu.”

Kwa hiyo shetani alipanga vita kwa njia nyingine ya kufaulu zaidi. Alisimamisha bendera yake katika kanisa la kikristo, ili kupata wakristo wadanganyifu, wenye hila, hivyo alifaulu kuliko alivyotumia mateso, akatumia vishawishi na heshima. Ibada ya Sanamu ilikubaliwa kuwa ni sehemu ya ukristo, na ukweli halisi akakataliwa. Walijidai kuwa watu wa Mungu lakini huku wakishikilia dhambi, bila kuwa na haja ya kuziungama na kuziacha. Hapakuwako badiliko lolote katika mioyo yao. Walikubaliana tu ya kuwa wote “waamini katika Kristo”

Sasa kanisa lilikuwa katika hatari kubwa. Magereza, mateso, kuchomwa moto na upanga, hayo yote yalikuwa nyeti kulinganisha na hali hii ya ukristo bandia. Baadhi ya wakristo walisimama imara. Wengine walipendelea kugeuza imani zao na kufuata ukristo huu bandia. Katika vazi hili jipya la ukristo wa kujifanya, shetani alijipenyeza kanisani na kuchafua imani yao.

Wakristo wengi baadaye walipotoka kabisa na kushusha hadhi yao. Mwisho mwungano wa ukristo na umizimu ulifanyika. Ingawa waabudu sanamu walijidai kuungana na kanisa, lakini walishikilia sanamu zao tu, ila walibadili sanamu zao ziwe mfano wa Yesu, na mfano wa Maria na watakatifu wengine. Wakaingiza mafundisho ya uongo mambo ya ushirikina na uchawi, na mambo ya ibada ya sanamu. Hivyo vyote vikawa sehemu ya imani na ibada ya ukristo. Kwa hiyo ukristo halisi ukachafuliwa sana, na kanisa likapoteza hadhi yake na uwezo wake. Walakini wengine hawakupotoshwa. Walishikilia kanuni yao ya imani ya kweli.

Makundi Mawili Kanisani

[11]

Kumekuwepo makundi mawili baina ya watu wajidaio kuwa wafuasi wa Kristo. Wakati kundi moja linajifunza maisha ya Kristo na

linapojitahidi kufuata kielelezo chake kundi jingine linaepa kabisa kujifunza mambo ambayo yangedhihirisha makosa yao, maana hawataki kufuata ukweli. Walakini, hata kanisa lilipokuwa katika hali bora, halikuwa kamilifu kabisa. Yuda alihesabika kuwa mmojawapo wa wanafunzi ili kwa njia ya mafundisho ya Kristo na kielelezo chake angeweza kuona kasoro zake na kutubu. Lakini kwa ajili ya kushikamana na dhambi aliyakaribisha majaribu ya Shetani. Alichukizwa wakati kasoro zake zilipotajwa, na hivyo aliendelea mpaka akamsaliti Bwana wake. Marko. 14:10-11.

Anania na Safira mkewe walijipendekeza kuwa wametoa mali yao yote kwa Mungu wakati walipoficha sehemu yake kwa choyo chao. Roho wa Mungu alimfunulia mtume Petro tabia yao hasa ya wajipendekezao hawa, na hukumu za usafi wa kanisa. Soma Matendo 5:1-11. Mateso yalipowajia wafuasi wa Kristo yaliwadhihirisha wale waliokuwa wafuasi halisi. Lakini mateso yalipokoma, wakaingia watu kanisani ambao hawakuwa wafuasi halisi, na kwa njia hiyo shetani alipata nafasi ya kuliharibu kanisa.

Wakati wakristo waliporidhika kuungana na watu ambao hawakuongoka sawasawa, shetani alishangilia. Halafu aliwaamsha watu kama hao wawaudhi wale walioshikilia kanuni ya Mungu barabara. Wakristo wapotovu hawa ambao ni nusu wamizimu, walielekeza upinzani wao katika mafundisho yale ambayo ni muhimu kwa ukristo, ndiyo maagizo ya Kristo. Kutakikana msi-mamo imara kabisa kukabiliana na mafundisho mapotevu yaliy- oingizwa kanisani. Biblia ilikataliwa wazi kuwa sicho kipimo cha ukristo. Uhuru wa dini ulihesabiwa kuwa kama uzushi na wale waliousikilia waliharamishwa

Baada ya mapambano ya muda mrefu, wale waongofu wa kweli waliona kuwa ni lazima kuwepo utengano. Hawakuweza kuvumilia makosa hayo mabaya yenye kuleta hatari kwao na kwa watoto wao na wajukuu wao. Wakaona kuwa amani ya kweli lazima igharimu. Kwamba ikiwa kuwa na amani na kutupilia mbali kanuni za Mungu ndiko kutaleta umoja, basi amani ya namna hiyo na ipotelee mbali, ikilazimu lazima kuwe na utengano na hata kwa vita.

[12] Wakristo wa kwanza walikuwa waongofu wa kweli. Walikuwa wachache, bila kuwa na mali, heshima au vyeo nao walichukiwa na wale wamizimu, sawa kama vile Kaini alivyomchukia Habili. Soma Mwanzo 4:1-10. Tangu wakati wa Kristo mpaka leo, wafuasi

wa kweli wa Mungu wamekuwa katika chuki na wale wapendao dhambi.

Sasa basi, Injili itawezaje kuitwa kuwa ujumbe wa amani? Malaika waliimba katika uwanda wa Bethlehemu “Atukuzwe Mungu juu mbinguni na dunia iwe amani kwa watu aliowaridhia.” Luka 2:14. Inaonekana kuwa iko tofauti kati ya maneno haya ya Unabii na maneno ya Kristo: “Sikuja kuleta amani, bali upanga” Mathayo 10:34. Lakini yakifahamika kwa kweli, hayana tofauti yoyote. Injili na ujumbe wa amani. Dini ya Kristo ikipokelewa na kutiwa hueneza furaha na amani duniani. Kazi ya Yesu ilikuwa kuwapatanisha watu na Mungu, mtu na mtu mwenzake. Lakini dunia kwa ujumla inatawaliwa na shetani, ambaye ni adui mkubwa wa Kristo. Injili inaonyesha kanuni za uzima na maisha kwa ujumla, na hizo hupingana na utawala wa shetani. Kanuni hizo za shetani hazitaki maisha matakatifu yanayokuwa kinyume na dhambi. Hilo huamsha vita kwa watu wanaong’ang’ania maisha matakatifu. Ni kwa njia hii ndiyo sababu Injili ikaitwa kuwa ni upanga. Soma Mat. 10:34.

Watu wengi walio dhaifu katika imani wako tayari kuutupa ujasiri wao katika Mungu, kwa sababu huwafanikisha watu wabaya na watu wema husumbuka tu bila mafanikio. Mtu mwema, mwenye haki anawezaje kuchukuliana na hali ya jinsi hiyo isiyo na haki? Mungu ametuonyesha upendo wake kwa namna inayotosha. Hatuwezi kuona mashaka kwa wema wake, eti kwa sababu hatuelewi tu mipango yake

Mwokozi alisema: “Likumbukeni lile neno nililowaambia, mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi” Yohana 15:20. Watu watakapopitia mateso, au hata mauti, huwa wamepitia njia ya Mwana mpendwa wa Mungu.

Wenye haki hupitia katika mateso machungu ili watakase wao wenyewe, na njia hiyo iwe kielelezo cha imani yao kwa wengine na uongofu wa halisi ulivyo. Hali yao izibe vinywa vya wapotovu wanaosema kuwa haiwezekani kuwa hiyo. Mungu huwafanikisha waovu na kuudhihirisha uadui wao jinsi inavyowastahili adhabu ya uharibifu wao. Kila kitendo cha ufedhuli kitendewacho mtu wa Mungu, kitahesabika kana kwamba kilitendwa kwa Kristo mwenyewe, nacho kitaadhibiwa.

Paulo asema, “Wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa” 2 Tim. 3:12. Kwa nini basi mateso yame-

[13] tulia? Sabatu yake ni kwamba kanisa limeungana na ulimwengu kimaisha, kwa hiyo hakuna upinzani wa kuchochea mashindano. Dini ya siku zetu hizi haifanani na ile ya siku za mitume katika utakatifu. Kwa kuwa ukweli wa Neno la Mungu unajaliwa kidogo tu, na kwa kuwa kuna uongofu kidogo tu kanisani, ukristo unakuwa kitu cha kawaida tu ulimwenguni. Hebu mwamko wa dini ya siku za mitume uwemo kanisani, hapo mto wa mateso utawashwa.

Marejeo:

Trertulian — Apology, paragraph 50

3/Giza la Kiroho Katika Kanisa la Kwanza

[14]

Mtume Paulo aeleza kwamba siku ya Kristo haitakuja “Usipokuja kwanza ule ukengeufu, akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi”. 2Wathesalonike 2:3,4-7. Hivyo hata siku hizo za mwanzoni mtume aliona uovu ukilitambalia kanisa ambao utaingiza upapa ndani.

Kidogo kidogo, “siri ya kuasi” iliendesha kazi yake ya udanganyifu. Kawaida za kimizimu ziliingizwa kanisani na kukubaliwa kuwa nia sawa, ingawa zilipingwa kwanza na kuleta mateso kwa njia ya wamizimu. Lakini mateso yalipokoma hali ya kanisa ilibadilika na kuacha kanuni halisi ya kikristo. Hali hiyo iliongozwa na mapapa na mapadri. Uongofu bandia wa mfalme Constatine ulileta burudiko kubwa kanisani. Kwa hiyo sasa uharibifu ulizidi mno kanisani. Ukafiri ulishinda kabisa na kutawala kanisani. Kawaida za kikafiri na mafundisho ya ushirikina viliingizwa kanisani na kuhesabiwa kuwa ni mojawapo ya kanuni za Kikristo.

Mapatano haya baina ya ukafiri na ukristo yalitokeza “mtu wa dhambi”, aliyetabiriwa katika Biblia. Dini ya uongo ni hila za Shetani, na juhudi yake ni kuketi katika kiti cha enzi apate kuutawala ulimwengu kama apendavyo.

Mojawapo ya mafundisho ya kanisa la Kiroma ni kwamba papa amepewa uwezo mkuu awe juu ya makasisi wote na wachungaji wote wa ulimwengu. Zaidi ya hayo, papa amepewa heshima ya kuitwa “Bwana Mungu Papa” na kwamba yeye hakosei hata kidogo. Dai lile lililodaiwa na shetani huko jangwani wakati wa majaribu ya Yesu lingali linaendelea katika kanisa la Kirumi; na watu wengi humtukuza jinsi hiyo.

Lakini wanaomcha Mungu huyapinga majivuno hayo kama Kristo alivyoyapinga ya mwovu shetani jangwani. “Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake” Luka 4:8. Kamwe Mungu

[15] hakumweka mtu ye yote kuwa kichwa cha kanisa. Ukuu wa upapa unapingwa na Maandiko Matakatiifu. Papa hawezi kuwa kichwa cha kanisa la Kristo isipokuwa ajitwalie mamlaka hayo kwa nguvu. Warumi hawalaumu waprotestanti, na kusema kwamba wamejitenga na kanisa la kweli. Lakini wao ndio waliojitenga na Imani “ambayo kwanza ilikabidhiwa kwa watakatiifu” Yuda 3.

Shetani alifahamu fika kuwa Mwokozi aliyapinga majaribu yake kwa njia ya Maandiko Matakatiifu. Kila jaribu la shetani Mwokozi alilipinga kwa ngao ya kweli, akisema “Imeandikwa”. Ili kusudi shetani awashinde watu, na wasifahamu Maandiko Matakatiifu. Ukweli Mtakatiifu lazima ufichwe usifahamike. Kwa muda wa miaka mamia Biblia ilikatazwa kusomwa kabisa na kanisa la Kirumi. Watu waliruhusiwa kusoma na kueleza maana yake, ili kufaulisha mpango wao. Kwa njia hiyo Papa alitukuzwa kabisa ulimwenguni kama kaimu wa Mungu duniani.

Jinsi Sabato “Ilivyobadilishwa”

Unabii unaeleza kuwa, Upapa utafikiri kubadili “Wakati na Sheria” Daniel 7:25. Ili kusudi kuimarisha ibada ya sanamu, hes-hima ya kuwakumbuka wafu na sura zao iliingizwa katika kanisa la Kikristo. Tamko la baraza lao kuu kwamba, mifano au picha za watu mashuhuri ziwekwe ili kuwakumbuka, lilithibitisha ibada ya sanamu. Kwa njia hiyo Rumi ikathubutu kufuta amri ya pili katika amri za Mungu, ambayo inakataza kuabudu sanamu, halafu wakagawa amri ya kumi kuwa amri mbili ili hesabu ya amri iwe kamili

Viongozi wa kanisa ambao ni wapotofu, wakageuza amri ya nne, wakaondoa Sabato ya siku ya saba, siku ambayo Mungu alibariki na kuitakasa (Mwanzo2:2-3), badala yake “wakatukuza siku ya jua” ambayo ilikuwa ikitukuzwa na wakafiri. Katika karne ya kwanza siku ya Sabato ilikuwa ikitukuzwa na wakristo wote. Lakini shetani alijitahidi kutimiza makusudi yake mapotofu, ndipo kutukuza Jumapili kulianza (siku ya jua) eti kuadhimisha siku ya ufufuo wa Kristo. Ibada za kidini ziliadhimishwa sasa hiyo kama kumbukumbu ya ufufuo wa Kristo. Walakini Sabato iliendelea kutumzwa kama siku Takatiifu.

Shetani aliwaongoza Wayahudi kuitilia Sabato vikwazo vingi mpaka ikawa mzigo. Na sasa kwa mpango huu mpya aliougundua

wa kutukuza siku ya ufufuo, alitupa laumu kwa Wayahudi kwamba Sabato ni ya Kiyahudi, wakati wakristo walikuwa wanafurahia siku ya ufufuo. Aliwaelekeza watu waone kuwa Sabato ya siku ya Saba ni ya huzuni na masikitiko tu, kwa hiyo haifai. Hii ilikuwa chuki kwa Wayahudi.

Mfalme Constantine aliamua kuwa Jumapili iwe siku ya kupunzika katika Dola yake yote. Siku ya jua ilitukuzwa na watu wake ambao ni wapagani, na wakristo pia wakitukuza. Makasisi wa makanisa wakatilia mkazo amri hiyo maana ndio waliomshauri mfalme atoe amri hiyo. Makasisi kwa kutaka vyeo walidhani kuwa kama watu wote, wakafiri na wakristo pia wakiitukuza siku hiyo ya jua, ukuu wa kanisa utaenea na kuwa na mvuto zaidi. Lakini watu wa Mungu waliendelea kutukuza Sabato ya kweli, ingawa walianza polepole kuitukuza Jumapili kama ilivyoamriwa na mfalme.

Mchanganyaji mkuu alikuwa hajamaliza kazi yake bado. Al-ijihusisha kabisa katika kutumia uwezo wake kwa njia ya naibu wake mwenye kiburi anayejidai kuwa wakili wa Kristo (Papa). Hal-mashauri kubwa zilifanyika ambazo ziliidhinisha cheo hicho na kukitangaza ulimwenguni pote. Karibu kila baraza lililofanyika, Sabato ilishambuliwa kidogo, na jumapili ilitukuzwa. Hivyo sikukuu ya kipagani mwishowe ikapewa heshima kama siku ya Mungu, na Sabato ya Mungu ikatajwa kuwa ni siku ya Wayahudi kwa hiyo ikatajwa kuwa ni siku ya Wayahudi, kwa hiyo ikapigwa marufuku.

Uasi ukafaulu kujitukuza kama “Mungu na kuabudiwa” 2 Thes. 2:4. Amethubutu kubadili amri ya Mungu inayomtaja Mungu kuwa Mungu wa kweli aliye hai. Katika amri ya nne Mungu anadhihirishwa kwamba ni Muumba. Siku ya saba ya juma ilitakaswa na kutengwa kuwa siku ya kupumzika kwa wanadamu, ikimkumbusha kwamba Mungu ndiye muumbaji na siku hiyo ndiyo ya kuabudu. Shetani alijitahidi kumgeuza mwanadamu asiitii sheria ya Mungu na kwa hiyo shambulio lake, lilielekezwa kwa amri ya nne ambayo inamtaja Mungu kuwa Muumbaji.

Sasa Waprotestanti husema kwamba ufufuo wa Kristo siku ya Jumapili, huifanya siku hiyo iwe Sabato ya Kikristo. Lakini hakuna heshima ya namna hiyo iliyotolewa na Yesu au mitume. Utunzaji wa Jumapili ulianza kwenye “Siri ya kuasi”. (2Thes. 2:7) ambayo ilianza kuonekana hata siku za Paulo. Itatolea sababu gani ya badiliko kama hilo, ambalo halikuidhinishwa na Biblia?

[16]

Katika karne ya sita askofu wa rumi alitajwa kuwa kichwa cha kanisa lote. Ukafiri umeingiza upapa. Joka amempa mnyama “uwezo wake na kiti chake, na mamlaka kuu” Ufu. 13:2.

[17] Sasa imeanza miaka 1260 ya mateso ya mapapa ambayo ilitabiriwa na Unabii wa Danieli 7:25 na Ufunuo 13:5-7. Wakristo walilazimika kuchagua moja kati ya mambo mawili. Kukana Imani yao na kukubaliana na mipango ya ibada ya Rumi; au kuteseka vifungoni na kupoteza maisha yao. Sasa maneno ya Yesu yalitimia, yasemayo: “Mtasalitiwa na wazazi, na ndugu na jamaa na marafiki; na baadhi yenu mtauawa. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu” Luka 21:16-17.

Dunia ikawa uwanja wa vita. Kwa miaka mamia kanisa la Mungu lilikuwa katika msukosuko mkuu. Watu wakawa wakiishi mafichoni tu. “Mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengezwa na Mungu, ili wamlishe huko Muda wa siku elfu na mia mbili na sitini” Ufunuo 12:6

Kule kutawala kwa kanisa la Kirumi kuliko wa mwanzo wa wakati wa Giza. Imani kwa Kristo iliamishwa kuwa kwa papa wa Rumi. Badala ya kumtegemea Kristo mwana wa Mungu kuwa ndiye mwondoa dhambi, na mwenye uzima wa milele, watu watalazimishwa kwa papa wa Rumi na kwa maaskofu ambao papa amewapa mamlaka. Papa alikuwa ndiye mwombezi wao. Kwao alikuwa kama Mungu. Mtu aliyepinga maongozi yake alistahili hukumu. Kwa njia hiyo mawazo ya watu waligeuzwa upande, kutoka kwa Mungu kuelekea kwa binadamu mwenye dhambi, aliye katili, na kwa mkuu wa giza mwenyewe ambaye hutumia uwezo wake kuwapotosha. Wakati maneno matakatifu ya Biblia yanapoachwa, mtu hujivuna na kujitukuza na kutumbukia katika upotofu.

Siku Za Hatari Kwa Kanisa

Watu waaminifu walioshikilia ukweli walikuwa wachache. Wakati fulani ilionekana kana kwamba ubaya utatawala na kufunika ukweli kabisa. Kiasi cha kutoweka nchini. Injili ilitoweka na watu walishikilia tu mambo yaliyoshurutishwa kufanya. Walifundishwa kutegemea matendo yao mema ili kuwatakasa, na kuwaondolea dhambi. Waliambiwa mambo mengi sana yawezayo kuwapatanisha na Mungu na kuwapa haki ya kuwa watakatifu mbele za Mungu.

Baadhi ya mambo hayo ni: kwenda safari ndefu za kuhiji, kulipa kitubio, kuabudu watakatifu kujenga makanisa, mahali patakatifu, madhabahu, kutoa mali nyingi kanisani. Mambo hayo yangewaletea upendeleo mbele za Mungu.

Panapo mwisho wa karne ya nane, wafuasi wa kanisa la Rumi (Roma Catholic) walidai kwamba kwenye karne za mwisho wa kanisa askofu wa Rumi alikuwa na uwezo katika mambo ya kiroho ambao unaonekana siku hizi. Maandiko ya kwanza yalikuwa yalikosewa na watawa. Maamuzi ya mabaraza ambayo yalikuwa hayajasikiwa yaligunduliwa, nayo yanamwezesha Papa kuwa na madaraka makuu ulimwenguni pote. Maamuzi haya ni ya mwanzoni kabisa. [18]

Waaminifu wachache ambao wanasimama katika msingi wa kweli (Kor. 3:10-11) walitatanika. Wakiwa wamechoshwa na mapambano ya daima juu ya kweli na uongo, na mateso yasiyokoma na matatizo ya kila aina ambayo shetani amewaletea, baadhi yao walikata tamaa. Kwa ajili ya kuhofia maisha yao na mali zao, waliacha unyofu wao, wakaondoka katika msingi wa kweli. Wengine walikuwa majasiri katika kupingana na adui zao.

Ibada ya sanamu ilienea pote. Mishumaa iliwashwa mbele ya sanamu, na watu walizifanyia ibada na maombi. Matendo ya kipumbavu yalienea kuhusu dini. Watu wakajifanyia mambo tu bila kufikiri. Wakati huo huo, maaskofu na makasisi walikuwa wameto-pea katika anasa na ufedhuli, ambavyo watu waliwatazamia katika kuwaongoza. Hivyo watu wakafungwa katika ujinga na ubaradhuli.

Katika karne ya kumi na moja, Papa Greory VII alidai kuwa kanisa kamwe halijakosa hata kidogo wala halitakosa kamwe kama maandiko yasemavyo. Lakini maandiko hayadhibitishi madai hayo. Hata papa wa Rumi mwenye majivuno pia adai kuwa anao uwezo wa kuwaondoa wafalme katika utawala. Kithibitisho cha majivuno hayo kilikuwa kivitendo kilichotendwa kwa mfalme wa ujerumani, Henry IV. Kwa kuwa hakujali Papa, alizuiliwa na kutolewa katika utawala kwa njia ya amri ya papa kuwaamuru watoto wake mwenyewe wamwasi.

Henry aliona kuwa ni lazima akaungame kwa Papa. Aliondoka Ujerumani yeye na mkewe na mtumishi wake mwaminifu wakasafiri kuvuka milima ya Alps wakati wa baridi, ili akajinyenyekeze mbele ya papa na kuomba msamaha. Alipofika kwa makao ya papa Gregory aliwekwa nje kwenye ukumbi wa baridi, pale akiwa hana

kitu cha kujifunika baridi na akiwa hana viatu alisubiri papa am-
ruhusu kufika mbele yake, huko ndani. Alingoja pale siku tatu
huku akiomba na kuungama, ndipo aliporuhusiwa kuingia ndani.
Hata hivyo aliruhusiwa kutawala kwa masharti. Hivyo papa Gre-
gory alijisifu kuwa anao uwezo wa kuweka na kuondoa kiburi cha
wafalme.

[19] Kuna tofauti kubwa kiasi gani baina ya mjivunaji huyu na Kristo.
Yeye anayejeleza mwenyewe kuwa anasimama mlangoni akingojea
kuingia. Kristo alifundisha kwamba: “Yeyote atakayekuwa mkubwa
kwenu, na awe mtumishi wenu”. Mathayo 20:27.

Jinsi Mafundisho ya Uongo Yalivyoingia.

Hata kabla ya kuingia upapa kanisani mafundisho ya kimizimu
yalionekana kupokewa kanisani. Watu wengi walikuwa na hali ya
mwenendo wa kimizimu, eti wapate kuwavuta wapagani kuingia
kanisani. Kwa njia hiyo makosa mabaya sana yaliingizwa kanisani.

Jambo kuu kati ya mafundisho haya ya uongo ni imani kwamba
mtu anayo hali ya kutokufa, na kwamba mtu akifa roho yake haifi.
Fundisho hilo ndilo lilikuwa msingi wa kanisa la Rumi kuimar-
isha sala ya wafu, na kumtumaini bikira Maria apate kuwaombea,
Kutokana na hapo uzushi ukaibuka kwamba kuna moto wa milele
utakaowateketeza waovu bila kuzimika.

Njia ikafunguliwa ya kuingiza uzushi mwingine, kwamba huko
ahera kuna mahali pa kutakasia dhambi (purgatory) ambao ni imani
ya wamizimu, inayotumika kuwatishia watu na kuwashikilia katika
hali ya ushirikina. Uzushi wa aina hiyo hudai kuwako huko ahera
kuna mahali pa mateso makali ambayo watu wanaokufa hupitishwa
humo kwanza mpaka watakaswe dhambi zao, ndipo huruhusiwa
kuingia mbinguni.

Kuna jambo jingine ambalo Rumi hilitumia ili kuzidi kuwao-
gofya wafuasi wake, nalo ni fundisho juu ya kusamehe dhambi.
Msamaha kamili wa dhambi uliahidiwa kwa wote ambao wange-
jiunga na papa katika vita vyake na adui zake, kwa njia ya kulipa
fedha kanisa, ambazo fedha za msamaha wa dhambi zote za za-
mani, na za sasa na zijazo. Basi walimwaga pesa ili kusamehewa
dhambi, na kuwaondoa rafiki na jamaa zao waliokufa ambao wamo
katika shimo la mateso. Kwa hiyo Rumi kajaza masanduku na pesa,

ambayo ziliwawezesha kuishi kifahari, na huku wakijidai kuwa wanamwakilisha yule ambaye hakuwa na mahali hata pa kulaza kichwa chake.

Huduma ya meza ya Bwana iliondolewa, badala yake akawekwa huduma ya kimizimu, yaani misa (mass). Makuhani wa papa wana-jidai kuwa hugeuza ule mkate na ile divai kuwa “mwili na damu ya Kristo halisi”. Kwa kufuru nyingi hujidai kwa kiburi kuwa wanao uwezo wa kumwumba Mungu na kumgeuza mkate na damu kuwa Mungu, ambaye ni Mwumbaji wa vitu vyote. Wakristo walilaz-imishwa kuinama na kutenda mambo hayo, kwamba ndiyo ibada ya mbinguni. [20]

Katika karne ya kumi na tatu lilianzishwa jambo jingine la kutisha la kipapa ndilo baraza kuu la kuwahukumu wapin-gaji. Katika mabaraza yao ya siri, shetani na malaika zake ndio waliowaongoza waovu hawa. Malaika wa Mungu alisimama katikati bila kuonekana akiandika mambo yote, historia yao yote, na maa-muzi yao ambayo ni ya kutisha. “Babeli mkuu amelewa kwa damu ya watakatifu” Ufunuo 17:5-6. Wafia dini mamilioni wanamlilia Mungu alipize kisasi kwa utawala huu mwasi.

Utawala dhalimu wa kipapa umetawala dunia. Wafalme wa wafalme humwinamia Papa kwa muda wa miaka mamia mafundisho ya Roma yamepokewa sana. Waongozi wake wameheshimiwa na kukubaliwa. Kanisa la Rumi halijastawi na kufaulu kama sasa.

Lakini, “adhuhuri ya upapa ilikuwa usiku wa manane wa ulimwengu”.

Maandiko matakatifu hayakujulikana. Waongozi wa kiapa wali-ichukia nuru isije ikafichua dhambi zao. Sheria ya Mungu, ambayo ni kipimo cha haki, ilipokuwa imeondolewa, waliishi kifedhuli bila wasiwasi. Majumba ya akina papa na maaskofu yalijaa zinaa na ufedhuli, na ufasiki. Baadhi ya maaskofu walikuwa na hatia ya uasi na uvunjaji wa sheria kiasi cha kutovumiliwa na watawala wa Serikali. Kwa karne nyingi ulaya haikuwa na maendeleo katika elimu, na ustaarabu. Maendeleo ya elimu na ujuzi vimekufa ganzi katika mahali pa Ukristo.

Hayo yamekuwa hivyo kwa sababu neno la Mungu lilipigwa marufuku.

Marejeo:

Cardinal Wiseman's Lectures on "The Real Presence" Lecture 8, sec. 3 para 26.

Wylie — History of Protestantism, Book 1, chapter 4.

4/Waldenses Waitetea Imani

[21]

Katika muda mrefu wa utawala wa upapa, kulikuwako na mashahidi wa Mungu waliothamini Imani katika Kristo kwamba ndiye Mwombezi na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu. Walishikilia mwongozo wa Biblia kuwa ndio kiongozi maishani, na kuitukuza Sabato ya kweli. Walidhihakiwa na kuitwa wazushi, maandiko waliyoandika yakapigwa marufuku na kuelezwa vibaya au kuharibiwa lakini walisimama imara tu.

Hawajulikani sana, isipokuwa mabarazani walikoshtakiwa. Walionekana kana kwamba ni wazushi, Rumi ilikusudia kuwaharibu wao au maandishi yao. Rumi pia ilijitahidi kuharibu kumbukumbu zote za mambo yao ya ukatili walivyowatendea wapinzani wao, yaani wale ambao hawakukubaliana na mafundisho yao. Kabla mashine za kuchapa vitabu hazijagunduliwa, vitabu vilikuwa vichache sana, kwa hiyo Warumi waliweza kuviharibu kwa urahisi na kuvimaliza. Muda si mrefu Papa alipata uwezo akafaulu kuwafuatilia mbali wale waliompinga.

Katika Uingereza ukristo uliingia na kustawi zamani sana, ambao haukupotoshwa na uasi wa Rumi. Mateso yaliletwa na watawala wakafiri, ndicho kitu kilichowapata huko England, walipata hifadhi huko Scotland. Na hivyo ukweli ukafika Ireland. Ukweli huo ulipokea kwa furaha na wenyeji wa nchi hizo.

Wakati watu wa Saxon walipovamia Uingereza, ukafiri ulipata nafasi ya kustawi huko, na hivyo wakristo walifukuziwa sehemu zilizo mbali. Kutoka Ireland alikuja Kolumba na wenzake ambao walifanya kazi yao na kuishi katika kisiwa cha Iona. Kati ya wahubiri hao alikuwamo mshika Sabato ya Biblia, na kwa hiyo Sabato ilijulishwa kwa watu. Shule ilianzishwa huko Iona, ambayo iliwatarisha wahubiri waliokwenda Scotland, Uingereza, Ujerumani na Uswisi na hata Italia.

Roma Yakutana na Dini ya Biblia

[22] Lakini Rumi iliazimu kuiweka Uingereza chini ya utawala wake. Katika karne ya sita wahubiri wake waliwageuza wapagani wa Saxon. Kazi ilivyozidi kuendelea waongozi wa papa walipambana na wakristo halisi wapole, wanyenyekevu, wenye kufuata Biblia, wenye tabia safi. Warumi walikuwa washirikina, watu wa fahari, wenye kiburi cha Kipapa. Rumi ilidai kuwa wakristo hawa hawana budi kumkiri papa na kujinyenyekeza kwake. Waingereza waliwajibu kuwa papa hasa hakuwa mkuu wa kansia, nao watamhesabu tu kama mtu wa kawaida. Hawajui bwana mwingine isipokuwa Kristo tu.

Sasa roho halisi ya upapa ilidhihirika. Kiongozi mmoja wa Rumi alisema: “Kama hamtaki kuwapokeeni ndugu wanaowaletea amani, mtawapokeeni maadui watakaowaleteeni vita! Vita na hila ndivyo vilitumiwa kwa wale walioitetea Biblia, mpaka waharibiwe kabisa, au wakubali kuacha imani yao na kufuata maongozi ya Rumi.”

Katika nchi ambazo zilikuwa mbali na utawala wa Rumi wakristo wa huko waliendelea na imani yao ya kweli bila kupotoshwa na mafundisho ya Rumi, kwa karne nyingi. Wao waliendelea kuiheshimu Biblia na kufuata mwongozo wake. Wakristo waliamini kuwa Sheria ya Mungu ni ya milele, walidumu kutukuza Sabato ya amri ya nne. Makanisa yaliyokuwa na kanuni hii yalionekana katika Afrika ya kati na katika Armenia katika bara la Asia.

Kati ya wale waliopingana na utawala wa papa, watu wa Waldenses walikuwa katika mstari wa mbele, mahali pale makanisa ya Piedomont yaliendelea na utaratibu wao sawia. Lakini wakati ulifika ambao Rumi iliwalazimisha waisalimu amri. Walakini hata hivyo baadhi yao walikataa kuanguka miguuni mwa papa, ila waliendelea kutunza unyofu wao. Ndipo mtengano ulitokea. Wale walioshikilia imani yao ya zamani walijitenga. Baadhi yao walihama makwao katika milima ya Alps wakaenda katika nchi nyingine na huko wakaendelea na imani ya wengine wakakimbilia milimani kwenye mapango na ngome za miamba, huko wakaendelea na imani yao na kumwabudu Mungu kwa uhuru.

Imani yao ilijengwa kwa Neno la Mungu. Wakulima wanyenyekevu hawa ambao wametengwa na ulimwengu hawakuupata ukweli huo kutokana na upinzani na upotovu wa Rumi. Imani

yao ilirithiwa toka kwa babu na baba zao. Waliendeleza imani iliyokuwa kwa kanisa la mitume. Kanisa la “Waldenses” wala sio kanisa la majivuno la Rumi, lilikuwa kanisa la kweli la Kristo, ambalo lilikuwa mtunzaji wa hazina kuu ya Mungu iliyotolewa kwa ulimwengu.

Baadhi ya sababu zilizosababisha mtengano na Rumi ilikuwa chuki ya Rumi kwa ajili ya Sabato ya Biblia. Kama ilivyotabiriwa katika Biblia, uwezo wa upapa uliikanyaga sheria ya Mungu mavumbini. Makanisa yalilazimishwa na mapapa kuiheshimu Jumapili badala ya Sabato. Katika makosa yaliyoenea ni kwamba, ingawa watu wa Mungu waliitunza Sabato, pia walistarehe na Jumapili. Jambo hilo halikuwaridhisha viongozi wa Rumi. Walidai kuwa Sabato ipigwe marufuku na kutangazwa kuwa haitakiwi tena wakiwalaani watu walioendelea kuitukuza.

[23]

Miaka mamia kabla ya matengenezo ya kanisa kuanza Waldenses walikuwa na Biblia katika lugha yao. Jambo hili lilisababisha mateso yawakabili. Walilitaja kanisa la Rumi kuwa ni kanisa asi, Babeli wa mwisho. Walisimama kiume wakipinga upotofu wa kila hali, ingawa kufanya hivyo kulihatarisha maisha yao. Katika muda mwingi wa uasi Waldeses walipinga majivuno ya Rumi kwamba ndio wakuu wakapinga ibada ya sanamu na kuheshimu watakatifu wa zamani kuwa wanastahili kuabudiwa, waliendelea kuitunza Sabato ya kweli.

Waldenses hawa walipata makao nyuma ya majabali ya milima na chini ya mapango ya miamba, walijificha. Wakimbizi waaminifu hawa, waliwaonyeha watoto wao vilele vya milima vilivyoinuka juu, na kuwasimulia habari za Mungu Muumbaji, ambaye neno lake linadumu milele kuliko milima mirefu hiyo. Mungu ameiweka milima: Hakuna mkono wowote uwezao kuitikisa, isipokuwa uwezo wa Mwenyenzi tu ndio uwezao kuondoa. Kwa hali hiyo hiyo ameweka sheria yake ya milele isiyoweza kuondolewa. Ni rahisi watu kuing’oa milima, kuliko yodi moja ya sheria ya Mungu. Wasafiri hawa hawakunung’unika kwa ajili ya taabu yao, maana katika makao yao ya milima hawakujikuta upweke. Walifurahia uhuru wao wa kumwabudu Mungu. Walimsifu Mungu kwa furaha katika miamba mirefu iliyowazunguka, na majeshi ya warumi hayakuweza kuwanyamazisha wasimwimbie Mungu.

Kanuni za Kweli Zilithaminiwa

Walithamini kanuni za ukweli kuliko nyumba, na mashamba, jamaa, na marafiki, hata maisha yao wenyewe. Tangu kuzaliwa watoto walifundishwa kuheshimu madai ya sheria ya Mungu. Biblia zilikuwa chache; kwa hiyo walifundishwa kukariri na kuweka mioyoni maneno matakatifu ya Biblia. Wengi waliweza kukariri sehemu kubwa ya Agano la kale na Agano Jipya.

[24] Walizoezwa kuvumilia taabu tokea utoto, na kujitegemea katika mambo mengi. Walizoezwa kushika madaraka, kuangalia usemi wao na kuelewa hekima ya kuwa kimya. Neno moja la kipumbavu linaaweza kuleta hatari kwa jamii nzima. Maana watu waliotetea uhuru wa dini waliwindwa sana, sawa na mbwa wa mwitu anavyowinda mawindo yake.

Waldenses walifanya kazi sana kwa uvumilivu ili kujipatia chakula chao. Kila kipande cha nchi milimani, ambacho kilifaa kulimika, kililimwa kwa uangalifu. Watoto walifundishwa kutotumia mali ovyo ovyo. Walifundishwa kuwa na tabia ya kujinyima. Walifundishwa kwamba uwezo wao wote ni wa Mungu. Kwa hiyo wautoe kwa kazi yake.

Makanisa ya Vaudois yalikuwa na imani sawa na makanisa ya siku za mitume. Walishikilia mafundisho ya Biblia tu kuwa ndiyo mwongozo usiokosea, na waliyapinga majivuno ya mapapa kuwa ndiyo mawakili wa Mungu. Wachungaji wao walilisha kundi la Mungu, wala hawakuwa kama mabwana wa Rumi walivyokuwa. Mafundisho yao yalikuwa katika neno la Mungu tu. Watu walikutanika, si katika majengo matukufu, au katika makanisa makubwa yaliyopambwa sana, ila walikutana katika mabonde ya milima chini ya miti, na wakati wa hatari, katika ngome imara milimani, ili wapate kusikia neno la Injili toka kwa watumishi wa Mungu. Walijitahidi kutembelea wagonjwa na kusistiza mfumo wa upendo wa ndugu. Walifanana na Paulo mtengenezaji wa mahema, nao kila mtu alijifunza aina fulani ya ufundi ili aweze kujisaidia kwa njia hiyo.

Vijana walipata mafundisho toka kwa wachungaji wao. Biblia ndiyo ilikuwa kitabu cha mafunzo. Injili ya Mathayo na Yohana pamoja na nyaraka nyingine vilikaririwa na kuwekwa vichwani.

Walijitahidi kuandika maneno matakatifu kwa shida sana, wakati mwingine ndani ya mashimo wakimulika na tochi (kurunzi), au vi-

jinga vya moto. Waliandika fungu kwa fungu. Malaika wa mbinguni waliwazunguka watu hawa waaminifu.

Shetani aliwaongoza mapapa na maaskofu wao kulifukia, lakini kwa njia ya ajabu neno la kweli lilihifadhiwa, bila kupotoshwa kwa muda wote wa karne za giza. Neno la Mungu lilivuka salama katika mawimbi makali ya safina ya Nuhu iliyovuka salama, katika uharibifu. Sawa kama dhahabu na fedha hupatikana kwa kuchimba chini sana ndivyo neno la kweli la Mungu, ambalo ni hazina ya kweli hufunuliwa kwa watu wanyenyekevu, walitafutao kwa bidii kwa njia [25] ya maombi. Mungu alikusudia kuwa neno lake yaani Biblia, kiwe ndicho kitabu cha mafunzo kwa wanadamu ili kimdhihirishe yeye mwenyewe. Kila ukweli unaojulikana ni ufunuo kamili wa tabia ya Mwenyewe.

Vijana wa Waldeses walipomaliza masomo katika shule zao, walitumwa katika shule za Ufaransa na Italia kuendelea na mafunzo ya juu zaidi. Vijana waliotumwa namna hiyo walihatarisha maisha yao, maana walikabiliana na majaribu mengi. Walikabiliana na madanganyo ya shetani, na mivuto mingi ya ufedhuli. Lakini mafundisho waliyopata katika utoto wao huko kwao, yaliwalinda wakasimama imara.

Katika shule hizo walikokwenda hawakuweza kuiga ukorofi wa aina yoyote. Mavazi yao yaliweza kuchukua hazina ya Maandiko matakatifu waliyokuwa nayo, yaani Biblia iliweza kuchukuliwa bila kuonekana; na kwa njia hiyo waliweza kuwafundisha na kuwapa watu wengine waliokuwa na haja ya kujua ukweli. Katika shule hizo waliweza kuongoa watu, na mara nyingi kanuni ya kweli ya msimamo wao iliweza kuenea katika shule nzima. Viongozi wa kipapa hawakuweza kugudua hali kama hiyo ilikotoka.

Vijana Walifundishwa Kuwa Wahubiri

Wakristo wa Vaudois walijisikia kuwa na wajibu wa kuangaza nuru yao kusiko na nuru. Kwa uwezo wa neno lake Mungu walitafuta kuvunjilia mbali utumwa ulioletwa na Rumi. Wachungaji wa Vausois walifanya kazi nje ya nchi yao muda wa miaka mitatu, kabla ya kurudi nyumbani kufanya kazi huko. Kufanya kazi nje kulivasaidia kuwa wahudumu bora wafaa kukabili hali zote. Vijana hawakuona kuwa watu wa fahari, au matajiri, bali waliowaona kuwa

watu wa kufanya kazi ngumu, wakikabili hatari kwa ujasiri, na mara nyingine kupoteza maisha yao. Wahubiri hawa walikwenda wawili wawili sawa kama wale waliotumwa na Yesu.

[26] Kazi hiyo ya kutangaza ukweli wa neno la Mungu iliwahatarisha kabisa, kuwafanya wapingwe na Rumi. Kila mchungaji alijua kazi fulani ya ufundi, hivyo kila mchungaji alifanya kazi ya kuhubiri, huku akifanya kuwa ni fundi wa aina fulani au mfanya biashara. Walichukua nyuzi za hariri, lulu, na vitu vingine, kana kwamba ni wafanya biashara, na kumbe ni wahubiri. Walichukua Biblia au sehemu ya Biblia na kuzificha sana zisionekane, na kwa hekima wakaingiza mafundisho ya Biblia kwa watu kwa njia ya siri. Ilipobidi wakaacha maandiko matakatifu kwa watu waliotaka.

Wahubiri hawa walisafiri katika miji mingi, wakienda kwa miguu na bila viatu, wakiwa na mavazi hafifu. Katika njia zao walimopita makanisa yalijitokeza na damu ya wafia dini ilikuwa mashahidi wa ukweli. Neno la Mungu lilipokelewa kimya kimya katika mioyo ya watu na katika nyumba za watu.

Waldenses waliamini kuwa mwisho wa ulimwengu hauko mbali sana. Walivyokuwa wakisoma Biblia, waliona kuwa wana wajibu wa kuwaonya watu wengine. Walifarijika sana na kujiona kuwa na amani kuu kwa ajili ya kumwamini Yesu Kristo. Nuru ya Injili iliyowamulikia, waliona haja ya kuwamulikia waliokuwa gizani katika vifungo vya mapapa.

Watu wengi walifundishwa na mapapa kuwa matendo yao mema yanatosha kuwaokoa. Kwa hiyo daima walijitumaini. Walijitesa kwa kila hali katika mchafuko wa dhamira zao za dhambi, bila kuona furaha yoyote. Watu maelfu waliishi katika majumba ya watawa, walifunga mara kwa mara, na kujitesa, kukesha usiku kucha, kusu- judu, na kujigaragaza katika unyevu, kukalia mawe yenye majimaji kwenda safari ndefu na kadhalika. Walirudia mambo hayo mara kwa mara, bila tumaini lolote mpaka dhamira zao zikafilisika, na mwisho wakaingia makaburini bila chembe ya faraja.

Wenye Dhambi Kutazamishwa Kwa Kristo.

Waldenses walitamani kuwapa masikini hawa ujumbe wenye imani katika ahadi za Mungu na kuwatazamisha Kwa kristo ambaye ndiye tumaini lao la pekee la wokovu. Mafundisho wanayoshikilia

kwamba matendo mema ya mtu yatamwoko, ni mafundisho ya uongo. Neema ya mwokozi aliyekufa na kufufuka ndiyo msingi wa dini ya Kikristo. Matengenezo ya watu kwa Kristo, lazima yawe na mshikamano wa hakika kama vile mbavu zinavyoshikamana na mwili, au kama tawi linavyoshikamana na mti.

Mafundisho ya mapapa na maaskofu yamewapotosha watu kiasi cha kumwona Mungu na hata Kristo kuwa ni wakatili sana, wasio na huruma, kwa hiyo lazima maaskofu na mapadri wawepo ili kuombea wenye dhambi. Wale waliofunguliwa giza hilo wakaona nuru ya Injili, hutambua kuwa mtu lazima amwendee Mungu moja kwa moja bila kupitia kwa mwombezi wa kibinadamu, aungame dhambi zake, naye atapata msamaha na amani moyoni mwake.

[27]

Kushambulia Ufalme wa Shetani.

Wahubiri wa Vaudois waliendelea kutoa sehemu za Maandiko Matakatifu kwa uangalifu. Nuru ya Injili ilipenya kwa watu wengi, mpaka Jua la haki likang'aa mioyoni mwa watu kwa nguvu za kuponya. Kila mara aliyesikia neno alitamani apate sehemu ya Maandiko, ili ahakikishe yale aliyosikia.

Wengi waliona upuuzi wa maombezi ya watu yaliyofanywa na mapadri kwa wenye dhambi. Wengi walisema kwa furaha, “Kristo ndiye Kuhani wangu. Damu yake ndiyo kafara yangu, madhabahu yake ndilo ungamo langu” Kwa hiyo nuru kuu iliwaangazia watu wengi, ambao ilionekana kana kwamba inawapeleka mbinguni. Hofu yote ya kifo ilitoweka. Sasa walikuwa tayari kuingia gerezani, ikilazimu kwa ajili ya Mwokozi wao.

Neno la Mungu lilisomwa kwa siri, wakati fulani kwa mtu mmoja tu pengine kwa kikundi cha watu, kilichotamani kupata nuru. Wakati mwingine usiku kucha ulitumika kwa kujifunza Biblia kwa njia hiyo. Mara nyingi maneno haya yalitamkwa: “Je, Mungu ataikubali kafara yangu? Je, ataifurahia? Je, atanisamehe?” Majibu kwa maswali hayo yalisomwa: “Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha” Mathayo 11:28.

Wahubiri hao walirudi nyumbani kwao kwa furaha ili kuen-deleza nuru ya Injili, na kuwasimulia wenzao mambo waliyoona.

Waligundua njia safi ya kuwafurahisha na kuwafariji. Maandiko matakatifu yalizungumza katika roho za watu walioyatamini.

Mjumbe wa kweli alikwenda zake. Na mara nyingi hakuulizwa kama atarudi au hatarudi. Watu walikuwa wamejazwa na furaha ya mshangao hata hawakuwa na nafasi ya kumwuliza maswali. Walijiuliza kwamba: Huenda akawa ni malaika aliyetoka mbinguni?

Wakati mwingine mjumbe wa Injili atakuwa amekwenda katika nchi nyingine, au anateseka gerezani, au amekwisha kufia dini na mifupa yake imetawanyika. Lakini maneno anayoyasema kabla ya kuondoka yanaendelea kutenda kazi.

Waongozi wa kipapa waliona hatari itokanayo na watumishi hawa wa Mungu. Waliona kuwa nuru ya Injili inayomulikwa na watu hao itaweza kuenea na kuondoa giza ilililowafunika watu. [28] Nuru hiyo itawaelekeza watu kwa Mungu peke yake, na kuharibu majivuno ya Rumi.

Watu hawa walioshikilia imani ya kanisa la kwanza walikuwa ushindi wa kufunua uongo wa Rumi na uasi wake. Kwa hiyo chuki na mateso yalitokea. Kule kung'ang'ania ukweli wa biblia kukataa kukubaliana na Rumi, kulichemsha chuki na vita.

Rumi Yaazimu Kuwaadhibu Waldenses

Sasa ulianzishwa mpango hatari wa kuwasaka watu wa Mungu katika maficho yao ya milimani. Wapelelezi waliwekwa ili kuwachunguza, Basi mara kwa mara, na tena na tena walishambuliwa na kuvurugwa. Makao yao na makanisa yao yaliharibiwa. Watu hawa hawakupatikana na uhalifu wa aina yoyote, isipokuwa walishitakiwa, eti kuwa ibada yao haifuati taratibu za papa. Na adhabu ya kosa hilo ilikuwa mateso makali mno ya ukatili usiosemeka.

Rumi ilipoazimu kuliondolea mbali dhehebu hilo la Wakristo wa Waldenses, tangazo lilitolewa na papa kuwa watu hawa wahesabiwe kuwa wazushi, na hukumu yao ni kuchinjwa. Hawakushitakiwa kwa kosa la uvivu, au uhaini au watangatangaji, bali walishitakiwa kwa kosa la uzushi, wenye kupotosha kondoo, kutoka katika zizi la kweli. Tangazo hilo lilitaka washiriki wote wa kanisa la Rumi kuhusika na kazi ya kuwaharibu wazushi hao. Kivutio kilichowekwa ni kwamba Wote wa watakaoshiriki kazi hiyo watakuwa huru kwa kila jambo wanalodaiwa, kama walikuwa na kesi yoyote iliyofanywa na watu

wa Vaudois ilifutwa, na watu wote walikatazwa kutoa msaada wa aina yoyote kwao. Watu wakaruhusiwa kuwanyanga'anya mali zao bila kizuizi. Tangazo hili lilidhihirisha ghadhabu ya joka, wala siyo sauti ya Kristo. Roho ile ile ilimsulubisha Kristo na kuwaua mitume, roho ya kikatili ya Nero kwa watu wa Mungu, ndiyo hiyo iliyowaongoza kuwaangamiza watu wapendwa wa Mungu.

Ingawa mipango ya kuwaangamiza ilikuwa ikitekelezwa lakini watu hawa hawakuacha kutumia wahubiri ili kuendeza ukweli wa Biblia. Waliwindwa sana na kuuawa, lakini damu yao ilikuwa ndiyo maji ya kuotesha mbegu ya Injili.

[29]

Hivyo ndivyo Waldenses walivyomshuhudia Mungu Kabla Martin Luther hajatokea. Walipanda mbegu ya matengenezo ya kanisa yaliyoanza siku za Wycliffe yakakuwa mpaka wakati wa Luther, na yataendelea mpaka mwisho wa wakati.

Marejeo:

J.H. Merle D'Aubigne — History of Reformation of Sixteenth Century, book 17, chap. 2

Wylie, book 1 chap 7.

Ibid, book 16, chap. 1.

5/Nuru Yapambazuka Uingereza

Mungu hakuacha neno lake liharibiwe kabisa. Katika nchi kadhaa wa kadhaa za Ulaya watu waliamshwa na roho wa Mungu ili watafute ukweli kama watafutavyo hazina iliyosetirika. Hasa wakielekea kwenye Neno Takatifu la Biblia, walikuwa tayari kuli-fuata bila kujali vitisho. Ingawa hawakuuelewa ukweli wote. Wali-gundua mambo mengine yaliyofichwa kwa muda mrefu.

Wakati ulikuwa umefika ili neno la Mungu liweze kutolewa kwa lugha za watu, kila mtu lugha yao. Ulimwengu ulikuwa umekaa gizani, na sasa mapambazuko yalikaaribia.

Katika karne ya kumi na nne, nyota ya asubuhi ya matengenezo ya kanisa ilitokea katika Uingereza. John Wycliffe alionekana katika chuo kikuu kuwa mcha Mungu sana na mwenye akili. Chuoni alijifunza utaalumu wa sheria na mambo ya dini. Mambo hayo yalimwandaa kwa kazi kubwa iliyokuwa mbele yake na uhuru wa dini. Alikuwa na elimu nzuri na kanuni imara. Hali hiyo ilimpatia heshima kwa rafiki zake na adui zake pia. Maadui zake walishindwa kudharau kazi ya matengenezo ya kanisa aliyokuwa akishughulikia, kwa ajili ya ujinga waliokuwa nao. Wycliffe alipokuwa angali mwanafunzi chuoni alikuwa akijifunza maandiko matakatifu. Wycliffe aliona upungufu mwingi sana ambavyo hakuweza kupata mahali pa kumridhisha. Katika neno la Mungu alipata jawabu la haja yake ambayo ameitafuta sana bila mafanikio. Hapa katika Biblia ndipo aliona kuwa Kristo ndiye Mwombezi wa pekee wa binadamu. Kwa hiyo alikusudia kuitangaza kweli hiyo aliyogundua.

Wycliffe hakuanza kazi hiyo na upinzani na Rumi mara moja. Lakini kwa kadiri alivyozidi kuona wazi makosa ya mapapa, ndi- vyo alivyoweza kufundisha ukweli hasa kama ulivyo katika Biblia. Aliona kuwa Rumi imekataa kufuata Biblia, ila inafuata hadithi za kibinadamu tu. Aliwalaumu mapadri kwamba hawafuati Biblia. Akasema kwamba Biblia lazima ifundishwe kwa watu na kufu- atwa kama katika kanisa. Alikuwa mhubiri hodari, na maisha yake yalishuhudia mambo yale aliyohubiri. Ujuzi wake wa maandiko

matakatifu, maisha yake ya utawa, na ujasiri wake, vilimpatia usikizi wa watu wote. Watu wengi waliona makosa ya kanisa la Rumi. [31] Wakaikubali wazi kweli iliyohubiriwa na Wycliffe, lakini waongozi wa mapapa walijazwa na ghadhabu; wakasema, mtu huyu anapata heshima kuliko yetu.

Mwepesi Kugundua Kosa.

Wycliffe alikuwa mwepesi wa kugundua kosa na kulitaja wazi bila hofu, ingawa Rumi ililitetea. Wakati alipokuwa kasisi wa mfalme, Wycliffe alipinga kwa ushujaa malipo ya ushuru ambayo papa alidai kwa mfalme wa Uingereza. Majivuno ya papa kwamba anayo mamlaka hata kwa watawala wa nchi, yalikuwa kinyume cha haki na maadili.

Madai ya papa yalichochea uchungu tu kwa watu, lakini mafundisho ya Wycliffe yalituliza watu. Kwa hiyo mfalme na mawaziri walikataa kulipa ushuru uliodaiwa na papa.

Maskini waombaji wa watawa walijazana Uingereza, wakatia kasoro ukuu na umaarufu wa taifa. Maisha ya watawa ya kivivu, na hali ya kuombaomba mabarabarani hayakupunguza mapato ya watu tu, bali yalileta hali ya kufanya kazi ionekane kuwa duni. Vijana walipotoshwa na kuharibiwa. Wengine walijiingiza katika hali ya kuwa watawa, bila kuruhusiwa na wazazi wao, bila wao kujua kile wanachotenda. Hali hii ya ufedhuli, ilitokeza hali ya kinyama kabisa, kama Luther alivyoisema baadaye.

Hata wanafunzi wa Chuo kikuu walishawishiwa na hawa watawa wakubali kufuata njia zao. Walipokwisha kunaswa ilikuwa vigumu kujinasua. Wazazi wengi walikataa kutuma watoto wao katika vyuo. Shule zilididimia, na ujinga ulistawi.

Papa alikuwa amewapa watawa hawa uwezo au idhini ya kusikia maungamo ya watu na kuwasamehe makosa yao. Jambo hilo ni asili ya uovu mkuu. Watawa hawa walijitahidi sana kuachilia makosa ya kila namna kwa watu ili kuongeza mapato yao maana mambo yote yalifuatana na malipo. Zawadi zilizowastahili wagonjwa na maskini, ziliingia mifukoni wa hao watawa. Utajiri wa hao watawa uliongezeka na ustawi wao na hali yao ya kianasa ilifilisi taifa. [32] Walakini watawa hao waliendelea kuwashikilia watu katika hali ya ushirikina, na kuwafanya waamini kuwa shughuli zote za kidini

ni kutambua utawala wa papa na kuitukuza heshima ya watakatifu pamoja na kutoa vipaji kwa watawa. Kutenda mambo hayo kulitosha kuwafikisha mbinguni.

Wycliffe akielewa vizuri, aligonga kwenye mzizi wa uovu, akieleza kuwa kawaida hiyo wanayoshikilia na kuiamini ni uongo mtupu, kwa hiyo lazima iachwe, na iondolewe. Mahubiri ya Wycliffe yaliamsha maswali na mawazo ya watu. Wengi walitaka kujua kama ni sawa kutafuta msamaha wa Mungu, au msamaha wa papa wa Rumi. “Watawa pamoja na maaskofu wa Rumi walisema, watu hawa (Wycliffe) wanatutafuna kama kanisa Mungu lazima atuokoe, au sivyo taifa litapotea” Watawa hao waombaji alisema kuwa wanafuata kielelezo cha Yesu na wanafunzi wake, ambao waliishi kwa kupata misaada ya upendo wa watu wasome Biblia ili waone ukweli ulivyo.

Wycliffe alianza kuandika vijizuu na kuvitoa kwa watu ili kuyapinga madai ya watawa na kuwaeleza watu katika mafundisho ya Biblia. Hakuna njia nyingine ambayo Wycliffe alitumia kubomoa ngome ya uongo iliyojengwa na Rumi kuwashikilia watu katika ujinga.

Wycliffe aliyeitwa kutetea haki ya taji ya Uingereza kwa maingilio ya papa, alichaguliwa kuwa balozi wa Netherlands. Hapo Wycliffe alikutana na mapadri kutoka ufaransa, Italia na Spain. Ali-pata nafasi ya kuona ndani ya pazia yaliyokuwa yamefichika kwake alipokuwa Uingereza. Wajumbe hawa wa papa walionyesha tabia halisi. Baadaye alirudi Uingereza na bidii mpya ya kuendeleza mafundisho yake. Alitangaza kuwa huko Rumi ni majivuno na udanganyifu tupu ndivyo vilivyoko. Hivyo ndivyo mungu wao.

Aliporudi uingereza Wycliffe aliwekwa na mfalme kuwa kasisi wa Lutterworth. Jambo hili lilithibitisha kuwa mfalme hakuchukizwa na mahubiri yake ya wazi. Mvuto wa Wycliffe ulienea katika nchi yote.

Ngurumo za papa zilikuwa tayari kumlipukia Maazimio matatu ya papa yalitangazwa ili kumnyamazisha kimya huyo mzushi, mwalimu wa uongo.

Matangazo ya papa yalipofika Uingereza yaliamuru kumfunga gerezani huyo mzushi.

[33] Ilionekana wazi kwamba Wycliffe karibu angeingia hatarini. Lakini yule aliyemwambia mtu wa zamani kuwa, “Usiogope. . . . Mimi ni

ngao yako” Mwa. 15:1 Aliunyosha mkono wake kumlinda mtumishi wake. Kifo hakikumpata mtengenezaji wa mambo ya kanisa, bali kilimpata papa aliyeamuru kufungwa kwa Wycliffe.

Kifo cha Gregory XI kilifuatiwa na uchunguzi wa mapapa wawili ambao walioshindana sana. Kila mmoja alijitahidi kuwataka wafuasi wampinge mwenzake na kutoa laana kubwa kwa mwenzake, na kuahidi zawadi kubwa za mbinguni kwa wasaidizi wake. Walishindana wao kwa wao siku nyingi. Kwa hiyo kwa muda Wycliffe alipata kustarehe kidogo wakati walipokuwa kipingana wao kwa wao.

Mafarakano hayo pamoja na uovu wote ulioletwa nayo yalitayarisha njia kwa matengenezo ya kanisa, maana watu waliona wazi maongozi ya upapa jinsi yalivyokuwa. Wycliffe aliawaambia watu wafikiri na kuona kama mapapa mawili hao na mashindano yao si hakika kwamba wao ni wapinga Kristo!

Wycliffe akikusudia kueneza nuru ya Injili kote katika nchi, alianzisha makundi ya wahubiri, ambao ni watu waongofu wa kweli waliokuwa tayari kueneza ukweli, Watu hawa walihubiri sokoni, katika njia kuu za mjini, waliwafikia wazee na wago-njwa, na maskini wakawasomea habari njema za neema ya Mungu.

Katika chuo cha Oxford Wycliffe alihubiri neno la Mungu katika ukumbi wa chuo. Alitunukiwa heshima ya kuitwa Daktari wa Injili (Gospel Doctor). Lakini kazi kubwa aliyoifanya maishani mwake ni ile ya kutafsiri Biblia katika lugha ya Kiingereza ili kila mtu wa Uingereza aweza kusoma maajabu ya Mungu katika lugha yake.

Alishikwa na Ugonjwa wa Hatari.

Kazi ya Wycliffe ilisimama kwa ghafla. Ingawa alikuwa hajafikia umri wa miaka sitini, kazi ngumu aliyoifanya, na shughuli za kuji-funza, pamoja na mashambulio ya adui zake vilimdhoofisha sana na kuchakaza afya yake. Mara akashikwa na ugonjwa wa hatari sana. Watawa walidhani kuwa ataungama maovu aliyotenda kwa kupinga msimamo wa kanisa. Kwa hiyo walikwenda chumbani mwake wakitazamia kusikia maungamo yake. Wakamwambia, “Una mauti kinywani mwako. Jutia maovu yako, ukane mbele yetu maneno yote uliyotushutumia”

[34] Wycliffe aliyasikiliza maneno yao hali amenyamaza kimya. Kisha akawaomba wamwinue juu ya kitanda. Halafu akiwakazia macho, alisema kwa ujasiri, kwa sauti kuu iliyokuwa ikiwatetemsha mara nyingi, “Sitakufa, bali nitaishi na nitaendelea kushutumu maovu ya watawa” kwa fadhaha na aibu, watawa hao walitoka kwa haraka chumbani humo.

Wycliffe aliishi na kuweka mikononi mwa watu wa nchi yake silaha kuu ya kuwapigia Warumi, yaani Biblia ambayo ilipangwa na mbingu ili iwaweke huru watu na kuwaangazia na kuwahubiria. Wycliffe alifahamu kuwa imebaki miaka michache ya kufanya kazi hiyo; aliona mapingano yaliyomkabili, lakini akifarijiwa na ahadi za neno la Mungu aliendelea mbele bila kusita. Akiwa na juhudi na moyo wa utendaji, na ujuzi mwingi, alikuwa ameandaliwa na Mungu kwa kazi hii kuu. Wycliffe akiwa kasisi wa Lutterworth, bila kujali dhoruba iliyokuwa ikivuma alijitia kazini mwake kamili.

Mwishowe kazi ilikamilika yaani Biblia ya Kiingereza iliyotafsiriwa ikatokea. Mtengenezaji wa kanisa amefaulu kuwapatia watu wa Uingereza nuru ya neno la Mungu katika lugha yao, ambayo haitazimika kamwe. Ametenda makuu kwa kuvunja ngome ya ujinga na kuwapatia watu uhuru kamili na kuiangazia nuru nchi yake, kuliko shujaa apiganaye vita.

Biblia ilipatikana tu kwa njia ya shida na kazi ngumu. Watu walipenda mno kupata Biblia, hata ikawa hazitoshelezi haja ya watu. Matajiri walinunua Biblia nzima na wengine walipata sehemu ya Biblia. Mara nyingi watu wa familia fulani fulani walishirikiana kununua Biblia moja nzima. Hivyo Biblia ya Wycliffe ilipata njia ya kuingia katika nyumba za watu.

Sasa Wycliffe akafundisha mafundisho ya Kiprotestanti, tofauti na yale ya Kirumi yaana wokovu hupatikana kwa njia ya imani na kwamba Biblia ni kamili hasa haina kasoro. Imani hii mpya ilikubaliwa na kupokelewa na karibu nusu ya watu wa Uingereza.

Kuonekana kwa maandiko kulifadhaisha utawala wa kanisa. Kwa wakati huo haikuwako sheria ya kupiga marufuku Biblia huko Uingereza, maana Biblia ilikuwa haijatafsiriwa katika lugha ya watu. Sheria hiyo iliwekwa baadaye na kusistizwa sana.

Tena waongozi wa papa walifanya njama ya kunyamazisha huyu mtengenezaji wa Kanisa. Kwanza mkutano wa viongozi wa Rumi waliamua kuyaharamisha maandiko ya Wycliffe, yaani kuwa

itakuwa ni maandiko haramu. Walipomshawishi mfalme kijana Richard II akakubaliana nao hivyo amri ya kifalme ikatangazwa kuwa mtu ye yote ambaye angeendelea kutoa mambo hayo yaliyopigwa marufuku angetiwa gerezeni.

Wycliffe akaomba rufaa kutoka kwa waongozi mpaka kwenye Bunge. Bila hofu aliwashitaki maaskofu mbele ya Bunge la taifa, na akadai matengenezo yafanywe ili kanisa lisitiwe madoa namna hii. Adui zake waliduwaa. Ilitazamiwa kuwa Wycliffe katika uzee wake, akiwa mwenyewe bila rafiki, atashindwa. Lakini badala yake, bunge likisisimka kwa habari za Wycliffe, likayafuta mashitaka yote yaliyotupwa juu ya mtengenezaji wa kanisa. Kwa hiyo Wycliffe aliwekwa huru tena. [35]

Mara ya tatu Wycliffe aliletwa hukumuni tena. Safari hii katika baraza kuu katika ufalme. Hapo kazi ya Wycliffe ingekomeshwa; ndivyo mapapa walivyodhani. Kama wangekamilisha makusudi yao, Wycliffe angetoka barazani kwenda motoni.

Wycliffe Akataa Kukana Imani

Lakini Wycliffe hakukana imani yake na msimamo wake. Alishikilia msimamo wake na kuyakanusha mashitaka yao. Aliwaita wasikilizaji wake mbele ya baraza, na akapima hila na udanganyifu wa washitaki wake, na kuona kuwa maneno yao hayaafikiani na ukweli wowote. Uwezo wa Roho Mtakatifu uliwakalia wasikilizaji. Maneno ya Wycliffe yakachoma nyoyo zao kama mshale wa Bwana uhomavyo. Mashitaka waliyomshitaki kwamba ni mzushi yakawarudia wao wenyewe.

Akauliza, “Mnashindana na nani?” “Mnashindana na binadamu mzee aliyekaribia kuingia kaburini? La, mnashindana na ukweli, ukweli ulio na nguvu kuliko zenu, nao utawashinda” Alivyosema hivyo akaondoka, na wala hakuna mtu aliyethubutu kumzuia.

Kazi ya Wycliffe ilikuwa karibu imekamilika. Lakini mara moja tena alipaswa kutoa ushuhuda wa Injili. Alitakiwa afike mbele ya papa huko Rumi, ambako damu nyingi za watakatifu zilikuwa zimemwagwa. Lakini alipata ugonjwa wa baridi yabisi, kwa hiyo safari ya kwenda Rumi haikuwezekana. Walakini, ingawa sauti yake haikuweza kusikika Rumi aliweza kusikika kwa njia ya barua. Alimwandikia papa barua, ambayo iliandikwa kwa heshima na roho

ya Kristo, lakini ilikuwa yenye masuto kwa majivuno ya upapa na hali yao ya ufedhuli.

Wycliffe aliweka mbele ya papa na maaskofu wake upole na unyenyekevu wa Kristo, akithibitisha kuwa hivyo ndivyo hali ambayo wao na wakristo wote wanapaswa kuiga. Wao wanajidai kuwa wajumbe wake, hali hawafanani naye.

[36] Wycliffe alitazamia kuwa maisha yake yangekuwa kafara ya uaminifu wake, yaani angeuawa.

Mfalme, papa na maaskofu wote waliungana ili kumwangamiza. Na ilionekana kuwa isingepita miezi mingi kabla hajauawa. Lakini hata hivyo ujasiri wake haukutishika.

Mtu ambaye alikuwa ameitetea kweli maisha yake yote, asingekufa kwa ajili ya chuki ya adui zake. Bwana alikuwa mlinzi wake, na sasa wakati maadui zake walipoona wazi kuwa angeangamia, Bwana alimhamisha na kumweka mahali pengine mbali nao. Katika kanisa la Lutterworth, alipokuwa akiandaa huduma ya Meza ya Bwana, alishikwa na ugonjwa wa kupooza na kwa muda mfupi akakata roho.

Ujumbe wa mwanzo Mpya.

Mungu alikuwa ameweka neno la kweli kinywani mwa Wycliffe. Maisha yake yalilindwa na kazi yake ilirefushwa mpaka misingi ya matengenezo ya kanisa iliwekwa. Hapakuwa na mtu aliyemtangulia Wycliffe, ambaye aliweka kielelezo cha kazi ya matengenezo. Alikuwa mjumbe mwanzo mpya. Walakini ukweli alioutangaza ulikuwa na mwungano na ukamilifu, ambao wale waliofuata baadaye hawakupata cha kuongeza, na hata wengine hawakufikia pale. Kazi yake ilikuwa kamili na imara, haikuhitaji marekebisho.

Kazi kuu ya kuondoa watu katika giza la Rumi, ambayo Wycliffe aliianzisha inatokana na Biblia. Hapo ndipo mibaraka yote inapobubujika ambayo inawafikia watu waache ujinga na kuamini kuwa Rumi na mafundisho yake haikosei. Kwamba mambo yote ya Rumi lazima yakubaliwe bila swali. Mambo hayo yameshikwa kwa muda wa miaka maelfu. Wycliffe aliwafundisha watu kusikia sauti ya Mungu tu katika neno lake basi. Badala ya sauti ya kanisa kupitia kwa papa, lazima watu waitii sauti ya Biblia tu. Kwamba mtafsiri wa Biblia ni Roho mtakatifu, siye papa.

Wyclife alikuwa mtengenezaji wa kanisa mashuhuri kabisa. Alilingana na watu wachache tu waliomfuata baadaye. Alikuwa mtu mwongofu, hodari katika kujifunza, mwenye bidii kazini, na mwenye upendo wa kikristo, mwenye tabia safi, na mtangulizi katika watengenezaji wa kanisa.

[37]

Biblia ndiyo iliyomfanya awe jinsi alivyokuwa. Kujifunza biblia kutabadilisha kila wazo na fikra na kuhekimisha, ambavyo hakuna majifunzo ya namna nyingine yawezayo kufanya hivyo. Huuimarisha makusudi, na kuongeza ujasiri. Matakatifu kwa kicho, kutawapa watu wa ulimwengu ufahamu zaidi wa hali ya juu pamoja na kanuni bora kuliko vile vilivyopatikana katika vituo bora vya kufundishia ambavyo vinatumika ulimwenguni.

Wafuasi wa Wycliffe waliojulikana kama Wycliffites na Lollards, walitawanyika katika nchi nyingine wakiieneza injili. Sasa kwa kuwa kiongozi wao amefariki, wao walifanya kazi kwa bidii zaidi kuliko zamani. Makundi ya watu walifurika kuja kusikiliza. Watu mashuhuri hata mke wa mfalme walikuwa ni baadhi ya waongofu. Mahali pengi sanamu zilizofanywa na Warumi, ziliondolewa makanisani

Lakini muda mfupi tu baadaye, mateso ya kikatili yalilipuka kwa wale walioshikilia imani ya Biblia kama mwongozo wao. Kwa mara ya kwanza, katika historia ya Uingereza amri ilipitishwa kwamba wale wanaoiamini injili wachomwe moto, huku wakifungwa mitini. Mauaji ya kufia dini yakafuatana mfululizo: Waumini wa Injili wakawindwa kama maadui na wasaliti wa serikali. Walakini watu hawa waaminifu waliendelea kuhubiri kwa siri, mahali mahali waki-jifichaficha nyumbani mwa watu maskini na hata mbali mapangoni mwa milima.

Upingaji wa dini ya uongo na uharibifu wa kawaida zote zilioingizwa na Rumi uliendela kwa karne nyingi. Wakristo wa siku hizo walimpenda Mungu kabisa na kulitii neno lake na kwa hiyo walivumilia mateso kwa furaha. Wengi waliacha mali zao kwa ajili ya Kristo. Wale waliachwa kukaa salama, waliwasaidia ndugu zao walioteswa bila kinyongo. Na wao waliposhambuliwa na kufukuzwa hawakunung'unika. Wale walipata mateso kwa ajili ya ukweli wa neno la Mungu hawakuwa wachache. Na wote walifurahi kwa ajili ya kuteseka pamoja na Kristo.

[38] Mapapa hawakuridhika kwamba mwili wa Wycliffe umezikwa kaburini, la. Baada ya kupita miaka zaidi ya arobaini tangu Wycliffe afe, walichimbua mifupa yake wakaichoma hadharani ili kuonesha chuki yao na majivu yake wakayatupa mtoni. Mwandishi mmoja alisema, “Mto huo uliyachukua majibu hayo mpaka mto wa Avon, Avon mpaka Sevem, Sevem mpaka bahari ndogo, toka hapa yatafikishwa katika bahari kuu. Hivyo majivu ya Wyclife ni mfano wa mafundisho yake, ambayo sasa yametawanyika na kuenea ulimwengu.”

John Huss wa Bohemia aliongolewa na maandishi ya Wycliffe, akakataa makosa mengi ya Warumi. Kutoka Bohemia kazi iliendela na kufika katika nchi nyingine. Mkono wa Mungu ulikuwa unaandaa matengenezo makuu zaidi ya kanisa.

Marejeo:

Barnas Sears. *The Life of Luther*, pp. 69-70

D’Aubigne, bk 17, ch.7

Augustus Neander, *General History of Christian Religion and Church Period 6*, sec. 2 pt 1. para 8.

D’Aubigne, bk 17, ch. 7

Wylie, bk. 2, ch. 13

T. Fuller — *Church History of Britain*, bk. 4. sec 2, para 54.

Mapema katika karne ya tisa Biblia ilikuwa imetafsiriwa na kutawanywa kwa watu wa Bohemia. Ibada ya hadhara ilikuwa ikifanyika kwa lugha ya Wabohemia. Gregory VII alikusudia kuwatia watu utumwani. “Basi tangazo lilipotolewa la kupiga marufuku ibada ya hadhara katika lugha ya Bohemia ilifanyika katika lugha isiyojulikana” Lakini mbingu imeandaa watunzaji wa kweli yake, yaani kanisa. Watu wengi wa Waldenses na Albigenses walifukuzwa na mateso wakakimbilia Bohemia. Walifanya kazi sirisiri, kwa bidii. Kwa hiyo imani ya kweli ilihifadhiwa hapo.

Kabla Huss hajatokea walikuwapo watu huko Bohemia walioyalaani maovu yaliyokuwa kanisani. Hofu ya maaskofu iliamshwa na mateso yakatokea juu ya injili. Baada ya muda amri ilitolewa kwamba watu wanaoabudu kinyume cha maongozi ya Rumi, lazima wachomwe moto. Lakini wakristo walitazama kufaulu kwa imani yao. Mmoja alipokuwa akichomwa alisema, “Atatokea mmoja katika watu, bila silaha wala cheo, wala hawatamshinda” Mmoja alikuwa anatokea tayari, ambaye ushuhuda wake juu ya Rumi, utayataharukisha mataifa.

John Huss alizaliwa katika jamaa ya kawaida tu, na alifiwa na Baba yake mapema sana, akakua katika hali ya yatima. Mama yake ambaye ni mcha Mungu, aliyeyathamini mafundisho sana, aliazimu kuyapitisha kwa mwanawe. Huss alisomea katika shule za kawaida za kwao halafu akaingia katika chuko kikuu cha Prague, akipokewa kama mtoto yatima.

Katika chuo kikuu Huss alisonga mbele kimaendeleo. hali yake ya upole ilimpatia heshima pote. Alikuwa mfuasi mwenye juhudi wa kanisa la Rumi. Alijitahidi kuzingatia mafundisho yote yaliyotelewa nao. Alipohitimu mafundisho ya Chuo kikuu aliingia kazi ya ukasisi. Alivyopanda upesi na kupata cheo aliungana na baraza la mfalme. Alifanywa kuwa mwalimu mtaalamu, baadaye akawa mkuu wa Chuo Kikuu. Mtoto yatima aliyeingia chuoni kwa rehema, amekuwa mkuu katika nchi yake na jina lake likajulikana katika Ulaya yote.

[40] Jerome, ambaye baadaye alikuwa mshiriki wa Huss, alileta maandiko ya Wycliffe kutoka Uingereza. Malkia wa Uingereza, ambaye aliongolewa na mahubiri ya Wycliffe alikuwa binti wa Bohemia. Kwa njia ya mvuto wake, kazi ya matengenezo ya kanisa ilienea katika nchi yake. Huss alielekea kuipenda kazi ya matengenezo ya kanisa. Alikuwa ameingia tayari katika barabara ambayo ingemwondoa kutoka Rumi, ingawa hakujua vizuri wakati huo.

Picha mbili Zilimvutia Huss

Wakati ule ule wageni wawili walitoka Uingereza wenye elimu, walikuwa wamepokea nuru ya Injili, nao wamekuja kuendeleza Prague. Haukupita muda mrefu, wakanyamazishwa, lakini kwa kuwa hawakutaka kuacha kusudi lao, wakatimia njia nyingine. Kwa kuwa walikuwa wachoraji wa picha pamoja na kuhubiri, wakachora picha mbili. Moja ilionyesha maingilio ya Yesu katika Yerusalemu, akiwa mpole, amepanda mwanapunda, (Mathayo 21:5) akifuatwa na wanafunzi wake wakiwa na mavazi ya viwi hivi na bila viatu. Picha nyingine ilikuwa na msafara wa Papa, akiwa na mavazi yake rasmi na taji yenye kung'aa akipanda farasi aliyepambwa vizuri, akitangulia na wenye matarumbeta, na kufuatwa na maaskofu katika mavazi yao rasmi.

Watu wakakusanyika kuja kuangalia picha zao. Hakuna mtu ambaye alikosa kuzitambua. Kulikuwa na msukosuko mkubwa huko Prague, hata ikabidi wale wageni waondoke na kwenda zao. Lakini picha zile zilimwingia Huss moyoni sana, hata ikabidi asome sana maandiko ya Wycliffe na kuyatafakari.

Ingawa alikuwa bado hajakubali mafundisho yote ya Wycliffe aliona tabia halisi ya papa, naye akalaani majivuno, kutakabari, na upotovu wa upapa.

Prague Iliwekwa Chini ya Karantini

Habari zilifika Rumi, na Huss akaitwa mbele ya papa. Kama akienda matokeo ni kifo tu. Mfalme na malkia wa Bohemia jamii ya Chuo Kikuu, watu mashuhuri wa wakuu wa serikali wote wakaungana kumsihi papa amwache Huss akae Prague asiende Rumi ili ajibu kwa kutuma mjumbe. Badala yake papa alitoa hukumu ya

Huss na akautangazia mji wa Prague kuwa umewekwa chini ya karantini. [41]

Hukumu ya papa katika

kipindi hicho iliwashtua watu. Watu walimhesabu papa kuwa mwakilishi wa Mungu, kwamba yeye anazo funguo za mbinguni na za kuzimuni pia na waliamini kuwa papa asipopendezwa, hawezi kumtoa mtu aliyekufa kutoka ahera na kuingia raha ya milele. Huduma zote za kidini zilikomeshwa. Makanisa yalifunga. Ndoa zilifungiwa katika uwanja wa kanisa. Wafu walizikwa bila kufanyiwa ibada, na wakazikwa popote mahandakini au mbugani.

Prague ilijaa ghasia nyingi. Watu walimlamu Huss, wakasema kuwa atolewe aende Rumi. Ili kutuliza ghasia, Huss aliondoka akaenda kwao kijijini. Lakini hakukoma kufanya kazi yake, ila alisafiri safari akiwahubiria watu waliopendezwa. Ghasia zilipopungua huko Prague Huss alirudi huko kulihubiri neno la Mungu. Maadui zake walikuwa hodari lakini Malkia pamoja na watu wengine mashuhuri walikuwa rafiki zake, na watu wengi pia walikuwa upande wake.

Huss alisimama mwenyewe katika kazi. Halafu Jerome aliungana naye. Watu hawa wawili waliungana kikamilifu hata mauti haikuwatenga. Sifa bora ndizo zilizofanya tabia zao zifae, Huss alikuwa nazo zaidi. Jerome ambaye alikuwa mnyenyekevu alikubaliana na Huss kamili. Wote kwa pamoja wakaieneza kazi ya matengenezo ya kanisa na kuisukuma mbele.

Mungu aliwajalia watu hawa kupata nuru, na kuwaonyesha makosa mengi ya kanisa la Rumi. Walakini hawakupata nuru yoyote iliyotakiwa kutolewa kwa ulimwengu. Mungu alikuwa akiwaongoza watu polepole kutoka katika giza la Rumi, hatua kwa hatua maana wasingeweza kupata yote mara moja na kuyachukua. Ni sawa na mwanga wa jua kwa wote walio gizani, huwazukia kidogo kidogo, ama kama nuru ingewazukia yote ingewapoteza. Kwa hiyo Mungu aliwafunulia taratibu.

Farakano kanisani liliendelea. Sasa mapapa watatu walikuwa wakishindania ukubwa. Mashindano yao yalileta fujo nyingi katika ukristo. Hawakutosheka na kulaumiana peke yake, lakini kila mmoja alitafuta silaha na askari. Bila shaka fedha zilikuwa lazima zipatikane. Kwa hiyo zawadi, vyeo na mibaraka ya kanisa vikatolewa kwa kuuzwa.

Kwa ujasiri Huss akaunguruma kuhusu machafuko hayo ambayo ni machukizo yanayoleta aibu kwa dini. Akashambulia kwa ushujaa kabisa. Watu wakailaumu Rumi wazi kuwa inaaibisha dini.

[42] Mara tena Praggue ikaonekana kuwa kwenye ukingo wa kumwaga damu kwa mapambano. Kama ilivyokuwa zamani mtumishi wa Mungu alivyolaumiwa kuwa “Mtaabisha Israeli” 1 Fal. 18:17. Mji ukawekwa tena chini ya karantini na Huss akaondoka kwenda kwao kijijini. Ilimpasa aseme kwa nguvu zaidi kuhusu ukristo kabla hajauawa kama mashahidi wa kweli.

Baraza kuu liliitishwa kukutana huko Constance (Kusini Magharibi ya Ujerumani). Liliitishwa kwa matakwa ya mfalme Sigismud, kwa ajili ya mmoja wa wale mapapa watatu, aitwaye John XXIII. Papa John, mwenye tabia ya vivi hivi, ndiye alishika kazi ya uchunguzi. Naye hakuweza kupinga matakwa ya mfalme Sigismund. Kusudi la baraza hili lilikuwa ni kutafuta njia ya kumaliza farakano lililomo kanisani; na kung’olea mbali mizizi ya uzushi. Wale mapapa wawili aliokuwa wanashindana walitakiwa wafike barazani pamoja na John Huss. Wale mapapa waliwakilishwa na wajumbe. Papa John alikuwa na wasiwasi sana, akiogopa asije akatakiwa kueleza sababu za kuhafifisha umaarufu wa taji yao na heshima yao. Walakini aliingia katika mji wa Constance kwa fahari na kishindo akifuatana na makasisi, na wafuasi wa mfalme. Juu ya kichwa chake alikuwa na chombo cha dhahabu kikishikiliwa na mahakimu wanne. Mkate wa kufanyia ibada ya pasaka ulikuwa umechukuliwa mbele yake na mavazi ya maaskofu na wakuu wote, yalikamilisha onekano la fahari kuu.

Wakati huo huo msafiri mwingine pia alikuwa akija Constance. Huss aliagana na rafiki zake akienda Constance kana kwamba hawataonana kamwe. Alisafiri safari ambayo alijisikia kana kwamba anakwenda kuchomwa moto kwenye mti. Alipata mlinzi kutoka kwa mfalme wa Bohemia na mwingine toka kwa Mfalme Sixmund. Lakini alijitayarisha kwa kifo.

Mlinzi Toka kwa Mfalme

Katika barua aliyowaandikia rafiki zake alisema, “Ndugu, zangu ninaondoka nikiwa na mlinzi toka kwa mfalme ili nikakutane na maadui wengi wenye kufisha. Yesu aliteseka kwa ajili ya wapenzi

wake; je, sisi tutaona ajabu kufuata kielelezo chake? Kwa hiyo wapendwa, ikiwa kifo changu kitamtukuza, ombeni basi ili kije upesi, na kwamba aniwezeshe kusimama kiume katika matatizo yote. . . . Hebu na tuombe kwa Mungu... kwamba nisivunje hata neno moja la heshim ya Injili, ili niwaachie ndugu zangu kielelezo safi cha kufuata”.

[43]

Katika barua nyingine, Huss alisema kwa unyenyekevu makosa aliyofanya ya kufurahia kuvaa mavazi ya fahari na muda liopoteza kwa kufanya mambo hafifu. Akaongeza, Hebu utukufu wa Mungu, na wokovu wa watu vijaze mawazo yenu, wala siyo mali na mashamba. Jihadharini na kupamba nyumba zenu kuliko kupamba mioyo yenu na zaidi ya yote kazaneni na mambo ya kiroho. Mwe wacha Mungu na wanyenyekevu, mkichukuliana na maskini. Msi-malize mali zenu kwa ulafi.

Huko Constance Hus alipewa uhuru kamili. Pamoja na mlinzi wa mfalme, papa pia alimwongezea ulinzi zaidi. Lakini pamoja na hayo yote amri ilitoka kwa Papa kwamba Huss akamatwe na kutiwa kifungoni. Baadaye alihamishwa na kufungiwa ngomeni ng’ambo ya mto Rhine, na huko akawa mfungwa hasa. Halafu papa naye alitiwa kifungoni katika ngome ile ile alimokuwa Huss. Alipatikana na hatia ya ufedhuli, uuaji, biashara haramu ya uasherati. Dhambi ambazo hazifai kutajwa kwa mtu kama yeye. Baadaye alinyang’anywa kofia yake ya heshima. Hata wale mapapa waliokuwa wakishindania ukubwa waliondolewa pia, akachaguliwa papa mwingine.

Ingawa papa mwenyewe amepatikana na dhambi kubwa kuliko Huss kama alivyoshitakiwa na mapadri, hata hivyo baraza lile lile lililowashusha mapapa kwa ajili ya ukorofi wao, liliendelea kumwangamiza Huss, mtengenezaji wa kanisa. Kufungwa kwa Huss kuliamsha uchungu mwingi katika nchi ya Bohemia. Mfalme akakataa kwa ujeuri kwamba Huss asishitakiwe. Lakini maadui wa Huss wakaleta mashitaka kwamba, yeye hana imani bali ni mzushi. Wakaendela kushindilia mambo kwake, ingawa alikuwa na ulinzi toka kwa wafalme.

Huss akiteseka kifungoni, mahali penye unyevu, alipata ugonjwa uliomdhoofisha sana. Walakini hata hivyo aliletwa mahakamani kujibu mashitaka. Alisimama mbele ya mfalme akiwa na pingu mikononi na miguuni. Mfalme alikuwa na huruma kwake tangu hapo. Huss alitetea ukweli na kuyataja maovu ya maaskofu wa

[44] Rumi Dhahiri. Alipoulizwa kuchagua kati ya kukana imani yake na kuchomwa moto akifungwa mtini, alichagua kufa kuliko kukana ukweli wa imani yake.

Neema ya Mungu ilimsaidia. Wakati alipokuwa anangoja mwisho wake, alikuwa mtulivu na amani ya Mungu ilimjaza. Alisema, “Ninaandika barua hii nikiwa gerezani mkono wangu ukiwa na pingu, huku nikingojea utekelezaji wa hukumu juu yangu kesho. . . . Wakati tutakapokutana kwa neema ya Mungu huko paradiso, katika maisha ya baadaye, utaelewa jinsi Mungu mwenye rehema alivyojidhihirisha kwangu, jinsi alivyonisaidia, katika majaribu na katika dhiki.”

Ushindi Unaonekana Kwa Njozi

Katika kifungo chake aliona ushindi wa imani ya kweli ki-mawazo. Katika ndoto alimwona papa na maaskofu wakiondoa picha ya Kristo ambayo aliyoichora kwenye ukuta huko Prague. Ndoto hiyo ilimwudhi, lakini kesho yake aliona ndoto nyingine yenye picha zaidi ya hiyo iliyofutwa. Aliona picha nyingi, tena zenye kung’aa zaidi zimechorwa kila mahali... Wachoraji... wakiwa wamezungukwa na kundi kubwa la watu wakisema, “Sasa Papa na maaskofu wake na waje waone, hawawezi kuzifuta tena” Mtengelezaji wa kanisa alisema, “Sura ya Kristo haiwezi kufutika kamwe. Wametaka kuiharibu, lakini itachorwa upya mioyoni mwa watu na wahubiri wa Injili vizuri zaidi kuliko mimi”

Mara ya mwisho, Huss aliletwa mahakamani, ambapo palikuwa pamejaa na penye fahari kuu. Palikuwako mfalme, wana wa kifalme, wajumbe, wakuu wa Roma, maaksofu, makasisi na kundi kubwa la watu.

Huss akitakiwa mara ya pili kutoa uamuzi wake: Kukana imani, au kufa, Huss alikanusha kwa nguvu kwamba msimamo wake ni ule ule na kushikilia imani yake. Akimkazia mfalme macho, alisema “Ninaazimu kusimama katika mahakama hii kwa nia yangu mwenyewe, nikiwa na haki ya kupata ulinzi wa taifa, na nikiwa na imani ya mfalme ambaye nasimama mbele yake.” Mfalme Sigismund akabadilika uso, kadri macho ya watu wote walipomtazama.

Baada ya kutamka maneno hayo, hali ya fedheha ilianza. Akisihiwa tena kukana imani, Huss alijibu huku akiwaelekea watu:

“Niutazame uso gani? Sio wa mbinguni? Naweza kutazama watu ambao niliwahubiri Injili ya kweli? La, nauhesabu wokovu wao kuwa una thamani zaidi ya mwili wangu huu wa kimaskini, ambao umetajwa kwamba ufe” Mavazi ya kikuhani yalianza kuvuliwa moja moja wakati maaskofu wakijitayarisha kumwua huku wakimlaani. Mwisho wakamvalisha kofia ya karatasi ya kiaskofu ambayo ilikuwa imechorwa sanamu za mashetani, maneno yaliyoandikwa kwamba: “Mzushi mkuu” kwa upande. Huss akasema “Furaha kuu”. Yesu, ninavaa taji hii ya aibu kwa ajili yako, ambapo wewe ulivaa taji ya miiba kwa ajili yangu.

[45]

Huss Achomwa Moto Mtini.

Sasa aliongozwa kwenda nje, Kundi kuu la watu lilimfuata. Matayarisho yote ya kuwasha moto yalikalilika, Huss alisihiwa tena ili aungame makosa ili ajiokoe. Akasema, “Nikane nini? Kuna kosa gani? Mimi sijui kosa lolote nililofanya”. “Namwita Mungu awe shahidi kwamba mambo yote niliyohubiri na kuyaandika, yalijihusu wokovu wa watu, ili waepukane na dhambi na wasipotee milele. Kwa hiyo ninayo furaha kuu kwa kuuthibitisha ukweli huo nilioandika na kuhubiri kwa damu yangu mwenyewe”.

Moto ulipowashwa katika mti alikofungiwa, alianza kuimba. “Yesu mwana wa Daudi unihurumie”. Aliendelea kuimba hivyo mpaka sauti yake ikaoma kwa milele, alipomalizikia katika ndimi za moto. Mfuasi wa Papa akizungumza baadaye, kuhusu kifo cha Huss na Jerome ambaye alichomwa moto baada ya Huss, akasema “Huss na Jerome walijitayarisha kwa kufa, kama wanavyojitayarisha kwa arusi. Hawakutoa neno la kulalamika kwa ajili ya maumivu. Moto ulipowashwa wao walianza kuimba. Wala ukali wa moto haukuweza kuzima sauti zao mpaka walipomalizikia humo. Mwili wa Huss ulipokwisha kutetekea majivu yake yalikusanywa na kutupwa katika mto wa Rhine, katika nchi zote mfano wa mbegu inavyotawanyika. Katika nchi ambazo hazikujua ujumbe wa Injili kutatokea matunda mengi, ushuhuda wa Injili. Sauti ya Huss iliyosikika katika mahakama ya Constance ilitoa mwangwi utakaosikika katika vizazi vijavyo. Kielelezo chake kilitia moyo wa imara kwa watu maelefu ili wakikabiliwa na kifo wasiogope. Kifo chake kimethibitisha

ulimwenguni ukatili wa Rumi. Maadui wa haki waliendeleza mbele kusudi lao la uharibifu!”

[46] Hata hivyo damu ya shahidi mwingine lazima ishuhudie ukweli. Jerome alikuwa amemia Huss moyo wa uthabiti, akisema, kwamba ikiwa itamlazimu apate hatari yeye atamsaidia. Aliposikia kuwa Huss amefungwa, Jerome alijitayarisha kutimiza ahadi yake. Hivyo alianza safari ya kwenda Constance bila kuwa na ulinzi wowote. Alipofika alijua kwamba aliingia hatarini na hatamsaidia lolote Huss. Alitoroka, lakini alikamwatwa na kurudishwa kwa pingu. Alipofikishwa mahakamani mara ya kwanza, usemi wake ulikutana na makelele ya mkutano yakisema, “Motoni, Motoni” Kisha alitupwa kifungoni akilishwa chakula haba. Ukatili aliotendewa ulimletea ugonjwa, nusura ya kufa. Hapo adui zake walikuwa na wasiwasi kwamba kama angekufa kwa ugonjwa, wangekuwa wamepoteza tazamio lao la kumchoma motoni, hivyo walimtunza ili asife. Alikaa kifungoni kwa muda wa mwaka mzima.

Jerome Asalimu Amri Mahakamani

Ukatili aliotendewa Huss uliwachukiza watu. Kwa hiyo mahakama ilikusudia kutomchoma Jerome, badala yake wamlazimisha kukana imani yake. Alipewa uchaguzi: Kukana imani au kuchomwa moto akifungwa mtini. Jerome, hali akiwa amedhoofishwa na ugonjwa, na mateso na kifungo na hali ya upweke, pamoja na masikitiko ya kifo cha Huss alisalimu amri. Aliahidi kushikamana na mafundsiho ya Rumi na kuwa na imani yao. Alikubali shauri la mahakama la kuyalaani mafundisho ya Wycliffe na Huss akikubali kuwa ni ukweli wote waliofundisha.

Lakini katika hali yake ya upweke kifungoni alitafakari na kuona alichofanya. Alifikiri juu ya ujasiri wa Huss na jinsi alivyovumilia msalaba kwa ajilia yake. Kabla ya kukana imani yake, alifikiri juu ya faraja aliyopata kwa Mungu katika mateso yake. Sasa alijuta, akaona uchungu moyoni mwake. Alijua kuwa kabla hajaafikiana na Rumi kuna mambo mengine anayotakiwa kuyafanya. Njia ambayo ameshika itamwingiza tu katika uasi mkuu.

Jerome Atubu na Kuwa na Ujasiri

Baada ya muda mfupi Jerome alifikishwa tena mahakamani. Kule kukiri kwa kwanza alikokiri kwamba ameacha imani yake, na kuwa atashikamana na mafundisho ya Rumi hakukuwaridhisha mahakimu. Angejiokoa tu, kwa maungamo kamili kuwa hana uhusiano tena na mafundisho ya kweli. Lakini aliazimu kukanusa maneno yake kwamba ameacha imani yake. Alikusudia kudhihirisha imani yake wazi na kufuata nyayo za mwenzake aliyechemwa moto. Kwa hiyo akafanya hivyo. [47]

Akataka apewe muda wa kujitetea vizuri kama mtu anayekuwa tayari kufa. Maaskofu walisisitiza kwamba Jerome alilaumu ukatili unaotendwa, bila haki, Akasema “Mmenifunga siku mia tatu na arobaini katika gereza chafu sana, mkasikiliza tu mambo ya adui zangu, na ya kwangu mkakataa kuyasikiliza. . . . Msinitendee dhambi, mkaiacha haki. Kwangu mimi, si kitu, mimi ni mtu dhaifu tu, na maisha yangu hayana maana yoyote, na ninapowasihi msinihukumu kikatili, hujisemea maneno yangu tu sio yenu”

Mwisho walikubali ombi lake. Jerome alipiga magoti mbele ya mahakimu, akaomba Roho wa Mungu ayaongoze mawazo yake, ili asiseme mapotofu. Kwake, siku hiyo ahadi ya Yesu ilitimia, kwamba: “Lakini hapo watakapowapeleka, msifikirifikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakavyosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni roho wa Baba yenu aliye ndani yenu” Mathayo 10:19-20.

Kwa muda wa mwaka mzima Jerome alikaa kifungoni, akiwa hawezi kuona wala kusoma. Hata hivyo alipozungumza wakati wa kujitetea, usemi wake ulikuwa wazi na wenye nguvu kama ulivyoandaliwa vema na mtu aliyekuwa na nafasi ya kujitayarisha. Alitaja orodha ndefu ya watu wema ambao walitendewa ukatili na mahakimu waovu. Katika karne zote, watu wanyofu walitafuta kuinua hali za watu walitupwa nje. Kristo mwenyewe alihukumiwa sawa na watenda maovu. Alihukumiwa na mahakimu wasio haki.

Sasa Jerome aliungama makosa aliyofanya safari ya kwanza, aliposema kuwa anaikana imani yake. Sasa alitoa ushuhuda wake wazi na kwamba msimamo wake ni sawa na ule wa Huss, aliyeuawa, yaani mfia dini. Alisema, “Nilimfahamu Huss tangu utoto wake. Alikuwa mtu maarufu, mwenye haki, na mtakatifu. Alihukumiwa,

walakini alikuwa mwenye haki Hata mimi niko tayari kufa. Sitayaepuka mateso yanayonikabili, ambayo yametayarishwa na adui zangu. Najua kuwa wao ni mashahidi wa uongo, ambao siku moja watatoa hesabu mbele za Mungu ya Matendo yao maovu, maana hakuna kitu asichojua”

[48] Jerome aliendelea kusema, “Dhambi zote nilizotenda tangu utoto wangu, hakuna hata moja inayonishitaki katika dhamira yangu, na kunijutisha, sawa na ile niliyofanya hapa wakati nilipowashutumu Wycliffe na Huss kuwa ni wazushi, hasa Huss ambaye ni bwana wangu na rafiki yangu. Ndiyo na ungama dhambi hiyo kwa moyo wangu wote, kwamba nilikosa kabisa niliposhuhudia kuwa mafundisho yao ni ya uongo, nikiogopa tu kufa. Kwa hiyo usemi huo naukanusha hasa. Mwenyenzi Mungu anisamehe, hasa dhambi hii.”

Akiwasonda mahakimu, alisema kwa ushujaa: “Ninyi mliwahukumu Wycliffe na Huss Kwa mambo ambayo hakika yasiyokanika Hata mimi pia nafikiri kama wao”

Hotuba yake iliingiliwa kati. Maaskofu wakiwa wamejaa ghadhabu nyingi, walipaza sauti na kusema “Tunahitaji ushahidi gani zaidi? Tumeona kwa macho yetu ukaidi wa mzushi huyu”.

Jerome akisimama imara alisema: “Ninyi, mnadhani kuwa mimi niliogopa kufa? Mmenifunga gerezani mwaka mzima mahali pabaya kabisa, panazidi kifo. Siwezi kueleza hali ya namna hiyo inayotendwa kwa wakristo”

Apangiwa Kufungwa na Kuuawa

Lakini yeye alijibu: “Nionyeseni fungu la Maandiko kuthibitisha kosa langu, nami nitakubali. Mmoja wa washawishi wake alisema,” Maandiko matakatifu ndiyo yenye kuhukumu kitu? Nani atayafahamu yasipotafsiriwa na kanisa?

Jerome akasema, Je, mapokeo ya wanadamu yanathaminiwa kuliko Injili ya Mwokozi? Akajibiwa kwa kishindo, “Mzushi!” Mmoja akasema “Nasikitika kuwa nimepoteza muda wangu bure kukusih, naona kuwa Ibilisi anakusukuma na amekujaza”

Kabla ya kupita muda mrefu aliongozwa kwenda mahali pale Huss alipochomewa. Alienda akiimba njia nzima. Uso wake uling’aa na alikuwa ametulia kabisa. Hofu ya mauti haikumtisha. Mwenye kuwasha moto alipokuwa tayari, Jerome alimwambia,

“Anzia kuwasha upande wa uso wangu, usianzie nyuma, maana kama ningeogopa moto nisingekuwa hapa.”

Maneno yake ya mwisho yalikuwa ni sala “Bwana mwenye uwezo, nihurumie. Unisamehe dhambi zangu maana unajua kuwa mimi nimependa kweli yako siku zote.” Baada ya kuteketea, majivu yake yalikusanywa na kutupwa katika mto wa Rhine, sawasawa na ya Huss. Ndivyo wajumbe wachukuzi wa nuru wa Mungu walivyopotea.

Kifo cha Huss kilileta hasira na ghasia katika Bohemia. Taifa lote lilimtaja kuwa mwalimu mwaminifu, afundishaye kweli ya Injili. Mahakama ilishitakiwa kwa kosa la kuuu. Mafundisho ya Huss yaliwavuta watu wengi kuliko hapo zamani. Na watu wengi waliamini. Basi papa na mfalme waliungana pamoja ili kuangamiza watu hawa wenye imani. Kwa hiyo majeshi ya mfalme Sigismund yalimwagwa Bohemia kwa kazi hiyo.

Lakini mkombozi alitokea Ziska, ambaye alikuwa amiri jeshi hodari sana, aliongoza majeshi ya bohemia. Watu hao wakiutumainia msaada wa Mugu waliweza kuyakabili majeshi makuu yaliyowavamia. Mfalme alivamia Bohemia mara nyingi na kila mara majeshi yake yalirudishwa nyuma kwa hasara kubwa. Wafuasi wa Huss walistushwa na kifo cha ukatili, wakawa wakali, wala hakuna kitu kilichoweza kusimama mbele yao. Shujaa Ziska alikufa, na mahali pake pakashikwa na shujaa zaidi jina lake Procopius.

Papa alitangaza vita na wafuasi wa Huss. Kwa hiyo jeshi kuu mno likapelekwa Bohemia kivamizi. Matokeo ni kuwa likashindwa vibaya kwa hasara kuu. Katika nchi zote za Ulaya mahali papa alipokuwa akitawala michango ilianzishwa ya fedha na mali, askari, zana za vita na kadhalika.

Basi jeshi kubwa mno likavamia Bohemia. Watu wakaungana kuwafukuza. Majeshi mawili yakakabiliana ila tu mto uli-watenga. Wavamizi walikuwa wengi mno. Badala ya kuvuka mto na kuwashambulia wafuasi wa Huss, walisimama wakiwatazama wapiganaji.

Kwa ghafla kishindo cha kimuujiza kikawaangukia wavamizi. Mara wakatawanyika kama wanafukuzwa na uwezo usiojulikana. Wafuasi wa Huss wakawakimbiza na kuwaangamiza wengi sana. Vita badala ya kuharibu Bohemia, ilitawisha.

Baada ya miaka michache chini ya papa mwingine, jeshi lika-

[49]

[50]

tumwa kuvamia Bohemia kwa mguu. Wafuasi wa Huss wakajifanya kukimbia ili wawavute adui waingie katikati ya nchi. Mwisho jeshi la Procopius likawashambulia. Hofu kuu iliwashika hata kabla Wahuss hawajafika. Watu wote wakuu, majemadari, askari wakakimbia huku wakitupa silaha zao chini. Mara hiyo tena wakaangukia mikononi mwa Wahuss.

Mara nyingine tena jeshi lililofundishwa lilipotumwa likakimbizwa na uwezo wa kimuujiza. Aliyempigania Gideon na watu mia tatu, ndiye aliyewapigania wafuasi wa Huss. Zaburi. 7:19-25, Zaburi 53:5

Walisalitiwa Kijanja

Viongozi wa papa mwishowe walitumia njia ya mazungumzo ya kijanja kama kwamba wana nia njema kumbe sivyo. Makubaliano yalifikiwa ambayo yaliwasaliti watu wa Bohemia, na kuwaweka chini ya mamlala ya Papa yaani utawala wa Rumi. Watu wa Bohemia walitaja masharti manne ya amani baina yao na Rumi (1) Uhuru wa kuhubiri na kufundisha Biblia bila kuingiliwa; (2) Haki ya kanisa zima kutumia mkate na divai wakati wa Meza ya Bwana, na uhuru wa kuabudu kwa kutumia lugha ya watu. (3) Waongozi wa kanisa (maaskofu, mapadri, makasisi na kadhalika) kutojihusisha na mambo ya serikali, wala kuchaguliwa kwenye madaraka serikalini. (4) Kuhusu uvunjaji wa sheria, mahakama za serikali ziwashughulikie wote, wanaohusika, kama ni askofu au mkristo wa kawaida. Utawala wa papa ulikubali mambo hayo manne, ila tu haki ya kuyaeleza na kuyafafanua iwe juu ya baraza ambalo huendeshwa na papa na mfalme. Rumi ikafanikiwa kwa njia ya udanganyifu na hila ambayo ilishindwa kwa njia ya kutumia nguvu. Katika kusafiri na kufafanua masharti ya watu wa Huss, papa alitumia ujanja wa kuyapotosha, na kuonekana kwamba yanatokana na Biblia. Hivyo alifaulu kwa hila kuendeleza upotofu wake.

Watu wengi wa Bohemia walipoona kuwa wamesalitiwa hawakukubali kushikana na mapatano hayo. Ugomvi ukazuka baina yao. Procopius alikufa. Na uhuru wa Bohemia ukaangamia.

[51] Mara nyingine tena majeshi ya kigeni yalivamia Bohemia na wale waliokuwa waaminifu kwa Injili walikabiliwa na mateso ya umwagaji damu. Hata hivyo walisimama kishujaa. Ingawa iliwalaz-

imu kukimbia mapangoni walidumu kusoma neno la Mungu na kuabudu. Kwa njia ya wajumbe watumwa kwa siri kwenda nchi yingine, walielewa kuwa katika milima ya Alps kulikuwepo na kanisa la watu waaminifu wacha Mungu wanaoshika kanuni ya Biblia na kuupinga upotofu wa rumi. Basi wakawa wakiwasiliana na Waldeses kwa furaha, maana ni wenzao katika ukristo.

Watu wa Bohemia wakishikilia kanuni za Biblia walisimama imara wakingoja na hata katika nyakati za giza la mateso makali walizidi kuwa imara kama walinzi wa usiku wangojavyo mapambazuko ya asubuhi.

Marejeo:

Wylie, bk 3, ch. 1 ibid

Bonnechose, Vol. 1 pp. 147, 148.

Ibid., pp. 148-149

Ibidi pp. 247

Jacques lenfant. History of Concil of Constance Vol. 1 p. 516

Bonnechose. Vol. 2p. 84

D'Aubigne, bk.1.ch. 6

Bonnechose, Vol. 2 p. 84

Wylie, bk. 3 ch.7

Ibid.

Ibid.

Bonnechose,, Vol. 1, p.234

Ibid. Vol 2 p. 141

Ibid. p. 146 — 147

Bonnechose, vol.2, p. 168

Wylie, bk. 3, ch. 10

Bonnechose, Vol. 2, p. 168.

Wylie, bk. 3, ch. 17

Ibid. ch. 18

Ibid. ch.19

[52]

7\Luther, Shujaa Kwa Wakati Wake

Katika watu waliotumiwa na Mungu kulitoa kanisa katika giza la upapa, na kuwaleta katika nuru ya kweli ya Biblia na imani halisi, Martin Luther ni mmoja wa hao katika mstari wa mbele. Hakujua kuogopa kitu kingine ila Mungu tu, wala hakujua msingi mwingine wa imani, ila ule uliomo katika Biblia. Alikuwa shujaa kwa wakati wake.

Alikulia katika jamaa ya mkulima katika nchi ya Ujerumani. Baba yake alikusudia kuwa afanye kazi ya uanasheria, lakini Mungu alimkusudia awe mjenzi wa hekalu lake ambalo lilikuwa likikua pole pole kwa karne nyingi. Shule ya Mungu iliyomfundisha Luther mpaka akahitimu ilikuwa shida, dhiki na maisha magumu sana.

Baba yake Luther alikuwa mtu hodari, mwenye nia thabiti. Mawazo yake yalimwamisha kuwa maisha ya utawa na kawaida zake, hayafai. Alichukizwa Luther alipoingia katika hali ya utawa bila kumwuliza. Ilipita miaka miwili kabla baba yake Luther hajap-atanishwa na mwanawe, hata hivyo nia yake ilikuwa ile ile.

Wazazi wa Luther walijitahidi kuwaelimisha watoto katika neno la Mungu. Juhudi yao ilikuwa ya kuendelea kuwatayarisha watoto wao wafae kutumika maishani, wakati mwingine walikazana kwa uaminifu hata Luther mwenyewe alipendezwa pia na nia hiyo.

Katika shule, Luther alitendewa kikatili. Mara nyingi alishinda na njaa. Hali ya mawazo ya kidini ilimwogofya. Alipolala usiku alikuwa na moyo wa huzuni. Mara nyingi alimdhania Mungu kuwa ni jitu kali lisilo na huruma, kwa wakosaji, kuliko Baba wa mbinguni mwenye huruma.

Alipoingia katika chuo kikuu cha Erfurt, alikuwa na hali nzuri kuliko kwanza. Wazazi wake wakiwa wamejiwekea akiba kidogo, waliweza kumsaidia katika mahitaji yake, na marafiki zake wema waliweza kumfariji ajione nafuu. Kwa njia hiyo hapa mawazo yake alipanuka. Kwa bidii yake mwisho akajikuta juu kati ya wenzake.

[53] Luter hakuacha kuomba kila siku. Roho yake ilikuwa na faraja na maongozi ya juu. Kila mara alisema “Kuomba vema ni bora, ni

nusu ya mafundisho”

Siku moja aligundua Biblia ya Kilatini katika maktaba ya Chuo Kikuu. Alikuwa hajaona kitabu hicho. Alikuwa amesikia sehemu ya Injili na nyaraka, ambazo alidhani kuwa ndizo Biblia kamili. Sasa kwa mara ya kwanza katika maisha yake, alisoma neno kamili la Mungu. Sasa kwa mara ya kwanza katika maisha yake, alisoma neno kamili la Mungu. Alisoma kwa kicho na mshangao mkubwa, huku akitulia mara ya kwanza na kusema, “Lo Mungu anijalie nipate Biblia yangu mwenyewe!” Malaika walikuwa karibu naye. Miali ya nuru ya neno la Mungu ilifunua hazina kuu katika mawazo yake. Akajiona wazi kuwa yu mwenye dhambi.

Amani na Mungu

Akitamani kuwa na amani pamoja na Mungu, Luther alijitahidi kuishi katika hali ya utawa. Katika hali hiyo alitakiwa kufanya kazi ngumu sana, yaani kutumika kitumwa, na kuomba omba vitu nyumba kwa nyumba. Alivumilia mambo hayo yote akidhani kuwa hivyo ndiyo njia ya kusamehewa dhambi zake.

Akitumika kwa jinsi hiyo, na kujinyima usingizi saa za kulala, na hata saa za kula pia. Luther alipendelea kusoma biblia kila alipopata nafasi hata kama ni kidogo. Alipata Biblia imefungwa ukutani kwa mnyororo, katika nyumba ya watawa, kwa hiyo alienda kuko kila mara ili kuisoma.

Aliishi maisha ya kitawa kweli kweli. Alifunga kila mara, na kukesha usiku kucha. Alijiadhibu mwenyewe ili kufukuza dhambi zilizomo ndani yake. Baadaye alisema, “Kama watawa wataingia mbinguni kwa njia ya kuishi kitawa, mimi bila shaka nitaingia. . . . Ikiwa inatakiwa zaidi ya haya, mimi nitaendelea hata kufa!” Pamoja na juhudi hizo zote, lakini Luther hakupata pumziko, wala faraja yoyote. Mwisho alifika ukingoni mwa kukata tamaa.

Ilipoonekana kwamba mambo yote yamekuwa kazi bure. Mungu alimwinulia mwenzi jina Staupitz. Huyu Staupitz, alimfunulia Luther neno la Mungu, mawazo yake yakafunguka.

Staupitz, alimshauri kumtazama Yesu, wala asijitumainie mwenyewe. Akamwambia “Badala ya kujitesa ili usamehewe dhambi, jikabidhi katika mikono ya Mwokozi. Mtumainie yeye na haki yake tu, ukitumainia dhabihu yake kwa ajili ya ondoleo la

dhambi zako. Maana alikufa ili tuishi. . . Mwana wa Mungu. . . Alifanyika kuwa mwanadamu ili kukupatia uhakika wa rehema za Mungu. . . Mpende yeye, maana yeye alikuwepo kwanza.” Maneno ya Staupitz yaliugusa moyo wa Luther, akapata faraja katika moyo wake wenye wasiwasi.

[54] Luther alipofanywa kuwa kasisi, alitwa kuwa mwalimu katika chuo kikuu cha Witttemberg. Alianza kufundisha juu ya Zaburi na Injili na Nyaraka kwa makundi ya watu waliokuwa na hamu sana kusikia. Staupitz akamshauri apande mimbarani ili ahubiri. Lakini Luther alijiona kuwa hastahili kuhubiri badala ya Kristo. Baada ya mashindano makubwa ndipo alikubali mashauri ya rafiki yake, yaani ahubiri. Alikuwa mtu hodari katika maandiko na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Maelezo yake ya wazi na ujuzi wake wa maandiko, viliwavutia watu katika kuzibua mioyo yao.

Wakati huo Luther akiwa bado mwana wa kweli wa Rumi, hakudhani kuwa atakuwa mwingine. Alipotakiwa kwenda kuzuru Rumi, alisafiri kwa miguu, akilala katika nyumba za watawa njiani. Alishangazwa fahari aliyoona. Watawa walikuwa wakiishi katika nyumba za fahari kabisa wakivaa mavazi rasmi yenye bei ghali sana, na kula chakula cha kianasaa kweli kweli. Mawazo ya Luther yakatatanika.

Baadaye, kwa mbali aliuona mji wa Rumi ukijengwa kwenye vilima saba. Akajitandaza chini akisema “Rumi mtakatifu Nakusalimu!” alizuru makanisa, akisikiliza hadithi za ajabu za mapadri na watawa na kushiriki katika kawaida zote zilizotakiwa. Kila mahali aliona mambo ya ajabu. Maovu yaliyoonekana kati ya viongozi, ufedhuli wa maaskofu vyote vilimstaajabisha. Alishangazwa na upotovu uliotendwa hata wakati wa huduma. Alikuta matendo ya uasherati ulevi na uchafu wa kila namna. Aliandika akisema hatuwezi kuwaza kwamba dhambi mbaya hizi hutendeka Rumi. Watu husema “Kama iko jehanam, Rumi imejengwa juu yake!”

Ukweli Juu ya Ngazi ya Pilato.

Msamaha umeahidiwa na papa kwa mtu yeyote atakayepanda ngazi ya Pilato kwa magoti. Yasemekana ngazi hiyo ililetwa kwa muujiza Rumi toka Yerusalemu. Siku moja Luther alikuwa akizipanda ngazi hizo, wakati aliposikia sauti kama ngurumo ikisema

“Mwenye haki ataishi kwa Imani” Warumi 1:17. Mara akasimama kwa hofu na mshangao. Tokea siku hiyo aliona dhahiri jinsi ilivyo upuuzi wa kutegemea matendo mema, kwa wokovu. Akageuzia Rumi uso wake, yaani akaondoa matumaini yake kwa Rumi. Tokea wakati huo nia ya mtengano wa Rumi ikazidi kukua mpaka akavunja uhusiano wote na kanisa la mapapa.

Baada ya kurudi kutoka Rumi Luther alipokea shahada ya juu [55] ya udaktari wa Biblia, yaani “Doctor of Divinity” Sasa alikuwa na uhuru wazi wa kushughulikia mambo ya Biblia kuliko zamani. Hayo ndiyo aliyopenda mno. Alikuwa amejawekea nadhiri kulihubiri kwa uthabiti neno la Mungu, wala siyo mafundisho ya mapapa. Sasa hakuwa mtawa wa kawaida tu, bali alikuwa mhubiri halali wa Injili, aliyelitwa kuwalisha kondoo wa Mungu ambao wanateseka kwa njaa na kiu ya neno la Mungu. Alitangaza kwa nguvu kwamba, wakristo lazima wapokee mafundiho kutoka kwa Biblia tu, wala si mahali pengine.

Makutano yenye hamu ya neno walimkusanyikia. Habari njema za upendo wa Mwokozi, na msamaha wa dhambi unaopatikana kwa njia ya damu yake vilijaza furaha katika mioyo yao. Huko Wittenberg nuru ya Injili ilikuwa imewashwa tayari, ambayo itazidi kung’aa mpaka mwisho wa wakati.

Lakini kuna mapambano baina ya kweli na kosa. Mwokozi wetu mwenyewe alisema, “Sikuja kuleta amani, ila upanga” Mathayo 10:34. Luther naye alisema badala ya kuanza matengenezo, “Mungu... ananisikuma kwenda mbele... Natamani kustarehe; lakini nimetupwa katikati ya machafuko na fujo”

Uuzaji wa Msamaha

Kanisa la Rumi lilifanya biashara ya neema ya Mungu. Chini ya ombi la kukusanya fedha za kujengea kanisa la Petro mtakatifu huko Rumi, vyeti vya msamaha wa dhambi vilitolewa kwa kuuzwa, kwa agizo la Papa. Kwa bei ya makosa kanisa lilijengwa ili kumwabudu Mungu. Jambo la namna hii ndilo lililochochea adui za papa wakaanzisha vita, vilivyotetemeshwa utawala wa Papa, na kuiondoa taji kichwani mwa papa.

Tetzel, ambaye aliwekwa huko Ujerumani ili auze vyeti hivyo vya msamaha wa dhambi, alipatikana na hatia ya kudhulumu watu

na kuasi sheria ya Mungu. Lakini aliwekwa kuajiri mradi wa askari wa kukodiwa na papa katika Ujerumani. Alijulikana kwa ulaghai wake wa kudanganya watu wajinga kwa hadithi za ajabu ajabu na kuwahadaa. Kama wangelipokea neno la Mungu wasingalidanganayika lakini Biblia iliondolewa kwao, kwa hiyo wakabaki tu katika hali ya ushirikina.

[56] Tetzal alipokuwa akiingia mji fulani mjumbe humtangulia na kutangaza “Neema ya Mungu na ya Baba mtakatifu imewafikieni”. Basi watu humkaribisha mwenye kufuru huyu kama kwamba ndiye Mungu hasa. Tetzal akipanda mimbarani, katika kanisa husifu sana vyeti vya msamaha na kusema kuwa hivyo ndivyo karama ya Mungu ya thamani kwa wanadamu. Husema kuwa kwa njia ya vyeti hivyo dhambi zote ambazo mtu atatenda baadaye husamehewa wala hakuna haja ya kutubu. Cheti kimekamilisha mambo yote. Aliwahakikishia wasikilizaji wake kwamba cheti hicho kina uwezo wa kuokoa mtu aliyekufa; mara ile fedha inapotumbukizwa katika kisanduku. Roho ya marehemu hupita moja kwa moja bila kuingia matesoni kwanza mpaka mbinguni.

Hivyo fedha na dhahabu vikamiminika katika sanduku la Tetzal. Wokovu ulipatikana kwa njia ya kuununua ulikuwa rahisi kuliko wokovu unaopatikana kwa njia ya kutubu. Imani na juhudi ya kupinga majaribu ya dhambi, mpaka upate mtu ushindi.

Luther alijazwa na hofu mno. Wengi hata katika watu wake walikuwa wamenunua vyeti vya msamaha. Mara wakaanza kumjia mchungaji wakiungama dhambi huku wakitazamia kupata ondoleo la dhambi kwa njia hiyo, wala si kwa njia ya kujuta na kuziacha, wakitumaini vyeti kwamba vitawakamilisha. Luther alikataa mambo hayo na kuwaonya kuwa wasipotubu kamili na kugeuka moyo, wataagamia katika dhambi zao. Wakamwendea Tetzal wakilalamika kwamba yeye waliyekwenda kumwungamia, amekataa vyeti vyao, hata wengine wakadai warudishiwe fedha yao. Yule mtawa Tetzal akatoa matusi mazito kwa hasira nyingi, akaagiza moto uwashwe uwanjani, na akasema kuwa ameagizwa na papa kumchoma mtu yoyote atakayeupinga mpango huo mtakatifu.

Kazi ya Luther Yaanza

Sasa sauti ya Luther ikawa ikisikika mimbarani, akitoa maonyo. Aliwaonya watu waziwazi ubaya wa tabia ya kutenda dhambi na ya kwamba mtu hawezi kwa bidii yake kujiondolea hatia ya dhambi, na kuondokana na adhabu yake. Hakuna njia nyingine ya kuondokana na hayo na kutuokoa ila tu ni toba ya kweli na imani kamili kwa Mwokozi aliyetufia. Neema ya Kristo haiwezi kununuliwa, ni kipawachabure. Akawashauri watu wasinunue vyeti vya msamaha ila wantazame mwokozi aliyesulubishwa kwa imani. Aliwasimulia jinsi alivyojitaabisha ili apate amani, lakini ikawa kazi bure, mpaka alipomwamini Kristo, ndipo akawa na amani na furaha.

Kadri Tetzl alivyoendelea na majivuno yake, Luther alikusudia kumpinga dhahiri. Kanisa la Wittenberg lilikuwa na vitu vya ukumbusho, ambavyo katika siku za sikukuu huonyesha. Msamaha kamili wa dhambi ulitolewa kwa wote waliofika kanisani, na kuungama. Mojawapo ya sikukuu za namna hiyo ilikuwa karibu kutokea. Luther pia akiungana na msafara huo wa kwenda kanisani, alikwenda akatundika katika mlango wa kanisa maneno tisini na matano yanayopinga uzaji wa vyeti vya msamaha.

[57]

Maneno hayo aliyoyatundika liwavutia watu wote. Waliosomwa na kukaririwa kila upande. Mji mzima ukataharuki. Ikaonekana wazi kuwa uwezo wa kusamehe makosa na kuondolea adhabu ya dhambi, haukutolewa kwa papa kamwe, au kwa mtu mwingine yeyote. Ikafahamika kuwa neema ya Mungu na msamaha wa dhambi ni bure kwa wote wanaotubu na kuamini.

Maneno ya Luther yalienea katika nchi yote ya Ujerumani na kwa muda wa majuma machache yalienea Ulaya yote. Watu wengi waliokuwa wafuasi kamili wa Rumi waliyasoma maneno hayo ya Luther kwa furaha kubwa. Wakatambua kuwa hiyo ni sauti ya Mungu. Wakaona kuwa Bwana amenyosha mkono wake ili awatoe watu katika upotovu unaoendeshwa na kanisa la Rumi. Wakuu wa nchi na mahakimu walifurahia kisirisiri kwamba kumetokea kigingi cha kusimamisha majivuno ya upotovu wa Rumi.

Makasisi wenye hila walipoona kuwa pato lao linahatarishwa, walichukizwa mno. Hivyo Luther akakabiliwa na washitaki wenye uchungu sana. Aliposhitakiwa alisema “nani hajui kuwa ni mara chache mno, mtu kuweka kitu kipya bila... kushitakiwa kuwa

mchafuzi? Kwa sababu walifanya mambo mapya bila kwanza kujinyenyekeza na kupata idhini ya wakubwa”.

Maalum ya adui za Luther, na kumwelewa kwao vibaya na chuki yao juu yake, vilimfurikia kama gharika. Yeye alitumaini kuwa viongozi watamwunga mkono, kwa hiyo alitulia tu. Katika jaribio lake, aliona matumaini mema na kuamsha kanisa.

Lakini sasa matumaini mema yamegeuka kuwa maalum. Wakuu na viongozi wengi wa kanisa waliona kuwa maneno hayo ya kweli waliyapokea yatadhoofisha mamlaka ya Rumi maana yatakomesha mafuriko ya fedha zinazokuja kwa hazina yake, na hivyo utukufu wa Rumi utafifia.

[58] Kufundisha watu wamtazame Kristo pekee yake kutaangusha utawala wa papa na mwishowe kuangamiza mamlaka yake. Kwa hiyo wakakataa ukweli huu wa kumtazama Kristo kwa kumpinga mtu aliyetumwa na kuwaleta nuru.

Luther alitetemeka alipojifikiria. Mtu mmoja kupingana na uwezo mkuu katika nchi. Aliandika na kusema: “Mimi ni nani nishindane uwezo mkuu wa papa. . . ambaye wafalme wa nchi na ulimwengu wote humtetemekea?”... Hakuna ajuaye jinsi moyo wangu ulivyofadhaika katika muda wa miaka miwili hii, na jinsi nilivyokata tamaa na kuzama. Lakini msaada wa kibinadamu uliposhindwa alitazama kwa Mungu peke yake. Aliweza kutulia kwa amani katika mkono wa Mungu mwenye nguvu zote. Akimwandikia rafiki yake Luther alisema, “Wajibu wako wa mwanzo ni kuanza na maombi... usitumaini kitu chochote kutoka kwako, kwa uwezo wako, au kwa akili zako. Mtumaini Mungu kamili, katika mvuto wa Roho wake”. Hilo ndilo fundisho kwa watu wote wanaojisikia kuwa wameitwa na Mungu kutoa ujumbe wa kweli kwa wakati huu. Katika mashindano na maovu kunahitajika uwezo zaidi ya ule wa kibinadamu na hekima zaidi ya kibinadamu.

Luther Asimama Na Biblia Tu

Wakati adui za Luther walipokuwa wakitetea mapokeo ya kibinadamu, Luther yeye aliwapinga kwa njia ya kutumia Biblia tu. Nao hawakuweza kumshinda. Kutokana na mahubiri na maandishi ya Luther, machache ya nuru ya Injili yalianza kutokea. Nuru hiyo iliwamulikia watu maelfu. Neno la Mungu lilikuwa kama upanga

mkali ukatao kuwili, uliokata mioyo ya watu. Macho ya watu yalifumbwa na mapokeo ya kibinadamu kwa muda mrefu, yalifumbuliwa, wakaacha matumaini ya bure ya kuwatumaini watu ili wapate wokovu. Wakamtumaini kwa imani Kristo, Mwokozi aliyewafia.

Mwamko mkuu huo uliwaogofya watawala wa kipapa. Ndipo Luther akapokea, “kuitwa shaurini” huko Rumi. Rafiki zake walifahamu hatari ya kwenda Rumi ambako kumejaa mauaji ya watakatifu. Wakamshauri asiende Rumi, ila shauri lake lisikilizwe Ujerumani.

Jambo hilo lilikubalika na papa akatuma mjume ili alisikilize huko Ujerumani. Mjumbe alifahamishwa kwamba Luther amekuwa mzushi tayari. Kwa hiyo lazima ashitakiwe bila kuchelewa. Mjumbe alikabidhiwa madaraka ya kumhamisha katika Ujerumani nzima, kumtia kizuizini na kumlaani, kumpiga marufuku na kumtoa katika umoja wa kanisa. Kuwaharamisha watu wote wanaoungana naye. Kuwazuia wote katika vyeo vyote walivyonyavyo kanisani na serikalini isipokuwa mfalme atakayepuuza kumkamata Luther na wafuasi wake na kuwatoa wakabidhiwe Rumi.

Hakuna alama ya ukristo wa kweli iliyoonekana katika hati hiyo, wala aina yoyote ya haki. Luther hakuwa na nafasi ya kujitetea, na kuonyesha sababu ya msimamo wake. Walakini alitajwa tu kuwa ni mzushi, na kuhukumiwa pale pale.

Wakati Luther alipokuwa mpweke, na kuhitaji mwenzi, Mungu alimtuma Melanchthon huko Wittenberg, ili amsaidie na kumshauri. Hali ya Melanchthon na tabia yake imara pamoja na hekima yake, vilimpatia sifa njema iliyokubaliwa na watu wote. Mara moja mtu huyo akawa mwenzi mpenzi wa Luther. Uangalifu wake, uaminifu wake na upole wake vilikuwa sifa za kumtia moyo na nguvu Luther.

Huko Augsburg palikuwa pamechaguliwa kuwa mahali pa kusikiliza mambo ya Luther. Na Luther akasafiri kwa miguu kwenda huko. Vitisho vilikuwa vitolewa kwamba ataviziwa njiani na kuuawa, kwa hiyo rafiki zake walimsihi asijihatarishe kusafiri. Lakini jibu lake lilikuwa “Mimi ni mtu anayetaka kuwa mhubiri wa neno la Kristo ulimwenguni hana budi atazamie kifo wakati wowote”

Habari za kwenda kwa Luther huko Augsburg ziliwafurahisha sana wajumbe wa Papa. Mtu mkorofi, anayechafua ulimwengu aonekana sasa kuwa katika uwezo wa Rumi. Hivyo hawataaweza kuepuka. Wajumbe wa papa waliazimu kumlazimisha Luther ili akane imani yake, au kama hilo halitawezekana, wamtie mikononi

mwa walinzi, wampeleke Rumi ili akashiriki mambo yaliyowapata akina Huss na Jerome. Hivyo basi, mjumbe wa papa akashauri, kwa njia ya balozi, kwamba wamshawishi Luther asafiri bila mlinzi akitumaini tu bahati yake. Jambo hili lilikataliwa na Luther. Hakukubali kusafiri, mpaka apate kuhakikishwa na mfalme kuwa atamlinda kamili, ndipo atakubali kwenda kuonana na wajumbe wa papa.

[60] Basi, wajumbe wa papa walikusudia kumshawishi Luther kwa ujanja. Wakaonekana kuwa watu wa upendo mwingi kwa Luther. Wakamshauri akubali tu kushikamana na kanisa na kanuni zake bila ubishi, wala kuhojiana. Lakini jawabu la Luther lilionyesha jinsi anavyolipenda kanisa na ukweli wa Biblia. Pia kwamba yuko tayari kujibu maswali yote kuhusu mafundisho yake, na kukubali wakuu wa chuo alikofundisha watoe uamuzi wao juu ya mafundisho yake. Lakini alikanusha mambo ya maaskofu kwamba akane imani yake bila kumthibitishia kosa lake.

Wao walikazana tu kusema, “Kana imani yako! Kana Imani yako”. Luther aliwaonyesha kuwa msimamo wake unatokana na maandiko matakatiifu na hakuweza kukana ukweli. Mjumbe wa Papa aliposhindwa kumthibitishia Luther kosa kutokana na Biblia, basi wafuasi wa Rumi wote wakamzomea na kumtukana, wakimwita kuwa mhalifu wa mapokeo ya wazee na mzushi na kadhalika. Wala Luther hakupata nafasi yoyote ya kusema. Baadaye alipata ruhusa ya kutoka kuonyesha majibu yake kwa maandishi.

Alipoandika rafiki yake, alisema, “mambo yaliyoandikwa yanaweza kutumiwa kumhukumu mtu mwingine. Pili, mtu anaweza kutatanika kwa hofu, wala si kwa dhamiri, wakati watu wanapopayuka payuka kwa majivuno na maneno mengi ya ovyo ovyo”.

Wakati mwingine Luther alipofikishwa barazani, alieleza wazi msimamo wake, ukiungwa mkono na maandiko matakatiifu. Alisoma maneno yake aliyoyaandika katika karatasi, baada ya kuyasoma kwa sauti wazi, akampa askofu mkuu hiyo karatasi. Askofu mkuu aliitupa kando huku akimlaani Luther na kusema ni mwingi wa maneno maovu ya kivivu yasiyohusu. Sasa Luther akakutana na askofu mwenye kiburi, akamgusa kwenye siri yake. Akagusa mafundishi wanayofundisha kanisa, ambayo ni mapokeo matupu.

Askofu akijaa na ghadhabu alipaza sauti, “Kana imani hiyo au sivyo nitakupeleka Rumi. Akarudia kusema tena Kana imani, au sivyo hutaonekana tena”.

Basi Luther na rafiki zake wakaondoka huku akisema kuwa wasitazamie kuwa atakana imani. Askofu hakukusudia kuwa mambo yatakuwa hivyo. Basi wakabaki wakitazamana kwa mambo yalivyotokea, na kwamba mpango wao umeshindwa.

Mkutano mkuu uliokutanika uliweza kupima kati ya watu hao wawili, roho ya aina gani waliyo nayo, na misimamo yao. Ukweli ulijidhihirisha uliko. Luther akiwa mtulivu, mwenye ukweli na imara mjumbe wa papa mwenye majivuno bila kuwa na neno lolote la Biblia lenye kumwunga mkono, huku akipiga tu kelele, “Kana imani, au sivyo nitakupeleka Rumi”.

Kuponyoka Kutoka Augsburg

[61]

Rafiki za Luther walisema kuwa ni kazi bure kuendelea kukaa Augsburg, kwa hiyo ingefaa aende tu Wittenberg bila kuchelewa, na hadhari kubwa lazima iangaliwe. Basi kesho yake asubuhi mapema akaondoka akiwa amepanda farasi, akifuatana na kiongozi aliyechaguliwa na hakimu. Aliondoka kungali giza akapita katika barabara za mji kisirisiri. Adui zake walikula njama ili wamwangamize. Wakati huo ulikuwa wa wasiwasi na maombi mengi. Alifika mlango mdogo wa ukuta wa mji. Alifunguliwa, akapita pamoja na kiongozi wake. Kabla mjumbe wa papa hajafahamu kuondoka kwa Luther, alikuwa ameenda mbali, na ilikuwa vigumu kumpata.

Mjumbe wa papa alipopata habari kwamba Luther ameponyoka, alighadhabika mno na kujaa uchungu. Alitumaini kujipatia sifa bora kwa kumkomesha mkorofi huyu anayevuruga kanisa. Katika barua aliyomwandikia mfalme Frederick wa Saxony alimlaani Luther kwa uchungu mwingi, akimtaka ampeleke Luther, Rumi au ampige marufuku huko Saxony.

Mfalme Frederick hakuelewa vizuri mafundisho ya Luther lakini alivutiwa sana na ujasiri, na usemi wake. Frederick alimleta Luther mpaka athibitishwe makosa yake. Katika majibu ya barua ya mjumbe wa papa, Frederick alisema “Kwa kuwa Doctor Martim Luther alifika mbele yako huko Augsburg, ungeridhika. Hatukutumaini kuwa ungemlazimisha kukana imani yake, bila kumdhihirishia

makosa yake. Hakuna mtu mtaalamu ambaye ameniambia kuwa mafundisho ya Luther ni mapotovu, yampingayo Kristo na ya uasi.” Mfalme aliona kuwa kazi ya matengenezo ya kanisa, ambayo inafanywa na Luther inahitajika sana. Alifurahi sana kwa kuwa hali ya kanisa inaleta mvuto mzuri.

Mwaka mmoja tu ulipita tangu Luther alipotundika yale maneno tisini na matano kwenye mlango wa kanisa. Na maneno hayo yalienea kila mahali, na kusababisha watu wengi wasome maandiko matakatifu. Wanafunzi waliokuja kusoma hapo Witternberg mara ya kwanza waliinua mikono yao mbinguni wakimtukuza Mungu kwa kuwezesha nuru ya Injili kung’aa katika mji huo.

[62] Luther hakuachana na mambo yote ya Rumi, aliyokuwa akifuata. Aliandika na kusema, “Lakini ninaposoma maagizo ya papa Nashindwa kuelewa. Sijui papa mwenyewe ndiye mpinga Kristo au mtume wake. Kwa hiyo Kristo huwakilishwa kwao kwa makosa sana na kusulubishwa kwake”.

Rumi ilizidi kukasirishwa na mashambulio ya Luther. Hapa wapinzani washupavu wa Luther madaktari katika vyuo vikuu vya katholiki walitangaza kwamba mtu atakayemwua Luther ataachiliwa dhambi zake kabisa. Lakini Mungu alikuwa mlinzi wake. Mafundisho yake yalisikika kila mahali, mashambani, katika nyumba ndogo, katika nyumba za watawa katika nyumba ya fahari ya wakuu katika vyuo vikuu, na katika majumba ya wafalme.

Wakati ule ule Luther akagundua kuwa ukweli wa kuhesabiwa haki kwa imani ulikuwa unaaminiwa na mtengenezaji mkuu wa kanisa Huss mtu wa Bohemia. Luther alisema “Sisi sote, yaani Paulo, Augustine na mimi, tumekuwa Wahuss tukifuata ukweli huu bila kujua ukweli huu umehubiriwa tangu karne iliyopita; na ukachomwa moto”.

Luther akiandika kuhusu vyuo vikuu alisema: “Naogopa, kwamba vyuo vikuu vitageuka kuwa malango ya jehanam, kama haiwezi kutia nia ya kuchunguza Biblia na kuifuata, na kuifundisha kwa vijana. Kila kituo cha mafunzo ambapo neno la Mungu halijaliwi, lazima kitapotoka”

Jambo hili lilienezwa kote katika Ujerumani. Taifa zima lilitaharuki. Wafuasi wa papa wakamtaka papa amchukulie Luther hatua kali. Basi mara moja amri ikatolewa kuwa mafundisho ya Luther

yalaaniwe na kupigwa marufuku. Na tena Luther na wafuasi wake wote, kama hawataikana imani yao waharamishwe.

Hatari Kuu

Jambo hili lililoamriwa lifanyike lilikuwa la hatari kuu kwa matengenezo ya Luther. Hakuwa gizani kuhusu tufani iliyokuwa tayari kuvuma juu yake. Lakini alimtumaini Kristo kwa matokeo yote ambayo yangetokea. Alitamka na kusema: “Yale yatakayotokea, mimi sijui, wala sijishughulishi kuyajua ... maana sivyo kama vile jani la mti liangukavyo bila amri kutoka kwa Baba. Basi kama ni hivyo sisi je hutunzwa kiasi gani! Ni jambo rahisi kufa kwa ajili ya Neno, ambaye neno alifanyika kuwa mwili, naye mwenyewe alikufa”.

Wakati amri ya papa ilipomfikia Luther, alisema “Mimi naidharau amri hiyo na kuilaani, maana ni ya kidhalimu tupu. Kristo mwenyewe ndiye anayeshutumiwa. Mimi najisikia kuwa huru rohoni mwangu, maana najua kuwa papa ni mpinga Kristo, na kiti chake cha enzi ni cha Shetani mwenyewe.”

Walakini utawala wa papa haukuwa bila misukosuko. Watu dhaifu wasio imara walitetemeka kusikia amri hiyo. Wengi [63] walipenda maisha haya. Je, kazi ya Luther mtengenezaji wa kanisa itakwisha?

Luther hakuwa na wasiwawi. Kwa ujasiri mkuu aliilaani Rumi, na kuichomelea mbali amri ya papa mbele ya watu wengi wa hali zote. Akasema, “Mashindano ya ajabu yameanza. Mpaka sasa tumekuwa tukicheza na papa. Mimi nimeanza kazi hizo kwa jina la Mungu, na kazi hii itamalizika bila mimi, ila kwa uwezo wake. Nani ajuaye kama Mungu hakuniteua na kuniita na iwapo hawaogopi kunidharau mimi hawajui kuwa wanamdharau Mungu?”

“Mungu hachagui mtu mkuu wa dunia ili awe nabii au kuhani, bali huteua watu wa hali ya chini, watu wa kawaida tu ambao hudharauliwa na watu, hata wachungaji kama Amosi. Katika kila kizazi watakatifu wa Mungu iliwapasa kukemea hata wafalme, watu wakuu watawala, na wenye hekima; ili wasiangamie dhambini. Sisemi kuwa mimi ni nabii; bali nasema kuwa lazima waogope, kwa sababu niko mmoja na wao ni wengi. Nina hakika ya jambo kwamba neno la Mungu liko ndani yangu na kwamba hawana Neno hilo”.

Walakini Luther alipita katika mashindano makuu alipoamua kutengana na kanisa la Rumi. Alisema, “Lo, ni maumivu kiasi gani yamenipata, ingawa Biblia inaniunga mkono, kwamba ni sawa kabisa kusimama imara katika kupingana na papa, na kumtaja kuwa ni mpinga Kristo! Ni mara ngapi sikujiuliza swali lile la uchungu, ambalo lilikuwa likitamkwa na papa kila mara, kwamba: Je, wewe peke yako ndiwe mwenye hekima? Je, watu wote ni wakosefu, ila wewe tu? Itakuwaje basi ikiwa wewe ndiwe mkosaji na kuwakosesha wengine wapate kuangamia? Hivyo ndivyo nilivyoshindana na nafsi yangu na shetani pia, mpaka Kristo kwa rehema zake aliuukaza moyo wangu kwa neno lake lisilo na makosa, nikaondolewa mashaka.”

Amri mpya ya papa ikatokea ya kusema kuwa Luther ameharamishwa kutoka katika kanisa la Rumi, akilaaniwa na kutukanwa vibaya, kama mtu aliyelaaniwa na mbingu. Pamoja na hayo, wote watakaoyafuata mafudnsiho yake, wamelaaniwa pia.

[64] Watu wote walioitwa na Mungu kuupeleka ujumbe kwa wanadamu “watapata mapingamizi” Katika siku za Luther kuliko wako na ukweli uliohusu wakati. Siku hizi kanisa linao ukweli wa wakati huu. Ukweli huu hauthaminiwi na watu kama vile haukuthaminiwa na papa na wenzake siku za Luther. Wanaotangaza ukweli wa wakati huu asitazamie kuwa utapokewa na watu wengi zaidi ya ulivyopokewa hapo mwanzao, siku za akina Luther. Mpambano makuu kati ya kweli na uongo, na kati ya Kristo na Shetani yataendelea na kuzidi mpaka mwisho wa historia ya ulimwengu. Soma Yohana 15:19-20; Luka 6:26.

Marejeo:

D’Aubigne, bk. 2, chap. 2

Ibid.

Ibid. ch. 3

Ibid. ch. 4

Ibid. bk. 2, ch. 6

Ibid.

Ibid bk. 5, ch. 2

See John C.L. Giesler. A compendium of Ecclesiastical History, para 4. sec. 1. para 5.

D’Aubigne, bk. 3, chap. 1

Ibid. ‘

See K.K. Hangenbach. History fo Reformation, Vol. 1, p. 96
D'Aubigne, London Ed. bk. 4, chap. 8
Ibid chap. 6.
Ibid.
Ibid chap. 7
Ibid. bk. 4 chap. 2
Ibid. chap. 4
Martyn — The Life and Times of Luther, pp. 271-272
D'Aubigne, London Ed. Bk. 4, chap. 8
D'Aubigne bk. 4 chap. 10
Ibid.
Ibid, bk. 4. chap. 1
Ibid. bk. 6. chap. 2.
Wylie bk. 6, chap. 1
D'Aubigne, bk. 6, chap. 3
D'Aubigne, 3rd London Ed. Walther 1840, bk. 6, chap. 9
Ibid.
Ibid. chap 10
Martyn p. 372-373.

8/Jasiri wa Kweli

Mfalme mpya alikalia kiti cha ufalme wa Ujerumani, ambaye ni Charles V. mtawala Saxony ambaye Charles alikuwa akimtegemea, alimshauri asijihusishe na habari za Luther, mpaka hapo akatapopewa nafasi ya kujitetea mbele zake. Kwa mashauri hayo mfalme alitiwa katika hali ya wasiwasi. Wafuasi wa papa wasingalitosheka na kitu chochote, ila kifo cha Luther. Mfalme wa Saxony alimwambia mfalme Charles V kuwa Luther apatiwe mlinzi ili “aje afike mbele ya wataalamu na watawa na mahakimu wasiopendelea”

Basi mkutano ukakutanika katika mji wa Worms. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa wakuu wa Ujerumani kukutanika pamoja na mfalme wao kijana. Viongozi wa kanisa wakuu wa serikali na mabalozi kutoka nchi mbalimbali walikutanika huko Worms. Lakini tamasha halisi iliyoutayaharukisha mkutano ilikuwa “Mtengenezaji wa kanisa” yaani Martin Luther. Mfalme Charles aliambiwa mkuu kuja pamoja na Luther, huku akimhakikishia ulinzi kamili na uhuru wa kusema bila kizuizi. Luther alimwandikia mkuu huyu hivi, “kama mfalme ndiye ameniita, siwezi kuwa na wasiwasi, maana ni kama kuitwa na Mungu mwenyewe Kama wanakusudia kunidhuru... Najikabidi mikononi mwa Bwana... Bwana asiponiokoa maisha yangu hayana faida... Unaweza kutazamia kila kitu kutoka kwangu... Ila huwezi kunitazamia kukimbia au kukana imani yangu. Kukimbia siwezi, na kukana imani siwezi pia.”

Habari zilipoenea kwamba Luther atasimama mbele ya baraza la wakuu, wasiwasi mwingi ulienea. Alexander, ambaye ndiye mjumbe wa papa, alikasirika mno. Kuhusika katika kesi ambayo papa mwenyewe amekwisha kutoa hukumu na kumpiga mtu huyo marufuku ni jambo baya sana, linalofedhehesha mamlaka ya papa. Alimshauri Charles kutoruhusu kusimama na Luther huko Worms, na kutoruhusu akamshawishi mfalme akubali. Alexander haku-tosheka na ushindi huo aliopata wa kumshawishi mfalme bali alijitahidi kusema kuwa Luther ni mwenye hatia anayestahili hukumu akimshitaki kuwa ni “Mchochezi, mwasi, mkaidi na mwenye ku-

furu”. Lakini harara yake ilidhihirisha aina ya roho iliyomwongoza kumshitaki. Alisukumwa tu na chuki kutaka kulipa kisasi. Hivyo ndivyo ilivyoonekana.

Alexander akamsisitiza mfalme kwa bidii sana ili atekeleze amri ya papa. Aliposhindwa na mashawishi ya Alexander mfalme akamwambia kuwa alete kesi hiyo mbele za wakuu. Wale waliomwunga Luther mkono wakasikiliza usemi wa Alexander kwa wasiwasi mwingi. Mtawala wa Saxony hakuwako siku hiyo, lakini baadhi ya washauri wake waliyaandika maneno ya hotuba ya ujumbe wa papa.

[66]

Luther Ashitakiwa Kuwa Mzushi

Alexander alimshambulia Luther kwa usemi wa nguvu na ufasaha, kwamba ni adui wa kanisa na wa serikali pia. Akasema kuwa makosa ya Luther yametosha, na yanasababisha kuwachomelea mbali wazushi laki nzima.

Kundi la wakufunzi wapotofu na wafedhulu, ambao ni makasisi walioharibika, na watawa wapumbavu, pamoja na jamii ya wa tu waovu, walisema. “Waluther hawa wana nini? Je hesabu yao inawiwa na hesabu ya Wakatoliki na uwezo wao ni kitu gani kwa uwezo wa Wakatoliki? Amri ikitolewa na watu hawa ingetekelezwa mara bila kupingwa na kitu”.

Mabishano yale yale bado yanaendelea kwa wote wanaoeneza ukweli wa neno la Mungu. Kila mara maswali hutokea, “ni nani hawa wanaojidai kutangaza mafundisho mapya? Kwanza hawana elimu, ni wachache kabisa, nao ni watu duni tu. Hata hivyo wanasema kuwa wanao ukweli na kwamba wamechaguliwa na Mungu. Ni wajinga kabisa na wamedanganyika. Je, kanisa letu linalinganishwaje nao kwa umaarufu na kwa wingi?” Mashindano ya jinsi hiyo hayatofautiani na yale ya wakati wa Luther.

Luther, akiwa na uwezo wa neno la Mungu ili kuwapinga na kuwaponda watetezi wa papa. Ilionekana kuwa sio mafundisho yake tu yangelaaniwa ila hata yeye angeangamizwa. Mambo yote Roma iliyokusudia kusema juu yake, yalisemwa kwa hiyo tofauti ilionekana baina ya ukweli na uwongo wakati wa mapambano ya wazi.

Sasa Bwana aliwaamsha wana baraza waone wazi juu ya udhalimu wa mapapa. Duke George wa Saxon akasimama katika baraza hiyo ya wakuu akafafanua kwa ukamilifu kabisa udanganyifu wa maovu ya kanuni za papa.

[67] Dhuluma. . . . hupiga kelele kuhusu Roma. Aibu yote imewekwa kando, kile wanachokazania ni fedha. . . . Kwa hiyo wahubiri ambao wangehubiri ukweli, hawasemi lolote, ila madanganyo. Hivyo sasa wanavuna walichopanda. Kadiri mpango huo ndimo maji ya udhalimu hububujika. Upotovu unaonyesha udhalimu na tamaa ya mali mkononi. . . . Lo! Ni aibu inayoletwa na viongozi wa kanisa, inayowatumbukiza watu maskini katika uangamivu wa milele. Kazi ya matengenezo ya kanisa lazima ipingwe. Kwa kuwa msemaji wa papa alikuwa adui wa Luther aliwashawishi wasikilizaji ili wamwunge mkono.

Malaika wa Mungu walitoa nuru katika giza nene la makosa, akafungua mioyo ya watu wauone ukweli. Uwezo wa Mungu uliwakirisha hata wapinzani wakuu ili waandae njia kwa matengenezo makuu zaidi. Sauti ya mkuu zaidi ya Luther imesikika katika baraza hilo.

Kamati ikachaguliwa ili ipange mambo maovu ambayo wame-tendea na papa kwa watu wa Ujerumani. Orodha hio imepelekwa kwa mfalme, akiombwa ili achukue hatua kuhusu mambo haya ya udhalimu. Mtu mmoja kati ya waombaji alisema, “Ni kazi yetu kuzuia maovu na kuwaheshimu watu wetu. Kwa hiyo tunakuomba kwa unyenyekevu uamuru matengenezo ya kanisa yafanyike na kukamilishwa”.

Luther Atakiwa Ahudhurie

Sasa baraza ilidai kuwa Luther ahudhurie kikaoni. Mwishowe mfalme alikubali, na Luther akahudhuria. Pamoja na hayo, alipewa ulinzi. Hayo yalitokea Wittenberg kwa njia ya kuweka walinzi pote njiani mpaka Warmos.

Rafiki zake wakijua kuwa chuki na uadui juu ya Luther ni mkubwa, waliogopa kuwa huenda walinzi wake wasijaliwe. Yeye alijibu kusema “Kristo atanipa roho yake ili kuwashinda wajumbe hawa waovu. Nawadharau hawa katika maisha yangu. Nitazidi kuwashinda wakati wa kifo changu. Huko Worms, wanashughu-

lika sana ili wanifanye nikane imani yangu. Na hii haitawezekana. Kwanza nilisema kuwa papa ni mjumbe wa Kristo sasa nasema kuwa papa ni adui wa Kristo na mtume mwovu”.

Rafiki watatu waliazimu kufuatana na Luther mbali ya mjumbe wa serikali aliyefuatana naye. Malanchthon ambaye ni mwenzi wa Luther, moyo wake ulifungwa na wa Luther naye alitaka sana kufuatana naye. Lakini matakwa yake ya kufuatana na Luther ya-likataliwa. Luther ambaye ni mtengenezaji wa kanisa, alimwambia Malanchthon: “Kama sirudi na kama adui zangu wakiniua wewe uendelee kufundisha na kudumu katika ukweli.

Ufanye kazi badala yangu Wewe ukibaki mzima, kifo changu [68] kitakuwa na faida kidogo”.

Mioyo ya watu ilisumbuliwa na wasiwasi. Walifahamu kuwa maandishi ya Luther yamelaaniwa huko Worms. Mjumbe wa Luther akihofia usalama wake katika baraza, alimwuliza kama anataka kuendelea mbele. Luther alijibu: “Ingawa ninapigwa marufuku kila mji, lakini nitaendelea mbele”

Katika mji wa Erfurt Luther alipita katika barabara kwa maringo, akiangalia magereza alimofungiwa zamani akitafakari juu ya mashindano aliyopitia wakati alipokuwa akimulikia Ujerumani nuru ya Injili ambayo sasa imeenea katika nchi yote. Kwanza alizuiliwa asihubiri, lakini akapata ruhusa ya kuhubiri. Mtawa ambaye alikuwa akijitesa kwa ajili ya dini sasa ni muhubiri, huyo ndiye Luther.

Watu walimsikiliza kwa makini kabisa. Mkate wa uzima ulitolewa kwa watu wenye njaa. Kristo aliinuliwa juu yao akizidi mapapa na wafalme na watawala wote. Luther hakujifikiria na hatari yake. Katika Kristo alipoteza ubinafsi kwa mambo yote. Alijificha katika Mtu wa kalwari akitaka tu kumwinua Kristo juu ya kila kitu kama Mwokozi wa dhambi.

Ujasiri wa Mfia Dini

Kwa kadiri mtengenezaji wa mambo ya kanisa, yaani Luther alivyoendelea na mafundiso yake walimkusanyikia huku wakiwa na hamu kuu ya kusikia ujumbe wa mbinguni, wakati huo sauti za amani zilimzungumzia kwamba adui zake Waroma wanamka-bili. Walisema, “Watakuchoma, na kukuteketeza kabisa uwe majivu, kama walivyomfanya John Huss” Luther akajibu akasema: “Hata

kama wakiwasha moto toka Worms mpaka Wittenberg ni-tapita kati yake kwa jina la Yesu Bwana, nitaonekana mbele yao. . . . nikimkiri Yesu Kristo”.

Kufika kwake huko Worms kulileta wasiwasi mkubwa. Marafiki zake walihofia usalama wake, na maadui zake walikuwa na wasiwasi juu ya kusudi lao. Kwa ajili ya chuki na mchocheo wa Kiroma, ilisisitizwa kuwa Luther aende katika makao ya Wakuu ambao ni wa amani, ambavyo kulitangazwa kwamba tofauti zote zimesawazishwa na kuachwa. Lakini marafiki wa Luther walisema kuwa hatari ni kubwa, na hilo ni kubwa. Lakini Luther akitulia bila kutetemeka, alisema “Ingawa waovu wataongezeka katika Worms kama vigae juu ya paa la nyumba, hata hivyo nitaingia humo”.

Alipoingia Worms watu walijazana ili kumkaribisha. Taharuki ilikuwa kubwa. Luther alisema, Mungu ndiye atakuwa mlinzi wangu.

[69] Kufika kwake kuliwatia wafuasi wa papa wasiwasi. Mfalme alivaita washauri wake akawauliza: “Ni hatua gani itakayochukuliwa. Wakadai wafuasi wa papa walisema ‘Tumeshughulikia jambo hili kwa muda mrefu sasa. Hebu, mfalme mtukufu amalize jambo hili kwa kumwondoa mtu huyu asiishi. Je, Sigismund hakutoa amri John Huss akachomwa moto? Hatupaswi kuendelea kumtunza mzushi huyu’ Mfalme akasema” “La, lazima tutunze ahadi yetu”. Ikaamuliwa kuwa mtengenezaji wa kanisa budi asikilizwe.

Mji mzima ulitamani sana kumwona mtu huyu mashuhuri. Luther alikuwa amechoka na safari ndefu, alihitaji pumziko. Lakini alikuwa amepumzika kwa muda wa saa chache tu, wakati wakuu, mapadri, watu mashuhuri na raia wa mjini walipomkusanyikia. Kati ya watu hao waliokuwamo watu waliomtaka mfalme amlaani na kumtukana Luther. Walio wengi, maadui na marafiki pia walikuja kumwona mtawa huyu jasiri. Alionekana kuwa mtu jasiri. Uso wake ulionekana mtulivu uliojaa furaha. Maneno yake yalikuwa ya kishujaa hasa, hata adui zake walitekewa. Baadhi ya watu walikiri kuwa alikuwa na uwezo wa kimbingu, wengine walitamka kuwa alikuwa na pepo sawa kama walivyotamka kwa Kristo. Yohana 10:20.

Siku ya pili, mkuu wa serikali alimleta Luther katika jumba la baraza, katika mkutano. Kila mahali palijaa watu waliotaka kumwona mtu aliyethubutu kumpinga papa. Jemadari mzee ambaye

alipigana vita vingi na kushinda alimwambia taratibu: “Wewe maskini, sasa uanenda kuamua uamuzi wa ajabu ambao, mimi au jemadari mwingine yeyote hakuufanya katika vita vyetu vya kumwanga damu. Lakini iwepo njia yako ni ya haki Endelea mbele katika jina la Mungu, usihofu kitu. Mungu hatakuacha”

Luther Asimama Barazani

Mfalme alikalia kiti, huku akizungukwa na watu mashuhuri katika utawala wake. Sasa Martin Luther atatakiwa atetee imani yake mbele ya baraza. “Onekano hilo lenyewe lilikuwa alama ya ushindi mkuu juu ya papa. Papa alikuwa amemlaani mtu huyu, na kumwita kuwa ni mzushi, na sasa anasimama mbele ya baraza ambalo lina uwezo kupita wa Papa. Papa alikuwa amempiga marufuku na kumtenga mbali na jamii ya wanadamu, na sasa alikuwa ameitwa mbele ya kusanyiko maarufu katika ulimwengu. Uwezo wa Roma sasa ulikuwa unafifia, na mtu mtawa huyu ndiye anayesababisha hali hiyo”.

[70]

Mtengenezaji huyu wa kanisa, ambaye alizaliwa katika hali duni, alionekana kuwa tishio na mwenye udhia. Wakuu walikutana naye safari kadhaa wa kadhaa, na mmoja wao alimnong’oneza akisema “Usiogope wale wanaoua mwili ambao hawawezi kua roho” Mwingine akasema: “Wakati watakapowachukua mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, mtapewa saa ile mtakayosema” Mathayo 10:28, 18-19. Mkutano wote ukanyamaza kimya kabisa. Halafu mkuu mmoja wa Serikali akasimama, huku akielekeza kidogo kwa maandiko ya Luther, akadai kwamba Luther anajibu maswali mawili kwamba anayakiri kuwa ni yake, au kwamba anakusudia kuyakanusha. Majina ya vitabu, yaliyosomeka kwa Luther: Swali la kwanza alilijibu kuwa vitabu hivyo ni vyake. Kuhusu swali la pili alijibu, “Ningetenda bila busara kama nigejibu swali la pili bila kusababisha fujo. Budi lithibitisha zaidi bila kujali hali ilivyo. Kwa ajili hiyo nakusihi wewe mtukufu kwa unyenyekevu unipatie muda wa kujibu bila kwenda kinyume na neno la Mungu”

Luther aliwaamisha watu wote kuwa maneno yake hayatokani na mawazo tu bali ni ya kweli isiyobishiwa. Hali ilimwezesha baadaye kujibu maswali kwa njia ya hekima na heshima kamili. Majibu yake yaliwafedhehesha wapinzani wake kabisa.

Siku iliyofuata alitakiwa kutoa jawabu lake la mwisho. Kwa muda alifadhaika. Wapinzani wake walionekana kwamba watahinda. Mashaka yalimjaa, akaonekana kana kwamba ametengwa mbali na Mungu. Katika wasiwasi huo wa uchungu alimlilia Mungu, ambaye ndiye pekee yake aliyefahamu fadhaa yake. Alilia akisema “Oh, Mungu Mwenyenzi, kama nategemea uwezo wa dunia tu, hakuna tena yamekwisha. Saa yangu ya mwisho imefika, hukumu yangu imetajwa... Oh, Mungu, hebu nisaidie na hila zote za dunia... kazi hii ni yako, nayo ni kweli na ya milele. Oh, Mungu Unisaidie! Mungu mwenye haki, ambaye habadiliki, Situmaini kupata msaada kwa mtu yeyote. Wewe ndiwe uliyenichagua kwa kazi hii. Hebu uniwie karibu kwa ajili ya Mwanao Mpendwa Yesu Kristo, ambaye ndiye ngao yangu na ngome yangu, na mwamba wangu”.

[71] Hata hivyo Luther hakufadhaishwa na hofu ya mateso au kifo. Alijiona kuwa hatoshi chochote. Kwa ajili ya udhaifu wake kazi itakwama. Hakujitahidi hivyo kwa ajili yake, bali kwa ajili ya kazi ya Mungu, ipate kufaulu. Katika wasiwasi wake, imani yake ilikazika kabisa kwa Kristo ambaye ni mwokozi mwenye uwezo. Kule barazani hangeonekana akiwa pekee yake. Mara utulivu ukajaa moyoni mwake, naye alifurahi kwa kuwa amepata nafasi ya kumwinua Kristo mbele ya watu na “mataifa”

Luther alifikiri juu ya jawabu lake. Akafungua kurasa na maandishi yake, na akapanga mafungu ya Biblia yatakayomsaidia wakati wa kujibu. Ndipo hapo, akaweka mkono wake wa kushoto juu ya maandiko Matakatifu akainua mkono wake wa kulia kuelekea mbinguni akaahidi kudumu katika maongozi ya Biblia na kuwa mwaminifu kwa injili hata kama matokeo yake ni kumwaga damu yake.

Luther Mbele ya Baraza Tena

Wakati Luther alipofikishwa kwa wakuu tena alikuwa mtulivu bila kuwa na wasiwasi, akiwa na hali ya ujasiri kama mjumbe wa Mungu kati ya wakuu wa nchi. Sasa mkuu wa serikali alitaka atoe uamuzi wake. Je, aliazimia kukana imani yake? Luther alijibu kwa utulivu bila kutumia maneno ya karaha. Hakujitukuza, lakini hali yake ilikuwa imara sana hata iliwashangaza watu wote waliokuwepo.

Mfalme mtukufu na wakuu mashuhuri Luther alisema “Nasi-mama mbele yenu leo kama nilivyoagizwa jana. Kama nikikosea kwa ujinga naomba samahani, maana sikukulia katika jamii ya kifalme, ila nilikuwa katika mazingira ya kishambashamba”

Kisha akaeleza katika baadhi ya maandishi yake yaliyopigwa chapa, ambayo hata adui zake wanayasifu kwamba yafaa, basi kuyakanusa hayo ni kuikanusha kweli ambayo inaaminiwa na watu wote. Sehemu ya pili ya maandishi yake yalikuwa juu ya uovu na udhalimu juu ya Roma ikiongozwa na mapapa. Kuyatangua maandishi haya kutaimarisha na kustawisha udhalimu na uonevu wa Roma na kufungua mlango wa ukaidi wa kutojali mambo matakatifu ya Mungu. Sehemu ya tatu ya maandishi yalikuwa shambulio juu ya watu mmoja mmoja waliokuwa wakiutetea uovu. Kuhusu sehemu hii alikubali kuwa alikosea kushambulia watu kupita kiasi. Lakini hata kuhusu sehemu hii hakubali kuifuta. Maana akiifuta maadui wa ukweli watapata nafasi ya kuwadhulumu watu wa Mungu kwa ukatili mkuu. [72]

Aliendelea kusema “Nitajitetea kama Kristo alivyofanya. Kama nimesema maovu, hayo yatanishuhudia Kwa rehema za Mungu nakusihhi mtukufu mfalme, na ninyi waheshimiwa wote, pamoja na watu wote mnithibitishie kutoka katika maandiko ya manabii, na maandiko ya mitume kwamba nimepotoka. Nikithibitishiwa hivyo kutoka katika Maandiko Matakatifu, nitakuwa tayari kukana na kuungama kila kosa nililolifanya. Nami nitakuwa mtu wa kwanza kuchukua vitabu vyangu na kuvitupa motoni.

Zaidi ya kuaibishwa, nafurahi kuona kuwa Injili sasa inaleta vita na mafarakano kama ilivyokuwa zamani. Hii ndiyo tabia ya hali ya Neno la Mungu. Yesu Kristo alisema, Sikuja kuleta amani duniani bali upanga. . . .” Jihadharini msije mkasababisha mafarakano kwa kiburi. Mnaweza kulidhihaki neno Takatifu la Mungu, na kutumia nguvu za kutisha kulazimisha mambo kwa uwezo mkuu na kuleta uangamivu wa milele.

Luther, alikuwa amezungumza katika lugha ya Kijerumani, na sasa alitakiwa aseme maneno yale yale kwa lugha ya Kilatini. Basi aliyarudia maneno yale kwa Kilatini katika ufasaha kamili. Mungu alimwongoza usemi wake. Mara ya kwanza baadhi ya wakuu walipofushwa wasielewe ujumbe wa Luther, lakini aliporudia kusema kwa Kilatini waliona maana yake.

Wale waliofumba macho yao kwa ukaidi walikasirishwa na maneno ya Luther. Msemaji mmoja alinena kwa hasira. “Hakujibu swali aliloulizwa. . . . unatakiwa utoe jawabu wazi na dhahiri. Je, utakanusha mafundisho yako au hutayakanusha?”

Luther alijibu, “Kwa kuwa mfalme mtukufu na waheshimiwa wote mnataka nijibu wazi na dhahiri, nitawajibu hivi: Mimi sitakana imani yangu mbele ya papa wala mbele ya baraza, kwa sababu ni ya hakika kama siku, hata wapinzani wangu wanatofautiana katika maoni. Mimi nisipothibitishiwa kosa la Maandiko Matakatifu, sitaikana imani yangu kamwe, maana siyo salama kwa mkristo kusema kinyume cha dhamiri yake. Huo ndio msimamo wangu, siwezi kufanya vinginevyo, Mungu anisaidie. Amen”

Hivyo ndivyo alivyosimama mtu huyu mwenye haki. Ukuu wake, na ubora wa tabia yake, utulivu wake na furaha ya moyo wake vilidhihirika kwa wote walioshuhudia ukuu wa imani hiyo ishindayo ulimwengu.

[73] Katika jawabu lake la kwanza Luther alizungumza katika hali ya heshima sana. Waroma walidhania kwamba kukawia kawia kwake kulikuwa kunatayarisha ili akane imani. Charles mwenyewe aliyemwona Luther katika hali hafifu, mdhaifu, mwenye mavazi ya kawaida tu, mwenye usemi wa taratibu sana, “Mtu huyu hatanidhihaki” Lakini ujasiri wake, uwezo wa maneno yake, uliwashangaza wote. Mfalme katika mshangao wake alisema “Mtawa huyu ananena kishujaa bila kutishika na lolote”.

Wafuasi wa Roma wameshindwa kabisa na sasa wanataka kutumia vitisho ili kurudisha heshima yao iliyopotea. Wameshindwa kimaandiko. Msemaji mmoja alisema. “Kama hutaikana imani yako, mfalme na dola yake watatafuta njia nyingine ya kumfanyia mtu huyu asiyewezekana”. Luther alisema kwa utulivu, “Mungu awe msaada wangu, maana hakuna kitu cha kukana katika imani yangu”.

Aliambiwa aondoke wakati wakuu walipokuwa wakishauriana. Kuendelea kwa Luther kukataa kukiri kwamba alikosa huenda kukaleta badiliko fulani katika taratibu za kanisa. Basi iliamuliwa kwamba angepewa nafasi moja zaidi ya kukana mafundisho yake. Lakini swali liliulizwa tena kwamba, “Je, angekubali kukana imani yake na mafundisho yake?” Luther akasema, “Mimi sina jawabu lingine kuliko hilo nililojibu”.

Viongozi wa papa walijawa na chuki na uchungu, kwamba madaraka yao na mamlaka yao yanadharauliwa na mtu tu wa kawaida kama Luther. Luther amezungumza mbele yao kwa ujasiri na utulivu wa Kristo, akasema bila kutapatapa wala kubahatisha. Alijisahau, akasema akiwa mbele ya Mkuu anayewazidi wote hata mapapa, wafalme na watawala Roho wa Mungu amekuwa karibu naye na kuwatia uvuli wakuu wote waliokuwa barazani.

Baadhi ya wakuu walikubali kuwa maandishi ya Luther ni ya kweli kabisa. Watu wengine hawakusema neno wakati huo, lakini baadaye walimwunga Luther mkono. Mheshimiwa Frederick alisikiliza kwa makini sana usemi wa Luther akikiri kuwa huo ni usemi murua kabisa na akaazimu kumlinda na kumtetea kwa kila njia. Aliona kuwa hekima ya papa na ya wakuu na wafuasi wote wa Roma imeonekana bure kabisa mbele ya ukweli wa Luther.

Mjumbe wa papa alivyoona matokeo ya usemi wa Luther alikusudia kutumia kila njia ili amwangushe. Alimshawishi kwa njia zote mfalme kijana ili asimwache Luther kuendelea. Siku ya pili yake baada ya jawabu la Luther, Charles alitangaza mbele ya wakuu kuwa anaazimu kuilinda dini ya Katoliki, Akasema kuwa njia zozote zitatumia kumpinga Luther na wafuasi wake. Akasema, [74] “Nitaacha utawala wangu, mali yangu, rafiki zangu, mwili wangu damu yangu, roho yangu na uhai wangu Nitaendelea kupingana naye pamoja na Wafuasi wake kama wazushi. Nitatumia kila njia ili kuwaangamiza”. Walakini mfalme alitaka kuwa Luther lazima alindwe kabisa, na lazima arudi kwao kwa usalama.

Luther Alindwa Hatarini

Mara nyingine tena wajumbe wa papa walidai kwamba Luther asipewe ulinzi. Wakasema “Mto wa Rhine budi upokee majivu yake kama ulivyopokea majivu ya Joh Huss”. Lakini wakuu wa Ujerumani, ingawa walikuwa adui wa Luther, hawakukubali dhana hiyo. Walikumbusha kuhusu fujo na maafa yaliyotokana na kifo cha Huss. Hawakutaka Ujerumani irudie kupata maafa ya namna hiyo mara ya pili.

Charles katika jawabu lake kuhusu madai ya wajumbe wa papa, alisema “Ingawa wenye imani tofauti wanapaswa kuondolewa mbali ulimwenguni, lakini pia wanapaswa kulindwa na wakuu” Baadaye

wajumbe wa papa walimhimiza Charles kama vile Sigsmund alivyomtendea Huss. Lakini Charles alikumbuka mabaya yaliyompata Huss kwa ajili ya imani yake, na msukosuko uliotokana na mambo hayo akasema, “Mimi sitaki kuingia katika hali ya aibu kubwa namna hii kama Sigsimund” Walakini Charles hakuamini ukweli ulipofundishwa na Luther. Hakupenda kuacha njia za mazoea yake na kufuata njia mpya. Kwa kuwa wazee wake waliishi humo, hivyo hata yeye hakutaka kuacha ukatoliki.

Siku hizi watu wengi huishi katika njia za baba zao. Hatutakubaliwa na Mungu eti kwa kuwa tunaishi kwa mapokeo toka kwa wazee wetu badala ya kuchunguza Maandiko Matakatifu sisi wenyewe. Nuru mpya inayotumulikia lazima tuifuate, ingawa baba zetu hawakuwa nayo.

[75] Uwezo wa mbinguni ulipita kwa Luther ukawafikia wafalme na wakuu wa Ujerumani. Roho wa Mungu aliwasihi watu katika baraza hilo. Charles V akawa kama Pilato wa amani, akajitoa kufuata anasa za ulimwengu, na kwa kiburi akaukataa ukweli aliopeva.

Njama za kumwangamiza Luther zilienea mahali pengi, na zikasababisha msukosuko mji mzima. Marafiki wengi wa Luther hali wakitambua ukatili wa kikatoliki waliazimia kwamba Luther asitolewe mikononi mwa Wakatoliki. Watu maelfu walijitolea kumlinda. Milangoni mwa nyumba na katika mahali pa hadhara matangazo yalipigiliwa pote, mengine yakimlaani na mengine yakimuunga Luther mkono. Tangazo moja liliandikwa maneno haya: “Ole wako nchi, akiwa mfalme wako ni kijana” Mhubiri 10:16. Watu wajulikanao kwa ajili ya vyeo au utajiri walimthbitishia mfalme na wakuu kwamba, ikiwa Luther atapatwa na baa lolote, amani ya ufalme itatahayarika, na hata ufalme wenyewe utakuwa hatarini.

Juhudi ya Kumpatanisha na Roma

Fredrick wa Saxony alijificha sana asitambulike na watu jinsi anavyomfikiria Luther. Hakuonyesha chuki wala wema. Alinyamaza kimya huku akimchunguza Luther kisirisiri. Lakini watu wengi hawakuweza kuficha hali zao hivyo. Wengi walionyesha chuki yao au wema wao kwake Spalatin, aliandika akasema Chumba kidogo cha Luther hakikuweza kuweka watu wote waliofika hapo kumtembelea. Hata wale ambao hawakukubaliana na mafundisho

yake walisifu ujasiri wake uliomfanya akabili hatari ya kifo bila hofu, ili mradi asipingane na dhambira yake.

Bidii nyingi ilifanywa ili kumshawishi Luther ili akubaliane na Roma. Watu mashuhuri na wakuu walimfikia mara nyingi wakimwambia kuwa akiendelea kupingana na Roma, ataharamishwa kabisa kutoka katika nchi yote, na hatapata mtu wa kumtetea. Tena na tena alishauriwa akubali kuungana na Roma kama mfalme alivyoshauri. Hapo akikubali atakaa salama. Yeye akajibu, “Nakubali kwa moyo wote kwamba mfalme na wakuu na wakristo wote, wachunguze mafundisho yangu wakiyalinganisha na neno la Mungu, kama wakiona tofauti basi nitasahihisha. Maana mwanadamu hana jingine ila kutii na kufuata neno la Mungu basi.”

Katika kishawishi cha siku nyingine, alisema, “Nakubali kuachana na walinzi wangu. Nitaweka maisha yangu mikononi mwa mfalme. Lakini kuacha neno la Mungu, kamwe sitaacha!” Alieleza kuwa, yeye yu tayari kukubaliana na uamuzi wa baraza, ikiwa uamuzi huo unasimama ndani na Maandiko mtakatifu kuhusu neno la Mungu na imani, kila mkristo anajua la kufanya vizuri sawa sawa na papa. Papa hana ujuzi wa peke kuliko mkristo mwingine yeyote. Basi watu waliokuwa wakimshawishi waliona kuwa ni kazi bure kuendelea kumshawishi.

[76]

Kama Luther angalikubaliana nao hata kwa neno moja tu, shetani na majeshi yake wanalipatia ushindi. Lakini msimamo wake wa imani ulikuwa njia ya kulipatia kanisa uhuru wa kuachana na udhalimu wa Roma. Mvuto wa mtu huyu shujaa aliyethubutu kusimama imara mwenyewe, ulisaidia kanisa, sio kwa wakati wake tu, ila hata kwa vizazi vijavyo.

Mara Luther aliamuriwa na mfalme arudi nyumbani. Tangazo hilo lingefuatiwa na hukumu yake. Vitisho vya kumwangamiza vilizagaa katika njia yake, lakini alipoondoka Woms, roho yake ilijaa furaha na sifa kwa Mungu.

Baada ya kuondoka alitaka ieleweke kwamba ujasiri wake sio wa uasi. Luther alimwandikia mfalme barua akisema “Mfalme mtukufu, nini niko tayari kutii wakati wowote, kwa heshima au kwa aibu, kwa uzima au kwa mauti, katika mambo yote, ila yanayotaka kunitenga na neno la Mungu, hayo siwezi kuyatii. Pale mambo ya milele yanapohusika, mambo ya binadamu budi yawekwe kando. Utii wa

jinsi hiyo wa moyoni ndiyo ibada ya kweli, inayotakiwa kumpa Mwumbaji wetu”

Katika safari kutoka Worms, alikaribishwa na waongozi, ingawa ameharamishwa katika ushirika. Hata watawala walimheshimu ingawa mfalme mwenyewe alimlaumu. Ingawa alimharamisha alitakiwa ahubiri. Alisema, “Siahidi kufungia neno la Mungu nisiluhubiri”

Hakukaa muda mrefu baada ya kutoka Worms kabla wafuasi wa papa kumlazimisha mfalme ampige marufuku Luther alitukanwa kwamba yeye ni shetani mwenye mfano wa mwanadamu, mwenye kuvaa vazi la mtu mtawa. Mara ulinzi wake ulikoma, watu wote walikatazwa kumsaidia kwa lolote. Walikatazwa wasimpe chakula au msaada wowowte. Aliwekewa ulinzi na wafuasi wake kukamatwa na mali zao kuchukuliwa. Vitabu vyake vikachomwa halafu watu wote waliokwenda kinyume na amri hii waliwekwa katika hukumu ile ile. Frederick wa Saxony rafiki wa Luther aliondoka Worm baada ya Luther. Amri ya mfalme ya kumpiga Luther marufuku ilipokewa na wakuu wote. Wafuasi wa Roma walishangilia kabisa.

[77] Walidhani kuwa maangamizo ya mtengenezaji wa kanisa yamekamili.

Mungu amtumia Frederick Saxony

Jicho la Mungu lisilosinzia lilikuwa likiangalia mienendo ya Luther. Mungu alimwandaa Frederick wa Saxony mtu mwenye moyo safi moyo wa kweli ili amtunze Luther. Katika safari ya kutoka Worms kurudi nyumbani, Luther alitengana na wenzake. Alichukuliwa kwa njia ya msituni kwenda katika gereza la Wartburg, ambako alifungiwa ili kumficha. Maficho yake yalikuwa ya siri hata Frederick mwenyewe hakufahamu. Kwa kuwa ilikuwa siri ya ulinzi Frederick alikaa bila wasiwasi bora tu yu salama. Majira ya kiangazi na masika yakapita, na Luther aliendela kukaa gerezani. Alexander, mfuasi wa Luther alifurahi sana. Nuru ya injili ilionekana kwamba imezimika. Lakini nuru ya Luther iling’aa kwa mng’ao mkubwa.

Usalama Huko Wartburg

Katika utulivu wa usalama wa Wartburg, Luther alifurahia hali hiyo ya utulivu kutoka katika joto la vita na matatizo. Lakini kwa kuwa amezoea maisha ya mapambano ukiwa sana kukaa kimya bila shughuli. Katika siku hizo za upweke hali ya kanisa ilififia. Alihofia kulaumiwa kuwa amekuwa mwoga na ya kuwa amejitoka kutoka katika mapambano. Basi akajilaumu sana kuwa na hali ya uvivu.

Hata hivyo kila siku alitimiza sehemu kubwa ya kazi kwa jinsi isiyodhaniwa kuwa mtu anaweza kufanya vile. Kalamu yake haikusinzia kuandika mambo. Adui zake walishangaa kwa uthibitisho wa ukweli aliokuwa akitoa; hivyo walichanganyikiwa. Vigazeti vingi sana viliandikwa na yeye na kusambazwa kote katika Ujerumani. Pia alitafsiri agano jipya katika lugha ya Kijerumani. Katika kifungo chake sawa na kile cha Patmo aliendelea kutangaza injili na kukemea maovu ya Roma kwa muda karibu mwaka mzima.

Mungu alikuwa amemwondoa mtumishi wake kutoka katika mapambano ya hadhara. Katika maficho yake milimani, Luther alitengwa mbali na mivuto ya misaada ya kibindamu. Aliwekwa mbali na hali inayoweza kuinuka kwa kiburi na kufaulu.

Kadri watu walivyofurahia uhuru ulioletwa na Injili, shetani alitaka kugeuza mawazo yao ili ajitegemee kuabudu kazi zao badala ya kuutegemea mkono wa Mungu unaofanya makuu. Mara nyingi viongozi wa dini wanaosifiwa namna hiyo hujitegemea wenyewe. Watu hushawishika kuwategemea na kutumainia uongozi wao badala ya kumtazamia Mungu. Kutoka katika hatari hiyo Mungu hutunza matengenezo ya kanisa. Macho ya watu yamgeukie Baba wa milele mwenye ukweli wote.

Marejeo:

D'Aubigne bk. 6 ch. 11

Ibid bk. 7, ch. 1

Ibid

Ibid

Ibid. ch. 4

Ibid

Ibid. ch.6

Ibid ch. 7

Ibid

[78]

Ibid

Ibid

Ibid. ch. 8 24

bid.Lenfant, Vol. 1. p422

Martyn Vol. 1 p. 404

D'Aubigne bk. 7 ch. 10

D'Aubigne bk. 7 ch. 11

Martyn vol 1 ch. 11

Martyn Vol. 1. p.420

D'Aubigne bk. 7 ch. 11

Majuma machache baada ya kuzaliwa Luther katika kibanda kidogo cha wachimba madini katika Saxony, Zuric Zwingli naye akazaliwa katika nyumba ya mfuga mifugo katika milima ya Alps. Kwa kuwa alikulia katika mazingira safi ya kawaida, mawazo yake yalianza kutafakari mambo ya Mungu na ukuu wake. Akiwa chini ya bibi yake, alisimuliwa hadithi nyingi za Biblia alizojifunza katika kanisa.

Alipopata umri wa miaka kumi na mitatu alikwenda katika mji wa Bern, ambako kulikuwa na shule maarufu katika Switzerland. Walakini hapo Bern hatari ilitokea. Watawa waliazimia kabisa kumshawisi ili aingie katika kundi la watawa. Kwa bahati nzuri baba yake alipata habari ya maazimio ya watawa hao. Akaona kuwa maisha ya mwanawe ya usoni hayatafaa lolote, tena yumo mashakani. Kwa hiyo alimwita arudi nyumbani.

Kijana alirudi lakini hakuridhika na maisha ya kwao kwenye mabonde ya milima. Baada ya muda akaenda Basel na kuanza tena masomo yake. Hapa ndipo Zwingli aliposikia Injili ya neema ya Mungu mara ya kwanza. Wittembach alipokuwa akijifunza Kigiriki na Kiebrania, aliongozwa na Roho kuchunguza Maandiko Matakatifu. Kwa njia hii nuru ya Mungu ikapenya mawazoni mwake. Akatangaza kwamba kifo cha Kristo ndicho fidia pekee ya mwenye dhambi. Maneno hayo yalipenya mawazoni mwa Zwingli, yakawa ndiyo mwanzo wa pambazuko la asubuhi.

Baadaye Zwingli aliitwa kutoka Basel kufanya kazi ya maisha. Mahali pake pa kazi poliko katika majimbi ya milima ya Alps. Alipowekewa mikono kuwa padri alishughulika na mambo ya kiroho, na kuchunguza maandiko ya kweli ya Mungu.

Kwa kadiri alivyozidi kuchunguza Maandiko Matakatifu ndivyo alivyozidi kupambanua wazi baina ya ukweli na uzushi wa Roma. Alijitolea kuamini Biblia kama Neno la kweli la Mungu, ambalo linatosha kuongoza watu. Aliona kuwa halina haja ya maelezo zaidi, maana lenyewe linajieleza. Alitafuta kila njia ya kumsaidia

ili aelewe bila kupotoshwa. Aliomba Roho Mtakatifu amsaidie. Aliandika akasema “Nilianza kumwomba Mungu anipe nuru yake, halafu Biblia iliniwia rahisi kuelewa”.

Mafundisho ya Biblia Zwingli aliyofundisha hakuyapata kwa Luther. Aliyapata kwa Kristo. Mswisi huyu aliandika na kusema “Kama Luther anamhubiri Kristo, anafanya kama vile nifanyavyo. . . . [80] Kamwe hakuna neno lolote nililoandika kwa Luther, wala Luther kwangu ambalo linahusu wokovu. Kwa nini? Kwa kuwa mahubiri ya Luther na ya kwangu yote huongozwa na Roho Mtakatifu na wala hayatofautiani kwakuwa yanatokea mahali pamoja”

Katika mwaka wa 1516 Zwingli alialikwa ahubiri katika nyumba ya watawa huko Einsiedeln. Mahali hapa aliacha mvuto bora kabisa kama mtengenezaji wa kanisa halisi. Mvuto huo ulienea katika nchi yote ya kwao, milimani Alps.

Baina ya mambo makuu ya Einsiedeln ilikuwa sanamu ya bikira, ambayo ilisemekana kuwa ilikuwa na uwezo wa kufanya miujiza. Juu ya lango la nyumba ya watawa palikuwa na andiko lisemalo, “Hapa msamaha kamili wa dhambi hupatikana” Hapo palipohesabiwa kuwa mahali patakatifu watu makundi makundi walitoka pote katika nchi ya Switzerland, ufaransa hata Ujerumani pia, ili kupata msamaha wa dhambi. Zwingli alitumia nafasi hiyo ya kuwatangazia uhuru upatikanao katika Injili ya neema ili kuwatoa katika kifungo cha ushirikina.

Zwingli aliwaambia “Msidhani kuwa Mungu yumo katika hekalu hili kuliko mahali pengine, je, mambo hafifu haya mtendayo, kama vile safari ndefu kwa ajili ya dini, kutoa sadaka, kuheshimu sanamu za watakatifu, na kadhalika yatawapatia msamaha wa neema ya Mungu? Kuna manufaa gani ya kuvaa kofia yenye kung’aa, majoho maridadi, na mapambao ya aina aina? Kristo aliyetolewa kafara juu ya msalaba ndiye fidia ya dhambi kwa wote wamwaminio milele”.

Kwa wengi, walitiwa uchungu kuambiwa kuwa matendo yao kama safari ndefu wasafirizo ni za bure. Hawakuweza kuelewa maana ya msamaha wa dhambi kwa njia ya imani katika Kristo. Walitosheka tu na njia zile za Roma ilizowapangia. Kwao waliwatumaini mapadri na papa ili wawapatie ukombozi wala hawakujishughulisha na usafi wa moyo.

Lakini watu wengine walipokea habari ya wokovu kwa njia ya kumwamini Kristo kwa furaha kuu. Kwa imani wakupokea damu ya Kristo kuwa ndiyo njia ya kuwapatia wokovu. Watu hawa walirudi makwao wakawatangazia wenzao habari njema hii aliyoipokea. Kwa njia hii ukweli ulienea toka mji mpaka mji mwingine. Hesabu ya wasafiri waliokuwa wanamwendea bikira ikapungua. Hivyo matoleo yalipungua, hata mshahara wa Zwingli pia ukakatwa, maana ulitokana na matoleo hayo. Lakini jambo hili lilimfurahisha kwa kuona uwezo wa ushirikina unavunjika. Ukweli ulizidi kushikwa na watu wengi.

Zwingli Aitwa Kwenda Zurich

[81]

Baada ya kupita miaka mitatu, Zwingli aliiitwa ili akahubiri katika kanisa kuu la Zurich, ambao ni mji maarufu sana katika Uswiss. Mvuto ambao ungeonyeshwa hapo ungeenea sana. Makasisi hawakukawia kumwongoza kuhusu kazi zinazompasa. Wakamwambia: “Utafanya bidii sana kukusanya mapato ya wakuu wa kanisa, bila kuachia hata kidogo kidogo. . . . uangalie sana kuongeza mapato katoka kwa wagonjwa, na kwa waabudu na kutoka katika huduma ya makasisi” “Kuhusu usimamizi wa huduma ya pasaka, na mahubiri, na utunzaji wa kundi . . . Unaweza kubadili mambo hasa mafundisho unayohubiri”.

Zwingli alisikiliza maagizo hayo kwa utulivu, kisha alijibu “Maisha ya Kristo yamefichika kwa watu siku nyingi sana. Mimi nitahubiri Injili ya Mathayo yote kama ilivyo Huduma yangu itakuwa lengo la kumtukuza Mungu, na kumtukuza Mwana wake Yesu Kristo, na kudhihirisha njia wazi ya wokovu, na imani ya kweli inayotakiwa”.

Watu walimiminika ili kusikia mahubiri yake. Alianza huduma yake kwa kufundisha mambo ya Injili zote, na kueleza habari za maisha na kazi ya kifo cha Kristo. Akasema. “Mimi nia yangu ni kuwaogoeni kwa Kristo ambaye ndiye asili ya wokovu.” Watu wataalamu wakuu, wenye elimu, na wakulima walimsikiliza Zwingli kwa makini. Aliyalaani maovu yanayotendwa na kanisa la Roma wazi wazi bila hofu. Wengi walikuwa na furarha na kumtukuza Mungu kwa mahubiri hayo. Walisema “Mtu huyu ni mhubiri wa ukweli. Atakuwa mkombozi wetu kama Musa, atakayetuongoza

kutoka katika giza la Misri” Baada ya muda upinzani ulitokea. Watawala walimshambulia kwa maneno ya dharau wakimcheka na kumdhihaki. Wengine walikuwa wakimwendea na kumfanyia ufedhuli na kumtisha. Lakini Zwingli aliyavumilia yote hayo.

[82] Mungu anapoandaa kuvunja pingu za ujinga na ushirikina, shetani naye hujitahidi sana kuwafunga watu wakae gizani. Roma ilijitahidi mno kueneza masoko yake ya kuuzia vyeti vya msamaha wa dhambi. Waliweka viwango mbalimbali vya dhambi na bei yake. Kama hazina ya kanisa ilikuwa imejaa vyeti vya msamaha wa dhambi vilitolewa bure. Kwa hiyo misimamo miwili ilikuwa inaendelea kusambaa: Roma inauza vyeti vya kusamehewa dhambi na kujaza hazina yake na Watengenezaji wa Kanisa wakilaani dhambi na kuwaelekeza wenye dhambi kwa Kristo ambaye ndiye mwokozi wao

Uuzaji wa Vyeti Vya Msamaha Huko Uswiss

Katika nchi ya Ujerumani uuzaji wa vyeti vya msamaha uliendesha na mdhalimu Tetzl. Katika Uswisi biashara hiyo iliwekwa mikononi mwa mtawa mmoja wa Kiitalia aitwaye Samson. Samson alikuwa amepata fedha nyingi kwa kazi hiyo kutoka Ujerumani na Switerland akaziweka katika hazina ya mapapa. Sasa alipitia Switzerland akiwanyang’anya wakulima maskini mapato yao, ili kuongezea utajiri juu ya utajiri. Mtengezezaji wa kanisa ambaye ni Zwingli, mara moja alijitolea kumpinga. Huo ulikuwa ushindi wa Zwingli wa kumbainisha mtawa huyo katika maazimio yake, na mwisho aliondoka kwenda mahali pengine. Huko Zurich Zwingli alihubiri kwa nguvu sana akipinga uovu na mfanya biashara huyu wa kuuza msamaha. Samson alipofika mahali alipokwenda alipata ruhusa ya kuingia hapo kwa njia ya udanganyifu. Lakini alipogunduliwa alifukuzwa bila kuuza cochote na mwisho akaondoka Switzerland.

Tauni kubwa ilipiga nchi ya Uswisi katika mwaka wa 1519. Watu wengi waliona kuwa ilikuwa kazi bure kununua vyeti vya msamaha. Kwa hiyo walitamani kupata msingi wa hakika wa kusimamia imani yao. Huko Zurich Zwingli alipatwa na ugonjwa, na habari zilienea kuwa amekufa. Katika saa ya giza kama hiyo aliu-tazamia msalaba wa kalwari na kujikabidhi kamili kwake Mweza,

akiwa na uthibitisho wa kusamehewa dhambi. Alipoona na kuondoka katika lango la mauti alihubiri Injili kwa nguvu zaidi kuliko kwanza. Watu wenyewe walikuwa wametoka katika hatari ya kifo cha tauni, kwa hiyo waliona thamani ya Injili kwa upya zaidi.

Zwingli mwenyewe alikuwa amefikia ujuzi dhahiri wa ukweli, na alikuwa ameona uwezo wa Injili katika maisha yake. Alisema “Kristo... ametununulia wokovu usio na mwisho. Hamu yake, dhabihu yake ya milele, na uwezo wake wa kuponya milele, hufanya haki yake itosheleze kila mtu anayemtumaini kwa imani isiyotikisika. Popote palipo na imani kwa Mungu juhudi huonekana ambayo huwabidisha watu ili watende matendo mema”

Matengenezo ya Kanisa yaliendelea hatua kwa hatua katika Zurich. Adui wa mtengenezaji walijitokeza wazi wazi na hatari hiyo ilionekana. Mara kwa mara Zwingli alipata mashambulio ya maneno. Kila mara sauti ilisikika ikisema, “Mwalimu huyu mzushi lazima anyamazishwe”. Askofu wa Constance alituma wajumbe watatu katika baraza au mahakama ya Zurich, akimshitaki Zwingli kuwa anahatarisha amani na kuleta machafuko katika jamii. Akasema “Kama uongozi wa kanisa ukikaa kimya kitakachotokea ni machafuko nchini”

[83]

Baraza lilisita kuchukua hatua yoyote juu ya Zwingli. Roma ikaandaa mashambulio mapya. Zwingli akasema “Haya na waje; hofu yangu kwao ni sawa na hofu ya genge litokezalo juu ya maji ya bahari linavyoogopa mawimbi yanayovuma chini yake” Bidii ya wakuu wa Roma ya kuzima kazi ya Zwingli iliisukuma mbele zaidi. Ukweli wa Injili uliendelea mbele. Katika Ujerumani wale wafuasi waliorudi nyuma kwa kutokuwepo Luther, waliamka tena na kusimama upya kwa kadiri walivyooona maendeleo makubwa katika Uswisi. Kwa jinsi matengenezo yalivyostawi katika Zurich, matunda yake yalionekana zaidi katika kushinda uovu na kuimarisha utaratibu wa kweli.

Mabishano Pamoja na Roma

Wafuasi wa Roma walipoona kuwa mateso hayakufaulu kuvunja mafundisho ya Luther katika Ujerumani, waliazimia kushindana na Zwingli. Walihakikisha ushindi wao kwa njia ya mabishano ya wazi na kwa kuchagua waamuzi ambao wangeamua ukweli ulivyo. Kama

wangemshinda Zwingli wangehakikisha kuwa asingeponyoka toka mikononi mwao. Kusudi hili walilificha kabisa.

Mahojiano yalipangwa yafanywa huko Baden. Lakini baraza la Zurich likishuku juu ya makusudio ya mapapa na kwa kuhadharishwa na wingi wa marundo ya kuni ya kuchomea wanaofuata imani ya watengenezaji wa kanisa, walimzuia mchungaji wao asijihudhurishwe kwenye mahojiano hayo ya hatari. Kwenda Baden, ambako damu za wafia dini wengi zimemwagwa, hakika ilikua kwenda mautini. Oecolampadius na Haller walichaguliwa wakamwakilishe Zwingli katika mabishano hayo na Dr. Eck alikuwa akiitetea Roma huku akiungwa mkono na wataalamu na makasisi wengi.

Waandishi wa mambo hayo wote walichaguliwa na Roma na wengineo wote walikatazwa kuandika lolote au sivyo, wangepata adhabu ya kifo. Walakini wanafunzi waliohudhuria waliandika mambo hayo kila siku jioni baada ya maojiano. Maneno hayo yaliyoandikwa na yalitumwa kwa Zwingili kila siku na wanafunzi wawili, pamoja na barua za Oecolampadius. Kila siku Zwingli alijibu na kutoa ushauri. Ili kuepa udhia wa walinda mlango, watu hao walikuwa wakibeba makapu ya kuku, kwa hiyo walikuwa wakiruhusiwa kupita bila taabu.

[84] Myconius alisema “Zwingli amefanya mengi zaidi kwa njia ya maombi, na kukesha, pamoja na kushauri kuliko vile ambavyo angehojiana na adui zake uso kwa uso”

Warumi walihudhuria huko Baden katika mavazi yao rasmi na taji zenye kung’aa vichwani mwao. Vyakula vyao vilikuwa vya kianasa kabisa. Kinyume cha hayo walionekana watengenezaji wa kanisa wakiwa katika hali ya kawaida, na chakula chao cha kiasi tu. Mwenye nyumba waliyokuwa wakikaa alikuwa akimtembelea Oecolampadius mara fulani fulani, na kila mara alimkuta akisoma, au akiomba. Taarifa aliyotoa alisema, “Mtu huyu mzushi ni mcha Mungu sana”

Kwenye mkutano, Eck alipanda madhabahuni kwa kiburi, huku akiwa amevalia rasmi kabisa, mavazi yenye kumetameta na wakati ule ule mnyenyekevu Oecolampadius akiwa na nguo zake za kawaida tu, alilazimika kuketi juu ya kiti kidogo mbele ya mpizani wake. Eck mwenye sauti ya ngurumo alikuwa na hakika ya kufaulu. Mtetea imani angekuwa atunukiwe hadhi ya utaalumu. Kama

majadiliano ya kawaida yangeshindikana, aliazimu kutumia matusi hata kuapiza.

Oecolampadius mpole, mwenye kujitumaini aliyakimbia mashindano. Ingawa ni mpole, jasiri mwenye nia thabiti alijithubutisha kuwa mtu imara asiyenymbayumba. Mtengenezaji wa kanisa aliambatana na Maandiko matakatifu. Alisema “kawaida tu, hazina nguvu katika Uswisi, isipokuwa zinaambatana na katiba. Lakini kuhusu mambo ya imani, Biblia ndiyo katiba yetu”

Hoja za kweli za mtengenezaji wa kanisa, zilitolewa kwa utulivu, ziliwaingia watu waliokusanyika, wakayadharau maneno ya Eck ya majivuno matupu.

Majadiliano yaliendelea siku kumi na nane. Wafuasi wa papa wakadai kuwa wameshinda. Wakuu wengi waliunga Roma mkono. Wakatangaza kuwa wafuaasi wote watengenezaji wa kanisa pamoja na Zwingli wameharamishwa na kufutwa kanisani. Lakini mashindano yalikuwa matokeo ya mvuto wa kuendelea katika njia ya upinzani. Muda haukupita, miji mashuhuri ya Bern na Basel ikajitangazia kuunga mkono matengenezo ya kanisa.

Marejeo:

Wylie, bk. 8. ch. 5

ibid bk. 8, ch. 6

D’Aubigne bk. 8 ch. 9

Ibid. bk. 8 ch. 9

Ibid

Ibid bk. 8, ch. 6

Ibid.

Ibid. bk. 8 ch. 9

Wylie bk. 8 ch. 11

D’Aubigne bk. 11 ch. 13

Ibid.

10/Maendeleo Katika Ujerumani

Kutoweka kwa Luther kwa siri kuliwataharukisha na kuwatia hofu watu wote wa Ujerumani. Uvumi mwingi ulitokea, na wa watu wengi waliamini kuwa ameuawa. Maombolezo mengi yalitokea na watu wengi walifunga kwa kiapo kwamba watalipiza kwa kifo chake. Ijapokuwa adui zake walifurahi hapo mwanzo kwa kudhania kuwa Luther amekufa, lakini baadaye walifadhaika kujua ya kuwa amefungwa tu, wala hakufa. Mmoja wao alisema, “Kitakachotuokoa ni kumtafuta kwa bidii mahali popote duniani, tumlete katika nchi maana taifa zima linamhitaji”. Habari za kwamba Luther yu hai, tu analindwa mahali fulani, ziliwatuliza watu. Na maandiko yake yaliyopokelewa watu waliyasoma kwa hamu kuliko hapo mwanzo. Watu wengi walizidi kujiunga na shujaa huyu aliyelitetea neno la Mungu.

Mbegu zilizopandwa na Luther ziliota kila mahali. Kutokuonekana kwake kulitimiza mengi ambayo yasingalitimizwa na kuwako kwake. Na sasa kwa kuwa kiongozi wao mkuu ameon-dolewa, budi wengine waendeleze kazi hiyo iliyoanzishwa isije ikazuilika.

Sasa Shetani alijaribu kuingiza kazi hiyo, kwa kuharibu misingi ya kweli na kutia mambo bandia. Kama vile kulivyozuka manabii wa uongo katika karne ya kwanza vivyo hivyo hata katika karne ya kumi na sita walizuka.

Watu wachache walijidai kuwa wamepata ufunuo kutoka mbin-guni ili waendeleze kazi ya matengenezo ya kanisa, ambayo walidai kuwa ilianzwa kwa unyonge na Luther. Kwa hakika hawakufanya kazi iliyofanywa na Luther na kukamilisha. Wao walikataa kanuni za utengenezaji, kwamba neno la Mungu ndilo mwongozo wa imani na maisha budi kufuatana nalo. Walipoacha neno la kweli la Mungu wakajiwekea kanuni zao zisizo za hakika kwa kufuata maoni yao.

Wengine ambao kwa asili ni watangatangaji walijiunga nao. Watu hawa waliendelea vikubwa sana, na kuleta msisimko mkubwa. Luther alikuwa amewaamsha watu na kuwaweka katika maten-

genezo kamili, lakini sasa watu hawa wamepotosha watu wa kweli wa Mungu. Wao ni manabii wa uongo.

Viongozi wa kundi hili walitupa madai yao juu ya Malancthon, wakisema, “Tumetumwa na Mungu kufundisha watu, tumekuwa na maongezi na Bwana tunafahamu matokeo yake, Sisi ni mitume na manabii. Walimtaja Luther awe mmoja wao.”

[86]

Watengenezaji wa kweli walitatanishwa. Melancthon alisema, “Katika watu hawa, kwa kweli kuna roho nyingine ndani yao. Lakini ni roho ya aina gani hiyo? Kwa vyovyote tujitahadhari tusije tukakufuru Roho wa Mungu, pia tujitahadhari tusije tukapotoshwa na roho wa Shetani”

Matunda ya Mafunzo Yadhihirika

Watu waliongozwa kinyume kabisa. Walifundishwa kutojali Biblia isemavyo, au kushika Biblia kidogo tu. Wanafunzi wakitupilia mbali vizuizi vyote, walitoka katika vyuo vilivyokuwa vikiwapa mafunzo, wakaendeleza mbele kazi ya matengenezo, ndiyo walioiharibu na kuangamiza. Sasa Waroma walijipa moyo, na kusema kwa majivuno “Shambulio moja tu la nguvu, na wote watakuwa mateka wetu”.

Luther akiwa huko Wartburg aliposikia mambo yaliyotokea alisema kwa kusisitiza “Mimi kila mara nilitazamia kuwa shetani atatuletea tauni hii.” Alifahamu tabia ya kweli ya hao waliojifanya kuwa manabii ilivyokuwa. Upinzani wa hao waliojifanya kuwa manabii ilivyokuwa. Upinzani wa papa na wa falme haukutetea wasiwasi kama ilivyo hivi sasa. Kutokana na watu waliojifanya kuwa marafiki wa watengenezaji wamezuka maadui wakali zaidi walioleta machafuko na matatizo katika kazi hii.

Luther alikuwa amesukumwa na Roho wa Mungu kuendesha kazi hii, naye alifanya. Walakini alitetemeka kwa matokeo ya kazi yake. Alisema, “Kama ningalijua kuwa kazi yangu ingemwumiza hata mtu mmoja tu ingawa awe mdogo ambavyo sivyo, maana ni Injili yenyewe, ingekuwa bora mara kumi mimi nife, kuliko kupotosha, na kupotoka”.

Mji wa Wittenberg wenyewe umeangukia katika udhalimu na machafuko. Maadui wa Luther walikuwa wakimlaumu Luther aliliza kwa uchungu, “Je, hayo yaweza kuwa ndiyo mwisho wa kazi

hii kubwa ya matengenezo ya kanisa?” Lakini alipokuwa akimlilia Mungu kwa njia ya sala, amani ilijaza moyo wake. Alisema “Kazi hii siyo yangu, bali ni kazi yako” Lakini aliazimu kurudi huko Wittenberg.

[87] Alikuwa amezuuliwa na utawala. Adui zake walikusudia kumwulia mbali, nao walikuwa huru kufanya hivyo. Rafiki zake walikatazwa kumlinda au kumsaidia. Lakini yeye aliona kuwa kazi ya Injili inahatarishwa. Kwa hiyo akatoka kwa jina la Bwana bila hofu akaitetea Injili. Katika barua aliyomwandikia mtawala, Luther alisema “Ninakwenda Wittenberg chini ya ulinzi mkuu kuliko ule wa wakuu na watawala. Sifikiri kukuomba msaada wa ulinzi, lakini badala yake mimi natamani kukulinda. Hakuna silaha itakayoendesha kazi hii. Mungu pekee yake ndiye awezaye kuifanya.” Kutoka barua ya pili Luther, alisema, “Mimi niko tayari kushutumiwa na wewe, ee mfalme, na kukasirikiwa na ulimwengu wote, je, watu wa Wittenberg sio kondoo zangu? Nami hainipasi kufa kwa ajili yao ikilazimu?”

Uwezo Wa Neno

Haukupita muda mrefu habari ikatangazwa katika Wittenberg kwamba Luther amerudi, na ndiye atakayehubiri. Kanisa likajaa tele. Naye kwa hekima kubwa na katika hali ya kiungwana aliwafundisha akisema “Misa ni kitu kibaya sana, Mungu anapinga, lazima iondolewe. Lakini mtu asiondelewe kwayo kwa nguvu. Neno la Mungu ndilo liondoe sio sisi. Ni haki yetu kusema, hatuna haki kuchukua hatua. Sisi tuhubiri, yaliyosalia ni ya Mungu. Kama mimi nikitumia nguvu, nitapata nini? Mungu hushughulika na roho, na roho ikiwa sawa mambo yote yatakuwa barabara.

Nitahubiri, nitaongea na nitaandika, lakini sitafaulu kwa lolote, maana imani ni hiari ya moyo. Nilipingana na papa, na kupinga vyeti vya msamaha pamoja na mafundisho yote ya Roma, lakini sikutumia nguvu wala kufanya ghasia. Nilitanguliza neno la Mungu, nilihubiri na kuandika. Hivyo ndivyo nilivyofanya. Hata hivo wakati nilipokuwa ninalala... maneno niliyohubiri yaliubomoa upapa, wala wakuu na watawala hawakufanya hivyo; Wala kuyadhuru. Mimi sikufanya kitu, neno lenyewe lilifanya. Neno la Mungu lilivunja

ushupavu wote wa kijinga. Injili tu iliwarudisha waliopotoshwa katika njia ya kweli.”

Baada ya miaka kadhaa kupita, hali ya ushupavu wa dini ulizuka kwa jinsi ya kutisha, ukaleta matokeo mabaya. Luther alisema, “Kwa watu hawa maandiko matakatifu yalikuwa kama herufi zilizokufa. Nao wakaanza kulia, Roho, Roho!” kwa kweli mimi sitafuata njia ambayo roho wao anawapeleka.

Thomas Munzer, mmoja wa watu hao wapotofu, ambaye ni mtu mwenye uwezo, naye hajui lolote la dini, yeye alikuwa na tamaa ya kuutengeneza ulimwengu kama wengine wenye juhudi wafanyavyo, lakini alisahau kuwa watengenezaji wote huanzia matengenezo kwao wenyewe kwanza. Hakutaka kuwa wa pili kwa Luther, maana alijidai kuwa yeye ndiye aliyepewa agizo na Mungu kufanya matengenezo halisi. Alisema kuwa mwenye roho ya jina hili anayo imani ya kwenda ingawa hasomi Biblia katika maisha yake.

[88]

Watu wa aina hii hujitoa ili waongozwe na maoni na kujisikia katika hali ya msimko. Baadhi yao walichoma Biblia. Mafundisho ya Munzer yalipokewa na watu maelfu. Mwisho akafundisha kuwa kuwatii wakuu na watawala ni sawa na kumtumikia Mungu na Baali.

Matengenezo ya Munzer na mafundisho yake yaliwaongoza watu waasi kupata mamlaka yote. Matokeo yakawa vita na fujo, na mabonde ya Ujerumani yalijaa damu za watu kwa ajili ya vita.

Maumivu Ya Roho Yaliwekwa Juu ya Luther

Wafuasi wa papa walitangaza kuwa maasi yote yaliyotokea yametokana na mafundisho ya Luther. Malaumu hayo hayakumhuzunisha Luther sawa na kule kuhesabu ukweli aliohubiri kuwa sawa na upotovu wa hawa washupavu wa dini. Waongozi wa kundi hili walimchukia Luther. Luther hakuyakanusha mafundisho yao tu, bali pia aliwalaumu kwa ajili ya maasi yao juu ya wenye mamlaka. Wao nao walimwita kuwa mtu mwovu ajifanyaye mfuasi.

Wafuasi wa Roma walikuwa wakitazamia maanguko ya utengenezaji wote wa kanisa. Wakalaumu Luther kwa makosa ambayo anasahihisha kwa juhudi. Wale wapotoshaji walidai kuwa wanatendewa ukatili, na kujihesbu katika kundi la wafia dini, nao waliungwa mkono na Waroma. Wapinzani hao walisifiwa na kuungwa mkono.

Hali ilikuwa kazi ya roho ile ile iliyojitokeza mbinguni ambayo ni roho ya uasi.

Shetani daima anatafuta kuwadanganya watu na kuwaongoza katika upotevu wa kuita dhambi kuwa haki, na haki kuwa dhambi. Maigizo kuwa kweli, kujipendekeza kuwa utakaso. Roho ya namna hiyo ingali inafanya kazi kama siku za Luther, ikiwaongoza watu waende mbali na Maandiko matakatifu, ili wafuate maoni yao na maongozi ya watu, badala ya maongozi ya sheria ya Mungu.

Luther alitetea Injili bila hofu katika upinzani. Alipigana na udhalimu wa Roma, akitumia Neno la Mungu. Alisimama imara kama mwamba akipingana na upotovu uliotaka kuunganika na kazi ya matengenezo ya kanisa.

[89] Vikundi hivi vya upotovu, kila kimoja kiliweka Biblia kando, kikatukuza hekima ya binadamu, na kujifanya kuwa kanuni ya dini ya kweli. Waroma wakijidai kuwa walipata utaratibu wao moja kwa moja tokea mitume, madai hayo yalitoa nafasi kubwa kwa ajili ya upotovu na udhalimu ulioingia kanisani kwa kifuniko hicho. Madai ya Munzer ya kwamba amefunuliwa na Mungu ambayo ni ya kipumbavu yaliongeza udhalimu. Ukristo wa kweli huongozwa na Neno la Mungu ambalo ndilo kipimo cha kupima madai ya kila namna.

Luther aliporudi kutoka Wartburg, alikamilisha kazi yake ya kutafsiri Agano Jipya, na injili katika lugha ya Kijerumani, na mara baadaye watu wa Ujerumani wakapata Neno la Mungu katika lugha yao. Tafsiri hii ilipokelewa kwa shangwe kuu na watu wote walioipenda kweli.

Sasa makasisi walishindwa kwa kuwa watu wa kawaida wangeweza kuusoma ukweli na kuujadili pamoja nao tena kwamba wangepahamu mambo na kuung'amua ujanja wao wa kijinga na udanganyifu wao. Roma ikawakutanisha wakuu wake wote ili wachukue hatua ya kuzuia Agano Jipya lililotafsiriwa lisitolewe kwa watu. Lakini kadiri walivyozuia Maandiko Matakatifu yasisomwe, ndivyo hamu ya watu ilivyoamshwa ili wachunguze na kuona ukweli ulivyo. Watu wote waliojua kusoma walinunua na kusoma na kukariri mafungu moyoni kwa wingi. Mara moja Luther alianza kutafsiri Agano la Kale.

Maandiko ya Luther yalipokewa mijini na mashambani katika nyumba za watu. Luther na rafiki zake walipomaliza sehemu fulani,

wengine walichukua na kueneza kwa watu. Watu walikubali upigaji marufuku wa vitabu hivi katika nyumba za watawa, lakini waliviuza vitabu vya Luther na rafiki zake, ingawa wenyewe hawakuweza kueleza Maandiko Matakatifu kwa usahihi. Mwisho Ujerumani ilifunikwa na jeshi hili la wauza vitabu.

Mafunzo ya Biblia Po Pote.

Wakati wa usiku walimu wa skuli waliwasomea vikundi vya watu vilivyokusanyika vikiwa kando ya moto wa jioni. Kwa njia mbali mbali watu waliongolewa. “Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga” Zaburi 119:130.

Wafuasi wa Roma, mapadri, makasisi wote waliitwa ili kila mtu awe tayari kukanusha mafundisho haya mapya. Lakini wakiwa gizani kabisa kukanusha mafundisho haya mapya, bila ujuzi wote wa Biblia walishindwa kukanusha ukweli huu. Mkatoliki mmoja aliandika, akiwa na masikitiko “Luther amewashawishi wafuasi wake wasiamini kitu kingine ila Maandiko Matakatifu peke yake” Watu waliweza kukusanyika ili kumsaikiliza mtu wa kawaida tu asiye na elimu ya juu, akiwahubiri. Aibu kubwa iliwapata watu maarufu, walipohojiana na watu wadogo walio na ukweli wa Neno la Mungu na kushinda vibaya, Vibarua askari, wanawake hata na watoto walifahamu Biblia kuliko makasisi na wataalamu. [90]

Vijana wenye mawazo mazuri walijitoa kujifunza Biblia, wachunguza maandiko na sehemu mbalimbali za Biblia ili wazoe na mafungu mbalimbali. Vijana hawa walikuwa waelekevu sana, na mioyo yao ilizingatia maneno mengi ya Maandiko, hata haikuwezekana kuwashinda. Watu waligundua katika mafundisho mapya haya mambo yale ambayo mafunzo ya Roma hayakuweza kuwatosheleza. Nao waliyatupilia mbali mambo yale ya Roma ambayo yalikuwa ya bure, yaliyojengwa kwa hadithi za biandamu.

Wakati mateso yalipotokea juu ya walimu hawa wa kweli hawakuyajali, ila walilishikilia neno la Mungu. “Watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine” Mathayo 10:23. Basi wakimbizi hawa wakapata mahali fulani wenye huruma wakawapatia msaada, na hao wakaendelea kumhubiri Kristo. Mahubiri yao pengine yalifanywa nyumbani au kanisani au uwanjani, ukweli ukaenea kwa nguvu ya ajabu.

Wakuu na watawala walijitia kuwatesa, kuwafunga, kuwachoma moto, lakini yote ilikuwa kazi bure. Watu maelfu walifunga maisha yao kwa damu zao wenyewe. Walakini mateso yalizidi kueneza injili tu. Wale watu wapotevu ambao shetani aliwaingiza ndani walidhirisha tu na kupambanua ukweli wa Mungu na uongo wa shetani.

Marejeo:

D'Aubigne, bk. 9, ch. 1

Ibid. bk. 9, ch. 7

Ibid.

Ibid.

Ibid, bk. 9 ch. 8

Ibid.

Ibid. bk. 10 ch. 10

Ibid. bk. 9 ch. 8

Ibid. bk. 10 ch. 10

Ibid. bk. 9, ch 11

Ibid.

Moja ya shuhuda bora kabisa zilizotolea kuhusu Matengenezo ilikuwa ushuhuda uliotolewa na watawala wa Ujerumani katika mkutano uliofanyika huko Spires katika mwaka 1929. Ujasiri na ushujaa wa watu hao wa Mungu ulipata uhuru wa dhamiri wa kudumu kwa ajili ya vizazi vijavyo, na kulipatia kanisa la matengenezo jina la “Protestant”

Mungu alikuwa amezuia majeshi ya upinzani ambayo yalikuwa yanapinga ukweli. Charles V alikazana kuangamiza matengenezo lakini kila mara alipounyosha mkono wake ili atende madhara, alilazimika kwa njia fulani kutotenda kitu. Tena na tena wakati ilipoonekana hatari kuu inakabili Matengenezo, majeshi ya uturuki yalionekana kwenye mpaka, au majeshi ya ufaransa, au papa mwenyewe alipingana nayo. Hivyo basi katikati ya misukosuko na ghasia za mataifa, matengenezo yalizidi kuwa imara na kuenea.

Walakini mwishowe utawala wa papa ukalifanya jambo la kupinga watengenezaji kuwa jambo la kawaida. Mfalme aliitisha baraza likutane huko Spares katika mwaka wa 1529 ili kupanga jinsi ya kuangamiza uzushi. Kama njia za kawaida amani zingeshindwa, Charles alikuwa tayari kutumia nguvu yaani silaha.

Wafuasi wa papa katika baraza la Spires walidhihirisha wazi uadui na chuki yao juu ya watengenezaji. Melancton alisema, “Tumekuwa machukizo na takataka katika ulimwengu, lakini Kristo atatazama hapo chini kwa watu wake maskini, na atawatunza”. Watu wa Spires wakiwa na kiu ya Neno la Mungu walifurika katika kanisa, bila kujali vizuizi vilivyowekwa ili kufanya ibada halali. Jambo hili liliharakisha hatari. Uhuru wa dini ulikuwako kisheria, na wainjilisti walikusudia kuwaondolea haki yao ya uhuru wa dini. Mahali pa Luther palikuwa pameshikwa na watendakazi wengine, na wakuu ambao Mungu aliwainua ili kulinda kazi hii. Fredrick wa Saxony alikuwa amefariki, lakini Duke John aliyewekwa badala yake aliyakaribisha Matengenezo na kuyaunga mkono.

Makasisi walidai kwamba majimbo ambayo yamekubali matengenezo yafanyike kwao lazima yasalimu amri na kukubali uamuzi wa Kiroma. Watengenezaji wa upande wao wasingekubali hata kidogo kuwa majimbo yaliyopokea Neno la Mungu yawekwe chini ya utawala wa Roma.

[92] Mwisho ilikusudiwa kuwa, pale ambapo matengenezo haya-jafanyika, sheria ya Worms itumike; na kwamba pale ambapo watu hawafuati matengenezo bila hatari ya kuasi na miisho ya misa, wala wasiruhusu Roman Catholic kuwaingilia watu wa Luther. Wakuu waliamua hivyo. Uamuzi huo uliwaridhisha makasisi na maaskofu.

Jambo Kubwa Hatarini

“Kama sheria hii ikitumika, matengenezo hayataendelea mbele, wala kuimarishwa kwenye msingi ulio imara, mahali ambapo yameanzishwa” Uhuru ungepigwa marufuku. Kuongoa roho kusingeruhusiwa. Tumaini la ulimwengu lingezimika.

Watu wa Chama cha Injili walitazamana kwa fadhaa. Je, na itakuwaje, waongozi wa matengenezo watasalimu amri na kukubaliana na sheria hiyo? Wafuasi wa Luther, yaani Walutheri walihakikishiwa uhuru wa dini. Fadhili zile zile ziliwafikia watu wao ambao kabla ya hapo walishirikiana na maoni ya watengenezaji. Je, hayo hayawezi kuwaridhisha?

Waliangalia kanuni hii kwa furaha, na wakatenda kwa imani, Je, kanuni hiyo ilikuwa ipi? Ilikuwa kwamba ni haki Roma ipige marufuku uhuru wa kutoa maoni na maswali ya udadisi Je, sio wao wenyewe na Waprotestanti wao kufurahia uhuru wa dini? Ndiyo, fadhili tu za kimasharti, lakini siyo haki. Ukubali wa mpango huu ungekuwa kwamba uhuru wa dini uwe katika Sazoni pekee yake, ambayo imekubali matengenezo, lakini mahali pengine pote maswali ya dini na kuhusu matengenezo vihesabike kuwa ni makosa, na lazima viadhibiwe kwa njia ya kifungo gerezani na kuchomwa moto. Itakubalika kuwa na uhuru wa dini katika tarafa tu? Je, watengenezaji wataridhika kwamba wao ni wema wala hawana hatia kwa damu ya watu maelfu watakaofuata mpango huu ambao watapaswa kutoa maisha yao katika nchi ya Kiroma.

“Hebu tukatae agizo hili” Huo ulikuwa usemi wa wakuu. Kuhusu mambo ya dhamiri, hakuna haja ya ukubali wa wengi. Kulinda uhuru

ni kazi ya serikali, pale ambapo serikali haina nguvu ni kuhusu mambo ya dini.

Wafuasi wa papa wameweka masharti kwa ukaidi wao. Wawakilishi wa miji huru walilazimika kutangaza kwamba watakubaliana na makusudio hayo. Walitaka wapewe muda wa kufikiri, lakini ilikuwa kazi bure. Katika nusu walioungana na watengenezaji wakijua kuwa siku zao za usoni zitakuwa na mateso na matatizo. Mmoja wao alisema “Yatupasa kulikataa neno la Mungu, au kuchomwa moto.”

[93]

Msimamo Bora wa Wakuu

Mfalme Fredinand mwakilishi wa mfalme mkuu alijaribu kutumia mvuto wa ushawishi. Aliwaomba wakuu waikubali amri iliyotolewa akiwahakikishia kuwa hata mfalme mkuu atapendezwa. Lakini watu hawa waaminifu walijibu kwa uthibiti wakisema “Tutamtii mfalme kwa kila jambo lenye kuleta amani na lenye kumtukuza Mungu”

Mwishowe mfalme alitangaza kwamba jambo lililobakia ni kufuata wingi wa watu. Baada ya kusema hivyo aliondoka bila kuwapa watengenezaji nafasi ya kujibu. Walituma ujumbe kwake, wakimwomba arudi. Yeye alijibu, “Imeamuriwa kufuata kama ilivyoamuriwa ndilo jambo lililobaki”

Wajumbe wa serikali walijivuna wenyewe kwamba shauri lao na la papa limefaulu na kuwa mambo ya watengenzaji yameshindwa. Kama watengenezaji wangelitegemea msaada wa kibinadamu peke yake, mambo yao yangalikuwa kazi bure, kama wafuasi wa papa walivyodhani. Lakini wao waliomba kutoka katika taarifa ya baraza kuhusu neno la Mungu na kuhusu mfalme Charles kwa Yesu Kristo, mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Kwa vile Ferdinand alikataa kutambua haki ya imani ya dhamiri zao, watawala waliamua kuendelea na mipango yao bila kujali kutokuwako kwake. Hasa kuleta maazimio ya mbele ya baraza la taifa bila kuchelewa. Basi tamko rasmi lilitayarishwa na kuletwa mbele ya baraza. Tamko lilisema, “Sisi tunapinga azimio au amri iliyotolewa pamoja na jambo lolote ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu, kwamba hatutakubaliana nayo kwa ajili yetu wenyewe, na watu wetu kwa ajili ya wokovu wa roho. Tunapinga hayo kwa ajili ya uhuru na haki ya dhamiri zetu. Kwa hiyo tunakataa kutiwa

chini ya kongwa. Na wakati ule ule matazamia yetu ni kwamba mtukufu mfalme atatufikiria kwa wema kama mkristo na mjumbe wa Mungu anayempenda kuliko kitu kinginecho; na sisi tunatamka rasmi kuwa tuko tayari kujitoa kwake kamili na kwako, tukiitii na kutumika na kutoa upendo wetu kwa kila kazi njema. Hivyo ndivyo haki na wajibu wetu”

[94] Wengi walishangaa kwa ujasiri wa hawa wapingaji. Ikaonekana kuwa, mafarakano na ugomvi na kumwagika kwa damu vitatokea. Lakini watengenezaji huku wakimtegemea Mungu walikuwa watulivu na wenye moyo mkuu.

Kanuni zilizokuwamo katika maazimio haya ya upingaji wa dhamiri kuliko mahakama, na uwezo wa Neno la Mungu kuliko maagizo ya kanisa. Manabii na mitume wanasema, taji ya mfalme Charles V waliinua taji ya Kristo. Wale wapingaji wa Spires walikuwa mashahidi halisi na watetea dini kweli, waliotafuta uhuru wa dini ili kila mtu amwabudu Mungu kufuatana na dhamira yake.

Hali ya watengenezaji hawa na kanuni zao hutoa fundisho kwa wote kwa vizazi vijavyo. Shetani angali anapinga Neno la Mungu ambalo ndilo kiongozi halisi maishani. Katika siku zetu hizi kuna haja ya kurudi na kusimama katika kanuni za watengenezaji hao, yaani, Biblia na Biblia peke yake, ndiyo mwongozo katika mambo yote. Shetani angali anajitahidi kuharibu uhuru wa dini. Uwezo wa wapinga Kristo kama ule wa Spires unatafuta njia ya kujiimarisha sasa, kuuimarisha uwezo ule ulioangushwa na watu wa Spires.

Baraza la Augsburg

Viongozi wa Injili walikuwa wamekataliwa kusikilizwa shauri lao na mfalme Ferdinand, lakini ili kutuliza machafuko na mfarakano yaliyotokea ambayo yalitia wasiwasi nchini, Charles V, katika mwaka uliofuata mapinzani ya Spires aliitisha baraza huko Augsburg. Alisema kuwa yeye ndiye angekuwa mwenyekiti. Viongozi wa Protestant walialikwa.

Mteule wa Saxony alishauriwa na washauri wake kuwa si vizuri kujihudhurisha barazani, si kuhatarisha kila kitu? Maana hao ni maadui hodari. Lakini wakuu wengine walisema, “Hebu wakuu na wapatane wenyewe, ndipo kazi ya Mungu itasalimika.” “Mungu ni mwaminifu, hatatuacha” Hayo aliyasema Luther.

Mteule wa Sazony alianza safari kuelekea Augsburg. Watu wengi walikwenda kwa huzuni na mioyo mizito. Lakini Luther aliyefuatana nao mpaka Coburg, aliifufua imani yao kwa njia ya kuimba wimbo aliouandika njiani, usemao “Mungu wetu ndiye ngome” Watu wengi wenye mioyo mizito walichangamshwa.

Wale wakuu waliokubali matengenezo walikuwa wameazimu kupitisha shauri lao likiwa ni ushindi wa maandiko matakatifu, mbele ya baraza. Matengenezo ya maandiko matakatifu, mbele ya baraza. Matengenezo ya jinsi ya kulifikisha barazani mikononi mwa Luther, na Melanchthon na wenzao. Jambo hilo lilikubaliwa na waprotessant wote, na sasa walipaswa kutia majina yao katika mkataba huo.

[95]

Watengenezaji walikuwa wenye kuomba sana ili kazi yao isije ikachanganyika na mambo ya siasa. Wakuu wa Kikristo walivyokuwa wakiandika majina yao, Melanchthon alifoka, “Mambo haya tunayaazimia kwa ajili ya wanafunzi wa Biblia na wachungaji, basi na tutunze mambo mengine makuu ya nchi.” John wa Saxony akajibu “Mungu apishe mbali, kwamba mimi nisiwe pamoja nawe” Nimekusudia kutenda mambo yote yaliyo ya haki, bila kujali taji yangu. Natamani kumkiri Bwana. Uteule wangu na kinginecho havina thamani kwangu kama msalaba wa Kristo. Mkuu mwingine alisema huku akichukua kalamu, “Ikiwa kumtukuza Bwana Yesu Kristo kutahitaji vitu hivyo, mimi niko tayari kuviacha, hata maisha yangu yenyewe”. Akaendelea kusema “Ingefaa kabisa kuwaacha raia zangu na utawala wangu kuliko kusaliti nchi ya baba zangu” Tena, kamwe sitaweza.

Wakati ulipofika Charles V akakalia kiti huku akizungukwa na wateule na wakuu, akawakabidhi watengenezaji wa ukweli Injili ulielezwa dhahiri mbele ya wote na makosa ya Roma yalitajwa wazi wazi. Siku hiyo imejulikana kuwa siku kubwa kwa watengenezaji na siku mashuhuri kwa kanisa la Kikristo katika historia ya binadamu.

Watawa wa Wittenberg walikuwa wamesimama peke yao huko Worms. Sasa wanasimama mbele ya watawala wenye uwezo mkuu katika nchi. Basi Luther aliandika akisema “Ninafuraha kuu, kwamba nimeishi mpaka kufikia saa hii, ambayo Kristo ametangazwa dhahiri mbele ya watu na kuona siku hii ambayo ni maarufu sana katika watengenezaji.”

Mambo yale mfalme aliyapiga marufuku yasitangazwe mimbarani kinyume chake, yametangazwa kutoka katika jumba la kifalme na yale yaliyodharauliwa hata yasisikilizwe na watu wa maana, yamesikilizwa na wakuu na mabwana katika ufalme. Wakuu, watawala ndiyo waliokuwa wahubiri na mahubiri yenyewe yalikuwa ukweli wa Mungu. “Tangu siku za mitume hapajawa na kazi iliyotendwa kwa ukubwa kama sasa”.

[96] Mojawapo ya kanuni zilizosisitizwa na Luther ni kwamba pasiwepo na utafutaji wa misaada ya serikali ili kuendeshea kazi ya kanisa, yaani ya matengenezo. Alifurahi kwa kuwa Injili ilikiriwa na wakuu wa utawala, lakini walipojiunga ili kupinga, alitamka. “Mafundisho ya Injili yatalindwa na Mungu mwenyewe. Ujanja wote wa kisiasa ulioshuriwa, kwa maoni yake, ni wa bure, wa hofu na wenye matumaini ya dhambi.”

Baadaye Luther alisema kuhusu mwungano wa wakuu kupinga matengaenezo, “Silaha ya mashindano hayo ni upanga wa Roho. Alimwandikia mteule wa Saxony, Sisi kwa maoni yetu hatuwezi kufuta maazimio ya wakuu, lakini msalaba wa Kristo lazima usimame. Mtukufu mfalme usihofu. Sisi tutafaulu kwa njia ya sala zetu zaidi ya adui zetu kwa majivuno yao”

Uwezo mkuu kutoka katika mahali pa siri hata ukautikisa ulimwengu kuhusu watengenezaji. Huko Augsburg, Luther hakupitisha siku bila maombi, mara nyingi mara tatu kwa siku. Katika chumba chake alikuwa akisikika akimlilia Mungu katika maombi, yaliyojaa uchaji na matumaini. Alimwandikia Melancthon akasema, “Kazi hii ikiwa si ya kweli iache; lakini ikiwa ni ya haki, kwa nini tusiamini ahadi zake yeye aliyetuagiza na kutuambia kuwa tutulie bila hofu?”

Watengenezaji wa Kiprotestant wamejenga juu ya Kristo Milango ya kuzimu haitashinda.

Marejeo:

D.Aubigne, bk. 13, ch. 5

Ibid.

Wylie, bk. 9ch. 15

Aubigne bk. 13 ch. 5

Ibid.

ibid. bk. 13 ch. 6

Ibid.

ibid. bk. 14, ch. 2

Ibid. bk. 14, ch. 6.

Ibid. bk. 14, ch. 7 Ibid.

D'Aubigne — London ed. Bk. 10, ch. 14

Ibid. bk. 14 ch. 1

Ibid. bk. 14 ch. 16

12/Kwapambazuka Ufaransa

Upinzani wa Spires na ungamo la Augsburg vilifuatiwa na miaka ya mapambano makuu na machafuko kabisa. Uprotestant ukiwa umedhoofishwa na mafarakano, ulionekana ukielekea kufa.

Mfalme akitazamia kuwa atafaulu, ndipo kushindwa kwake kulimtokea ghafla. Mwishowe alilazimika kukubali kupitisha ushindi wa mafundisho aliyokusudia kuyaharibu tangu zamani. Aliona majeshi yake yakiangamizwa katika vita, hazina zake zikikaushwa na sehemu kubwa ya nchi yake ikikabiliwa na uasi, ambavyo imani ile aliyochukia na kuipinga ikizidi kustawi na kufanikiwa. Charles V amekuwa akijaribu kupigana na mwenyenzi na uwezo wake. Mungu alikuwa amesema “Na iwe nuru”, lakini mfalme alikuwa amedumisha giza. Akiwa amedhoofishwa na mapambano ya muda mrefu, mwisho alijiuzulu kiti chake cha enzi, akajikalia kama mtawa.

Katika Uswisi, wakati wengi walipoipokea imani ya Watengenezaji, wengine waling’anga’ania imani ya Rumi. Mateso yaliyokuwepo yalisababisha vita ya wenyewe kwa wenyewe. Zwingli na wengine wengi ambao walijiunga na watengenezaji waliangukia katika vita na kumwaga damu vilivyokuwa vikipiganwa huko Cappel. Rumi ilikuwa ikishinda, na mahali pengi ilionekana kwamba inarudisha mali yake iliyotekwa. Lakini Mungu hakuwa ameachilia mbali kazi yake na watu wake. Katika nchi nyingine Mungu aliamua watendakazi wengine ili waendeleze kazi ya matengenezo.

Katika ufaransa aliyepata nuru mara ya kwanza alikuwa Lefevre, aliyekuwa mwalimu mtaalamu katika chuo kikuu cha Paris. Katika uchaguzi wake wenye maandiko ya zamani, aligundua Biblia, na akaanza kuwafundisha wanafunzi. Alijishughulisha na historia ya watakatifu na wafia dini kama ilivyonakiliwa na kanisa. Naye alikuwa ameendelea sana, katika uchunguzi huo, ndipo wazo lilipomjia la kutafuta msaada wa Biblia juu ya habari hiyo. Basi akaanza kuisoma na kuichunguza. Kwa kweli alikuta watakatifu

wanatajwa katika Biblia, lakini hawatajwi kwa namna wanavyotajwa katika taratibu za kanisa la Roma Catholic. Basi akachukia na kuachilia mbali uchunguzi huo, akijishughulisha na mafunzo ya Biblia, yaani Neno la Mungu.

Katika mwaka wa 1512, kabla Luther au Zwingli hawajaanza kazi ya matengenezo, Lefevre aliandika na kusema “Mungu ndiye alitupatia haki kwa njia ya imani, ambayo inatupeleka katika uzima wa milele, kwa neema tu”. Wakati alipokuwa akifundisha kwamba utukufu wa wokovu ni wa Mungu peke yake, akasema kuwa wajibu wa utii ni wa binadamu. [98]

Baadhi ya wanafunzi wa lefevre walimsikiliza kwa makini sana, hata wakatamani kuwa watangazaji wa maneno hayo ya Mungu, wakati mwalimu wao atakapofariki. Mmojawapo wa watu hao alikuwa William Farel. Wazazi wake walikuwa waumini mashuhuri katika kanisa la Roman. Naye alichukizwa sana na watu waliokuwa wakipinga mafundisho ya kanisa la Rumi. Alikuwa na nia ya kuwaangamiza watu kama hao alisema, “Ninaposikia mtu akisema maneno kinyume cha papa, ninamsagia maneno kama mbwa mwitu mwenye ghadhabu”. Lakini taratibu za ibada, kutukuza watakatifu kuabudu madhabahuni na kutoa matokeo ya kila namna haviwezi kuleta amani moyoni. Kutubu na kutoa kitubio cha dhambi na kadhalika haviwezi lolote. Maneno ya Lefevre yalikuwa, “Wokovu ni wa neema Msalaba wa Kristo pekee yake ndio hufungua mlango wa mbingu, na kufunga mlango wa kuzimu”.

Farel akiwa ameongoka kama Paulo aligeuka kabisa kutoka katika kifungo cha mapokeo na kuingia katika uhuru wa wana wa Mungu. Alisema, “Badala ya kuwa na roho ya ghadhabu kama ya mbwa wa mwitu, aligeuka akawa mpole kama mwana kondoo, akiwa ameachana kabisa na papa na kumgeukia Kristo”

Wakati lefevre alipokuwa akiitawanya nuru ya Injili kwa wanafunzi, Farel aliitawanya kwa watu wote hadharani. Mkuu wa kanisa, askofu wa Meaux alijiunga pamoja nao. Walimu wengine pia waka-jiunga nao katika kutangaza Injili, na kuongoa watu wa aina mbalimbali, tangu mafundi, wakulima hata watu wa Ikulu, katika jumba la mfalme. Dada wa mfalme Francis I aliipokea imani ya waten-genezaji. Watengenezaji walitazamia kwa matumaini makubwa wakati ambapo ufaransa ingeongolewa kwa Injili.

Agano Jipya La Kifaransa

Lakini matumaini ya Watengenezaji hayakutimia. Mateso na majaribu yaliwangojea wanafunzi wa Kristo. Walakini ni wakati wa amani ulipita kati; ili wajiandae kukutana na tufani kali. Wakati huo watengenezaji waliendelea sana. Lefevre alijishuhgulisha na kazi ya kutafsiri Agano Jipya kwa lugha ya Kifaransa. Wakati ule Biblia ya Kijerumani iliyotafsiriwa na Luther ilipotoka mitamboni huko Wittenberg. Agano Jipya ya kifaransa pia ilichapishwa huko Mequx. Basi wakulima wa Mequx wakapata kisomo Neno la Mungu. Basi wafanyakazi, mafundi, wakulima waliburudika sana na kuchangamka wakati walipokuwa wakingojea na kutafakari mafungu ya Biblia. Wao hao, ingawa hawakuwa wenye elimu ya juu, wakiwa wakulima tu, nguvu ya neema ya Mungu ilionekana katika maisha yao.

Nuru iliyowashwa huko Meaux ilipeleka mwanga wake mbali. Hesabu ya waumini ilizidi kila siku. Kwa muda ghadhabu ya serikali ya kanisa la Rumi ilizuiliwa isiwaingilie watengenezaji, lakini baadaye viongozi wa papa walifaulu. Uchomaji moto wa wale wanaopinga Rumi ulianza. Wengi walichomwa moto hadharani kwa ajili ya imani yao.

Katika majumba ya mabwana, na majumba ya wafalme, kulikuwamo watu waongofu ambao walithamini ukweli wa Biblia zaidi ya vyeo, mali, hata maisha yao. Lois de Bequin alikuwa mtu wa uzao wa kikubwa, yaani wazazi wake walikuwa maarufu. Yeye alijishuhgulisha na kujifunza Biblia akaongoka, ingawa kwanza alikuwa amewachukia Waluther, Baadaye aliposoma Biblia akaona kuwa mafundisho yaliyomo siyo ya Rumi, bali ya Luther. Basi akawa mfuasi. Warumi wa Ufaransa walimtupa kifungoni kama mtu mzushi, lakini alifunguliwa na mfalme. Kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa Francis alisitasita kati ya Rumi na matengenezo.

Berquin naye alifungwa na wafuasi wa papa mara tatu, lakini alifunguliwa na mfalme aliyekataa kumtia hatiani kama mzushi. Bequin alionywa mara kwa mara kuhusu hatari iliyomkabili katika ufaransa, na akashauriwa atoke nchini akae mahali pengine penye usalama.

Berquin Shujaa

Juhudi ya Bequin ilizidi kuwa kubwa. Alikusudia kutenda makuu kijasiri. Yeye hakuitetea kweli peke yake, bali alishambulia makosa bila kujali. Wapinzani wake walikuwa watawa wasomi hasa waliosomea Biblia katika chuo kikuu cha Paris, ambacho ni chuo maarufu nchini. Katika maandiko ya watu hawa Berquin alipata makosa kumi na mawili ambayo alidai kuwa ni kinyume cha Biblia. Watu hawa walikuwa wataalamu. Alimwomba mfalme aamue katika mashindano hayo.

Akifurahia nafasi hii ya kushusha kiburi cha watawa hawa, mfalme aliwaagiza Warumi wajitetea na kutetea msimamo wao kwa kutumia Biblia. Silaha hii itawasaidia kidogo tu. Mateso na kuchoma moto, ndizo silaha zao wazijuazo bora zaidi. Sasa wakaona kuwa wamo mtegoni kunaswa katika shimo walilotaka kumtupa Berquin na sasa wakatazamana na kutafuta njia ya kukwepa.

[100]

Wakati huo huo sanamu ya bikira Maria iliyokuwa imesimamishwa kwenye kona ya barabara, ilikuwa imevunjwa. Watu wengi walijazana mahali hapo penye sanamu wakiomboleza na wenye uchungu. Hata mfalme alisikitika. Watawa walipaza sauti zao wakisema “Haya ni matokeo ya mafundisho ya Bequin Vitu vyote vitaondolewa sasa, yaani dini, sheria na serikali yenyewe na hawa Waluther waasi”.

Mfalme akaondoka toka Paris, na watawa wakaachwa peke yao ili wafanye wapendavyo. Basi Berquin akashitakiwa na kuhukumiwa kufa. Na isiwe mfalme Francis kuingilia kati na kumwokoia, hukumu ingetekelezwa siku ile ile. Wakati wa aduhuri watu wengi walikusanyika ili kushuhudia tukio hili. Wakashangaa kuona kuwa mtu aliyehukumiwa ni mtu mashuhuri katika nchi ya ufaransa. Mshangao na uchungu na wasiwi vilijaa nyusoni mwa makutano. Lakini uso wa mtu mmoja tu ulikuwa na utulivu. Huyu aliyehukumiwa kufa, yaani Berquin, ndiye alijua kuwa Bwana wake yuko karibu hapo.

Uso wa Berquin uling'aa kwa nuru ya mbinguni. Alivaa vazi la mahameli, la hariri na soksi za dhahabu, Alikuwa karibu kumshuhudia mfalme wa wafalme. Hakuwa na alama ya huzuni katika uso wake. Alijaa furaha.

Wakati mkutano ulipoanza safari barabarani kwa taratibu, watu wakashangaa kumwona akiwa mwenye furaha. Watu wakasema, “Alifanana na mtu anayekaa hekaluni akitafakari mambo matakatifu”.

Berquin Achomwa Moto

Berquin alipokuwa amefungwa kwenye mti wa kuchomewa, alijitahidi kuwazungumzia watu maneno, lakini watawa wakaanza kupiga kelele, na askari kupigapiga makofi, basi ghasia hizo zikaziba sauti ya mfiadini. Hivyo katika mwaka wa 1529 kasisi mkuu wa Paris aliwawekea watu wa 1793 msingi wa kuigwa, kwa maneno matakatifu ya mtu anayekufa. Berquin alinyongwa, na mwili wake ukateketea ndani ya ndimi za moto.

[101] Walimu wa matengenezo ya imani waliondoka huko wakaenda mahali pengine. Lefevre yeye alikwenda Ujerumani. Farel alirudi kwao upande wa mashariki huko Ufaransa; ili kuhubiri kwa watu wa kwao. Mahubiri yake yalipata wafuasi. Baada ya muda alifukuzwa mahali hapo. Alipitia vijijini akifundisha Biblia katika nyumba za watu kwa siri; akijifichaficha misituni na milimani ndani ya mapango yaliyokuwa mazoea yake wakati wa utoto wake.

Kama ilivyokuwa wakati wa mitume, mateso yalishindwa kuzuia injili isiendelee mbele. Wafilipi 1:21; ndivyo ilivyokuwa kwa watenenezaji. Walipofukuzwa kutoka Paris na Meaux, waliotawanyika wakaenda “huko na huko wakalihubiri Neno” Matendo 8:4. Hivyo nuru ya Injili ikafika mahali pa mbali katika nchi ya ufaransa.

Mwito wa Calvin

Katika mojawapo ya shule za Paris, kulikuwamo kijana mmoja, mwangavu, mtu asiye na lawama yoyote, mwenye akili, mcha Mungu. Hali yake bora alifanya chuo chake kijivune kwa ajili yake. Na ilitumainiwa kwamba kijana huyu ambaye anaitwa John Calvin atakuwa mtetea ukweli kanisani.

Lakini nuru ya Mungu ilipenya kuta za chuo ikamfikia Calvin na kuupenya ushirika uliomzunguka. Olivetan binamu wa Calvin alikuwa amejiunga na watenenezaji. Wawili hao waliongelea mambo yaliyokuwa yakitatiza ukristo. Oliven alisema, “Kuna dini

mbili duniani Protestant: Moja ambayo imebuniwa na watu, ambayo ni hujiokoa mwenyewe kwa njia ya maadhimisho yake na matendo yake mema. Dini nyingine ni ile inyofunuliwa katika Biblia, ambayo humwelekeza mtu apate wokovu kwa njia ya neema ya Mungu itolewayo bure”

Calvin akasema “Sitataka mafundisho yako mapya unadhani kuwa nimeishi makosani kwa miaka hii yote?” Lakini Calvin alipokuwa peke yake katika chumba chake aliyatafakari maneno ya binamu yake. Alijikuta hana mtetezi mbele ya hakimumu wa haki; yaani Mungu mkuu. Matendo mema, maadhimisho ya kanisa, yote yalikuwa bure kuweza kusamehe dhambi. Maungamo ya kitubio haviwezi kumpatanisha mtu na Mungu.

Mashahidi Katika Kuchomwa Moto

Kwa bahati, siku moja Calvin alibahatika kushuhudia tendo la kuchoma mtu aliyedhaniwa kuwa ni mzushi hadharani. Katika tukio hilo la mateso ya kikatili akibisha kwa ajili ya hukumu iliotolewa na kanisa, kijana huyu aliona mfia dini akionyesha imani na ujasiri kabisa, na alipojipambanisha na yeye mwenyewe alijiona kuwa hafai. Akashangaa kuona kuwa mafundisho ya Biblia ndiyo “uzushi” na imani ya mzushi imejengwa katika Biblia. Kwa hiyo yeye aliazimu kujifunza Biblia na kuichunguza kwa makini.

[102]

Katika Biblia alimkundua Kristo. Akapaza sauti na kusema “O Baba, dhabihu yake imetuliza ghadhabu yako, damu yake imeniosha uchafu wangu, msalaba wake umenitetea; kifo chake kimenipatanisha na Mungu. Umenigusa moyo wangu ili niyachukie mambo yote, isipokuwa yale ya Yesu tu”

Sasa akakusudia kujitolea kwa Injili katika maisha yake yote. Lakini aliogopa na akajishughulisha kujifunza. Ila kwa ajili ya maoni na mashauri ya rafiki zake, mwisho akakubali kuwa mwalimu. Maneno yake yalifanana kana kwamba ni umande unavyoanguka majanini, na kuiburudisha nchi. Sasa alikuwa katika mji mkuu wa mkoa, akiwa chini ya ulinzi wa Margaret, binti wa mfalme, ambaye kwa kupenda injili, aliwalinda wapenda injili wenzake. Kazi ya Calvin ilianza katika nyumba za watu. Waliosikia Ijili, nao walipitisha kwa wenzao, na vivi hivi. Aliendelea kuweka msingi wa kanisa ulio imara, ambalo litatoa ushuhuda bila woga.

Ilipasa Paris ipate nafasi nyingine ya kuhubiriwa Injili. Mahubiri ya Lefevre yalikataliwa, walakini ilipasa Injili ihubiriwe kwa watu wote wakaao humo. Mfalme alikuwa hajawaunga mkono Warumi na kuwapinga watengenezaji. Margret alikubali kuwa imani iliyosahishwa lazima ihubiriwe katika mji wa Paris. Akaamuru kuwa mchungaji wa Kiprotestant lazima ahubiri makanisani. Jambo hili lilipigwa marufuku na waongozi wa Papa. Margret akaruhusu Injili ihubiriwe hata katika jumba la ufalme. Iliamriwa kuwa kila siku mahubiri yatolewe mara moja. Watu maelfu walikuwa wakihudhuria kwenye mahubiri hayo. Mfalme akaamuru kuwa makanisa mawili ya Paris yafunguliwe. Mji wa Paris ulikuwa haujahubiriwa Neno la Mungu kama wakati huu. Hali ya kiasi, usafi na utulivu pamoja na shughuli vilichukua mahali pa ulevi, ufisadi, ugomvi na uvivu. Watu wengine walipoiamini Injili, wengine walikataa. Baadae watu wa papa walifaulu kupata madaraka kwa hiyo wakaamuru makanisa yafungwe, na kuanza tena kuchoma watu moto waliowapinga.

[103] Wakati huo Calvin alikuwa angali Paris. Mwishowe wenye madaraka wakakusudia kumwingiza katika ndimi za moto. Calvin hakuwa na wazo lolote kuhusu hatari, wakati rafiki zake walipomwendea chumbani mwake, na kumwambia kuwa wakuu wako njiani wanakuja kumkamata. Basi muda si muda pakasikika hodi kwenye mlango wa nje. Basi rafiki zake hawakupoteza wakati. Walikwenda kuwachelewesha wakuu pale mlangoni wakati wengine walimshusha Calvin dirishani, akakimbilia katika nyumba ya mtu mmoja aliyekuwa rafiki yake. Huko akajigeuza na kuvaa mavazi mengine, akatia jembe begani akaaza safari. Alisafiri kwenda kusini ya ufaransa, mwisho alijikuta amefika katika utawala wa Margret, Huko akapata hifadhi.

Calvin hakuzidi kujikalia bila kazi. Mara ile hatari iliyomkabili ilipotulia alitafuta mahali pengine pa kufanyia kazi huko Poitiers, ambapo paliyakaribisha mawazo mapya. Hapo watu walisikiliza Injili kwa moyo. Wafuasi walipoongezeka ilionekana kuwa ni bora watoke mjini wawe nje ya mji. Pango moja zuri lilichaguliwa liwe mahali pa mkutano. Mahali hapo pa siri neno la Mungu lilisomwa na kutafakariwa. Mahali ambapo hapo waliadhimisha siku kuu ya meza ya Bwana kwa waprotestant wa Ufaransa. Kutoka katika kanisa dogo hili watu kadhaa wa kadhaa waaminifu walitumwa huko na huko kuitangaza Injili.

Mara nyingine tena Calvin alirudi Paris, lakini alikuwa karibu kila aina ya kazi ya matengenezo imefungwa. Mwisho akakata shauri kwenda kuishi Ujerumani. Wakati tufani ya mateso ilipolipuka ufaransa, Calvin alitoka huko kwa shida sana. Waprotestant wa ufaransa, yaani watengenezaji walikusudia kuanzisha sham-bulio maalumu juu ya Rumi ambalo lingetaharikisha nchi nzima. Matangazo ya kushambulia ubatili wa misa yaliwekwa usiku moja mahali pote nchini. Bidii hii ambayo ilikuwa dhaifu iliwapa Warumi sababu ya kutaka wazushi hawa waangamizwe, kwamba wanahatarisha serikali, na kuvuruga amani nchini.

Mojawapo ya tangazo hili lilibandikwa kwenye mlango wa mfalme ujasiri huu wa ovyo uliothubutu hata kufika katika nyumba ya mfalme ulichochea ghadhabu. Ghadhabu yake ilikuwa katika usemi huu: “Washikwe wote bila kujali wanaoshukiwa. Bora wawe Waluther. Nitawango’a wote” Mfalme aliunga mkono Warumi.

Utawala wa Hofu Kuu

Mfuasi mmoja wa imani ya matengenezo aliyezoea kuita waumini, wakutane mahali pa siri ili waabudu na kujifunza neno la Mungu, alikamatwa. Mtu huyu alikabiliwa na kifo cha kuchomwa moto, na matisho yake, aliamuriwa aingie kila nyumba ya mfuasi wa Kiprotestant katika mji huo ajitambulishie kama mfuasi wa papa. Hofu ya kuchomwa moto ilimtisha, naye akakubali kuwasaliti wenzake, yaani akafanya jinsi alivyoamuriwa kufanya. Morin, mpelelezi wa serikali pamoja na msaliti huyu alipita pole pole barabarani mjini. Walipofikia nyumba ya mfuasi wa Luther, yaani mluther, yule msaliti alionyesha dalili bila kutamka neno. Basi msafara ukasimama, ukaivamia nyumba hiyo ya mkristo mluther, watu waliokuwaamo wakakamatwa na kufungwa, halafu wakaendelea kutafuta wakristo wengine. “Morin aliutetemeshwa mji, ulikuwa utawala wa hofu kuu”

[104]

Wale waliokamatwa waliuawa kikatili mno. Walipochomwa moto, iliamriwa kwamba moto upunguzwe makali yake ili wazidi kuungua kwa muda mrefu bila kuteketea. Lakini hata hivyo walikufa kishujaa bila kuonyesha hali ya kubabaika wakiwa washindi wa kweli. Watesi wao waliaibika, wakafedheheka. Watu wote wa Paris wakatambua aina ya wakristo wanaofuata imani ya matengenezo. Hapakuwako na madhabahu ya kuhubiri Injili sawa na iliyong’aza

nyuso za watu hao waliopitia katika matatizo makuu mpaka kufa ilitangaza uwezo wa Injili.

Waprotestanti walishitakiwa kuwa wanafanya njama ya kuwaangamiza Wakatoliki, na kuipindua serikali na kumwua mfalme. Lakini hakuna ushahidi hata kidogo uliopatikana kuhusu mambo hayo. Hata hivyo walitendewa yasiyosemeka. Lakini baada ya kupita karne moja, mambo hayo waliyowasingizia Waprotestant yaliwapata, yaani mauaji ya kupindua serikali na mfalme wao. Hayo yaliletwa na Uprotestant ndiyo ilileta maafa haya ya kutisha katika nchi ya ufaransa. Tuhuma, mashaka, hofu na wasiwasi vilikumba watu wote, wala hapakuwako na utulivu. Watu maelfu walikimbia kutoka Paris, wakawa wakimbizi katika nchi nyingine. Hali hii ikawafanya watu wapende imani ya matengenezo zaidi. Wafuasi wa papa walishangaa kuona watu hawa wazushi hawaonewi mashaka, ila watu wanaridhika kuwa nao.

Uchapaji Watangazwa Kuondolewa

[105] Francis I alikuwa anapendelea kujikusanyia watu wa kila hali, kutoka nchi zote. Kwa kuwa alikuwa na hamu ya kuwafutilia mbali wazushi wote, basi kundi hili la wataalamu likatoa sheria ya kupiga marufuku uchapaji wote katika nchi ya Ufaransa. Francis alitoa mfamo mmoja kati ya mingi iliyochapwa na kuhifadhiwa, akasema, kuwa utamaduni wa kisomi haufai kupingia dini na kuafikiana na mateso. Mapadri walidai kwamba matusi yaliyotolea kutukana mbingu kwa njia ya kudharau misa, lazima yalipwe kwa damu. Januari 21, 1535 ndiyo siku iliyochaguliwa kwa ajili ya adhimisho rasmi. Kila nyumba penye mlango paliwashwa kimuli kwa ajili ya kuheshimu ushirika mtakatifu (sacrament ya Kikatoliki). Kabla ya kupambazuka msafara ulianzishwa kwenye jumba la mfalme.

“Msafara uliongozwa na askoru wa Paris katika fahari kubwa, huku akiungwa mkono wa wana wanne wa kifalme hakuvaa taji, wala mavazi ya kifalme” katika kuenenda, alijiinamisha kwa kila madhabahu, si kwa ajili ya makosa yaliyomtia unajisi, wala si kwa ya damu isiyo na hatia aliyomwaga, ila kwa ajili ya dhambi ya kifo ya watu wake ambao wamethubutu kuidharau huduma ya misa.

Katika ukumbi wa jumba la askofu, mfalme alionekana katika maneno ya masikitiko, akiombolezea maovu yaliyoliangukia taifa.

Aliitangaza siku hiyo kuwa ni siku ya kazi ya kuwang'olea mbali “wazushi” hawa wenye madhara, ambao wanatishia nchi yetu ya ufaransa. Alipokuwa akisema hayo machozi yalikuwa yakimtoka, na mkutano wote ukalia huku wakisema, “Tutaishi na kufa tukishikila dini ya Kikatoliki” Neema iletayo wokovu imeonekana na kuimulikia Ufaransa, lakini imesukumwa mbali, wakichagua giza zaidi ya nuru. Wameyaita maovu kuwa ndiyo mema, na mema wakayaita kuwa maovu, mpaka wakazama kabisa katika udanganyifu mkuu. Nuru ambayo ingewaongoza kutoka katika udanganyifu na kifungo cha giza. Wameitupilia mbali.

Mara nyingine tena msafara wa maandamano ulianzishwa. Mbali kidogo majukwaa ya kuchomewa wakristo wa Kiprotestanti yalijengwa, na ikapangwa kuwa kuni za kuchochea watu hao ziwashwe wakati mfalme atakapoonekana, na ya kwamba maandamano yatasimama kushuhudia mambo hayo. Mambo yalipotokea, wale waliochomwa hawakuonyesha alama yoyote ya kusitasita wala kufadhaika. Walipoambiwa wakane imani yao mmoja alisema, “Mimi ninaamini kile manabii na mitume walichoamini na kuhubiri na wakristo wote wanachoamini. Imani yangu imejengwa kwa Mungu atakayeshinda nguvu za kuzimu”

Waliporudi na kufika jumba la mfalme, watu walitawanyika na mfalme na maaskofu wakaenda zao huku wakijitia moyo kwamba, wataendelea na kazi hiyo ya kuwaangamiza “wazushi”

[106]

Amani ya Injili ambayo ufaransa imeikataa itaendelea kwa hakika, lakini matokeo ya Ufaransa yatakuwa ya hatari. Katika Januari 21, 1793 maandamano mengine yalipita katika barabara za Paris. Safari hii tena mfalme ndiye alikuwa mwanzilishi wa maandamano. Tena kulikuwa na makelele na ghasia wakitafuta wazushi wapya. Tena siku hiyo ilishia kwa kuchoma watu wengine. Mfalme Louis XVI alipokamatwa alijaribu kushindana sana na walimkamata, mwisho akakatwa kichwa na kuchomwa. Mahali hapo pa kuchomea watu, karibu watu 2,800 walipoteza maisha yao.

Matengenezo yameifunua Biblia katika ulimwengu. Upendo mkuu wa Mungu ulizidhihirisha wazi kanuni za mbinguni. Ufaransa ilipokataa kipawa cha mbinguni, ikajiwekea akiba ya uharibifu. Mwenendo wa njia yao na makusudi yao ilitokeza uasi na mapinduzi yaliyoleta utawala wa hofu kuu.

Shujaa Farel alifukuzwa nchini kwao akaenda Uswisi. Hata hivyo mvuto wake haukuzimwa ufaransa. Akisaidiana na wengine waliofukuzwa kama yeye, walitafsiri maandiko ya Kijerumani katika lugha ya Kifaransa; walitafsiri pia Biblia katika Kifaransa, na vyote vikachapishwa. Kwa kuwa vilichapishwa kwa wingi, Wainjilisti wa vitabu walikuwa wakiviuza huko ufaransa.

Farel aliifanya kazi yake huko Uswisi akiwa kama mwalimu, huku akieneza mafundisho ya Biblia kwa hadhari kubwa. Watu wengine waliamini, lakini mapadri waliinuka na kukomesha kazi hiyo, na washirikina waliipinga kazi Mapadri walisema “Kazi hiyo haiwezi kuwa ya Mungu maana kuhubiri kwake hakuleti amani ila vita”.

Farel alisafiri kijiji kwa kijiji, huku akivumili njaa baridi, uchovu na hatari ya maisha yake. Alihubiri sokoni makanisani, na mara nyingine katika mahekalu ya Wakatoliki. Mara moja alikamatwa na kupigwa karibu kufa, lakini aliendela mbele. Alikwenda mji hata mji, mahali ambapo ni ngome ya Ukatoliki, akigongagonga milango yao kwa Injili.

[107] Farel alitamani kuimarisha Uprotestant huko Geneva. Kama akifaulu kupanda Uprotestanti katika mji huu, ndipo patakuwa kituo kikubwa cha kuendeshea kazi katika Ufaransa, Uswisi na Italia. Miji mingi na vijiji vilivyozunguka vilipokea Injili.

Aliingia Geneva akiwa na mwenzake mmoja tu. Huko aliruhusiwa kuhubiri mahubiri mawili peke yake. Mapadri walimwita katika baraza, ambako walikuja na silaha wameficha nguoni, ili wapate kumwulia mbali. Watu wengi walikusanyika kuhakikisha kuwa hawezi kutoroka. Hata hivyo mahakimu na askari walimwoko. Kesho yake asubuhi mapema alisindikizwa akavuke ziwa kwenda mahali pa usalama. Huo ndio ulikuwa mwisho wa mahubiri yake ya kwanza huko Geneva.

Jaribio la pili walichagua kijana mnyonge aliyetendewa vema na watengenezaji. Lakini yeye atafanya nini mahali ambapo Farel alikataliwa? “Mungu amechagua mambo mapumbavu ya dunia, awaabishe wenye hekima” Kor. 1:27

Forement, Mwalimu

Forement alianza kazi kama mwalimu. Ukweli ule aliofundisha watoto katika skuli, watoto waliukiri walipofika nyumbani kwao. Hivyo wazazi nao wakaupata ukweli wa Biblia. Agano jipya pamoja na vijizuu viligawiwa bure kwa watu. Baada ya kupita muda Forement pia akafukuzwa nchini. Ingawa aliondoka lakini ukweli alioupanda mioyoni mwa watu uliota. Imani ya matengenezo umepandwa nchini. Wahubiri walirudi na ibada ya kiprotestant ikaanzishwa Geneva.

Wakati Calvin alipoingia Geneva mji ulikuwa umetangazwa kwamba unafuata imani ya matengenezo. Alikuwa akienda Basel wakati alipolazimika kuzungukia Geneva.

Katika matembezi haya Farel alitambua uongozi wa Mungu. Ijapokuwa Geneva ulikuwa umeipokea imani ya matengenezo hata hivyo nguvu ya uongofu kamili lazima itokane na Roho Mtakatifu; wala siyo agizo la Baraza. Ijapokuwa Geneva imekataa mambo ya Rumi, ilikuwa bado inaambatana na makosa yaliyotapakazwa na Rumi.

Farel alimsihi mwinjilist Calvin akae hapo na kufanya kazi hapo. Lakini Calvin aliondoka kwa ajili ya hadhari. Aliogopa kukabiliana na watu wa Geneva waliokuwa wagumu na wakaidi. Alitafuta mahali patulivu ili apate kujifunza. Hapo akaandika mafundisho na kuyachapisha. Na kwa njia hiyo akasaidia kujenga makanisa. Hakuweza kukataa. Ilionekana kwake kana kwamba mkono wa Mungu umemwangalia mahali ambapo ataishi bila kubadilika.

[108]

Ngurumo za Laana

Ngurumo za papa zilielekezwa huko Geneva. Sasa mji huu mdogo utawezaje kushindana na uwezo mkuu huu ambao huwa-tetemeshwa wafalme na wafalme wakuu?

Ushindi wa watengenezaji umekwisha kupita, na Rumi ikakusanya nguvu mpya ili ikamilishe kazi ya kuangamiza hawa waten-genezaji. Kanuni ya hawa Warumi wa Jesuits walikuwa wakatili na wenye uwezo mkuu wa kutisha. Waliangamiza kabisa bila kujali lolote, ila tu kutimiza agizo lao.

Injili ya Kristo imesababisha na kuwezesha watu kuvumilia mateso, baridi, njaa, kazi ngumu na umaskini. Walishikilia ukweli wa Injili bila kuogopa aibu, vifungo, na kifo cha kuchomwa moto. Warumi wa Jesuit walileta mtindo mpya. Kusudi lao lilikuwa kuung'oa Uprotestant, na kuusimamisha utawala wa upapa.

Walivaa mavazi ya utawala na kutembelea magereza na hosipitali, wakiwahudumia wagonjwa na maskini wakijifananisha na Yesu aliyekwenda huko na huko akitenda kazi njema. Lakini katika kifuniko hiki cha utawa, ulifichika uovu na makusudi ya uasi.

Kanuni ya mambo yao ilikuwa kuhalalisha mambo yao huko wakiongopa, wakiiba, wakiua, kana kwamba mambo hayo ni halali kufanyika wakiwa wanalihudumia kanisa. Katika hali hiyo yao ya hila walipata nafasi ya kufikia hata vyeo vya serikali vilivyo vikuu. Walikuwa kama watumishi waaminifu sana huku wakiwa majasusi. Walifungua skuli na vyyo vikuu vya kufundishia wana wa kifalme, na watu wote. Waprotestanti walivutwa kijanja hata wakaingizwa na kufuata kanuni za kipapa. Kwa kuwa watoto walizoezwa kufuata kanuni za Kirumi, hivyo wakausaliti uhuru ambao baba zao waliupigania na kumwaga damu. Popote hawa Jesuits walipokwenda walizidi kuimarisha ukatoliki.

[109]

Ili kuwatia nguvu papa alitoa tangazo la kuanzisha kikosi cha ujasusi. Watu wengi sana sana wenye ujuzi na utaalumu waliuawa na kukimbia nchi nyingine.

Ushindi wa Matengenezo

Hivyo ndivyo njia ambayo Rumi ilivumbua ili kuzimisha nuru ya matengenezo na kazi ya kuwashikilia watu katika ushirikina zama zile za giza. Lakini chini ya baraka za Mungu kazi za watu watawa wa Mungu aliowainua baada ya Luther, Uprotestant haukuzimika na kuangamizwa. Hakupata uwezo wake kutokana na wakuu wa dunia. Mataifa dhaifu kabisa ndiyo yaliyouhimili. Geneva mji mdogo, na Uholanzi kinchi kidogo kilichokuwa kikishindana na Hispanina na Swiden nchi maskini ndiko ushindi wa matengenezo ulikoimarika.

Kwa muda wa karibu miaka thelathini Calvin alifanya kazi huko Geneva akieneza matengenezo Ulaya nzima. Kazi yake haikukosa kuwa na kasoro, lakini alikuwa chombo cha kutetea ukweli na maana

kubwa, kukabiliana na uovu wa papa na kueneza usafi wa mafundisho ya Biblia katika makanisa.

Kutokea Geneva vitabu vilivyochapwa vyenye ujumbe wa Mungu pamoja na walimu walitumwa huko na huko kuutangaza ukweli. Kwa hiyo walioteswa katika nchi zote walitazamia kupata mafunzo ya kuwatia moyo. Mji wa Calvin ulikuwa ngome kwa wote waliokuwa wakiwindwa. Katika Ulaya yote ya Magharibi, wote walikaribishwa na kutunzwa. Nao waliufaa mji kwa utaalamu wa aina mbali mbali waliouleta. Watu kama John Knox wa Scotland, ambaye ni mtengenezaji hodari, na Waingereza wengi, na waprotetanti wa Uholanzi na Spain walipata nuru huko Geneva wakaenda nayo huko kwao ili kuwamulikia watu wa kwao.

Marejeo:

Wylie, bk. 13 ch. 1

Ibid. bk. 13, ch. 2

D'Aubigne, bk. 12 ch. 3 Ibid.

D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, bk. 2 ch. 16

Wylie, bk. 13 ch. 9

Ibid. bk. 13 ch. 7

Martyn, Vol. 3 ch. 13

D'Aubigne, bk. 2ch. 30

Ibid. bk. 4 ch. 10

Wylie, bk. 13 ch. 20

Ibid. bk. 13 ch. 21

D'Aubigne, bk. 4 ch. 12

Wylie, bk. 13 ch. 21

D'Aubigne, bk. 4 ch. 12

Wylie, bk. 13 ch. 21

Ibid. bk. 14 ch. 3

D'Aubigne, bk. 9 ch. 17

13/Huko Uholanzi

Katika nchi ya Uholanzi udhalimu wa papa ulipingwa mapema sana. Miaka mia saba kabla Luther hajatokea askofu wa Rumi alishutumiwa wazi bila hofu na makasisi wawili Warumi waliotumwa kama mabalozi huko Rumi, ambao walikuwa wamejifunza ukweli. Walimwambia, “Wewe waketi hekaluni mwa Mungu. Badala ya kuwa mchungaji wewe umekuwa mbwa wa mwitu katika kondoo. Inapokupasa kuwa mtumishi wa watumishi, wewe wajitahidi kuwa bwana wa mabwana, na kulidharau jina la Mungu na amri zake”

Wengine waliinuka toka karne hata karne, wakaendeleza upinzani huo. Katika tafsiri ya Biblia kwa lugha ya Kidachi iliyotafsiriwa na Waldenses, kuna usemi usemao, “Kulikuwa na mafanikio makubwa ndani yake. Hakuna mzaha, hadithi, upuuzi, udanganyifu au jingine kama hayo; ila ukweli tu ndio uliomo” Huo ulikuwa usemi wa marafiki wa imani wa zamani, katika karne ya kumi na mbili.

Sasa mateso ya Warumi yalianza, lakini waumini walizidi kuwa wengi, huku wakitangaza kuwa Biblia ndiyo isiyo na kasoro wala kosa lolote, katika kuingoza dini na kwamba mtu hashututishwi kuamini, ila mtu huaminishwa na mafundisho yake.

Mafundisho ya Luther yalipata watu waaminifu katika Uholanzi, ambao walikwenda kulihubiri neno la Mungu. Menno Simons, mtu msomi hasa, wa dhehebu ya Kirumi, ambaye aliwekewa mikono kuwa padri, hakufahamu cho chote kuhusu Biblia. Naye aliogopa kuisoma kwa hofu asidhaniwe kuwa mzushi. Alipoingia katika maisha ya ufedhuli, akijaribu kuzima sauti ya dhamira yake, haku-faulu. Baada ya muda alianza kusoma Agano Jipya. Masomo hayo pamoja na maandiko ya Luther yalimwongoa akajiunga na imani ya watengenezaji.

Baada ya kushuhudia kwa muda mtu mmoja akiuawa kwa ajili ya kubatizwa mara ya pili. Jambo hili likamfanya asome Biblia kuhusu ubatizo wa watoto wachanga. Akagundua kuwa kutubu na kuamini ndiyo vilivyotakiwa ili mtu abatizwe.

Menno akatoka katika kanisa la Rumi, akajishughulisha na kazi ya kufundisha ukweli alioupata katika Biblia. Katika nchi ya Ujerumani na Uholanzi vikundi vya dini kali vilikuwa vimepatikana. Vikundi hivyo vilikuwa viovu, visivyokuwa na heshima wala adabu, visivyo na utaratibu, vikawa na fitina na maasi. Menno akapigana nao na mafundisho yao mapotofu. Kwa muda wa miaka ishirini na mitano alizungukazunguka katika Uholanzi na Ujerumani ya kaskazini akiendeza mvuto mzuri pamoja na mafundisho yake. Alikuwa mtu mwongofu, mnyenyekevu na mpole na mwenye bidii. Watu wengi waliongoka katika kazi yake. [111]

Katika Ujerumani Charles V alikuwa amepiga marufuku mambo hayo maovu. Katika Uholanzi uwezo wake ulikuwa mkubwa zaidi. Hivyo tangazo la kuanza mateso lilifuata mara kwa mara. Mambo kama vile, kusoma Biblia, kuhubiri habari za Biblia, kumwomba Mungu kwa siri, kutokuinamia sanamu, na kuimba Zaburi vyote hivyo, mtu akionekana anafanya hivyo, adhabu yake ni kifo. Watu maelfu walipoteza maisha yao chini ya utawala wa Charles V. na Philip II

Wakati mwingine jamaa nzima waliletwa kuhojiwa barazani kwamba hawakuhudhuria misa, au kwamba waliabudia nyumbani. Katika tukio moja la namna hiyo kijana mdogo alijibu: “Tulipiga magoti, tukamsihi Mungu atuangazie nuru ya mbinguni na kusamehe dhambi zetu, Tulinwombea mfalme wetu, ili ufalme wake ufanikiwe, na awe na furaha. Tuliwaombea watawala wetu, ili Mungu awalinde” katika tukio hili baba na mwana wake mmoja walihukumiwa kuchomwa moto.

Sio wanaume tu walioonyesha ujasiri wao, ila hata wanawake na wasichana wengi walioonyesha ushujaa mkubwa. Wanawake wengi walisimama kishujaa kando ya waume wao walipokuwa wakichomwa moto, na kuwafariji. Wasichana wengi walikuwa wakikabili moto wamevalia maridadi kama kwamba wanakwenda arusini.

Mateso yaliongeza waumini zaidi katika ukweli. Mwaka kwa mwaka mfalme alijitahidi kuwatendea ukatili wa kila namna, lakini ilikuwa kazi bure. Baadaye William wa Orange aliletauhuru katika Uholanzi wa kuabudu Mungu bila wasiwasi.

Matengenezo Katika Denmark

Katika nchi za kaskazini Injili iliingia huko kwa amani. Wanafunzi waliokuwa wakijifunza katika chuo cha Wittenberg waliporudi kwao huko Scandinavia walipeleka ujumbe wa Injili. Hata maandiko ya Luther pia yalieneza nuru ya Injili. Watu wagumu wa kaskazini waligeuka, wakaacha upotovu wa Rumi na kushika ukweli wa Biblia.

[112] Tausen, Mtengenezaji wa Denmark, alipokuwa kijana mdogo, alijithibitisha kuwa mpenda dini, akaingia na kuishi katika nyumba ya watawa. Mtihani ulikuwa ukimthibitisha kuwa na uwezo na kuitumikia kanisa. Kijana huyu akiwa shuleni alipata nafasi ya kuchagua chuo apendacho; Ujerumani au Uholanzi. Watawa wakamshauri asiende huko Wittenberg au asije akaharibiwa na wazushi.

Tausen akachagua kwenda Cologne, chuo mashuhuri cha Waroma. Mara akachukizwa, kwa maana alisoma maandiko ya Luther, akayapenda sana na kuyathamini. Lakini kufanya hivyo lazima akosane na wakubwa wake, na anyang'anywe msaada wote. Mara akaamua kwenda kusomea Wittenberg.

Aliporudi Denmark hakuweza kufunua siri yake, alijitahidi kuwafundisha watu Neno la kweli na kuwaleta katika nuru ya kweli ya Injili. Aliwafundisha Biblia, na kumhubiri Kristo ambaye ndiye tumaini la mwenye dhambi. Wakuu wake ambao walimtumaini kuwa atakuwa mtetezi wa Warumi, walikasirika sana. Mara moja wakamwondoa katika nyumba yake ya utawa na kumweka kwingine, ambako kulikuwa sawa na kifungo. Mle katika chumba chake aliweza kuzungumza na wenzake walio nje na kuwapa ukweli wote. Wazee hao wa Denmark kama wanalikuwa werevu wa kutosha wanalimkomesha Rausen kabisa, lakini badala yake wakamhamisha tu katika nyumba ya utawa.

Amri ya serikali ilikuwa kwamba watu hawa wanaohubiri imani ya namna mpya walindwe, wasidhuriwe. Makanisa yakafunguliwa kwake, na watu wakakusanyika kumsikiliza. Agano Jipya katika lugha ya Kidachi lilitawanywa kila mahali. Juhudi iliyofanywa ili kuzuia kazi ya matengenezo ilieneza mpaka nchi nzima ya Denmark ikatangaza kuwa imekubali amani ya matengenezo.

Maendeleo Katika Swideni

Katika Sweden pia, vijana waliokuwa wakisomea Wittenberg waliporudi kwao walikwenda na ujumbe ambao ni maji ya uzima, wakawapelekea watu wa kwao. Watangulizi katika matengenezo ya Sweden, ambao ni Olaf na Laurentius Petri, walifundishwa ukweli huo na Luther na Melanchthon. Olaf aliwaamsha watu na ukweli huo wa Injili kama watengenezaji wengine kwa njia ya mahubiri. Lakini Laurentius alikuwa mtulivu sawa na Melanchthon. Wote wawili walikuwa mashujaa. Mara kadhaa Olaf aliponyoka asife kwa bahati. Walakini watengenezaji hawa walikuwa wakilindwa na mfalme, aliyekuwa anapendelea matengenezo, na aliyekuwa anapenda watu hawa wapigane na ufedhuli wa Rumi.

[113]

Olaf alitetea imani ya matengenezo kwa nguvu sana mbele ya mfalme na waku wake. Akadai kwamba mafundisho ya mapadri wa Rumi yangekubaliwa tu kama yanakwenda sawa na Biblia. Kwamba kanuni za imani zote zinaongozwa na Biblia, na ziko wazi za kufahamika na watu wote.

Tofauti hii hutudhihirishia baina ya ukweli na uongo kati ya mahaaba na watengenezaji. Hawa sio wajinga, wenye fujo, wabishi, wao ni watu waliolisoma neno la Mungu, na wanajua jinsi ya kutumia silaha ambazo neno la Mungu linazitengeneza. Wao ni Wasomi kamili na wenye elimu ya Neno la Mungu, wanaoufahamu ukweli kamili, ambao wanafaulu katika ubishi na hila za Rumi.

Mfalme wa Sweden aliikubali imani ya matengenezo na bunge la taifa likapitisha ukubali wake. Ndugu wawili hao wakashika kazi ya kutafsiri Biblia kwa lugha ya Kiswedish kwa utashi wa ufalme. Ikapitishwa na wakuu kwamba wachungaji wako huru kufundisha Biblia katika nchi nzima, na kwamba watoto wanaosoma katika shule zote wafundishwe Biblia.

Taifa hilo baada ya kufunguliwa kutoka katika udhalimu wa Rumi, likastawi na kufanikiwa, ambavyo haijawa hivyo wakati wowote. Baada ya karne moja kupita, taifa hili dhaifu katika Ulaya nzima, likaingia kuisaidia ujerumani katika vita vilivyodumu miaka thelathini. Ulaya ya Kaskazini yote ikaonekana kuwa chini ya mamlaka ya Rumi. Majeshi ya Sweden ambayo hayakuweza kuifanya Ujerumani ishinde, ili ifanye Uprotestanti uendeleo na kufanya uhuru wa dini udumu katika nchi zilizoyapokea matengenezo.

Marejeo:

Gerard Brandt — History of Reformation in and About the Low Countries, bk.1 p. 6

Ibid. p. 14

Martyn, Vol. 2 p. 87

Wylie, bk. 18 ch. 6 Ibid.

Ibid. bk. 10 ch. 4

14/Ukweli Unaendelea Uingereza

[114]

Wakati Luther alipokuwa akiwaeleza watu wa Ujerumani habari za Biblia ambayo ilikuwa imefungwa, Tyndale alikuwa akifanya kazi hiyo hiyo huko Uingereza kwa uongozi wa roho Mtakatifu. Wycliffe alikuwa ameitafsiri Biblia kutoka kwa Kilatini, lakini ilikuwa na makosa mengi. Bei yake ilikuwa kubwa sana, kwa hiyo ilinunuliwa na watu wachache tu.

Katika mwaka wa 1515 Agano Jipya lilikuwa limechapwa, ambalo lilikuwa limetafsiriwa kutoka kwa Kigiriki. Makosa mengi yaliyokuwamo hapo kwanza yalisahihishwa, na ikaeleweka wazi. Watu wengi miongoni mwa wenye elimu walisoma na kuuona ukweli wazi, na kuongeza nguvu kwa kazi ya matengenezo. Lakini watu wa kawaida walikuwa gizani kwa wingi kuhusu Neno la Mungu. Tyndale alipaswa kuitimiza kazi ya kutafsiri Biblia kwa lugha yao, kazi ambayo ilianzishwa na Wycliffe.

Alihubiri imani yake bila hofu. Yale madai ya papa kwamba kanisa ndilo lenye haki ya kuisoma na kuieleza Biblia ni wewe uliyetuficha ukweli huu, na ni wewe uliyewachoma moto wale waliofundisha ukweli wa Biblia, na kama ungeweza ungeichoma hata Biblia pia.

Mahubiri ya Tyndale yaliwachangamsha watu sana. Lakini mapadri walijitahidi kuiharibu kazi yake. Tyndale alisema, “La kufanya ni jambo gani?” Mimi siwezi kufika kila mahali, Oh, kama wakristo wakipata Biblia katika lugha yao wangeweza wenyewe kupinga ufedhuli huu. Pasipokuwa na Biblia haiwezekani kuwadumisha wakristo katika ukweli

Kusudi jipya likazuka mawazoni mwake, “Je, Injili haitazungumza kwa lugha yetu ya Kiingereza kati yetu? Je, nuru ya kanisa iwe ndogo wakati wa adhuhuri kuliko wakati wa mapambazuko? Wakristo lazima wasome Biblia katika lugha yao” Mtu ataafahamu ukweli kwa njia ya Biblia tu Tyndale alipokuwa akihojiana na mkatoliki ambaye ni msomi, alisema, “Tulikuwa heri bila kuwa na sheria ya Mungu kuliko papa. Namdharau Papa na sheria zake zote, na kama

Mungu atanilinda niishi miaka mingi, nitawaelimisha watu, hata kijana mdogo mwenye kuchunga au mkulima atajua Biblia kuliko wewe”.

[115]

Tyndale Atafsiri Agano Jipya Kwa Kiingereza

Akifukuzwa na mateso kutoka nyumbani, Tyndale alikwenda London kufanya kazi huko kwa muda. Baadaye wafuasi wa papa walimlazimisha akimbilie mahali pengine. Nchi nzima ya Uingereza ilionekana kana kwamba haina nafasi kwake. Alikimbilia nchi ya Ujerumani. Huko alianza kuchapisha Agano Jipya katika lugha ya kiingereza. Walipokataa kumchapia katika mji fulani, alikwenda kuchapiwa katika mji mwingine. Mwisho akafika katika mji wa Worms ambapo Luther alitoa ushuhuda mbele ya baraza. Katika mji huo kulikuwako wafuasi wengi wa imani ya matengenezo. Agano Jipya zaidi ya elfu tatu ziliuzwa hapo.

Neno la Mungu liliingia London kwa siri halafu likaenea katika nchi yote. Wafuasi wa papa walijaribu kuiharibu, lakini ilikuwa kazi bure. Askofu wa Durham alinunua Biblia nyingi kwa kusudi la kuzichoma. Akidhani kuwa kwa njia hiyo kazi itakomeshwa. Lakini fedha zilizotolewa kununua Biblia hizo, zilinunua vifaa vya kuchapishia nyingie na bora zaidi.

Wakati Tyndale alipofungwa, baadaye alipaa kufunguliwa kwa sharti kwamba awataje watu wanaomsaidia kifedha kuchapisha vitabu hivyo. Akajibu kuwa askofu wa Durham ndiye ametoa msaada zaidi ya mtu mwingine yeyote, kwa kutoa fedha nyingi kwa kununua vitabu vyote vilivyobakia.

Mwishowe Tyndale akatoa ushuhuda wa imani yake kwa njia ya kifo. Lakini silaha alizoandaa ziliwasaidia askari wengine waendeleo na vita kwa muda wa karne nyingi mpaka wakati wetu huu.

Latimer aliona kuwa kutoka mimbarani Biblia lazima isomwe kwa lugha ya watu wa kila mahali kwa lugha yao. Akasema “Tusijali maoni yetu, eti kwamba yatuongoze, ila neno la Mungu lituongoze” Wala tusiongozwe na mapokeo ya baba zetu, wala mambo waliyofanya, ila tuone mambo ambayo ingepasa wayafanye, lakini hawakufanya.

Watu kama Barnes, Frith, Ridley na Cranmer, ambao walikuwa wasomi watangulizi wa matengenezo huko Uingereza, walikuwa

wasomi kamili, walioheshimiwa katika kanisa la Rumi. Upinzani wao kwa papa ulikuwa matokeo ya kugundua makosa yake.

Usahihi Wa Uwezo Wa Maandiko

Kanuni iliyoshikiliwa na watengenezaji hao, ni ile ile iliyoshikiliwa na Waldenses, Wyclife, Huss, Luther, Zwingli na wenzao wote kwamba Biblia ni sahihi kabisa na uwezo wake ndio wenye kuongoza imani. Mafundisho yake ndicho kipimo cha madai yote. Imani ya watu hao kwa neno la Mungu, ndiyo iliwafanya kushikilia bila kuacha mpaka kifo cha kuchomwa moto. Latimer alisema: “Jipeni moyo, tangu leo tutawasha moto wa neno la Mungu kwa neema yake, katika Uingereza. Ndivyo nitumainivyo” maneno haya aliwaambia wenzake walipokuwa wanachomwa moto. [116]

Baada ya kupita miaka mamia tangu makanisa ya England yajitolee kufuata Roma, lakini makanisa ya Scotland yalidumisha uhuru wao. Walakini katika karne ya kumi na mbili Ukatoliki ukaimarika huko, na nchi ikawa gizani kamili. Lakini nuru ya ukweli ilikuwa ikilipenya giza hilo taratibu. Lolards alikuja kutoka England akiwa na Biblia pamoja na maandiko ya Wycliffe, alifanya mambo mengi kulinda ukweli wa Injili. Katika kuanza matengenezo walitumia pia maandiko ya Luther na Agano Jipya lililotafsiriwa kwa kiingereza na Tyndale. Wajumbe hawa walisafiri wakipanda milima na kutelemka mabondeni kimya kimya wakiwasha nuru ya Injili ambayo ilikuwa karibu kuzimika, na kujaribu kuharibu kazi ambayo kwa muda wa karne nne imefanywa na udhalimu.

Mara ghadhabu ya Wakatoliki ikaamshwa na uchomaji wa waungwana wa Uskoch ukaanzishwa. Vifo vya mashahidi hawa viliamsha nia za watu kwa kuona jinsi walivyoushikilia ukweli mpaka kufa, ili kuupinga ufedhuli wa Rumi.

John Knox

Hamilton, Wishart na wengine wengi sana, watu wanyenyekevu na wenye imani walimalizia maisha yao motoni. Lakini kutokana na kuchomwa moto kwa Wishart alitokea mtu ambaye asingewezekana kunyamazishwa na ndimi za moto, mtu ambaye chini ya uongozi wa Mungu atapiga pigo la mauti kwa udhalimu wa papa katika Uskochi.

John Knox alitupilia mbali mapokeo ya kansia apate kujulisha kwa neno la Mungu. Mafundisho ya Wishart yalimsaidia kukata shauri la kuachana na Rumi, na kuambatana na watengenezaji.

[117] Akisukumwa na rafiki zake ili ahubiri alishinda kwa kuona jinsi hiyo ilivyo nzito. Palikuwa na mashindano makuu ndani yake, na hofu nyingi ikijaribu kubeba madaraka hayo ya kuhubiri, lakini mwishowe alishinda woga, akaanza kuhubiri, wala hakuogopa nyuso za watu. Alipokutana na malkia wa Uskochi, John Knox hakushawishika na lolote, wala hakutishika na chochote. Aliwafundisha watu kuamini dini hiyo ya matengenezo, ingawa ilipigwa marukufu na serikali. Malkia alimwambia kuwa kufundisha watu kushika dini hiyo ni kinyume, tena ni kuasi amri za Mungu. Knox akajibu kishujaa: “Kama watu wote wa uzao wa ibrahimu wangukuwa na dini ya Farao wangukuwa raia wa nani mshemiwa? Tena kungalikuwa na dini gani ulimwenguni? Au kama watu wote wa siku za mitume wangukuwa na dini ya Warumi (serikali) kungalikuwa na dini gani ulimwenguni?”

Malkia Mary Akasema, “Ninyi mnatafsiri maandiko kwa namna moja na Warumi wanatafsiri kwa namna nyingine, sasa nitamwamini nani na mwenye ukweli ni nani?”

Knox akajibu “Utamwamini Mungu, ndivyo neno lake lisemavyo dhahiri. Neno la Mungu ni dhahiri, wala halina siri na ikionekana sehemu isiyoeleweka Roho Mtkatibu ambaye hana kinyume, hueleza mambo yale wazi kabisa mahali pengine katika Maandiko”

Knox akiwa na ujasiri, bila kuhofia hata maisha yake kutoka katika ukafiri wa Rumi Katika Uingereza kusimamishwa kwa dini ya Kiprotestant kama dini ya Taifa kulipungua sana, lakini hakukulizika kabisa. Kawaida za Kirumi za ibada ziliendelea kuwako. Utawala wa papa ulikataliwa kuwa juu ya mambo ya dini, lakini badala yake mfalme akakubaliwa kuwa mtu wa kanisa pia. Mpaka wakati huo kulikuwa na machafuko makubwa kuhusu Injili. Uhuru wa dini haukuwepo: ingawa ukatili wa Kirumi ulikuwa umekoma, haukuendelezwa na Waprotestant, walakini uhuru wa kila mtu kuabudu apendavyo haukuwapo. Wapinzani waliendelea kuteseka kwa miaka mingi.

Maelfu Ya Wachungaji Walifukuzwa

Katika karne ya kumi na saba, Wachungaji maelfu walifukuzwa na watu walikatazwa kuhudhuria mikutano yoyote ya dini, isipokuwa ile iliyoidhinishwa na kanisa peke yake. Wana wa Mungu wa kweli walikimbilia katika msitu, na huko wakakusanyika na kuomba na kumsifu Mungu wao. Kilichosababisha mambo hayo ni mateso. Wengi waliteswa kwa ajili ya imani. Magereza yalijaa tele na jamaa zilitenganishwa. Walakini mateso hayakuwanyamazisha. Wengi walikimbilia ng'ambo ya bahari mpaka Amerika, na huko wakaweka msingi kamili wa utengano wa dini na serikali, na uhuru wa kuabudu kila mtu kama apendavyo.

[118]

Ndani ya gereza lililojaa wafungwa John Bunyan aliandika kisa chake cha ajabu, akijawa na mwamko wa mbinguni aliandika kisa cha safari ya msafiri kutoka katika nchi ya uharibifu kwenda katika mji wa raha. Maendeleo ya msafiri na neema nyingi mwenye dhambi mkuu, au kwa jina lingine "SAFARI YA MSAFIRI"; Kitabu hicho kimesaidia watu wengi wakafuata njia ya uzima.

Wakati wa giza kuu la kiroho Whitefield na Wesleyes walionekana kuwa wachukuzi wa nuru kwa ajili ya Mungu. Kanisa watu walikuwa wamepotoka sana, hata ilikuwa vigumu kuwapambanua na wamizimu. Watu wakuu waliwadhihaki wacha Mungu, na watu wa kawaida wakaachwa maovuni. Kanisa halikuwa na uwezo wa kuwasaidia walioangusha ukweli wa injili.

Kuhesabiwa Haki Kwa Imani

Fundisho kuu la kuhesabiwa haki kwa njia ya imani kama ilivyofundishwa na Luther karibu limepoteza maana yake.

Kanuni ya Warumi ya kwamba wokovu hutokana na matendo mema tu imekuwa badala ya haki kwa imani Whitefield na Wesleyes walikuwa watafuta upendo wa Mungu kwa kweli. Wao walikuwa wamefundishwa kuwa upendo wa Mungu hupatikana kwa njia ya kuwa mwema na kushika kanuni na taratibu zote za dini.

Wakati Charles Wasley alipougua na kuona kuwa kifo kiko karibu, aliulizwa aeleze tumaini lake la kupata uzima wa milele liko wapi. Jibu lake lilikuwa hili: "Nimemtumikia Mungu kwa uwezo wangu wote" Rafiki zake walielekea kutosheka na jibu

hulo. Wesley alidhani kuwa hakuna kizuizi cha kupata fadhila za Mungu. Akasema, “Ni kitu gani kitanizuia kupata uzima?” Hakuna nilichobakiza. Hilo ndilo giza lililokuwa limefunika kanisa, liki-waelekeza watu kutegemea matendo yao mema ili wapate wokovu, badala ya kutegemea damu ya Mwokozi aliyesulubishwa.

Baadaye Wesleye na wenzake walifahamu kuwa sheria ya Mungu inahusu mambo yote, ya ama mawazo, maneno na matendo. Walipingana na utu wa kale ndani yao kwa maombi mengi na mashindano makuu. Waliishi maisha ya kujikana na kujitoa pamoja na unyenyekevu, wakishika kila kitu walichodhani kuwa kitawaletea maisha matakatifu yatakayowaletea fadhili za Mungu. Lakini [119] ilikuwa kazi bure tu, hayo yote hayakuweza kuwapatia maisha ya utulivu wala kuwaondoa katika hukumu ya dhambi.

Moto wa ukweli wa neno la Mungu uliokuwa ukizimika madhabahuni mwa waporotestant, ulipasa uwashwe tena kutoka katika kimuli cha zamani kilichokabidhwa na waumini wa zamani wa Bohemia. Baadhi yao walikimbilia Saxony, na walihifadhi imani yao, Nuru iliyotokea kwa wakristo hao ilimwongoa Wesley.

John na Charles Wesley walitumwa kwenda Amerika kama wahubiri. Katika meli waliyosafiria kulikuwamo kikundi cha Moravian. Dhoruba kali sana ilitokea, na John akakabiliwa na mauti. Akajisikia kuwa hajawa sawa na Mungu. Wajerumani wa Moravian walionekana kuwa na utulivu mkuu wa imani kuu kwa Mungu, hali ambayo kwa John ilikuwa ngeni. Baadaye alisema, “Nimewachunguza watu hawa kwa muda mrefu, nikaona utulivu wao na hali yao na sasa nina nafasi ya kujua kama wao hawana woga, kiburi, hasira wala roho ya kulipiza kisasi. Katikati ya nyimbo wakati ambao huduma inianza, bahari ikachafuka, ikapasua tanga kubwa vipande vipande maji yakafunikiza meli na kumwagika stahani tukawa kama kwamba kilindi cha bahari kimetumeza. Kilio cha hofu kilianza baina ya Waingereza. Lakini Wajerumani waliendelea kuimba kwa utulivu. Baadaye nilimwuliza mmoja wao, ‘Je, ninyi hamkuogopa?’ Akajibu, ‘La namshukuru Mungu’. Nikamwuliza ‘Je, wanawake wenu na watoto wenu hawakuogopa?’ Akajibu kwa upole, ‘Wanawake wetu na watoto wetu hawakuogopa kufa’”

Roho ya Wesley Ilichangamka Kiajabu

Wesley aliporudi Uingereza alikuwa na ufahamu kamili wa Biblia na imani ya kweli, kwa kuwa alifundishwa na watu wa Moravian, katika makutano wa watu wa Moravia, uliokuwa London, palisomwa andiko la Luther. Wesley aliposikiliza, imani iliwaka moyoni mwake. Alisema, “Nilijisikia kuchangamka kwa ajabu, nilijisikia kumtumaini Kristo, Kristo mwenyewe tu ndiye aletaye wokovu. Nikajisikia kuwa na hakika ya kusamehewa dhambi zangu, kwamba nimeokolewa na sheria na adhabu ya kifo”

Sasa akajua kuwa neema ya Mungu aliyokuwa akiitafuta kwa njia ya maombi ya kufunga na kujitesa kwa kila hali, ilikuwa “kipawa cha bure”. Moyo wake ukajaa, naye akawa na hamu ya kutangaza neema ya Mungu ya bure kila mahali. Akasema, “Nikatazama ulimwengu wote kuwa mtaa wangu wa kazi. Kila mahali pakaonekana kuwa pananipasa kupahubiri Injili” [120]

Aliendelea na maisha yake ya kujikana na kujinyima, lakini sasa si kama tegemeo la wokovu, bali kama matokeo ya imani, Wala si kama shina, bali matawi ya utakatifu. Neema ya kristo itadhihirishwa kwa njia ya utii, maisha ya Wesley yalitolewa kuhubiri Injili aliyoipokea, ambayo ni Roho Mtakatifu, uzao matunda maishani yaimarishayo mfano wa Kristo.

Whitefield na Wesley walidharauliwa na kuitwa wafuasi wa “Medhodist” na wanafunzi wenzao, jina ambalo kwa wakati wa sasa ni la heshima. Roho Mtakatifu akawaongoza wahubiri Kristo tu aliyesulubishwa. Watu wengi waliongoka kwa mahubiri hayo. Basi ulikuwa lazima waamini hawa kama kondoo wa Mungu walindwe na mbwa mwitu. Wesley hakuwa na wazo la kuanzisha dhehebu jipya; ila aliwaunga Methodist.

Majaribu na matatizo ya siri yaliwapata wahubiri hawa kutoka kwa kanisa mama. Walakini ukweli huingia popote hata kama milango imefungwa. Hata wakuu waliamshwa wakatoka usingizini na kuwa wahubiri hodari katika mitaa yao.

Siku hizo za Wesleye watu wenye vipawa mbalimbali hawakupatana katika mafundisho. Kukubaliana baina ya whitefield na Wesleye wakati fulani kulileta tisho la kufarakana lakini basi walijifunza upole wa Kristo, na uvumilivu wa kusutana na kufarakana, wakati makosa ya wazi yalikuwa yameanza kila mahali.

Wesley Aponyoka Kifo

[121] Watu mashuhuri walitumika kuwapinga wahubiri hao. Walionyesha hali ya kiuadui sana, na hawakuwapa nafasi ya kuhubiri makanisani. Kwahiyo ukweli wa neno la Mungu ukafungiwa nje. Watu hao waliwalaumu wazazi katika mikutano ya hadhara. Hivyo wakaongeza hali ya giza nene nchini. Kwa hali hiyo maisha ya Wesley yalikuwa hatarini kila mara. Wakati fulani John Wesley aliepuka kifo kwa mwujiza wa Mungu. Alipozingirwa na kundi la watu waovu na ikaonekana kuwa hakuna njia ya kuokoka, Malaika akawa na umbo la binadamu akawafukuza watu hao, na Wesley akapita salama, katika hatari hiyo.

Katika habari za kuokoka kwa Wesley alisema “Ijapokuwa majaribio mengi ya kuninasa yamefanyika, hayakufaulu, ingawa moja lilikaribia kuninasa. Mkorofi mmoja alinipiga mara nyingi akanijia kwa nyuma, akitumia fimbo, ambayo mara kama angenipiga kichwani kazi yake ingakamilika. Kila mara kipigo kilinikosa bila sababu, kwa sababu sikujaribu kukwepa hata kidogo.” Wakristo wa Methodist wa siku hizo walivumili mateso na kufanyiwa mizaha, na kutendewa ukatili. Wakati mwingine tangazo lilitolea kwamba, wale wanaotaka kushambulia wakristo wa Methodist wakakutane mahali fulani na saa fulani. Mateso ya kuendelea yaliwahusu wale wanaowaongoa watu toka katika upotevu, na kuwaleta nuruni.

Upotovu wa kiroho katika Uingereza kabla ya siku za Wesley, ulikuwa matokeo ya mafundisho maovu ya kwamba, eti Kristo aliondoa sheria ya amri kumi, na ya kwamba hakuna haja ya kuzishika. Wachungaji wengine waliwaambia wakristo wao kuwa kuzitii amri hizo ni kupoteza wakati tu, kwa maana wale Mungu aliowachagulia uzima waatadumu watakatifu daima, na wale Mungu aliowapangia kufa, hata wafanyeje wasingefaulu.

Wengine tena walishikilia imani kwamba wateule wasingeweza kufanya dhambi, na ya kwamba waovu ni waovu tu milele, wasingeweza kubadilika wala kutubu, wamevuka mpaka wa rehema. Hata walithubutu kusema kuwa kuvunja sheria ya Mungu siyo dhambi, kama tendo hilo lingetendwa na mteule yeyote.

Mafundisho haya machafu ni sawa na mafundisho yaliyotokea baadaye yasemayo kuwa hakuna sheria yoyote ya Mungu isiyobadilika ambayo ndiyo kipimo cha kuongoza mambo yote; lakini she-

ria yoyote huweza kubadilishwa na watu ili ifuatane na hali yao. Mambo haya yote hutokana na yule aliyeanzisha uasi katika viumbe vya mbinguni visivyo na dambi, na kujaribu kuvunja amri ya Mungu isiyovunjika. [122]

Mafundisho ya mbinguni ni kwamba, sheria ya Mungu ni ya milele, haibadiliki ambayo watu wameikataa na kumkataa Mungu pia. Wesley aliyapinga mafundisho hayo maovu. “Neema ya Mungu iletayo wokovu, imefunuliwa kwa watu wote” Mungu mwokozi wetu “...anataka watu wote waokolewe, na kuufikia ujuzi wa kweli. Maana Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu ana wanadamu. Mwanadamu Yesu Kristo aliyejitoa kuwa fidia ya wote” “Kristo, nuru inayomwangazia kila mtu ajaye ulimwenguni” Tito 2:11; 1Tim. 2:3-6; Yohana1:9 Watu waliukosa wokovu kwa kukataa kupokea kipawa cha uzima.

Katika Kuitetea Sheria Ya Mungu

Wesley akijibu hoja ya kwamba eti Yesu alipokufa aliifuta sheria ya Mungu pamoja na sheria ya Musa, alisema, “Sheria ya Mungu ambayo ni amri kumi, na iliyotukuzwa na manabiii, haikufutwa kamwe. Sheria hii haivunjiki kabisa nayo husimama mbinguni kama shahidi mwaminifu”

Wesley alieleza mwungano wa sheria na Injili. Kwa upande mwingine, sheria hutuelekeza kwa Injili, nayo ni njia ambayo sisi tunapitia kuenda Injili. Na kwa upande mwingine Injili daima hutuweka katika utimilifu wa sheria. Kwa mfano, sheria hututaka tumpende Mungu, tuwapende wenzetu, tuwe wapole, na wanyenyekevu na watakatifu. Nasi hujionakuwa hatuwezi kuwa kama sheria inavyotaka tuwe, lakini tunaona ahadi ya Mungu ya kutuwezesha tuwe na upendo, na kuwa na upole na unyenyekevu na utakatifu. Nasi tunaishikilia Injili ambayo ni habari njema. Haki ya sheria hutimizwa ndani yetu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.

Wesley alisema: “Maadui wakubwa wa Injili ni wale wanao-fundisha kuwa sheria haina haja kushikwa. Kuvunja hata kipande kidogo tu, na kujidai kuwa wana wa Mungu huwa na heshima kama ile ya Yuda aliyokuwa nayo kwa Kristo akijidai kumsalimu. ‘Salam Bwana, na kumbusu’ ‘Ni usaliti’ kuzungumza juu ya damu yake na

kuiondoa taji yake kuangaza kwa sehemu ya sheria yake kwa ujanja kueneza Injili yake ni usaliti.”

[123]

Umoja Wa Sheria Na Injili

Kwa watu wale wanaodai kuwa “Kuhubiri Injili kumeifuta sheria Wesley aliwajibu, maana sheria ndiyo ijulishayo dhambi. Huo ndio uliokuwa usemi wa Wesley. Sheria hudhihirisha dhambi na kuwaamsha watu watoke katika usingizi wa mauti. Ni upuuzi kuwaganga watu walio wazima wana afya kamili. Ni upuuzi pia kuwapa watu Kristo ambaye hawana haja naye”

Wesley alipokuwa akihubiri Injili ya neema ya Mungu alikuwa akiitukuza sheria kwanza kama Bwana wake alivyoitukuza sheria na kuiadhimisha. Isaya 42:21. Matokeo yalikuwa matukufu, aliporuhusiwa kuyatazama. Mwisho wa kazi yake nusu ya karne wafuasi wake wal ikuwa wamefikia nusu milioni. Lakini watu wengi maelfu waliosaidiwa na kuokolewa katika utumwa wa dhambi na kuletwa katika nuru ya Injili na maisha matakatifu, hawatajulikana katika ulimwengu huu mpaka jamaa nzima itakapokusanywa katika ufalme wa Mungu. Maisha ya Wesley yameweka kielelezo halisi cha maisha ya Kikristo.

Je, imani, juhudi, kujikana na dini safi ya mtumishi huyu wa Mungu, haiwezi kuigwa katika makanisa ya leo?

Marejeo:

D’Aubigne, History of Reformation of the Sixteenth Century, bk. 18 ch. 4

Ibid

Ibid

Anderson - Anals fo the English Bible (Rev. Edition 1862) p. 19

Hugh Latimer — First Sermon Preached Before King Edward

VI

Works of Hugh Latimer, Vol; 1 p. xiii

David Laing — The collected Works of John Knox. Vol. 2 p. 281-284.

John Whitehead Life of Rev. Charles Wesley p. 102

Ibid p. 10

Ibid p. 52

Ibid p. 74

John Wesley Works, Vol. 3 p. 297-298

Mc. Clintock and Strong, Cyclopedia, art Antionomias

Wesley, Sermon 25

Wesley, Sermon 35

[124] **15/Utawala Wa Ufaransa Wa Kitisho: Ukweli Wake**

Baadhi ya mataifa yaliyopokea matengenezo haya kama kwamba ni ujumbe wa mbinguni. Lakini katika nchi nyingine nuru ya Biblia ilikuwa karibu kuzimika kabisa. Katika nchi moja kulikuwa na mashindano makubwa baina ya ukweli na huo kwa karne nyingi. Mwishowe ukweli wa mbinguni ulitupiliwa mbali. Mvuto wa Roho wa Mungu uliwaondokea watu wale waliokidharau kipawa cha neema yake. Na ulimwengu wote uliona matunda ya ukaidi wa kuikataa nuru ya Mungu.

Vita ya kuipinga Biblia katika Ufaransa iliishia katika mapinduzi, ambayo ni matokeo ya kuuficha ukweli wa Biblia kwa Rumi. Hali hiyo ilidhihirisha wazi kabisa mambo ambayo hayajaonekana katika mafundisho ya kanisa la Rumi.

Mwandishi wa ufunuo alitaja matokeo ya kutisha yatakayotokea katika Ufaransa kwa ajili ya kutawaliwa na “mtu wa dhambi”

“Wataukanyaga mji mtakatifu kwa muda wa miezi arobaini na miwili. Nami nitawaruhusu mashahidi wangu wawili, wamevikwa magunia. Hao ndio ile mizeituni miwili na vile vinara viwili visimavyo mbele ya Bwana wa nchi. Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutokea katika vinywa vyao na kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru hivyo ndivyo impasavyo kuuawa. Hao wana amri ya kuzifunga mbinguni, ili mvua isinye katika siku za unabii wao. Nao wana amri juu ya maji kuyageuza kuwa damu, na kuipiga nchi kwa kila pigo, kila watakapo. Hata watakapomaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua. Na mizoga yao itakuwa katika njia ya mji ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodom, na Misri, tena ni hapo Bwana wao aliposulubiwa. . . Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili aliwatesa wao wakaa juu ya nchi. Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu itawaingia wakisimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama”. Ufunuo 11:2-11

“Miezi ya arobaini na miwili” na “siku elfu na mia mbili na sitini” ni kitu kimoja. Ni muda ule ambao kanisa la Mungu liteswa na Rumi Siku 1260 au miaka 1260 ilianza mwaka 538 baada ya Kristo na ikamalizika katika mwaka 1798. Katika mwaka wa 1798 jeshi la ufaransa lilimteka Papa na kumfunga. Papa aliwekwa kizuizini mpaka akafia huko. Tangu hapo utawala wa kanisa la Rumi ulififia.

Mateso ya kanisa hayakuendelea muda wote wa miaka 1260. Kwa rehema za Mungu aliyakatiza, maana aliwahurumia watu wake. Mungu aliyakatiza kwa njia ya mvuto wa watengenezaji wa kanisa.

[125]

“Mashahidi wawili” wanawakilisha maandiko matakatifu ya Agano la Kale na Agano Jipya. Ushahidi halisi wa sheria ya Mungu ya milele na mpango wa ukombozi.

“Watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini wakivaa nguo za magunia” Biblia ilipofafanua ushuhuda wake uliopotoshwa, ukaelezwa kinyume; na wao waliueleza halisi waliitwa wazushi, wakateswa, na kuuawa, hata ikawalazimu kukimbia ili wajiponye. Hao ndio mashahidi waaminifu wakati wa giza kuu la kiroho watu wa Mungu waaminifu walipewa hekima na uwezo wa kulihubiri neno la Mungu.

“Na kama mtu atawadhuru moto ulitoka katika vinywa vyao ukawateketeza adui zao. Na kama mtu atawadhuru hivyo ndivyo ilimpasa uawe” Ufunuo 11:5. Watu hawewezi kukanyaga juu ya Neno la Mungu kwa dharau na kiburi!

“Watakapokwisha kutoa ushahidi wao”. Kama wale mashahidi wawili walipokuwa wakikaribia mwisho wao kimya kimya, vita vitafanywa; kwao na mnyama atokaye kuzimu. Hapa uwezo wa shetani unaonekana.

Imekuwa kanuni ya Rumi ambaye anadai kufuata Biblia kuisitiri Biblia isijulikane, na watu wakae gizani bila nuru ya Biblia Wale mashahidi wawili wenye mavazi ya maguni walitoa unabii katika utawala wao. Lakini mnyama atokaye

“Mji mkuu” ambao mashahidi wawili aliuawa katika njia zake na mizoga yao ililala ni Misri ya Kiroho. Mataifa yote yanayotajwa katika Biblia, Misri ndilo taifa kaidi mno ambalo lilikana kwa ushupavu kuwako kwa Mungu aliye hai na kuzipinga amri zake. Hakuna mfalme yeyote aliyekaidi na kujitoa katika uasi mkuu kama mfalme wa Misri, Farao alivyofanya. Alisema, “Simjui Bwana, wala

sitawaacha Waisraeli” Kutoka 5:2. Huu ndio ukafiri wa kukanusha kwamba hakuna Mungu, na taifa linalohusiana na hali hiyo ya Misri litasema vivyo hivyo.

[126] “Mji Mkuu” pia ni mfano wa kiroho, ufananao na Sodoma, udhalimu wa Sodoma ulidhihirika hasa katika hali ya uasherati na ufedhuli na kila namna. Dhambi hii ilikumba taifa lote lililohusika kutimiza unabii huu wa Biblia.

Kwa kufuata unabii ni kwamba muda kitambo kabla ya mwaka 1798 uwezo mwingine wa kishetani ungeinuka kupigana na Biblia. Katika nchi ile mashahidi wawili wa Mungu watakapouawa, kutaonekana ukafiri kama ule wa Farao na ufisadi kama ule wa Sodoma.

Ajabu Ya Utimizo wa Unabii

Unabii huu ulitimizwa kwa ajabu sana katika nchi ya Ufaransa wakati wa mapinduzi katika mwaka 1793. Ufaransa husimama peke yake katika historia ya ulimwengu, ikiwa ni nchi ya pekee iliyotangaza rasmi kwa sheria iliyopitishwa katika Bunge lake kuwa hakuna Mungu, ambavyo watu wote nchini na mjini wake kwa waume walifurahi na kushangilia waliposikia tangazo hilo.

Ufaransa ilijidhihirisha kuwa na tabia ya Sodoma. Waandishi wa historia hujumlisha ukafiri na ufisadi wa ufaransa kwa maneno haya “Undani wa sheria hizi zihusuzo dini, ndio uliopunguza uhalali wa ndoa, jambo takatifu ambalo mwanadamu anaweza kuwa nalo, jambo la kudumu liwezalo kuimarisha jamii ya watu ndoa ya nchi (ya serikali) na kawaida tu ya mambo ya juu juu yasiyodumu ya kuwaunganisha watu wawili wafuatao anasa Sophie Armoult mchezaji maarufu wa michezo ya kuchekeka alisema, Ndoa ya serikali ni sawa sawa na ‘Sakramenti ya Uzinzi’”

Uadui Dhidi Ya Kristo

“Pale Bwana wetu aliposulubishwa”. Jambo hili lilitimizwa na Ufaransa pia. Hakuna nchi iliyopinga ukweli kwa ukatili sana kuliko Ufaransa. Katika mateso yaliyowapata wakristo walioamini Injili, Ufaransa, ilimsulubisha kristo kwa njia ya wanafunzi wake.

Karne baada ya karne damu za watakatifu zilizidi kumwagika. Wakati watu wa Waldenses walipouawa katika milima ya Piedmont kwa ajili ya Kristo, mambo yale yalitokea katika Ufaransa kwa wa Albigenes. Wafuasi wa matengenezo ya kanisa waliteswa na kuuawa kikatili mno. Mfalme na wakuu wanawake waheshimiwa na vijana walishibisha macho yao kwa kuyaona mateso ya ukatili mkubwa yaliyowafikia wafia dini wa Yesu. Mashujaa wale wahuguenots walimwaga damu zao katika vita vingi vigumu, walipokuwa wakiwindwa kama wanyama pori.

[127]

Wazao wachache wa wakristo wa zamani waliokuwa wangali Ufaransa katika karne ya kumi na nane, waliokuwa wakijificha katika milima ya kusini, waliendelea kushikilia imani ya baba zao. Walivutwa wakitiwa katika kazi za kitumwa maisha yao yote. Waliokuwa na akili na uwezo katika Ufaransa walikamatwa na kufungwa, na kuteswa kikatili mno, wakiwa pamoja na wanyang'anyi na wauaji. Wengine walipigwa na risasi wakafa walipokuwa wakipiga magoti kusali. Nchi yao iliachwa ukiwa kwa upanga na mashoka. “Ilifanywa jangwa moja kubwa lenye majonzi”

“Maovu haya yalifanyika kisheria siyo katika nyakati za giza bali katika nyakati za maendeleo, wakati wa mfalme Louis XIV, Elimu ya sayansi ilikuwa inaendeshwa, sheria halali za mahakama zilikuwa zikitungwa na watu wenye busara na wasomi ambazo zilisakama hali nzuri ya wema na unyenyekevu na upendo”.

Maasi Makuu Ya Kutisha.

Lakini matendo maovu mno ya kishetani yaliyotendeka katika karne za kutisha ni yale mauaji ya St. Bartholomew. Mfalme wa ufaransa akihimizwa na makasisi wa Rumi aliunga mkono maazimio hayo maovu. Kengele iliyopigwa usiku wa manane ndiyo iliyokuwa alama ya machinjo yake.

Waprotestanti kwa maelfu walikuwa wamelala manjumbani mwao huku wakimheshimu mfalme wao, walikokotwa na kupelekwa machinjioni ili wakauawe.

Mauaji yaliendelea muda wa siku saba katika mji wa Paris. Kwa amri ya mfalme mauaji yaliendelea na kufika hata katika miji mingine, ambako Waprotestanti walikutwa, watu wakuu na

wakulima watu wazima na watoto, akina mama na vijana wamechinjwa wote pamoja. Katika Ufaransa watu kiasi cha 70,000 walipotea.

[128] “Habari ya mauaji haya ilipofika Rumi, shangwe ya waongozi wa kanisa ilizidi mno. Kadinali wa Lorraine alimtuza mleta habari taji maelfu. Kasisi wa Angelo aliposikia alishangilia sana, kengele za shangwe zikapigwa kwa kila mnara wa kanisa. Mioti ikiwashwa ambayo iliungaza usiku ukawa kama mchana; na Gregory XIII aki-fuatana na makasisi, makadinali na wakuu wengine waliandamana mpaka katika kansia la St. Louis ambako kadinali wa Lorraine alimimba. Chuma kiligongwa ili kuadhimisha mauaji hayo. . . . Kasisi wa Kifaransa aliinena siku hiyo kuwa siku iliyojaa furaha na shangwe, ambapo papa alipopata habari hizo alikwenda ikulu kutoa shukrani zake kwa Mungu na kwa mfalme Louis”

Roho ile ile iliyoongoza kwenye mauaji ya St. Bartholomew ndiyo iliyoongoza katika mapinduzi. Yesu Kristo alitajwa kuwa mlaghai na mdanganyifu. Kwa hiyo usemi wa Wafaransa wakafiri ulikuwa: “Mwangamize huyu movu” yani Kristo. Kufuru na ufisadi vilienda bega kwa bega. Kwa njia hii walimheshimu na kumtukiza shetani na Yesu mwenye tabia safi ya kweli, mwenye upendo “alislubishwa”

Mnyama aliyetoka kuzimu alifanya vita nao, na kuwashinda ufunuo 11:10. Roho ya ukafiri iliyotawala Ufaransa wakati wa mapinduzi na utawala wa kitisho, ilifanya vita na Mungu na Neno lake. Ibada ya kumwabudu Mungu ilipigwa marufuku na bunge la taifa. Biblia zilikusanywa na kuchomwa moto hadharani. Shule za biblia zilipigwa marufuku. Siku ya badala yake ikawekwa kila siku ya kumi ya juma iwe ndiyo siku ya kupumzika. Ubatizo na meza ya Bwana vilikatazwa. Matangazo yakawekwa pote penye makaburi yakisema, kuwa kifo ni cha milele, hakuna ufufuo.

Ibada zote za kidini zilipigwa marufuku, ila tu siku ya kuadhimisha uhuru. Askofu halali wa Paris aliletwa mbele Atangaze wazi hadharani kuwa dini aliyokuwa akifundisha kwa miaka mingi ilikuwa upuuzi tu, wala haina msingi kihistoria wala kimaandiko matakatifu. Alikana dhahiri kwamba hakuna Mungu, ambaye alikuwa amejitoa kuabudu miaka yote hii. “Nao wakao juu ya nchi walifurahi juu yao na kushangilia. Nao walipelekeana zawadi wao kwa wao juu ya nchi” Ufunuo 11:10. Wakafiri wa Ufaransa wamewanyamazisha mashahidi wawili wa Mungu. Neno la Mungu

likaanguka limekufa katika barabara za ufaransa, na wale waliomchukia Mungu walishangilia. Watu wakamkana dhahiri mfalme wa mbinguni.

Makufuru ya Ukaidi

Mmojawapo wa mapadri alisema “Mungu, ikiwa upo lipiza kisasi kwa ajili ya kuliharibu jina lako. Nakuomba utangaze vita! Wakakaa kimya, huthubutu kunguruma. Kama ni hivyo, nani ataamini kuwa wewe upo?” je, huo sio mwangwi wa sauti ya matakwa aliyodai Farao, “Bwana ni nani hata nitii sauti yake?” [129]

“Mpumbavu anasema moyoni Hakuna Mungu”. “Na wote” Zaburi 14:1-2; 2Tim. 3:9. Baada ya nchi ya ufaransa kukataza ibada ya Mungu aliye hai, walizidi kudidimia chini kwa kuanzisha ibada ya Mungu wa hoja au maoni mwanamke Malaya. Huyu ndiye aliyewakilisha taifa la Ufaransa! Mojawapo ya maadhimisho ya sikukuuu ya upumbavu huu wa kuabudu Mungu wa madhumuni ambaye ni mwanamke Malaya, mambo ya kiwazimu na ya kipumbavu yalifanyika. . . . Milango ya jumba la makutano lilifunguliwa. . . . Wabunge wakaingia kwa heshima wakifuatana kwa utaratibu, huku wakiimba wimbo wa uhuru, wakimsindikiza mwanamke aliyevaa shela, ambaye ndiye tamasha ya maadhimisho hayo, huyo ndiye Mungu Hoja. Wakimleta mpaka kwenye ukingo wa mahali pakuu, wakuu humfunua shela na kumkalisha pale kwa kiongozi na hapo hutambuliwa kuwa ni msichana ambaye hucheza michezo wa Opera.

Mungu Hoja

Kule kubuni na kuweka Mungu wa madhumuni kuliendeleza sana kuigwa katika taifa zima; hasa pale watu walipotaka kuafikiana na hali ya mapinduzi.

Wakati “mungu” huyu wa hoja alipokuwa akiletwa katika mkutano (msichana mrembo), msemaji alimshika mkono akawageukia makutano akisema, “Wanadamu sasa komeni kuhofu na kutetemeka mbele za ngurumo zisizo na uwezo kuhofu na kutetemeka mbele ya ngurumo zisizo na uwezo ambazo watu walibuni kwamba ni za Mungu ambaye hakuna. Kwa hiyo tangu sasa msiamini kwamba kuna Mungu wa ngurumo la sasa ni ‘madhumuni’ tu. Nawatoleeni

sura safi ya kupendeza, na mkipenda kuwa na sanamu, hii ndiyo ya kuwa nayo. . . . Huyu mungu madhumuni baaada ya kupokelewa akitiwa katika motokaa zuri sana akapelekwa katika kanisa kuu la Noore Dame ili awe badala ya Mungu. Huko akawekwa juu ya madhabahu, na kutukuzwa badala ya Muumbaji.”

[130] Upapa ukaanza kazi ambayo ukafiri ulikuwa ukiimaliza, kazi hiyo ikaharakisha Ufaransa ipate kuangamia. Waandishi wakiandika juu ya madhara ya mapinduzi husema kuwa wanaohusika na lawama hizo ni serikali na kanisa. Hasa mhusika mkubwa ni kanisa. Mapapa waliloga mawazo ya watawala kuhusu matengenezo ya kanisa. Warumi walisistiza ukatili na mateso juu ya Watengenezaji, na mambo haya yaliungwa mkono na utawala.

Po pote pale Injili ilipopokelewa mawazo ya watu yaliamshwa. Wakaanza kutupilia mbali hali ya ujinga na ushirikina ambavyo vimewafunga utumwani. Watawala waliona na wakatetemeka kwa ajili ya utawala wao wa kidhalimu.

Rumi haikuchelewa kuchochea hofu yao ya wivu. Papa alimwambia mtawala wa ufaransa. Katika mwaka 1525, akasema “dini hii ya kiporotestani haitaangamiza dini kweli tu, bali itaangamiza hata na utawala, na mamlaka na sheria na kanuni zote pia” Mjumbe wa papa alimtahadharisha mfalme, akasema “Waprotestanti watavuruga raia na pamoja na kanuni za dini pia Utawala umo hatarini sawasawa na dini pia” Rumi ilifaulu kuifanya Ufaransa kuyapinga matengenezo ya kanisa.

Mafundisho ya Biblia yangependa kanuni za haki katika mioyo ya watu. Yangewafanya watu kuwa wa kiasi na kweli, mambo ambayo ndiyo msingi wa taifa lolote, nayo ndiyo yanayoleta mafanikio “haki huinua taifa” “Kwa hiyo kiti cha enzi huthibitika” Mithali 14:34;16:12; Isaya 32:17. Mtu ambaye hutii sheria ya Mungu kikweli hutii sheria ya nchi pia. Ufaransa ilipiga marufuku Biblia. Karne baada ya karne watu mashuhuri, wenye uwezo na akili, ambao walikuwa na imani, waliteseka kwa ajili ya imani, wengine wakitumikishwa kitumwa, wengine wakichomwa moto, wengine kuangamia vifungoni. Wengine kwa maelfu walijiponya kwa kukimbilia katika nchi nyingine. Hali kama hiyo iliendelea kwa miaka 250 tangu matengenezo yalipoanzishwa.

Ilikuwa vigumu kwa vizazi vya ufaransa, kwa muda huo wote kutoshuhudia wakimbizi wa Injili kwa ajili ya mateso ya kishetani

yaliyokuwako. Wakimbizi hao walikwenda na ujuzi wao wa sayansi na ufundi na maarifa ya aina nyingi kuzifaidia nchi zile walikokimbilia. . . . Kama wote hao waliofukuzwa, wangeishi Ufaransa. . . nchi hiyo ingekuwa na mafanikio makubwa kiasi gani! Tena Ufaransa ingalikuwa na mvuto na kielelezo kwa mataifa mengine. Lakini kwa ujinga na upofu ukawafanya wafukuze kila mwalimu wa haki, kila mwenye tabia bora, kila mtetea kweli hata kwenye utawala. Mwishowe nchi ikaangamia kabisa. Mapinduzi na maafa yake ndiyo yalikuwa matokeo ya hali hiyo.

Jinsi Ingalipasa Kuwa

[131]

Kule kukimbilia kwa Wahunguenots kutoka Ufaransa kulileta upungufu mkubwa sana nchini. Miji iliyokuwa ikistawi kwa wingi wa viwanda ilibakia kuwa magofu ya kutu. . . . Imekadiriwa kuwa wakati wa mapinduzi kulikuwako maskini laki mbili katika mji wa Paris waliokuwa wakilishwa na kusaidiwa na mfalme. Waliokuwa na mafanikio katika taifa zima ni wa Jesuits peke yao. Wengine wote walikuwa wamenyauka.

Injili peke yake ingetatua matatizo yaliyoipata nchi ya Ufaransa, ambayo yaliwafadhaisha waongozi wa serikali, na wadini, wafalme na mwisho kuliangamiza taifa zima. Lakini chini ya uongozi wa kanisa la Rumi watu wamepoteza mafundisho ya Kristo yahasuyo kujikana nafsi, na kutoa huduma isiyokuwa na ubinafsi kwa wahi-taji. Matajiri hawakuwa na shughuli kwa maskini. Choyo cha kujitajirisha kilizidisha hali ya maisha kuwa ya matatizo makubwa. Kwa karne na karne hapakuwa na maafikiano baina ya matajiri na maskini. Matajiri waliwaonea maskini, na maskini waliwachukia matajiri.

Katika mikoa mingi wakulima wa hali ya chini waliishi kwa rehema za makabaila, nao walilazimishwa kutii na kufuata kama vile mabwana wanavyotaka. Walitozwa kodi kubwa sana na watawala na makasisi.

Wakulima walikuwa nusura kufa njaa kwa vile wakubwa wao walivyowaonea. Maisha ya kilimo hayakuwa na pumziko la aina yoyote, na ya ufukara kabisa. . . . Malalamiko yao Yalihesabiwa kuwa ni ujeuri, wala hayakujaliwa. Rushwa ilienea, hata mahakamani ilijaa tele. Kodi iliyotozwa kwa watu, haikuingia katika hazina

ya serikali, hata nusu yake. Karibu yote ilipita katika mikono ya wapenda mali, ambao ni watumishi wa serikali. Kodi hiyo iliyotozwa kwa wingi hivyo, wale watumishi wao hawakuhusika na utoaji huo, ila tu raia wa kawaida. Wale waliongoja kunyakua na kujinufaisha. Ufedhuli ulikuwa hausemeki.

Kwa muda wa zaidi ya nusu karne kabla ya mapinduzi utawala ulikuwa mikononi mwa Lois XV, mfalme aliyejidhihirisha kuwa mtu mlegevu, apendaye uasherati. Kifedha aliisumbua sana serikali na kuitia katika matatizo, na kukasirisha raia mno, hata hapakutakiwa kuwa na nabii wa kutabiri maafa yatakayotokea karibu, maana mambo hayo yalijitangaza yenyewe. Walijaribu kurekebisha mambo, lakini ilikuwa kazi bure. Ajali iliyokuwa inakabili Ufaransa ilionekana kwa maneno ya mfalme, aliyosema, “Baada yangu, ndipo uharibifu utatokea”

[132] Rumi ilikuwa imewashawishi watawala wa Ufaransa wawafungie watu gizani kwa kutopata nuru ya Neno la Mungu, ikiazimu kuwafunga wote watawala na raia katika giza la kutopata neno la Mungu. Hatari mbaya zaidi ya ile ya kuangamia kimwili ilikuwa uharibifu wa kiroho. Kuwanyima watu Biblia, na kuwaacha gizani kuliwafanya wazame katika ufasiki na uovu mpaka wakawa hawafai kujitawala.

Matokeo ya Kuvuna Damuni

Rumi badala ya kuwashikilia watu katika hali ya ujinga wa kukubali tu mambo bila kuwaza, na kuwafuatafuata tu mambo ya Rumi, watu wakawa wakafiri waliojanjaruka na kuwa waasi. Wakadharau mafundisho ya Rumi na kuyaona mkatili na mwonevu, kwa hiyo hawakutaka kujihusisha naye. Wakadhani kuwa hayo ndiyo matokeo ya Biblia kama inavyofundishwa na Rumi.

Warumi wamemwakilisha Mungu vibaya mbele za watu, na sasa matokeo yake yamekuwa kuikataa Biblia na mwenye Biblia. Katika hali hiyo Voltaire na wafuasi wenzake wakaiasi Biblia kabisa, wakaueneza ukafiri tu. Rumi imewafunga watu chini ya mongozi yake, na sasa watu walitupilia mbali mambo yote ya Rumi. Kwa chuki hiyo wakakataa mambo yote ya uongo na ya kweli pia.

Walipoanza mapinduzi kwa ukubali wa mfalme watu walipata wawakilishi wengi zaidi kuliko wakuu wa kila hali. Kwa hiyo

walikuwa na uwezo mwingi zaidi. Lakini walikuwa hawajui jinsi ya kutumia uwezo huo kiakili. Wakawa wenye kuonea na kudhulumu watu. Halafu watu wakaazimia kujipigania na kulipa kisasi. Walioonewa wakawageukia waliowaonea.

Ufaransa ilivuna mavuno katika damu kwa matokeo ya kuyakubali mambo ya Rumi. Pale Ufaransa ilipoanzia kuchoma watengenezaji ikiongozwa na Rumi, ndipo pale pale mashine za kukata vichwa zilipowekwa ili kukata vichwa vya wakuu wakati wa mapinduzi. Mahali pale mfiadini wa kwanza wa Kiprotestanti alipofia katika karne ya kumi na sita, ndipo pale mtu wa kwanza alipopokwa kichwa wakati wa mapinduzi katika karne ya kumi na nane. Wakati hifadhi ya sheria ya Mungu ilipotupiliwa mbali, taifa zima liliasi, na nchi yote ikiwa yenye machafuko ya kuuana ovyo. Vita ya kupigana na Biblia inajulikana kama utawala wa kitisho katika ulimwengu. Mshindi wa leo, kesho atahukumwa.

Mfalme, kiongozi wa dini, wakuu wa serikali, wote walilazimika kutii na kufuata amri za watu waliochafuka mawazoni na kuwa kama wenda wazimu. Wale waliotangaza kifo cha mfalme walimfuata pia kwa kumnyonga. Machinjano yalikuwa mengi sana. Watu wote wliodhaniwa kuwa hawayauungi mkono mapinduzi walichinjwa ovyo. Ufaransa ikawa mbuga ya majeshi ya watu wasio na utaratibu, wakizunguka zunguka na kuchijana. Katika mji wa Paris machafuko yalikuwa yakifuatana mfululizo, na raia waligawanyika katika vikundi vya usaliti; visivyokuwa na jambo la kufanya ila kuzungukazunguka tu na kufanya ghasia Nchi ilikuwa karibu kufilisika, jeshi la askari ililikuwa likifanya ghasia, likidai mishahara ya nyuma ambayo haikulipwa. Watu katika mitaa walikuwa shidani kukosa chakula, mikoani kulijaa maharamia ambao walipora kila kitu kilichoonekana, na ustaarabu ulikuwa katika ukingo wa kutoweka kwa ajili ya fujo na ghasia zilizoenea kila mahali bila mtu wa kuzikomesha.

[133]

Sasa watu walikuwa wamejifunza mafundisho ya ukatili na mateso ambayo Rumi imewafundisha kwa bidii, Sasa watu waliokamatwa na kuchomwa moto sio wanafunzi wa Yesu Kristo. Wanafunzi wa Yesu walichomwa zamani, na wengine walifukuzwa nchini zamani. Wakati huu mapadri wa Rumi na mfuasi wa Rumi ndiyo wanaouawa. Magereza yaliyojaa Wahuguenots zamani, sasa yalijaa watesi wao. Mateso yote ya kila namna ambayo kanisa la Ro-

man Katoliki ili watesa wafuasi wa Kristo ambao waliitwa wazushi, yamewageukia waongozi wa Rumi.

Halafu zikafika siku. . . . Ambapo majasusi walienea kila mahali wakivizia wahusika; wakati mashine za kunyongea watu zilikuwa hazitulii; wakati magereza yalijaa watu kama merikebu iliyopakia watumwa; wakati damu za watu zilitiririka katika mto wa Saine. . . . Mistari mirefu ya wafungwa ilikatwakatwa na marisasi. Matundu yalifanywa chini ya mashua zilizojaa watu. . . . Hesabu ya wavulana na wasichana wa umri wa miaka kumi na saba waliochinjwa kwa ajili ya kupinga serikali ni mamia na mamia. Watoto wachanga walinyakuliwa kutoka kwa mama zao na kuchomwa mikuki popote walipokutwa.

Haya yote yalikuwa matakwa ya Shetani. Kampuni yake ni udanganyifu, na kusudi lake ni kuangamiza watu, ili kuchafua kazi ya Mungu na kuvuruga mpango wa upendo, ili kuleta huzuni mbinguni. Halafu kwa njia ya udanganyifu wa kihila atupe lawama zote kwa Mungu. Ndivyo anavyowaongoza watu waamini, kana kwamba ndivyo Mungu alivyopenda. Watu walipougundua udanganyifu wa Warumi, shetani akiwaongoza waamini kuwa dini yote ni udanganyifu mtupu, na Biblia ni hadithi tupu za uongo.

[134]

Kosa Baya Kuliko Yote

Kosa baya mno lililosababisha maafa mabaya katika Ufaransa lilikuwa kutojali ukweli mkuu: uhuru wa kweli umo katika kuliitii Neno la Mungu. Lakini kulikataza au kulipinga marufuku hukaribisha maafa. “Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari”. Isaya 48:18. Wote ambao hawajifunzi fundisho katika kitabu cha Mungu wanaagizwa wajifunze kutokana na historia.

Wakati shetani alipolitumia kanisa la rumi liwaongoze watu waziasi amri za Mungu, kazi yake ilikuwa najisi. Kwa kazi ya roho ya Mungu, kazi ya shetani ilizuilika isifikie maazimio yake. Watu hawakufuatia asili ya maafa yao, na kugundua kiini chake. Lakini wakati wa mapinduzi sheria ya Mungu ilikataliwa dhahiri na bunge la taifa. Na wakati wa utawala wa kitisho uliofuta, watu waliona asili yake.

Uasi wa sheria ya kweli na haki lazima matokeo yake yawe uangamivu. Roho ya Mungu inayozuia ukatili wa shetani ilikuwa ikiondelewa kwa sehemu kubwa, kwa hiyo mtu yoyote aliyetaka kutenda matendo ya ukatili kwa wenzake hakuwa na kizuizi. Watu hawakufuatia asili ya maafa yao, na kugundua kiini chake. Lakini watu wa mapinduzi sheria ya Mungu ilikataliwa dhahiri na bunge la taifa. Na wakati wa utawala wa kitisho uliofuata, watu waliona asili yake.

Uasi wa sheria ya kweli ya haki lazima matokeo yake yawe uangamivu. Roho ya Mungu inayozuia ukatili wa shetani ilikuwa ikiondolewa kwa sehemu kubwa, kwa hiyo mtu yeyote aliyetaka kutenda matendo ya ukatili kwa wenzake hakuwa na kizuizi. Watu waliochagua kuasi, basi walivuna mavuno yake. Nchi ilijaa uharamia na uasi wa kila hali. Maombolezo ya uchungu yalisikika kote, tangu mijini mpaka mashambani kwa ajili ya maharamia walikuwa wakiharibu vitu popote. Ufaransa ilitikiswa kana kwamba imekumbwa na tetemeko la nchi. Dini, sheria, uhuru na utulivu, jamaa, serikali na kanisa, vyote vilivurugwa kabisa na wafedhuli ambao wameelekezwa kuikana sheria ya Mungu.

Mashahidi wa Mungu waliochinjwa na wenye kukufuru “wataokao katika shimo la abuso”. Hawatakaa kimya daima. “Na baada ya siku hizo tatu u nusu roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama” ufunuo 11:11. Mwaka 1793 sheria ilipitishwa na bunge la ufaransa ya kupiga marufuku Biblia. Baada ya miaka mitatu na nusu tangu sheria hiyo ipitishwe, bunge lile lile lilikutana na kufuta sheria hiyo. Watu walitambua kuwa imani kwa Mungu ndiyo msingi wa maadili na wema.

Kuhusu Mashahidi wawili, agano la kale na Agano Jipya nabii husema zaidi kuwa “Wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku. Wakapanda mbinguni katika mawingu adui zao wakiwatazama” Ufunuo 11:12. Mashahidi wawili wa Mungu wameheshimiwa kwa namna ambayo haijaonekana. Katika mwaka 1804 chama cha kupiga chapa Biblia, yaani British and Foreign Bible Society kiliundwa, kikifuatiwa na mashirika mengine yaliyoundwa barani Ulaya. Mwaka 1816 Chama cha Kimarekani cha Biblia kilianzishwa. Tangu hapo Biblia ilitafsiriwa katika lugha mamia, nzima au sehemu.

Kabla ya mwaka 1792 kazi za misheni zilijaliwa kidogo sana. Lakini katika mwisho wa karne ya kumi na nane mageuko makuu yalitokea. Watu hawakuridhika na maongozi ya kibinadamu tu ila waliona haja ya maongozi ya Mungu; ambayo hupatikana kwa dini. Tangu wakati huo kazi za misheni zimekuwa na kuendelea kiajabu.

Maendeleo katika uchapaji husukuma mbele kazi ya kueneza Biblia kwa namna ya pekee. Kuvunjilia mbali chuki za kitaifa ambayo ni hali ya zamani, na kuondolewa mbali uwezo wa makasisi wa Rumi, kumefungua njia ya kuliingiza Neno la Mungu pale lilipozuiliwa zamani. Sasa Biblia imefika pande zote za dunia.

Kafiri mmoja Voltaire alisema “Nashangaa kusikia kuwa watu kumi na wawili ndio walioimarisha dini ya Kikristo. Nathibitisha kwamba mtu mmoja atosha kuifuta.” Watu mamilioni walijiunga kupinga Biblia, lakini iliwashinda. Kama wakati wa Voltare palikuwa na Biblia mia moja, basi kuna malaki ya vitabu hivo sasa hivi. Kwa maneno ya watengenezaji wa zamani “Biblia ni fuawe lililochakaza nyundo nyingi” Chochote kilichojengeka kwa msingi ya kibinadamu, kitaangamia lakini kilichojengeka Mwambani, ambao ni neno la Mungu kitadumu milele.

Marejeo:

Blackwood Magazine, November 1870

Sir. Walter Scott, Life of Napoleon, Vol. 1 ch. 17

Wylie, bk. 22, ch. 7

Henry White the massacre of St. Bartholomew, ch. 14 p. 34

Scott, Vol. 1 ch. 17

Lacretelle History Vol. II p. 309 in Sir Archibad Alison History of Europe, Vol. ch. 10

Scott Vol. 1 ch. 17

M. A Thiers, History of the French Revolution, Vol. 2 p. 370-371.

D' Aubigne, History of Reformation in Europe in the Time of Calvin, bk. 2 ch. 36.

Wlie, bk. 13 ch. 20

Ibid.

Ingawa mamlaka na mafundisho ya Rumi yalikataliwa, lakini kawaida nyingi za imani yao ziliunga na kuendeshwa katika ibada ya kanisa la Aglikan. Ilidaiwa kwamba mambo ambayo hayakukanushwa katika Biblia hayakuwa na ubaya wowote. Kule kushikilia kawaida nyingi za Rumi kulipunguza mtengano uliokuwapo baina ya kanisa la Matengenezo na Rumi na ikahimizwa kwamba kwa kufanya hivo watazidi kuingiza kanuni za matengenezo zikubaliwe na Rumi.

Watu wengine hawakukubaliana na mawazo hayo. Waliona kuwa kawaida hizo ni alama ya utumwa ambao walipigana ili kujiondoa humo. Hawawezi kuzikubali ziingizwe katika ibada zao. Walisema kuwa Mungu amepanga kanuni za kufuatwa katika ibada, ambazo zimeandikwa katika Neno lake, na ya kwamba watu hawana ruhusa kuongeza mambo yao juu ya kanuni hizo, wala kuondoa mambo mengine. Rumi ilianza kwa kukataza mambo ambayo Mungu hakukataza, na ikaishia na kukataza mambo ambayo Mungu aliamuru yafanyike.

Watu wengi waliona kuwa kawaida hizo zinazofuatwa na kanisa la Anglikana ni ukumbusho wa ibada ya sanamu, na kanisa hilo likiungwa mkono na serikali likasisitiza mambo yawe hivyo tu, na ibada iwe kama inavyoendeshwa na kanisa la Anglikana. Mtu akikaidi, adhabu ni kifungo, kutiwa kizuizini au kifo.

Waprotestant hawakuweza kuona uhakika na maisha yao kwa siku za mbele, kwa vile walivyokuwa wakiwindwa kila mahali, wakiteswa na kufungwa ovyo magerezani. Wengine waliotafuta makimbilio katika nchi ya Uholanzi, walisalitiwa na kutiwa katika mikono ya adui zao. Lakini kwa juhudi na uvumilivu walifaulu, wakapata hifahdi katika pwani za watu ambao ni marafiki.

Walikuwa wameacha nyumba zao na mali zao pia. Walikuwa wakimbizi katika nchi za kigeni, wakilazimika kufanya kazi ngumu ili wapate chakula. Lakini hawakuishi kivivu au kwa manung'uniko.

Walimshukuru Mungu kwa ajili ya mibaraka aliyowapa, na furaha ya ushirika waliyopata bila masumbufu yo yote.

Mungu Alitawala Mambo

Wakati mkono wa Mungu ulipoonekana ukiwaonyesha nchi iliyoko ng'ambo ya bahari, ambayo itakuwa makao yao ya amani na uhuru, itakayokuwa urithi wa watoto wao wenye uhuru wa dini, walifuata maongozi hayo. Mateso na kufukuzwa vilifungua njia ya uhuru.

[137] Wapuritani walipolazimika kuachana na kanisa la Kiingereza, walijiunga wenyewe kwa kiapo kwamba watakuwa “watu huru” watakaofuata njia ya Bwana, kadiri walivyofunuliwa katika Maandiko Matakatifu. Hapa ndipo palikuwa kanuni hasa ya Kiprotestanti. Wakiwa na maazimo hao wasafiri hawa waliondoka Uholanzi kwenda kutafuta makao mapya katika nchi mpya. Mchungaji wao aitwaye John Robinson, katika ujumbe wake wa kwaheri kwa wakimbizi hawa alisema:

“Nawaagiza mbele za Mungu na mbele za Malaika zake watakatifu kuwa msinifuate zaidi ya ninavyomfuata Kristo. Ikiwa Mungu atawafunulia jambo jipya kwa njia yake mwenyewe, lipokeeni kwa moyo jinsi mlivyopokea mambo katika huduma yangu; maana nina matumaini kwamba Bwana anazo kweli nyingi ambazo atazifunua zaidi katika Neno lake Takatifu.”

“Kwa upande wangu, sitaombolezea hali ya makanisa ya matengenezo kiasi cha kutosha. . . . Ambao kwa wakati huu hawatakuwa kama vyombo vya matengenezo ya kanisa. Walutheri hawawezi kuvutika kuwa namna nyingine zaidi ya ile ya Luther aliyoona, na wafuasi wa Calvin, mnaona, wanasimama pale walipoachwa na mtu huyu wa Mungu, ambaye hakuona mambo yote vile vile,... Ingawa katika nyakati zao walikuwa huru waking'aa na hata hivyo hakufunuliwa mambo ya Mungu yote. Kama wangukuwa wangali hai leo wangukuwa tayari kupokea mambo zaidi kama walivyokuwa hapo mwanzo”

“Kumbukeni ahadi zenu na agano lenu na Mungu na mapatano yenu ninyi kwa ninyi, kwamba mtakuwa tayari kupokea ukweli wote utakaofunuliwa katika Neno lake. Walakini nawatahadharisha kwamba, chochote mpokeacho kuwa ni kweli, kichunguzeni

na kukipima kwa njia ya Neno takatifu la Biblia, mkilinganisha andiko na andiko kabla hamjalipokea, maana haiwezekani kuwa ukristo utoke katika giza la kumpinga Kristo, ujuzi wa kweli uatajidhihirisha”.

Hamu ya uhuru wa dhamiri iliwachochea wasafiri hao kuvuka bahari, wakivumilia shida, na kupambana na matatizo ya jangwani ili kuweka msingi halisi wa taifa. Hata hivyo wasafiri hao wahakufahamu kanuni za uhuru wa dini. Uhuru ambao walijitolea kuupata, hawakuwa tayari kuuachia. Makosa ya upapa ambayo yalikuwa ndiyo shina la uovu wao, yalikuwa kwamba, mafundisho ya Mungu anataka kanisa litawale dhamiri za watu, na kwamba mpingaji yeyote aadhibiwe. Watengenezaji hawakuachana na kosa hilo la Rumi la kutovumilia. Giza nene la makosa ambayo Rumi imeanzisha halikufutika kabisa.

Aina ya utawala wa kanisa ulianzishwa na wananchi, mahakama yalipewa uwezo wa kuwaadhibu wapingaji wa mambo ya kidini. Kwa hiyo kanisa lilikuwa na uwezo kama ule wa serikali. Hali hii ilileta mateso.

[138]

Roger Williams

Roger Williams alifika nchi mpya ili kuufurahia uhuru wa dini sawa kama wasafiri wengine waliomtangulia. Lakini aliona kuwa uhuru huu ni haki ya kudumu kwa wote hilo lilikuwa jambo ambalo watu wengi walikuwa hawajaliona. Williams alikuwa mtafuta ukweli hasa. Alikuwa mkristo wa kwanza zamani hizi aliyebuni serikali ya kiraia yenye misingi ya uhuru wa “dhamiri” Alisema, hakimu, au watu wanaweza kuamua mambo yampasayo mtu amtendee mwenzake; lakini wanapojaribu kuingilia mambo yampasayo mtu amtendee Mungu, hapo huwa wamepotoka kabisa, wala hakuna usalama. Maana ni dhahiri kuwa kama hakimu akiwa na uwezo, anaweza kutunga mawazo, au imani kuhusu leo na kutunga wafalme wengi; na ilivyokuwa ikifanywa na mapapa na mabaraza ya kanisa la Rumi.

Mahudhurio katika kanisa, ilitolewa adhabu ya fani au kifungo, kama mtu hakufuata kanuni za kanisa sawasawa. Williams alisema, “Kuwalazimisha watu wasiokuwa wa dhehebu moja nawe, ili kufuata dhehebu lako ni kuvunja uhuru wa dhamira ya mtu, na kumlazimisha

mtu aabudu bila dhamira yake, ambayo ni unafiki mtupu . . . Mtu yeyote asilazimishwe kuabudu bila hiari yake”

Roger Williams aliheshimiwa, walakini msisitizo wake kuhusu uhuru wa dini haukupendwa. Ili kuepuka asikamate ililazimika kutoroka wakati wa baridi kali na dhoruba, akakimbilia katika msitu mnene. Asema, “Kwa muda wa majuma kumi na manne nilihangaika msituni katika baridi bila kula wala kulala” Lakini, kunguru walinilisha jangwani, na mvungu wa mti ulikuwa maficho yangu. Aliendelea na mahangaiko yake katika barafu msituni mpaka kafika kwa mhindi mmoja aliyemhurumia na kufanya naye urafiki, akamtunza.

[139] Aliweka msingi wa kwanza wa serikali ya kisasa ambayo hutambua uhuru halisi ya kwamba kila mtu budi amwabudu Mungu kwa hiari ya moyo wake, sio kulazimishwa. Kisiwa kiliendelea na kustawi mpaka kanuni zake za uhuru wa dini na wa mtu binafsi zikawa msingi halisi wa serikali ya Marekani.

Mkataba wa Uhuru.

Tamko la tangazo la uhuru wa Marekani lilisema, “Tunashikilia kweli hizi ziwe mashahidi, ya kwamba, watu wote waliumbwa kwa usawa; kwamba kila mtu alipewa na Muumba wake haki fulani ya kudumu; baadhi ya haki hizi ni uzima (maisha), uhuru, na starehe (furaha). Katiba inatoa haki ya hiari ya kila mtu, yaani kutoingilia dhamira ya mtu. Bunge halitatunga sheria yoyote ikiegemea upande wa dini, au ikiunga mkono dini yoyote, au kukataza dini yoyote. Waundaji wa katiba walielewa kanuni za utu, kwamba uhusiano na mtu na Mungu wake hauingiliwi na sheia yo yote, na hata ya kwamba hiari yake ni ya kudumu haiingiliwi na chochote.”

Habari zikaenea Ulaya nzima kuwa nchi ya Marekani kila mtu yu huru kufuatilia matunda ya kazi yake bila kuingiliwa; na kila mtu hufuata jinsi dhamira yake inavyomwongoza. Kwa hiyo watu maelfu wakafurika kwenda katika Nchi Mpya. Kwa muda wa miaka ishirini tangu wasafiri wa kwanza walipofika Pylymouth (1620) watu maelfu wamehamia New England (Marekani). Hawakukaa na kutapatapa, ila kila mtu alishika jembe na kulima na kupata mavuno ya kazi yake. Walivumilia upungufu wa vitu walivyoacha ulaya bila

manung'uniko, wakisamadi mti wa uhuru wao kwa machozi, na kwa jasho la uso waliendelea mpaka mafaniko makubwa yakatokea.

Ukuu wa kweli wa Usalama wa Taifa.

Kanuni za Biblia zilifundishwa nyumbani, shuleni na kanisani. Matunda yake yalionekana maishani mwa watu wakiwa waangalifu, wenye maarifa, wanyofu, wenye kiasi. Mtu alimaliza mwaka mzima bila kuona mlevi, wala mfedhuli, au kuona mtu akiombaomba barabarani. Kanuni za Bibia ndizo usalama wa kweli kwa ustawi wa taifa. Mahamio mapya yaliyokuwa na hali ya ufukara yaligeuka kuwa nchi zenye usatawi mkuu, na ulimwengu ulio na ustawi wa kanisa bila kuwa na papa, na serikali bila kuwa na mfalme.

Lakini ongezeko la watu huko Marekani lilikuwa na nia tofauti na ya wale wasafiri wa kwanza waliohamia huko. Ongezeko la watu lilikuwa na nia ya kutafuta uchumi, mali ya dunia hii tu.

Serikali ya mahamio, iliruhusu tu washiriki kupiga kura, kuweka wakristo tu katika madaraka. Hali hiyo ilikubaliwa ili kutunza serikali iwe na watu waaminifu. Lakini matokeo yake yakawa kuchafua kanisa. Watu wengi walijiunga na Constatine mpaka leo, jaribio la kutaka msaada wa serikali katika kuendesha mambo ya kanisa ingawa inadhaniwa kuwa ni kuvuta ulimwengu ukae kanisani, lakini ukweli ni kulivuta kanisa liende ulimwenguni.

Makanisa ya Kiprotestanti ya Marekani, hata yale ya ulaya, yameshindwa kuendelea katika njia ya watengenezaji wa kwanza. Watu wengi wanafanana na Mafarisayo wa wakati wa Kristo, au Warumi siku za Martin Luther, kwamba ufedhulli vinaendelea katika imani zao. Baadaye matengenezo yalizimika polepole mpaka ikawako haja ya kuwa na makanisa ya Kirumi, wakati wa Luther. Wakati huo mawazo ya kibinadamu ndiyo yaliyoheshimiwa kuliko neno la Mungu. Watu walikoma kuchunguza Neno la Mungu, hivyo walibaki na mapokeo tu ya watu ambayo hayana msingi katika Biblia

Kiburi na anasa viliingia kanisani na kuhesabiwa kuwa ni sehemu ya dini, na kanisa likaoza kabisa. Mapokeo tu ambayo yalikuwa na uharibifu yalikuwa na nguvu kanisani. Kanisa likayashikilia mapokeo hayo badala ya imani iliyokabidhiwa kwa watakatifu.

Hivyo kanuni za kweli zilizowekwa na Watengenezaji zilidhaurauliwa na kuwekwa kando.

Marejeo:

J. Bown, *The Pilgrim Fathers*, p. 74

Martiny, Vol. 5. p. 70

D. Neal, *History of Puritants* Vol. 1 p. 269

Martyn, VI. 5 p. 70-71.

Bancroft, pt. 1 ch. 15 para. 2

Martyn, Vol. 5 p. 340

Bancroft, pt. 1 ch. 15 para. 2

Martyn, Vol. 5 p., 349-350

Ibid. Vol. 5 p. 354

Conresional Documents (USA), serial No. 200.

Ahadi za kurudi kwake Kristo mara ya pilli ili kukamilisha kazi kuu ya ukombozi ndio msingi wa Maandiko matakatifu. Tangu huku Edeni watu waaminifu wa Mungu amekuwa walingoja Kristo aje na kurejesha Paradiso iliyopotea. Enoko, ambaye ni kizazi cha saba, cha wale walioishi Edeni, yeye alitembea na Mungu kwa karne tatu, asema, “Angalia Bwana alikuja na watakatifu wake, elfu, maelfu ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu. Kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake” Yuda 14:15. Ayubu naye katika usiku wa mateso alisema, “Najua ya kuwa Mtetezi wangu yu hai. Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi Nami nitamwona Mungu pasipokuwa na mwili wangu nitamwona, naam nafsi yangu mwenyewe. Na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine” Ayubu 19:25-27. Mtunga zaburi na manabii wamenena juu ya kurudi kwa Kristo hivi: “Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie Mbele za Bwana, kwa maana anakuja, aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa uaminifu wake” Zaburi 96:11-13.

Isaya naye asema, “Katika siku hiyo watasema, Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie. Huyu ndiye Bwana tuliyemngoja, Na tushangilie na kuufurahia wokovu wake” Isaya 25:9.

Mwokozi aliwafariji wanafunzi wake kwa uhakikisho wa kuja kwake, “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi Nakwenda kuwaandalia makao Nikienda Nitakuja tena, niwakaribishe kwangu” “Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wake na malaika watakatifu wote pamoja naye. Ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake, na mataifa yote watakusanyika mbele zake” Yohana 14:2-3; Mathayo 25:31-32.

Malaika walirudia kusema ahadi ya kurudi kwa Kristo wakisema, “Huyu atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni”

Matendo 1:11 Paulo naye alishuhudia kwa kusema “kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu” 1Tes. 4:16. Nabii wa Patmo naye asema, “Tazama yuaja na mawingu na kila jicho litamwona” ufunuo 1:7.

[142] Halafu, ndipo uovu uliowatawala muda mrefu duniani utaangamizwa, “Falme za ulimwengu zimekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na Kristo wake, naye atamiliki milele na milele.” Ufunuo 11:15. “Bwana Mungu ataotesha haki na sifa mbele ya mataifa yote” Isaya 61:11.

Ufalme wa Masihi ambao ni wa amani utasimamishwa. “Maana Bwana atafariji Sayuni, atapafariji mahali pake palipokuwa ukiwa, atafanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, nyika yake kama bustani ya Bwana”. Isaya 51:3.

Kurudi kwake Bwana kumekuwa tumaini la wateule wake nyakati zote. Katika mateso na shida, kuonekana kwa mwokozi wetu na Mungu mkuu, kumekuwa tumaini lenye baraka. Tito 21:13. Paulo akitaja ufufuo utakaotokea wakati wa kuja kwa Bwana, wakati waliokufa katika Kristo watakapofufuliwa na walio hai kunyakuliwa pamoja ili kumlaki Bwana hewani, asema, “Hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele” “kwa hiyo farijianeni kwa maneno hayo”. 1 Thes. 4:17.

Katika kisiwa cha Patmo mwanafunzi mpendwa alisikia ahadi ikisema, “Tazama naja upesi” jawabu lake ambalo ni maombi ya kanisa yasema, “amina, na uje Bwana”. Ufunuo 22:20. Tangu kule magerezani ambako watu wa Mungu walifungwa, na kwenye majiko walikochomea, na kule walikofia waaminifu wa Mungu, sauti zao za imani na tumaini hutujia katika karne zetu. Baada ya kuona hakika ya kuja kwake na ya ufufuo wa wafu, mkristo mmoja alisema, Walikidharau kifo, “wakakutwa wameshinda mauti” “Waldenses walishikilia imani hiyo. Wycliffe, Luther, Calvin, Knox, Ridley na Baxter, wote walikutazia kurudi kwake Bwana katika imani thabiti. Hilo ndilo lilikuwa tumaini la kanisa la siku za mitume, na kanisa la Waldenses na tumaini la Watengenezaji kanisa (Reformers)”

Unabii hauonyeshi jinsi na kusudi kwa kurudi kwa Kristo tu, lakini unaonyesha pia dalili za kuja kwake ambazo kwazo watu watafahamu wakati wa kuja.

“Kutakuwa na ishara katika jua na mwezi na nyota”. Luka 21:25
 “Jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota za mbinguni zitaanguka na nguvu za mbingu zitatikisika. Ndipo hapo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni na nguvu na utukufu mwingi.” Marko 13:24-26. Mwandishi wa ufunuo anaeleza hivi kuhusu dalili ya kwanza ya kurudi kwake Kristo. “Kulikuwa na tetemeko kuu, na jua likawa jeusi kama guni la singa, mwezi wote ukawa kama damu” Ufunuo 6:12

Tetemeko Lililotikisa Ulimwengu

[143]

Katika kutimiza unabii huo kulitokea tetemeko kuu la nchi katika mwaka 1755. Hilo lilizidi matetemeko yote yaliyotangu-
 lia. Linajulikana kama tetemeko la Lisbon. Lilienea ulaya, Afrika na Marekani. Tetemeko hilo lilisikika katika nchi za Greenland, West Indies, Madeira, Norway, Sweden, Uingereza na Ireland. Lilienea katika umbali wa maili za mraba milioni nne. Katika Afrika mtikiso wa ardhi ulikuwa wa nguvu sawa na ule wa Ulaya. Sehemu kubwa ya mji wa Algiers uliharibiwa. Wimbi kuu la maji lilifurikisha mji wa Algiers uliharibiwa. Wimbi kuu la maji lilifurikisha miji ya Hispania na ya Afrika. Milima ya Ureno, ambayo ni mikubwa ilitikishwa kwa nguvu sana hata ikawa kana kwamba inang’olewa, mingine ilipasuka kileleni kwa ajabu. Udongo kutoka milimani ulitiririka na kujaza mabonde. Miali ya moto ilionekana katika milima hiyo.

Katika mji wa Lisbon, ngurumo ya radi ilisikika ndani ya ardhi, baada ya muda kidogo mtetemo wa nguvu sana uliangamiza sehemu kubwa ya mji. Katika tetemeko hilo ambalo lilidumu muda wa dakika sita hivi, watu sitini elfu waliangamia. Bahari kwanza ilikuwa kana kwamba inakupwa, na kuacha nchi kavu, halafu ilirudi kwa nguvu ikigharikisha vitu. Iiinuka juu zaidi ya futi hamsini kuliko kawaida yake. Yalikuwa yamejaa watu wakiabudu. Katika hao na wachache sana waliopona. Hofu na vilio vya watu vilizidi kiasi, hata haielezeki. Maombolezo yalizidi hata inashindikana kuyaeleza. Walikimbia huku na huko katika fadhaa yao na mahangaiko ya kushangaza. Katika shida iyo walikuwa wakilia na kusema kuwa “Mwisho wa ulimwengu umekuja” Akina mama walikimbilia wakilia huku wamewasahau watoto wao, wakizikumbatia sanamu zao

za kusulubishwa kwa Yesu. Wengi walikimbilia makanisani wakitafuta wongofu, lakini ilikuwa kazi bure. Walikimbia madhabahuni, wakikumbatia sanamu zao, lakini wote, mapadri na watu wengine walifunikwa na uangamivu katika tetemeko hilo

Jua Mwezi Kutiwa Giza

[144] Baada ya kupita miaka ishirini na mitano, ilionekana dalili nyingine tena iliyotajwa katika unabii, yaani jua kutiwa giza na mwezi pia. Muda wa kutukia dalili hizo ulitaja na mwokozi katika mazungumzo yake na wanafunzi wake. Alisema, “Lakini siku zile baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake” Marko 13:24. Miaka au siku 1260 ambazo ni za dhiki ile kuu zilimalizika mwaka 1798. Robo karne kabla ya muda huo haujamalizika, mateso yalikuwa karibu kukoma, ila kidogo tu. Kitakachofuata mateso hayo ni jua kutiwa giza. Tarehe 19 mei, 1780, dalili hii ilitimia.

Mtu aliyeshuhudia tukio hilo huko Massachusetts alieleza hivi: “Wingu zito sana lilitanda mbinguni, likifunika mbingu nzima, ila nafasi ndogo pembeni, na ilikuwa giza kama inavyokuwa wakati wa kiangazi saa tatu za usiku. . . . Woga na wasiwasi viliwajaa watu. Wanawake walisimama milangoni mwa nyumba zao wakiangalia nchi katika giza. Wanaume waliokuwa wakifanya kazi katika mabanda ya ufundi walirudisha vyombo vyao. Shule zilifungwa na watoto wakarudi nyumbani katika hali ya hofu na kutetemeka. Wasafiri wakatua na kupiga kambi. Kitu gani kitatukia? Hilo ndilo lilikuwa swali la kila mtu. Ilionekana kwamba tufani kuu ilikuwa karibu kuvamia nchi, au jambo la uangamivu lingetokea na kuangamiza vitu vyote.”

Mishumaa iliwashwa kana kwamba ni usiku wa giza pasipokuwa na mbalamwezi. Kuku waliingia kulala kama kawaida. Ng’ombe wakakusanywa na kulia, vyura wakalia, ndege wakaimba nyimbo za jioni, na popo wakaruka ruka kama wafanyavyo. Lakini watu walijua kuwa usiku bado haujaja.

Watu walikusanyika mahali mahali. Mahubiri ya haraka haraka yasiyoandaliwa yakasomwa na kutaja mafungu yanayokubaliana na tukio hilo katika unabii. Giza lilizidi zaidi baada ya saa tano asubuhi.

Mahali pengi nchini giza lilikuwa kubwa kiasi ambacho walishindwa kuona chochote bila mwanga wa mishumaa.

Mwezi Kama Damu

Wala giza la usiku lilikuwa silo la kawaida, na la kutisha kama la mchana. Walakini lilikuwa mbalamwezi pevu bila kitu cha kuiziba. Lakini weusi uliukuwa mzito, ambao kama mwanga wa mshumaa au taa, ukionekana katika nyumba za jirani au mahali pengine mbali kidogo, ilionekana kama giza la Misri lisilopenyeka kwa nuru. Kama kila mtu angekuwa amefunikwa na kitu kisichopenyeka kwa nuru, hata hivyo giza lisingekamilika kwa jinsi lilivyokuwa kubwa. Baada ya usiku wa manane giza lilitoweka, na mwezi mara ya kwanza ukaonekana kama damu.

[145]

Mei 19, 1780 unajulikana kihistoria kama, “Siku ya Giza” Tangu wakati wa Musa hakuna giza lililolinganishwa na hilo lililotokea. Maelezo ya shahidi aliyeshuhudia giza hilo ni mwangwi wa yale yaliyomo katika Yoeli yaliyoandikwa zamani za miaka 250 kabla nayo husema “Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo” Yoel 2:31.

Kristo alisema, “Basi haya yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia Wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu. Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yaanzapo kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu”. Luka 21:28, 30-31.

Lakini upendo wa Kristo na imani ya kuja kwake vimepoa kanisani. Watu wa Mungu walikuwa vipofu, wasizitambue dalili za kuja kwake, wala mafundisho ya Mwokozi kuhusu dalili hizo. Fundisho la kurudi kake Yesu halikujaliwa, mpaka baadaye likasahauliwa, hasa huko Marekani. Shughuli za uchumi na kutafuta mafanikio heshima zimewasahaulisha watu wasielewe kuwa mambo ya sasa yatapita.

Mwokozi alitaja hali ya uasi itakayoonekana duniani kabla ya kuja kwake mara ya pili. Kwa watu wale wanaoishi wakati huu, Kristo anawaonya akisema “Basi jiangalieni mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafla, kama mtego unasavyo”. “Basi, kesheni ninyi kila

wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayo-otokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu” Luka 21: 34,36. Ilikuwako haja ya lazima ya kuwaamsha watu wajiandae kukabili mambo yanayoambatana na kufungwa kwa muda wa rehema

[146] “Kwa kuwa siku ya Bwana ni kuu, yenye kitisho sana naye ni nani awezaye kusimama?” Nani atasimama mbele yake Mwenye “Macho safi” yasiyotazama ukaidi na uovu? “Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake, na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao; nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi, nami nitayaangusha chini majivuno yao makali” “Falme yao wala adhabu zao havitaweza kuwaokoa” “Na huo utajiri wao utakuwa mateka na yumba zao zitakuwa ukiwa” Yoel 2:11; habakuki 1:13; Isaya 13:11; Sefania 1:18;13.

Mwito Wa Kuamka

Kuhusu siku hiyo kuu, neno la Mungu huwaita watu wake ili wautafute uso wake kwa njia ya toba hivi: “Kwa maana siku ya Bwana inakuja kwa sababu inakaribia”. “Takaseni sanamu, kusanyeni kusanyiko kuu. Kusanyeni watu, likataseni kusanyiko, kusanyeni wazee, kusanyeni watoto... Hao makuhani wahudumu wa Bwana, na walie kati ya patakatifu na madhabahu na waseme, Nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga na kwa kulia, na kwa kuomboleza.” “Rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, makamrudie Bwana, Mungu wenu, kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema naye hughairi mabaya” Yoel 2:1, 15-17, 12-13.

Kazi kuu ya matengenezo yaani kuwatayarisha watu ili kukutana na Mungu, budi ikamilishwe. Kwa rehema zake Mungu alikuwa tayari kuwatumia watu wake ujumbe wa Mungu alikuwa tayari kuwatumia watu wake ujumbe kuwaamsha ili wajitayarisha kwa kurudi kwake Yesu.

Ujumbe huu umo katika Ufunuo 14; Hapa ndipo ujumbe wa sehemu tatu, unaowakilishwa kana kwamba ni tangazo linalotolewa na viumbe wa mbinguni warukao, ambalo hufuatiwa mara moja na kuja kwa Mwana wa Adamu ili avune mavuno ya nchi. Nabii aliona malaika akiruka katikati ya mbingu akiwa na Injili ya milele

itakayohubiriwa kwa watu wote wakaao duniani, watu wa kila taifa na kabila na lugha na jamaa, ikisema kwa sauti kuu, “Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake inakuja. Msujudieni yeye aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na chemichemi za maji.” Ufunuo 14:6-7.

Ujumbe huu ni sehemu ya “Injili ya Milele”. Kazi ya kuhubiri ujumbe huu imekabidhiwa kwa wanadamu. Malaika watakatifu huongoza, walakini utangazaji hasa wa ujumbe ni wa watumishi wa Mungu waliomo duniani, watu waaaminifu, wanaofuata maongozi ya roho wa Mungu na kufuata mafundisho ya neno lake, ndiyo wanaohusika na utangazaji wa ujumbe huu. Wamekuwa wakitafuta maarifa ya Mungu, “wakiyahesabu kuwa ya thamani kuliko fedha na dhahabu. Siri ya Bwana iko kwao wamchao, naye atawaonyesha agano lake” Mithali 3:14; Zaburi 25:14.

[147]

Ujumbe Ulitolewa na Wanyenyekevu

Kama Wasomi na wataalamu, wachunguzi wa maandiko, wangelikuwa waaminifu na wacha Mungu, ambao wanasoma Biblia kwa roho ya maombi na unyenyekevu wa kweli, wangelifahamu wakati. Unabii ungeeleweka kwao, na mambo yaliyotabiriwa kuwa yatatokea yasingaliwakuta gizani. Lakini basi ujumbe haukutolewa na wasomi hao, bali ulitolewa na watu duni, wanyenyekevu tu. Wale walipuuza kushikilia nuru iliyokuwa karibu nao, waliachwa gizani. Lakini Mwokozi alisema “Anifuataye mimi hatakwenda gizani, bali atakuwa na nuru ya uzima” Yohana 8:12. Mtu wa aina hiyo nuru ya mbinguni itamwongoza kwenye kweli yote.

Wakati Kristo alipokuja mara ya kwanza kuzaliwa makuhani waandishi waliokuwa katika mji mtakatifu ingelipasa wafahamu ishara na kutangaza kuzaliwa kwake. Mika alitaja mahali atakapozaliwa, Daniel naye akataja wakati atakapozaliwa. Mika 5:2; Daniel 9:25. Waongozi wa Kiyahudi hawakuwa na udhuru wo wote, kwa kutojua kwao.

Wazee wa Israeli, kama wangelitia nia kusoma unabii wangukuwa mahali, na wakati wa kuzaliwa kwa Kristo, ambako lilikuwa tukio kuu ulimwenguni; kuja kwa Mwana wa Mungu ulimwenguni. Lakini katika mji wa Bethlehemu wasafiri wawili waliochoka sana kutoka Nazareth walikuwa wakipitia kinjia mahali

pa kulala usiku. Hakuna nyumba iliyokuwa tayari kuwakaribisha. Mwisho wakaingia katika kibanda kibovu cha ng'ombe, na mle ndimo Mwokozi wa ulimwengu alimozaliwa.

Malaika waliagizwa kuwapasha habari watu waliokuwa tayari kuzipokea, na kuzipitisha kwa wengine. Kristo amejishusha kabisa ili atwae haki ya asili ya binadamu, na maafa yao mpaka atoe nafsi yake iwe kafara ya dhambi. Hata hivyo malaika walitamani kuwa, ingawa amejishusha kiasi hicho, Mwana wake Mungu aliye juu, heri aonekane kwa watu wengine heshima na fahari inayofanana na hadhi yake.

Je, wakuu wa Israeli, watakusanyika Yerusalemu ili kumsalimu? Je, malaika watamjulishwa kwao?

[148]

Malaika alikuja duniani ili kuona kuwa ni watu wangapi waliokuwa tayari kumkaribisha Yesu. Lakini hakisikia sauti yoyote ya kumshangilia Masihi. Malaika aliruka juu ya mji mteule wa Yerusalemu na hekalu tukufu ambapo upendeleo wa mbinguni umekuwa kwa miaka mingi, lakini hata hapo mambo yalikuwa yale yale ya kutoamini. Makuhani waliendelea kutoa dhabihu ambazo ni najisi juu ya madhabahu najisi. Mafarisayo waliendelea kupaza sauti zao kwa majivuno wakisali popote walipopenda, mabarabarani. Wafalme wenye elimu, waalimu wote hao hawakushughulika na habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi.

Mjumbe wa mbinguni alikuwa karibu kurudi mbingu kwa mshangao mkuu, ndipo alipogundua kundi la wachungaji wakilinda kondoo zao. Walipokuwa wakiangalia nyota huko mbinguni, walikumbuka unabii unaohusu kuzaliwa kwa Mwokozi, nao wakatamani sana utimizo wa unabii huo. Kumbe, hapa liko kundi la watu walio tayari kupokea habari za mbinguni. Ghafila, utukufu wa mbinguni ukaangaza uwanda mzima. Malaika wengi sana wasiohesabika wakatokea, kana kwamba malaika mmoja asingetosha kuleta habari hiyo, kwa kuwa nyingi mno; Sauti za waliokombolewa wa mataifa yote, zikisema “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na dunia yote iwe amani, kwa watu waliowaridhia” Luka 2:14.

Lo, hili ni fundisho gani la hadithi ya ajabu ya Bethlehemu! Hadithi hii inatuaibishaje? Inatufanyaje tuwe tayari, tusije tukashindwa kutambua dalili za wakati wa majilio.

Malaika hawakukuta watu alio tayari kwa wachungaji peke yao, la. Katika nchi ya watu wa mataifa pia kulikuwa na wakashaji. Ma-

majusi wa Mashariki, watu waheshimiwa na matajiri. Wenye elimu wa Mashariki walikuwako. Walijifunza kutoka katika maandiko ya Waebrania juu ya Nyota itakayotoka kwa Yakobo. Basi walingoja kwa hamu sana, yule atakayekufa Mariji, sio wa Israeli pekee, bali na watu wote wa ulimwengu mzima. “Nuru ya kuwaangazia mataifa, na wokovu mpaka mwisho wa nchi” Luka 2:25, 32; Matendo 13:47. Nyota ya mbinguni iliwaongoza Mamajusi, ambao ni wageni mpaka mahali alipozaliwa mfalme.

Kristo atatokea kwa wale wanaomtazamia kwa wokovu. Waebrania 9:28. Kama habari za kuzaliwa Kristo, zilivyokuwa, zikiwafikia watu wa hali ya kawaida, ujumbe wa kurudi kwake umekabidhiwa kwa watu wa hali ya kawaida, sio kwa wataalamu, wala waalimu wa makanisa ya Kikristo ya dunia. Wao wameikataa nuru ya mbinguni, kwa hiyo hawamo katika hesabu inayosemwa na Paulo: “Bali ninyi, ndugu hamno gizani mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza”. 1Tes. 5:4-5.

[149]

Walenzi juu ya kuta za Sayuni wangekuwa wa kwanza kupata habari za kurudi kwa Mwokozi, na kuzitangaza. Lakini wanajikalia tu, wakati watu wanafia dhambini. Yesu aliona kanisa lake likiwa kama mti usiozaa, lakini wenye majani tele. Roho ya unyenyekevu na uchaji wa imani ya kweli imepungua sana. Kilichoko ni kiburi, ubinafsi, mfano wa utawa na unafiki. Kanisa asi limefumba macho halizioni dalili. Wamejitenga na Mungu na upendo wake. Kwa jinsi wasivyohusiana na ahadi zake hazitimii kwao.

Wafuasi wengi wa Kristo wanaikana nuru ya mbinguni. Sawa na Wayahudi wa kale hawatambui dalili za majilio yao. Bwana aliwaacha, akawafunulia waliokuwa wakikeshwa kama Wachungaji wa Bethlehemu, na Mamajusi wa Mashariki.

Marejeo:

Tazama Daniel T. Taylor, *Te Reign of Christ on Earth or the Voice of the Church in all Ages* p. 33

Sir, Charles Lyell — *Principles of Geology* p. 495

Encyclopedia American Art “Lisbon” (ed. 1831)

The Assex Antiquarian, April 1899 Vol. 3 No. 4 p. 53-54.

William Gordon, *History of the Rise* — *Progress* Vol. 3 p. 57.

Isaiah Thomas, *Massachusetts. Spy or American Oracle of Liberty* Vol. 10, No. 472 (May 1780)

Letter by Dr. Samuel Tenney of Exeter New Hampshire, Collection 1792 (1st Series Vol. 1 p. 97).

18/Nuru Mpya Katika Ulimwengu Mpya.

[150]

Mkulima mmoja mtawa, mwaminifu na mtafutaji wa ukweli, ndiye aliyeteuliwa na Mungu ili kukiongoza kikundi cha watu waliokutangaza kurudi kwake Yesu mara ya pili. William Miller aliishi maisha ya kimaskini, na ya kujikana kama watengenezaji wengine walivyoishi maisha ya kujinyima.

Miller alijionyesha kuwa hodari na mwelekevu tangu utoto wake. Alivyoendelea kukua mawazo yake yalipanuka na kuendelea, naye alikuwa na kiu ya kupata elimu Upendo wake wa kujifunza, na nia yake thabiti, vilimsaidia kuwa mtu mwenye kufaa sana. Alikuwa na tabia njema na nyofu naye aliheshimiwa sana. Alijipatia cheo kikuu katika kazi zake za kiraia na za kijeshi pia. Kwa hiyo utajiri na heshima vilikuwa wazi kwake.

Alipokuwa mtoto alivutiwa sana na mambo ya dini. Walakini alipokuwa mtu mzima alijikuta akiwa katika watu wanaoamini kuwa Mungu yuko aliyeumba vitu, lakini hana uwezo wa kuvitawala vitu hivo, ila kila kitu hujiendesha chenyewe kama kitakiwavyo. Watu hawa walimvutia sana, maana walikuwa watu wema, waungwana, wenye hali ya utawa. Miller alivutiwa na hali yao. Tabia yao ili-wapatia sifa iliyotokana na Biblia, hata hivyo vipawa hivyo vyema viliharibiwa na kutoa mvuto wao katika Neno la Mungu.

Sasa walivyoitafsiri Biblia kulileta tatizo kwake ambalo lilikuwa gumu sana. Lakini imani yake, isiyofuata kama Biblia inavyosema, haikumfaidia lolote, kama hakuridhika. Alipokuwa na umri wa miaka thelathini na minne roho Mtakatifu akimwangazia moyoni, akajiona kuwa yu mwenye dhambi. Hakuwa na uhakika wa maisha ya baadaye baada ya kufa. Kwa hiyo aliona giza tu kwa maisha ya mbele. Akajisemea moyoni hivi:

“Mbingu ilikuwa ngumu juu ya kichwa changu, na nchi ilikwa kama chuma chini ya miguu yangu Kadiri nilivyofikiri, ndi- vyo mawazo yalivyotawanyika. Nilijaribu kujizuia nisiwaze, lakini sikuweza. Kwa kweli nilikata tamaa, kwa vile nilivyosindwa. Lakini

[151]

sikuelewa sababu ya hali hiyo. Nililalamika na kugugumia, lakini kasoro gani, nami sikujua namna ya akuiondoa”.

Miller Apata Rafiki

Miller asema, “Kwa ghafla tabia ya mwokozi ikajidhihirisha katika moyo wangu na katika nia yangu. Ilionekana kwamba, kulikuwa na wema wa huruma kwake, kiasi cha kumsukuma ajitoe kwa ajili yetu ili tuokoke na adhabu ya dhambi. Sasa swali ni kuwa, Inathibitikaje kuwa mtu wa namna hiyo yuko? Bila kupata habari hizo katika Biblia, hakuna pengine pa kuthibitishia. Mwokozi wa aina hiyo aelezeki kwingineko, ila katika Biblia.”

Nikaona kuwa Biblia ndiyo inatoa maelezo dhahiri kuhusu kitabu ambacho hakikuandikwa kwa uongozi wa Mungu kinawezaje kuonyesha njia sahihi kwa ajili ya walimwengu walioanguka dhambini. Ni lazima Biblia kiwe ndicho kitabu cha Mungu. Basi Biblia kikawa ndicho kitu nilichokipenda na katika Yesu nikapata starehe kamili. Ndiye rafiki wa kweli. Basi Yesu akawa ndiye mpenzi wangu, miongoni mwa elfu kumi. Biblia ambayo kabla ya hapo ilikuwa giza sasa ikaniwia taa ya miguu yangu. Nikaona kuwa Mungu ndiye mwamba katika mawimbi ya maisha. Biblia ikiwa ndilo somo langu. Nikashangaa kwa kutoona thamani yake hao mwanzoni. Sikupenda kusoma kitabu kingine, na kupata hekima ya Mungu katika Biblia.

Miller akaiungama imani yake dhahiri. Lakini wakafiri ambao walikuwa wenzake walimbishia yote aliyokuwa anawaeleza sana. Akaazimu kujifunza na kuhakikisha kuwa sehemu zile alizodhani kuwa hazikubaliani, sivyo ilivyo.

[152] Akitumia Commentary, alichunguza fungu kwa fungu na kulinganisha fungu na fungu, na kutumia vitabu vingine, kama Concordance akaanzia tangu Mwanzo, akisoma fungu kwa fungu na kulinganisha, alipoona kuwa hakuna mafarakano, basi alikaza mafundisho yake kwa ukamilifu, akilinganisha fungu na fungu. Ndipo akaona yale Daudi aliyoonna katika Zaburi 119:130: “Kufafanusha maneno yako kwatia nuru na kumfahamisha mjinga”.

Kwa juhudi nyingi, huku akifurahiwa sana, Miller alijifunza unabii wa Daniel na Ufunuo na kuona kuwa mifano, iliyotumiwa katika vitabu hivyo inaweza kufahamika, ingawa ni ya unabii. Akaona

kwamba inaweza kujieleza na kufahamika, au kuelezwa na mafungu mengine. Juhudi yake ikampatia ujuzi halisi. Akafuatia unabii hatua kwa hatua, Malaika wa mbinguni walikuwa wakimwongoza.

Alitosheka kuwa, mawazo ya watu juu ya miaka elfu ya muda kabla mwisho wa dunia, hayaungwi mkono na Neno la Mungu. Mawazo haya yanayosema kuwa kutakuwa na muda wa starehe ya miaka elfu kabla Kristo hajaja, ni kinyume cha mafundisho ya Kristo na mitume wake, ambayo husema, ngano na magugu yatakuwa pamoja mpaka wakati wa mwisho, na kwamba waovu watazidi kuwa waovu tu. 2Timotheo 3:13.

Kuja Kwa Kristo Waziwazi

Mafundisho yasemayo kuwa ulimwengu mzima utaongoka, na kuwa ufalme wa kristo ni wa kiroho, hayakufundishwa na kanisa la mitume. Hayakukubaliwa na kanisa mpaka katika karne ya kumi na nane. Mafundisho hayo yaliwaelekeza watu kukutazamia kurudi kwa Kristo mbele sana, na ya kuwa dalili hizi zilizotajwa hazina maana. Kwa hiyo watu hawakujiandaa kwa kurudi kwake.

Miller aligundua kuwa Kristo atakuja waziwazi, wala sio kiroho. Ndivyo Maandiko Matakatifu yasemavyo, “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni, pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu...” Nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni, pamoja na nguvu na utukufu mwingi “Kwa maana kama hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu” “Atakapokuja mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake” 1Thes. 4:16-17; Mathayo 25:31; 24:31.

Wakati wa kuja kwake watakatifu waliokufa watafufuliwa, na wenye haki walio hai watabadilishwa. “Hatutalala sote, lakini wote tutabadilishwa kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda Italia na watu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, na sisi tutabadilika. Maana huu wa kuharibika sharti uvae kutokuharibika, na huu wa kufa sharti uvae kutokufa. Wafu katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao mawinguni ili kumlaki Bwana hewani, na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.” 1Kor. 15:51-53; 1Thes. 4:16-17.

[153]

Mtu katika hali aliyo nayo sasa, ni ya kufa na kuharibika. Kwa hiyo mtu katika hali aliyo nayo sasa hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Yesu ajapo ataondoa hali ya uharibifu kwa watu wake, kisha atawaita kuingia katika urithi wa ufalme wake, ambao wanakuwa warithi.

Maandiko na utaratibu wa Kuhesabu

Maandiko hayo yanayohusu hesabu za mambo mbalimbali yalimthibitishia Miller kuwa utawala wa ulimwengu wa amani na kusimamishwa kwa ufalme wa Mungu duniani vyote vilikuwa vya baadaye, wakati wa kurudi kwa Yesu. Zaidi ya hayo, hali ya ulimwengu, kama unabii unavyoeleza kuhusu siku za mwisho, alikubali kuwa katika hali hii kwa wakati huu ilionyesha kuwa mwisho wake unakaribia.

Alisema hivi: “Ushahidi mwingine mkubwa ulioniingia mawazoni ni ule wa namna ya kuhesbu mambo mbalimbali Niliona kuwa mambo yaliyotabiriwa yaliyotimilika wakati uliopita, yalikuwa yakitajwa wakati wake, na kutimia jinsi hiyo bila kukosa.

Alipokuta mambo mbalimbali yanaendelea kutajwa mpaka kurudi kwake Kristo, hakuweza kuona namna nyingine, ila tu mambo ambayo yamepangwa kabla ya wakati wake, ambayo Mungu aliwafunulia watumishi wake. Mambo ambayo yanatuhusu sisi na watoto wetu milele. Hakuna kitu ila Mungu amewafunulia watumishi wake, mambo ambayo yanatuhusu sisi na watoto wetu milele. Hakuna kitu kingine ila Mungu amewafunulia watumishi wake siri yake” Kumbukumbu 29:29; Amosi 3:7. Wanafunzi wa neno la [154] Mungu watatazamia kuona matukio mengi sana kuhusu historia ya wanadamu yamepangwa katika Maandiko Matakatifu.

Miller alisema, Niliamini na kuthibitisha kuwa, “Kila andiko lenye pumzi ya Mungu linafaa... kwamba watu watakatifu waliandika wakiongozwa na roho wa Mungu nayo yaliandikwa ili kutufundisha sisi, ili kwa saburi na faraja ya maandiko, tuwe na tumaini... kwa hiyo najisikia kuwa katika juhudi ya kufahamu kile Mungu alichotaka kutufahamisha kwa rehema zake, sina budi kukizingatia kwa kufuata jinsi unabii uanavyoelekeza.”

Unabii ulioelekea kufunua zaidi wakati wa kurudi kwake Kristo ulikuwa ule wa Danieli 8:14, unaosema, “Hata nyakati za jioni na

asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakasika” Miller aliacha Biblia ijitafsirri yenyewe, kwa hiyo alijifunza mfano wa unabii unaotaja mwaka kama siku na siku kama mwaka. Aliona kuwa siku za unabii 2300, ambazo ni sawa na miaka 2300 zitaendelea mpaka kuzidi muda waliopewa Wayahudi, kwa hiyo zisingeweza kuhusu patakatifu.

Miller alikubaliana na imani ya wakristo ya kuamini kuwa nchi ndiyo “hema takatifu” kwa hiyo alifahamu kuwa kutakaswa kwa patakatifu kunahusu nchi hii, ambako kunatajwa katika Danieli 8:14. Hivi moto wa mwisho ungetakasa dunia. Akaona kuwa kama mwanzo wa siku 2300 ukiwa sawa, basi siku ya kurudi kwake Yesu ingejulikana.

Kugundua Musa wa Unabii.

Miller aliendelea kuuchunguza unabii usiku na mchana, akichunguza jambo hili kubwa. Katika Daniel 8 Miller hakuweza kugundua mwanzo wa siku au miaka 2300, ingawa malaika Gabriel aliamuriwa amwelimishe Danieli, alimweleza sehemu tu. Wakati mateso ya kutisha yalipofunuliwa kwa nabii kwa njia ya njozi, hakuweza kustahimili tena, maana mateso hayo yatakayolipata kanisa yalikuwa ya kutisha kabisa. Danieli alizimia, akaugua siku kadhaa wa kadhaa. Anasema, “Nami naliyastaajabia yale maono, ila hakuna aliyefahamu” Daniel 8:27. Walakini Mungu alikuwa amemwagiza mtumishi wake, “Mjulishe njozi” Basi malaika alirudi ili kumjulisha. Alisema “Basi sasa nimekuja kukufahamisha Kwa hiyo fahamu na kuitafakari njozi” Jambo moja la maana katika Danieli nane limeachwa, halikufafanuliwa, yaani siku 2300. Kwa hiyo malaika alianzia maelezo yake akielekeza katika wakati. Alisema, “Majuma sabini yameamuriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu Basi ujue na kufahamu ya kuwa, tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye mkuu, kutakuwa na majuma saba, na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam katika nyakati za taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja, na kwa nusu

ya juma hilo ataikomesha sadaka ya dhabihu.” Daniel 8:16; 9:22-23; 24-27.

[155] Malaika alikuwa ametumwa kwa Danieli ili kumweleza jambo hilo, ambalo hakulieleweshwa, nalo ni “Hata elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakasika” Maneno ya kwanza ya malaika ni haya: “Majuma sabini yameamuriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu”. Majuma sabini, ambayo ni siku au miaka 490 iliyoamriwa kwa Wayahudi lazima iondolewe katika jumla ya miaka 2300.

Nyakati Mbili Kuanza Pamoja

Lakini ni nini kilikatwa? Kwa kuwa siku 2300 ndicho kitu kimetajwa kama muda wa unabii katika sura ya 8 ya Danieli, hivyo basi majuma sabini ni sehemu ya 2300. Vipande viwili basi huanzia wakati mmoja majuma sabini kuanzia pale amri ya kujenga Yerusalemu tena ilipotolewa. Ikiwa mwanzo wa kutolewa amri hiyo ukipatikana, ndipo mwanzo wa 2300 utathibitika.

Katika Ezra saba amri hiyo inapatikana, iliyotolewa na mfalme Artastasta mwaka B.C. 457. yeye ni mfalme wa Persia. Wafalme watatu walioanza kuamuru na kukamilisha amri hiyo, hutimiliza, kama unabii usemavyo, mwanzo wa siku au miaka 2300. Tukichukua mwaka 457 wakati amri hiyo, ilipotekelezwa kama ndiyo amri ya kuujenga mji, kila kitu kilichosemwa katika majuma sabini kilitimia bila makosa.

[156] Tangu kuwekwa amri ya “kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye mkuu, kulikuwa na majuma saba, na katika majuma sitini na mawili” Majuma sitini na tisa au miaka 483. Amri ya Artashasta ilitolea mwaka B.C 457 na kutimizwa. Toka mwaka huo aliendelea mpaka A.D 27, ndipo Kristo alipobatizwa na Yohana Mbatizaji na kutiwa mafuta kwa njia ya roho. Baada ya ubatizo wake akaenda Galilaya, akihubiri ufalme wa Mungu na kusema, “Wakati umetimia” Marko 1:14-15.

Injili kwa Ulimwengu

“Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja” — Miaka saba ya mwisho wa wakati huo ilitolewa kwa ajili

ya taifa la Wayahudi. Wakati huo wote, tangu 27 AD mpaka 34 AD Kristo na wanafunzi wake walieneza Injili kwa Wayahudi tu. Agizo la Kristo lilikuwa “Msiende kwenye njia ya mataifa, wala katika miji ya Samaria. Lakini nendeni kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli”. Mathayo 10:5-6.

“Na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka ya dhabihu” Katika AD 31, miaka mitatu na nusu baada ya kubatizwa kwake, Bwana wetu alisulubishwa. Dhabihu kuu iliyotolewa huko Kalwari dhabihu za wanyama zilikoma. Huduma zote zilizokuwa kivuli zilikwisha.

Miaka 490 iliyotolewa kwa ajili ya Wayahudi ilimalizika katika A.D 34. Wakati huo kitendo cha bunge kuu la Kiyahudi cha kuamua kumwua Stefano kilifunga na kutiwa muhuri kanusho lao, kwamba hawana haja na Injili tena, nao wakaanza kuwatesa wafuasi wa Kristo na kuwaua. Hapo sasa Injili ya wokovu ikapelekwa kwa watu wa mataifa, katika ulimwengu wote. Wanafunzi waliolazimika kukimbia mateso kutoka Yerusalemu, “wakaendea huko na huko kila mahali wakilibiri lile neno” matendo 8:4.

Hivyo basi unabii ulitimizwa hatua kwa hatua kama ilivyopangwa. Mwanzo wa majuma sabini miaka 490 ni wa hakika hakuna shaka ni B.C 457, na mwisho wake ni A.D. 34. kwa kuwa majuma sabini yamekatwa katika 2300 kilichobaki ni miaka 1810. Baada ya kumalizika miaka 490 ile 1810 iliyobaki lazima nayo itimilike. Kutoka A.D. 34 miaka 1810 lazima iendelee mpaka 1844. Kwa hiyo siku au miaka 2300 ya unabii wa Danieli 8:14 zitakwisha katika 1844. Mwisho wa unabii huu mrefu, “ndipo patakatifu patakapotakasika”.

Kwa hiyo wakati wa kutakaswa patakatifu unaaminia pote kuwa kutatokea wakati wa kurudi kwake Yesu.

Mwisho wa Kushangaza

[157]

Mwanzoni mwa mafunzo ya Miller juu ya unabii huu hakutazamia hata kidogo kufikia hatua aliyofikia sasa. Hata yeye mwenyewe hakuelewa ugunduzi huo jinsi ulivyotokea. Lakini ushahidi wa Biblia ulikuwa dhahiri, kama ukweli usingelipuuzwa.

Katika mwaka 1818 alifikia uamuzi katika uchaguzi wake kuwa Kristo atarudi kuwachukua watu wake, katika muda wa miaka

ishirini na mitano ijayo. Miller alisema, “Sina haja kutaja furaha iliyojaa moyoni mwangu kwa ajili ya tazamio hilo la fahari, wala kutaja hamu ya tunu niliyonayo kuhusu kushiriki furaha ya ukombozi Lo, huonekana kufurahisha kiasi gani!”

Swali lilinjia kuhusu wajibu wangu kwa ulimwengu, juu ya haya niliyogundua katika uchunguzi wangu. Hakuona vingine, ila tu wajibu wake kuwafunulia wengine yale aliyogundua. Alitazamia upinzani kutoka kwa watu wasioamini, lakini ajitulize kwamba wakristo wote watafurahi katika tumaini la kukutana na mwokozi. Alisita kutoa habari hizo za furaha, isiwe amekosea kuchunguza, na kuwakosesha wengine. Kwa hiyo alichunguza kwa uangalifu sana kila neno lenye shaka. Miaka mitano ilitumika katika upelelezi huu na kujisahihisha.

“Nenda Uyangaze Ulimwenguni”

Asema, “Nilipokuwa nikifanya kazi, masikioni mwangu neno liliendelea kusikika likisema, ‘Nenda ukautangazie ulimwengu hatari inayoujilia’ Fungu hili lilinjia kila mara kusema: ‘Nimwambiapo mtu mwovu, Ee, mwovu, hakika utakufa katika uovu wako; kama wewe husemi na kumwonya mwovu huyo aache njia zake mbaya, hakika atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka katika mkono wako’ Niliona kuwa kama waovu wakionywa hakika, wengi wao watatubu; na kama hawakuonywa damu yao itadaiwa mkononi mwangu maneno haya yaliendelea kugoga katika dhamiri yake daima, yakisema, ‘Nenda, ukayangaze ulimwenguni’ na damu yako nitaitaka mkononi mwako” Miller alingoja muda wa miaka tisa, huku mzigo wa nia hiyo ukizidi kumkandamiza, mpaka katika mwaka 1831 ndipo kwa mara ya kwanza akajitokeza kueleza maana ya imani yake.

[158] Wakati huo alikuwa na umri wa miaka hamsini, ingawa hakuzoea kuhubiri mbele ya watu, lakini alifaulu. Hotuba yake ya kwanza iliwaamsha watu kidini. Familia kumi na tatu kasoro watu wawili, ziliongoka. Watu walichangamka sana kiroho, wakapata uvuvio mpya. Wakafiri na wenye mizaha wakauamini ukweli wa Biblia. Alihubiri huku na huko na kila mahali wenye dhambi walitubu. Mahubiri yake yaliwaamsha watu kiroho, na kukemea hali ya ulimwengu na ufedhuli vilivyokuwa vikihangaisha kizazi.

Mahali pengi makanisa ya kiprotestanti ya madhehebu yote yalimsikiliza na kuamini, na miito ilikuja hasa kutoka kwa Wachungaji. Haikuwa kawaida yake kuhubiri mahali asipoitwa, hata hivyo miito ilikuwa mingi kiasi ambacho hakuweza kuitimiza yote. Watu wengi walithibitika na kuamini kuwa Kristo yu karibu kurudi, na haja yao kujiweka tayari. Katika miji mingi wenye maduka ya kuuza vileo waliyageuza maduka yao kuwa sebule za mikutano ya dini. Wacheza kamari waliacha; makafiri na wafedhuli mno waligeuka, kila mtu akafanya matengenezo ya dini. Mikutano ya ibada ilifanyika, na kuendeshwa karibu kila saa na madhehebu yote, hata wenye biashara walikuwa wakikutana kwa ibada na maombi. Hapakuwapo na msisimko wa ovyo ovyo. Kazi yake ilifanana na ile ya watengenezaji, yaani kuwafikisha watu wala sio kuwasisimua tu.

Katika mwaka 1833 Miller alipata hati ya kuhubiri kutoka katika kanisa la Baptist. Wachungaji wengi wa kanisa walikubaliana na mafundisho yake. Alisafiri akihubiri bila kukoma na wala hakuwa na fedha za kutosha kujibu miito yote. Kazi hiyo ilimgharimia fedha nyingi zake binafsi.

Nyota Zaanguka

Katika mwaka 1833 dalili ya mwisho iliyosemwa na Mwokozi kuwa ni ishara ya kuja kwake, ilionekana. “Nyota zitaanguka kutoka mbinguni”. Na Yohana katika ufunuo husema, “Na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi”. Mathayo 24:29; ufunuo 6:13.

Unabii huu ulitimizwa kabisa katika maanguko ya nyota ya [159] November 13, 1833, ambayo ni ya ajabu kabisa yasiyopata kutokea kabla ya hapo. Mvua haijanyesha kamwe kwa wingi nchni kama zilivyoanguka nyota hizo. Pande zote, mashariki, magharibi, kaskazini na kusini hali ilikuwa ile ile. Kwa kifupi ni kwamba mbingu ilionekana kana kwamba inatikusika Tangu saa mbili asubuhi mpaka mchana mmemetuko na yota zilivyokuwa zikian-guka.

Ilionekana kana kwamba nyota zimekusanyika mahali pamoja, na sasa zinaanguka kwa kumetameta kwa mng’aro mkubwa, kutoka pande zote. Zilionekana kufuatana kwa maelfu kwa mfano wa mitini upukutishavyo mapoozo yake.

Katika gazeti la New York ilionekana habari ndefu iliyoandikwa kuhusu tukio hilo, ikisema, “Hakuna mtaalamu yoyote aliyeweza kuandika usahihi wa tukio hilo. Nabii aliyetabiri tukio hilo miaka 1800 iliyopita ndiye alisema kwa usahihi anguko la nyota. Hivyo ndiyo dalili ya mwisho ya kuja kwa Kristo ilivyotokea, ambaye Yesu aliwaambia wanafunzi wake akisema ‘Ninyi myaonapo hayo yote, fahamuni kuwa yu karibu tena milangoni’ Mathayo 24:33. Wengi walioshuhudia kuanguka kwa nyota walikuhesabu kuwa tangazo la kuja kwa hukumu ya Mungu.”

Katika mwaka 1840 jambo jingine la unabii lilitukia likishangaza watu. Miaka miwili kabla, Josia Litch alitangaza, na kueleza habari ya ufunuo 9 ikitabiri anguko la dola ya Ottoman katika mwaka 1840, katika mwezi wa Agosti. Aliandika siku chache mbele akisema, “Itaanguka katika Agosti 11, 1840, wakati uwezo wa Ottoman utakapoangamia katika Constantinople”

Utabiri Ulitimia

[160] Wakati ule uliotabiriwa, Uturuki ilikubali kuwa katika ulinzi wa utawala wa Ulaya ambao ni wa mataifa ya Kikristo, kwa njia hii Uturuki ikajiweka chini ya mataifa ya Kikristo. Jambo hili likatimiza utabiri uliotabiriwa bila kukosea. Watu walikubali kanuni ya tafsiri ya Miller kuhusu unabii. Wenye elimu na cheo walijiunga na Miller katika kazi ya kuhubiri na kuchapisha vitabu, vinavyoeleza maoni yake. Tangu mwaka 1840 mpaka 1844 kazi iliendelea kwa upesi sana.

William Miller alikuwa mwenye uwezo mwingi wa akili na kuongezea hekima ya mbinguni kwa njia ya kujiunga na mtoa hekima wa mbinguni. Aliheshimiwa na wote, na tabia yake ya Kikristo ilipendwa na wote. Alijaribu maneno yote ya dini kwa kuyalinganishwa na neno la Mungu.

Hata hivyo ujumbe aliotoa haukupokelewa na walimu wa dini, kama ujumbe wa watengenezaji wengine usivyopokelewa. Kwa kuwa hawa waliotosheka tu na maoni ya wanadamu, na mapokeo ya baba zao. Lakini neno la Mungu ndilo tu ambalo wahubiri wangetegemea kushuhudia kuhusu kurudi kwake Bwana. Wapinzani walifanya mizaha na kuwadhihaki wale waliofurahia habari ya kurudi kwake Yesu, na kuishi maisha ya utawa na kuwatayarisha wengine pia.

Iiionekana kana kwamba ni dhambi kujifunza unabiiii uhusuo kurudi kwake Yesu, na maisha ya dunia. Kwa hiyo wahubiri wa kawaida waliliacha neno la Mungu, linaloongoza njia ya imani kwa Mungu. Mafundisho yao yaliwafanya watu kuwa makafiri, na kuishi maisha ya ufedhuli. Kisha mwovu akatupa lawama ya hali hiyo kuwa ni matokeo ya watu wa marejeo.

Wakati watu wengi wenye maarifa walipokuwa wakija kwa wingi, jina la Miller lilitajwa mara chache sana na magazeti ya kidini isipokuwa wakati wa malaumu na mizaha. Wakorofi wakitiwa moyo na walimu wa kidini walimdhihaki Miller na kumlaani na kubeza kazi yake. Mzee huyu mwenye mvi, aliyeacha maisha ya starehe na kusafiri safari kwa gharama zake mwenyewe, ili kutoa maonyo kuhusu hukumu itakayoujia ulimwengu, alidhihakiwa na kuhesabiwa kuwa mzushi tu.

Kupendezwa na Kutokuamini

Watu wenye kupendezwa walizidi kuongezeka. Waumini wameongezeka kutoka mmoja mpaka maelfu. Lakini baada ya muda, upinzani ulitokea kuhusu waumini hawa. Makanisa yalichukua hatua kuhusu watu waliokubaliana na mafundisho ya Miller. Kutengwa [161] makanisani. Mambo haya yakafanya Miller aandike hivi:

“Ikiwa sisi tumekosa, tuombeeni, mtuonyeshe makosa yetu. Tuonyesheni katika Neno la Mungu mahali tulipokosea; maana ni neno la Mungu pekee yake ndilo litaweza kutubadili katika msimamo wetu. Tumefanyiwa mizaha kiasi cha kutosha; na hivyo haiwezi kutuondoa katika msimamo wetu. Msimamo huu tumeupata kwa uangalifu, na kwa maombi huku maandiko Matakatifu yakituunga mkono”.

Wakati maovu ya watu wa siku za Nuhu yalipomlazimisha Mungu alete gharika juu ya nchi, kwanza aliwaonya kwa muda wa miaka 120 aliwapa maonyo ili watubu. Lakini hawakutubu. Walimdhihaki mjumbe wa Mungu. Kama ujumbe wa Nuhu ulikuwa wa kweli, mbona hawakutubu wote? Ushuhuda wa mtu mmoja ukipingana na watu maelfu! Hawakuujali ujumbe, wala hawakuingia safinani.

Wenye dhahaka walibisha wakitaja majira mbalimbali kwamba mbingu haijanyesha mvua. Katika mizaha yao walimtaja mjumbe

wa haki kuwa mwenda wazimu. Basi waliendelea na njia zao mbovu kama zamani. Lakini wakati uliopangwa na Mungu hukumu ili-waangukia wakaidi hao waliokataa rehema zake.

Wakaidi na Wasioamini

Kristo alisema kuwa jinsi watu wa siku za Nuhu “wasitambue, hata gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu”. Mathayo 24:39. Wakati watu wa Mungu watakapounganika na ulimwengu, wakati anasa za dunia zitakapoingia kanisani, wakati wote watakapotazamia siku 7 za mafanikio duniani, ndipo kwa ghafla, kama umeme umulikavyo, ndivyo utakavyokuwa mwisho wa matumaini yao. Jinsi Mungu alivyomtuma mtumishi wake kuwaonya walimwengu wa siku za Nuhu juu ya gharika, ndivyo atakavyowatuma watumishi wake waaminifu kutangaza ukaribu wa kuja hukumu yake, na jinsi watu wa Nuhu walivyomcheka na habari aliyotangaza, kadhalika siku za Miller watu walidhihaki maonyo yake.

Hakuna ushahidi zaidi kuliko huu ya kwamba makanisa yaliyo-jitenga na Mungu yanaudhihaki ujumbe uliotumwa na Mungu.

[162] Wale walioupokea ujumbe wa marejeo waliona kuwa huu ndio wakati wao wa kuwa na msimamo halisi. Mambo ya milele yameingia katika nia zao hakika. Mbingu ilikaribiana nao, nao wakajiona kuwa ni wenye hatia mbele za Mungu Wakristo walijisikia kuwa wakati walio nao ni mfupi sana, na kwamba yawapasayo kuwafanyia wenzao, budi yafanye upesi. Umilele ulionekana kufika karibu. Roho wa Mungu aliwawezesha kujitayarisha kwa ajili ya siku ya Mungu. Maisha yao ya unyofu yaliwahukumu wasiomcha Mungu, ambao ni wakanisa, maana hawakutaka kuingiliwa katika shughuli zao za anasa na uchumi, na upendo wa ulimwengu. Hayo yote yalileta upinzani kwa watu wa marejeo.

Wapinzani hawa walijitahidi kuwakatisha tamaa, kwamba unabii wa hukumu ya Mungu umefungwa, hauna haya kushughulikiwa. Na kwa jinsi hii Waporotestanti walifuata njia ya Rumi. Waprotestanti walidai kwamba jambo la muhimu linalohusu wakati wetu haliwezi kufahamika, maana limefungwa. Wahubiri wakasema kuwa vitabu vya Danieli na ufunuo ni vya siri zisizojulikana.

Lakini Kristo aliwaelekeza wanafunzi wake katika maneno ya Danieli kuwa, “Asomaye na afahamu” Mathayo 24:15 na Ufunuo pia utafahamika. “Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo hayana budi kuwa upesi. Heri asomaye, na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yalioandikwa humo; kwa maana wakati u karibu” ufunuo 1:1-3.

“Heri asomaye” - kutakuwa na watu wasiosoma. “Na wale wao wayasikiao” — Kuna watu wanaokataa kusikiliza kitu chochote cha unabii. “Na kuyashika yalioandikwa humo” - Wengi hukataa kushika mafundisho ya ufunuo. Hawa hawana udhuru, wala hawata-pata mibaraka iliyoahidiwa.

Watu wanathubutuje kusema kuwa ufunuo hautafahamika? Ni siri iliyofunuliwa, kitabu kilicho wazi. Ufunuo huongoza mawazo kuelekea Danieli. Vitabu vyote hutoa mafundisho yahusyo matukio ya siku za mwisho.

Yohana aliona hatari, mapambano, na mwisho aliona ukombozi wa watu wa Mungu. Aliandika juu ya ujumbe wa mwisho utakaoy-akomaza mavuno ya nchi, yaani wafuasi wa Mungu. Mavuno ya aina mbili, yale yatakayopelekwa mbinguni na yale yatakayochomwa motoni. Kwa hiyo wale wanaogeuka kutoka katika ukafiri na kuingia katika nuru, hupata mafundisho ya siku za mwisho kuhusu hatari na mapambano yanayowakabili.

Kwa nini basi watu huishi ujingani kuhusu mafundisho ya Danieli na Ufunuo, ambayo ni sehemu ya maandiko Matakatifu? [163] Ni makusudi ya yule mwovu kuwafunga watu wadumu gizani wasiyajue mambo yajayo yanayofunua udanganyifu wake. Kwa ajili hii Kristo mfunuaji wa siri, aliona jinsi vitabu hivyo vitakavy-opigwa vita, ndipo akasema, “Heri asomaye” naye “Asikiaye”. Na “Kuyashika”, mambo ya unabii huu.

Marejeo:

S. Bliss *Memories of William Miller*, pp. 65-67

Ibidi., pp. 74-75

Ibidi., 76-77, 81

Ezekiel 33:8-9 Bliss, p. 92 R.M Devens. *American Progress of The Great Events of Greatest Century*, ch. 28 para. 1-5

F. Reed — *Christian Advocate and Journal*, Dec. 13, 1833

The Old Countryman — Portland (Maine)

Evening Advertiser, Nov. 26, 1833

Josiah Litch — Signs of the Times, August 1, 1840

Bliss, pp. 250, 252

Ibid., p. 146

19/Kwa Nini Uchungu Mkuu?

[164]

Kazi ya Mungu hufanana sana kizazi hata kizazi na karne hadi karne, wakati matengenezo makuu ya uamsho yanapofanyika. Kanuni za Mungu za kuongezea watu ni zile zile. Msimamo wa kanisa kwa wakati huu ni sawa na wa wakati uliopita, na msimamo wa kanisa wa wakati uliopita unalo fundisho kwa wakati huu.

Mungu huwaongoza watumishi wake kwa njia ya Roho wake ili kuendesha kazi yake duniani. Watu huwa vyombo tu katika mkono wake. Kila mtu amepewa nuru ya kutosha kufanyia kazi aliyokabidhiwa. Lakini hakuna hata mtu ye yote aliyepata kufahamu mambo yote ya Mungu kwa wakati wake. Watu hawaelewi mambo yote ya pasayo kazi ya Mungu wanayofanya. Hata manabii hawakufahamu ujumbe wote na mafunuo waliyofunuliwa. Maana ya maono hayo ilikuwa ikifunuliwa taratibu karne kwa karne.

Petrol asema, “Katika habari ya wokovu huo manabii walitafuta tafutta na kuchunguza chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulionywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakao kuwako baada ya hayo. Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu.” 1 Petro 1:10 - 12. Katika kizazi cha ukristo, hilo ni fundisho muhimu kiasi gani! Wale watu watakatifu wa Mungu walitafutatafuta kwa bidii, mambo yaliyofunuliwa wakati wa vizazi ambavyo havijazaliwa bado. Jambo hili linakanusha usemi wa wakristo wanaostarehe tu na kusema kuwa unabii haufahamiki.

Sio kwa nadra akili hata za watumishi wa Mungu huwa vipofu wakabaki kufuata mapokeo tu na hadithi za mafundisho ya uongo, kwamba hushika mambo yaliyofunuliwa katika Neno la Mungu sehemu sehemu basi. Wanafunzi wa Kristo, hata wakati ule Mwokozi alipokuwa pamoja nao walikuwa na mawazo hafifu kuhusu Masihi, kwamba ni mtawala wa muda tu atakayekuja kuwasaidia. Wala hawakuyafahamu maneno yake kuhusu mateso yake na kifo chake.

[165]

Wakati Umetimia

Kristo aliwatuma wakiwa na ujumbe wake kwamba: “Wakati umetimia”, na “ufalme wa Mungu umekaribia: tubuni mkaiamini Injili.” Marko:15. Unabii huo ulikuwa umejengwa katika Danieli 9. Majuma sitini na tisa yataendelea mpaka kwa Masihi Mkuu. Wanafunzi walitazamia kwamba masihi atausimamisha ufalme katika Yerusalemu, ili kuitawala nchi yote.

Walihubiri ujumbe waliokabidhiwa, ingawa walikosa kuielewa maana yake halisi. Ijapokuwa mahubiri yao yalisimama katika Danieli 9:25 hawakuliona fungu lililofuata lisemalo kwamba Masihi atakatiliwa mbali. Mawazo yao yalikuwa tu juu ya utukufu wa ufalme utakaosimamishwa duniani. Hili liliwapofusha kabisa. Wakati ule walipotazamia Bwana wao kuwa mfalme katika kiti cha Daudi, walimwona akikamatwa, na kuteswa, na kudhihakiwa na mwisho kufa msalabani. Kwa hiyo walivunjika na kukata tamaa kiasi gani!

Kristo amekuja katika wakati ule ule ilivyotabiriwa. Maandiko yametimizwa kwa ukamilifu kabisa. Neno la Mungu na Roho wa Mungu wameshuhudia agizo la mbinguni kuhusu Mwana wa Mungu. Walakini mawazo ya wanafunzi yalikuwa yamejazwa na mashaka tu. Je, kama Yesu angekuwa Masihi kweli wangejazwa na masikitiko, na uchungu? Hilo ndilo swali lililokuwa likiwahangaisha siku hiyo ya Sabato baina ya kifo chake na kufufuka kwake.

Hata hivyo hawakukataliwa na kuachwa, “Nikaapo gizani Bwana atakuwa nuru kwangu..... atanileta nje kwenye nuru, nami nitaiona haki yake.” “Nuru huwa-zukia wenye adili gizani.” “Nitafanya giza kuwa nuru mbele yao, na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka. Haya nitayatenda, wala sitawaacha.” Mika 7:8,9; Zaburi 112:4; Isaya 42:16.

Matengenezo yaliyotangazwa na wanafunzi yalikuwa sawa, kwamba, “Wakati umetimia, ufalme wa Mungu umekaribia.” Mwisho wa wakati ule, - yaani majuma sitini na tisa ya Danieli 9, ambayo yangeendelea mpaka Masihi, mwenye kutiwa mafuta, ndiye Kristo aliyetiwa mafuta ya Roho Mtakatifu alipobatizwa na Yohana Mbatizaji. Ufalme wa dunia haukuwa ufalme wa wakati huo wa milele ambao falme zote zitamtumikia. Danieli 9:27.

Neno, “ufalme wa Mungu,” humaanisha ufalme wa neema na ufalme wa utukufu. Mtume husema, “Basi na tukaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema wakati wa mahitaji.” Waebrania 4:16. Kuwapo kiti nikuwapo ufalme. Kristo hutumia neno, ufalme wa mbinguni, kumaanisha kazi ya neema mioyoni mwa wanadamu. Kwa hiyo kiti cha utukufu humaanisha ufalme wa utukufu. Mathayo 25:31, 32. Ufalme huu ni wa baadaye, utasimamishwa katika kurudi kwake Yesu.

[166]

Wakati Mwokozi alipotoa maisha yake na kulia, “Imekwisha”, ahadi iliyotolewa kwa Adamu na Hawa huko Edeni ilithibitishwa. Ufalme wa neema ambao kwanza ulikuwako kwa njia ya ahadi tu, ukasimikwa.

Hivyo basi kifo cha Kristo, tukio ambalo wanafunzi walidhani kuwa limeharibu tumaini lao, ndicho kilithibitisha uhakika wa tumaini lao milele. Ingawa kilikuwa na ukatili wa hali ya juu kabisa, ndicho kilihakikisha kuwa imani yao ni ya hakika. Tukio lililowatia uchungu na kukata tamaa, lilifungua mlango wa tumaini kwa watu wa Mungu wa nyakati zote. Kwa kuchangamanisha upendo halisi kwa Yesu na anasa ndiko kuliwafanya wanafunzi wakakuza ubinafsi wa tamaa ya kutaka vyeo. Njozi zao zilijazwa na enzi na taji za kifalme na utukufu wake, kiburi chao, kiu yao ya heshima viliwaongoza, nao hawakuyajali mafundisho ya Kristo yahusuyo ufalme wa neema, na yale yahusuyo mauti yake. Makosa haya yalileta matokeo ya majaribu yaliyowapata ili kuwarekebisha. Kwao Injili ya utukufu itakayotangazwa ulimwenguni, ilikabidhiwa. Injili hiyo ni ya kufufuka kwake Mwokozi. Ili kuwaandaa kwa kazi hiyo, majaribu makali yaliwapitia.

Baada ya kufufuka kwake Yesu, aliwatokea wanafunzi wake waliokuwa wakienda Emau, na kuwafunuliwa mambo yote yaliyomhusu yeye, kama Maandiko yasemavyo. Lilikuwa kusudi lake kukaza imani yao juu ya unabii (Luka 24:27; 2 Petro 1:19) si kwa kumwona yeye binafsi, ila kufuata unabii wa agano la Kale. Kama hatua ya kwanza ya kuwafundisha, Yesu alielekeza mawazo yao juu ya Musa na manabii wote wa agano la Kale.

Kufa Moyo Hadi Ushindi

[167] Sasa wanafunzi walimpata kwa hakika yule ambaye Musa na manabii waliandika habari zake. Sasa mashaka na kukata tamaa vimetoweka, na badala yake wamekuwa na imani na ushindi kamili. Wamepita katika kipindi kigumu, na mwisho wameona jinsi neno la Mungu lilivyoshinda na kutimia. Sasa ni nini tena kitawatatanisha? Katika masikitiko makuu wamepata ushindi na tumaini la hakika, ambalo ni sawa sawa na nanga iliyo imara. Waebrania 6:18, 19.

Bwana asema, “Watu wangu hawataaibika milele”, “Huenda kilio huja kukaa usiku, lakini asubuhi huwa furaha.” Yoeli 2:26; Zaburi 30:5. Siku ya kufufuka kwake Bwana wanafunzi hawa walimlaki, na roho zao ziliburudika wakati walipokuwa wakisikiliza maneno yake. Kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni, Yesu aliwaagiza wanafunzi, akisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili.” Akaongeza kusema, “tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote.” Marko 16:15; Mathayo 28:20. Siku ya Pentekoste Mfariji aliyehidiwa alishuka, na roho za wanafunzi zikaburudishwa kwa kuwako kwake Bwana.

Ujumbe wa wanafunzi Ulifanana na wa 1844

Hali ya mambo ilivyokuwa wakati wa mwanzo wa marejeo ya Kristo, ndivyo pia ilivyokuwa kwa wale waliokutangaza kurudi kwake mara ya pili. Jinsi wanafunzi walivyohubiri kwamba, “Wakati umetimia, ufalme wa mbinguni umekaribia”, ndivyo hivyo Miller pia na wenzake walivyohubiri kwa kipindi cha unabii cha mwisho katika Biblia kilikuwa karibu kumalizika, na kwamba hukumu iko karibu, na ufalme wa milele uko karibu. Mahubiri ya wanafunzi kuhusu wakati yalijengwa juu ya Danieli 9. Ujumbe uliotangazwa na Miller na wenzake ulikuwa ukisema kuwa unabii wa siku 2300 ulikuwa karibu kumalizika, Unabii huo umo katika Danieli 8:14, ambao sehemu yake ni majuma sabini. Mahubiri yote hayo yalihusu utimizo wa nyakati tofauti katika unabii ule ule wa muda ule ule.

Sawa na wale wanafunzi walivyokuwawa, hali kadhalika William Miller na wenzake hawakuelewa kamili ujumbe waliokuwa wakiuhubiri. Makosa ambayo yalikuwa kanisani yaliwazuia wasiutafsiri vizuri unabii. Kwa hiyo ingawa walikuwa wakihubiri ujumbe wa

Mungu, lakini kwa kukosa kuutafsiri vizuri, waliangukia katika hali ya uchungu na kukata tamaa.

Miller alishikilia maoni ya wengi kwamba nchi hii ndiyo “patakatifu”, na akaamini kuwa kutakaswa kwa patakatifu ni kule kuchomwa moto wa utakaso wa dunia. Moto huo ni ule wa wakati wa kuja kwa Bwana, yaani mwisho wa dunia. Kwa hiyo akaamua kuwa mwisho wa siku 2300 ni wakati wakuja kwa Bwana mara ya pili. [168]

Utakaso wa patakatifu kilikuwa kitendo cha huduma ya mwisho ya kuhani mkuu, kwa kila mwaka. Ilikuwa huduma ya upatanisho inayofunga huduma zote katika mwaka mzima, yaani kuondoa dhambi zote katika Israeli. Ilikuwa ni kivuli cha huduma ya Kuhani wetu Mkuu huko mbinguni, yaani huduma ya kuondoa dhambi za watu wake zilizoandikwa vitubuni mbinguni. Kazi hii inahusu upelelezi au uchunguzi na hukumu, ambayo inatangulia kuja kwa Bwana mbinguni. Wakati Bwana akija kila jambo litakuwa limeamuriwa. Yesu asema, “Na ujira wangu u pamoja nami kumlipa kila mtu kwa kadiri ya kazi, au matendo yake.” Ufunuo 22:12. Kazi hii ndiyo iliyotangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:7, kwamba, “Mcheni Mungu na kumtukuzwa, maana saa ya hukumu yake imekuja.”

Watu wanaoutangaza ujumbe huu, hutangaza ujumbe wa kweli, na wakati ufaao. Jinsi wanafunzi walivyokosea kuhusu ufalme utakaosimamishwa mwisho wa “majuma sabini”, hali kadhalika watu wa Marejeo walikosa kuhusu tukio litakalotukia mwisho wa siku 2300. Katika mambo yote mawili maoni ya watu yaliwapoteza. Wote walitimiza mapenzi ya Mungu kwa kutangaza ujumbe, ambao ulipaswa utolewe na wote wakaangukia katika masikitiko na uchungu mkali, kwa ajili ya kutafsiri vibaya unabii.

Walakini Mungu alitimiza kusudi lake la kutangaza kwa ujumbe wa hukumu kama ilivyokusudiwa. Kwa maandalio yake, ujumbe ulileta jaribu na utakaso wa kanisa. Je, nia zao zilikazwa ulimwengu au mbinguni? Je, walikuwa tayari kuukana ulimwengu na kumlaki Bwana? Ule msiba wa uchungu ungewapima watu wanaojidai kuwa wafuasi wa Mungu, kama watayapokea maonyo. Je wangekuwa tayari kumtegemea Mungu kamili wakati walimwengu wanapowazomea? Wangevumilia uchungu wa kutokurudi Bwana

wao? Kwa kuwa hawakufahamu jinsi Mungu anavyofanya, Je, wangeutupilia mbali ule ukweli unaothibitika katika neno lake?

Jaribu hili litatoa fundisho kuhusu kukubaliana na tafsiri za binadamu, badala ya Neno la Mungu hasa. Wana imani watajitahidi kuchunguza Biblia, ili kupima msimamo wao na kukataa kitu chote ingawa kinakubaliwa na wakristo ulimwenguni, kitu ambacho hakipatikani katika Maandiko Matakatifu.

[169]

Mambo ambayo wakati wa majaribu huonekana kuwa giza, baadaye yatakuwa dhahiri. Ingawa majaribu yatokane na makosa yao, lakini kwa maongozi ya Bwana, ambaye “Njia zote za Bwana ni fadhili na kweli, Kwao walishikao agano lake na shuhuda zake.” Zaburi 25:10.

20/Upendo kwa Kurudi Kwake Yesu

[170]

Mwamko mkuu wa kidini ulitangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14. Malaika alionekana akiruka katikati ya mbingu, “mwenye injili ya milele ili awahubiri watu wakaa duniani, watu wa kila taifa, na kabila na lugha na jamaa”. Akisema kwa sauti kuu, “Mcheni Mungu na kumtukuzwa, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyefanya mbingu na nchi na bahari na chemichemi za maji. Ufunuo 14:6-7.

Malaika anafananishwa na nguvu na uwezo wa ujumbe utakaotangazwa na kukamilishwa. Kule kuruka kwa malaika katikati ya mbingu, na sauti kuu, na kutangazia watu wa kila taifa, na kabila na lugha na jamaa huonyesha wepesi wa kuendesha kazi na watu wahusikao. Wakati watu hao watakapotoka na kuanza kazi, watatangaza hukumu itakayoanza.

Ujumbe huu ni sehemu ya Injili itakayohubiriwa wakati wa mwisho tu, ambapo saa ya hukumu imekuja kwa hakika. Sehemu hiyo ya ujumbe uhusuo wakati wa mwisho, Danieli aliambiwa aufunge, mpaka wakati wa mwisho”. Daniel 12:4. Ujumbe huu wa hukumu ambao utahubiriwa wakati wa mwisho, haukutimilika wakati mwingine mpaka wakati huo, kama unabii ulivyotabiri.

Paulo alilionya kanisa la wakati wake kuwa, lisikutazamie kurudi kwa Kristo wakati huo mpaka uasi mkuu utakapotokea, na “mtu wa dhambi” kushika uongozi wa kanisa kwa muda mrefu, ndipo tutakutazamia kurudi kwa Bwana. 2Wathesalonike 2:3. “Mtu wa dhambi” — “pia siri ya kuasi” “Mwana wa uharibifu” — ni upapa, ambao ulijitwalia mamlaka ya kuongoza dini kwa muda wa miaka 1260. Muda huo ulimalizika mwaka 1798. Kurudi kwa Kristo kusingeweza kutokea kabla ya muda huo. Paulo alijumlisha kipindi chote cha ukristo mpaka mwaka 1798. Tangu wakati huo kurudi kwake Yesu kunaweza kutangazwa.

Kabla ya wakati huo ujumbe wa aina hiyo haukutangazwa. Kama tuonavyo, Paulo hakukutangaza kurudi kwa Yesu, ila alionyesha kuwa kurudi kwa Bwana kungali mbali. Watengenezaji wa kanisa

hawakuhubiri kurudi kwa Bwana. Martin Luther alisema kuwa kurudi kwa Yesu kunaweza kutokea baada ya miaka 300 tangu wakati wake. Lakini tangu mwaka 1798 kitabu cha Danieli kilifunguliwa, kwa hiyo watu wengi walianza kuhubiri saa ya hukumu.

[171]

Mwamko kwa Nchi Mbalimbali Wakati Ule Ule

Watu wa marejeo walionekana mahali mbalimbali kwa wakati mmoja sawa na watengenezaji wa karne ya kumi na sita. Wakati wenye imani waliyachunguza Maandiko na unabii, wakaona ushahidi wa kuonyesha kuwa mwisho unakaribia. Wakristo wa vikundi huku na huko walipochunguza Biblia waliamini kuwa kurudi kwa Kristo kumekaribia.

Miaka mitatu baada ya Miller kuufasiri unabii huu, Dr. Joseph Wolf, ambaye ni mhubiri alianza kuhubiri juu ya kurudi kwake Yesu. Alizaliwa huko Ujerumani, akiwa wa ukoo wa Kiebrania, aliongoka, akawa mkristo wakati wa angali mtoto. Alikuwa akipenda kusikiliza masimulizi ya kuja kwa Masihi na kuanzishwa kwa ufalme wa Israeli. Siku moja alisikia habari za Yesu wa Nazareti zikitajwa, aliuliza kuwa huyo Yesu ni nani? Alijibiwa kwamba ni Myahudi mwenye ujuzi mwingi na uwezo. Lakini Myahudi huyu alipojifanya kuwa Masihi, baraza la kiyahudi lilimhukumia kifo. Akaendelea kuuliza, “Kwa nini Yerusalemu iliharibiwa, na sisi tuko utumwani?” “Baba yake akajibu, Ole, Ole Kwa sababu Wayahudi waliwaua manabii” Jambo hili lilimwingia kijana moyoni. Akafikiri, “Labda Yesu pia alikuwa nabii, na Wayahudi walimwua mtu mwenye haki”. Ingawa kijana huyu alizuiwa asiingie katika Kanisa la Kikristo, lakini alipendelea kunyemelea huko na kusikiliza mahubiri wakati akiwako nje. Alipokuwa na umri wa miaka saba, siku moja alikuwa akijisifu kwamba siku zijazo wakati Masihi atakapokuja ataleta fahari ya Israeli. Mzee yule aliyekuwa akiongea naye, alisema, “Kijana wangu, nitakuambia masihi alikuwa nani; alikuwa ni Yesu wa Nazareti, ambaye mababu zako walimsulubisha . . . Hebu nenda nyumbani usome Isaya sura ya hamsini na tatu; ufahamu kuwa Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu”.

Alikwenda nyumbani akasoma sura ile. Lo, ilitimizwa kwa ukamilifu gani juu ya Yesu. Kijana akamaka na kusema, “Kumbe maneno ya Wakristo ni ya kweli?” Alipomwuliza babaye amweleze

unabii huo, hakupata jibu. Basi hakumwuliza tena. Alipopata umri wa miaka kumi na saba, akaenda zake kujitafutia elimu na kazi, na kuchagua dini apendayo. Akaenda bila fedha kutafuta kazi. Aliji- [172] funza kwa biddii, na kujua lugha ya Kiebrania barabara. Aliingia katika dini ya Kirumi, na akaenda Rumi katika chuo cha utafiti. Hapa aliona machafuko ya kanisa, akayashambulia wazi na akataka Matengenezo yafanyike kanisani. Baada ya muda aliondolewa pale, kwa kuwa hakukubaliana na hali hiyo ya Kirumi. Alihesabika kuwa mkaidi, asiyejirudi, kwa hiyo akaenda zake. Akasafiri mpaka Uingereza, huko akajiunga na kanisa la Anglikana, yaani kanisa la Kiingereza. Baada ya miaka miwili akaondoa mwaka 1821 kwenda kazini.

Wolff aliamini juu ya kurudi kwake Yesu kuwa ku karibu. Tafisiri ya unabii ilionyesha kuwa yu karibu kabisa kurudi. Anaona kuwa jinsi Miller alivyotangaza ndivyo. Je Bwana hakutuonyesha dalili za kuja kwake ili tujue wakati huo? Hakutaja mfano wa mtini? Hakika tutajua kwa ishara ili tujiandae sawa kama Nuhu alivyojiandaa kuingia safinani.

Kinyume cha Tafisiri Nyingine

Kuhusu namna watu wanavyotafisiri maandiko, Wolff aliandika akasema, “Fungu kubwa la wakristo, au makanisa ya wakristo wamepotoka na kuacha njia ya Maandiko Matakatifu, wakidhani kuwa wanaposoma”, “Myahudi”, huelewa, “Mmataifa” na wasomapo “Yerusalemu” huelewa “Kanisa” na inaposemwa “nchi” huelea “mbingu” na inaposemwa “Kurudi kwake Bwana” huelewa “Kuedeshwa kwa kazi”, na “Kwenda mlimani” maana yake ni “madaraka ya mkutano wa Methodist”.

Tangu mwaka 1821 mpaka 1845 Wolff alisafiri katika nchi za Misri, Abyssinia, Palestine, Syria, Persia, Bokhara, India na Marekani.

Uwezo Kitabuni

Dr. Wolff alisafiri katika nchi nyingi za watu wakorofi bila kuwa na ulinzi wo wote, huku akivumilia shida nyingi sana, na [173] kupita katika hatari za kila namna. Alikuwa akishinda njaa; akiuzwa

kama mtumwa, mara tatu alihukumwa kufa, akishambuliwa na wanyang'anyi, na mara nyingine akiwa karibu kufa kwa kiu. Mara moja alitekwa na kutembezwa maili mamia kwa miguu, akipitishwa milimani kwenye barafu akiwa karibu uchi.

Alipoonywa kuwa asitembee katikati nchi za makatili bila kuwa na ulinzi kamili, alisema kuwa yeye anazo silaha kamili, ndiyo maombi na matumaini yake kwa Kristo. Silaha nyingine niliyo nayo ni upendo wa Mungu nilio nao moyoni mwangu anaoniwezesha kuwapenda watu wengine. Na Biblia niliyo nayo mkononi mwangu ndiyo silaha mahsus. Kitabu hiki cha Biblia ndiyo nguvu yangu. Ndicho msaada wangu.

Aliendelea hivyo mpaka sehemu kubwa ya nchi ikasikia ujumbe. Alieneza Injili na kutoa sehemu za Injili kwa baadhi ya Wayahudi, Waturuki, Waparisi, Wahindu na mataifa mengineyo. Kila mahali alikutangaza kurudi kwa Masihi kuliko karibu sana.

Katikati ya Bokhara alikuta kikundi cha watu wakikutangaza kurudi kwake Bwana. Alisema, Waarabu wa Yemen wanacho kitabu cha Seera, ambacho hueleza habari za kurudi kwake Bwana, na kumiliki kwake kwa fahari watu hao anakutazamia kurudi kwa Bwana kutatokea katika mwaka 1840 Niliwakuta wana wa Israeli wa kabila la Dani pamoja na wana wa Rekabu wakikutazamia kurudi kwa Bwana kwa hamu sana.

Imani hiyo hiyo ilionekana katika Wamishenari wengine wa Tatari. Kuhani wa Tatari aliuliza kuwa, ni lini Kristo atarudi pamoja na mawingu? Huyu mtu wa misheni alipoonekana kuwa hana habari, yule Kuhani wa Tatari alishangaa sana kuwa mwalimu huyu wa Biblia hana habari juu ya jambo hili. Huyu mtu wa Tatari alionyesha imani yake kwa yale yaliyomo katika unabii kwamba Kristo atarudi katika mwaka wa 1844.

Ujumbe wa Marejeo Huko Uingereza

Ujumbe wa marejeo ulihibiriwa Uingereza mapema kama mwaka 1826. Ujumbe kamili haukuhibiriwa, lakini habari ya kurudi kwake Kristo katika mawingu ilikuwa imetangazwa. Mwandishi

[174] mmoja aliandika kwamba, kiasi cha Wachungaji 700 wa kanisa la Anglikana (uingereza) walikuwa wakihubiri kuhusu “Injili hii ya” “Ufalme”

Injili iliyokuwa ikitaja kuwa Kristo atarudi mwaka 1844 ilikuwa ikihubiriwa huko Uingereza. Magazeti yaliyohusu marejeo ya Kristo yalichapishwa Marekani yalikuwa yakitolewa kwa wingi huko Uingereza. Katika mwaka 1842 Robert Winter, mwingereza aliyeukubali ujumbe wa marejeo huko Marekani, alirudi nyumbani kwao kutangaza ujumbe huo. Watu wengi walijiunga pamoja naye katika kazi hiyo ya kutangaza, katika sehemu kadhaa za Uingereza.

Huko Amerika ya Kusini Lacunza, mtu wa Hispania wa dhehebu la Jesuit, aliupokea ujumbe wa marejeo akauamini. Ili kusudi kuepuka maalumu ya Rumi, aliandika habari zake, akijiita kuwa Mwalimu Ben-Ezra, akijipendekeza kuwa ni mwongofu wa Kiyahudi. Panapo mwaka 1825 kitabu chake kilitafsiriwa katika lugha ya kiingereza. Kitabu hicho kiliongezea mkazo wa imani juu ya ujumbe ambao umeshahubiriwa tayari, huko Uingereza.

Aliyofunuliwa Bengel

Katika Ujerumani mafundisho ya Biblia yalikuwa yamefundishwa na Bengel, mchugnaji wa Kiluther. Alipokuwa anatarisha mahubiri kutoka katika ufunuo 21 nuru ilimulika katika mawazo yake kuhusu kurudi kwa Yesu. Ufunuo wa unabii uling'aa mawazoni mwake na akashangaa kwa fahari ya kurudi kwake Kristo, kama ilivyoelezwa na nabii. Alitafakari kwa muda habari hiyo. Hata alipokuwa mimbarani, fahari ya kurudi kwake Yesu iling'aa tena mawazoni mwake. Tangu wakati huo alijitia katika kujifunza habari za unabii, na halafu ukafikia uamuzi kuwa Kristo atakuja upesi. Muda aliোধani kuwa Yesu atarudi ulikuwa karibu na ule wa Miller.

Maandiko ya Bengel yalienezwa kwanza katika mkoa wa kwao wa Wirtemberg, na baadaye yakaenda katika nchi nzima ya Ujerumani, na wakati huo kuvutia na nchi nyingine pia.

Huko Geneva Gaussen alihubiri kuhusu kurudi kwake Kristo. Alipoingia katika kazi ya kuhubiri alielekea kuwa mtu wa mashaka. Wakati wa ujana wake alikuwa anapenda sana mambo ya unabii. Baada ya kusoma kitabu cha Rollins, juu ya “Historia ya Kale”, ilielekezwa mawazoni juu ya Daniel sura mbili. Alishangazwa na jinsi unabii ulivyotimia bila kukosa, hata kidogo. Huu ulikuwa uthibitisho wa uvuvio wa Maandiko Matakatifu. Basi hakutosheka

na imani ya juu juu. Alipoendelea kuchunguza Biblia zaidi, alibadili imani yake ya kwanza.

Alifikia uamuzi ya kwamba kurudi kwa Yesu kuko karibu. Alipokuwa na imani hiyo, alitamani kuwafunulia na watu wengine pia. Lakini watu waliokuwa hawauamini unabii wa Daniel walimpinga vibaya. Mwisho akaazimu kufundisha watoto, sawa kama Farel alivyofanya Geneva. Alitumaini kuwa watoto wakiamini watawavuta wazazi wao. Alisema, “Nilikusanya kundi la watoto, kama watoto hawa watasikiliza, nina hakika kuwa nitapata kundi la pili; na kwa hiyo hata wazazi wataingia”. Jambo hili likifanyika, kazi imetimilika.

Alipofundisha watoto, watu wazima pia walikuja kusikiliza. Basi kanisa lake lilijaa na wasikilizaji, watu maarufu, wenye elimu na wageni wanaokuja Geneva. Hivyo ndivyo Injili ilivyoenezwa. Gausen akitiwa moyo na hayo aliyochapisha masomo yake, akiwa na nia ya kuanzisha mafunzo ya unabii. Baadaye alikuwa mwalimu katika chuo kimoja na kila jumapili aliendelea na mafunzo ya katekismu, akiwafundisha watoto maandiko Matakatifu. Mafundisho yake yaliyotolewa kwa kinywa na kuandika mambo kwa njia ya kuchapa. Na kama mwalimu wa watoto wa muda mrefu aliwafundisha watu juu ya kurudi kwa Yesu kulikoa karibu.

Wahubiri Watoto wa Scandinavia

Huko Scandinavia pia ujumbe wa marejeo ulihibitwa. Wengi waliongoka na kuzitupilia mbali njia zao mbaya, wakataka rehema na msamaha wa Kristo. Lakini wenye dini ya kawaida ya jumla waliwapinga waongofu wenye dini hawa, na baadhi ya wahubiri hao walitupwa kifungoni. Wakafika mahali pengine ambapo wahubiri wa marejeo ya Kristo walinyamazishwa hivyo, Mungu aliwatumia watoto wadogo kuhubiri. Kwa kuwa walikuwa wadogo serikali haikuweza kuwachukulia hatua yoyote.

Katika nyumba za watu ndimo watu walikuwa wakikutana ili kusikia ujumbe wa marejeo. Baadhi ya watoto hao waliokuwa wakihubiri umri wao ulikuwa miaka sita au minane. Walipokuwa wakishuhudia juu ya upendo wa Mwokozi, maisha yao yalikuwa ya kawaida kwa watoto wa umri huo. Waliposimama kuhubiri hali yao ilikuwa tofauti na hali ya kawaida. Nguvu ya pekee ilikuwa

ndani yao. Walitoa maonyo kwa uthabiti wa pekee. Walisema kwa ujasiri, “Mcheni Mungu na kumtukuza, maana saa ya hukumu yake imekuja” [176]

Watu walisikia maonyo haya kwa hofu na kutetemeka. Roho wa Mungu aliwazungumzia. Wengi walilazimika kuyachunguza maandiko kwa makini, wakasahihisha njia zao. Kazi ilifanyika mpaka wakuu wa serikali wakakiri kuwa mkono wa Mungu ulikuwa ukiwaongoza.

Yalikuwa mapenzi ya Mungu kwamba habari za kurudi kwa Kristo zihubiriwe katika Scandinavia, kwa hiyo aliwawezesha watoto ili wafanye kazi hiyo. Wakati Yesu alipokaribia Yerusalemu, watu walitishwa na makuhani na watawala ili wanyamaze ama wasishangilie, Yesu anapoingia mjini. Lakini watoto katika hekalu walipaza sauti zao na kuimba “Hosana Mwana wa Daudi”. Mathayo 21:8-16. Jinsi Mungu alivyowatumia watoto katika kuja kwa Kristo mara ya kwanza, hali kadhalika atawatumia kutangaza kurudi kwake mara ya pili.

Ujumbe Ulienea.

Marekani ilikuwa ndiyo kiini cha ujumbe na kusanyiko la Marejeo. Maandiko ya Miller na wenzake yaliendelezwa katika nchi nyingine za karibu na mbali, walikokwenda wahubiri. Huku na huko ujumbe wa marejeo wa Injili ya milele ulisikika ukisema, “Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja”.

Unabii ulioonekana kuonyesha kuwa kurudi kwa Kristo kungekuwa katika mwaka 1844 ulieleweka vizuri na watu wa marejeo. Wengi waliamini kuwa hesabu miaka na taratibu zake vilikuwa sawa. Kwa hiyo waliacha kazi zao, na mishahara yao wakajiunga na wale waliokuwa wakitangaza kurudi kwake Kristo. Walakini hata hivyo, wachungaji wachache waliupokea. Kwa hiyo watu wa kawaida tu ndio walikuwa wakiutangaza. Wakulima waliacha mashamba yao, mafundi wakaacha kazi zao, wenye biashara wakaacha biashara zao, wataalamu wakaacha kazi zao za kitaalamu. Wote wakajiunga kwa furaha kuwaambia watu habari njema ya kurudi kwake Yesu. Ujumbe wa marejeo ulipokelewa na watu maelfu. [177]

Andiko Rahisi Huleta Uthibitisho

Wahubiri waliweka shoka kwenye mashina ya miti sawa na Yohana Mbatizaji alivyofanya, na kuwahimiza watu kuuza matunda yapasayo toba. Maneno ya ushuhuda kwamba hali ya toba imepatikana, yalisikika yakisemwa dhahiri na wahubiri mimbarani waziwazi. Wengi walimtafuta Bwana kwa moyo wa toba halisi. Anasa za dunia zilizowajalia kwa muda mrefu sasa waliziachilia mbali, na kutafuta yale ya mbinguni. Walijiunga kutangaza kwa moyo wote, kwamba, “Mcheni Mungu na kumtukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja”

Wenye dhambi walijuta kwa machozi, na kuuliza, “Je, tufanye nini ili tupate kuokoka?” Watu ambao waliishi katika hali ya ufedhuli, wakatafuta jinsi ya kurekebisha hali zao. Wale waliopata amani katika Kristo walikuwa na hamu kuu ya kuwaelezea wengine ili nao wapate amani hiyo. Mioyo ya wazazi iligeukia kwa watoto wao, na ya watoto kwa wazazi wao. Malaki 4:5-6. Vizuizi viletwavyo na kiburi na kutakabari viliondolewa mbali. Mioyo ya maungamo ilikuwa dhahiri kwa wote. Kila mahali watu walikuwa wakimlilia Mungu. Wengi alikuwa wakiomba usiku kucha ili kuhakikisha kuwa wamepata msamaha kwa ajili ya dhambi zao.

Watu wa hali zote, wakubwa kwa wadogo, wenye elimu na wasio na elimu, matajiri kwa maskini walikuwa na hamu ya kusikia ujumbe wa kurudi kwake Yesu. Roho wa Mungu aliwezesha ujumbe huu utangazwe kwa nguvu. Katika mikutano yote malaika watakatifu walikuwamo na waumini wakazidi kuja kwa Bwana kila siku. Maku-tano makubwa yalikuwa yakikutana na kukaa kimya ili kusikiliza ukweli huu. Mbingu na nchi zilionekana kukutana. Watu walirudi nyumbani kwao wakijaa furaha na kuyatafakari yote yaliyosemwa usiku kucha. Mtu aliyehudhuria mikutano hiyo hakuweza kuisahau.

Ujumbe Ulipangwa

[178] Kutangaza kwa wakati hasa wa kuja kwa Kristo kulipingwa na watu wote, tangu wachungaji mpaka wenye dhambi. Wengi walisema kuwa hawapingi fundisho la kurudi kwake Yesu, ila wanapinga ule muda hasa wa kurudi kwake. Lakini macho ya Mungu yalisoma mioyo yao. Hawakutaka kusikia kuwa Mungu

atakuja kuuhukumu ulimwengu kwa haki. Kazi zao zilikuwa mbovu, na zisingeweza kusimama katika hukumu ya Mungu. Hawakuwa tayari kukutana naye, sawa kama Wayahudi hawakuwa tayari kumkaribisha Yesu alipokuja mara ya kwanza. Hawakutaka kusikia ujumbe wa Biblia tu, bali waliwadhihaki wale waliokutazamia kurudi kwake. Shetani alimdhahiki Kristo, kwamba watu wake hawataki arudi. Wale waliokuwa wanapinga ujumbe walisema kuwa, “Hakuna ajuaye saa ya kuja kwake”. Andiko linasema, “Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna ajuaye, hata malaika walio mbin-guni, wala Mwana, ila Baba peke yake”. Mathayo 24:36. Elezo hilo dhahiri lilielezwa na wale waliokuwa wakikungojea kurejea kwa Bwana, lakini wale wapingaji walipotosha maana yake.

Mmoja alisema kuhusu Mwokozi kwamba lazima asingemharibu mtu. Ingawa hakuna ajuaye wakati wa kuja kwake, tunapaswa kujua anapokaribia. Tusipojishughulisha kujua itakuwa bahati mbaya kwetu kama ilivyokuwa kwa wote wa ulimwenguni, wakati wa siku za Nuhu. Kristo alisema, “Usipokeshwa nitakuja kwako kama vile mwizi ajavyo, nawe hutajua saa nitakayokuja kwako.” Ufunuo 3:3.

Paulo anasema kwa wale wenye kujali maonyo, “Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwizi. Ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana” 1Tes. 5:2-5.

Lakini wale wanaotafuta udhuru wakiziba masikio wasiyajali maonyo yale maneno, “Hakuna ajuaye siku wala saa”, huendelea ku-gonga kwao kama mwangwi, hata kwa wafuasi ya Kristo pia. Kadiri watu walivyokuwa wakiutafuta ukweli, wapotofu hawa waliingilia na tafsiri potofu ili kuwapotosha.

Watu wanyofu katika kanisa walikuwa wa kwanza kupokea ujumbe. Pale watu walipotawaliwa na waongozi wao, na pale watu wanapochunguza Maandiko kupambanisha andiko na andiko.

[179]

Wengi walipotezwa na waume, wake, wazazi, watoto hata ikaonekana kana kwamba ni dhambi hata kwenda kusikiliza tu. Ujumbe wa marejeo ukahesabika kana kwamba ni uzushi. Malaika waliagizwa kuwalinda waaminifu hawa, ili waendele mpaka nuru zaidi ifunuliwe kwao, kutoka katika kiti cha Mungu.

Watu waliupokea ujumbe wa marejeo walikesha na kukungojea kurudi kwake Bwana, maana muda uliokuwa ukitazamiwa ulikuwa umekaribia. Waliingoja saa hii kwa utulivu na kicho hasa. Katika kundi hilo lililokuwa likingojewa, hakuna awezaye kusahau hali

waliyokuwa nayo. Kwa muda wa majuma kadhaa kabla ya muda huo shughuli zote za kidunia ziliachwa kabisa. Waumini walijichunguza mioyo yao kwa uangalifu sana, kwa vile baada ya wakati mfupi tu wangeicha dunia hii. Hapakuwa na utengenezaji wa mavazi ya kuvaa wakati wa kupaa, lakini wote walikuwa na tunu ya milele ya kumwona Bwana. Usafi wao haukuwa wa mavazi, bali wa mioyo, tabia iliyotakaswa kwa damu ya Kristo. Je, wanaliko watu wa Mungu namna hiyo, waaminifu wanaotafuta utakaso wa namna hiyo?

Mungu alitaka kuwajaribu watu wake. Mkono wake ulifunika kosa katika kuhesabu tarehe katika unabii. Wakati wa kurejea kwa Kristo, (yaani katika mwaka 1844) ukapita bila Kristo kurudi. Hivyo, wale waliotazamia Mwokozi wakati huo walipata uchungu na masikitiko yasiyoelezeka. Wakati Mungu alikuwa akiwajaribu wale walikuwa walingojea, ambao ni wafuasi wake. Wengi walikuwa wamevutwa kujiunga kwa njia ya hofu tu. Hawa walisema kuwa hawakuamini kuwa Yesu angerudi kwa wakati huo. Walakini walikuwa kati ya kwanza kuwadhihaki waaminifu wa kweli.

Lakini ni Yesu na mbingu yote ndiyo waliwahurumia watu wake. Kama pazia lingefunuliwa wangeweza kuona jinsi malaika wanavyowashughulikia kwa upendo usiosemeka, ili wasikumbwe na gharika ya shetani.

Marejeo:

Travels and Adventures of Rev. Joseph Wolff, Vol. 1 pp. 6-7.

Joseph Wolff, Researches and Missionary Labour, pp. 404 -405.

Journal of the Rev. Joseph Wolff, p. 96

W.H.D Adams, In Perills Oft. Pp. 192, 201

Journal of the Rev. Joseph Wolff, pp. 377, 389

L. Gaussen Daniel the Prophet — Vol. 2 preference.

William Miller na wenzake walitaka kuamsha wataalamu wa dini ili wasimame katika tumaini la imani ya kweli na ukristo halisi wa kanisa. Walishuhgulika pia na kuwaongoa wale wasiokuwa na imani wapate kutubu na kuungama. Wao hawakujishughulisha na habari ya madhehebu, walichotaka ni kuona watu wanasimama katika ukweli halisi. Miller alisema “Nataka kufaidia kila mtu bila kujali ni wa dhehebu gani”. Kama wakristo watakufurahia kurudi kwa Kristo litakuwa jambo muhimu. Hata wale wasiouona umaana wake sina la ziada kwao. Wala sina nia ya kutenganisha mikutano. Wengi wa walioongolewa nami waende kujiunga na makanisa tofauti, tu bora wawe waongofu halisi.

Lakini waongozi wa makanisa walitenga wale walioamini ujumbe wa marejeo. Waumini waliyapenda makanisa yao. Lakini walipoona kuwa inawapasa kuchunguza unabii, walikataliwa. Lakini kwa ajili ya uaminifu wao kwa Bwana walikubali kutengana na makanisa hayo. Katika mwaka 1844 watu kiasi cha hamsini elfu walijitenga na makanisa hayo.

Katika makanisa mengi kumekuwako ongezeko la kawaida za kidunia zikiingia taratibu, na hizo hudhoofisha mambo ya kiroho. Lakini katika mwaka huo kulionekana hali ya badiliko katika makanisa yote nchini. Hayo yalithibitishwa kwa kusemwa kanisani na kuandika magazetini.

Mchungaji Barnes, Mwandishi wa Komentari na kiongozi wa makanisa ya Philadelphia alisema kwamba “..... sasa hakuna mwamko, hakuna uongofu, hakuna kukua kwa neema katika uongozi, wala hakuna wasiwasi kuhusu kuongoa watu na kuwaleta katika wokovu.” Kuna maongezeko ya anasa za kidunia kanisani. Na hayo yanakumba madhehebu yote.

Katika mwezi wa Februari mwaka ule ule, Mwalimu Finney wa Oberlin College, alisema, “Kwa jumla makanisa ya Kiprotestanti katika nchi yetu, yamefifia sana na kuwa na hali ya uadui katika msimamo wake. Hali ya kiroho imefifia mno kiasi cha kutisha.

Washiriki wake wameingia katika hali mbaya sana, kumbakia ku-fuata mitindo tu. Wameungana na walimwengu kwa hali zote za kianasa na siku za ulafi na starehe. Mekanisa yanaendelea kuzama uovuni kwa namna ya kutisha. Yamejitenga mbali sana na Bwana, naye Bwana ameondoka kati yao”

Kukataa Nuru kwa Mwanadamu

Giza la kiroho lilikuwa ndani yao, si kwa sababu wanadamu wamekataa nuru ya Mungu. Wayahudi walipojitia katika mambo ya ulimwengu na kumsahau Mungu, waliachwa gizani wala wa-sitambue kuzaliwa kwa Masihi. Na kwa kutokuamini kwao wal-inkataa Mwokozi. Mungu hakuwa na kusudi la kuwakatilia mbali na wokovu, bali wao wenyewe ndio walijikatilia mbali. “Wale wanaoikataa kweli hugeza giza kuwa nuru, na nuru kuwa giza”. Isaya 5:20.

Baada ya kuikataa Injili, Wayahudi waliendelea kuadhimisha mambo yao ya mfano wa dini, ambavyo sivyo yalivyo, huku wakikubali wazi kuwa Mungu hayumo kati yao. Unabii wa Danieli ulionyesha dhahiri wakati wa kuja kwa Masihi na wa kufa kwake pia. Hawakushughulika kujifunza unabii huo, na mwishowe vion-gozi wao wakalaani mtu yeyote anayejaribu kuweka muda wa tokeo hilo. Katika upofu wao na kutokuamini kwao Waisraeli waliendelea kuuupuza wokovu wao kwa mfuatano wa vizazi. Hawakuona hatari yo yote ya kuikataa nuru ya Injili iliyokuwa bahati yao, ambayo ni nuru ya mbinguni.

Mtu anayeshupaza shingo yake asifanye wajibu umpasao, mwishowe atapotewa na uwezo wa kupambanua baina ya kweli na makosa, ndipo atatengana na neema ya mbinguni hubaki katika giza, imani hupoa na upendo wao hupoa pia, na mafarakano hutokea. Mekanisa hushughulikia mambo yao ya ulimwengu tu, na wenye dhambi hushupaa wasione haja ya kutubu.

Ujumbe Wa Malaika Wa Kwanza

Ujumbe wa malaika wa kwanza wa ufunuo 14 ulikusudiwa kuwa-tenga watu wa Mungu na udhalimu. Katika ujumbe huu Mungu

galiwarekebisha na kuwasahihisha kutokana na maovu yaliyokuwa yakiwatenga na Mungu. Kama wangelipokea onyo hilo na kujinyenyekeza mbele za Mungu, na kujiandaa kusimama mbele yake, Roho wa Mungu angaliwajaza na kuwaongoza. Kanisa lingeufikia umoja, imani na upendo wa siku za mitume, “ambapo waumini walikuwa na moyo mmoja, na Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliookolewa”. Matendo 4:32; 2:47.

Kama watu wa Mungu wangepokea nuru ya Neno lake, wangelifikia umoja wa imani, ambapo mtume anaueleza kwa “Umoja wa Roho katika kifungo cha amani”. Asema, “Mwili mmoja na roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja” Waefeso 4:3-5.

Wale waliouamini ujumbe wa marejeo walitoka katika madhehebu mbalimbali, na mpangilio wa madhehebu yao ulitupiliwa mbali. Mashindano yote na faraka vilipondwa pondwa kabisa. Makosa yalisahihishwa, kasoro zo zote zilinyooshwa, mioyo iliungana katika ushirika mtamu ukafikiwa kwa furaha. Upendo ulitawala mambo yote. Fundisho hili lingeleta matokeo yale yale, kama wote wangelipokea.

Wachugaji ambao ni walinzi wangukuwa wa kwanza kuzitambua dalili za kurudi kwa Mwokozi, walishindwa kujifunza ukweli toka katika unabii au kutoka katika dalili za nyakati. Upendo kwa Mungu na kwa Neno lake umepoa, na ujumbe wa marejeo umeamsha hali zao za kutokuamini zipate kuchangamka. Lakini kutojishughulisha kwao kumefanana na jinsi watu wa kale walivyoouhesabu ujumbe wa Yesu, wakisema “Ni nani katika wakuu au Mafarisayo Amwaminiye?” Yohana 7:48.

Wengi walikata tamaa kujifunza unabii. Walikata tamaa kujifunza unabii wakisema kuwa vitabu vya unabii vimefungwa, wala havieleweki. Makundi ya watu walikataa kusikiliza ujumbe wa marejeo, ingawa walikubali kuwa ni hakika. Waliwatumainia wachungaji wao, na kuogopa kutengwa katika makanisa. Yohana 9:22. Ule ujumbe Mungu aliowatumia watu ulidhihirisha jinsi watu wengi walivyokuwa wakiupenda ulimwengu kuliko mambo ya mbinuni.

Kule kukataa ujumbe wa malaika wa kwanza, ndiko kulikuwa sababu ile ya kuogofya ya hali ya ulimwengu na uasi mwingi, kifo cha kiroho katika makanisa mwaka 1844.

Ujumbe Wa Malaika Wa Pili

[183] Katika Ufunuo 14 malaika wa kwanza alifuatwa na malaika wa pili akitangaza “anguko la Babeli ule mji mkuu, kwa sababu umeyanyweshwa mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake” Ufunuo 14:8. Jina hili, Babeli hutokana na jina lile la zamani la Babeli, maana yake machafuko. Katika Biblia jina hili humaanisha machafuko ya kidini, kutokana na aina mbalimbali za mafundisho. Katika Ufunuo 17 jina hili Babeli husimama badala ya mwanamke, ambaye kimaandiko Matakatifu ni kanisa. Bikira safi hufananishwa na kanisa takatifu. Mwanamke mchafu hufananishwa na kanisa potofu lililoasi, katika Biblia uhusiano baina ya Kristo na kanisa hufananishwa na ndoa. Bwana husema, “Nami nitakuposa uwe wangu kwa milele; naam, nitakuposa kwa haki”. “Maana mimi ni mume wenu” Na Paulo husema, “Kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi”. Hosea 2:19; Yeria 3:14; 2Kor. 11:2.

Uasherati wa Kiroho

“Kutokuwa mwaminifu kwa Kristo, kanisa hukaribisha mambo machafu ya ulimwengu yaliingilie, ambavyo hufananishwa na uasherati unaovuruga ndoa safi. Dhambi ya Israeli ya kujitenga na Bwana, hufananishwa na jambo hili. Hakika kama vile mke amwachavyo mumewe kwa hiana, ndivyo mlivyonitenda mimi kwa hiana, Ee nyumba ya Israeli, asema Bwana”, “Mke wa mtu aziniye! Akaribishaye wageni badala ya mumewe” Eze. 16:32. Yer. 3:20.

Mtume Yakobo asema, “Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu Basi kila anayetaka kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu”. Yakobo 4:4.

Mwanamke (Babeli) alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, “BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI” Nabii alisema, “Nikamwona mwanamke yule amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu”. Babeli ni Mji ule

mkubwa “wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi” Ufunuo 17:4-6, 18.

Uwezo uliokuwa ukitawala Wafalme na Wakuu wa jamii za wakristo kwa karne nyingi ni Rumi. Mapambo ya rangi mbalimbali na dhahabu na lulu yote yalikuwa ya Rumi. Hakuna uwezo mwingine wowote ambao unaweza kulingana na elezo lisemalo, “umelewa kwa damu za watakatifu” kama kanisa lililowatesa watu wa Mungu yaani Rumi. [184]

Babeli pia imelaumiwa kama kuungana na wafalme wa nchi. Kanisa la Kiyahudi kwa kule kujiunga na mataifa makafiri na kujitenga na Mungu likawa kahaba. Rumi nayo kule kutafuta msaada kwa serikali ili kuendesha mambo ya kanisa, lilipata lawama ile ile.

Umoja wa Ulimwengu

Makanisa mengi ya Kiprotestanti yamefuata mfano wa Rumi kwa kuungana na “wafalme wa dunia” — makanisa na serikali kwa uhusiano wao na serikali za kidunia na madhehebu mengine kwa kutafuta kupendelewa na dunia. Neno Babeli — machafuko — linaweza kuhusisha makanisa haya yanayodai kupata mafundisho yao kutoka katika Biblia, na hali bado yanagawanyika katika vidhehebu vingi mno ambavyo vinapingana kwa mafundisho.

Kazi ya kanisa la Kirumi, lasema kwamba “Kama kanisa la Rumi lilipata kuwa na hatia ya kuabudu sanamu kwa kuhusu watakatifu, binti yake kansia la Anglikani linasimama kwa hatia ile ile, ambalo lina makanisa kumi yaliyojitoa kumwabudu Maria kwa moja lilijitoa kwa Kristo.”

Na pia Dr. Hopkins atangaza, “Hakuna sababu ya kufikiri roho ya kumpinga Kristo na kujizoeza kushikamana kwa kile ambacho sasa kinaitwa kanisa la Roma tu. Makanisa ya Kiprotestanti yanampinga ndani yao na yako mbali sana na matengenezo sahihi kutoka katika uasi na ufisadi.” [185]

Kuhusu kujitenga kwa kanisa la Presbyterian kutoka Rumi, Dr. Guthrie aliandika, “Miaka mia tatu iliyopita, kanisa letu lilijitenga na Rumi, likishikilia Biblia katika mikono yake na likiwa na neno kuu lisemalo, ‘Chunguza maandiko’ Halafu aliuliza swali hili, ‘Je, walitoka Babeli wakiwa safi?’”

Upotovu wa Kwanza Kutoka Katika Ukweli wa Injili

Je, kanisa lilifarakana jinsi gani na usafi wa Injili? Lilifarakana kwa njia ya kujiunga na ukarifi, na kushusha kanuni za ukristo ili iwe rahisi wakafiri kujiunga na kanisa. Kuelekea mwisho wa karne ya pili makanisa mengi yalikuwa na umbo jingine kabisa. Wanafunzi wa kwanza walipomalizika na kulala makaburini, watoto wao pamoja na waongofu wapya wakafuata njia nyingine “Desturi za kikafiri zikafurikia ndani ya kanisa, na sanamu zikahalalishwa Ukristo ukategemea msaada wa serikali. Ukristo wa jina tu ukakubaliwa na wengi. Lakini wengi waliendelea kuwa wakafiri tu, wakizidi kuabudu sanamu kwa sirisiri”

Je, mambo yayo hayo hayakurudiwa rudiwa karibu yote ya watu wanaojiita Waprotestanti? Kadiri watangulizi wa kweli walivyokufa, ndivyo walivyofuata walivyogeuzi njia. Wakawa vipofu kabisa wasipokee ukweli uliopokelewa na baba zao. Wakawa kana kwamba sio wana wa watengenezaji, wakijitenga na kujikana nafsi na kuacha ulimwengu.

Lo, makansia yamejitenga na ukweli wa Biblia kiasi gani! John Wesley alisema, kuhusu fedha, “Usipoteze sehemu yoyote ya talanta ya thamani kwa mapambo na kujirembesha. Wala usipoteze muda kupamba nyumba yako, na vitu vya thamani, na mapicha na maridadi za kila namna. Lakini uridhike na heshima itokayo kwa Mungu.”

[186] Mtawala, wana siasa, madaktari, wanasheria, wafanya biashara, wote walijiunga na kanisa kama washriki, ili iwe njia ya kuendeleza mambo yao ya ulimwengu. Halimashauri za kanisa zilikuwa zikiongozwa na makafiri hao ambao walijifanya kana kwamba ni waongofu wa kweli, huku wakitafuta anasa za ulimwengu. Makanisa makubwa, maridadi sana yalijengwa. Wachungaji hodari, ambao kazi yao hasa ilikuwa kuwaburudisha watu, walikuwa wakilipwa mishahara mikubwa sana, mahubiri yao yalikuwa ya kuwaburudisha tu wasikilizaji. Hivyo dhambi zilifichika chini ya uongofu wa mfano tu.

Dhambi kuu iliyoshitaka dhidi ya Babeli ni kwamba “uliwafanya mataifa kunywa mvinyo wa ghadabu ya mafundisho ya uongo yanayokubalika na Babeli kama mvuto wake wa kupotosha juu

ya dunia kwa kufundisha mafundisho yapingayo matamshi ya kweli ya Biblia.”

Ingekuwa siyo dunia kulewa na mvinyo wa Babeli, maelfu ya watu wangesadikishwa na kuongolewa na ukweli halisi wa Neno la Mungu. Lakini imani ya dini huonekana kuvurugwa na kutolingana kiasi cha kuwafanya watu kutofahamu cha kuamini. Dhambi ya ugumu wa moyo wa dunia imesimama mlangoni mwa kanisa.

Marejeo:

Bliss p. 328

Congregation Journal, Mei 23, 1844.

Richard Challoner, *The Catholic Christian Instructed*, Preface, pp. 21-22

Samuel Hopkins, “*A Treatise on the Millenium*” Works, Vol 2, p. 328.

[187]

22/Unabii Ulitimia

Wakati walipomngojea Bwana katika mwaka 1844, na Bwana hakuja wale waliomtazamia walikuwa katika wasiwasi na mashaka sana. Wengi waliendelea kuchunguza Maandiko, ili kuhakikisha msimamo wa imani yao. Unabii ulikuwa wazi ukionyesha kuwa kurudi kwake Bwana ku karibu. Mibaraka watu waliyopokea na uongofu wao vilionyesha kuwa ujumbe ulikuwa wa mbingu. Utatanisho wa unabii ambao walidhani kuwa unawaonyesha kurudi kwa Kristo katika mwaka 1844, lilikuwa fundisho la kuwafunza kuwa wavu-milivu ili kungojea ufunuo zaidi katika mambo ambayo hawayajui.

Kati ya unabii huu uko wa Habakuki 2:1-4. Hakuna hata mtu aliyeona kuwa kule kukawia kumo katika unabii. Baada ya uchungu wao na kukata tamaa kwao fungu hili la Habakuki lilikuwa la muhimu. “Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamuriwa. Inafanya haraka kufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo ijapokawia ingojee, kwa kuwa haina budi kuja haitakawia. Mwenye haki ataishi kwa imani”.

Unabii wa Ezekiel pia uliwafariji waumini. “Bwana Mungu asema hivi Siku hizo ni karibu, na utimizo wa maono yote Mimi nitanena na neno lile nitakalolinena litatimizwa wala halitakawilishwa tena. . . . nitanena neno hilo na kulitimiza, asema Bwana Mungu”. Ezekiel 12:23-25, 28.

Wenye kungojea walifurahi. Mungu ajuaye tangu mwanzo mpaka mwisho ameatumainisha. Kama mafungu ya sehemu kama hizo yasingelikuwako, imani yao ingetoweka kabisa.

Mfano wa wanawali kumi uliomo katika Mathayo 25 unatoa kielelezo cha watu wa marejeo pia. Hapa kanisa la mwisho linaelekezwa jinsi mambo yalivyo. Hali yake inafananishwa na arusi za huko mashariki.

“Ndipo ufalme wa mbinguni unafanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki Bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale walikuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja

nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya, Bwana arusi, tokeni mwende kumlaki” Mathayo 25:1-6.

Wote walichukua taa zao ambazo ni mfano wa Biblia. Basi wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Lakini wakati wale wapumbavu hawakuchukua mafuta, wenye busara walichukua mafuta pamoja na taa zao. Wenye busara hawa walijifunza Maandiko Matakatifu ili kujua ukweli ulivyo, kwa hiyo wakawa na imani ambayo haikuweza kuyumbishwa na hali yo yote. Wengine walikuwa wakichangamka tu kwa ajili ya ujumbe bila kuwa na imani ya kweli, ila msisimko tu, wanapokutana na wengine katika mikutano. Hawa walikuwa wakikutazamia kuja kwa bwana arusi ili wapokee zawadi. Hawakuwa na imani ambayo inasimama imara katika matatizo na kukawia kwa wakati. Walimtazamia Bwana aje mara moja. Imani yao haikufaulu.

[189]

Kuja kwa Kristo kama kulivyotangazwa na ujumbe wa malaika wa kwanza, kulifananishwa na kuja kwa bwana arusi. Tangazo la kuja kwake lilienea pote lilijibika kwa mfano wa wanawali kumi. Katika mfano huu “wote walichukua taa zao, ambazo ni mfano wa Biblia. Basi wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Lakini wakati wale wapumbavu hawakuchukua mafuta, wenye busara walichukua mafuta pamoja na taa zao.” Wenye busara hawa walijifunza maandiko matakatifu ili kujua ukweli ulivyo, kwa hiyo wakawa na imani ambavyo haikuweza kuyumbishwa na hali yoyote, Wengine walikuwa wakichangamka tu kwa ajili ya ujumbe bila kuwa na imani ya kweli, ila msisimko tu, wanapokutana na wengine katika mikutano. Hawa walikuwa wakikutazamia kuja kwa bwana arusi ili wapokee zawadi. Hawakuwa na imani ambayo inasimama imara katika matatizo na kukawia kwa wakati. Walimtazamia Bwana aje mara moja. Imani yao haikufaulu.

“Hata bwana arusi alipokawia, wote walisinzia na kulala usingizi.” Kule kukawia kwa bwana arusi kunafananishwa na kukawia kwa wakati, uchungu wa kutojua, yaani kukawia. Wale waliokuwa na imani ya kweli walikuwa wamesimamishwa mwambani, ambako hakuna kung’olewa na fujo yoyote. “Wote walisinzia na kulala” Kundi moja lenye kuacha imani yao, kundi jingine lenye kungoja kwa uvumilivu nuru ilipowamulikia wazi. Imani ya juu juu haiwezi

kufaidia lolote, wala kutegemea msaada wa ndugu. Kila mtu hana budi kusimama mwenyewe binafsi.

Ukakamavu Kidini Waonekana.

Wakati ule ushupavu kidini ulionekana. Baadhi yao walionekana kuwa na msimamo mwingine mwingine. Mawazo yao ya aina nyingine ya kishupavu hayakukubaliwa na wengine wa imani ya marejeo. Mambo yao yalileta shutuma kwa ukweli wa marejeo.

[190] Shetani alikuwa akipoteza raia zake walioongolewa katika imani ya marejeo, kwa hiyo alileta machafuko katika waumini, kiasi kwamba wengine walipita kiasi. Alikuwa tayari kutafuta vikasoro vyo vyote na kuvifanya viwe ndiyo sababu ya kulaumu msimamo wa watu wa marejeo. Kadiri alivyowashawishi watu wengi waonekane kana kwamba wameongoka na kujiunga na ujumbe wa marejeo ndivyo walivyofanikiwa.

Shetani ni “mshitaki wa ndugu”. Ufunuo 12:10. Malaika zake wako tayari kuona kasoro za watu wa Mungu ili kuzishika na kutoa lawama kubwa. Wakati huo wema wote wa uteule wa watu wa Mungu hauseremi.

Katika historia yote ya kanisa hakuna matengenezo yo yote yaliyofanywa bila kuingizwa ili kuvuruga. Pale Paulo alipoanzisha kanisa, baadhi ya wale waliojidai kuwa waumini walionekana kuingiza maneno ya uzushi. Luther pia alisumbuliwa na watu wa jinsi hiyo, ambao walikuwa wakijidai kuwa Mungu amewaagiza kufanya vile na vile, watu ambao walitegemea maoni yao badala ya maandiko matakatifu. Wengi walidanganywa na waalimu wa namna hii na kujiunga na Shetani kuharibu kazi ya Luther aliyoambiwa na Mungu. Wesley alipambana na hila za Shetani kwa kuwasukuma watu ambao hawakuwa na utaratibu, wala si waongofu ila walikuwa washupavu tu wakitaka mawazo yao yafuatwe na kila mtu.

William Miller hakuwahurumia watu wa aina hiyo ya ushupavu katika dini. Alisema, “Mwovu anao uwezo mkuu juu ya baadhi ya watu wa siku hizi”. Mara nyingi nimeshuhudia ukristo wa mtu wa kweli, rohoni mwake, na usemi wake kuliko kelele zote zinazopigwa na wakristo.

Wakati wa Matengenezo, maadui walitupa lawama juu ya watu waliokuwa na juhudi mno kuyapinga kwamba ni washupavu. Hali ile

ile ilionekana katika kuwapinga watu wa marejeo. Wala hawakuridhika na kuyasema makosa yao tu, lakini walieneza uvumi ambao sio kweli. Walichafuliwa na kule kumtangaza Kristo kuwa yu karibu. Waliogopa, isije ikawa ni kweli, lakini alitumaini kuwa si kweli. Hii ndiyo iliyokuwa siri ya vita yao na watu wa marejeo.

Kuhubiriwa kwa ujumbe wa malaika wa kwanza kulielekea kukomesha ushupavu. Wale waliokubaliana na kundi hili walipatana, wala haikuweko tofauti yoyote. Walipendana, na walimpenda Yesu, ambaye walitazamia kumwona karibuni. Imani yao moja ya tumaini moja viliyakinga mashambulio ya Shetani.

Makosa Yalisahihishwa.

“Na Bwana arusi alipokawia wote walisinzia, wakalala”. Lakini usiku wa manane palikuwa na kelele, “Haya bwana arusi anakuja, ondokeni kwenda kumlaki” katika mwaka wa 1844 ujumbe ulitangazwa kwa maneno yale yale ya Biblia. [191]

Kilichoonyesha kuwa huu ndio wakati wa tangazo hilo kutolewa na kundi hilo kuunganika pamoja na kule kugunduliwa kwa amri ya Artashasta ya kuujenga na kuurudisha mji wa Yerusalemu, ambayo ndiyo mwanzo wa muda wa miaka 2300 ya unabii, iliyotukia katika B.C 457. Haikutokea mwanzo wa mwaka kama ilivyoaminiwa, bali ni katika miezi ya Septemba, Oktoba na Novemba, yaani robo ya tatu ya mwaka. Kwa hiyo kuhesabu kutoka 457 B.C miaka 2300 itamalizika mwaka 1844 robo ya tatu ya mwaka. Anguko la Kale pia hutaja robo ya tatu ya mwaka kama ndiyo siku ya upatanisho katika habari za ukuhani, na siku ya kutakasa patakatifu.

Kule kuchinja kondoo wa pasaka kulikuwa kivuli cha kifo cha Kristo, kitakachotimia kwa wakati wake, katika tarehe ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza wa Kiyahudi, ambayo kwa karne nyingi palikuwa pakichinjwa kondoo wa pasaka, Kristo alianza siku kuu ya kukumbuka kifo chake, kama “mwanakondoo wa Mungu” Usiku ule ule alikamatwa ili akasulubiwe na kuchinjwa.

Hali kadhalika kivuli cha kuhusika na kurudi kwa Kristo budi kitimilike. Kwa wakati ulioamriwa kwa njia ya mfano. Kutakaswa kwa patakatifu, au siku kuu ya upatanisho iliyokuwa ikitokea katika siku ya kumi ya kila mwezi wa saba ya Kiyahudi, ambayo Kuhani mkuu alifanya upatanisho kwa Waisraeli wote, na kuondoa dhambi

zao zote kutoka mahali patakatifu, watu walitakasika. Ndivyo hivyo ilivyoaminiwa kuwa Kristo pia atatokea ili kuitakasa dunia kwa njia ya kuiangamiza dhambi pamoja na wenye dhambi, na kuwachukua watu wake. Siku ya kumi ya mwezi wa saba, ambayo ni siku ya upatanisho, wakati wa utakaso wa patakatifu, ambapo katika mwaka 1844 ilikuwa Oktoba 22, ilihesabiwa kuwa ndiyo siku ya kurudi kwake Kristo, miaka 2300 ingemalizika mwaka 1844. Kwa hiyo ikakubaliwa kuwa wakati huo ndio wa kurudi kwa Kristo.

Kilio Cha Usiku Wa Manane

[192] Hoja hizo zilikuwa kubwa kiasi cha kuwasadikisha watu, na mahubiri yakatolewa, yale yajulikanayo kuwa ni “kilio cha usiku wa manane” Watu maelfu wakajiunga kuyatoa, hali ya ushupavu wa dini iliendelea kutoweka sawa na ukungu wakati wa mapambazuko. Mambo yakaenea kwa upesi, sawasawa na mawimbi, toka mji hata mji, na toka kijiji hata kijiji. Kazi ikafanana na ile ya wakati wa uamsho katika Israeli, baada ya kudidimia dhambini. Kulikuwa na mwamko mkubwa sana, maungamo ya dhambi na kujichunguza mioyo. Waliachilia mbali anasa za dunia wakaambatana na uongofu wa kweli.

Katika madhehebu yote tokea siku za mitume hakuna dhehebu lililokuwa huru kutoka katika dhambi na katika mwaka 1844.

Kama vile katika mwito “Bwana arusi anakuja, walingoja, walianka wakaanza kuzitengeneza taa zao.” Ndivyo watu walivyoamka kuchunguza maandiko kwa bidii sana. Watu wa kawaida tu ndio walioitikia mwito mara ya kwanza, wala sio watu wataalamu. Wakulima waliacha mavuno yao mashambani, mafundi wakaacha vyombo vyao, wote wakaondoka kwenda kulitangaza neno la Mungu. Kwa kawaida makanisa hayakujali ujumbe huu, na wale walioupokea walifutwa katika makanisa hayo. Wale wasioamini walikuja kujiunga na watu wa marejeo waliona kuwa kuna uwezo mkuu katika ujumbe huu. “Haya! Bwana arusi yuaja” Imani ilileta jawabu kwa maombi.

Kama manyunyu ya mvua yanavyokuwa chini, hali kadhalika na neema ya Mungu ilivyokuwa kwa wale waliokuwa wakiutafuta ukweli. Wale waliotumaini kusimama mbele ya Mwokozi karibuni

alikuwa na furaha isiyo kifani. Roho Mtakatifu aliyeyusha mioyo yao.

Wale walioupokea ujumbe walitazamia wakati wa kukutana na Bwana wao. Waliombeana sana. Kila mara walikutana faraghani kuzungumza na Bwana, na sauti za waombaji hawa zilipaa juu kutoka kila mahali. Walihitaji Mwokozi zaidi ya chakula chao. Wakati wo wote walipokuwa na shaka lolote, hawakutulua mpaka waone uthibitisho juu ya jambo hili, hasa msamaha wa dhambi zao.

Uchungu Tena

Lakini tena wakati waliomtazamia Mwokozi ulipita, na Mwokozi hakutokea. Sasa wakawa kama Mariamu alivyokuwa alipokwenda kaburini walikomzika Yesu. Alipofika huko asiune mwili wa Yesu, alianza kulia huku akisema, “Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka” Yohana 20:13.

Waliogopa kwamba wasioamini watazidi kuhakikisha kuwa ujumbe wao sio wa kweli. Lakini hakuna dalili kuwa ujumbe wao sio wa kweli. Lakini hakuna dalili ya ghadhabu ya Mungu iliyo tokea, basi waliendela tu kuvumilia mizaha na mashutumu. Watu wengi walioamini walitupilia mbali imani yao, na kurudi nyuma. Wenye mizaha walifaulu kuvuta wenye mashaka na waoga kuacha msimamo waliokuwa nao. Wote hawa walijiunga na kusema kuwa ulimwengu utaendelea kuwa kama ulivyo kwa miaka maelfu.

[193]

Waumini wa kweli walikuwa wametoa mali zao zote kwa ajili ya Kristo, na kama walivyoamini, walikuwa wametoa maonyo ya mwisho kwa walimwengu huku wakiomba na kutumaini kurudi kwa Bwana, wakisema, “Naam, na uje Bwana”, na sasa Bwana hakuja. Basi kuanza maisha upya, na kukabili mizaha ya walimwengu juu yao, lilikuwa jaribu lisilowezezana kuchukulika.

Wakati Yesu alipoingia Yerusalemu kwa shangwe, wafuasi wake waliamini kuwa alikuwa tayari kukikalia kiti cha enzi cha Daudi, na kuwaokoa watu wake mikononi mwa watesi wao. Kwa matumaini na shangwe kuu, wengi walitandika nguo zao njiani ili apite na kukanyaga juu yake, na wengi walibeba matawi ya mitende kufurahia tukio hilo. Wanafunzi walikuwa wakilitimiza shauri la Mungu, lakini walishangazwa na kuingia uchungu kwa yaliyotokea. Walakini baada ya muda mfupi waliyashuhudia mateso ya Kristo na

kifo chake, wakamzika kaburini. Matumaini yao yalikufa pamoja na Yesu. Hawakuelewa mpaka Bwana alipofufuka ndipo wakafahamu kuwa yote yalitabiriwa na manabii.

Ujumbe Ulitolewa Kwa Wakati Hasa.

Hali kadhalika Miller na wenzake walitimiza unabii, wakatoa ujumbe ambao ulitabiriwa kuwa utatolewa ulimwenguni. Kama wanalitambua kuwa wakiutoa utawaletea uchungu wasingetoa. Ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitolewa kwa wakati wake hasa, na ukatimiza kusudi la Mungu.

Ulimwengu ulikuwa ukitazamia kuwa kama Kristo hataonekana, hali ya marejeo ingeachwa, yaani kanisa la marejeo lingetupwa. Lakini kwa kuwa wengi walitupa imani yao kulikuwako na wengine waliosimama imara. Matunda ya marejeo, roho ya kujichunguza, na kuukana ulimwenguni, huthibitisha kuwa ilikuwa kazi ya Mungu. Hawakuthubutu kukana kuwa Roho Mtakatifu hakuwaongoza waliohubiri ujumbe wa malaika wa pili. Wala hawakupata kasoro yo yote kama unabii na nyakati zilizosemwa. Wapinzani wao hawakuweza kukanusa tafsiri ya unabii, jinsi walivyoueleza. Hawakuweza kukanusha hali ya kiroho iliyokuwako kwa maombi ya bidii na [194] kuchunguza Maandiko kwa bidii ili kuweza kuwapinga wapinzani wote walio hodari.

Watu wa marejeo, yaani Waadventista waliamini kuwa Mungu alikuwa amewaongoza ili kutoa maonyo ulimwenguni, kuhusu saa ya hukumu. Wasema, Ujumbe huu umewajaribu wote waliousikia kwamba wale wote watakaojichunguza mioyo yao watafahamu upande wanaosimama “watakapokuwa wamekutwa, kama Bwana angekuja” Sijui kama wangeweza kusimama na kusema, “Huyu ndiye Bwana wetu, tumemngojea, atuokoe au wangelikimbia uso wake wakiita miamba iwaangukie ili kuwafunika wasiouone uso wake aketiye juu ya kiti cha enzi”.

Hali ya watu ambao bado wanaamini kuwa Mungu bado anaongoza wanaelezwa kwa usemi wa Miller: “Tumaini langu la kurudi kwake Bwana linasimama imara kama hapo mwanzo. Nimetenda yote kama nilivyoona kuwa ni wajibu kutenda, baada ya miaka ya kutafakari” “Maelfu mengi ya watu wamejifunza na kuhubiri kuhusu wakati, na kwa damu ya Yesu wamepatanishwa na Mungu”.

Imani Iidumishwa

Roho wa Mungu bado anakaa kwa watu ambao hawakuharakisha kuikanusha nuru waliyopokea, na kukanusha watu wa marejeo. “Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu, Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi”.

“Bado kitambo kidogo sana, yeye ajaye atakuja wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani. Naye akisitasita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwa wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa walio na imani ya kutuokoa roho zetu” Ebr. 10:35-39.

Onyo hili linatolewa kwa kanisa la siku za mwisho. Linaeleza kuwa Bwana ataonekana kana kwamba anakawia. Watu wanaoonywa hapa ni wale waliofanya mapenzi ya Mungu, wakitaifuta maongozi ya Roho wake na Neno lake hata hivyo huwa hawaelewi makusudi ya Mungu katika maisha yao. Walijaribiwa kuwa na mashaka na kufikiri kuwa, “Kweli Mungu yu pamoja nao” Wakati kama huo maneno yalikuwa dhahiri, “Mwenye haki wangu ataishi kwa imani”. Watu hao wangeweza kusimama tu kwa imani juu ya Mungu, baada ya kukandamizwa na uzito wa mambo yaliyowakabili. Kukana imani na kukanusa uongozi wa Roho Mtakatifu aliyeongoza kazi hiyo mpaka kufikia hatua hiyo, ingekuwa kurudi na kuangukia mbali usalama wao ungekuwa kufuatia nuru hiyo waliyopokea, na kudumu kuchunguza Maandiko zaidi na zaidi, na kwa uvumilivu kungojea maongozi zaidi toka kwa Mungu.

Marejeo:

Bliss pp. 236 — 282

The Adventist Herald na Signs of the Times Reporter Vol. 8 No. 14 (Nov. 13, 1884).

Bliss pp. 277-281.

23/Kufunua Siri ya Patakatifu

Maandiko ambayo yamekuwa msingi na kiini cha imani ya watu wa marejeo (Waadventista) kuliko yote ni yale yasemayo, “Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakasika” Daniel 8:14. Usemi huu umekuwa ukijulikana sana miongoni mwa wale waliokuwa wakikutazamia kurudi kwake Bwana kuliko karibu. Lakini Bwana hakutokea. Waumini walifahamu kuwa Neno la Mungu halina kasoro, ni lazima walivyoutafsiri unabii, andiko kuna makosa. Lakini basi kosa lilikuwa wapi?

Mungu amewaongoza watu wake katika mkusanyiko mkuu wa marejeo. Na wala asingewaacha wamalizikie gizani, katika huzuni kuu na kushutumiwa kwa aibu; kana kwamba ni wahuni tu wanaotangatanga. Ingawa wengi waliacha msimamo wao wa kuutafsiri unabii, na kukanusha imani ya wale walioambatana nao, lakini wengine hawakuikana imani ambayo inathibitishwa na Maandiko na Roho wa Mungu. Ilikuwa wajibu wao kushikamana na ukweli walioupata. Walijifunza maandiko kwa bidii na kwa maombi ili wapate kugundua kosa lao. Kwa kuwa kwa upande wa kuhesabu miaka ya unabii hawakuona kosa lolote. Waligeukia fundisho lihusulo patakatifu.

Wakagundua kwamba hakuna andiko lolote linalosema kuwa dunia hii ndiyo patakatifu, kama wengi wanavyoamini. Bali waligundua maelezo tele kuhusu patakatifu, asili yake na mahali pake pamoja na huduma zake, kama isemavyo: “Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida zake za ibada, na patakatifu pake pa kidunia. Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya wonyesho ndipo palipoitwa patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo patakatifu pa patakatifu yenye chetezo cha dhahabu sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; na juu yake Makerubi ya utukufu yakikitia kivuli kiti cha rehema; basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari ya vitu hivi kimoja kimoja” Waebrania 9:1-5.

Patakatifu palikuwa ni hema iliyojengwa na Musa, kwa agizo la Mungu kuwa mahali patakatifu pa kukaa Mungu. “Na wanifanyie patakatifu, ili nipate kukaa kati yao” Kutoka 25:8. Hivyo ndivyo Musa alivyoagizwa. Patakatifu na patakatifu pa patakatifu, vyumba hivyo vilitengwa na pazia. Na pazia kama hilo lilifunga mlango wa chumba cha kwanza.

[197]

Patakatifu Pa Patakatifu Mno.

Katika patakatifu palikuwamo kinara cha taa upande wa kusini pamoja na taa zake saba zikiwaka mchana na usiku. Upande wa kaskazini ilikuwako meza ya mikate ya wonyesho. Mbele ya pazia linalotenganisha patakatifu na patakatifu mno, palikuwako madhabahu ya uvumba ulifukizwa kila siku moshi ukipaa pamoja na sala za Waisraeli, mbele za Mungu.

Katika patakatifu mno lilikuwamo sanduku lililonakishiwa kwa dhahabu ambalo lilikuwa likitunza amri kumi za Mungu. Juu ya sanduku kulikuwa na kiti cha rehema kikikabiliwa na makerubi wawili walioumbwa kwa dhahabu. Katika chumba hiki kuwako kwa Mungu kulionekana daima kati ya makerubi. Baada ya Waebrania kukaa Kanani, hema takatifu ilibadilishwa na hekalu lilijengwa na Sulemani, ambayo ingawa ilikuwa jengo la kudumu na kubwa lilifanya kazi ile ile ilikuwa na mfano ule ule; mpaka ilipobomolewa siku za akina Daniel mpaka maangamizo yake na Warumi katika mwaka 70 Ad. Hii ndiyo hema takatifu duniani ambayo tunasoma habari zake katika Biblia. Hema takatifu ya agano la kale. Lakini je, agano jipya haina hema takatifu?

Msomaji na mtafutaji ukweli akifungua kitabu cha Waebrania huona kuwa agano jipya, au agano la pili huzungumzwa katika maneno hayo yaliyosemwa hapo kwanza “hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida zake na ibada, na patakatifu pake pa kidunia”. Tukigeukia kusoma sura iliyopita twasoma, “Basi katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili”, “Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu” Waebrania 8:1-2.

Hapa ndipo inafunuliwa hema takatifu ya agano jipya. Hema takatifu ya agano la kwanza ilifanywa na Musa, hii ya sasa ime-

[198] fanywa na Bwana. Katika hema ya kwanza waliohudumu ni makuhani wa kidunia, katika hii ya pili, Kristo kuhani wetu Mkuu huhudumu akiwa upande wa mkono wa kuume wa Mungu. Hema moja ilikuwa duniani, na nyingine iko mbinguni.

Hema iliyojengwa na Musa ilijengwa kwa kielelezo kile kile cha ile ya mbinguni. Bwana aliagiza akisema, “Sawasawa na hayo yote nikuonyeshayo, mfano wa maskani na mfano wa vyombo vyako vyote, ndivyo nitakavyofanya” “Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano ulioonyeshwa mlimani” “Hema ya kwanza ilikuwa mfano wa wakati ule ambamo ndani yake sadaka na kafara zilitolewa” patakatifu pake, “mfano wa mambo ya mbinguni”. Makuhani walihudumu. “Kwa mfano na kivuli cha mambo ya mbingu”. “Kristo hakuingia patakatifu palipotengenezwa kwa mikono ndio mfano wa patakatifu halisi, lakini aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu” Kutoka 25:9-10. Waebrania 9:23; 8:5; 9:24.

Hekalu la mbinguni ndilo asili ya hema lililojengwa na Musa ikiwa mfano. Uzuri wa hema la duniani ulionyesha mfano wa utukufu wa hekalu la mbinguni mahali ambapo Kristo anahudumu kwa ajili yetu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ukweli wa hekalu la mbinguni na wokovu wa mwanadamu ulifundishwa hasa kwa huduma zilizofanyika katika hema takatifu la hapa duniani.

Vyumba Viwili.

Mahali patakatifu pa mbinguni palionyeshwa kwa njia ya vyumba viwili vya patakatifu pa duniani. Yohana alionyeshwa hekalu la Mungu mbinguni. Aliona “taa saba zikiwaka mbele ya kiti cha enzi” alimwona malaika akiwa na “chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu iliyo mbele ya kiti cha enzi” ufunuo 4:5; 8:3. Hapa nabii aliona chumba cha kwanza, yaani patakatifu pa mbinguni. Huko aliona taa saba, na madhabahu ya dhahabu, ambayo ni kama vile vya hema takatifu ya duniani, yaani kinara cha taa na madhabahu ya uvumba.

Tena, “Kisha hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa na sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake. Sanduku hili lilionekana ndani. Katika hema takatifu ya dunia, ni ndani ya

patakatifu mno, mlimo kuwa na sanduku lenye amri za Mungu.” Ufunuo 11:19.

Kwa hiyo wale wanaojifunza habari hizi wanapata ushahidi wa Biblia kuwa kuna hema takatifu huko mbinguni. Yohana asema [199] kuwa aliliona huko mbinguni.

Katika hekalu la mbinguni, huko katika patakatifu mno, kuna sheria ya Mungu. Sanduku linalotunza sheria ya Mungu limefunikwa na kiti cha rehema, ambapo Kristo anaombea kwa ajili ya damu yake, akitushughulikia sisi, wenye dhambi wa dunia yetu. Hizi haki na rehema hukutana katika mpango wa wokovu. Muungano huu huistaajabisha mbingu kabisa, yaani Haki na Rehema hukutana. Hii ndiyo siri ya rehema ambayo malaika hupenda kuchungulia; kwamba Mungu anaweza kuwa mwenye haki wakati akimhesabia mwenye dhambi atubuye haki; na kwamba Kristo aliwaza kushuka chini kabisa na kuwainua watu kutoka katika uharibifu na kuwavika vazi la haki yake mwenyewe.

Kazi ya Kristo kama mtetezi au mwombezi wa wanadamu, inaonyeshwa hivi katika Zekaria. “Naye atalijenga hekalu la Bwana, naye atauchukua huo utukufu, ataketi akimiliki katika kiti cha enzi, na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili” Zekaria 6:12,23.

“Atalijenga hekalu la Bwana” Kristo ndiye msingi na mjenzi wa kanisa la Mungu, anakuwa hivyo kwa njia ya kafara yake na maombezi yake. “Naye Kristo Yesu mwenyewe ndiye jiwe la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana” Waefeso 2:20-21. “Kwake yeye aliyetupenda na kutuocha dhambi zetu katika damu yake Utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele amina” Ufunuo 1:5-6.

“Naye atakaa na kutawala na kuwa kuhani katika kiti chake cha enzi. Ufalme wa utukufu bado haujaanzishwa. Bado, mpaka kazi yake ya uombezi itakapomalizika, ndipo Mungu atampa ufalme usiokuwa na mwisho” Luka 1:33. Kristo sasa anakaa pamoja na Baba katika kiti cha enzi, akiwa Kuhani. Akiwa katika kiti cha enzi ndiye huyo aliyeyachukua masikitiko yetu yote, na kuchukua huzuni zetu. “alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, bila kufanya dhambi, ili aweze kuwasaidia wao wanaojaribiwa” Isaya 53:4; Waebrania 4:15;2:18. Mikono iliyojeruhiwa, mwili uliochomwa mkuki, na miguu iliyochohubuliwa huwaombea wanadamu walioanguka, am-

bao ukombozi wao umegharimu gharama ya jinsi hiyo. “Na shauri la amani litakuwa kati yao wawili” Upendo wa Baba ndio msingi wa ukombozi kwa wanadamu waliopotea. Yesu alisema kwa wanafunzi wake, “Baba mwenyewe awapenda ninyi” “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee ...” Yohana 16:27; 2Kor. 5:19; Yoh. 3:16.

[200]

Siri ya Hema Takatifu Yadhihirika

“Hema takatifu” ya kweli iliyoko mbinguni, ndiyo hema takatifu ya agano jipya. Kristo alipokufa huduma ambazo zilikuwa kivuli tu, zilikoma. Wakati Daniel 8:14 ilipotimizwa kama ilivyoamuriwa, patakatifu panapotajwa lazima pawe pale pahusupo agano jipya. Hivyo basi unabi unaposema “hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa” huzungumzia patakatifu pa mbinguni.

Lakini kutakaswa kwa patakatifu humaanisha nini? Je, inawezekana kuwa ni kitu mbinguni kinachohitajika kutakaswa? Katika Waebrania 9 utakaso wa patakatifu na duniani na pa mbinguni kumeelezwa dhahiri. “Na katika Torati karibu vitu vyote husafirishwa kwa damu, na pasipo damu hakuna ondoleo. Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo(damu za wanyama); lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo.” Waebrania 9:22-23, yaani damu ya thamani ya Kristo.

Kutakaswa kwa Patakatifu

Utakaso kwa kweli lazima utimizwe kwa damu ya Kristo. “Pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo” Ondoleo au kuweka dhambi mbali ndiyo kazi inayotakiwa kukamilishwa.

Lakini dhambi na mbingu huhusianaje? Jambo hili litaeleweka kwa kuchunguza huduma iliyokuwa ikifanyika katika patakatifu pa duniani, jinsi makuhani walivyokuwa wakihudumu. Waebrania 8:5.

Huduma ya patakatifu pa duniani ilikuwa na sehemu mbili. Makuhani walihudumu kila siku katika patakatifu wakati ambapo kuhani mkuu alihudumu mara moja kwa mwaka katika patakatifu mno. Huduma hiyo ya mara moja kwa mwaka iliitwa huduma ya

upatanisho, ambayo ilihusu utakaso wa patakatifu. Siku kwa siku mwenye dhambi aliyetubu alileta sadaka yake, akaweka mikono yake juu yake, akaungama makosa yake, ambayo ni sawa ana-hamisha dhambi zake na kuziweka kwa sadaka hiyo isiyo na hatia. Kisha mnyama huyo wa sadaka alichinjwa. “Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu” Lawi. 17:11. Sheria ya Mungu iliyovunjwa ilidai uhai wa mvunjaji. Damu huwa badala ya uhai wa mwenye dhambi ambaye hatia yake imechukuliwa na yule mnyama wa sadaka. Basi kuhani alichukua damu hiyo mpaka patakatifu akainyunyiza mbele ya pazia, ambalo hukinga sheria ya Mungu iliyovunjwa. Kwa huduma hiyo dhambi iliamishwa na kuwekwa katika patakatifu. Wakati mwingine damu haikupelekwa katika patakatifu, ila kuhani aliila nyama ya sadaka. Mambo yote mawili, yaani kunyunyiza damu na kula nyama, yalifananisha jambo moja tu, ndiyo kuihamisha hatia kutoka kwa mwenye hatia na kuiweka katika patakatifu. Kazi hiyo iliendelea daima mwaka mzima. Dhambi za Waisraeli zilihamishwa namna hiyo na kuwekwa katika patakatifu, na hiyo ilikuwa kazi ya lazima ya kuhamisha dhambi zao.

[201]

Siku Kuu ya Upatanisho

Kuhani mkuu aliingia katika patakatifu mno mara moja kwa mwaka ili kutakasa patakatifu. Mbuzi wawili waliletwa na kupigiwa kura. Kura moja kwa Bwana na kura moja kwa Azazeli. Mbuzi wa Bwana alichinjwa kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya watu. Na kuhani alichukua damu akaingia patakatifu mno, akainyunyiza kwenye kiti cha rehema na juu ya madhabahu ya uvumba. “Na haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. Na yule mbuzi atachukua juu yake uovu wao wote, mpaka nchi isiyo watu; naye atamwacha mbuzi jangwani.” Law. 16:21-22.

Huduma hiyo ilikusudiwa kuwaonyesha Waisraeli utakatifu wa Mungu, na jinsi anavyoichukua dhambi. Kila mtu alitakiwa kujitakasa kwa njia ya kujichunguza wakati huduma hii inapokuwa ikiendeshwa. Kazi zote na shughuli ziliachwa kabisa, na Waisraeli

walitumia siku hiyo katika ibada na maombi, hali wakifunga na kujipeleleza mioyo yao na kuungama.

Damu ya kafara ilikubaliwa badala ya mwenye dhambi kufa, lakini hatia ya dhambi haikufutwa kwa njia ya damu ya mnyama, ila ilihamishwa mpaka katika patakatifu. Kule kutoa damu mwenye dhambi alikiri madaraka ya sheria, akaungama kuwa amevunja sheria, na akaamini na kuonyesha imani juu ya mkombozi atakayekuja, ambaye anafananishwa kwa mfano wa huduma hiyo. Walakini alikuwa hajafunguliwa kabisa atokane na hukumu ya kuvunja sheria. Siku ya upatanisho kuhani mkuu akiisha kupotea sadaka ya watu, aliingia patakatifu mno. Alinyunyiza damu ya sadaka hiyo juu ya kiti cha rehema moja kwa moja kwenye sheria, ili kuiridhisha kwa kule kuvunjwa kwake.

[202] Halafu kama mwombezi alizichukua dhambi zote juu yake kutoka patakatifu. Wakati anapoweka mikono yake juu ya yule mbuzi wa Azazeli huzihamisha dhambi hizo na kuziweka juu ya mbuzi. Basi mbuzi huzichukua zote. Ndipo kuhesabiwa kana kwamba zimetoweka milele, kutoka kwa watu.

Ukweli wa Mbinguni

Yale yaliyofanyika katika huduma ya patakatifu pa duniani, ambapo palikuwa kivuli cha yale ya mbinguni, ndivyo yalifanyika mbinguni ambako ndiko jambo halisi, katika patakatifu pa huko. Mwokozi wetu baada ya kufufuka kwake na kupaa mbinguni na kuanza kazi yake kama kuhani Mkuu. “Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu”. Ebr. 9:24.

Huduma ya kuhani iliyokuwa ikifanyika katika chumba cha kwanza cha patakatifu, ni mfano wa huduma ya Kristo iliyoanza mbinguni baada ya kupaa kwake. Kuhani katika huduma yake ya kila siku, alileta damu ya sadaka mbele za Mungu, ambayo ni sadaka ya dhambi, pamoja na uvumba uliopaa juu pamoja na sala za watakatifu (Waisraeli). Vivyo hivyo Kristo aliombea damu yake mbele za Baba, kwa ajili ya wenye dhambi, na kuweka harufu njema ya haki yake mwenyewe mbele za Baba, sala za wenye kutubu

makosa yao. Hiyo ilikuwa huduma iliyokuwa ikifanyika katika patakatifu, katika mbingu.

Hapo imani ya wanafunzi ilimfuata alipopaa juu, hapo matumaini yao yaliimarika, “tumaini tulilo nalo kama nanga ya rohani, ambalo ni la hakika lililo imara” yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu amekuwa Kuhani Mkuu hata milele. “Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele”. Ebr. 6:19-20; 9:12.

Kwa muda wa karne kumi na nane kazi hiyo imekuwa ikifanyika mbinguni katika chumba cha kwanza cha patakatifu. Damu ya Kristo imeleta msamaha wa dhambi na kibali cha Baba cha kuwakubali wenye kutubu. Walakini dhambi zao bado zingali katika vitabu. Kama katika mfano ulivyo, kuna siku ya upatanisho kwa mwaka, vivyo hivyo kazi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu haikamiliki mpaka kazi ya kulipa, au kafara ya malipo ifanyike. Kazi hiyo ni ya kuziondoa dhambi katika patakatifu. Hii ilianza wakati siku 2300 zilipomalizika. Wakati huo Kuhani wetu Mkuu aliingia katika patakatifu mno ili kutakasa patakatifu.

[203]

Kazi ya Hukumu

Katika agano jipya dhambi za watu wenye kutubu huwekwa juu ya Kristo, na kuhamishiwa mpaka katika patakatifu pa mbinguni. Na jinsi ilivyokuwa katika patakatifu pa duniani, dhambi zilikuwa zikiihamishwa kutoka patakatifu ili kukamilisha kazi, hali kadhalika na kutakasa patakatifu pa mbinguni patakamilika kwa njia hiyo hiyo ya kuhamisha dhambi kutoka vitabuni. Kazi hii itakuwa kuangalia vitabu na kupima kuona ni nani ametubu kikweli na kuwa na imani kwa Kristo, ili afaidike kulipiwa adhabu yake kwa dhabihu ya Kristo. Kutakaswa kwa patakatifu basi ni kazi ya uchaguzi, kazi ya hukumu, kuona kuwa ni nani anastahili kupata uzima, na ni nani hastahili. Kazi hii itafanyika kabla ya kuja kwa Kristo. Maana ajapo atakuja na ujira wake kumlipa kila mtu kama kazi yake itakavyokuwa. Ufunuo 22:12.

Hivyo wale waliofuata unabii unavyoelekeza, waliona kuwa badala ya Kristo kuja dunia mwisho wa siku 2300, yaani mwaka 1844, aliingia katika patakatifu pa patakatifu mbinguni ili kumaliza

kazi yake ya uombezi na malipo ya adhabu kwa ajili ya dhambi, kabla ya kuja kwake duniani.

Kristo akimaliza kuondoa dhambi za watu wake kutoka patakatifu pa mbinguni mwishoni mwa kazi yake ataziweka zote juu ya Shetani, atakayepata adhabu ya mwisho.

Mbuzi wa Azazeli alipelekwa porini na kuachwa huko. Hali kadhalika Shetani naye atatengwa mbali na Mungu milele, wala asionekane tena, kwa watu wa Mungu. Naye ataangamizwa kabisa, wala hatasalia na aina yoyote ya kumbukumbu. Wakati huo dhambi pia na wenye dhambi pia wataangamizwa milele.

24/Kristo Anafanya nini Sasa?

[204]

Fundisho la patakatifu lilifungua siri ya chungu ule uliowapata. Fundisho hilo liliwafungulia ukweli wote jinsi ulivyo. Huonyesha jinsi mkono wa Mungu ulivyowaongoza watu wa marejeo. Wale waliokuwa wakitazamia kuja kwake Yesu mara ya pili kwa utukufu mwingi, walitiwa chungu kwa kutokurudia kwake, walipoteza matumaini yao kwa Yesu. Sasa katika patakatifu mno walimwona kwa upya Kuhani wao mkuu, ambaye atakuja kama mfalme na Mwokozi wao. Nuru ya fundisho la patakatifu ilianguza giza la wakati uliopita. Wakaona patakatifu ilianguza giza la wakati uliopita. Wakaona wazi wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao. Ingawa hawakuelewa ujumbe waliohubiri, walakini walikuwa sawa.

Makosa hayakutokana na kuhesabu miaka ya unabii, lakini yalikuwa katika mambo yatakayotokea mwisho wa siku 2300. Lakini yote yaliyotabiriwa na unabii yalikuwa yametendeka.

Kristo hakuja duniani, ila aliingia katika patakatifu mno huko mbinguni. “Nikaona katika njozi za usiku na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye” Daniel 7:13.

Kuja huko kulitabiriwa na Malaki pia. “Naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafla; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi”, Malaki 3:1. Kuja kwa Bwana katika hekalu lake kulikuwa kwa ghafla, bila kutazamiwa, kwa watu wake. Hawakumtazamia.

Watu hawakuwa tayari kumlaki Bwana wao. Kulikuwa bado kazi na maandalio yaliyokuwa yakitakiwa.

Kwa jinsi walivyomfuata kuhani wao mkuu kwa imani, katika huduma yake wajibu mpya ungefunuliwa kwao. Ujumbe mwingine ulipasa utolewe kanisani.

Nani Atasimama?

[205] Nabii asema, “Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au nani atakayesimama atakapoonekana yeye? Naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki” Malaki 3:2-3. Watu watakaoishi ulimwenguni wakati maombezi ya Kristo yatakapokoma, lazima wasimame wenyewe bila mwombezi mbele za Mungu. Mavazi yao lazima yawe meupe bila waa, tabia zao zikiwa zimetakaswa kwa damu ya Kristo. Kwa njia ya neema ya Mungu na jitihada zao inawalazimu kuwa washindi katika vita na dhambi. Wakati hukumu ya upelelezi inapoendelea mbinguni, wakati dhambi za watu wanaotubu zinapoondolewa kutoka katika patakatifu, lazima kazi ya kutengana na dhambi ifanyike kwa watu wa Mungu hapa duniani. Kazi hii inaelezwa katika Ufunuo 14. Kazi hii itakapomalizika, wafuasi wa Kristo watakuwa wamekuwa tayari kumlaki Bwana. Ndipo kanisa, ambalo Bwana wetu atalipokea litakuwa “tukufu, lisilo na ila, wala kunyanzi, wala lolote kama hayo”. Waefeso 5:27.

“Haya Bwana Arusi Yuaja”

Kule kuja kwa Kristo katika patakatifu mno, kama Kuhani Mkuu ili kutakasa patakatifu, (Daniel 8:14) na kule kuja kwa Kristo, yaani Mwana wa Adamu kwa mzee wa siku, (Daniel 7:13) na kule kuja kwa Bwana katika hekalu lake, (Malaki 3:11), yote ni tukio moja tu. Hili pia hufananishwa na kuja kwa Bwana arusi kama inavyoelezwa katika mfano wa wanawali wa Mathayo 25.

Katika mfano huo, bwana arusi alipokuja, wale waliokuwa tayari waliingia arusini pamoja naye. Kuja huku kwa bwana arusi hutokea kabla ya arusi. Arusi ni mfano wa kukaribishwa na Kristo katika ufalme wake. Mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ambao ndio makao makuu ya ufalme wake huitwa bibi arusi, mke wa mwana Kondoo. Malaika aliwaambia Yohana, “Njoo huku, nitakuonyesha ule mji mkuu, Yerusalemu ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu”. Ufunuo 21:9-10.

Bibi arusi anafananishwa na Mji Mtakatifu, na wanawali waliokwenda kumlaki Bwana arusi ni mfano wa kanisa. Katika Ufunuo

watu wa Mungu wasemwa kuwa ndio wageni katika karamu ya arusi. Kama ni wageni, hawawezi kuwa bibi arusi. Kristo atapokea kutoka kwa Mzee wa siku huko mbinguni, mamlaka na utukufu na ufalme. Yerusalemu mpya, ambao ni makao makuu “ya ufalme wake, umepambwa kama bibi arusi anayepambwa kwa mumewe”. Baada ya kuupokea ufalme, atakuja kama mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana ili kuwaokoa watu wake, ambao watashiriki karamu hiyo ya arusi ya Mwana Kondoo. Daniel 7:14; Ufunuo 21:2.

Kumngojea Bwana Wao.

[206]

Lile tangazo kwamba, “Haya bwana arusi yuaja, liliongoza watu maelfu kukutazamia kuja kwa Bwana mara moja. Wakati ulipofika Bwana arusi alikuja, lakini sio duniani, bali alifika kwa Mzee wa siku huko mbinguni, katika karamu ya arusi, katika karibisho la ufalme wake. Wale waliokuwa tayari waliingia pamoja naye arusini. Hawakuweza kufika katika mwili, maana wao wako duniani. Wafuasi wa Kristo lazima wamngojee Bwana wao, mpaka atakaporudi kutoka katika arusi.” Luka 12:36. Lakini ni lazima wafahamu kazi yake, na kumfuata kwa kiroho katika imani. Kwa njia hii husema kuwa wanaingia arusini.

Katika mfano, wale waliokuwa na mafuta katika taa zao waliingia arusini. Wale waliovumilia katika giza kuu na uchungu, walingoja nuru zaidi huku wakichunguza Maandiko, walielewa fundisho la patakatifu pa mbinguni, na huduma Kristo aliyochukua. Walimfuata kwa imani katika kazi anayofanya katika patakatifu pa mbinguni. Na wote watakaopokea ukweli wa namna hiyo wakimfuata Kristo kiroho katika imani jinsi anavyofanya kazi yake ya uombezi, huingia arusini.

Kufunga kazi Katika Patakatifu

Katika mfano wa Mathayo 22 hukumu hutangulia arusi. Kabla ya karamu ya arusi kuendeshwa, mfalme aliingia kuona kama wageni wake wote wako sawa; wakiwa na mavazi ya arusi, yaani tabia safi ya kweli iliyooshwa kwa damu ya Mwana Kondo. Ufunuo 7:14. Wote watakao onekana kuwa wanayo mavazi ya arusi, wanakubaliwa ili ashiriki katika ufalme wa Mungu na kuketi katika kiti chake

cha enzi. Kazi hii ya kuchunguza tabia za watu ndiyo hukumu ya upelelezi, ambayo ndiyo kazi ya mwisho katika patakatifu pa mbinguni.

Mambo yote ya watu waliojiita kuwa wakristo tangu vizazi vyote, yatakapokuwa yamekwisha kuchunguzwa na kuamuliwa, ndipo wakati wa rehema na mlango wa rehema utafungwa. Ndipo kwa kifupi ni kwamba, “Na wale waliokuwa tayari kuingia pamoja naye arusini, mlango ukafungwa. Hapo tunapelekwa moja kwa moja mpaka mwisho wa kazi ya kushughulikia wokovu wa mwanadamu. Huo ndio mpango mkuu wa wokovu.”

[207] Katika patakatifu pa duniani, siku ya upatanisho, wakati kuhani mkuu alipoingia katika patakatifu mno, huduma katika chumba cha kwanza cha patakatifu zilikoma. Hali kadhalika Kristo naye alipoingia katika patakatifu mno huko mbinguni ili kukamilisha kazi ya ukombozi, huduma katika chumba cha kwanza ilikoma. Halafu kazi katika chumba cha pili, yaani patakatifu mno; ilianza. Kristo alikuwa amemaliza sehemu moja ya kazi yake ya ukombozi, ndipo alianza sehemu ya pili ya kazi. Bado angali akiombea kwa Baba damu yake iwatakase wenye dhambi.

Jinsi ukweli ulivyo kwamba mlango wa tumaini rehema ambao kwa miaka 1844 ulikuwa wazi, ulivyokuwa ukifungwa, mlango mwingine ulikuwa ukifunguliwa. Msamaha wa dhambi ulikuwa ukitolewa kwa maombezi ya Kristo katika patakatifu mno. Bado kulikuwa na mlango wazi katika patakatifu pa mbinguni, ambako Kristo anawahudumia wenye dhambi.

Sasa itadhihirika maana ya maneno ya Kristo katika Ufunuo yaliyosemwa hasa kwa wakati huu: “Haya ndiyo anenayo yeye aliye Mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunguaye wala hapana afungaye. ‘...Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hakuna awezaye kuufunga’”. Ufunuo 3:7-8.

Wale wanaofuatana na Kristo katika kazi yake ya uombezi watafaidika na kupata ukombozi, ambapo wale wasiojali nuru wanayofunuliwa hawatapata lolote. Wayahudi waliokataa kumwamini Kristo kuwa Mwokozi wao hawakuweza kupata msamaha kwake. Wakati Yesu alipopaa mbinguni na kuwamwagia wafuasi wake karama yake, Wayahudi waliachwa wakitangatanga gizani huku wakiendelea kutoa dhabihu za wanyama na sadaka am-

bazo ni za kazi bure. Mlango ambao watu waliingia kwa Mungu kwa njia ya dhabihu za wanyama ulikuwa umefungwa. Wayahudi walikataa kumtafuta yeye ambaye ndiye mlango, naye angepatikana katika patakatifu pa mbinguni.

Wayahudi hao wasioamini waliweka kielelezo cha kutojali na kutoamini kati ya wakristo wengi ambao hujipumbaza wenyewe wasishughulike kujua kazi ya Kuhani wetu mkuu. Katika mfano wa huduma ya kuhani hapa duniani, Kuhani mkuu alipoingia katika patakatifu mno, Waisraeli wote walitakiwa kukusanyika na kuzunguka patakatifu, huku wakijinyenyekeza mbele za Mungu kwa mioyo yao yote, ili wapate msamaha wa dhambi zao, wasije wakakatiliwa mbali na kusanyiko la watakatifu. Je, ni muhimu kiasi gani kwa huduma ya Kuhani wetu Mkuu sasa ambayo ni kama siku ya upatanisho, jinsi inavyotupasa kuelewa wajibu unaotupasa?

Ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni kuja ulimwenguni wakati wa Nuhu. Wokovu wao ulitegemea jinsi walivyojali ujumbe huo. Mwanzo 6:6-9; Waebrania 11:7. Wakati wa siku za Sodoma ilikuwa ni Luthu na mkewe na binti zake wawili tu, ndio wangepona, na wengine wote waliangamizwa na moto ulitoka mbinguni. Mwa. [208] 19. Hali kadhalika siku za Kristo. Mwana wa Mungu aliwahubiria Wayahudi wasiojali, akasema, “Nyumba yenu mmeachiwa ukiwa”. Mathayo 23:38. Akaingia siku za mwisho, mwokozi alisema, “Wala hawakuipenda ile kweli ili waokoke. Kwa hiyo Mungu atawaletea nguvu ya upotevu ili wauamini uongo”. 2Thes. 2:10-11. Kwa vile wasivyojali neno Lake wala mafundisho yake, Mungu atawaondolea Roho Yake, na kuwaacha waamini uongo ambao wanaupenda. Lakini Kristo bado anawaombea wanadamu, na nuru itatolewa kwa wale wanaoitafuta.

Kupita kwa wakati katika 1844 kulifuatiwa na kipindi kigumu cha majaribu mazito kwa wale walioshikilia imani ya marejeo. Nafuu yao ilikuja tu kwa nuru iliyowaongoza waone umuhimu wa huduma ya patakatifu pa mbinguni. Walipongojea na kuomba waliona kuwa Kuhani wetu Mkuu ameingia katika patakatifu mno ili kuanza kazi ya sehemu ya pili. Wakimfuata kiroho kwa imani, waliongozwa pia kuona kufungwa kwa kazi ya kanisa. Walifahamu kwa dhahiri ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili, nao walijitayarisha kupokea na kutangaza ulimwenguni onyo kuu la ujumbe wa malaika wa tatu wa Ufunuo 14.

25/Sheria ya Mungu Haibadiliki

“Hekalu la Mungu lilifunguliwa huko mbinguni, ndipo sanduku la agano lake likaonekana katika hekalu lake”. Ufunuo 11:19. Sanduku la agano la Mungu jipya liko mbinguni katika patakatifu mno, chumba cha pili cha patakatifu. Katika huduma ya hema takatifu duniani, ambayo ilikuwa mfano wa kivuli cha ile ya mbinguni, chumba hiki kilifunguliwa tu wakati wa siku kuu ile ya upatanisho kwa ajili ya kutakasa patakatifu. Kwa hiyo upatanisho kwa ajili ya kutakasa patakatifu. Kwa hiyo tamko lile lisemalo kuwa hekalu la Mungu lilifunguliwa, na kwamba sanduku la ushuhuda likaonekana, lilikuwa utangulizi wa kuonyesha kuwa patakatifu mno mbinguni palikuwa tayari kufunguliwa katika chumba cha pili ili Kristo, Kuhani wetu Mkuu yuko tayari kuingia na kuanza kazi hiyo mwaka 1844. Watu ambao wangepuatana naye katika huduma hiyo, waliona sanduku la agano lake. Kadiri walivyojifunza juu ya hekalu waligundua kuwa Kristo anabadili huduma na sasa anahudumu mbele ya agano la Mungu.

Sanduku lililokuwa katika hema takatifu hapa duniani lilikuwa na mbao mbili za mawe ambazo zilikuwa zimeandikwa juu yake sheria ya Mungu. Hekalu la Mungu lilipofunguliwa huko mbinguni, sanduku la agano lake lililonekana humo. Sheria hii ilionekana katika patakatifu pa patakatifu iliyonenwa na Mungu na kuandikwa na kidole cha chanda chake juu ya mbao mbili za mawe.

Wale walioelewa fundisho hili walifahamu vyema maneno ya Mwokozi yasemayo: “Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka; yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka” Mathayo 5:18. Sheria ya Mungu ambayo ndiyo mafunuo ya mapenzi yake, na maelezo ya tabia yake, itadumu milele na milele.

Katikati ya mpangilio wa sheria ya Mungu, husimama amri ya Sabato, ambayo ni amri ya nne. Roho wa Mungu aliwaagizia wanafunzi hao Neno la Mungu, wakaona kuwa wameipuuza siku takatifu ya Mungu kwa ujinga wao. Wakaanza kuchunguza sababu za kushika Jumapili, ambayo ni siku ya kwanza ya juma. Hawakuona

mahali popote panapoeleza kwamba Sabato ya siku ya saba imefutwa, wala kubadilishwa. Walikuwa wakitafuta kwa bidii kufanya mapenzi ya Mungu; na sasa wamegundua kuwa kushika sabato ni mojawapo ya mapenzi yake, kwa hiyo wakaishika kwa furaha.

Juhudi nyingi zilifanyika ili kutafuta imani ya watu wa Marejeo. Hakuna mtu aliyekosa kuona kuwa fundisho la patakatifu huko mbinguni linahusiana na madai ya Mungu ya kushika sheria yake pamoja na Sabato. Hii ndiyo ilikuwa siri ya upinzani wa maandiko yaliyokuwa yakionyesha huduma ya Kristo mbinguni, katika patakatifu pa huko. Watu walijitahidi kufunga mlango uliofunguliwa na Mungu, na kufungua mlango uliofungwa na Mungu. Lakini Kristo amefungua mlango wa huduma yake katika patakatifu pa patakatifu. Amri ya nne yaani ya Sabato ilikuwako kati ya sheria za Mungu ikitunzwa huko. Wale waliouamini ukweli huo unaohusu uombezi wa Kristo wa sheria ya Mungu, waligundua kuwa huo ndio ukweli wa ufunuo 14, ambao ni ukweli wa maonyo ya namna tatu utakaowatarisha wenyeji wa dunia juu ya kurudi kwake Yesu. Lile tamko kwamba, “Sasa hukumu yake imekuja ni tangazo la ujumbe wa kweli ambao hauna budi kuhubiriwa mpaka Kristo atakapokoma kuombea watu, naye atakuja kuchukua watu wake kwake. Hukumu iliyoanza katika mwaka 1844 lazima iendelee mpaka mambo ya watu wote yaamuliwe, wale waliokufa na walio hai pia. Itaendelea mpaka mlango wa rehema utakapofungwa kwa binadamu wote.”

[210]

Makusudi watu wawe tayari kusimama hukumuni, ujumbe unawaamuru kwamba, “Mcheni Mungu na kumtukuza” na “Msujudi-eni yeye aliyefanya mbingu na nchi na bahari, na chemichemi za maji” Matokeo ya kuukubali ujumbe huu yamesemwa: “Hapa ndipo penye subira ya watu washikao amri za Mungu na imani ya Yesu” Ufunuo 14:7-12.

Ili kujitayarisha kwa hukumu, watu ni lazima wazishike amri za Mungu, ambazo ndiyo kipimo cha tabia katika hukumu. Paulo asema, “Wote waliokosa wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria ... katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, kwa Kristo Yesu”. “Watendao sheria watahesabiwa haki” Imani ni muhimu kwa kushika sheria ya Mungu. “Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu”. Warumi 2:12-16; Waebrania 11:6; Warumi 14:23.

Ujumbe wa malaika wa kwanza uliwaita watu wamche Mungu na kumsujudia yeye aliye Mwumbaji; wa mbingu na nchi. Kufanya hivyo ni lazima waitii sheria yake. Bila utii hakuna ibada inayompendeza Mungu. “Huku andiko kumpendeza Mungu, kwamba tuzishike amri zake” 1 Yoh. 5:3 Mithali 28:9.

Mwito Kumwabudu Mwumbaji

[211] Wajibu wa kumwabudu Mungu unahusika kwa kuwa yeye ni Mwumbaji. “Njooi tuabudu tusujudu, tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba” Zaburi 95:6; 96:5; 100:3; Isaya 40:25, 26; 45:18.

Katika ufunuo 14 watu wanaitwa ili kumwabudu na kumsujudu Mwumbaji na kushika amri zake. Mojawapo ya amri hizi humwonyesha Mungu kuwa ni Mwumbaji. “Siku ya saba ni sabato ya Bwana Mungu wako Maana kwa siku sita Bwana alizifanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo, akapumzika siku ya saba akaitakasa”. Kutoka 20:10-11. Bwana asema, “Sabato ni ishara Mpate kujua kuwa mimi ni Bwana Mungu wenu”. Ezekieli 20:20. Kama sabato ingeshikwa na watu wote wa ulimwengu, watu wangeelekeza ibada zao kwa Mungu. Pasingalikuwako mtu yeyote aabuduye sanamu, kafiri wala asiyeamini. Kushika Sabato ni ishara ya uaminifu na utii kwa yule aliyeumba mbingu na nchi, na bahari, na chemichemi za maji. “Ujumbe unaowaita watu kumwabudu Mungu na kushika amri zake, hasa huwaita washike amri ya nne, yaani Sabato.”

Mbali na wale washikao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, ujumbe wa malaika wa tatu huonyesha kundi jingine la watu; “Mtu yeyote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu”. Ufunuo 14:9-10. Ni nini kinachomaanishwa na mnyama, sanamu au chapa?

Uthibitisho wa Joka

Unabii ambao mifano hii inatajwa unapatikana tangu katika Ufunuo 12. Joka lililotaka kumharibu Kristo wakati wa kuzaliwa

kwake, yasemekana kuwa ni Shetani (Ufunuo 12:9) alimchochea Herode amwangamize Mwokozi. Lakini mjumbe wa Shetani katika kupingana na Kristo na watu wake katika karne ya kwanza, ilikuwa ni serikali ya Rumi, ambamo ukafiri ulistawi ndani yake kama dini. Kwa hiyo joka kwa upande wa pili ni Rumi ya kikafiri.

Katika Ufunuo 13 kunatajwa mnyama mwingine, “afananaye na chui” ambaye joka alimpa “nguvu zake” “na kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi”. Mfano huu kama unavyokubaliwa na Waprotestanti wengi, ni mfano wa upapa; ambao ulishika utawala uliokuwa ukiendeshwa na serikali ya Rumi. Ule mfano wa Chui unaonekana kuwa; “apewa kinywa chenye kunena maneno makuu ya kufuru. . . akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na masikani yake, nao wakaa mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila jamaa na lugha.” Ufunuo 13:2, 5-7. Unabii huu ambao karibu ufanane na ule wa Danieli 7 wa pembe ndogo, bila shaka unaeleza habari za Upapa wa Rumi. [212]

Walimpa uwezo wa kufanya kazi yake “miezi arobaini na miwili”- Miaka mitatu na nusu au siku 1260 za Daniel 7, wakati ambao uwezo wa papa utawatesa watu wa Mungu. Muda huu kama unavyoelezwa katika sura zilizopita ulianza na uwezo wa upapa katika A.D 538 mpaka ukamalizika mwaka 1798. Wakati huo ndipo uwezo wa upapa ulipopata pigo la mauti, na utabiri ukatimia kwamba; “Mtu akichukua mateka atachukuliwa mateka.”

Kuinuka kwa Uwezo Mpya

Wakati huu mfano mwingine uliletwa. “Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwanakondoo” Ufunuo 13:11. Taifa hili hali-fanani na mataifa yaliyoelekezwa katika sura zilizotangulia, yaani mifano iliyoendelezwa hapo mwanzoni. Mataifa makuu yaliy-outawala ulimwengu yalielezwa katika unabii wa Danieli kuwa kama wanyama wakubwa wa mawindo, waliotokea katika bahari kuu, wakati “pepo za mbinguni zilipovuma juu yake” Daniel 7:2. Katika Ufunuo 17:15 malaika alielekeza kwamba yale maji uliy-oyaona ni jamaa na makutano na mataifa na lugha. Upepo au dhoruba ni mapambano au alama ya vita. Pepo nne zishindanazo juu ya

bahari ni mapambano ya kutisha ya ushindi na mapinduzi ambayo falme zimejipatia utawala.

Lakini mnyama aliye na pembe zifananazo na za mwanakondoo alionekana akiinuka “kutoka katika nchi” Badala ya kushinda utawala mwingine ili yeye apate kutawala, taifa linaloelezwa kwa mfano huu liliinuka katika nchi ambayo haikuwa na watu. Taifa hilo lilistawi katika amani na utulivu. Taifa hili lazima litafutwe katika bara la magharibi.

Katika mwaka 1798 ni taifa gani lililoinuka na kustawi likawa na nguvu, ambalo lilivuta macho ya ulimwengu mzima kuelekea? Ni taifa moja tu, moja peke yake, ndilo linalopatana na unabii huu — yaani Marekani (United States of America). Maneno ya Maandiko Matakatifu ndiyo yamelieleza taifa hili karibu na kila kitu bila kasoro; jinsi kuinuka kwake kutakavyokuwa. Mwandishi fulani mashuhuri akiandika siri ya kuinuka kwa taifa hilo kutoka mahali pasipokuwa na watu, asema, “Tumekuwa taifa kuu, katika hali ya ukimya sawa kama mbegu inavyokuwa kimya kimya”. Gazeti la Ulaya, likiandika habari za Marekani katika mwaka 1850, lilisema, “Marekani imezuka kimya kimya” “kila siku huongezeka kuwa maarufu” kwa uwezo na kiburi.

“Ana pembe mbili kama mwanakondoo”.

- [213] Pembe kama mwanakondoo, huonyesha hali ya ujana, bila madhara, na hali ya uungwana. Baina ya wakristo waliokimbilia Marekani mara ya kwanza, kutoka katika mateso ya Ulaya na shuruti za dini, wengi waliazimu kuwa na uhuru wa dini, na uhuru wa utu binafsi. Tangazo la kujitawala lilifafanua kuwa, “watu wote waliumbwa sawa, wakapewa haki ya uhuru wa kila mtu, kujiamulia mambo yanayomhusu yeye binafsi, kama maisha anayotaka kuishi, uhuru bila kutegemea mtu mwingine amwamulie mambo yake, na kufuata furaha yake. Katiba ya kujitawala iliweka wazi mambo hayo ya kila mtu kufuata matakwa yake. Kwamba utawala hautakuwa katika mikono ya mtu mmoja, ila utakuwa katika mikono ya wajumbe wanaowakilisha watu. Uhuru wa dini uliotolewa, kuwa kila mtu afuate dini anayopenda, sio kulazimisha. Serikali na Uprotestanti vikawa ndiyo msingi wa taifa hilo. Hivyo ndio ilikuwa siri ya kustawi na kufanikiwa kwa taifa. Mamilioni ya watu wamehamia huko, na Marekani imekuwa mojawapo ya mataifa makuu yenye nguvu kabisa na ustawi wa ajabu duniani.

Tofauti ya Ajabu

Lakini mnyama mwenye pembe mfano wa mwanakondoo alinena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia yote na wote wakaao ndani yake wamsujudu mnyama wa kwanza ambaye jeraha la mauti lilipona. Akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi” Ufunuo 13:11-14.

Pembe za mfano wa mwanakondoo na joka hunena tofauti. Utabiri kwamba, “akanena kama joka?” na atumia uwezo wote wa mnyama wa kwanza, huonyesha roho ya kutokubaliana na ya mateso iliyoonyeshwa na joka na mnyama chui. Na elezo kwamba, mnyama kama mwanakondoo “awafanya wakaao katika nchi kumsujudu mnyama wa kwanza” huonyesha kuwa uwezo wa taifa hili utatumika kuwalazimisha watu kuuheshimu upapa.

Tendo hilo litakuwa kinyume cha katiba yao na kiapo chao walivyoapa wakati walipotunga katiba ya serikali. Katiba ilisema kuwa, bunge halitunga sheria yoyote kuambatana na dini, au kuzuia jambo lolote kuhusu dini. Wala kujaribu kutawala dhamiri za watu au kuingilia uhuru wao. Dini haitakuwa kipimo cha kumweka mtu yeyote katika madaraka ya utawala, katika nchi ya Marekani. Kukiuka miiko hiyo, kama ilivyokubaliwa hapo mwanzo, kunaonyeshwa katika mfano huu. Mnyama huyu mfano wa mwanakondoo mwenye pembe mbili; aliyeonekana kuwa safi, mwungwana, asiye na madhara, huonena kama joka.

“Akiwaambia wote wakaao juu ya nchi wamfanyie sanamu mnyama” Hapa inaonyeshwa aina ya serikali ambayo itatunga sheria katika bunge lake la serikali ya watu, ambavyo kutakuwa tofauti ya kushangaza katika nchi ya Marekani. Hiyo inaonekana kuwa hiyo katika Marekani.

[214]

Lakini Sanamu kwa Mnyama Ni Nini? Ilitendekaje?

Wakati kanisa la kwanza lilipopotoka, lilitafuta msaada katika serikali ili liweze kutekeleza mambo yake ya kanisa. Matokeo yakawa upapa kutawala serikali na kutumia serikali katika kuwaadhibu wale wasiokubaliana na taratibu na imani yao. Vivyo hivyo, ili

Marekani ipate kutengeneza sanamu kwa mnyama, lazima uwezo wa dini utawale serikali ili kanisa liweze kutumia serikali kutekeleza mambo yake.

Makanisa ya Kiprotestanti ambayo hufuata nyayo za kanisa la Rumi, yameonyesha hamu yao ya kulazimisha watu katika mambo yao, yaani wameonyesha hamu ya kuondoa uhuru wa dhamiri za watu. Mfano mmoja ni yale mateso wanayopata watu wasiokubaliana na Kanuni za imani ya Kanisa la Anglikana (Church of England).

Mateso hayo yamekuwa ya kudumu. Wakati wa karne ya kumi na sita na kumi na saba hakuna mpinzani yoyote wa kanuni za imani ya kanisa la Uingereza aliyepewa adhabu ya kutozwa faini au kifungo au mateso yoyote au kifo. Uasi uliongoza kanisa la kwanza kuomba msaada wa serikali, na hii ilitayarishia upapa njia. “Mnyama” Paulo alisema “Utakuja ukengeufu. Akafunuliwa yule mtu wa kuasi” 2Thes. 2:3.

Biblia husema, “Siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiowatii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake” 2Tim. 3:1-5. “Basi Roho anena wazi wazi ya kwamba nyakati za mwisho, wengine watajitenga na imani, wakisikiliza Roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani”. 1Tim. 4:1.

“Na katika madanganyo yote ya udhalimu, kwa sababu hawakukubali kuipenda kweli wapate kuokolewa. Watapokea nguvu ya upotevu wauamini uongo”. 2Thes. 2:10-11. Wakati hali hii ikifikiwa, na matokeo yake yale yatatokea kama katika karne za kwanza ilivyokuwa.

[215] Watu wengi huamini kuwa kwa kuwa kuna tofauti nyingi katika makanisa ya Kiprotestanti, hakuna unguano lolote la makanisa litakalotokea. Lakini kumekuwa na msukumo mkubwa katika makanisa hayo na kutaka muungano wa makanisa uwepo. Mwingano huo ukipatikana, mazungumzo ya mambo ambayo hawakubaliani, watayaacha katika juhudi za kutaka mwingano, itakuwa ni hatua ya kuelekea kutumia nguvu.

Wakati makanisa makubwa ya Marekani, yakikubaliana kamili katika jambo hilo, kadiri wanavyoamini watashawishi serikali iwaunge mkono kwa kutoa amri ya kulazimisha. Hapo basi itakuwa Waprotestanti wa Marekani wamefanya sanamu kwa yule mnyama; ambaye mkuu wa kanisa la Rumi na hapo adhabu kwa wale wasiokubaliana na mambo hayo itatolewa kisheria.

Mnyama na Sanamu Yake

“Mnyama wa pembe mbili kama mwanakondoo aliwaamuru wote, wadogo kwa wakubwa matajiri kwa maskini, walio huru kwa watumwa, wapokee alama ya mnyama katika mkono wake wa kuume au vipaji vya nyuso zao ya jina lake” Ufunuo 13:16-17. Malaika wa tatu hutoa onyo kuwa “Mtu awaye yote akimsujudia huyo mnyama na sanamu yake, na kupokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadabu ya Mungu”.

“Mnyama” ambaye ibada yake inalazimishwa ni yule mnyama chui, wa ufunuo 13, yaani papa. Sanamu ya mnyama inamaanisha Uprotestanti uliopotoka ambao wakati makanisa ya Kiprotestanti yatakapotafuta msaada wa serikali ili kutekeleza mambo ya kanisa, watafikia kipeo. Alama ya mnyama bado haijatekelezwa.

Wale washikao amri za Mungu watatofautiana na wale waabuduo mnyama na sanamu yake, na kupokea chapa yake. Kushika sheria ya Mungu, kwa upande mmoja; na kuivunja kwa upande mwingine, kutapambanua baina ya wamwabuduo Mungu, na wamwabuduo mnyama.

Tabia maalum ya mnyama na sanamu yake ni kuvunja amri za Mungu. Daniel asema Kuhusu pembe ndogo, yaani upapa, “Naye ataazimu kubadili majira na sheria” Daniel 7:25. Paulo naye anena kuhusu uwezo huo huo. “mtu wa kuasi” (2Thes. 2:3) ajiinuaye juu ya Mungu. Kule kubadili amri za Mungu ndilo jambo la kujiinua juu ya Mungu ambalo papa ametenda. Mtu yeyote anayeendelea kushika amri hizo jinsi zilivyobadilishwa, huwa anatoa heshima yake kwa papa, na sheria ya papa.

Hivyo ndivyo alama ya utii kwa papa, na wala sio kwa Mungu.

[216]

Mapapa wamejaribu kubadili sheria ya Mungu. Amri ya nne, yaani Sabato, imebadilishwa na kuweka siku ya kwanza badala yake,

na watu wanaishika badala ya Sabato ya siku ya saba. Badiliko hilo limefanywa kwa makusudi kabisa. “ataazimu kubadili majira na sheria” Kubadili amri ya nne ya amri za Mungu, hutimiza kabisa unabii. Hapo ndipo uwezo wa papa hujiinua dhahiri juu ya Mungu.

Wanaomwabudu Mungu watajulikana wazi kwa vile vile watakavyoishika amri ya nne, yaani Sabato, ambayo ni ishara ya uwezo wake wa kuumba. Wanaoabudu mnyama watajulikana kwa juhudi yao ya kuharibu ukumbusho wa uwezo wa Mungu wa kuumba; nao wataiheshimu siku iliyowekwa na kanisa la Rumi. Ilikuwa kule kushika Jumapili kama siku ya Bwana, ndipo papa alitetea na kudai kwa kiburi kuwa siku hiyo iheshimiwe na watu wote. Lakini Biblia inasema kuwa siku ya saba ndiyo Sabato ya Bwana. Kristo alisema, “Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato” Marko 2:28. Soma pia Isaya 58:13; Mathayo 5:17-19. Madai yanayodaiwa na watu kuwa Kristo alibadili Sabato ni uongo, yanakanushwa na yeye mwenyewe.

Kimya Kabisa Katika Agano Jipya

Waprotestanti wanakiri kabisa kuwa katika Agano Jipya hakuna neno lo lote linalotaja kuwa amri ya nne, yaani sabato imeondolewa, wala neno la kushika Jumapili kama siku takatifu ya kuabudu.

Mpaka wakati Kristo alipokufa msalabani, hapakuwako badi-liko lolote kuhusu siku, kama maandiko yasemavyo. Mitume hawakubadili chochote kuhusu kuondoka sabato ya siku ya saba, na kuweka siku ya kwanza badala yake.

Kanisa la Rumi linakiri kuwa wao ndio walibadili sabato, na kusema kuwa Waprotestanti wanapokubali kushika siku ya Jumapili kama siku ya ibada, wanayatambua mamlaka yao. Wao husema: “Sheria ya zamani, yaani sabato, ndiyo iliyotakaswa; lakini kanisa letu likiagizwa na Yesu na Roho wa Mungu, limebadili sabato ya Jumamosi na kuweka Jumapili badala yake. Sasa tunatakasa siku ya kwanza, wala sio siku ya saba. Hivyo sasa Jumapili ndiyo siku ya Bwana”

[217] Ili kuonyesha uwezo au mamlaka yao, wafuasi wa Rumi huandika kwamba kule kubadili sabato na kwenda jumapili badala yake, ambavyo hata Waprotestanti wanakubali kushika, huonyesha

uwezo wa kanisa kuamuru sikukuu na kuamuru ushikaji wake chini ya dhambi.

Basi kubadili sabato kuna maana gani basi, isipokuwa kuonyesha uwezo au alama ya mamlaka ya kanisa la Rumi? Hivyo ndivyo “alama ya mnyama”

Kanisa la Rumi halijaacha madai yake ya ukuu. Ulimwengu na makanisa ya Kiprotestanti wanapokubaliana na sabato bandia iliyowekwa na Rumi, na kukataa sabato ya Biblia, hukiri kuwa kanisa la Rumi lina uwezo kamili. Kwa kufanya hivyo wanapuuza kanuni zile zilizawatenganisha na Warumi, ambazo husema, “Biblia na Biblia tu, ndiyo dini ya Waprotestanti” Kwa kadri msukumo wa Jumapili unavyozidi kusonga mbele, na kuungwa mkono na wengi, baadaye makanisa yote ya Kiprotestanti yatajikuta yako chini ya bendera ya Rumi.

Warumi husema kuwa kule kushika jumapili kwa Waprotestanti huonyesha kuwa wanaheshimu Rumi na kukubaliana nayo. Kutaka msaada wa serikali ili kulazimisha watu washike Jumapili kutafanya sanamu kwa mnyama. Hivyo basi amri ya jumapili katika Marekani itakuwa amri ya kuabudu mnyama na sanamu yake.

Wakristo wa zamani walishika jumapili wakidhani kuwa walikuwa wakishika sabato ya Biblia, na bado jumapili iliwekwa na Mungu. Watu hao Mungu hupokea ibada zao na uaminifu wao. Lakini wakati amri ya jumapili itakapowekwa kisheria, ulimwengu utaangazwa na kuiona sabato ya kweli, ndipo hapo wale watakaoasi amri ya Mungu na kuendelea kushika jumapili iliyowekwa na Rumi, watakuwa wanaheshimu Rumi badala ya Mungu. Watakuwa wanamwabudu mnyama na sanamu yake. Basi watakuwa wanaipokea ishara ya Rumi — yaani alama ya mnyama. Bado mpaka amri ya jumapili itakapowekwa, ndipo watu watachagua kati ya kumtii Mungu au mwanadamu, na wale watakaoendelea kumwasi Mungu watapokea “alama ya mnyama”.

Onyo la Malaika wa Tatu

Onyo la kutisha mno, ambalo halijasikika katika sikio la mwanadamu ni lile linalotolewa na malaika wa tatu. Watu hawataachwa gizani wasijue mambo haya muhimu. Walimwengu wataonywa kabla Mungu hajaleta hukumu zake, ili kuwapa nafasi

ya kuepukana na hukumu hivo. Malaika wa kwanza anawatangazia watu kila taifa na kabila na jamaa, na lugha. Onyo la malaika wa tatu litahusu watu wote pia kama tangazo la malaika wa kwanza. Litatangazwa kwa sauti kuu ili wote wapate kutaharuki, katika ulimwengu mzima.

Watu wote watagawanyika katika makundi mawili, yaani wale washikao amri za Mungu na imani ya Yesu; na wale wamwabuduye mnyama na sanamu yake, ambao wamepokea alama yake. Kanisa na serikali wataungana pamoja ili kulazimisha watu wote kupokea alama ya mnyama. Walakini watu wa Mungu hawataipokea. Nabii aliwaona wenye “kushinda na kujiepusha na yule mnyama na sanamu yake na alama ya jina lake, wanasimama katika bahari ya kioo wakiwa na vinubi vya Mungu” Ufunuo 15:2.

Marejeo:

G. A Townsend, *The New World compared with the Old* p. 462.
Dublin Nation.

George Elliott, *The Abiding Sabbath* p. 184.

A.E. Waffle — *The Lord’s Day* pp. 186-188.

Catholic Catechism of Christiana Religion

Henry Tuberville, *an abridgement of the Christian Dctrine* p. 58.

Mgr Segur, *Plain Talk the Protestantism of Today* p. 213.

Matengenezo ya Sabato katika siku za mwisho yalitabiriwa katika Isaya “Bwana asema hivi, shikeni hukumu, mkatende haki; kwa maana wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa. Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye sabato asizivunje, auzuia mkono wake usifanye uovu wowote. Na wageni, walioandamana na Bwana ili wamhudumu na kulipenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake; kila aishikaye sabato asivunje, na kulishika sana agano langu; Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala” Isaya 56:1-2,6-7.

Maneno haya yanahusu ukristo. Kama inavyoonyesha kwenye fungu la nane. Hapa ni kivuli cha mkusanyo wa mataifa kwa njia ya Injili kinavyoonyeshwa, wakati watumishi wa Mungu watakapotawanyika duniani kuhubiri habari njema.

Bwana anaamuru akisema, “Ufungu huo ushuhuda, ukatie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu” Isaya 8:16. Muhuri wa sheria ya Mungu unapatikana katika amri ya nne. Ni amri hii pekee yake kati ya hizo kumi inayotaja jina na cheo cha mtoa sheria. Sabato ilipobadilishwa na mapapa, muhuri iliondolewa kutoka kwenye sheria. Wanafunzi wa Yesu wanatakiwa waurudishe muhuri huo kwa njia ya kuitunza sabato kama ukumbusho wa Mwumbaji na alama ya uwezo wake.

Agizo linatolewa likisema, “Piga kelele usiache, paza sauti kama tarumbeta, uwahubiri watu wangu kosa lao. Watu ambao Bwana huwaita, ‘Watu wangu’, lazima waonyeshwe uasi wao, ambao hujiona kuwa wenye haki katika kumtumikia Mungu. Lakini makemeo ya kutisha na maonyesho yanapotolewa na mchunguza mioyo hujikuta kuwa wanavunja sheria ya Mungu”. Usata 58:1-2,

Nabii huonyesha sheria ambayo imeachwa bila kujaliwa. “Utainua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa mwenye kutengeneza mahali palipobomoka, na mwenye kurejeza njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako usiihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya

utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu yenye heshima; ukitukuza kwa kutozifanya njia zako mwenyewe, na wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana” Isaya 58:12-14.

[220]

Mabomoko yaliyofanywa katika sheria ya Mungu wakati Sabato ilipobadilishwa, na uwezo wa mapapa. Lakini wakati umefika ambapo lazima kuziba mabomoko hayo.

Sabato ilishikwa na Adamu katika bustani ya Edeni alipokuwa hajaanguka, tena aliendelea kuishika hata alipokuwa ameanguka na kutubu, akiwa amefukuzwa katika bustani. Ilishikwa na wazee wote, tangu Habili mpaka Nuhu, Ibrahimu, mpaka Yakobo. Bwana alipowaokoa watu kutoka Misri, aliitangaza Sabato mbele ya makutano, pamoja na sheria nzima.

Sabato ya Kweli Ilishikwa Daima

Tangu siku hiyo mpaka leo Sabato imekuwa ikishikwa. Ingawa mtu wa dhambi amefaulu kuikanyaga sabato ya Bwana chini ya miguu yake, walakini watu waaminifu wa Mungu wamekuwa wakitunza kwa siri hapa na pale. Tangu wakati wa matengenezo, watu wa kila kizazi wamekuwa wakitunza wakati wote.

Ukweli huu wa sabato pamoja na Injili ya milele vitawapambanua watu wa kweli wa Mungu, na kanisa la kweli na wapotovu mpaka Kristo arudi. “Hapa ndipo penye uvumilivu wa watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu” Ufunuo 14:12

Wale waliopata nuru ya hema takatifu na huduma zake na kuona sheria ya Mungu walijazwa na furaha na kuona jinsi ukweli unavyoingana bila kasoro. Walitamani kuwafikishia wakristo wote nuru hii. Lakini ukweli huu wa aina mbali mbali haukukubaliwa na walimwengu; hasa wale wanaojiita kuwa ni wafuasi wa Kristo.

Wakati madai ya Sabato yaliposisitizwa wengi walisema “Tumekuwa tukishika Jumapili tangu zamani, na kwamba baba zao walitunza pia, na watu wengi watauwa walikufa wakifurahi katika utunzaji wake. Kuanza kutunza sabato hii mpya kutatutenga na waengine ulimwenguni. Kikundi kidogo cha watu wanaotunza Sabato ya Jumamosi watafanya nini kulinganisha watu wote wanaoshika Jumapili katika ulimwengu?” mambo kama hayo yalifanywa na Wayaudi pia siku za Kristo, ndiyo sababu walimkataa

na mafundisho yake. Hali kadhalika na wakati wa Luther, wafuasi wa Rumi walibisha wakisema kuwa watu wengi watauwa wamefia katika imani ya Rumi, kwa hiyo dini hiyo ilitosha kabisa, haina hitilafu. Mambo kama hayo ndiyo yatakayopinga maendeleo yote ya matengenezo katika imani.

Wengi walidai kuwa kushika siku ya Jumapili kumeenea sana duniani, na kumekuwa kawaida ya makanisa kwa karne nyingi. Lakini upinzani wa jumapili ulielezwa kuwa sabato ni ya zamani kabisa, nayo imeshikwa hivyo tangu zama za kale. Ni ya zamani, umri wake ni kama wa ulimwengu. Ilianzishwa na Mzee wa siku, yaani Mungu.

Mbali na maelezo ya Biblia, wengi hubisha na kusema “kwa nini watu wengi wakuu, maarufu hawaitambui sabato hiyo? Ni wachache tu wanaoishika. Haiwezekani kwamba ninyi mkawa sawa na wengine wote wakakosea; na hali ni watu wataalamu, wenye ujuzi mkubwa!” [221]

Ili kukomesha mabishano hayo ilikuwa lazima kuchunguza maandiko Matakatifu kuhusu mpango wa Mungu na jinsi anavyotenda watu katika vizazi vyote. Sabato inayofanya Mungu asiwachague watu wakuu na wenye elimu, ili kuongoza watu wake, ni kwa kuwa wao hawamtegemei, ila tu hutegemea ukuu na elimu yako, na kujiona kuwa hawana haja ya kuongozwa naye. Watu ambao wanao ujuzi mdogo, huitwa mara kwa mara ili waeneze neno lake, si kwamba kutoelimika kwao ndiko kunampendeza Mungu, bali katika hali yao huwa hawana la kujisifia wasifundishwe na Mungu. Unyenyekevu wao na utii huwafanya kuwa wakuu.

Historia ya Waisraeli wa kale inatuwekea kielelezo cha kushangaza sisi wa Marejeo. Mungu aliwaongoza watu wake wa Marejeo sawasawa alivyowaongoza Waisraeli kutoka Misri. Kama wale waliofanya kazi mwaka 1844 wangaliupokea ujumbe wa malaika wa tatu, na kuutangaza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ulimwengu ungekuwa umeonywa zamani, na Kristo angekuwa amekuja kuokoa watu wake.

Siyu Mapenzi ya Mungu

Hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba Waisraeli watangetange jangwani miaka arobaini. Alikuwa na nia ya kuwaongoza moja kwa

moja mpaka Kanaani na kuwamilikisha huko, wakiwa watakatifu wenye furaha. Lakini, “hawakuweza kuingia huko kwa ajili ya kutokuamini kwao” Waebrania 3:19. Vivyo hivyo hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba Kristo angekawia kurudi namna hiyo, na watu wake wazidi kukaa katika dunia hii yenye dhambi na huzuni kwa miaka mingi. Kutokuamini kwao kuliwatenga na Mungu. Kwa ajili ya kuuhurumia ulimwengu, Yesu amekawiza kurudi kwake, ili wenye dhambi wasikie maonyo na kutafuta mahali pa kukimbilia, wakati ghadhabu ya Mungu itakapomwagwa duniani.

Sasa, kama wakati wa zamani, utangazaji wa ujumbe wa Mungu utakabiliwa na mapingamizi. Wengi wanaoitetea ukweli na kupinga imani ya wengi. Eliya alitwa kuwa “msumbua Israeli; Yereimia akaitwa kwamba ni msaliti” Paulo akaitwa kuwa “mchafua hekalu” [222] Tangu wakati huo mpaka sasa, wale wanaoitetea kweli wameonewa kuwa mahaini, wazushi, wenye faraka.

Ungamo la imani ya wakatatifu wa kale, na wafia dini, ambayo ni vielelezo vya ushujaa wa ukweli huwatia moyo wale walioitwa kuwa mashahidi wa Mungu. Agizo kwa mtumishi wa Mungu kwa wakati huu: “Paza sauti yako kama tarumbera, uwaonyeshe watu wangu makosa yao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao”. “Nimekuweka uwe mlinzi wa nyumba ya Israeli; kwa hiyo sikia neno langu, ukawape watu maonyo yangu”. Isaya 58:1; Eze. 33:7.

Pingamizi kubwa la kuzuia watu wasiukubali ukweli ni kwa sababu huwaingilia katika furaha zao na kuwakemea. Huu ndio ubishi tu wa kutoipokea kweli. Lakini wafuasi wa kweli wa Mungu, hawangojei ukweli upendwe na kuamini na watu wote. Wanaukubali msalaba, kama Paulo asemavyo: “Maana dhiki yetu nyepesi iliyo ya muda kitambo tu yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana” Na tena, “akahesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri” 2Kor. 4:26; Waebrania 11:26.

Yatupasa kuchagua haki kwa kuwa ni haki; na kumwachia Mungu mengine yote. Mtu ashikaye kanuni, mwenye imani, aliye jasiri, ndiye ahitajikaye ulimwenguni ili alete matengenezo. Mtu, au watu wa namna hiyo ndiyo wanaotakiwa wafanye matengenezo kwa wakati huu na kuyaendeleza.

27/Uamsho wa Kisasa Unafauluje?

[223]

Popote pale ambapo Neno la Mungu lilipohubiriwa kwa uaminifu matokeo yake yamethibitisha kuwa neno hilo ni la Mungu hakika. Wenye dhambi walijutishwa. Na toba ya kweli ilionekana kwao. Wakaufahamu utakatifu na haki ya Mungu jinsi ilivyo, kwa hiyo wakalia: “Ni nani ataniokoa na mwili huu wa mauti?” Warumi 7:24 Msalaba ulipoelezwa wazi wao walijiona kuwa si kitu ila huruma za Kristo na neema yake ndiyo itawaokoa tu. Kwa damu ya Yesu tu watapata “msamaha wa dhambi zilizopita”. Warumi 3:25

Watu hawa waliamini na kubatizwa, wakawa wakitembea katika upya wa uzima. Kwa imani ya Mwana wa Mungu wakawa wakifuata nyayo zake, na kudhihirisha tabia yake ulimwenguni. Wakawa wakijitakasa kama yeye alivyo mtakatifu. Mambo ambayo waliyapenda zamani, sasa wanayachukia na kuyaacha; na mambo ambayo hawakuyapenda zamani, sasa wanayapenda na kuyatenda. Kiburi kimegeuka kuwa unyenyekevu, kutakabiari upuuzi vinageuka kuwa utu mwema. Walevi wanakuwa watu sawa. “Wakristo wanatafuta urembo wa moyoni, sio mapambo ya nje, yaani kusuka nywele, na kujipamba kwa dhahabu na lulu, na kuvalia mavazi ya thamani, bali utu wa ndani Wenye thamani kuu, ndiyo roho nyenyekavu, tulivu, ipendezayo mbele za Mungu”. 1Pet. 3:3-4.

Uamsho uliwahusu wenye dhambi, kwa njia ya kuwaita ili watubu. Matunda yalionekana, sio kwa kufurahi katika anasa, ila kwa kuwa watu wanastahili kuteswa kwa ajili ya Kristo. Watu waliona mabadiliko katika maisha yao hao walioliungama jina la Kristo. Hali kama hiyo ndiyo ilikuwa ikionekana kwa watu waliopata uamsho miaka ya zamani.

Lakini uamsho wa kisasa unatofauti. Ni kweli kwamba watu hujidai kuwa wameongoka na wako washiriki wa kanisa wengi makanisani. Walakini matokeo yake hayaonekani kufanana na uongofu halisi unaoonyesha hali ya maisha ya kiroho ya kweli. Huwa hali ya msisimko tu ambao haudumu ila baada ya muda kitambo hufifia na kurudi hali ya kawaida.

Uamsho wa kijumla jumla huwa ni msisimko tu kwa ajili ya jambo lililoletwa. Uamsho wa namna hiyo huwa hauna haja na mafundisho ya Biblia ambayo ndiyo kweli. Ibada yo yote isipokuwa na mambo ya kuburudisha na kuchangamsha, haiwapendezi kabisa; wala haiwavutii.

[224] Mwongofu ye yote, uhusiano wake na Mungu, na mambo ya ufalme wa mbinguni, ndicho kitu kikuu katika maisha yake. Katika makanisa ya washiriki wengi iko wapi roho ya uwakfu wa kweli? Waumini hawakichukii kiburi na upendo wa anasa za ulimwengu.. Hawako tayari kujinyima na kujitoa wakfu. Wala hawako tayari kujikana nafsi, na kufuata unyenyekevu wa Kristo. Utauwa umetoka katika makanisa mengi.

Ijapokuwa hali ya kuanguka kiimani imeenea makanisani, walakini kuna wafuasi wa kweli wengi katika makanisa haya. Kabla ya kuleta hukumu ya mwisho ya Mungu, kutakuwa na mwamko mkubwa katika watu wa Mungu ambao haujaonekana tangu siku za mitume. Roho wa Mungu atamwagwa. Watu wengi wataondoka katika makanisa hayo ambayo yanaongozwa na roho ya ulimwengu, na badala ya kumpenda Mungu na Neno lake. Wachungaji wengi wa watu wengi wataupokea ujumbe wa kweli kwa furaha, nao watajiandaa ili kumlaki Bwana arudipo.

Adui wa wanadamu anatamani kuizuia kazi hii, atafanya hivyo kwa njia ya kuinua kundi la kuigiza. Ataigiza uongofu, kana kwamba Mungu amewamwagia Roho Mtakatifu. Atafanya hivyo katika makanisa yatakayompa nafasi hiyo. Watu wengi watajipa kwamba Mungu anatenda maajabu, kumbe kazi hiyo hutendwa na watu wenye roho tofauti na Roho wa Mungu. Shetani atataka kuenenda mvuto wake kwa wakristo, kwa njia ya kujifanya kuigiza kazi ya kanisa la Mungu. Ataigiza kazi ya Mungu ili apotoshe watu. Basi patakuwa na msisimko mkubwa wenye mchangayiko wa ukweli na uongo, ili apate kuwakosesha watu.

Lakini kwa nuru ya neno la Mungu, watu hawa watatambulikana kuwa ni wa aina gani. Popote watu wanapopuza uthibitisho wa Neno la Mungu, na kugeukia mambo mengine tutakuwa na hakika kuwa Mungu hayumo kati yao. Jambo ni kwamba: “Mtawatambua kwa matunda yao” Mathayo 7:16. Hicho ndicho kipimo kwamba hawa sio wanaoongozwa na roho wa Mungu.

Ukweli wa neno la Mungu ni ngao ya kuyapinga madanganyifu ya Shetani. Kutojali ukweli huu kumfungulia Shetani apate kuingiza maovu ya kila namna ulimwenguni. Sheria ya Mungu haikujaliwa kabisa. Makosa katika kueleza toba na utakaso yameingia yaliyoleta udanganyifu mwingi, ukawafanya watu washushe kipimo cha Ukristo. Hapa ndipo siri ilipo ya upungufu wa Roho wa Mungu katika uamsho wa siku hizi.

Sheria ya Uhuru.

[225]

Walimu wengi wa dini hudai kuwa Kristo alipokufa msalabani aliiondoa sheria. Wengine huiita kongwa ya utumwa, kwa hiyo hudai uhuru wa dini, katika furaha ya Injili.

Lakini manabii na mitume hawakudai jinsi hiyo kuhusu sheria takatifu ya Mungu. Daudi alisema, “Nami nitakwenda panapo nafasi kwa kuwa nimejifunza mausia yako”. Zab. 119:45. Mtume Yakobo asema kuhusu amri za Mungu, “Sheria kamilifu ya uhuru” Yakobo 1:25. Mwandishi wa ufunuo hutaja mibaraka kwa mtu yule “ashikaye amri, awe na ruhusa ya kuuendea mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake”. Ufunuo 22:14.

Kama ingewezekana kuwa sheria ifutwe au ibadilishwe, Kristo asingelikufa ili kumwokoia mwanadamu atoke katika adhabu ya dhambi ya kuvunja sheria. Mwana wa Mungu alikuja ili kuitukuza sheria na kuifanya iheshimiwe, Isaya 42:21, alisema, “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati” Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka Kumhusu yeye mwenyewe, alisema, “Kuyafanya mapenzi yako, Ee, Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu” Mathayo 5:17-18; Zaburi 40:8.

Sheria ya Mungu haibadiliki ni ufunuo wa tabia ya Mtoaji wake. Mungu ni pendo na sheria yake ni pendo. “Pendo ni utimilifu wa sheria” Mtunga Zaburi asema, “Sheria yako ni kweli” “Maagizo yako yote ni ya kweli” Paulo asema, “Torati ni takatifu na ile amri ni takatifu, na ya haki na njema,” Warumi 13:10; Zaburi 119; 142, 172; Warumi 7:12. Sheria kama hiyo inadumu sawasawa na mwenye kuitoa anavyodumu.

Ni kazi ya kuongoka kwa kweli na kutakaswa ndiyo inayoleta upatanisho na Mungu; na kuwaleta wanadamu wapatanane na sheria

yake. Hapo mwanzo mtu alikuwa katika umoja kamili na Mungu wake, na sheria yake. Lakini dhambi ilimfarakanisha na Mwumbaji wake. Moyo wake daima ukawa haupatani na sheria ya Mungu. Na ya mwili ni uadui juu ya Mungu, “kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii” Warumi 7:8. Lakini “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee” ili mtu apatanishwe na Mungu na kurudishiwa uhusiano na Muumba wake. Badiliko hili ndilo kuzaliwa kupya, na ambako lisipopatikana mtu hawezi kuuona ufalme wa Mungu Yohana 3:16.

[226]

Thibitisho la Dhambi

Hatua ya kwanza ya kupatanishwa na Mungu ni uthibitisho wa dhambi, yaani mtu ajione kuwa mwenye dhambi, na anahitaji msaada. “Dhambi ni uasi wa sheria” “Kujua dhambi huja kwa njia ya sheria” 1 Yohana 3:4. Warumi 3:20. Ili kusudi mwenye dhambi ajue hali yake ya dhambi, hana budi kujipima katika kioo cha Mungu cha tabia ya ukamilifu na haki ndipo ataweza kupambanua hali takatifu na hali ya uovu.

Sheria humwonyesha mtu dhambi zake, lakini haipimi dawa. Humwambia kuwa kufa ni adhabu ya mwenye dhambi. Injili ya Kristo pekee yake ndiyo inaweza kumfungua kutoka katika hukumu au lawama ya dhambi. Yampasa atubu makosa yake kwa Mungu, ambaye sheria yake imevunjwa na awe na imani kwake Yesu aliyetoa kafara ya kumwoko. Hivyo atapata msamaha wa dhambi zake za wakati uliopita, (Warumi 3:25) na atahesabiwa kuwa mwana wa Mungu.

Je, sasa yu huru, kuvunja sheria ya Mungu? Paulo asema, “Basi je, twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha. Sisi tuliofia dhambi tutawezaje kuishi ndani yake?” Yohana asema, “Hili ndilo pendo la Mungu, ya kwamba tuzishike amri zake, na amri zake si nzito.” Katika kuzaliwa kupya moyo huletwa ukapatana na Mungu na sheria yake. Badiliko hili linapomfikia mwenye dhambi huwa amepita toka mautini hata uzima, naye huwa ametoka katika hali ya uasi hata utii. Maisha ya kale yamepita na kutokomea huko, maisha mapya yaliyopatanishwa na Mungu, ambayo ni ya imani na upendo yameanzishwa. Ndipo hapo “Maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu, tusioenenda kwa kufuata mambo

ya mwili, bali mambo ya roho”. Hapo lugha ya roho itakuwa, “Sheria naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa” Warumi 3:31, 6:2; 1Yohana 5:3; Warumi 8:4; Zaburi 119:97.

Bila kuwa na sheria uongofu wa mtu ni wa kutojua dhambi ni nini, na kwa hiyo huwa hawana haja ya toba. Hawatambui haja zao za kupatanishwa kwa damu ya Kristo. Matumaini ya wokovu huwa hayana badiliko la moyo la kweli, na maisha huwa yale tu ya kawaida. Hivyo basi uongofu wa juu juu hudumu, na watu makundi makundi hujiunga na kanisa, ambao hawana uhusiano wowote na Kristo.

Utakaso ni Nini?

Mafundisho mapotofu kuhusu utakaso hutokana na kutojali na kukataa kutii sheria ya Mungu. Upotofu huu wa mafundisho ya uongo na ya hatari kubwa hupendelewa na watu wengi.

[227]

Paulo asema “maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kutakaswa kwenu” Biblia hufundisha dhahiri kuwa utakaso ni nini na jinsi iya kuupata. Mwokozi aliomba akisema “Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndiyo kweli. Na Paulo afundishe akisema kuwa wanafunzi lazima watakaswe kwa Roho Mtakatifu” 1Thes. 4:3; Yohana 17:17; Warumi 15:16.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni nini? Yesu aliwafundisha wanafunzi wake akisema “Atakuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote” Yohana 16:13,. Na mtunga Zaburi asema “Sheria yako ndiyo kweli” kwa kuwa sheria ya Mungu ni takatifu, na ya haki na njema, tabia inayofanywa kwa kuitii sheria ya Mungu lazima itakuwa takatifu. Kristo ndiye kielelezo cha tabia takatifu. Naye alisema “Nimeshika amri za Baba yangu” “Kila mara nafanya mapenzi yake” Yohana 15:10; 8:29. Wafuasi wake lazima wafanane naye - kwa neema ya Mungu waumbe tabia inayoambatana na kanuni za utakatifu wa sheria yake. Huu ndio utakaso wa Biblia.

Ni kweli Imani Peke Yake

Kazi hii inaweza kukamilika kwa imani peke yake, katika uwezo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani ya mtu. Mkristo atasikia hali ya dhambi ikimkabili, lakini atapata uwezo wa kushidana nayo. Hapo

ndipo msaada wa Kristo unapohitajika. Udhaifu wa kibinadamu unapounganika na uwezo wa kimbingu, ndipo imani husema, “Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” 1Kor. 15:57

Kazi ya utakaso ni ya maendeleo. Mwenye dhambi anapotubu na kupata kibali cha Mungu, hapo ndipo maisha ya ukristo huanza. Sasa yapasa aendeleo mpaka ukamilifu, kukua hata kimo cha utimilifu wa Kristo. “Nakaza mwendo niifikie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.” Waebrania 11:6; Waefeso 4:13; Wafilipi 3:14.

[228] Watu ambao wanapata utakaso wa Biblia, wataonyesha hali ya unyenyekevu. Huona upungufu wao, wanapojilinganisha na ukamilifu wa Mungu. Nabii Daniel alikuwa kielelezo kizuri kuhusu utakaso. Badala ya kujidai kuwa mtu safi na mtakatifu, nabii mkuu huyu alijiweka pamoja na wenye dhambi wengine wa Israeli wakati alipokuwa akiomba kwa ajili ya watu wake. Daniel 10:11; 9:15,18,20: 10:8,11.

Kwa wale wanaotembea chini ya kivuli cha msalaba wa Kalvari, hapata kuwako kujitukuza, wala kujivuna kuwa hawana dhambi. Hujisikia daima kuwa dhambi zao ndizo zilizosababisha mateso ya Mwana wa Mungu, kwa kuwa na mawazo hayo watakuwa na fedhaha tu. Wale wanaoishi karibu na Kristo wanapambanua hali ya unyonge na uovu wa wanadamu, na huona kuwa tumaini lao ni kwa mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka ufuni.

Utakaso unaoonekana katika ulimwengu wa kidini sana, ambao ni wa majivuno bila kujali sheria ya Mungu ni mgeni kwa Biblia. Hufundisha kuwa utakaso huo ni wa kitambo tu, bora uwe na imani, basi unapata mara moja bila kungoja. Bora uamini, tu utaupata utakatifu kamili. Hakuna juhudi yoyote inayohitajika ili kuupata, ni kuamini tu. Watu hujidai kuwa wamepata utakatifu, na kwa wakati ule ule wanakana uwezo wa mamlaka ya sheria ya Mungu, wakisema kuwa wamewekwa huru kutokana na kushika sheria. Lakini je, inawezekana kufikia hali ya utakatifu bila kufikiana na kanuni za utakatifu, ambazo huoyesha mapenzi ya Mungu?

Ushuhuda wa neno la Mungu hukanusha mafundisho mapotofu ya jinsi hiyo ya imani bila matendo. Siyo imani ya peke yake yenye kufikia matakwa ya mbinguni, bila kuwa na masharti ambayo kwayo rehema hupatikana. Huo ni ufedhuli mtupu. Yakobo 2:14-24.

Watu wasijidanganye kuwa wanaweza kufikia utakatifu wakati wanapozivunja sheria za Mungu kwa makusudi. Dhambi inayojulikana hunyamazisha sauti ya Roho wa Mungu anayeshuhudia katika mioyo ya watu, nayo humtenganisha mtu na Mungu. Ijapokuwa Yohana anaeleza kabisa habari za upendo, hakusita kutaja tabia ya watu ambao hujidai kuwa wametakaswa na kwa wakati ule ule wanaziasi amri za Mungu.

“Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, hakika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli” 1 Yoh. 2:4-5. Hiki ndicho kipimo cha uchaji wa Mungu. Kama wakizihafifisha amri za Mungu au wakivunja mojawapo ya amri zake na kuwafundisha watu hivyo (Mathayo 5:18-19) tutajua ya kuwa madai yao hayana msingi.

Wale wanaojidai kuwa hawana dhambi ni dhahiri kuwa wako mbali na utakatifu. Mtu wa jinsi hiyo hana ule uongofu wa kweli, wala hajui utakatifu wa Mungu ulivyo na hana habari na jinsi dhambi ilivyo mbaya mno. Kiasi anavyokuwa mbali sana na Kristo, ndivyo anavyojiona kuwa mtakatifu yeye mwenyewe.

[229]

Utakaso wa Biblia

Utakaso kuhusu mtu mzima, yaani roho, dhamiri na mwili. Soma 1Thes. 5:23. Wakristo wanaagizwa kutoa miili yao kuwa dhabihu iliyo hai, takatifu, inayokubalika mbele za Mungu Rum. 12:1. Kila kitendo kinachoudhoofisha mwili au akili, humfanya mtu asifae kufanya huduma ya Mwumbaji wake. Wote wanaompenda Mungu kwa mioyo yao yote daima watatafuta kuhusianisha viungo vyao na nguvu zao wapate kuzitii amri za Mungu, na kufanya mapenzi yake. Hawatajichafua au kujinajisisha kwa hali yo yote mpaka wakuwa hawafai kutoa dhabihu ya miili yao kuwa takatifu, kwa Baba yao wa mbinguni.

Kila kitendo cha dhambi au cha tamaa ya mwili au chakula huelekea kudhoofisha uwezo wa akili ya utambuzi. Neno la Mungu, au Roho wa Mungu huwa na mvuto kidogo tu kwa mtu wa namna hiyo. Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu 2kor. 7:1.

Ni wakristo wangapi ambao hujinajisisha wenyewe kwa njia ya ulafi, ulevi na anasa haramu. Kanisa mara nyingi huunga mkono maovu kwa njia ya kujaza urembo na madoido ya kila namna, ambayo hunyang'anya, upendo wa Kristo katika mioyo yao. Je, kama yesu angaliingia katika makanisa ya leo na kuona mambo ya kianasa yaliyomo, ambayo yanatajwa kwa jina la dini asingaliwafukuza, kama alivyowafukuza wale wabadili fedha hekaluni zamani?

“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu” 1Kor. 6:19-20. Mtu ambaye mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu, hawezi kujitia utumwani kwa njia ya kufanya mazoezi ya ufedhuli. Uwezo wake ni mali ya Kristo. Mali yake yote ni mali ya Bwana. Basi anawezaje kuharibu mali hiyo?

Wakristo hugharimia fedha nyingi kwa mwaka kwa ajili ya mambo ya anasa. Mungu hunyang'anywa zaka na sadaka, wakati matumizi ya anasa huchukua sehemu kubwa ya mali yao, zaidi kuliko wanayotoa kwa ajili ya kusaidia masikini na kwa kueneza Injili. Kama wote wanaojiita kuwa ni Wakristo wangukuwa waaminifu katika kutumia mali zao, badala ya kuzitumia ovyo, wakaziweka katika hazina ya mbinguni, wangukuwa mfano mzuri wa kiasi na kujinyima. Ndipo wangukuwa nuru ya ulimwengu.

[230]

Tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima (1 Yoh. 2:16) huwatawala watu maelfu na maelfu. Lakini wafuasi wa Kristo wanao mwito mtakatifu. “Tokeni kati yao mkatengwe nao asema Bwana, msiguse kitu cho chote kilicho kichafu” kwa wale wanaoafikiana na masharti haya, ahadi ya Mungu kwao ni hii, “Nami nitawakaribisha, nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike” 2Kor. 6:17-18.

Kila hatua ya imani na utii, humleta mtu katika kuunganika na Nuru ya ulimwengu. Nuru kamili za jua la haki huwamulikia watumishi wa Mungu, nao huwangazia wengine. Nyota hutuambia kuwa kuna nuru huko mbinguni ambayo utukufu wake huzingarisha. Hali kadhalila wakristo huudhihirishia ulimwengu kuwa yuko Mungu atawalaye, ambaye anastahili kutukuzwa na kuheshimiwa. Utakatifu wa tabia yake utadhihirika kwa watumishi wake ambao ni mashahidi wake.

Kwa fadhili zake Kristo tunapta njia ya kufikia kiti cha enzi cha Mungu, mwenye uwezo. “Yeye asiyemwachilia mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukarimia mambo yote bure?” Yesu asema, “Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa roho Mtakatifu hao wamwombao? Mkiomba lo lote kwa jina langu hilo nitalifanya” “Ombeni nanyi mtapata ili furaha yenu iwe timilifu” Rum. 8:32; Luka 11:13; Yoh. 14:14; 16:24.

Ni jukumu la kila mtu kuishi maisha yanayotambulika kwa Mungu ili apate baraka zake. Siyo mapenzi ya Baba wa mbinguni kwamba sisi tuishi gizani katika hali ya kutangatanga na kuhukumiwa. Hakuna ushahidi wo wote kwamba unyenyekevu humfanya mtu atembeke akiinama chini na kuliwazwa na mawazo ya ubinafsi. Twapaswa kumwendea Yesu na kutakaswa na kusimama mbele ya sheria bila hofu wala waa.

Wana wa Adamu walioanguka wanaweza kuwa wana wa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Yeye haoni haya kuwaita ndugu zake. Maisha ya ukristo yapasa yawe maisha ya imani, ya ushindi na ya furaha katika Bwana Mungu. “Furaha ya Bwana ndiyo nguvu yenu” “Furahini siku zote” “Ombeni bila kukoma Shukuruni kwa mambo yote, maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwenu” Ebr. 2:11; Neh. 8:10; 1Tes. 5:16-18.

Hayo ndiyo matunda ya uongofu wa Kibiblia na utakaso. Kwa kuwa kanuni kuu za sheria kama zilivyowekwa na Biblia, hazifuatwi ndiyo sababu ya hali hafifu makanisani. Hii ndiyo sababu mwamko wa kiroho ni mdogo sana, wala haufuatani na ule wa watu wa zamani wa matengenezo. Ni kwa kutazama tu ndipo tunabadilika. Kanuni zile takatifu zionyeshazo tabia ya Mungu zisipojaliwa, na watu wakitia nia zao kwa hadithi za kibinadamu matokeo yake ni hali ya mauti ionekanayo katika kanisa, yaani kanisa mtu. Ni wakati sheria ya Mungu inapoheshimiwa ipasavyo ndipo mwamko wa kiroho unapoambatana na imani ya kweli ya uongofu halisi vitaonekana katika maisha ya wakristo.

[231]

28/Kukubalika Kumbukumbu ya Maisha yetu.

“Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye Mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji na nywele za kichwa chake kama sufi safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto; na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa” Daniel 7:9-10.

Haya ndiyo maono aliyopewa Daniel ya siku ile kuu ya hukumu ambayo maisha ya kila mtu yatakapopitishwa katika uchunguzi wa Hakimu wa dunia yote. Mzee wa siku ni Baba Mungu. Yeye ambaye ndiye asili ya maisha yote ya kila kitu, chemichemi ya sheria zote, ndiyo atakuwa mwenye kiti katika hukumu. Na malaika watakuwa wahudumu na mashahidi.

“Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja na mawingu ya mbinguni akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wantumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo haitapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa” Daniel 7:13-14.

Kuja kwa Kristo kunakoelezwa hapa siko kurudi kwake mara ya pili duniani. Anakuja kwa Mzee wa siku huko mbinguni ili kupokea ufalme atakaopewa mwisho wa kazi yake ya uombezi. Kuja huko ndiko kulitokea mwaka 1844, wala si kurudi duniani mara ya pili. Hivyo ndiyo ilikuwa mwisho wa unabii wa siku 2300. Kuhani wetu Mkuu anaingia katika patakatifu pa patakatifu ili kufanya kazi yake ya mwisho ya kuwaombea wanadamu.

Katika huduma ya hema takatifu hapa duniani, watu ambao dhambi zao zilihamishiwa kutoka patakatifu, ndivyo waliofaidi siku ya upatanisho. Hali kadhalika katika siku kuu ya uchunguzi wa mwisho, watu ambao yao yataangaliwa ni wale watu wa Mungu

tu. Hukumu ya waovu itakuwa wakati mwingine. “Hukumu lazima ianzie katika nyumba ya Mungu” 1Petro 4:17.

Vitabu vya kumbukumbu vya mbinguni vitahusika na uamuzi wa kesi ya kila mtu. Kitabu cha uzima kimeandikwa majina ya watu wote walioingia katika huduma ya Mungu. Yesu aliwaagiza wanafunzi wake, “Furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni”. Paulo anasema kuhusu wakazi wenzake, “ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima” Danieli asema kuwa watu wa Mungu wataokolewa, “Kila mmoja atakayeonekana ameandiwa kitabuni” Na mwandishi wa ufunuo “asema kuwa wale watakaolingia katika mji wa Mungu, ni wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwana Kondoo” Luka 10:20 Wafilipi 4:3; Danieli 12:1; Ufunuo 21:27.

[233]

Katika kitabu cha ukumbusho yamo majina ya matendo mema ya wale wamchao Bwana, na kulitafakari jina lake; Kila jaribu linapingwa, kila uovu unashindwa, kila neno la fadhili linalosemwa, kila tendo la kujinyima, na kila tendo la kusikitisha lililovumiliwa, kwa ajili ya Kristo, huandikwa. “Umehesabu kutangatanga kwangu, uyatie machozi yangu katika chupa yako. Je, hayamo katika kitabu chako?” Malaki 3:16; Zaburi 56:8.

Makusudi ya Siri

Kuna kumbukumbu ya dhambi za watu pia. “Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema, au likiwa baya” “Kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu” “Kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa” Makusudi ya siri huandikwa katika kitabu cha kumbukumbu. “Kwa maana Mungu, atakayemulikisha yaliyositirika, ya giza na kuyadhihirisha mashauri mioyo” Mhubiri 12:14; Mathayo 12:36-37; 1Kor. 4:5. Mbele ya kila jina la mtu, pataandikwa, kila neno ovu mtu alilonena, kila tendo la ubinafsi alilotenda, kila jambo alilopaswa kufanya lakini hakulifanya, na kila dhambi ya siri, kila onyo la mbinguni au ujumbe ambao haukujaliwa, kila nafasi iliyopotezwa bure, na mvuto ulioingwa, kuelekeza kubaya au kuzuri. Yote hayo huandikwa kwa usahihi kabisa na malaika.

Kanuni ya Hukumu

Sheria ya Mungu ndiyo kanuni au kipimo katika hukumu “Mche Mungu, na uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu” “Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi” “Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru”. Mhubiri 12:13-14; Yakobo 2:12.

[234] Wale watakaohesabiwa kuwa wanastahili, watakuwa na sehemu katika ufufuo wa wenye haki. Yesu alisema “Wale wahesabiwao kuwa wanastahili kuupata ulimwengu ule na kufufuka katika wafu Nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo” “Wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima”. Luka 20:35-36; Yohana 5:29. Wafu, ambao ni wenye haki hawafufuki mpaka hukumu ambayo imewahesabu kuwa wanastahili “ufufuo na uzima” imalizike Hivyo hawatakuwako katika hukumu hiyo, wakati mambo yao yanapoamuliwa.

Yesu ndiye atakuwa mtetezi wao mbele za Mungu “Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki”. “Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndiyo mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu” “Naye kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombe” 1Yoh. 2:1 Waebrania 7:25; 9:24.

Vitabu vinapofunguliwa katika hukumu, maisha ya watu wote waliomwamini Yesu yanachunguzwa mbele za Mungu. Wakianza na watu wa kwanza kabisa kuishi ulimwenguni. Mtetezi wetu analeta habari za wote wa kila kizazi. Majina mengine yanakubalika, na mengine yanakataliwa, maana kila jina linatajwa na habari zake zinachunguzwa barabara. Mtu ye yote akionekana kuwa dhambi zake bado ziko kitabuni, wala hajaziungama ili zifutwe, naye asamehewe, jina lake hufutwa katika kitabu cha uzima. Bwana alimwambia Musa, “Yeyote aliyetenda dhambi ndiye nitamfuta katika kitabu changu” Kutoka 32:33.

Watu wote ambao wametubu kwa kweli na kwa imani wamedai damu ya Kristo kuwa ukombozi wao, wamesamehewa, na majina yao yameandikwa mbinguni. Kwa jinsi walivyokuwa washiriki wa haki ya Kristo, na tabia zao zimeonekana kuwa zinaafikiana na tabia

ya Kristo na sheria ya Mungu, dhambi zao hufutwa, na wao watahesabiwa kuwa wanastahili kupata uzima wa milele. Bwana asema “Mimi naam mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe; wala sitazikumbuka dhambi zako” “Yeye ashindaye atavikwa mavazi meupe. . . . Nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele za malaika zake” Basi, kila mtu atakayenikiri mbele za watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Isaya 43:25; Ufunuo 3:5; Mathayo 10:32-33.

“Yesu mtetezi atetea wote walioamini damu yake ili awapeleke katika makao ya Edeni, akiwafanya washiriki katika urithi na utawala wake na katika mamlaka ya kwanza” Mika 4:8. Sasa Kristo ataka hali ya mpango wa kwanza wa uumbaji, irudishe, na kuwafanya watu hawa kana kwamba hakufanya dhambi. Anaomba kwamba watu wake wasisamehewe na kupewa haki peke yake bali wawe washiriki katika utukufu wake, na waketi katika kiti chake cha enzi. [235]

Wakati Yesu anaomba kwa ajili ya raia zake wa neema, shetani anawashitaki mbele za Mungu. Anataja habari za maisha yao ya nyuma, anataja tabia zao mbaya, walivyokuwa wabovu wasifanane na Kristo, anaonyesha dhambi zao zote, ambazo aliwashawishi wakafanya. Kwa hiyo anadai kuwa ni watu wake wenye dhambi kama yeye.

Yesu hatetei dhambi zao, bali huonyesha toba zao na imani yao. Anadai kuwa wasamehewe kwa ajili ya toba walivyotubu. Anainua mikono yake iliyopigwa na misumari, mbele za Baba, akisema “nimewachora katika viganja vyangu. Dhabihu za Bwana ni roho iliyovunjika. Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee, Mungu, hutaudharau”. Zab. 51:17.

Bwana Amkeme Shetani

Kuhusu mshitaki huyo, yaani shetani, Yesu alitamka “Bwana na akukeme, Ewe shetani; naam, Bwana aliyechagua Yerusalemu, na akukeme, Je, hiki si kinga kilichotolewa motoni?” Zekania 3:2. Kristo atawavika watu wake waaminifu na haki yake mwenyewe,

ili awafikishe kwa Baba yake wakiwa “Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi, wala lolote kama hayo”. Waefeso 5:27

Kwa hiyo ahadi ya agano jipya itakamilika, isemayo “Nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena” “Katika siku hizo na wakati huo, asema Bwana uovu wa Israeli utatafutwa, wala uovu hapana; na dhambi za Yuda zitatafutwa wala hazitaonekana”. “Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa Mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu”. Yereimia 31:34; 50:20 Isaya 4:3.

Kufutwa Kabisa kwa Dhambi

Kazi ya hukumu ya upelelezi na ya kufutwa dhambi itakamilika kabla ya kurudi kwake Yesu duniani. Katika mfano wa hema takatifu, kuhani alitoka na kuwabariki watu wa mkutano siku ya upatanisho. Vivyo hivyo na Kristo pia, baada ya kazi yake ya uombezi, atatokea bila “dhambi kwa hawa wamtazamao kwa wokovu” Waebrania 9:28.

[236] Kuhani alipokuwa akizihamisha dhambi kutoka katika patakatifu aliziungama na kuziweka juu ya mbuzi wa Azazeli. Kristo naye ataweka dhambi zote juu ya Shetani ambaye ndiye mwanzilishi wa dhambi. Mbuzi wa Azazeli alikuwa akipelekwa porini Mambo ya Walawi 16:22. Shetani naye akichukua dhambi alizosababisha na kuwashawishi watu wa Mungu kufanya, atafungwa maabusu muda wa miaka elfu moja, katika nchi iliyoharibika na kubomoka, baadaye ataadhibiwa katika ziwa la moto ambao utawatetekeza waovu. Hivyo basi mpango wa wokovu utafikia ukamilifu wake, wakati dhambi itakapokuwa imeharibiwa kabisa kabisa.

Kwa Wakati ulioamriwa.

Katika wakati ulioamriwa, ndio mwisho wa siku 2300 yaani mwaka 1844, kazi ya uchunguzi wa majina ya watu na kufutwa kwa dhambi za watu ilianza, dhambi ambazo hazikuungamwa na kuachwa hazitafutika, katika vitabu vya mbinguni. Malaika wa Mungu huona kila dhambi na kuiandika. Dhambi inaweza kukanwa, kufichwa kabisa kwa baba, mama, mke, watoto au kwa watu wote,

lakini mbele za Mungu huwa iko wazi. Mungu hadanganywi na hali ya mtu ionekanayo kijuu juu tu. Yeye hadanganyiki wala hakosei. Watu wanaweza kudanganyika na hali ya kujifanya kijuu juu, lakini sivyoy Mungu, yeye husoma na kujua mambo ya moyoni. Lo! Ni jambo la kutisha kiasi gani, ambavyo hakuna shujaa awezaye kurudisha mambo yake ya siku moja. Matendo yetu maneno yetu hata makusudi ya mioyo yetu ambayo ni ya siri ingawa sisi tumeyasahau, yatatushuhudia kwa wema au kwa ubaya.

Katika hukumu matumizi ya kila kipawa, au talanta yatachunguzwa kwa makini. Jinsi tulivyotumia wakati wetu, karamu zetu, sauti zetu fedha zetu, mivuto yetu. Tumefanya nini kwa ajili ya Kristo. Kuhusu maskini wenye dhiki, yatima, wajane? Tumefanya nini na nuru ya ukweli tuliyopeva? Matendo ya upendo tu ndiyo yatahesabika kuwa kitu cha thamani machoni pa mbingu.

Ubinafsi wa Siri Wadhihirika

Ubinafsi wa kisirisiri huwa wazi kabisa katika vitabu vya mbinguni. Mara ngapi watu humpa shetani nyakati zao, mawazo yao na nguvu zao ambazo ni mali ya Mungu. Wanaojidai kuwa wafuasi wa Kristo, wanajitumbukiza katika kutafuta mali ya dunia, au katika anasa za dunia. Fedha, wakati na nguvu hutumiwa katika mambo ya kujinufaisha na kutukuza ubinafsi. Muda wa kutumiwa katika maombi ni kidogo sana, na muda wa kuchunguza Maandiko na kuungama dhambi ni kidogo sana.

Shetani amevumbua mambo mengi mno ya kutushughulisha. Mdanganyifu mkuu huyu, anachukia ukweli ambao hutuelekeza kwa Mkombozi wetu anayetuomba. Mambo yake yote hutoa mawazo ya watu yasimfikiri Kristo na uombezi wake. [237]

Watu ambao wanataka kufaidi uombezi wa Kristo, inawapasa wasiruhusu kitu cho chote kiwazuie kutimiza wajibu wao unaopasa wokovu wao mbele za Mungu. Nyakati zao za thamani, lazima zitumike katika kuomba na kujifunza neno la Mungu, badala ya kujifurahisha na kufukuzana na uchumi wa nchini. Patakatifu pa mbinguni na kazi ya uchunguzi wa hukumu huko mbinguni vingekuwa dhahiri katika mawazo yao daima. Wote wanahitaji kuelewa barabara kazi ya kuhani wao Mkuu, uombezi wake kwa ajili yao. Au la, sivyoy watashidwa kuelewana naye katika shughuli anayowashughulikia.

Patakatifu pa mbinguni ndipo kiini cha kazi Kristo anayowashughulikia wanadamu. Kazi hiyo inamhusu kila mtu aliyeko duniani. Inadhihirisha mpango wa wokovu, inatuleta mpaka kwenye mashindano makuu baina ya haki na uovu.

Uombezi wa Kristo

Uombezi wa Kristo kwa ajili ya wanadamu, ambao anaoufanya katika patakatifu pa mbinguni, ni muhimu sana na kifo chake juu ya msalaba. Alipokufa msalabani ndipo alianza kazi yake, ambayo alikwenda kuimalizia mbinguni. Kwa imani, inatupasa sisi tupaingie patakatifu, “alimoingia Yesu mtangulizi wetu” Waebrania 6:20. Hapo ndipo nuru kutoka msalabani inamulika. Hapo ndipo tunaelewa siri ya ukombozi.

“Afichae dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha, atapata rehema” Mithali 28:13. Kama wale wanaofanya udhuru na kuficha makosa yao wangaliona jinsi shetani anavyomdhihaki Kristo kwa ajili ya mambo yao, wangeziungama dhambi zao na kuziacha. Shetani hujitahidi kutawala mawazo yote ya watu, naye anajua kuwa, kama hali ya kimakosa ikipendelewa atafaulu katika kazi yake ya kuwapotosha na kuwapoteza. Kwa sababu hii huwadanganya wafuasi wa Kristo daima kwa hila zake, ili aweze kuwashinda. Lakini Yesu huwaambia wote wamfuatao, “Neema yangu yakutosha” “Nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi”. 2Kor. 12:9; Mathayo 11:30. Mtu asidhani kuwa makosa na kasoro haviwezi kuponyeka. Mungu atatupa imani na neema ya kushinda.

[238] Sasa sisi tunaishi katika siku kuu ya upatanisho. Wakati kuhani alipokuwa akifanya upatanisho kwa ajili ya wana wa Israeli, iliwapasa wote kutesa roho zao kwa njia ya maungamo ya toba kamili. Hali kadhalika, wale wanaotaka majina yao yaandikwe katika kitabu cha uzima yawapasa sasa kujitesa kwa njia ya kuungama dhambi zao. Lazima kuwepo toba ya kweli. Hali ya uzembe, ambayo watu wengi wanayo, lazima iachwe kabisa. Mashindano ni makali kabisa kwa wale wanaotafuta kuwa wana wa Mungu wa kweli, maana shindano kati ya haki na uovu ni kali. Kila mtu hana budi kukutwa bila kuwa na “hila wala kunyanzi, wala lolote kama hayo”. Waefeso 5:17

Wakati kama huu, zaidi ya wakati wo wote, inapasa kila mtu ajali wosia wa Kristo, “Kesheni, mkaombe kwa kuwa hamjui wakati huo ni lini” Marko 13:33.

Mambo ya Wote Yamekatwa

Rehema inafungwa muda mfupi kabla ya kuonekana kwa Kristo, akirudi duniani, katika mawingu ya mbinguni. Kristo akitazamia wakati huo, anatangaza akisema “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo” Ufunuo 22:11-12.

Watu watakuwa wakipanda na kujenga, wakila na kunywa, wote bila kuwa na habari kwamba tangazo la mwisho limekwisha kutolewa katika patakatifu huko mbinguni.

Wakati ule kabla ya gharika, baada ya Nuhu kuingia safinani, Mungu alimfungia mlango akiwa ndani, na waliendelea na anasa zao, hali wakidhihaki maneno ya Nuhu. Mwokozi alisema, “Ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu. Kimya, kimya bila kujua, kama mwizi ajavyo usiku, ndivyo itakavyokuwa saa ya kuamuliwa mambo ya mwanadamu.” “Kesheni basi, asije akawajia na kuwakuta mnalala” Mathayo 24:39; Marko 13:35-36.

Hatari itawakumba wale waliochoka kukesha, na kugeukia mambo ya ulimwengu. Wakati wenye biashara wakiwa katika kufukuzana na uchumi, wakati wapenda anasa wanajishughulisha na anasa, wakati warembo wanaendelea kujipamba, inawezekana katika saa hiyo ndipo tangazo la Mwamuzi wa dunia yote, litasema “Umepimwa kwa mizani ukaonekana umepungua” Daniel 5:27.

29/Kwa nini Dhambi Iliruhusiwa?

Watu wengi huona kazi za mwovu, zenye matokeo ya maafa na taabu za kila aina. Swali linachipuka vichwani kwamba inaweze kanaje mambo kuwa hivyo chini ya Mungu mwenye hekima yote, uwezo wote, na upendo wote. Watu wanaopata kuwa na mawazo ya jinsi hii hujipatia udhuru wa kuukana ukweli wa maandiko matakatifu. Mapokeo na kulitafsiri vibaya neno la Mungu kuhusu tabia ya Mungu ilivyo, na asili au msingi wa serikali yake, na kanuni zake za kushughulikia dhambi huwatia watu gizani na mashakani.

Haiwezekani kueleza asili ya dhambi ili kufahamu mwanzo wake na jinsi ilivyo. Walakini kuna maelezo ya kutosha kufahamu mambo ya dhambi na mwisho wa dhambi pia, ili kudhihirisha ukarimu na haki ya Mungu. Mungu hakuwa ndiye asili ya dhambi. Kwa Mungu hakuna hali ya machafuko, wala unyimivu wa neema yake, wala upungufu wowote katika serikali yake, ambao unaweza kusababisha uasi na machafuko. Dhambi ni mwingilio wa uasi bila kutakiwa, na hakuna awezaye kuelezea. Kuitetea ni kule kuikubali. Kama isingelitetewa, isingalikuwapo kabisa. Dhambi ni uhasama kati yake na sheria ya upendo, ambayo ndiyo msingi wa serikali ya Mungu.

Kabla dhambi haijaingia duniani, kulikuwa na amani na furaha kote katika malimwengu. Kumpenda Mungu kulikuwa jambo kuu kabisa, na upendo kati ya viumbe ulikuwa hausemeki, Kristo, ambaye ni Mwana wa pekee alikuwa pamoja na Baba wa milele, katika asili, tabia na makusudi. Ni yeye tuliyeingia katika mashauri yote ya Mungu, na makusudi ya Mungu. “Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni Ikiwa ni vitu vya enzi, na usultani, au enzi, au mamlaka.” Kol. 1:16.

Sheria ya upendo ndiyo iliyokuwa msingi wa serikali ya Mungu. Furaha na raha ya viumbe vyote vilivyoubwa ilitegemea jinsi walivyoafikiana na kanuni za haki. Mungu hana furaha na kulazimisha viumbe wamtii. Kwa viumbe vyote alitoa uhuru kamili,

uhuru wa dhamiri ili wamtumikie kwa uhuru kila mmoja kwa hiari yake, siyo kwa shuruti.

Lakini alikuwako mmoja aliyechafua mpango huu wa uhuru. Dhambi ilianza kwake ambaye ndiye aliyekuwa wa pili kwa Kristo, mwenye heshima kuu mbele za Mungu. Kabla hajaanguka, Lusifa alikuwa “Kerubi wa kwanza afunikwaye” mtakatifu, asiye na waa. Bwana Mungu asema hivi: “Wewe wakitia muhuri kipimo umejaa hekima na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako. . . . Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye, nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huo kati ya mawe ya moto ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako. . . . Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; Umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu” “Nawe ulisema nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu. . . . nami nitaketi katika mlima wa mkutano Nitapaa kupita vimo vya mawingu, nitafanana na yeye aliye juu” Eze. 28:12-17; 28:6; Isaya 14:13-14.

[240]

Heshima ya kufunika ambayo Baba aliitoa kwa mwanawe ilitamaniwa na malaika huyu, ingawa alikuwa na heshima. Heshima ya Kristo, ilimhusu yeye tu, wala si mwingine. Basi sasa alama ya kutoridhika ilionekana katika umoja wa ajabu uliokuwa mbinguni. Kujitukuza kwa ubinafsi hakukuruhusiwa huko. Lilikuwa chukizo baya mno kufikiri. Utukufu wa Mungu ulikuwa unatosha kabisa. Baraza la mbinguni lilimsihi juu ya nia yake, kuwa aiache. Mwana wa Mungu alimweleza uzuri na haki ya mwumbaji, pamoja na utakatifu wa sheria yake. Kama akijitenga na sheria hiyo, Lusifa atakuwa amemdharau Mwumbaji wake, na kujiletea uharibifu mwenyewe. Lakini onyo hilo lilipingwa. Lusifa aliendelea kumwonea Kristo wivu.

Kiburi kiliongeza tamaa ya ukuu wa Lusifa, akawa mtaka makuu. Heshima kuu aliyopewa haikumfanya awe na shukrani, kwa Muumba wake. Alikaza nia yake ya kufanana na Mungu. Walakini mwana wa Mungu peke yake ndiye alikuwa na cheo hicho, yaani yeye alikuwa katika umoja na Baba kwa kila hali katika mashauri yote ya Mungu Kristo alishiriki. Lakini Lusifa hakuwa na hadhi

hiyo. Hivyo aliuliza kwa nini Kristo tu awe na hadhi hiyo na mimi sivyo?

Kutoridhika Miongoni Mwa Malaika

[241] Lusifa alipotoka mbele za Mungu alikwenda kwa malaika ili kueneza kutoridhika kwake na roho ya manung'uniko kati yao. Ali-tenda hivyo kwa siri sana, akificha kusudi lake hasa, na kueleza tu ya kuwa Mungu anataka heshima ya lazima, wala si ya uhuru na hiari. Akaishambulia sheria ya Mungu ambayo inatawala katika enzi yote kuwa ni ya ubeberu. Akasema kuwa malaika wangeachiwa uhuru kamili ili wafanye wapendavyo kwa hiari yao. Kwamba Mungu hakufanya haki yo yote, kumwinua Kristo juu kuliko yeye (Lusifa) Alisema kuwa hakuwa na kusudi la kujitakia heshima ila alitaka uhuru kwa wote wa mbinguni, ili wawe na heshima. Mungu alimvumilia Lusifa muda mrefu. Hakumwachisha cheo chake hata wakati aliponekana akienda kinyume cha utaratibu, na kuwaeleza malaika mambo yasiyo ya kweli. Alipewa muda wa kutubu na kujirekebisha mara nyingi. Juhudi za Mungu za upendo za kumtaka Lusifa ajirekebisha ilikuwa kana kwamba ni kumthibitishia kosa lake. Manung'uniko na kutoridhika havikujulikana mbinguni kabla ya wakati huo. Hata Lusifa hakuelea matokeo hasa ya hali hiyo anayoanzisha. Kwa kuwa hoja zake hazikuwa na sababu yo yote. Lusifa aliamini kuwa madai yake kwamba sheria ya Mungu ina kasoro ni ya uongo, na kwamba hana budi kukiri wazi mbele ya wakaa mbinguni kuwa amekosa. Kama angalifanya hivyo angalijiokoa yeye pamoja na malaika wengi. Kama angelihiari kumrudia Mungu akiridhika na cheo chake angalirudishwa katika hadhi yake kama kwanza. Lakini kiburi kilimzuia kujitua. Akajiona kuwa hana haja ya kukiri, wala kutubu, na kwa njia hiyo akajitia katika mapambano na mwumbaji wake.

Uwezo wake wote akautumia katika udanganyifu tu, hivyo akajipendeza kwa malaika ili wamwunge mkono. Shetani alisema kuwa hakutendewa haki, wala hakueleweka vema. Kwa njia ya kuyapinda maneno ya Kristo, akamshitaki kwa malaika kuwa anakusudia kumwondolea cheo chake, na kumshusha mbele ya wote wa mbinguni.

Wote wale ambao hakuweza kuwashawishi, aliwashitaki kuwa ni wachafuzi wa mbingu na wenyeji wake. Alitafuta kumtia dosari Mwumbaji. Lilikuwa kusudi lake kuwatatanisha malaika kwa mashauri yake ya uongo kuhusu makusudi ya Mungu. Kila kitu alijaribu kukitia dosari halafu kusukuma malaumu yote kwa Mungu kuwa ndiyo nia yake. Cheo alichokuwa nacho kilimwezesha kufaulu kushawisi na kuchafua mambo. Wengi walidanganyika, wakijiunga pamoja naye, katika uasi huo.

Shetani alikuwa mwenye heshima kuu, na matendo yake yote yalifunikwa na hali ya siri ajabu, hata haikuwezekana kwa malaika kuelewa mambo yake hasa. Dhambi haikueleweka mpaka ilipodhihirika wazi kabisa. Viumbe watakatifu hawakuweza kufahamu matokeo ya kuiacha sheria ya Mungu. Mara ya kwanza shetani alidai kuwa analeta heshima ya Mungu na ufanisi wa wote wakaao mbinguni. [242]

Mungu alipoishughulikia dhambi alitumia njia ya haki na kweli peke yake. Shetani aliweza kutumia mambo au njia zile ambazo Mungu hawezi kutumia, yaani njia ya ubembelezi na udanganyifu. Tabia ya mnyang'anyi shetani lazima idhihirike wazi kwa wote. Lazima apate muda wa kutosha wa kujidhihirisha jinsi alivyo, na jinsi matendo yake yalivyo, ambayo ni ya udhalimu. Mafarakano, ambayo ameyaleta huko mbinguni, alimlaumu Mungu kuwa ndiye ameyasababisha. Maovu yote aliyosababisha aliyatupa kwa Mungu, kwamba yamesababishwa na utawala mbaya wa Mungu. Kwa hiyo alipewa muda wa kuonyesha uzuri wa kubadili kanuni za utawala wa Mungu, na kushika kanuni mpya. Kazi zake mwenyewe zitamhukumu. Malimwengu yote yataona udanganyifu wa shetani uliofunikwa, na sasa uko wazi.

Hata wakati ilipoamuriwa kuwa hawezi kuishi mbinguni tena, Mungu kwa hekima yake hakumharibu na kumwangamiza. Uti wa viumbe vya Mungu lazima usimame juu ya haki yake tu. Kama Mungu angemwangamiza shetani kabla ya viumbe wa Mungu hawa-jaona uovu wa udanganyifu wake, wasingeelewa ukweli wa haki ya Mungu. Kama angeangamizwa mara moja viumbe vya Mungu wangestuka sana na kujaa hofu, hivyo wangemtumikia Mungu kwa hofu tu, wala si kwa hiari na upendo. Kwa ajili ya mema ya viumbe wote wa Mungu shetani aliachiwa muda aonyeshe kazi zake za uovu

mpaka kila kiumbe kione wazi na kufahamu ili katika kumharibu, pasiwepo na ye yote atakayestuka.

[243] Shetani na uasi wake wa sheria ya Mungu, vitakuwa ushuhuda wa madhara ya dhambi. Utawala wake utakuwa kielelezo cha kuacha sheria ya Mungu. Historia ya utawala wa shetani, na uasi wake, utakuwa fundisho la kudumu kwa viumbe wote, kwamba Mungu ni wa haki na sheria yake ni ya haki na kweli. Viumbe wa Mungu watajiepisha na dhambi, na adhabu yake.

Ilipotangazwa kwamba shetani na wafuasi wake wanafukuzwa kutoka katika makao ya raha ya milele, mbinguni, alikubali bila aibu na kukiri kuwa sheria ya Mungu ina kasoro. Akitaja sheria ya Mungu kuwa ni ya kibeberu inayowanyima viumbe uhuru. Akatangaza nia yake ya kuiondoa sheria hio na kuleta sheria yake ambayo ni bora zaidi kuliko hiyo ya Mungu, yake ni ya uhuru, wala haina vikwazo.

Kufukuzwa Mbinguni

Shetani na jeshi lake walitupa lawama ya uasi wao juu ya Kristo, kwamba, kama wasingalishurutishwa wasingaliasi. Hata hivyo kwa shingo ngumu walizidi kudai kuwa wamekatili watu kwa nguvu bila haki. Walakini hata hivyo mwasi mkuu na wafuasi wake walifukuzwa kutoka mbinguni. Ufunuo 12:7-9.

Roho ya uasi ya Shetani bado inachochea hali ya uasi duniani kwa watu wenye hali ya kuasi. Kama yeye afanyavyo, huwaahidia watu uhuru hali wamo katika kuiasi sheria ya Mungu. Uthibitisho wa dhambi hata leo huamsha chuki kwa watu. Shetani huwaaminisha watu kwamba wao ni wenye haki, na kuwatafuta wengine waunge mkono, katika hali yao ya kufanya dhambi. Hudai kwamba wale wanaowathibitishia dhambi zao ndiyo wenye makosa, hufanya hivyo badala ya kujutia dhambi zao.

Jinsi alivyosema mbinguni kuwa Mungu ni mkatili ndivyo anavyowaingiza watu katika dhambi. Hudai kuwa ukatili wa Mungu umewaingiza watu dhambini, sawa kama ulivyomwingiza yeye katika uasi.

Kitendo cha kumfukuza shetani kutoka mbinguni kilionyesha haki ya Mungu na heshima yake. Lakini wakati mwanadamu alipokosa, Mungu alithibitisha upendo wake kwa kumtuma mwanawe ili awafie wakosaji. Katika upatanisho, tabia ya Mungu

hudhihirishwa. Msalaba wa Kristo ulidhihirisha kuwa dhambi haikutokana na serikali ya Mungu. Wakati wa huduma ya Kristo duniani mdanganyifu mkuu, shetani aliwekwa peupe. Maneno yake ya kufuru kwamba Kristo amsujudie, chuki ya ajabu aliyokuwa nayo kwa Yesu akimwinda mchana na usiku, alivyowachochea makuhani wa watu, ili wakatae upendo wake, na kupaza sauti zao na kusema “Msulubishe, msulubishe!” Hayo yote yalishangaza malimwengu yote. Mwovu huyu alitumia uwezo wake wote ili amwangamize Kristo. Shetani aliwatuma watu kama wajumbe wake wa kuleta matatizo na huzuni katika maisha ya Yesu, alipokuwa hapa duniani. Hasira na ghadhabu na kila aina ya mateso vyote vilitumika kwa Mwana wa Mungu pale katika msalaba wa kalwari.

[244]

Sasa hatia ya shetani haifichiki tena, nayo haina udhuru. Amonyeshwa tabia yake ya kweli jinsi ilivyo. Uwongo wa shetani juu ya kulaumu mpango wa Mungu umedhihirika kwa wote. Amemshitaki Mungu kuwa ni mtaka makuu, ni mkatili, ni kibeberu, ni mpenda ubinafsi. Sasa ilionekana kuwa mtawala wa malimwengu, amefanya toleo la ajabu kwa upendo. “Kwa kuwa Mungu alikuwa ndani ya Kristo kuupatanisha ulimwengu kwake mwenyewe”. 2Kor. 5:19. Kristo alijinyeyekeza na kuwa mtii mpaka mauti, ili apate kuiharibu dhambi.

Hoja kwa Ajili ya Mwanadamu

Mbingu yote iliona haki ya Mungu imedhihirika. Shetani alikuwa amesema kuwa dhambi ya mwanadamu haina cha kuiponya. Lakini kumbe, adhabu ya kuvunja sheria ilimwangukia aliye sawa na Mungu, kwa hiyo, wamadamu aliyekuwa huru, kuipokea haki ya Kristo, na kwa njia ya toba, atashinda nguvu za mwovu. Lakini Kristo hakuja kumwokoia mtu vivi hivi tu kwa kumfia. Alikuwa ili aonyeshe kwa malimwengu yote kuwa sheria ya Mungu haibadiliki. Kifo cha Kristo kilithibitisha kuwa haki na rehema ndiyo msingi wa serikali ya Mungu. Katika hukumu ya mwisho itaonekana kuwa hakuna sababu ya kuibakiza dhambi iendelee. Wakati Mhukumu wa ulimwengu atakapomwuliza shetani akisema “Kwa nini uliniasi?” Mwasi huyu hatakuwa na la kujibu.

Kwa kilio cha Mwokozi msalabani, “Imekwisha” matanga ya Shetani yalitangazwa. Mashindano makuu yaliamuliwa, adhabu ya

mwisho ya uovu ilipangwa. Siku itakapowadia iwakayo kama tanuri “...Na wenye kiburi wote, na watendao maovu, watakuwa makapi, na siku hiyo itayatekeleza, asema Bwana wa Majeshi, isiliachie shina, wala tawi” Malaki 4:1.

[245] Uovu hautainuka tena kamwe. Sheria ya Mungu itaheshimiwa kama sheria ya uhuru. Viumbe vyote vya Mungu vilivyokombolewa na vile vilivyoshuhudia shindano hili havitainuka kamwe kwenda kinyume cha sheria ya Mungu, ambayo ni ya haki na uhuru na upendo usiopimika.

30/Shetani na Mwanadamu Vitani

[246]

“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino”. Mwanzo 3:15. Uadui huu sio wa kawaida. Mtu alipoasi amri ya Mungu hali yake ya asili iligeuka kuwa uovu, ikipatana na hali ya shetani. Malaika waovu pamoja na wanadamu wakapatana. Kama Mungu asingeingilia kati, shetani na wanadamu wangalishirikiana kushindana na mbingu, na kwa njia hiyo watu wote wangejiunga pamoja kuwa wapinzani wa Mungu.

Shetani aliposikia kuwa kutakuwako uadui kati yake na mwanamke, na kati ya mzao wake na mzao wa mwanamke, alifahamu kuwa kwa vyo vyote mtu atawezeshwa kuwa mpinzani wake.

Kristo aliweka uadui katika mwanadamu kumpinga Shetani. Bila kuwa na uwezo huu wa neema uliowekwa kwa mwanadamu, daima angalikuwa mtumishi wa kutenda mapenzi ya shetani. Lakini kanuni mpya rohoni mwa mtu ilianzisha mashindano. Uwezo ambao Kristo alimpa mtu humwezesha kupingana na utawala wa shetani. Kuichukia dhambi badala ya kuipenda huonyesha kanuni ya mbinguni.

Uhasama baina ya Kristo na shetani ulionekana dhahiri wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza, jinsi ulimwengu ulivyompokea. Usafi na utakatifu wa Kristo uliamsha chuki kubwa kati yake na watu wasiomcha Mungu. Hali yake ya kujikana nafsi ilikuwa shutuma kwa mwenye majivuno, mwenye tamaa. Shetani pamoja na malaika waovu waliungana na watu wafedhuli kumpinga mwenye ukweli halisi. Hali ile ile ya uhasama ilionekana kwa wafuasi wa Kristo pia, wakipingana na maovu. Mtu yeyote anayepinga majaribu ya shetani huamsha chuki yake na kumletea mashambulio. Kristo na Shetani hawawezi kupatana. “Wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa” 2Tim. 3:12.

Wajumbe wa Shetani hutafuta kuwadanganya wafuasi wa Kristo, ili kuwaondoa katika njia nyofu ya kuafikiana na Kristo, ili kuwaon-

doa katika njia nyofu ya kuafikiana na Kristo. Huyapotosha maandiko ili kutimiza makusudi yao maovu. Roho ile iliyomwua Kristo, ndiyo hiyo inayowaamsha waovu kuwaangamiza wafuasi wa Kristo. Haya yote ni kivuli cha lile tangazo la kwanza la unabii kwamba, “Nitauweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya mzao wako na mzao wake”

Kwa nini shetani hakutani na upinzani mzito? Ni kwa kuwa askari wa Kristo wanashikamana na Kristo kidogo tu. Dhambi haiwachukizi kiasi kikubwa kama ilivyo mchukiza Bwana wao.

[247] Hawakutani nayo wakiwa na nia kamili ya kuipinga. Wamepushwa na mkuu wa giza. Watu wengi hawajui kuwa adui yao ni jemadari hodari wa vita, akipingana na Kristo. Hata wachungaji, wahubiri wa Injili hupita tu bila kujali kuwa adui yao halali daima. Hujifanya kana kwamba hawajali kuwako kwake shetani.

Adui Mwangalifu

Adui huyu mwangalifu hujiingiza kila mahali bila kukaribishwa. Huingia kwa kila nyumba, barabara, kanisa, mabarazani, mahakamani. Kazi yake ni kutia wasiwasi, kudanganya, kushawishi, kuhadaa watu, kuangamiza roho na miili ya wake kwa waume, watu wazima na watoto na kuleta fujo za kila aina. Huvunja nyumba za watu na kutangua ndoa. Hupanda mbegu za chuki mashindano na mauaji ya kila namna. Ulimwengu huyaona mambo haya kama kwamba yanaletwa na Mungu. Wote ambao hawamfuati Kristo ni wafuasi wa Shetani. Wakristo wanapochagua kujiunga na watu wasiomcha Mungu, hujitia majaribuni wenyewe. Shetani hujificha asionekane, na halafu hushawishi watu bila kuonekana.

Kuungana na desturi za dunia ili kuvuta watu kuwaleta waumini ulimwenguni. Kuzoeana na dhambi huifanya isiwe mbaya sana. Kama tukiletwa katika majaribu tutakuwa na hakika kuwa Mungu atatulinda. Lakini tukijipeleka wenyewe majaribuni tutaanguka tu bila shaka.

Kila mara majaribu hufaulu kuwateka wale wanaoonekana kwamba wako mbali na mitego yake. Uwezo na ujuzi wa vipawa vya Mungu. Lakini vitu hivi vikiwaongoza watu kutoka kwake, hugeuka kuwa mitego. Watu wengi wenye uwezo wa akili na ujuzi mkubwa, na hali safi, huwa vyombo mikononi mwa shetani.

Msisahau kamwe onyo lililotolewa zamani ambalo linatuhusu sisi wa siku hizi: “Mwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye, huzungukazunguka, akitafuta mtu ammeze” “Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani” 1 Pet. 5:8; Waefeso 6:11. Adui wetu mkuu anajiandaa kabisa kwa shindano kuu la mwisho. Wote wanaomfuata Kristo watahusika katika shindano hili la adui mkuu, Kadiri wakristo wanavyomwigiza Yesu, ndivyo watakavyopambana na mashambulio ya mwovu. [248]

Shetani alimjia Kristo na majaribu makali: lakini alishinda kwa kila jaribu. Ushindi huo unatuwezesha hata sisi kushinda pia. Kristo atawapa uwezo wote wanaotaka. Hakuna mtu atakayeshindwa na Shetani bila ukubali wake mwenyewe. Mjaribu hana uwezo wa kumlazimisha mtu atende dhambi. Anaweza kufanya itokee fujo au matatizo, lakini siyo kitendo cha dhambi. Kwa kuwa Kristo alishinda majaribu yote ya shetani, mambo hayo yatawapa shime wafuasi wake waendeleo kupigana kishujaa na shetani katika vita vya dhambi.

31/Roho Chafu

Malaika wa Mungu na malaika wa Shetani yaani roho wachafu, huelezwa dhahiri katika Maandiko Matakatifu nao wamejihusisha katika Historia ya wanadamu. Malaika watakatifu ambao huwahudumia wale watakaorithi wokovu, (Waebrania 1:14) hudhaniwa na wanadamu kuwa ni roho za wafu. Lakini maandiko hueleza wazi kuwa hawa sio zo roho za wafu.

Kabla mtu hajaumbwa, malaika walikuwako, kwa maana wakati msingi wa dunia ulipowekwa, “nyota za asubuhi ziliimba pamoja, na wana wa Mungu walipinga kelele za shangwe”. Ayubu 38:7. Badala ya kuanguka kwa mwanadamu dhambini, malaika walitumwa ili kuulinda mti wa uzima kabla mtu hajafa. Malaika wanawazidi wanadamu maana mwanadamu alifanywa “mdogo punde kuliko malaika” Zab. 8:5

Nabii husema, “Nilisikia sauti za malaika wengi pande zote za kiti cha enzi” mbele ya mfalme wa wafalme malaika hawa walikuwa tayari ili, “Mtendao neno lake”. Na “Kusikiliza sauti yake” “wasiohesabika” Ufunuo 5:11; Zaburi 103:20-21; Ebr. 12:22. Wao huenda huko na huko kama watumishi wa Mungu. Huruka kama umeme mbio yao ni ya ajabu. Malaika aliyeonekana kwenye kaburi la Mwokozi, uso wake ulikuwa kama “umeme” aliwafanya walizi wazimie kama wafu. Wakati mfalme Senakeribu aliomkufuru Mungu na kutisha Wana wa Israeli, malaika wa Bwana akatoka na kuwapiga Waashuri katika matuo yao watu mia na themanini na tano elfu. Ezekieli 1:14; Mathayo 28:3-4; 2Fal. 19:35.

Malaika wa Mungu hutumwa kwa kazi nzuri kuhusu watu wa Mungu. Kwa Ibrahimu walileta ahadi za mibaraka; huko Sodomu kumwokoa Lutu katika ajali; kwa Eliya, alipokuwa karibu kuangamia jangwani: kwa Elisha, katika gari la moto na farasi wa moto; alipozungukwa na adui; kwa Danieli, alipotupwa tunduni mwa simba; kwa Petro, alipofungwa na Herode ili auawawe, kwa wafunga wa Filipi kwa Paulo, katika dhoruba kali baharini; kwa Kornelio ili kufungua mawazo yake apokee Injili: kwa Petro, kupewa

ujumbe wa wokovu kwa mataifa. Hivyo ndivyo malaika wa Mungu wanavyowahudumia watu wa Mungu.

Malaika Walinzi

[250]

Kila mfuasi wa Kristo huwekewa malaika wa kumlinda. “Malaika wa Bwana hufanya kituo, akiwazunguka wamchao Bwana na kuwaokoa.” “Mwokozi alisema, kuhusu watu wanaomwamini”, “malaika zao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu” Zab. 34:7 Mat. 18:10. Watoto wa Mungu huzungukwa na hatari za mkuu wa giza, ambaye halali, lakini wanahakikishiwa ulinzi kamili wa malaika, ambao haukomi. Wamehakikishiwa ulinzi hivyo kwa sababu adui mkuu anao wajumbe wengi hodari wasiosinzia wanawakabili wana wa Mungu.

Roho wachafu, hapo mwanzo waliumba wakiwa malaika wema wasio na dhambi. Walikuwa wanalingana sawa na malaika wema ambao ni watumishi wa Mungu. Lakini wale walioanguka na kuasi, sasa wanafanya kazi ya kupingana na Mungu na sheria yake, pamoja kuwaharibu wanadamu. Waliungana na Shetani katika uasi wake, na sasa wanafanya kazi pamoja naye kupigana na mamlaka ya Mungu. Historia ya Agano la Kale hutaja kuwapo kwao. Lakini wakati Kristo alipokuwa duniani roho au malaika hawa walijidhihirisha kwa hali ya juu kabisa. Kristo alikuja kwa ajili ya kuwaokoa wanadamu na shetani alidhamiria kuutawala ulimwengu. Alikuwa amefaulu kusimamisha ibada ya sanamu pote palipowezekana, isipokuwa Palestina peke yake. Pale tu ambapo shetani hakuweza kusimamisha ibada ya sanamu, Kristo alikuja akiinyosha mikono yake ya upendo akiwaita wote wamjie ili wapate amani, na msamaha kwake. Majeshi ya mwovu pia yalifahamu kwamba iwapo kazi ya Kristo itafaulu, utawala wao utakwisha.

Watu waliokuwa wamepagawa na pepo wachafu walielezwa wazi katika Agano Jipya. Wale walikuwa wamepagawa na pepo hawakuwa na ugonjwa wa kawaida. Na Kristo alitambua kuwa hawa ni wajumbe wa Shetani tu wanaowasumbua watu. Yule mwenda wazimu wa Gadara, alivyokuwa akijiharibu na kuharibu watu waliokutana naye, au nao, maana walikuwa zaidi ya moja, walitenda hivyo kwa msukumo wa hawa pepo wachafu. Hali yao ya majeraha na upotevu wa mawazo huonyesha dhahiri kazi ya mwovu

[251]

Shetani. Mmoja wa mapepo hao alisema “Jina lake Legion, maana tu wengi” Marko 5:9. Katika jeshi la Kirumi, legioni ni kikosi cha watu baina ya elfu tatu mpaka elfu tano. Kwa amri ya Kristo mapepo wachafu walimtoka mtu huyo, hali akiwa sawa mwenye akili kamili. Lakini pepo wale waliwaingia nguruwe wakawatumbukiza haharini. Wenyeji wa Gadara badala ya kuwa na shukrani kwa mponyaji huyu aliyemponya maskini huyu, wakamwambia aondoke kwao. Mathayo 8:L22-34. Shetani akawazuia watu hao wasiupokee ujumbe wa Kristo, kwa kuwachochea wenyeji waone kuwa Yesu amewatia hasara ya nguruwe wao. Kwa hiyo wakamwambia aondoke kwao aende zake.

Kristo aliwaruhusu pepo wawaharibu nguruwe, kuwa kama kemeo kwa Wayahudi waliokubali kufuga wanyama hao wachafu kwa ajili ya uchumi. Kama Kristo asingewazuia wale pepo wasingewaangamiza nguruwe peke yao, bali hata wafugaji wao pia wangeotoswa baharini.

Zaidi ya hayo yote kitendo hivyo kiliruhusiwa ili wanafunzi wapate kuona uwezo wa shetani juu ya wanadamu na wanyama pia, ili wasikubali madanganyo yake. Pia lilikuwa kusudi lake kuwaonyesha uwezo wake wa kuwafungua watu kutoka katika vifungo vya uovu. Ingawa Yesu aliondoka, mtu yule aliyeponywa kwa ajabu alibaki huko akitangaza rehema za mponya wake.

Matukio mengine yaliandikwa pia. Binti wa mwanamke wa msirofoiniki aliyekuwa amepagawa na pepo ambaye Yesu alimponya kwa neno. (marko 7:26-30); kijana ambaye alikuwa akipagawa na pepo na kutupwa motoni na majini mara nyingi ili amharibu, (Marko 9:17-27); mwenda wazimu aliyekuwa na pepo, ambaye alifanya ghasia siku ya sabato huko Kapernaumu, ambaye Yesu alimwamuru asimsumbue tena (Luka 4:33-36). Wote hao waliponywa na Mwokozi. Karibu kila tukio Kristo aliwaamuru mapepo kana kwamba ni wenye akili na kuwaagiza wasiwasumbue tena. Waliokuwa wakiabudu Kapernaumu, walishangaa, wakaambiana wao kwa wao, “Ni jambo gani hili! Kwa nini uwezo na kwa nguvu, huwaamuru pepo, nao huwatoka.” Luka 4:36.

Watu wengine walikubali kushiriki mambo ya kishetani ili kusudi wapate uwezo ambao si wa kawaida. Watu kama hao hawakuwa na tatizo la pepo wachafu. Katika watu wa aina hiyo walikuwemo wenye nguvu ya uaguzo. Simon Magnus, Elimas mchawi,

na yule kijakazi aliyewafuata Paulo na Sila huko Filipi, Matendo 8:9, 18: 13:8; 16:16-18.

Hakuna watu walio katika hatari kuu, ila ni wale wanaobisha kwamba hakuna mashetani na pepo wachafu ambao ni malaika wa Shetani. Wengi hufuata mashauri yao, huku wakidhani kuwa wanafuata mashauri ya nia zao wenyewe. Kadiri tusogeleavyo mwisho wa wakati, ambavyo shetani anafanya juhudi kubwa kuwahadaa watu, hueneza habari po pote kuwa yeye hayuko. Kawaida yake ni kujificha asitambulikane wakati anapofanya kazi yake ya udanganyifu. [252]

Mdanganyaji mkubwa huyu huogopa kwamba akijidhihirisha tutang'amua hila zake. Kwa hiyo hajifunui wala njia zake. Hupendezwa sana anapodhaniwa kuwa kitu ovyo, mwenye sura chafu, jitu lisilo la maana. Hufurahi asikiapo jina lake likitajwa ovyo ovyo kimzaha. Maana mwenyewe anajifanya kuwa kitu cha ovyo. Kwa hiyo watu hujiuliza Je, kitu cha aina hiyo kweli kipo? kwa ajili ya ujanja wa shetani ndivyo sababu neno la Mungu hutufunulia siri zake, ili tujihadhari naye.

Tunaweza tu kupata usalama kwa Mwokozi wetu mwenye uwezo kuliko wake. Kila mara hulinda nyumba na watu waovu, lakini ni mara chache sana tujihadhari na mashambulio ya Ibilisi, ambayo kwa nguvu zetu wenyewe hatuyawezi. Kama akiruhusiwa, atapotosha nia zetu, atavuruga miili yetu, ataharibu mali zetu, na kutuamamiza. Lakini wafuasi wa Kristo wako salama katika ulinzi wake. Malaika wenye uwezo mkuu hutumwa kuwalinda. Mwovu na waovu wenzake hawawezi kupenya ngome Mungu aliyowazungushia watu wake.

32/Jinsi ya Kumshinda Shetani

Mashindano makuu baina ya Kristo na Shetani karibu yatak-wisha; kwa hiyo mwovu Shetani anajitahidi sana mara mbili ili kuishinda kazi ya Kristo anayowafanyia wanadamu., Anakusudia kuwashikilia watu katika giza la kutoamini mpaka Kristo amalize kazi yake ya kuwapatanisha wanadamu. Hali ya ubaridi inapotokea kanisani shetani hutulia, maana hayo ndiyo matakwa yake. Lakini watu wanapoamka na kuuliza swali: “Tufanye nini ili tupate kuokoka?” Basi huamka na kuingiza hali ya kupotosha, ili kupinga kazi ya Kristo na Roho Mtakatifu.

Wakati fulani malaika walipohudhuria mbele za Bwana ili kuabudu, shetani pia alihudhuria, sio kuabudu bali kuendeleza udhalimu wake wa kupinga haki. Ayubu 1:6. Wakati wakristo wanapokusanyika kwa ibada, naye huhudhuria ili kuyapotosha mawazo ya wenye kuabudu. Anapona watumishi wa Mungu wanaandaa mahubiri, yeye naye huyanakili, ili kuyapotosha kwa ujanja, kabisa kusudi yasiwafikie watu kama itakwiavyo, hasa kwa wale aliowadanganya. Mtu ambaye angepaswa kuusikia ujumbe huo, hushughulika na mambo mengine ambayo yatamzuia asiisikie ujumbe huo.

Shetani huwaona watumishi wa Mungu wakiwa na mzigo kwa ajili ya giza linalowafunga washiriki. Huwasikia wakiomba Mungu awasaidie katika hali yao ya ulegevu. Kisha kwa nguvu mpya huwavuta wafuate mambo mengine labda ya ulafi, au ubinafsi, ili kuwapumbaza wasiweze kupambanua mambo ya lazima wanayohitaji.

Shetani anajua kuwa wote ambao hawajali maombi na kusoma Biblia hawawezi kuyashinda mashambulio yake. Kwa hiyo huvumbua kila aina ya vitu vyenye kuwashughulisha hata wakose nafasi ya kuomba na kusoma. Wasaidizi wake wako tayari kabisa kuleta upinzani katika mambo ambayo Mungu anawatendea waadamu. Watawaonyesha watumishi hodari wa Mungu kama watu waliodanganyika na wadanganyaji. Ni kusudi lao kupotosha kila kusudi jema, na kazi bora, ili kutia mashaka kwa watu ambao hawana uzoefu na

ujuzi mwingi. Hutia kasoro na masuto kwa kila kazi njema. Lakini watu hao watafahamu baadaye wale wanaomfuata na kumtumaini. “Mtawatambua kwa matunda yao”. Mathayo 7:16; ufunuo 12:10.

Ukweli Hutakasa

[254]

Mdanganyifu mkuu anazo hila nyingi sana alizoandaa ili kuwapotosha watu wa aina mbalimbali ambao atawapata. Ni nia yake kuingiza watu kanisani ambao sio waongofu ili alete mashaka na hali ya kutoamini kwa wakristo kwa ajili ya hao. Watu ambao hawana imani kwa Mungu huingia na kushika kanuni kanisani na kuhesabiwa kuwa ni wakristo, kwa hiyo huingiza mambo ya kikafiri kanisani, na kuhesabiwa kuwa ni sehemu ya ukristo. Shetani anajua kuwa ukweli ukipokelewa kamili mioyoni hutakasa maisha. Kwa hiyo hutafuta kuingiza mafundisho ya uongo yahesabike kuwa ni sehemu ya Injili. Tangu mwanzo watumishi wa Mungu walikuwa wakishindana na waalimu wa uongo sio kuwa ni watu wabaya tu, bali ni waangamizaji halisi. Eliya, Yerima, Paulo waliwapinga vikali watu ambao waligeuka upande, wakaacha neno la Mungu na kufundisha mambo mengine. Hivyo wenye imani potofu ambao wanauhafifisha ukweli wa Biblia na imani ya kweli, hawakukubaliwa na watumishi hawa wa Mungu ambao walikuwa watetea kweli.

Maelezo hafifu na mapotofu ya Maandiko Matakatifu na imani potofu katika makanisa ya ulimwengu ambayo huleta mapingano na mafarakano, ni kazi ya mdanganyaji mkuu ili kupotosha mawazo ya watu. Mafarakano na tofauti katika makanisa ni matokeo ya kuacha ukweli wa maandiko Matakatifu, ili kuunga mkono nia zao.

Uli kusudi wapate uthibitisho wa nia zao, wengine husoma sehemu ya maandiko wakidhani kuwa inawaunga mkono ambavyo fungu zima la maandiko huwapinga. Kwa ujanja wa yule joka huyatengeneza yapate kufaa kwa njia potofu yadhaniwe kuwa yamo katika ukweli. Wengine hutafsiri mifano na vielelezo kwa upande wao, wala hawajali ukweli wote wa maandiko. Kisha huleta makosa yao ya kuieleza Biblia vibaya kuwa ndiyo ukweli wa Biblia.

Biblia Nzima ni Kiongozi

Wakati Biblia inaposomwa bila maombi, bila kuwa na nia ya kujifunza, ukweli wake utapotoshwa na kudhanikuwa Biblia inasema hivi, kumbe siyo maana yake. Biblia nzima lazima isomeke kikamilifu bila kuhafifisha sehemu yo yote.

[255] Mungu alitoa neno la unabii lililo imara, malaika na hata Kristo mwenyewe alikuja kumjulisha Danieli na Yohana mambo yatakayokuwa upesi sana “Ufunuo 1:1 mambo muhimu yahusu- yo wokovu wetu hayakufunuliwa kwa njia ya kutatanisha watu, kiasi cha kupoteza wengine, bali yako wazi kwa mtu anayeutafuta ukweli. Neno la Mungu liko wazi kwa mtu anayeutafuta ukweli. Neno la Mungu liko wazi kwa mtu yeyote anayelisoma kwa roho ya maombi na kujifunza.

Kule kuwa wafadhili kumewapofusha wengi wasigundue hila za adui wao. Amefaulu kuwapotoshea maana ya Biblia halisi na kuweka badala yake maelezo ya watu. Sheria ya Mungu imetupiliwa mbali, na makanisa yamo katika utumwa wa dhambi, wakati yakidhani kuwa yako huru.

Mungu amewajalia watu wawe na nuru nyingi ya elimu ya sayansi. Walakini hata wataalamu maarufu wa elimu kama hawaongozwi na Biblia hupotea katika majaribio yao ya uhusianisho baina ya sayansi na Biblia kama inavyofunua elimu halisi.

Elimu ya kibinadamu ina sehemu tu na sehemu nyngine siyo kamili. Kwa hiyo wengi hawawezi kuhusianisha sayansi na Neno la Mungu. Hujiendea tu na kujidhanika kuwa wenye elimu, wasilitambue Neno la Mungu lielezavyo sayansi halisi. 1Tim. 6:20. Kwa kuwa wanashindwa kueleza Mwumbaji na kazi zake katika vita vya asili, na sheria za asili, habari zinazoelezwa katika Biblia huziona kuwa si yakini, na hafifu. Watu wasiotumaini habari za Agano la kale na Agano Jipya, mara nyingi huendelea kiasi cha kutoamini kuwa Mungu yuko. Basi kinachowabakia ni kutangatanga tu, kama meli isiyokuwa na nanga. Huendelea kuishi katika ukafiri, Ni makusudi ya Shetani kuwashikilia watu katika giza la kubahatisha bahatisha, na kujaribu kugundua mambo ambayo Mungu hakuyadhihirisha. Shetani au Lusifa hakuridhika kwa sababu Mungu hakumfunulia siri zake, na makusudi yake, na sasa anawatia watu nia ya namna ile ile, hata wasijali amri za Mungu.

Kweli Ilikataliwa kwa Kuwa Huhusu Msalaba.

Kwa kadiri mambo ya kiroho yanapopuuzwa, na mkazo wa kujikana nafsi unapofifia, ndivyo watu wanavyopenda na kujiingiza kwa wingi makanisani. Shetani huwa tayari kutoa mambo kama hayo yasiyohitaji mkazo wa kiroho. Badala yake huleta maneno rahisi yenye kupendeza masikioni mwa watu. Hivyo ndivyo mapapa walivyopata nafasi ya kujiimarisha na kupendelewa. Na Waprotestanti wanafuata barabara ya namna hiyo, ndiyo maana wanaukataa ukweli wa Biblia, kwani unahusiana na msalaba. Wote wanaofuata kanuni ya kupendeka ulimwenguni, wataachwa wapokee uharibifu usiokawia” 2Pet. 2:1. Wote wanaoangalia udanganyifu kilegevu watapambana na hatari. “Kwa hiyo Mungu atawaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo, ili wahukumawe wote ambao hawakuamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu”. 2Thes. 2:11-12.

[256]

Makosa ya hatari

Baadhi ya makosa ya hatari ambayo Mwovu hutumia kwa ufanisi zaidi ni ishara za uongo za kuongea na wafu. Watu wanapokataa ukweli huangukia ndani ya madanganyo.

Kosa jingine ni kule kukana Uungu wa Kristo, wakisema kuwa kabla ya kuzaliwa hapa duniani, hakuwako kamwe. Jambo hili hupingana na elezo lake mwenyewe linalozungumza juu ya uhusiano wake na Baba yake kabla ya kuja hapa duniani. Fundisho hili huharibu ukweli wa Biblia kuhusu uhusiano huo. Iwapo watu wanakanusha ushahidi wa Biblia kuhusu Uungu wa Kristo, ni kazi bure kubishana nao. Hakuna hoja itakayowaamisha. Mwenye kushikilia mambo hayo hawezi kufahamu habari za Kristo, wala mpango wa Mungu wa wokovu wa Biblia.

Kosa jingine ni kule kukanusha kuwa shetani siye kiumbe kamili chenye utu na nafsi. Husema kwamba jina hilo hutumika kuonyesha mawazo ya watu waovu na tamaa zao ovu.

Kosa jingine ni lile lifundishwalo kwamba kuja kwa Kristo mara ya pili ni kule kunakotukia mtu afapo. Fundisho hilo hupotosha ukweli wa Biblia kuhusu kuja kwake katika mawingu ya mbinguni.

Shetani amekuwa akiwaambia watu kuwa, “Tazameni yuko sirini” Mathayo 24:23-26. Na wengi wamepotea kwa kuamini uongo huo.

Tena wanasayansi husema kuwa hakuna jawabu la kweli katika maombi. Hilo ni uvunjaji wa sheria ya kawaida ya miujiza, na miujiza haipo. Husema kuwa ulimwengu hutawaliwa na sheria za asili, ambazo Mungu hahusiki nazo. Hivyo huonyesha kwamba Mungu pia hutawaliwa na sheria hizo, kana kwamba yeye hana la kufanya na sheria hizo. Je, Kristo na wanafunzi wake hawakufanya miujiza? Kristo yule yule yu tayari kusikiliza sala za watu wake, sawasawa na wakati ule alipokuwa akiishi kati yao. Ni mpango wa Mungu kwetu kujibu maombi yetu, na kutenda maajabu, ambayo

[257]

kama tusingemwomba, yasingelitendeka.

Vionyesho Vya Neno

Makosa yanayofundishwa makanisani huondoa vionyesho vya Neno vilivyowekwa na Mungu katika Neno lake. Wachache hukataa ukweli fulani na wengine ukweli mwingine, mwisho huacha kweli na kuendesha hali ya umizimu katika jina la kanisa. Makosa ya wataalamu wa Biblia yamekwaza watu wengi na kuwatia mashakani. Inakuwa vigumu kwa mtu kupokea ukweli ambao ndani yake anakuta dhuluma, ukatili, na ubatili.

Neno la Mungu linaonewa kijicho upande, kwa sababu huke-me dhambi. Wale wasiotaka kulitii hulikataa. Wengi hulikana ili lisiwaingilie katika mipango yao. Wengine hulikataa kwa sababu huwazuia wasiwe wataka makuu.

Wengi huona kuwa ni vyema kusimama upande wa watu wa-sioamini wenye kutatanika na kutangatanga na watu wenye adili, ila mambo hayo yaliyotajwa, huyaficha ndani. Wengi hutafuta kitu katika Biblia cha kuwagongea wengine. Na wengine hujipanga kwanza upande mbaya ili wapate kubishana na baadaye hupatia huko kutokomea ukafirini.

Ushahidi Utoshao

Mungu ametoa ushahidi utoshao katika Neno lake kuonyesha tabia yake halisi, walakini mawazo hafifu ya binadamu hayawezi kufahamu mawazo ya Mungu. “Jinsi zilivyokuu, tajiri, hekima na

maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani” Warumi 11:33. Tunaweza kuufahamu upendo wa Mungu kwa uwezo wake tu. Baba yetu wa mbinguni atatufunulia kadiri ya vile inavyotufaa, ili tuweze kufahamu zaidi ya hayo tumtumaini tu.

Mungu hawezi kuondoa udhuru wa kutoamini. Wanaotafuta vichaka vya kujificha ili wasiamini watavipata. Na wale wanaotoa vikwazo vyote viondoke kwanza ndipo waamini, hawatafikia nuru. Roho isiyooongoka ni adui wa Mungu. Lakini imani inayochochewa na Roho Mtakatifu itastawi. Hakuna mtu atakayeimarisha imani yake bila kujitahidi. Watu wakijilegeza, mashaka yatawagharikisha.

[258]

Wala wenye mashaka, wasiamini humdharau Kristo. Wao ni miti isiyozaa, na huzuia miti mingine isipate nuru huwafunika na majani yao yanayozuia mwanga wa jua usiwafikie. Maisha ya watu hawa watawashuhudia kama watu wasiofaa.

Kuna njia moja ya kufuata kwa wale wenye mashaka. Badala ya kushughulika na mambo ambayo hawayajui wakazanie nuru ile waliyokwishaangaziwa na ndipo watapokea nuru zaidi.

Shetani ataleta vitu vinavyofanana na ukweli ili uwapotoshe wenye mashaka. Lakini hawezi kamwe kumpotosha mtu mtafuta ukweli kwa uaminifu. Kristo ndiye kweli, “Nuru inayomwangazia kila mtu ajaye ulimwenguni” “Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake atajua habari ya yale mafunzo.” Yohana 1:9; 7:17.

Bwana huwaruhusu watu wake waingie majaribuni, si kwa kuwa anapendezwa iwe hivyo, ila kwa sababu ni muhimu kwao kwa ajili ya ushindi wao wa mwisho. Angetaka kuwaficha wasiingie majaribu kwa utukufu wake, lakini hafanyi hivyo, kwa kuwa majaribu huwaandaa kushindana na hali zote za uovu. Hakuna kitakachowatenga na Mungu, wale wanaomtumaini kamili. Hakuna kitu, shetani au wanadamu waovu hawetaweza kuwatenganisha na Mungu. Kila jaribu la wazi au la siri linaweza kushindwa, “si kwa ushujaa au kwa nguvu, bali kwa Roho yangu, asema Bwana wa majeshi”. Zekaria 4:6.

“Ni nani atakayewadhuru, iwapo mnafuata mambo ya kweli na yaliyo mema?” 1 Pet. 3:13. Shetani anajua kuwa mtu mnyonge anayemtumaini Kristo, huwa na nguvu kuliko majeshi yote ya mwovu. Kwa hiyo hutafuta kuwatoa askari wa msalaba watoke katika ngome yao, aliwashawishi kutoka apate kuwaaangamiza wote

[259] watakaothubutu kutoka. Kuambatana na Mungu na kushikilia ari zake tu, ndipo tutakuwa salama.

Hakuna mtu atakayekuwa salama kwa siku au saa bila maombi. Msihi Bwana akupe hekima ujue Neno lake. Shetani ni hodari kusoma Maandiko, akiyatafsiri kama aonavyo, hasa sehemu anazooka kuwa zitakunasa. Tunapasa kujifunza kwa unyenyekevu na kuomba, wakati wote katika imani, ili tupate kujua hila za shetani. Ombi letu na liwe: “Usitutie majaribuni” Mathayo 6:13

33/Baada ya Kufa Kuna Nini?

[260]

Shetani ambaye alianzisha uasi huko mbinguni, anatamani kuwaunga weneyji wa dunia hii katika vuta yake na Mungu. Adamu na hawa kwa furaha walikuwa watiifu wa sheria ya Mungu, utii wao ulikuwa hakikisho la daima kwa madai ya Shetani kwu sheria ya Mungu ni ya kukandamiza. Shetani aliazimia kuwaangusha, ili apate kutawala duni hii, na kuusimamisha utawala wenye kupingana na Mungu.

Adamu na hawa walikuwa wametahadharishwa kuhusu hatari ya adui huyu. Lakini Shetani alijificha kabisa akitenda mambo yake kisirisiri. Akimtumia nyoka kama chombo chake, nyoka ambaye alikuwa kiumbe kizuri alimzungumzia Hawa, akisema, “Eti hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustanini?” hawa hakuthubutu kushauriana na adui akaanguka kwa ulaghai wake adui; “Mwanamke akamwambia nyoka; Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya busatani Mungu amesema Msiyale wala msiyaguse msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, hakika hamtakufa; kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua mema na mabaya”. Mwanzo 3:1-5.

Hawa akakubali kushindwa, na kwa mvuto wake Adamu naye akaingia dhambini. Wote wakayakubali maneno ya nyoka, wakaonea mashaka maneno ya Mwumbaji wakaona nafsinini mwao kuwa aliingilia uhuru wao.

Lakini Adamu aligundua nini maana ya maneno ya Mungu, Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtakufa hakika? Je, yalikuwa na maana ya kumzuia asiingie katika hali bora zaidi? Adamu hakuona kuwa maana ya maneno ya Mungu ilikuwa hivyo alivyosema nyoka. Mungu akasema kuwa adhabu ya kutotii maneno yake ni kurudi mavumbini, yaani kufa. “Maana wewe ni mavumbi, na mavumbini utarudi”. Mwanzo 3:19. Maneno ya shetani kuwa, macho yenu yatafumbuliwa, yalikuwa na ukweli tu katika sehemu hii, maana macho

yao yalifumbuliwa wakaona upumbavu wao. Wakajua mabaya na kuonja uchungu wa matunda ya uasi wao.

[261]

Mti wa uzima ulikuwa na uwezo wa kuendeleza uzima. Adamu alikuwa na hiari ya kuuendea mti wa uzima bila kikomo na kuyafurahia matunda yake, naye angeishi milele. Lakini alifanya dhambi akazuiliwa asiyale tena matunda ya mti wa uzima, hivyo akawa mtu wa kufa. Hali ya kutokufa ilikuja kwa ajilia ya uasi, na mwanadamu asingekuwa na tumaini lolote la kuishi milele, kama Mungu kwa rehema zake asingemtoa Mwanawe kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. “Mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wametenda dhambi” “Kristo Yesu aliyebatilisha mauti na kufunua uzima na kutokuharibika kwa ile Injili” Ni kwa njia ya Yesu tu ndipo hali ya kutokufa hupatikana. “Amwaminiye Mwana yu na uzima wa milele, asiyemwamini Mwana hataona uzima” Rumi 5:12; Tim 1:10; Yohana 3:36.

Uwongo Mkuu

Aliyewaahidi watu uzima kwa kutotii sheria, alikuwa mwongo mkuu, na mdanganyaji mkuu. Akizungumza kwa njia ya nyoka huko Edeni, alisema, “Hamtakufa hakika”. Hilo lilikuwa tangazo lake la kwanza kuhusu kutokufa kwa roho. Walakini tangazo hili ambalo ni uwongo wa Shetnai ni mwangwi unaohubiriwa na wahubiri wengi, na hupokelewa na watu maelfu, sawa kama vile lilivyopokelewa na wazazi wetu wa kwanza. Tangazo la Mungu ni hili “Roho itendayo dhambi itakufa (Eze. 18:20) lakini Shetani akageuza kuwa, maana yake ni roho itendayo dhambi haitakufa. Kama mtu ageruhusiwa kutwaa matunda ya mti wa uzima baada ya kukosa, dhambi ingedumishwa milele. Lakini hakuna hata mmoja wa wazao wa Adamu aliyeruhusiwa kula matunda ya uzima. Kwa hiyo hakuna mwenye dhambi ambaye hudumu milele.

Baada ya anguko la mwanadamu, shetani aliwaagiza malaika zake wawafundishe wanadamu waamini kuhusu umilele wa roho, kwamba hata kama mtu amekufa, roho yake huendelea kuishi. Baada ya kuwaaminisha watu namna hiyo, huwaongoza waamini kwamba mtu mbaya afapo huendelea kuteseka katika uharibifu milele. Sasa mwovu huyu hutupa lawama kwa Mungu kwamba huwaadhibu wote ambao hawampendezi, na ya kwamba wakati wanapoteseka

motoni namna hii, Mungu huwachungulia na kutosheka. Hivyo ndivyo mwovu anavyompaka Mwumbaji matope. Ukatili ni wa shetani. Mungu ni Upendo. Shetani ndiye huwashawishi watu kufanya dhambi na kuwaharibu ikiwa anaweza. Shetani hupinda mafundisho kuhusu upendo, rehema, haki, yakaonekana kuwa machukizo ya ukatili wa kutesa watu katika moto huko ahera milele na milele.

Je, katika Neno la Mungu mafundisho ya jinsi hiyo yanapatikana wapi? Hali ya kawaida ya kujisikia kwa kibinadamu ndiyo ilinganishwe na ukatili wa kishetani? La, Neno la Mungu halifundishi namna hiyo “Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu na kuiacha njia yake mbaya, akaishi, ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa?” Eze. 33:11.

[262]

Je, Mungu hupendezwa kuona mateso ambayo hayana mwisho ya watu wake? Je, hufurahia kuona viumbe wake wakiomboleza siku zote katika moto anaowachoma? Je, vilio hivyo vya huzuni vinakuwa nyimbo tamu za kusikilizwa na Mungu Mwenyezi mwenye pendo? Hayo ni makufuru na matusi kwa Mungu. Utukufu wa Mungu hauongezwi na kustawishwa kwa mateso ya dhambi milele na milele.

Uzushi Kuhusu Mateso ya Milele.

Mwovu ameleta uzushi wa mafundisho kuhusu mateso ya milele. Dini ya Biblia yenye kujaa pendo na wema wa kila hali, imetiwa giza na kufunikwa na hali ya hofu na ushirikina. Shetani amechafua tabia ya Mungu kwa kumsingizia mambo ya kila namna. Mwumbaji wetu mwenye rehema anahesabiwa kana kwamba ni mkatili mwenye kuogopwa kwa hofu na kutetemeka kiasi cha kuchukiwa. Hali ya kutisha ya tabia ya Mungu imeelezwa ulimwenguni pote na wahubiri, hata imewafanya watu mamilioni kuwa watu wenye mashaka kwa Mungu na wakafiri.

Fundisho la mateso ya milele ni moja ya mafundisho mapotofu, mvinyo ya makufuru (Ufunuo 14:8; 17:21) ambayo Babeli imevalevya mataifa yote. Wajumbe wa Kristo wameyapokea mafundisho haya kutoka kwa Rumi, kwa vile walivyokubali kuipokea sabato bandia, ambayo ni siku ya jumapili. Tunapoliacha neno la

Mungu na kugeukia mafundisho ya uwongo kwa ajili ya mapokeo kutoka kwa baba zetu, pale tunatumbukia katika hukumu iliyotangazwa juu ya Babeli; yaani tunakunywa mvinyo wa uasherati wake.

Watu wengi wamevutwa kusimama upande mpotovu. Wao huona jinsi Biblia inavyomwonyesha Mungu kwamba ni Baba mwenye huruma na upendo hawawezi kukubali kuwa hawezi kuwatia viumbe wake katika hali ya kuwa matesoni milele na milele. Wakiamini kuwa roho za binadamu hazifi kamwe; na tena kwamba watu wote wataokolewa. Hivyo basi mwenye dhambi anaweza kuishi katika anasa za dhambi bila kujali maagizo ya Mungu, na baadaye Mungu atampokea tu. Mafundisho ya namna hiyo husisitiza juu ya rehema za Mungu na kupuuza haki yake. Mambo kama haya huwafurahisha watu wawezao mambo ya kimwili tu.

Wokovu wa Jumla Maandiko Hayausemi.

[263] Watu wanaoamini kuwa uko wokovu wa jumla, hufuta maandiko ya Biblia. Wahudumu wa Kristo huukariri kariri uwongo ule nyoka aliosema katika Edeni, kwama “Hamtakufa hakika” “Siku mtakayokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafumbuliwa, nanyi mtakuwa kama Mungu” alisema kuwa mdhambi mashuhuri — mwuaji, mwizi, mzinzi, baada ya kufa huingia katika raha ya milele. Jambo ambalo ni hadithi ya uwongo kabisa. Hivyo huwafurahisha wapenda anasa za ulimwengu.

Kama ingalikuwa kweli kwamba watu wote huenda mbinguni moja kwa moja wakati wanapokufa, basi sote tungalitamani kifo kuliko kuishi. Wengi wameongozwa na imani ya jinsi hii. Wamejiua wenyewe ili wapate kwenda katika ulimwengu wa raha huko mbinguni kuliko kuhangaika hapa chini na maisha haya ya taabu.

Mungu amesema wazi katika Neno lake kuwa atawaadhibu wote wavunjao sheria yake. Je, anazo huruma nyingi kiasi cha kuwaacha wenye dhambi bila kuwaadhibu? Hebu tazameni msalaba wa kalvari. Kifo cha Mwana wa Mungu huthibitisha kuwa, “Mshahara wa dhambi ni mauti” Warumi 6:23, kwamba kila uvunjaji wa sheria ya Mungu ni lazima upate mshahara wa namna hiyo. Kristo asiye na dhambi akafanywa kuwa dhambi kwa ajili ya wanadamu. Aliuchukia uasi na hatia ya mwanadamu, akifichwa uso

wa Babaye mpaka roho yake ilipovunjika na uhai wake kutoweka kabisa, yote hayo yalitendeka ili mwanadamu akombolewe. Na kila mtu anayekataa kupokea toleo hilo lililotolewa kwa gharama kuu namna hiyo, lazima apate mshahara ambao ni malipo ya uasi wake mwenyewe. Adhabu hiyo ataibeba mwenyewe.

Masharti Yamewekwa

“Nami nitampa mwenye kiu chemichemi za maji ya uzima bure”. Ahadi hii ni ya wenye kitu tu “Yeye ashindaye atarithi haya yote, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu” ufunuo 21:6-7. Masharti yamewekwa. Ili kurithi mambo yote, ni lazima tushinde dhambi, “Haitakuwa heri kwa mwovu” Mhubiri 8:13. “Mwovu anajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira ya ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake” “Dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu” Warumi 2:5-6,9.

“Hakuna mwasherati wala mchafu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu” “Heri wazishikao amri zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya” Wae-feso 5:; ufunuo 22:15.

[264]

Mungu amewaonyesha wanadamu namna anavyofanya na dhambi. “Wote wasio haki atawaharibu” “Wakosaji wataangamizwa pamoja. Wasio haki mwisho wao wataharibiwa” Zab. 145:20; 37:38. Mamlaka ya Mungu yatakomesha maasi walakini malipo ya haki yatadumishwa katika tabia ya Mungu mwenye rehema na fadhili.

Mungu halazimishi dhamiri ya mtu. Hana haja ya utii wa juu juu. Anataka viumbe vyake wampende kwa sababu anastahili upendo. Anataka wamtii kwa kuwa wanatambua kuwa kwa yote anayowatendea wanaona ni haki na inapasa kutoa shukrani, kwa hekima na haki na fadhili zake.

Kanuni ya serikali ya Mungu inaafikiana na maneno ya Kristo, kwamba “Wapendeni adui zenu” Mathayo 5:44.

Mungu huwapatiliza waovu kwa ajili ya manufaa ya wote wa ulimwengu, na hata kwa manufaa ya hao wanaopatilizwa. Angetaka kuwafanya wajisikie wenye furaha. Huwazungushia na kila aina ya

upendo wake na rehema zake. Wakipokea vipaji vyake, lakini bila kujali. Daima wanapokea vipawa vyake lakini hawamtii Mungu. Bwana amevumilia muda mrefu upotovu wao lakini wakiendelea kuasi tu. Je, atawafunga kwa minyororo upande wake ili wafanye mapenzi yake?

Hawako Tayari Kuingia Mbinguni

Wale waliomchagua Shetani kuwa kiongozi wao hawako tayari kuingia mbingui mbele za Mungu, Kiburi, udanganyifu, ufedhuli, ukatili vimekwisha kukazwa katika tabia zao. Je, wanaweza kwenda mbinguni wakaishi pamoja na wale waliowachukia walipokuwa duniani? Ukweli hautakubaliana na uwongo; unyenyekevu hauendi pamoja na majivuno; usafi wa maisha hautapatana na udhalimu; upendo usio na ubinafsi hautaafikiana na hali ya ubinafsi. Mbingu itawapa kitu gani wale waliozama katika kujipenda nafsi?

Ingewezekana kwa watu ambao wanamchukia Mungu, na ukweli, na utakatifu, kuunganika na kundi la mbingu, linalopenda kuimba nyimbo za furaha na sifa?

[265] Walipata muda wa miaka mingi ya kujirekebisha, lakini hawaku-jishughulisha kupenda usafi wa maisha. Wala hawakujifunza lugha ya mbinguni. Sasa, wamechelewa.

Muda wa miaka mingi ya kumwasi Mungu imewathibitisha kuwa hawafai lo lote, wala hawawezi kufaa kuingia mbinguni. Utakatifu wa mbinguni na amani yake vingaliwawia mateso makuu. Utukufu wa Mungu, wao ungekuwa moto uteketezao. Wangalitamani kukimbia kutoka mahali hapo patakatifu, hata kutamani kufa kuliko kukaa mbele za yule aliyewafia ili kuwaokoa. Maangamizi ya waovu wanasababishwa na uchaguzi wao wenyewe. Kufungiwa wasikanyage mbinguni kunatokana na hiari yao wenyewe. Mungu ni wa haki na mwenye fadhili. Moto wa siku ya mwisho, sawa na maji ya gharika ya siku za Nuhu, ni hukumu ya Mungu kwa ajili ya maovu ambayo watu walijichagulia kupata. Nia zao zimejizoeza kuasi. Na wanapokufa, hufa na hali ile ile ambayo haibadiliki kuwa na utii. Huwa wenye chuki wala sio upendo.

Mshahara wa Dhambi

“Mshahara wa dhambi ni mauti, lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu” “Mauti ya pili” “inachukua mahali pa uzima wa milele” Warumi 6:23; ufunuo 20:14.

Katika dhambi ya Adamu mauti iliwapitia watu wote. Wote hufa sawasawa, bila tofauti. Kwa njia ya mpango wa wokovu, wote watatoka makaburini. “Kutakuwako ufufuo wa wenye haki na waovu”. “Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika katika Kristo wote watahuishwa.” Lakini patakuwa na tofauti katika makundi mawili. “Wote waliomo makaburini watasikia sauti yake, nao watatoka, wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliofanya mabaya kwa ufufuo wa hukumu” Matendo 24:15 1kor. 15:22, Yoh. 5:28-29.

Ufufuo wa Kwanza

Wale “wanaohesabiwa kuwa wanastahili kuupata ule ufufuo wa wafu” “ni heri na watakatifu” juu yao mauti ya pili haina nguvu. Luka 20:35; Ufunuo 20:6. Lakini wale ambao hawakutubu na kupata msamaha kwa imani, lazima wapokee “msamaha wa dhambi” “adhabu kwa kadiri ya matendo yao” nao watamalizikia katika “mauti ya pili”

Kwa kuwa haikuwezekana Mungu kumwokoia mdhambi, kwa kuwa hakutaka kuokolewa, basi humwondolea hali ya kutokuishi ambayo uasi wake mwenyewe umeisababisha, na kwa vile ame- [266] jithibitisha mwenyewe kuwa hafai lolote. “Maana bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo” “Nao watakuwa kama kwamba hawakuwepo kwemwe” Zaburi 37:10; Obadia 16. Watazama huko kusikokuwa na matumaini na kusahauliwa milele.

Hivyo ndivyo dhambi itakavyokomeshwa. “Umemwangamiza mdhalimu, umelifuta jina lao milele na milele. Adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele” Zab. 9:5-6. Yohana mwandishi wa ufunuo, alisikia nyimbo za sifa zikiimbwa bila machafuko yoyote. Hakuna mpotevu yeyote aliyekuwa akiteswa na kumkufuru Mungu. Hakuna vilio vya mateso vilivyokuwa vikichanganyikana na nyimbo za furaha za kumtukuza Mungu za waliookolewa.

Juu ya kosa la asili la hali ya umilele, sasa kunakuwa na ufahamu wa kifo. Kama ilivyodhaniwa kuwa kuna mateso ya milele ambayo ni kinyume cha maandiko na mawazo ya binadamu. Kufuata imani ya wengi ni kwamba waliookolewa ambao wako mbinguni wanafahamu mambo yote ya hapa duniani. Lakini itawezekanaje kuwa na furaha kwa wafu kufahamu maisha ya kusumbuka na dhiki waliyo navyo wenyeji wa duniani? Kungekuwa na machukizo sana kujua mtu afapo huingia motoni huko ahera.

Lakini Biblia inasemaje? Mtu hafahamu neno lo lote wakati afapo. “Pumzi yake hutoka, hurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake hupotea”. “Walio hai wanajua kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao hupotea yote pamoja. Wala hawana sehemu tena katika jambo lolote lililofanyika chini ya jua. Kwa kuwa kuzimu hakuwezi kukusifu; mauti haiwezi kuadhimisha.

Wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako. Aliye hai naam aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo” “Maana mautini hakuna kumbukumu yako, katika kuzimu ni nani atakayekusifu?” Zab. 146:4; Mhubiri 9:5-6; Isaya 38:18-19; Zab. 6:5.

Siku ya Pentekoste Petro alisema kuwa Daudi “alikufa, akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo” “Maana hututhibitisha kuwa wenye haki wanapokufa hawaendi mbinguni.”

[267] Paulo alisema “Maana kama watu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka imani yenu ni bure: na hao waliolala katika Kristo wamepotea” 1Kor. 15:16-18. Kama kwa muda wa miaka 4000 wenye haki waliokufa wamekwenda mbinguni moja kwa moja, Paulo aliwezaje kusema kuwa, kama hakuna ufufuo, waliolala katika Kristo wamepotea?

Yesu alipokuwa karibu kuwaacha wanafunzi wake hakuwaambia kuwa watakwenda kwake karibuni, bali alisema, “nakwenda kuwaandalia mahali, nikienda kuwaandalia mahali nitakuja tena, niwakaribisheni kwangu” Yoh. 14:2-3. Paulo anatuambia zaidi kuwa, “Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele”. Na

kisha aongeze kusema “Basi farijianeni kwa maneno haya” 1 Thes. 4:16-18. Wakati wa kuja kwa Kristo makaburi yatafunguliwa, na waliokufa katika Kristo watafufuliwa ili wapate uzima wa milele.

Wote watahukumiwa kufuatana na mambo yaliyokuwa yameandikwa vitabuni, nao watapokea thawabu kadiri ya kazi yao ilivyo. Hukumu hii haitendeki wakati mtu afapo. “Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki”. “Angalia, Bwana anakuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya wale wote”. Matendo 17:31. Yuda 15.

Sasa, kama watakatifu wako mbinguni tayari, au waovu wamo motoni tayari, kuna maana gani ya kukaa na kuwahukumu watu tena? Maneno ya Mungu yanaweza kufahamiwa na watu wa kawaida. Lakini watu wanyofu hawewezi kuona hekima au haki katika maneno ya kawaida? Je, watu hawa watapewa heko na Bwana, wakiambiwa “Vema mtumishi mwema na mwaminifu, na kuingizwa katika furaha ya Bwana, wakati wameishi muda huo wote? Je, waovu nao watatolewa katika moto, halafu waambiwe ‘Ondokeni kwangu ninyi nyote mtendao maovu?’” Mathayo 25:21,41.

Mafundisho yale yanayohusu kutokufa kwa roho ni madanganyo yaliyokazwa na kanisa la Rumi, kutokana na imani ya wakafiri. Mafundisho, kutokana na imani ya wakafiri. Mafundisho hayo Luther huyaita hadithi chafu za kipumbavu na udanganyifu mbaya mno, ambazo kanisa la Rumi huzishikilia kama chombo chao cha kupoteza na kupumbaza watu. Biblia hufundisha kuwa watu waliokufa wanalala makaburini mpaka siku ya ufufuo.

Wenye haki hupumzika katika taabu zao. Kwa muda wa kupumzika ni mfupi tu, ingawa huonekana mrefu. Kwao muda ni mfupi. Wao wanalala, wataamshwa na parapanda ya Mungu ili wapokee hali ya kutokufa. “Maana parapanda Italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu Basi mwili huu wa kuharibika utakapova kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakuwa neno lililoandikwa: mauti imemezwa kwa kushinda” 1Kor. 15:52-54.

Wakiamshwa kutoka usingizini wa mauti, hawataanza kufikiri mahali walikofia na maisha yao ya mwisho, kabla ya kuingia kaburini. Watakapoamshwa kutoka makaburini kitu cha kwanza watakachona ni ushindi na kelele za ushindi. “Ku wapi Ewe mauti kushinda kwako? U wapi ewe Mauti ushindi wako? U wapi ewe

mauti uchungu wako? Ku wapi Ewe kaburi kushinda kwako?” 1 Kor. 15:55.

Marejeo:

E. Peteavel. *The Problem of Immorality* p. 225.

34/Mizimu ni Nani Katika Imani ya Roho

[269]

Mafundisho yahasuyo kutokufa kwa roho kwanza yalitokana na imani ya wapagani, na wakati wa giza la kiroho mafundisho haya yaliingizwa katika imani ya kikristo na kuhesabika kuwa ni mojawo ya ukweli, na yakashika mahali pa Maandiko yasemayo kuwa, “wafu hawajui neno lo lote” Mhubiri 9:5. “Watu wengi huamini kuwa roho za wafu ndizo zile, zisemwazo kuwahudumu wale watakaourithi wokovu” Waebrania 1:14.

Imani ya kuwako roho za wafu kuja kuwahudumia watu wanaoishi, imeandaa njia ya kuingizia mambo ya kisasa ya kuongea na wafu. Kama watu wanaoufahamu unaozidi ule waliokuwa nao wakati walipoishi, mbona hawaji tu kiwazi na kuwaelimisha watu? Ikiwa roho za wafu huwazungukia jamaa zao walioko duniani, mbona hawakai na kuongea nao? Mbona wanaoamini kuwa mtu akifa huwa anajua mambo, hukataa nuru ya Mungu inayoeleza mambo ya roho? Hapa ndipo Shetani hufanyia kazi yake. Malaika waovu huonekana kama wajumbe katika ulimwengu wa roho.

Mkuu wa uovu yaani shetani anao uwezo wa kuleta sura za watu waliokufa ambao ni jamaa. Maigizo ya watu hao ni kamili kabisa. Huonekana kama wao halisi. Watu wengi hufarijika kuwa ndugu na rafiki zao wako wanaishi huko mbinguni. Bila kujihadhari na hatari yo yote, hutega masikio kwa “roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani” 1 Tim. 4:1.

Waliokufa bila kujitayarisha, yaani bila kujitoa kwa Kristo, huda kuwa wako katika furaha kuu huko mbinguni. Watu hawa bandia wanaojidai kuwa wanakaa rahani mbingu, mara nyingine husema maneno ambayo huwa ya kweli. Wakishakuaminiwa, hutoa mafundisho yaliyo kinyume cha Biblia. Kwa kuwa mara nyingine husema maneno ya kweli na kutabiri mambo fulani ambayo hutokea kuwa kweli, hivyo mafundisho yao ya uongo hukubaliwa kama mafundisho ya kweli ya Biblia. Sheria ya Mungu imewekwa kando, na Roho wa neema amedharauliwa. Hiyo ndiyo mizimu, na roho

za mashetani. Roho hizi hukataa Uungu wa Kristo na kumhesabu Mwumbaji kuwa na hali sawa na yao.

[270] Wakati matokeo ya udanganyifu huo hukubaliwa kama ukweli, hutokea ishara ambazo ni kazi za yule mwovu huwadangaya watu wakaziamini kama ishara za Mungu. Watu wengi huamini kuwa hali ya kuongea na wafu. Au mizimu ni ujinga wa kibi-nadamu. Wanapokabiliwa na maonyesho ya wazi ambayo hawawezi kuyakanusha, hukubali kuwa hayo kutoka kwa Mungu.

Kwa msaada wa shetani wachawi wa Farao waliigiza kazi ya Mungu na kufanya miujiza. Soma Kutoka 7:10-12. Paulo ashuhudia kuwa kuja kwa Bwana kutatangiwa na “Kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na maajabu za uongo, na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea” 2Tes. 2:9-10. Yohana naye anasema, “Naye, afanye ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaa juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya” ufunuo 13:13-14. Hapa sio ujanja wa kibinadamu unaoelezwa. Watu hudangaywa na shetani kwa ishara ambazo wajumbe wake huzifanya, sio wanazojifanya kuzifanya.

Mwito wa Shetani Wenye Akili

Kwa kuwa wataalamu na wenye akili, Shetani huwaingilia kwa njia ya kuwaletea mizuka ya kiroho kwa njia ya akili sana, yaani sura za rafiki na jamaa zao waliokufa, kana kwamba wanaweza kuongea. Hupendelea kuwaza mawazo ya ajabu ya kuisisimua na ya utaalumu, yaliyojaa mambo ya upendo na fadhila tele. Huwafanya watu kupendelea mambo ya jinsi hiyo, na kupuuzia mambo ya milele ya Mungu.

Shetani huwadanganya watu sasa kama vile alivyomdanganya Hawa katika bustani ya Edeni, kwa njia ya kuwafanya wawe na hamu ya kujitukuza. Huwaambia “Mtakuwa kama miungu”, “mkijua mema na mabaya” Mwanzo 3:5. Wenye hali ya mizimu hufundisha kuwa mtu ni kumbe chenye maendeleo ambayo huchunguza mambo ya Mungu. Tena, husema, maamuzi yote ni sawa kutokana na ubinafsi. Husema, “Mtawala”. Mwingine husema, “Ye yote wa kweli aliye mkamilifu ni Kristo”

Hivyo shetani amejiweka na kumweka mtu wa dhambi kama mtaalamu na mtawala wa haki. Haya ni maendeleo, siyo kupanda juu, bali ya kudidimia chini. Mtu hawezi kupanda zaidi ya kipeo chake cha uzuri na wema. Kama kujitukuza nafsi ndilo kusudi la shabaha yake kuu, hataweza kamwe kufika popote. Neema ya Mungu ndiyo pekee yake iwezayo kumkweza mtu. Kama mtu akiachwa ajiendeshe mwenyewe, ataanguka tu. [271]

Mwito Kwa Wapenda Anasa

Kwa watu wenye kupenda anasa, wataka makuu, na wenye majivuno hali ya mizimu hufanya hila kwao kidogo tu. Kwa kuwa hali zao hufanana na zao. Shetani huona aina ya dhambi ambazo kila mtu huzipenda, halafu hutafuta nafasi ya kuzihimiza ili zifanywe. Huwajaribu watu na kuwatumbukiza katika hali ya kutokuwa na kiasi, ili apate kuwadhoofisha miili yao, akili na hali ya utambuzi ili wawe watu wasiofaa. Huwajaribu watu maelfu kwa njia ya tamaa na kuuharibu utu wote. Ili kukamilisha kazi yake, mizimu husema kuwa, “elimu halisi ni ile inayomweka mtu awe na sheria ya Mungu kwamba cho chote ni cha haki, hata ni dhambi ya aina yo yote Mungu hahukumu, yaani hana la kusema juu yake, na kwamba dhambi zote hazina hatia” watu wanapoamini kuwa dhamiri zao na matakwa yao ndiyo tosha kabisa, wala hawana haja na sheria, na kuwa huo ndio uhuru, kwamba mtu ni juu yake kujiamulia yote. Je, katika hali kama hiyo, uharibifu, si utajaa kila upande? Watu maelfu huwa tayari kukubali mambo ya tamaa. Shetani huwakumba watu maelfu katika mtego wake ambao hujidai kuwa ni wafuasi wa Kristo.

Lakini Mungu ametoa nuru ya kutosha ili kugundua mitego hiyo. Misingi hasa ya mizimu ni mapigano makuu ya Maandiko Matakatifu. Biblia husema wazi kuwa wafu hawajui neno lolote. Kwamba mawazo yao yamepotea, wala hawana sehemu katika watu wanaoishi nchini.

Zaidi ya hayo Mungu amekataza kabisa hali yo yote ya kujifanya kana kwamba mtu ameongea na mizimu. Maongezi ya mizimu, ambayo watu hudai kuwa wanaongea na watu wa ulimwengu mwingine, huitwa na Biblia, kuwa ni “roho za mashetani” Soma Hes. 25:1-3; Zab. 106:28; 1Kor. 10:20; Ufu. 16:14. Kufuata

[272]

mambo yao kulikatazwa na adhabu ya kifo iliyotolewa kwa mwenye kuzifuata. Lawi. 19:31; 20:27. Lakini mizimu au miungu hawa wameingia katika wanasayansi, wameshambulia makanisa, na kupata ukubali katika vikao vya bunge, hata na katika mahakama na ofisi za watawala. Udanganyifu huu mkuu ni umbo jingine la wachawi wa zamani.

Kwa kuwa anayatukuza mambo ya kibinadamu kana kwamba ni ya mbinguni, shetani huambia ulimwengu, “Si kitu, au haidhuru, uamini Mungu au usiamini, ukubaliane na Biblia au la, ishi upendavyo tu, mbingu ni yako” neno la Mungu husema, “Ole wao waitao baya jema na jema baya waitao giza nuru, na nuru giza” Isaya 5:20.

Biblia Huhesabiwa Kama Hadithi

Mitume, ambao wanaigizwa na roho hizi au mizimu hufanywa watofautiane katika usemi na vile walivyoandika walipokuwa wakiishi duniani. Hivyo ndivyo mizimu huwafanyia wale wanaojifanya kuwa wanaongea na wafu. Shetani huwafanya walimwengu waamini kuwa Biblia ni hadithi tu za kupiga chuku sawa na zinginezo, kinawafaa watoto wa jamii lakini sasa hakifai kutumika siku hizi. Kitabu ambacho kitamhukumu pamoja na wafuasi wake, hukiweka katika kivuli. Mwokozi wa ulimwengu hufananishwa na mtu tu. Wale wanaoamini katika kuongea na roho hizi, hawaoni mwujiza wowote katika maisha ya Mwokozi. Wanasema kuwa miujiza yao inazidi ile ya Kristo alipokuwa hapa duniani.

Uzungumzaji wa wafu sasa umehesabiwa kuwa dini ya Kikristo, na umevaa sura ya Kikristo, na mafundisho yake hukubaliwa waziwazi. Katika hali yake ya sasa ni ya hatari sana, ya kijanja sana, na ya hila sana. Wenye kuamini hali hiyo hukubali mambo ya Kristo na Biblia, lakini kwa ujanja na hila kubwa. Biblia hutafsiriwa kwa namna ya kupotosha ili iwafurahishe wale wasioongoka. Upendo husisitizwa kuwa ndiyo tabia kuu ya Mungu, lakini hupotoshwa na kumwelekeza katika njia za uasherati. Chuki ya Mungu kuhusu dhambi, na kanuni ya Mungu kuhusu utakatifu hufichwa bila kutajwa. Hadithi huwafanya watu wasione kuwa Biblia ndiyo msingi wa imani yao. Kumkiri Kristo kwa kinywa tu, lakini kwa kweli humkataa kimatendo.

Ni watu wachache sana ambao wamegundua hila hiyo ya kuongea na mizimu, au wafu. Wengi hujaribu ili kufanya utafiti. Huwa na hali ya hofu juu ya kuongea na roho hizo, lakini huthubutu kwenda mahali palipokatazwa. Hivyo mwovu huwakamata kwa hila na kuwashikilia katika hali ya mateka. Hakuna kinachoweza kuwatoa katika hali hiyo ila maombi ya kweli kweli.

Watu wanaopendelea kufaya dhambi, hali wanajua kuwa ni dhambi, hujiweka wenyewe katika mikono ya shetani. Hujitenga na Mungu kwa hiari yao, na malaika walizi huwaacha peke yao bila ulinzi.

[273]

“Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunog’ona; je, waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria ya ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi” Isaya 8:19-20.

Kama watu wamepata mafundisho ya kweli kuhusu hali ya wafu na asili ya mtu, wataona wazi kuwa wenye pepo wanaojidai kuwa waongea na wafu, ni uwezo wa shetani ufanyao kazi ndani yao, kwa maajabu na ishara za uwongo. Lakini watu wengi hufumba macho yao wasione nuru kuhusu jambo hili, na shetani huwafunikiza nawavu wake. “Kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu amewaleta nguvu ya upotevu, wauamini uwongo” 2 Thes. 2:10-11.

Wale wanaopinga mambo ya pepo humshambulia Shetani na mamlaka zake. Shetani hata kubali kushindwa hata kidogo, isipokuwa afukuzwe na wajumbe wa mbinguni. Atataja Maandiko hali akiyapotosha, ili ashinde. Watu watakaoshinda hatari ya wakati huu, lazima wafahamu ushuhuda wa Maandiko barabara.

Roho za mashetani, hujionyesha kama ndugu na marafiki wa watu ambao walikufa, hutujia na kutushauri mambo fulani fulani. Halafu hufanya maajabu. Lazima tuwapinge kwa Biblia na ukweli wake, kwamba wafu hawajui neno lolote, kwa hiyo hawa wanaaonekana kama kwamba ni jamaa zetu waliokufa ni roho za mashetani yaani pepo.

Wale ambao imani yao haikujengeka kwa neno la Mungu, yaani Biblia, watadanganyika na kupotezwa na shetani. Maana Shetani hufanya kazi yake kwa madanganyo yote ya upotevu, na madangayo haya yatazidi kadiri tunavyokaribia mwisho. Lakini wote

wanaotafuta ukweli wa Biblia na kutakasa roho zao kwa njia ya kulitii neno la Mungu, watahinda. Mwokozi atawatumia malaika wote wa mbinguni kuwalinda. Hatamwaacha hata mtu wake mmoja ashindwe na Shetani. Wale wanaojifariji kwamba hakuna adhabu yo yote itakayowapata wenye dhambi, na kudharau maonyo ya mbinguni watapotezwa na udanganyifu wa shetani katika mizimu na kuangamia.

[274] Wenye mizaha wataendelea kukataa maonyo ya mbinguni, kuhusu mpango wa wokovu na adhabu itakayowapata katika mizimu wanaoikataa kweli, na kujiona wako salama. Watatajihafifisha kabisa, kiasi cha kutojali sheria ya Mungu. Kadiri walivyojiunga na shetani, itakuwa vigumu kujitenga naye na hila zake.

Msingi wa kazi ya shetani ni ule uliowekwa katika Edeni kwa Hawa, kwamba, “Kufa hamtakufa” “Siku mtakayokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafumbuliwa, na mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya” Mwanzo. 3:4-5. Madangayifu yake yatafikia mpaka kwenye masalio ya mwisho ya Mungu. Nabii asema, “Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura . . . Hizo ndizo roho za mashetani zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote, kuwakusanya kwa vita vya siku ile kuu ya Mungu Mwenyenzi.”

Sasa makanisa ya Kiprotestanti yanaliona kanisa la Kirumi kuwa rafiki yao zaidi ya walivyoliona katika miaka iliyopita. Katia nchi hizo, ambako ukatoliki umeenea sana, mawazo ya wengi huona kuwa tofauti kati yetu na wao sio kubwa, bali katika mambo makuu ya imani tunakubalina nao, ila kuwa vipengele vidogo tu vikirekebisha, tutakubalina nao katika mambo yote. Kulikuwako nyakati hapo zamani, Waprotestanti walipowafundisha watoto wao kuwa kukubaliana na wakatoliki kidini kumwasi Mungu. Sasa hali ya maoni yao inatofauti kiasi gani!

Watetezi wa Ukatoliki husema kuwa kanisa lilifanya vibaya sana kufikiri kuwa waprotestanti walikuwa wapotofu. Hizi zilikuwa zama za giza, za ujinga. Wanalaumu ukatili waliowatendea watu kuwa ulikuwa wa kinyama wakati huo.

Je, watu hawa sasa wamesahau madai yao kuwa wao (Kansia la Rumi) hawakosi? Kanisa la Kirumi hudai kwamba, “kanisa halikosi kamwe, wala halitakosa kamwe. Hivyo ndivyo Maanandiko yanavyosema.”

Kanisa la mapapa halitapunguza madai yake kuwa halikosi. Ngoja serikali izuie mambo ya ukatili sana, baadaye Rumi ikapata uwezo wake wa kwanza itafufua hali yake ya mateso.

Ni kweli kwamba wako wakristo halisi katika kanisa la Rumi. Watu maelfu wanamtumikia Mungu kwa kadiri ya ujuzi walio nao katika kanisa hilo. Mungu huwaangalia kwa huruma watu hao. Wao wamepotoshwa na kufundishwa kinyume cha ukweli. Mungu atawaletea nuru, na wengi watajiunga pamoja na watu wake, katika kanisa la kweli.

Lakini kama kanuni za Ukatoliki zilivyo, wanaachana na Biblia kabisa, sawa kama walivyokuwa hapo kwanza.

Kanisa la Rumi hutumia kila njia ili lipate kukubalika katika ulimwengu, ili liweze kurudisha hali yake ya zamani ya kutesa, na kuvuruga mambo yote ya Kiprotestant.

[276] Wakatoliki wanaendelea kufaulu katika makusudi yao. Angalia jinsi makanisa yao yanavyozidi kuongezeka na tazama Koleji zao na vyo vyao vinavyozidi na kujazwa na wanafunzi wa Kiprotestanti. Angalia jinsi kawaida zao za ibada zinavyoongezeka huko Uingereza, na maasi yanavyozidi kwa upande wa wakuu wa Katoliki.

Mapatano na Kuridhiana

Waprotestanti wamewafadhili wakatoliki, wamefanya mapatano na kuridhiana nao, kiasi kwamba hata mapapa wenyewe wanashangaa. Watu wanafumba macho wasiione tabia hasa ya ukatoliki. Inawapasa watu kupigana hatari hii inayoukabili uhuru wa watu na uhuru wa dini pia.

Ijapokuwa ukatoliki unaendeshwa kwa njia ya hila na udanganyifu, lakini siyo ovyo. Ibada zao hufanywa kwa heshima kubwa na kicho halisi. Hali ya mambo katika ibada kanisani na mapambo yote huwafanya waabuduo kuwa na kicho kabisa na utulivu. Macho hupendezwa sana. Makanisa makubwa sana yenye kupambwa kwa vito mbalimbali madhabahu ya dhahabu, na rangi zing'aazo, huwavutia wenye kupenda uzuri. Vinanda vikubwa vya kuimbia na mambo mengi ya kurembesha huwafanya waabuduo kuwa na hali ya kicho kamili inayostahili ibada ya kweli.

Mambo haya nje na maadhimisho ya ibada humwacha mwenye dhambi katika hali ya mzaha, ambao haumtoshenzi na kumridhisha hasa. Dini ya Kristo haina haja na mambo kama hayo. Nuru inayong'aa kutoka msalabani hung'aa kwa uzuri na upendo kwamba hakuna mapambo ya nje yanayolinganishwa kwa thamani yake na uzuri moyoni. Mapambo na urembo wa kuvutia upendezao macho hutumiwa na shetani kuwasahaulisha watu haja ya roho, na kuwafanya wawe wapenda mambo ya ulimwengu tu.

Mashindano ya ibada ya Kikatoliki yana hali ya kuwapumbaza watu wapate kudangayika. Wanatazama kanisa la Kikatoliki kana kwamba ndio mlango wa mbinguni. Hakuna awezaye kukanusha mambo yake kuwa ya uongo, isipokuwa wale waliosimama imara katika mwamba ambao wanaimarishwa na Roho Mtakatifu katika ukweli wa Maandiko Matakatifu. Watu hutaka kuwa na mfano tu wa utawa lakini wakikana nguvu zake.

Madai ya kanisa kwamba lina haki na uwezo wa kumsamehe dhambi yalifanya kanisa la Kirumi lijisikie kuwa lina uhuru kufanya dhambi bila kizuizi, na ile hali ya maungamo huwaelekeza watu kutenda maovu. Mtu anayepiga magoti mbele ya mwanadamu mkosaji, na kuungama makosa yake mbele yake, na kufunua siri za moyo wake kwa huyo, hujihafifisha yeye mwenyewe na kujiondolea uthamani wake na kujitia unajisi. Mawazo yake kuhusu Mungu hushuka chini na kumfananisha na mwanadamu mwenye dhambi, maana kwa mtu huyo padri huwa badala ya Mungu. Maungamo haya yanayofanywa kwa binadamu mwenye dhambi sawa na yule anayeungama, ndiyo yamekuwa asili ya uovu uliojaa katika ulimwengu mzima. Hata hivyo kwa mwenye kupenda anasa za ulimwengu, huonekana kuwa fahari kuliko kujidhili mbele za Mungu na kumfunulia siri za moyo wake. Humfurahisha mtu kulipa malipo ya kitubio kuliko kuacha dhambi na kujitenga nayo. Mtu anaona urahisi wa kujitesa yeye mwenyewe kwa njia mbalimbali kuliko kuusulubisha mwili na tamaa zake.

[277]

Mfanano wa Kushangaza

Wayahudi wakati wa Kristo, walikuwa wamezikanyaga amri za Mungu, lakini kwa juu juu walikuwa wakionekana kuwa wacha Mungu wa kweli, wakikaza sana amri za Mungu na kuzifanya kuwa mzigo kwa watu. Jinsi Wayahudi walivyokuwa wakidai kwamba wanashika sheri ya Mungu, hali kadhalika Warumi hujifanya kuwa wanautukuza msalaba.

Huweka misalaba kila mahali: makanisani, madhabahuni, kwenye mavazi, n.k. Kila mahali wanautukuza msalaba kijuu juu. Lakini mafundisho ya Kristo wakiyazika chini, na kuyainua mapokeo ya bure ya kibinadamu. Dhamira za watu zikitishwa daima kuwa wasipotimiza hayo Mungu atawaadibu, huku wakuu wao wakiishi katika anasa na uasherati.

Daima Shetani hujitahidi kuieleza vibaya tabia ya Mungu, asili ya dhambi, na msingi wa mashindano makuu. Hila zake huwapa watu uhuru wa kutenda dhambi. Wakati ule ule hueleza uongo kuhusu tabia ya Mungu ili watu wamwone Mungu kuwa ni katili asiye na huruma ye yote, wala hana upendo. Kwa kupotosha tabia ya Mungu, mataifa ya kikafiri waliongozwa kuamini Mungu awakubali.

Katika ibada hizo za sanamu na matoleo yao ukatili mwingi ume-fanyika.

[278]

Mwungano wa Umizimu na Ukristo

Kanisa la Romani Katoliki, likiunganisha ukafiri na ukristo, nalo kama wamizimu walivyo, wanaielezea tabia ya ukristo, nalo kama wamizimu walivyo, wanaielezea tabia ya Mungu vibaya, wametafuta njia ya utesaji. Njia ya kanuni za kusababisha mateso hukubaliana na mafundisho yao. Waongozi wa kanisa walichunguza na kubaini mambo yatakayosababisha mateso kwa wale ambao hawatakubaliana na kanuni zao. Hivyo ndivyo walivyofanya. Lakini wale walioteswa waliona kuwa ni afadhali kufa na kupumzika kuliko kukubaliana na mambo ya kinyume cha imani yao.

Kwa waumini wa Rumi, walikuwa wakiadhibiwa kwa kushindishwa kwa njaa na mateso mengineyo. Hivyo ndivyo ilikuwa njia ya kuwarudi, na kuwaadibisha. Ili kusudi waingie mbinguni, walifundishwa kukataa mafundisho ambayo Mungu ameyaweka kwa ajili ya hawa wasafiri wa mbinguni, wakati wakipewa wangali duniani. Uwanja wa kanisa ulikuwa umejaa watu hawa wenye kujitesa ili wapate upendeleo kwa Mungu, nayo ni kazi bure isiyokuwa na faida.

Mungu hakuwawekea wanadamu mizigo hiyo mizito ili apate kuwafadhili. Kristo hakuwapa watu kielelezo cha kujifungia katika majumba ya watawa, ili wapate kufaa kuingia mbinguni. Haku-fundisha kuwa upendo lazima ulazimishwe.

Papa anajidai kuwa yeye ni mjumbe wa Kristo. Lakini alipokuwa hapa hakuwafunga watu magerezani, eti kwa kuwa hawakumheshimu na kumtukuza kama mfalme wa mbinguni. Je, alifanya hivyo? Je, sauti yake ilisikika ikiwahukumu watu ambao hawakumwamini?

Kanisa la katoliki sasa linajionyesha katika ulimwengu kama linasikitikia vitendo vyake vya zamani, hali likijaribu kufunika tabia yake ya utesaji na ukatili. Limejifunika na vazi la kikristo, lakini hali yake ni ile ile. Kanuni ya upapa tangu zamani ni hiyo hiyo, ilivyo siku hizi. Mafundisho yao ya wakati wa zama za giza, ndiyo hayo waliyo nayo. Msimamo wa mapapa kuhusu waprotestanti ni ule ule; tangu siku za watengenezaji, wakati watu wa Mungu

walipokuwa hatarini kwa ajili ya kupinga papa. Upapa ni vile unabii ulivyotabiri kuwa uasi utaendelea kuzidi siku za mwisho 2 Thes. 2:3-4. Kama vile mabadiliko ya kinyonga ndivyo unavyojibadili, lakini hali yake ikiwa ni ya sumu ya joka. Je, kanisa asi hili ambalo kwa miaka maelfu historia yake imeandikwa katika damu ya watakatifu waliouawa nalo, litabadilika kuwa kanisa la Mungu?

Badilio katika Uprotestanti

[279]

Katika nchi za Kiprotestanti watu husema kuwa, imani yao hutofautiana na ile ya Kikatoliki kidogo sana kuliko ilivyokuwa zamani. Kumekuwako na badiliko; lakini badiliko hilo haliko upande wa Wakatoliki, ila upande wa waprotestanti, Sasa ukatoliki unafanana na uprotestanti kwa sababu uprotestanti umeharibika sana ka kurudia hali ya ukatoliki kuliko ilivyokuwa siku za watengenezaji wa kanisa.

Makanisa ya Kiprotestanti kwa ajili ya kutaka yapendeke ulimwenguni huamini mema ya uovu wote, na katika hayo matokeo yake yatakuwa kuamini uovu wote kuwa wema. Sasa kama hapo kwanza wanaomba samahani kwa Rumi kwa kutokuwa na mawazo ya upendo kwao.

Wakiomba msamaha kwa ajili ya ushupavu wa wengi hudai kuwa ufedhuli na ushirikia uliokuwako wakati wa giza ulisaidia Rumi kuwa mkatili; sasa wakati huu wa elimu, na kuongezeka kwa hali bora katika mambo ya dini, mambo ya karaha yamezuilika. Mambo ya jinsi hiyo hayawezi kufikiriwa katika nyakati hizi. Lakini ni lazima ikumbukwe, kuwa, kadiri nuru kubwa inavyozidi kung'aa, ndivyo giza kuu linavyozidi kuwafunika wale wanaoipinga nuru.

Siku bora za hali nzuri ya mwisho, ndizo zimeleta hali ya giza zaidi kwa Warumi, na kuimarishwa kwa upapa. Hali bora ya kinuru inalingana na hali ya kigiza. Zamani wakati watu hawakujua neno la kweli, watu maelfu walinaswa katika mitego ya mwovu, bila kujua lolote. Wakati wa kizazi hiki wengi pia hawaoni mitego iliyotegwa miguuni pao, hujinasa kama vipofu. Watu wanapotukuza mawazo yao zaidi ya Neno la Mungu, hali ya kitaalamu hufanya madhara mengi zaidi kuliko katika hali ya ujinga. Kwa hiyo sayansi ya uongo ya siku zetu, hutimiza sehemu kubwa sana ya kufaulisha upapa, na kukubaliwa kwake, kama ilivyofanyika katika zama za giza.

Utunzaji wa Jumapili

[280] Utunzaji wa Jumapili ni desturi iliyoanzishwa na kanisa la Rumi, ambayo hujidai kuwa hiyo ndiyo alama ya uwezo wake. Roho ya Upapa, ambayo ni ya kujiambatanisha na ulimwengu, na desturi zake za kujali mapokeo ya wanadamu zaidi ya sheria za Mungu, roho hiyo hiyo imeenea katika makanisa ya Kiprotestanti na kuwaongoza kushika Jumapili kama Warumi walivyofanya zamani.

Amri za kitawala na za mabaraza, pamoja na mpango ya kanisa na kanuni zake, ambazo zilisaidiwa na serikali ndizo zilikuwa hatua za kuingiza ukafiri katika makanisa ya Kiristo, na kuheshimiwa na ulimwengu. Hatua ya kwanza ya kuiheshimu Jumapili, ilikuwa amri iliyotolewa na mfalme Constantine. Ingawa ilikuwa karibu kuwa kawaida ya kishenzi, ilisisitizwa na mfalme iwekwe katika upande wa dini, baada ya kuongoka

Eusebius, kasisi aliyetafuta msaada wa serikali ili atekeleze mambo ya kanisa, na ambaye alikuwa rafiki mpendwa wa mfalme Constantine, ndiye alieneza habari kuwa Kristo amehamisha heshima ya Sabato kutoka Jumamosi na kuiweka Jumapili. Hakuwa na ushahidi wa Biblia kuhusu madai hayo. Eusebius mwenyewe alikiri kuwa ni uongo bila kujua kuwa anakiri. Alisema, “Mambo yote yaliyopaswa kutendeka siku ya Sabato yalihamishiwa katika siku ya Jumapili, yaani siku ya Bwana”.

Upapa ulipoimarika, utunzaji wa Jumapili uliendelea. Kwa muda, siku ya saba iliendelea kuheshimiwa kama Sabato, lakini badiliko lilikuwa linafanyika. Baadaye papa aliamuru kwamba wakuu wa majimbo, lazima wawaadhibu wote wanaovunja Jumapili wasije wakaleta balaa kwao wenyewe na majirani.

Maagizo ya mabaraza ya kanisa, hayakutosha, hivyo walitafuta msaada wa serikali ili amri ya kutofanya kazi Jumapili ikazwe kisheria. Katika baraza la wakuu lililofanyika Rumi, lilirudia mashauri yote yahusuyo kutunza Jumapili, yaliyofanyika nyuma, na kuyakaza upya, kuwa amri ya kanisa likikazwa na mamlaka ya serikali.

Hata hivyo kutokuwako na fungu la Biblia linalounga mkono juu ya utunzaji wa Jumapili, kulizidi kuwatia wasiwasi. Watu waliuliza sababu ya kupuuza usemi wa Mungu, unaoamuru, “Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako” na kuheshimu siku ya jua.

Kwa kuwa walikosa fungu la Biblia la kuthibitisha, walitoa maelezo yote waliyoona kuwa yanafaa.

Mtu mwenye juhudi ya kuisitiza utunzaji wa Jumapili, alitembelea Uingereza mwishoni mwa karne ya kumi na mbili mtu huyo alipofika katika makanisa ya huko na kufundisha mambo hayo, alipingwa vibaya na mashahidi waaminifu wa ukweli, na kwa kuwa hakupata matunda, aliondoka kwa muda. Baadaye aliporudi tena alikuja na maandiko aliyodai kuwa yametoka kwa Mungu mwenyewe. Maandiko hayo yalikuwa yanasema juu ya utunzaji wa Jumapili, na kwamba mtu yeyote atakayepinga utunzaji huo ataona cha mtema kuni, maandiko haya ilisememekana kuwa yameanguka kutoka mbinguni, kwamba yalikutwa juu ya madhabahu ya kanisla la Simeon huko Yerusalemu, kwenye kilima cha Golgota. Lakini kwa kweli yaliandikwa na papa wa Rumi. Hila zote za udanganyifu vimekuwa vikifanywa na mapapa wa Rumi.

[281]

Lakini juhudi zote za kuimarisha utunzaji wa Jumapili kuwa sabato zimetokana na mapapa ambao hukiri wazi sabato iliwekwa na Mungu. Katika karne ya kumi na sita, baraza la mapapa lilitangaza hivi: “Wakristo wote wajue kuwa siku ya saba ya juma ilitoka kwa na Mungu mwenyewe, nayo imekuwa ikitunzwa siku zote, wala si Wayahudi peke yao, bali na watu wote wanaokiri kumwabudu Mungu; ingawa sisi wakristo tumeibadili Sabato na kuifanya iwe jumapili, ambayo ndiyo siku ya Bwana” Wale walioharibu amri ya Mungu, walijua aina ya kazi yao.

Adhabu Kali

Kielelezo cha kushangaza cha kanuni ya Rumi, kilitolewa katika mateso ya Waldenses ya muda mrefu na kumwaga damu sana, ambayo yaliwakumba baadhi washika sabato. Historia ya makanisa yaliyokuwa katika Ethiopia na Abyssinia ni ya muhimu sana. Katika ukiwa wa wakati wa giza wakristo wa Afrika ya kati walisahauliwa katika malimwengu, yaani hawakujulikana na kwa hiyo walikuwa salama, wakiufurahia uhuru wao wa kuabudu. Baadaye Rumi ikawagundua na mfalme wa Abyssinia akavutwa kwa ujanja ili amkiri papa kuwa ndiye wakili wa Mungu. Amri ilitolewa ya kutangaza watu kutunza sabato, na mtu asipojali atapata adhabu kali. Baadaye utawala wa papa ukawawia watu mzigo mchungu, kwamba

Abyssinia akakusudia kuuvunjilia mbali. Basi urumi ukapigwa marufuku katika nchi hiyo na imani yao ya kwanza ikawarudia.

[282] Wakati makanisa ya Afrika yalipokuwa yakiishika sabato ya siku ya saba, ambayo ndiyo amri ya Mungu lakini walijiepusha kufanya kazi na siku ya Jumapili kufuata kawaida ya kanisa. Rumi iliikanyaga amri ya Mungu ili kutukuza amri yake mwenyewe, lakini makanisa ya Afrika ambayo hayakujulikana karibu miaka elfu moja, hayakuingia katika uasi huu. Walipoletwa chini ya Rumi walilazimishwa kuiacha Sabato ya kweli na kushika ile ya uongo. Lakini hawakuweza kupata uhuru wa kurudi kushika amri ya nne.

Mnyama Mwenye Pembe Mbili Kama Kondoo

Unabii wa Ufunuo 13 unasema kuwa mnyama afananaye na mwana kondoo mwenye pembe mbili, utawafanya watu wote wakaa duniani wamsujudie papa ambaye afananishwa na mnyama kama chui. Mnyama afananaye na mwanakondoo atawaambia watu wakaa duniani wamfanyie mnyama chui sanamu. Zaidi ya hayo mnyama huyu atawaamuru watu, wadogo na wakubwa matajiri na maskini, walio huru na wafungwa, wadogo na wakubwa, matajiri maskini, walio huru na wafungwa watiwe alama ya mnyama. Ufunuo 13:11-16. Marekani ndiyo inayofananishwa na mnyama kama mwanakondoo, mwenye pembe mbili. Unabii huu utatimia wakati Marekani itakapolazimisha watu washike Jumapili ambayo Rumi hudai kuwa ndiyo alama ya ukuu wake. “Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule” ufunuo 13:3. Pigo la mauti linaelekeza kwenye anguko la upapa la mwaka 1798. Baada ya haya, unabii husema, “pigo lake la mauti lilipona, dunia yote ikamstaajabia mnyama yule”. Paulo asema kuwa “mtu wa dhambi” atatenda kazi yake ya udanganyifu mpaka mwisho wa wakati 2 Thes. 2:3-8. “Na watu wote wakaa juu ya nchi watamsujudia, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo”. Ufunuo 13:8. Katika nchi zote za dunia papa atatukuzwa kwa ajili ya Jumapili aliyoibuni.

Tangu kati ya karne ya kumi na tisa wanafunzi wa Biblia walileta ushuhuda huu ulimwenguni. Sasa utimizo wa unabii huu unaonekana kuwa unaharakisha sana kutimizwa kwake. Hata wal-

imu wa Kiprotestanti wanakutimizwa kwake. Hata walimu wa Kiprotestanti wanakubaliana na mamlaka hii iliyoweka Jumapili kuwa sabato, na wala hawana fungu la Biblia linalowaunga mkono, sawa kama wakatoliki walivyokosa fungu. Thibitisho kuwa hukumu ya Mungu itawaangukia washikao Jumapili, litarudiwa tena na hata sasa hukumu ya Mungu inaanza kuharakisha.

Kanisa la Rumi lina werevu sana. Linasoma mambo yanayoonekana kuwa kwamba makanisa ya Kiprotestanti yanaliheshimu, kwa vile yanakubali kushika jumapili, ambayo ni sabato ya uongo, na kwamba linajitayarisha kulazimisha watu kuishika Jumapili kwa nguvu, kwa kutumia njia zile zile zilizotumika zamani. Jinsi litakavyokuwa tayari kuunga mkono Uprotestanti ili kutimizia shabaha yake ni wazi. [283]

Kanisa la katoliki limebuni shirika kuu linalosimamiwa na papa. Washiriki au ajumbe wake, ambao ni mamilioni wako kila nchi, na kila mahali, wote wakiwasiliana na papa, bila kujali taifa gani au serikali gani wao waliomo. Ingawa hula kiapo cha kutumikia nchi na serikali yao lakini kwa chini chini huwa na kiapo kingine cha kutimiza maazimio ya papa wa Rumi.

Historia inaonyesha jinsi kanisa hili linavyojihusisha na mambo mbalimbali ya nchi na mataifa mbalimbali. Hivyo hufaulu kuingilia mambo hata ya mapinduzi ya watawala, ili mradi watimize makusudi yao.

Wanajivuna kuwa wao hawabadiliki kwa vyo vyote. Waprotestanti wanajua kidogo sana kuhusu mhimizo wao wa mwungano wa dini, kwamba Rumi ina makusudi mbalimbali vile hawa wanavyodhani. Hata kule kushika Jumapili hawana habari juu yake.

Waprotestanti wanaposhughulika na kutafuta mwungano wa Rumi, Warumi wao hushughulika na jinsi ya kujiimarisha na kushika uwezo wote mikononi mwao, ule waliokuwa nao zamani, ambao uliwapotea. Kusudi lao ni kuweza kuwa na uwezo wa kutawala kanisa na serikali pia, ili ikiwezekana kwamba matakwa ya kanisa yaweze kutimizwa kwa nguvu ya serikali, si muda mrefu ujao mwungano baina ya kanisa na serikali utafikiwa, na hapo ushindi wa Rumi utakamilika. Mwungano wa makanisa ya Kiprotestanti kwanza; halafu mwungano wa makanisa ya Kiprotestanti na Rumi; mwisho, mwungano wa kanisa na serikali.

Makanisa ya Kiprotestanit yatakuja kung'amua makusudi ya Rumi, yakiwa yamechelewa tayari, wala hayataweza kujitoa mtegoni. Kanisa la Rumi linaendelea kupata uwezo kimya kimya. Mvuto wao unaingia katika majumba ya kutunga sheria, makanisa, na katika mioyo ya watu. Wanajiimarisha ili waweze kukamilisha maazimio yao; wakati ukifika watatenda mambo yao. Mambo yao ni kupigana vita na Mungu na neno lake. Hivi kila mwenye kutii neno la Mungu atakabiliana na mashutumu na mateso.

Marejeo:

John L. Von Mosheim — Institutes of Ecclesiastical History Book 3 Century II, sehemu ya 2 sura kifungu 9 Note 17.

Robert Cox Sabbath laws and Sabbath Duties p. 558

Angalia Heylyn. History of the Sabbath pt. 2 sura 5 sec 7.

Thomas Morer — Discourse in Six Dialogues on the Name, nation and Observation of the Lord's Day pp. 281, 282

Angalia Michael Geddes Church History of Ethiopia pp. 311, 312.

Angalia kwa ajili ya mfano John Dowling. The History of Romanism bk. 5, sura 6 sec 55 and Mosheim bk 3 cent 11 part 2 chap. 2 see sec. 9 note 17.

Tangu mwanzo wa mapambano huko mbinguni, limekuwa azimio la shetani kuharibu sheria ya Mungu na kuondoa. Haidhuru ama ni kuindoa sheria yote nzima, au kukataa kutambua sehemu moja tu ya sheria, matokeo ni yale yale. Mtu avunjaye sehemu moja ya sheria hudhihirisha nia yake ya kuvunja sheria nzima, maana mvuto wake na kielelezo chake huelekea upande wa kuasi. Basi “amekosa juu ya yote” Yakobo 2:10.

Shetani amepotosha mafundishi ya Biblia, kwa hiyo makosa yamefanywa na watu maelfu katika ukristo wao. Pamoja na mwisho baina ya ukweli na uovu ni kuhusu sheria ya Mungu, baina ya mafundisho ya Biblia na sehemu ya dini. Biblia inaweza kufikiwa na watu wote lakini ni watu wachache tu wanaoikubali Biblia kuwa ndiyo kiongozi wa maisha yao. Katika kanisa wengi hukataa misingi au nguzo za imani ya Kikristo, yaani uumbaji, anguko la mwanadamu dhambini, upatanisho na sheria ya Mungu. Nguzo hizi zimekataliwa, yote au sehemu yake. Wengi huona kuwa ni udhaifu tu kuitegemea Biblia peke yake.

Ni vyepesi kufanya sanamu ya mafundisho ya uongo, sawasawa na kufanya sanamu za kuchonga. Kule kumweleza Mungu kwa njia potofu, yaani kuitafsiri tabia yake vibaya, shetani huwaongoza watu kwa njia potofu. Sanamu ya wenye elimu inatwalishwa na kuabudiwa, badala ya kumwabudu Mungu. Kama anavyofunuliwa katika Neno Lake, na katika Kristo, na katika kazi zake za kuumba Mungu na wenye elimu, watungaji wa mashairi, wana siasa, waandishi wa magazeti, wa vyuo vikuu vingi, hata vyuo vya kufunza mambo ya dini, anazidi Baali kidogo tu, mungu jua ambaye ni mungu wa Wafoeniki kama ilivyo siku za Eliya nabii.

Hakuna kosa la ujasiri kabisa kuhusu mamlaka ya Mungu lenye matokeo ya hatari zaidi kuliko kosa la kufundisha kuwa sheria ya Mungu imefutika. Tuseme kuwa, wachungaji mashuhuri wahu-biri waziwazi kuwa, sheria ya mtawala wa nchi yao haina ulazima kuishika, kwamba inazuia uhuru wa watu, kwa hiyo haina lazima

ya kutiiwa. Je, mtu kama huyu angevumiliwa muda gani aendelee kufundisha hivyo?

[285] Hata hivyo ingekuwa rahisi kama taifa kuondoa sheria zao kuliko mfalme wa malimwengu kutangua sheria yake. Jaribio la kuziepuka sheria za Mungu lilifanywa ufaransa, wakati nchi ilipotawaliwa na makafiri. Ilionekana kuwa kuondoa ua wa ulinzi uliowekwa na Mungu, na kukubali kuweka nchi hiyo mikononi mwa utawala wa mfalme wa uovu.

Kuweka Kando Sheria ya Mungu

Watu wanaofundisha wengine kuipuzia sheria ya Mungu, huwa wanapanda mbegu za uasi zitakazozaa uasi. Hebu basi uzio unaowekwa na sheria ya Mungu uondolewe, hapo matokeo yatakuwa kutojaliana huyu na huyu, na maisha yatakuwa ovyo yasiyo na maana. Mali hazitakuwa katika hali ya usalama. Watu atanyang'anyana mali kwa nguvu, na mwenye nguvu ndiye atatajirika. Maisha yenyewe hayataheshimiwa, kiapo cha ndoa hakitajaliwa tena, mwenye nguvu atachukua mke wa jirani kwa nguvu. Amri yatano itawekwa kando na ya nne. Watoto watawainukia wazazi wao ili wapate watakavyo. Ulimwengu utakuwa mahali pa wanyang'anyaji na mauaji tu. Amani na furaha vingefutika duniani.

Fundisho hili la kufuta amri ya nne limekwisha kufungua mlango tayari wa maovu duniani. Ujeuri na uharibifu huingia duniani kama mkondo wa maji. Hata katika nchi za Kikristo unafiki umejaa tele. Kumekuwako na usaliti na tamaa kwa wingi. Kanuni za dini ambazo ndizo msingi wa maisha zimebomolewa vibaya, karibu kuanguka. Uasi na maovu hufurahiwa sana na wenye kuyatenda kama vile kitu kizuri. Magazeti huandika matokeo ya uovu kila aina; unyang'anyi, uharamia na mauaji.

Mambo haya ya ufedhuli na uovu usio na kipimo budi uwashitushe watu wote. Kutafanywa nini ili kuyakomesha mabaya haya?

Ulevi umewafumba Wengi

Mahakama yamechafuka na kuwa mahali pa ufedhuli, watawala wamekumbwa na tamaa ya kupata faida ya haramu pamoja na

uasherati. Ulevi wa pombe na kutokuwa na kiasi vimewafumba watu wengi wasitambue lo lote, kwa hiyo shetani amewatawala kabisa. Mahakimu wanaongoza katika kula rushwa. Ulevi wa kila aina, utovu wa uaminifu, vimewatawala wanasheria. Na sasa kwa vile shetani hawezi kuwashikilia walimwengu ili waache kusoma Maandiko matakatifu amebuni njia nyingine ili apate kukamilisha kazi yake. Kuharibu imani za watu wasiamini Biblia pia sawa na kuiharibu Biblia yenyewe. [286]

Kama ilivyokuwa hapo mwanzoni, amefanya kazi yake ya upotovu kupitia katika makanisa. Katika kupotosha Maandiko, amewangoza kutafsiri vibaya mafungu ya Biblia, na kwa hali hiyo amepanda mbegu za ukafiri kwa watu. Watu wakishikilia maneno ya Wakatoliki kuwa mtu afapo, roho yake haifi, wamekataa maneno ya kweli ya msingi ambao Mungu ameuweka, wakaandamana na mapotofu ya giza, kwa hiyo hawezi kuepushwa na udanganyifu wa pepo wanaojifanya kuwa ni jamaa za watu waliokufa wanaowatembelea walio hai. Mafundisho ya kwamba kuna moto wa milele unaowaunguza watu wakati wanapokufa, yamewapotosha wengi wauache ukweli wa Biblia. Kama amri ya nne inavyohimiza, inaonekana kuwa utunzaji wa Sabato ya siku ya saba unalazimishwa, na kwa kuwa hawapendi kufanya hivyo, walimu wanaopendwa na watu wake wameitupilia mbali sheria ya Mungu pamoja na sabato. Kwa kadiri msistizo wa sabato unavyoenea, kuikataa sabato pia kutaenea ulimwenguni. Viongozi wa makanisa wanafungua milango ili ukafiri uingie, na kuamini pepo na kukataa sheria ya Mungu. Kuna hali ya kutisha ya umizimu katika makanisa ya kikristo leo, katika ulimwengu.

Hata hivyo, watu hawa wanajidai kuwa kule kushika Jumapili kutaleta uheri katika jamii. Ni kusudi la shetani kuchanganya kweli na uongo, halafu kuwafanya watu wajione kuwa wanaridhika na hali hiyo. Wanaosisitiza ushikaji wa Jumapili wanaweza kutangaza matengenezo watu wanayotaka wakiunganisha ukweli wa Biblia, ambao huwa kinyume cha sheria ya Mungu. Watumishi wa Mungu hawawezi kujiunga na watu wa jinsi hii. Hakuna kitu kinachotoshleza kutoa sheria ya Mungu na kuweka kitu kingine, ambacho ni cha mwanadamu.

Shetani atawaingiza watu katika madangayo yake kwa njia ya makosa mawili makuu, yaani kosa la kwanza ni lile la kutokufa kwa

[287]

roho, na kosa la pili ni kushika jumapili badala ya sabato ya siku ya saba. Shetani ataweka watu katika udanganyifu wake. Kosa la kwanza huweka msingi wa kuongea na wafu, na kosa la pili hutia kifungo cha kuwafungamanisha na Rumi. Waprotestanti wa Marekani watakuwa wa kwanza kunyosha mikono yao kuvusha ghuba na kunganisha na uongejaji wa wafu; wataunganika na Rumi; na chini ya nguvu hizi tatu, nchi hii itafuata nyayo za Rumi za kutawala uhuru wa dhamiri. Kwa vile imani ya kuongea na wafu, itajifananisha na dini ya kikristo ya kisasa, itakuwa na uwezo wa kudanganya. Shetani mwenyewe atajigeuza kuwa mfano wa malaika wa nuru. Kwa njia ya pepo hao wa kuongea, miujiza itafanyika, wagonjwa watapona, na ishara nyingi zisizoweza kukanushwa zitatendeka.

Mapapa ambao hujidai kuwa dini ya kweli hujulikana kwa ishara hizo watadanganyika kabisa kwa ishara hizo, na Waprotestanti wakiwa wametupa ngao ya ukweli, wao pia watadanganywa. Wakatoliki, Waprotestanti na walimwengu wote wataona katika mwungano huo kuwa ulimwengu unaongolewa na Kristo.

Kwa njia ya pepo hawa Shetani ataonekana kana kwamba ndiye mfadhili wa wanadamu, akiwaponya wagonjwa na kuwaletea dini ya namna mpya, lakini wakati ule ule akiwapeleka watu katika uharibifu. Ulevi huaribu uwezo wa kufikiri. Kupenda anasa na uasherati, ugomvi na kumwaga damu ndiyo matokeo yake.

Vita husisimua tamaa mbaya ya rohoni na kuingiza hali hiyo mpaka ndani, kwenye damu. Ni kusudi la shetani kuwachochea mataifa wapigane, ili kuwazuia wasijiandae kusimama mbele za Mungu.

Shetani amejifunza siri za vitu vya asili, naye anaweza kutumia vitu vya asili ili kuleta madhara kwa kadiri ile Mungu aruhusu-vyo. Mungu ndiye huzuia madhara yanayoweza kuletwa na shetani kwa viumbe vyake. Lakini wakristo wameidharau sheria yake, naye atafanya kama alivyosema, yaani ataondoa ulinzi wake kwao na kuwaacha watupu bila kinga. Shetani huwashika wale ambao Mungu amewaondolea ulinzi wake. Atawafanikisha wengine na wengine kuwapa taabu ili wapate kumlaumu Mungu, kuwa ndiye anasababisha taabu yao. Hayo yote huyatenda ili kuendeleza kazi yake ya udanganyifu.

Wakati shetani anapojidai kuwa ni mfadhili wa watu wakati ule ule huwaletea magonjwa na dhiki kubwa mpaka wengi waangamie,

na miji mikubwa ibaki katika maganjo matupu. Ajali zinazotokea katika bahari na nchi kavu.

Katika milipuko ya moto, katika tufani na dhoruba katika matetemeko ya nchi, na katika kuumuka kwa mawimbi, na mafuriko makubwa na mambo mengi ya kutisha yanayoangamiza maisha ya watu, shetani hutumia uwezo wake ajionyeshe alivyo. Hugarikisha mavuno mashambani, ili kusababisha njaa. Hukoroga hewa na kuwa ya hatari iwezayo kuangamiza watu maelfu.

Kisa mwovu mkuu huyo huwasingizia watu wanaoshika amri za Mungu kuwa ndio wanaosababisha maafa hayo yote. Pia husema kwamba kwa sababu watu wamemkosea Mungu kwa kutoshika siku ya Jumapili, ndiyo sababu ya kutokea mambo haya, nayo hayatakoma mpaka siku ya jumapili itakapoheshimiwa na kushikwa barabara. Wale wanaoasi siku ya jumapili huzuia mibaraka ya Mungu. Kwa hiyo mashitaka waliyoshitakiwa watu wa Mungu zamani, yatarudiwa tena. “Wakati Ahabu alipomwona Eliya Ahabu alimwambia wewe ndiye unayetaabisha Israeli?” 1Fal. 18:17-18. Uwezo wa kutenda miujiza utawavutia watu kuwaelekeza kwa wale wanaomtii Mungu kuliko jumuiia. Roho watamwaambia kuwa wametumwa na Mungu ili kuwahakikishia kuwa, wale wanaopinga utunzaji wa jumapili wanafanya makosa. Watauombolezea uovu uliomo ulimwenguni, na ushuhuda wa pili wa walimu wa dini walivyohafifisha hali ya kiroho kwa kutoiheshimu jumapili.

Chini ya uongozi wa Rumi, wale walioteseka kwa ajli ya Injili walishutumiwa kama watenda maovu, wakihesabiwa katika jamaa ya Shetani. Hivyo ndivyo itakavyokuwa sasa. Shetani atawaletea mateso wale wanaoshika sheria ya Mungu, ili washitakiwe kuwa ndio wanaosababisha maafa duniani. Atajitahidi kuwatisha kwa njia ya hofu, akiwachochea watu pamoja na serikali wapingane na sheria ya Mungu.

Wale wanaoiheshimu sabato ya Biblia watahutumiwa kuwa ni maadui wa nchi, na wavunja sheria, ya jamii, Ni watu wako-rofi wasio na utaratibu, nao ndio wanaosababisha maafa haya yote. Watahitakiwa kama wahaini, walio kinyume cha serikali. Wachungaji wanaovunja sheria ya Mungu, hujipendekeza kana kwamba ni wapenzi wa serikali. Katika majumba ya kutunga sheria na katika mahakama, watunza amri za Mungu watahutumiwa, Watatajwa

vibaya kila mahali na wapakwa matope katika mambo yao yote, kwa uongo.

[289] Wakuu wa kanisa na waongozi wa serikali watahirikiana kuwalazimisha watu wote kushika Jumapili. Hata watu wa Marekani, ambao ni nchi huru, watu watajitolea kufuata mkumbo wa wengi na kulazimisha watu kushika jumapili. Uhuru wa dhamiri ambao umegharimu gharama kuu, hautaheshimiwa, wala kujaliwa. Wakati wa mapambano yaliyo karibuni, tutaona maneno ya nabii yasemayo, “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu” Ufunuo 12:17.

Watu wa Mungu wameelekezwa kwa Neno la Mungu kuwa ndilo litakuwa usalama wao katika udanganyifu wa giza. Shetani hutumia kila njia anayobuni ili kuwafanya watu wasipate ukweli wa Biblia. Kila mara kazi ya Mungu inapoanzishwa, yeye naye huamka kwa juhudi ili kuinga. Mapambano ya mwisho baina ya Kristo na wafuasi wake karibu yatatokea waziwazi, mbele yetu. Shetani ataigiza mambo yafanane na yale ya kweli, mpaka itakuwa vigumu kupagundua, isipokuwa kwa njia ya Maandiko matakatifu peke yake.

Wale wanaojitahidi kushika amri za Mungu, watapingwa na kudhihakiwa. Ili kusudi waweze kusimama na kushinda, ni lazima wafahamu mapenzi ya Mungu jinsi yalivyofunuliwa katika Biblia. Wataweza kumheshimu tu wakiwa na ufahamu wa kweli kuhusu tabia yake serikali yake, na makusudi yake; halafu watende kama yalivyo. Hakuna wengine, isipokuwa wale waliojiimarisha kiroho kwa njia ya ukweli wa Biblia, ndio watafaulu katika mapambano ya mwisho.

Kabla mwokozi hajasulubishwa aliwaeleza wanafunzi wake kwamba, atauawa na kufufuka tena. Malaika waliokuwako ili kuyakazia maneno yake katika mioyo ya watu. Lakini maneno yake yalitoweka katika mioyo ya wanafunzi wake, na wakati jaribu lilipokuja, na Yesu alipokufa, matumaini yao yalitoweka, wakafanana kama kwamba hawakuonywa juu ya mambo hayo. Vivyo hivyo unabii umetufunulia mambo yajayo waziwazi, kama wanafunzi walivyofunuliwa na Kristo. Mungu anapotuma maonyo, hutazamia kuwa kila mtu atatega sikio na kuyajali, lakini makundi mengi hawaelewi ukweli huu muhimu na wakati wa taabu utawapata bila kuwa tayari. Adhabu ya kutisha itakayowaangukia watakaomwabudu mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9-11) ingewafanya watu waamke na kuchunguza maana ya alama ya mnyama, na jinsi ya kujiepusha nayo. Lakini watu hawashughuliki na ukweli

wa Biblia na mafundisho yake, kwa sababu huwapa kile wanachotaka, yaani udanganyifu.

[291] Lakini Mungu atakuwa na watu wenye kushika Biblia na mafundisho yake peke yake, kuwa ndiyo kanuni ya maisha ya msingi wa matengenezo yote. Mawazo ya wataalamu, na tafsiri potofu za Biblia wanazoeleza watu wa sayansi, na mashauri yanayofanywa na kuamuriwa na mabaraza kwa kura ya wengi, hata mojawapo lisingefikiriwa kuwa ushahidi wa mafundisho. Sisi tungeshikilia neno kuwa, “Ndivyo asemavyo Bwana” Shetani anawatazamisha watu kwa wachungaji wao, na wataalamu wa theolojia kuwa ndio wanaotosha kuwaongoza, badala ya kuangalia Biblia na kujisomea wenyewe. Kwa vile anavyowaongoza wawategemee viongozi hawa, basi anawavuta wengi.

Kristo alipokuja watu wa kawaida tu walimsikiliza kwa furaha. Lakini wakuu wa makuhani waongozi wa watu, walizama katika chuki, wakamkataa masihi. Waliuliza, Inakuwaje watawala wetu na wenye maarifa na akili hawamwamini Yesu? Walimu hao waliongoza taifa la Kiyahudi kumkataa Mkombozi.

Kutukuza mamlaka ya Kibinadamu

Kristo alikuwa na maono kuhusu jinsi watu watakavyoitukuza hekima ya kibinadamu, mpaka iwatawale dhamiri. Hekima hii imekuwa laana kuu katika vizazi vyote. Maonyo yake ya kutofuata waongozi wa kibinadamu, katika hali ya upofu yameandikwa ili kuwaonya watu wa vizazi vijavyo.

Kanisa la Rumi limewapa tu viongozi wa kanisa uwezo wa kutafsiri Biblia kama wapendavyo, na kuwaaminisha watu wafuate hivyo. Ingawa watengenezaji wa kanisa walitoa Biblia isomwe na watu wote, lakini msingi ule ule ulioshikiliwa na Rumi huzuia watu wengi katika makanisa ya Kiprotestanti wasichunguze Biblia wao wenyewe, walifundishwa kufuata tafsiri ya kanisa. Maelfu hawakupata chochote. Ingawa Biblia hueleza wazi kilicho kinyume cha imani yao.

Watu wengi wako tayari kujitolea roho zao kwa waongozi wao wa kanisa. Mafundisho ya Mwokozi huyasoma kijuu juu tu bila kuyajali. Je, hao wachungaji wao ni watu wasioweza kukosa? Hawana upungufu wo wote? Tunawezaje kuwategemea watuongoze,

tusipowathibitishawa kwa Neno la Mungu kuwa ni wachukuzi wa nuru. Upungufu wa unyofu ndio husababisha watu wengi kuwa-tegemea wataalamu, na kujitundika katika makosa yao bila kuwa na habari. Huona ukweli wao mambo katika Biblia, na huona uwezo wa Roho Mtakatifu ukiwaongoza wahubiri wa Injili, walakini hata hivyo hukubali waongozi wao wawapotoshe kutoka nuru.

Shetani hunasa watu wengi kwa njia ya kuwaunganisha pamoja na maadui za Mungu, na msalaba wa Kristo. Mwungano huu unaweza kuwa wa kuzaliwa, kuoana, au urafiki. Watu wa namna hii hawatamani kutimiza wajibu wao.

Wengi husema kuwa, haidhuru kitu, mtu aweza kuamini katika kanisa lolote, bora tu maisha yake yawe safi, ukweli upo, lakini hatuujali, mwisho tutaokataa, na kuchagua njia za giza kuliko nuru. [292]

Kutojua hakuwezi kuwa udhuru wa kutenda dhambi, ambavyo kuna uwezekano wa kujua mapenzi ya Mungu. Msafiri akifikia mahali pa njia panda, na vidokezo vinaonyesha mahali kila njia inakokwenda, asipojali hizi alama, na akafuata njia yo yote tu anayopenda, anaweza kusafiri kwa makini, lakini kwa kweli atakuwa amepotea njia.

Wajibu wa Kwanza wa Mkuu

Kuwa na nia njema peke yake Na kufanya kama vile mchungaji anavyomwambi kuwa ndivyo haki hakutoshi.

Inampasa kila mtu kuchunguza maandiko kwa ajili yake mwenyewe. Humo ataona vibao vinavyooneysha baraka ya mbinguni na wala asibahatishe.

Ni wajibu, tena wajibu mkuu wa kila mtu kujifunza kutoka katika Maandiko ili apate kujua ukweli wa Mungu ulivyo, halafu atembee katika nuru ya ukweli huo; na kuwa na mawazo yetu wenyewe, kwa vile tutakavyosimama wenyewe mbele za Mungu.

Watu wasomi pamoja na majivuno yao ya hekima, hufundisha kuwa Maandiko yanazungumza kwa njia ya siri sana, na lugha ya kifumambofumbo isiyoeleweka kwa watu wa kawaida. Watu hawa ni waalimu wa uongo. Lugha ya Biblia ingeelezwa kwa maana yake hasa kama ilivyoandikwa, isipokuwa pale mifano, au vielelezo vilipotumiwa. Kama watu wangeichukua Biblia jinsi ilivyo, kama

inavyosomeka, kazi ya kuwaleta watu maelfu zizini mwa Kristo, ingekamilika. Watu hao ambao sasa wanatangatanga katika makosa.

Maandiko mengi ambayo wataalamu huyapitia bila kuyajali, humfaa sana kumfariji, mtu yule aliyejifunza katika skuli ya Kristo. Kuielewa Biblia hakutegemei akili ya mtu na elimu aliye nayo, bali hutegemea jinsi mtu anavyotia nia yake, na kuwa na kiu ya haki ya Neno la Mungu.

Matokeo ya Kutosoma Biblia na Kuomba.

Biblia isingalisomwa kamwe bila kuomba. Roho Mtakatifu pekee ndiye hutuwezesha na kutufanya tufahamu mambo ya Biblia, au kutuzuia tusiny'ang'anywe ujumbe unaoonekana kama mgumu.

[293] Malaika wa Mungu huandaa mioyo ili kulipokea Neno la Mungu. Tutapendezwa na uzuri wake, na kuimarishwa na ahadi zake. Majaribu kila mara huonekana kana kwamba ni magumu, kwa sababu mwenye kujaribiwa huwa hakumbuki ahadi za Mungu, na kukutana akiwa na silaha ya Maandiko Matakatifu. Lakini malaika wa Mungu huzungukia wale walio tayari kufundishwa, na watawakumbusha ukweli wanaouhitaji. "Atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" Yoha. 14:26. Lakini mafundisho ya Kristo lazima yawe yameota kamili mioyoni, ndipo Roho mtakatifu apate kuwakumbusha, wakati wa hatari.

Mambo ya mwisho ya dunia iliyojaa watu karibu kuamuliwa. Kila mfuasi wa Kristo lazima aulize, "Bwana unataka nifanye nini?" Matendo 9:6. Lazima sasa tutafute kwa uhakika kuwa na mambo makuu ya Mungu katika maisha yetu. Hatuna muda wa kupoteza. Tumo katika ardhi ya shetani. Msilale enyi walinzi wa Mungu.

Wengi hujifariji kwamba hawafanyi makosa kadha wa kadha. Kule kuwa mti katika bustani ya Mungu hakutoshi. Lazima wazae matunda. Katika vitabu vya mbinguni watu hawa huandikwa kama wanaoharibu ardhi. Walakini wale ambao wameidharau rehema ya Mungu na kushutumu neema yake upendo na uvumilivu wa Mungu bado unawashughulikia.

Wakati wa kiangazi miti yote huwa haina tofauti, ya kijani na mingine lakini wakati wa baridi ukifika, miti ya kijani hubaki katika hali ile ile na mingine hupukutisha kabisa majani yake. Hebu upinzani wa aina fulani utokee, hebu dhiki itokee, hebu mateso

yachemke, wakati huo wanafiki na wajipendekezao wote watakana imani yao, lakini wakrsito wa kweli watasimama imara, imani yao itadumu kuwa imara, matumaini yao yatang'aa kuliko wakati wa raha na mafanikio.

“Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautaona hofu wakati wa hari ujapo; basi jani lake litakuwa bichi, wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda”. Yeremia 17:8.

38/Ujumbe wa Mungu wa Mwisho

“Naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu akisema, umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu, umekuwa masikani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza . . . Nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, tokeni kwake enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake” Ufunuo 18:1-2,4.

Tangazo lililotolewa na malaika wa pili wa ufunuo 14:8 linarudiwa tena hapa pamoja na nyongeza ya adhabu inayomhusu Babeli, tangu tangazo la kwanza lilipotolewa.

Hapa inaelezwa hali ya kutisha sana. Kwa kukataa ukweli, mioyo ya watu itazidi kuwa giza zaidi na zaidi nao watazidi kushupaa. Wataendelea kukanyaga mojawapo ya amri za Mungu, mpaka watafikia hatua ya kuwatesa, wale wanaoitunza amri hiyo. Kristo atadharauliwa pamoja na Neno Lake na watu wake.

Jina la dini litakuwa kama vazi la kufunika maovu, yaani watu watajidai kuwa dini, lakini sivyo. Kule kuamini pepo kwamba ni maongezi na wafu, kunafungulia mafundisho ya shetani, na kuingiza mivuto ya malaika waovu iwe kanisani. Babeli imejaza kikombe cha ghadhabu ya uovu wake, na uangamivu wake uko karibu kutokea.

Lakini Mungu bado anao watu wake katika Babeli, na watu waaminifu hawa lazima watolewe humo, ili wasishiriki dhambi zake na wasipate mapigo yake malaika anashuka kutoka mbinguni aking’arisha nchi kwa utukufu wake, na kutaja maovu ya Babeli. Wito unasikika, “Tokeni kwake enyi watu wangu”. Wito huu ndio maonyo ya Mungu ya mwisho kwa ulimwengu.

Uwezo wote wa ulimwengu ukijiuna pamoja ili kupingana na sheria ya Mungu, utatangaza wazi kuwa “watu wote, wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru na watumwa” (Ufunuo 13:16) lazima wafuate mpango wa kanisa, na kupumzika katika sabato ya uongo (Jumapili). Watakaokataa kufuata amri hiyo mwis-

honi watatajwa kuwa wanastahili kuuwa. Kwa upande mwingine sheria ya Mungu inayohusiana na pumziko la Mwumbaji, yaani siku ya sabato, inatishia adhabu kubwa kwa wale watakaovunja.

Tukiwa na jambo linalotangazwa wazi namna hii, mtu yeyote atakayeikanyaga siku ya Mungu, yaani sabato ya siku ya saba, na kutii siku iliyoamriwa na binadamu, atapokea alama ya mnyama na sanamu yake, alama ya uwezo wa kibinadamu, mtu kama huyo huwa amechagua kumtii mtu badala ya Mungu.

“Mtu yeyote akimsujudia huyo myama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake, naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana Kondoo”. Ufunu 14:9-10.

Hakuna mtu atakayestahili kuteswa mateso hayo mpaka awe amepata ukweli sawasawa na akaukataa. Wengi hawajapata nafasi ya kusikia ujumbe maalum, unaopasa kwa wakati huu Mungu aonaye mioyo yote hawezi kumwacha mtu yeyote anayehitaji maonyo haya. Kila mtu atapata nafasi ya kufanya uamuzi wake kwa hakika.

Jaribu Kuu la uaminifu

Sabato ambayo ndiyo jaribu kuu la uaminifu wa mtu, ndiyo kiini cha mapambano. Ingawa kutunza jumapili ndiyo itakuwa ikiadhimishwa na wale wapiganao na Mungu, lakini utunzaji wa Sabato ya kweli utaonyesha uaminifu kweli kwa wale wanaomtii Mungu, ambao ni wanyofu wa kweli. Wakati kundi moja litapokea alama ya mnyama, kundi jingine litapokea Muhuri wa Mungu.

Utabiri kwamba makanisa na serikali watakuja kuwatesa watu wa Mungu wazishikao amri zake, umedhaniwa kuwa hauna msingi wo wote, tena ni upuuzi mtupu. Lakini kwa vile utunzaji wa Jumapili utakavyoenea na kustawi mambo yaliyodhaniwa kuwa upuuzi yataonekana kukaribia sana, na ujumbe wa maonyo utatolewa kwa nguvu kuliko ulivyoelezwa zamani.

Kwa kila kizazi Mungu amekuwa akituma wajube ili kuke-meza dhambi, ulimwenguni na kanisani pia. Watengenezaji wengi walipofanya kazi yao, walitumia hekima kubwa, katika kushambulia dhambi za makanisa na za taifa. Walitumia kuwavuta watu kwa njia

ya maisha yao manyofu ya kikristo, ili watu wapate kurudi katika njia ya Biblia. Lakini badala ya kufanya kama walivyokusudia, Roho wa Mungu aliwavuvia, wakautangaza waziwazi ujumbe wa Mungu wenye maonyo yake bila hofu.

Hivyo ndivyo ujumbe wa mwisho utakavyotangazwa. Bwana Mungu atafanya kazi kwa njia ya watu wa kawaida tu, ambao watajitoa kufanya kazi yake. Watu hao watakuwa wamepata maandalizi yao kwa kuvuviwa na Roho Mtakatifu zaidi ya kupata katika vyo.

Watu watabidishwa na Roho Mtakatifu kwenda kulihubiri neno la Mungu; kwa kadiri alivyowajalia kujua. Dhambi za Babeli zitatajwa dhahiri.

[296] Watu watataharuki na kustuka. Watu wengi walikuwa hawajasikia ujumbe wa namna hiyo. Babeli ni kanisa lililoanguka kwa sababu ya dhambi za kukataa ujumbe wa Mungu. Watu watakapowaendea Wachungaji wao na swali, Je, mambo haya ni kweli, ndivyo yalivyo? Wao watawafariji kwa kuwaambia hadithi za burezisizo za kweli. Lakini kwa kuwa watu wathibitishwe kwa maandiko. “Ndivyo asemavyo Bwana” ndipo wasipopata maandiko watawaita wahu-biri kuwa ni wazushi, kwa hiyo watawachochea watu ili wawatese wahubiri hawa.

Viongozi wa makanisa, watajitahidi kwa nguvu zote ili kuzuia nuru ya Injili, na kuzuia watu wasiongelee swala hili; wala kuyajali mambo haya yahubiriwayo.

Kanisa litaomba msaada wa nguvu ya serikali kuingilia kati. Wakatoliki na Waporotestanti wataungana. Kwa kadiri msukumo wa kushika jumapili utakavyozidi kukazika, wale washikao amri za Mungu, yaani wanaoshika sabato watakabiliwa na adhabu za kufungwa kulipa faini. Wengine watapandishwa vyeo ili kusudi waikane imani yao, wengine wataahidiwa zawadi kubwa ili wauache unyofu wao. Lakini jawabu lao litakuwa “Tuonyesheni kosa letu katika Biblia”, Wale wataoletwa mahakamani, wataitetea kweli kwa uthabiti, kiasi cha kuwaaminisha wasikilizaji kujiunga katika kundi hili, na kushika amri za Mungu. Maelfu wasingejua ukweli huu, kama isingalikuwa kwa njia hiyo.

Kule kumtii Mungu na kushika amri zake, kutahesabiwa kuwa ni uasi. Wazazi watawatendea watoto wao walioamini ukatili mkubwa. Watoto wengine watafukuzwa kutoka nyumbani kwao, na kunyimwa urithi. “Wote wapendao kuishi maisha ya utawa katika

Kristo, wataudhiwa” 2Tim. 3:12. Kwa kadiri washikao sabato watakavyokataa kushika jumapili, wengine watatupwa magerezani, wengine watafukuzwa kuwa wakimbizi na wengine watatendewa kama watumwa. Kadiri Roho wa Mungu atakavyokuwa ameondolewa kwa watu, ulimwengu utakuwa na hali ngeni. Watu watakuwa wakali na wakatili sana, kicho na upendo wa Mungu vitakapoondolewa.

Tufani yakaribia

Kwa kadiri tufani ikaribiavyo, watu waliojidai kuwa waumini katika ujumbe wa malaika wa tatu, lakini hawakutakaswa kwa ile kweli, watauacha uamini wao na kujiunga na upande wa upinzani. Kule kujiunga na ulimwengu wanafahamu mambo ya kanisa vizuri, ingawa si kamili. Watu ambao zamani walikuwa wakilitumikia kanisa vizuri, sasa wanajiunga na upande wa wengi kukwaza wengine na kuwapoteza. Wamekuwa maadui wakali wa wale wa zamani walikuwa wenzao. Waasi hawa ambao sasa wamekuwa watumishi wa Bwana wametoa maonyo kwa ukamilifu, kwa kuongozwa na Roho Mtaktifu. Hawakuzuilika kwa kutafuta faida zao, wala kutafuta heshima na vyeo vya duniani. Kazi hiyo ilikuwa kubwa zaidi ya uwezo wao, lakini hawakuiacha. Wakijisikia katika hali ya unyonge na kutoweza kwao, walimkimbilia mweza yote, ili awasaidie. [297]

Watumishi wa Bwana wametoa maonyo kwa ukamilifu, kwa kuongozwa na Roho Mtaktifu. Hawakuzuilika kwa kutafuta faida zao, wala kutafuta heshima na vyeo vya duniani. Kazi hiyo ilikuwa kubwa zaidi ya uwezo wao, lakini hawakuiacha. Wakijisikia katika hali ya unyonge na kutoweza kwao, walimkimbilia mweza yote, ili awasaidie.

Katika vipindi mbalimbali vya historia ya dunia kazi ya Mungu imeonyesha maendeleo makubwa, kufuatana na hali ya watu kwa vipindi hivyo. Kila kipindi ukweli ulipenya katikati ya upinzani. Wajumbe wa Bwana hutimiza wajibu wao, na kumwachia mwenyewe matokeo, yaani Mungu.

Upinzani Kufikia Kikomo Kipya

Mapingamizi yalifikia hali ya mateso makali, watumishi wa Mungu walitiwa wasiwasi, maana huonekana kwamba wamejiletea matatizo. Lakini neno la Mungu huwathubutisha kuwa hawakukosa. Basi imani yao huzidi na juhudi zao huongezeka. Usemi wao huwa

“Kristo ameshinda uwezo wa dunia, kwa hiyo sisi nasi tutahofuje ulimwengu ulioshindwa tayari?”

Hakuna mtu anayemtumikia Mungu bila kujiandikisha katika vita vya mwovu. Malaika waovu watamshambulia, kwa sababu huwanyang’anya watu wao, yaani huteka mateka. Watu waovu watajaribu kumtenganisha na Mungu kwa kumletea majaribu. Hayo yote yakishindwa, ndipo nguvu hutumika kumlazimisha.

Lakini kwa kuwa Kristo ni mtetezi wa binadamu katika hekalu la mbinguni, mvuto wa roho Mtakatifu huwavuvia watawala na waamuzi. Ingawa wengi wa watawala ni wajumbe wa shetani, lakini Mungu anao wajumbe wachache watazuia tufani iliyokuwa karibu kutokea. Upnzani wa ukweli wa Mungu utazuilika mpaka ujumbe wa malaika wa tatu utangazwe. Ujumbe wa mwisho utawashika baadhi ya wakuu hawa, na baadhi yao watakata shauri kujiunga na watu wa Mungu wakati wa matatizo.

[298]

Mvua ya Masika na Kilio Kikuu

Malaika ambaye anaungana na malaika wa tatu ataung’azia ulimwengu wote kwa utukufu wake. Ujumbe wa malaika wa kwanza ulitangazwa kwa kila kituo cha Misheni Ulimwenguni pote. Katika nchi nyingine palikuwa na mwitikio mkuu wa ujumbe, ambao tangu siku za watengenezaji haukuonekana mwitikio kama huo. Lakini mwitikio huo utazidiwa na ule wa ujumbe wa mwisho kwa ulimwengu, ule wa malaika wa tatu.

Kazi itafanana na ile ya siku ya Pentekoste. “Mvua ya vuli ilitolewa ili kuotesha mbegu za Injili huko mwanzoni”; “Kadhalika mvua ya masika itatolewa wakati Injili inapofungwa; ili kukomaza mavuno ya Injili.” Hosea 6:3; Yoeli 2:23.

Kazi kuu ya Injili haitafungwa vivi hivi tu, bila maonyesho makuu ya uwezo wa Mungu, kama ilivyofunguliwa. Unabii ulio-timizwa katika kufunguliwa kwake, utatimizwa pia katika kufungwa kwake. Hapa ndipo wakati wa kuburudishwa, ambako Petro alikutazamia Matendo 3:19-20.

Watumishi wa Mungu wenye nyuso za kung’aa kwa kujitoa kwao kamili, wataharakisha wakienda huku na huko kuutangaza ujumbe wa mbinguni. Miujiza itatendeka, wagonjwa wataponyeshwa. Shetani atafanya miujiza yake ya uongo, hata kushusha moto ku-

toka mbinguni, machoni pa wanadamu, Ufunuo 13:13. Hivyo walimwengu watakabiliwa na uamuzi halisi, kule watakakosimama.

Ujumbe hautatangazwa kwa njia ya mabishano, bali kwa njia ya uthibitisho kwa Roho wa Mungu. Majadiliano yamefanyika, vitabu pia vimefanya sehemu yake, hata hivyo wengi hawakuweza kuufahamu ukweli kamili. Sasa ukweli unadhihirika. Kwa hiyo hakuna mtu awezaye kuzuiwa na jamaa, au na waongozi wa kanisa asijiunge na kundi la kweli la Mungu. Walakini watu wengi sana watajiunga upande wa watu wa Mungu.

39/Wakati wa Taabu

“Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako: na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati huo huo, na wakati huo watu wako wataokolewa: kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile”. Daniel 12:1.

Wakati ujumbe wa malaika wa tatu ufungwapo, watu wa Mungu watakuwa wamekamilisha kazi yao, Watakuwa wamepokea mvua ya masika, nao sasa wako tayari kukabiliana na saa ya kujaribiwa inayowajia, Ujumbe wa mwisho wa kukata shauri umekwisha kutolewa ulimwenguni, na wote waliojithubutisha kuwa waaminifu kwa Mungu wametiwa “mhuri wa Mungu”. Ndipo Yesu anapokomesha kazi yake kama mwombezi wa wanadamu huko mbinguni. Hapo atasema kwa sauti kuu, “imekwisha” “mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa”. Ufunuo 22:11. Kristo amekwisha kufanya ukombozi kwa watu wake, na amefuta dhambi zao. “Na ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu” (Daniel 7:27) karibu kutolewa kwa warithi wa wokovu, na Yesu atatawala kama mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana.

Atakapotoka patakatifu, giza kuu litawafunika watu dunaini. Wenye haki hawana budi waishi machoni pa Mungu mtakatifu bila kuwa na mwombezi. Kile kinachowalinda waovu kimeondolewa, na shetani anachukua utawala kamili bila kizuizi kwa watu ambao hawakutubu. Roho wa Mungu ameondolewa dunaini. Shetani atawatumbukiza wenyeji wa ulimwengu katika taabu kuu ya mwisho. Malaika wa Mungu waliokuwa wakizuia pepo kuu, sasa wanaziachia pepo hizo ni fujo ya ajabu na mauaji yasiyosemwa. Ulimwengu mzima utahusikia katika kuangamizana bila huruma, zaidi ya maangamizo yaliyouangukia Yerusalemu wa zamani. Mpaka sasa majeshi yako tayari, yanangoja tu ruhusa ya Mungu ili yaanze kazi ya kuangamizi kila kona.

Wenye kushika sheria ya Mungu watahesabika kama ndio wenye kusababisha maafa hayo, yaliyojaa ulimwenguni. Nguvu na uwezo uliofanya kazi ya kumaliza Injili iliwachukiza waovu, na shetani atachochea roho ya chuki isiyo na kifani, ili kuwaandama wale waliopokea ujumbe na kujiunga na kundi la Mungu.

Wakati Mungu alipowaacha Wayahudi wao pamoja na makuhani wao walikuwa bado wakijihesabu kuwa ni wapendwa wa Mungu. Huduma za kanisani zilikuwa zinaendeshwa kama kawaida, kila siku waliomba baraka kwa Mungu, kama watu wataua, na hali wamejaa uharibifu, wakiwa na hatia ya damu ya Mwana wa Mungu. Hali kadhalika, mstari wa ulimwengu utakapokuwa umepigwa, na kesi yake imeshakatwa milele, wenyeji wa ulimwengu hawatatambua hata kidogo. Aina za ibada ambazo hazina misingi zitakuwa zinaendeshwa kimitindo, na watu ambao Mungu hayumo kati yao. Shetani ndiye atakuwa akiwaongoza ili kukamilisha kusudi lake la udanganyifu. [300]

Wakati wa Taabu ya Yakobo

Kwa vile Sabato itakuwa ndilo jambo hasa la kushindania katika ulimwengu wa Kikristo, itaamuliwa kuwa watu wachache wanaosimama peke yao kinyume cha kanisa na serikali, ambao huabudu siku ya jumamosi badala ya jumapili, hawawezi kuvumiliwa zaidi. Ni bora watu wachache washughulikiwe kikamilifu kuliko taifa zima kuingia katika machafuko. Mambo yale yale yaliyoletwa pia kwa Kristo. Kayafa alisema, “Hamfikirii ya kuwa yafaa mtu mmoja afe, kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima” Yohana 11:50. Jambo hili hili litaletwa tena ili kuwapinga washika sabato ya amri ya nne. Itasemwa kwamba, kama hawasikii na kuacha ibada ya jumamosi baada ya muda fulani, afadhali wauawe. Warumi katika ulimwengu wa zamani pamoja na kanisa lililoasi walitumia jambo hili, Waprotestanti waliasi kutoka ulimwengu mpya watafuata njia ile ile. Ndipo watu wa Mungu watakuwa na wakati mbaya, kama ilivyoandikwa kwamba “wakati wa taabu ya Yakobo” Yakobo wakati aliposhindana katika maombi ili aokolewe mikononi mwa Esau, husimama kuwakilisha maisha ya watu wa Mungu wakati wa taabu.

Yakobo alikimbia kutoka kwao, kwa sababu ya udanganyifu aliofanya ili apate mibaraka ya baba yake iliyokusudiwa kwa Esau.

Alikimbia bila silaha yoyote, ili apate kujiponya. Baada ya kukaa katika hali ya ukimbizi miaka mingi, alianza safari kurudi kwao. Alipofika mipakani, alitishwa na habari kwamba Esau alikuwa akimjia, bila shaka kulipiza kisasi. Tumaini la Yakobo lilikuwa kwa Mungu tu; ngao yake ikiwa maombi yake.

[301] Akiwa peke yake na Mungu, aliungama dhambi zake kwa unyenyekevu na kujidhili mbele za Mungu. Tatizo kuu katika maisha yake limefika. Aliendelea kuomba gizani, kwa ghafla mkono ukamshika begani mwake. Alidhani kuwa ni adui fulani ataka kumwangamiza. Basi akashikana naye kwa nguvu zake zote, akashindana naye. Wakati wa mapambazuko, yule mgeni akatumia uwezo wa pekee usiokuwa wa kibinadamu. Yakobo akaona kuwa amepooza, na akaanguka chini hana nguvu huku akilia na kuomba akiwa shingoni mwa huyo mgeni wa kimiujiza. Halafu alifahamu kuwa malaika wa agano ndiye aliyekuwa akishindana naye. Alikuwa na majuto kwa ajili ya dhambi yake kwa muda mrefu, na sasa lazima awe na hakika kuwa amesamehewa. Malaika akasema, “niache kwani kunapambazuka” lakini mzee Yakobo akasema, “Sikuachi, usiponibariki” Yakobo akatumaini rehema za Mungu kwa kushika maagano. Kwa njia ya toba na kujitoa kikweli, mtu dhaifu huyu alishinda mshimiwa wa mbinguni.

Shetani alikuwa amemshitaki Yakobo mbele za Mungu kwa ajili ya dhambi zake, alikuwa amechochea Esau ili amshambulie. Wakati mzee Yakobo alipokuwa akiomba usiku ule, shetani alijitahidi kumfisha moyo na kumkatisha tamaa, ili kuharibu ushirika wake na Mungu. Alikuwa mashakani kabisa; lakini alitubu kweli kweli na kumshikilia malaika, na kusihi apate kibali mpaka akamshinda. Jinsi shetani alivyomshitaki Yakobo, ndivyo atakavyowashitaki watu wa Mungu, lakini kundi linaloshika amri za Mungu litashindana na ukuu wake. Aona kuwa malaika wa Mungu wanawalinda, na anafahamu kuwa dhambi zao zimesamehewa. Anajua dhambi zile alizowashawishi kutenda, kwa hiyo anadai kuwa Mungu hawezi kuwakubali watu wa jinsi hiyo na waangamize shetani na malaika zake. Akasema kuwa watu hao ni mali yake, ili waangamizwe pamoja.

Bwana humruhusu awajaribu kabisa. Uaminifu wao kwa Mungu, imani yao, na matumaini yao vyote vitajaribiwa na Shetani kabisa kabisa. Shetani atawaogofya kwa bidii yake yote. Hutumaini kuwa

kwa kufanya hivyo atavunja matumaini yao, na kuvunja imani yao kwa Mungu, ili wasalimu amri.

Uchungu Kwamba Mungu Alaumiwe.

Walakini uchungu ambao utawapata watu wa Mungu sio ule wa kuogopa mateso. Huogopa kwamba kwa kukosa kuangalia, waweza kuwa na makosa yatakayosababisha wasielewe ahadi ya Mungu isemayo “Mimi nitakulinda utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujiua ulimwengu wote” ufunuo 3:10. Kama wangeonekana hawastahili kwa ajili ya makosa katika maisha yao, jina la Mungu takatifu lingeshutumiwa.

Wanaonyesha jinsi walivyotubu dhambi zao za nyuma ambazo ni nyingi sana, wanaomba ahadi ya Mwokozi kwamba “Au azishike nguvu zangu, afanye amani nami, naam, afanye amani nami” Isaya 27:5.

Ingawa wana maumivu ya rohoni sana na masumbuko, hawakomi kuomba na kusihi. Wanamshikilia Mungu kiroho kama Yakobo alivyofanya kwa malaika. Usemi wao utakuwa ule ule, “sikuachi, usiponibariki” [302]

Dhambi Zilifutwa

Katika wakati wa taabu, kama watu wa Mungu watakuwa na dhambi ambazo hazijaungamwa mbele yao wakati wakisumbuka kwa hofu na uchungu rohoni watashindwa. Kukata tamaa kutaondoa matumaini yao na imani yao kwa Mungu, na kwa hiyo hawatajishughulisha na kuomba ukombozi. Lakini hawakuficha makosa yao yasionekane. Dhambi zao zimewatangulia kwenda hukumuni, zimefutwa, nao hawewezi kuzikumbuka.

Kwa habari za Yakobo, Bwana ameonyesha kuwa hawezi kuchukulina na ubaya. Wote wanaotoa udhuru au kuficha dhambi zao, na kuziacha ziwe vitabuni mbinguni bila kuungamwa na kusamehewa, watashindwa na shetani. Kadiri ya madaraka makuu wanayoshika, ndivyo adui wao anavyofurahi. Wanaochelewa kujiandaa hawataweza kujiandaa wakati wa taabu. Watu wa namna hiyo hawana tumaini.

Habari ya Yakobo pia huonyesha kuwa Mungu hawezi kuwatupa wale waliotumbukizwa dhambini bila mipango, lakini wamemrudia kwa toba na kujitoa kabisa. Mungu atawatumia malaika wawafariji wakati wa taabu. Macho ya Bwana yako juu ya watu wake. Ndimi za moto huonekana kuwateketeza, lakini mtakasaji atawaleta wametakasika katika dhahabu iliyojaribiwa kwa moto.

Imani Idumuyo

Wakati wa matatizo na dhiki ulio mbele yetu unataka imani halisi, imani yenye kudumu, yenye kustahimili taabu, uchelevu, na njaa, imani iliyo imara, ijapokuwa inajaribiwa vikali sana, haitafia. Ushindi wa Yakobo ni uthibitisho wa nguvu ya maombi. Wote watakaozishika ahadi za Mungu kama Yakobo alivyofanya watafaulu kama yeye. Kushindana na Mungu ni wachache kiasi gani wanajua maana yake! Wakati mawimbi ya mashaka na kukata tama yanapomvamia mtu, ni watu wachache kiasi gani wenye kuzishikilai ahadi za Mungu.

[303] Wale wanaoonyesha imani kidogo wakati huu, wamo katika hatari kuu ya kutumbukia katika udanyanyifu wa shetani. Hata kama watastahimili jaribu, hata hivyo watakumbwa na mashaka kwa sababu siyo mazoea yao kumtegemea Mungu. Lazima sasa tuhakikishe ahadi zake na kuzithibitisha. Kila mara matatizo huwa makubwa wakati wa kutokea kuliko wakati wa matazamio. Lakini sivyo itakavyokuwa katika dhiki iliyo mbele yetu. Maelezo yanayoelezwa kuhusu dhiki hiyo, hata yawe na ufundi namna gani hayatalingana na jambo halisi. Katika muda huo kila mtu lazima asimame peke yake mbele za Mungu.

Sasa wakati Kuhani wetu mkuu, anapofanya upatanisho kwa ajili yetu, ingetupasa tuwe wakamilifu katika Kristo. Mwokozi wetu hakujitolea kwa majaribu ya mwovu hata kwa wazo. Shetani hupata vitu katika mioyo ya wanadamu ambavyo huvishikilia na kumwezesha awaingilie; huwa na aina fulani za dhambi ambazo hupendelewa na watu, ambazo humpa nafasi washinde. Lakini Kristo alisema kumhusu yeye: “Yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu” Yohana 14:30. Shetani hakuweza kupata jambo kwa Yesu Mwanawa Mungu, ambalo kwalo angeweza kumshinda. Hapakuwa

na dhambi yo yote ndani yake ambayo angeingilia kwake. Hii ndiyo hali ambayo wale watakaosimama wakati wa taabu watakuwa nayo.

Ni katika maisha haya ndiyo inatupasa kujitenga na dhambi kabisa, kwa imani katika damu ya ukombozi wa Kristo. Mwokozi wetu anaturalika tuungane naye, tuunge udhaifu wetu na nguvu zake, kutostahili kwetu na haki yake. Anatumegemea sisi kuungana na mbingu ili kurekebisha tabia zetu zifanane na za Mungu.

Mambo ya ajabu kuhusu tabia ya kishetani zitaonekana mbinguni, kama alama ya pepo wachafu wafanyao miujiza. Roho za mashetani zitawaenda “wafalme wa dunia” na ulimwengu wote kuwahimiza waungane na shetani katika pambano lake la mwisho na serikali ya mbinguni. Watu watainuka wakijifanya kuwa Kristo mwenyewe. Watafanya miujiza ya kuponya na kudai kuwa wamepata mafunuo kutoka mbinguni kupingana na Maandiko.

Tendo la Kutawazwa

Katika mfululizo wa mambo ya kutawazwa ya udanganyifu, Shetani mwenyewe atajifananisha kama Kristo. Kanisa limemtazamia Mwokozi kwa muda mrefu kutimiliza matumaini yake. Sasa mdanganyaji mkuu atajifanya kwamba ndiye Kristo anakuja. Shetani atajionyesha mwenyewe katika hali ya mng’ao, kama kiumbe maarufu kabisa chenye kung’aa kikimwigiza Mwana wa Mungu kama anavyoelezwa katika Ufunuo 1:13-15.

[304]

Utukufu unaomzunguka ni mwingi sana unashinda kitu chote macho ya wanadamu walichopata kuona. Kishindo cha kelele ya ushindi kinasikika, “Kristo amekuja!” Watu wanamwangukia. Anainua mikono yake na kuwabariki. Sauti yake ni laini, imejaa muziki. Kwa sauti ya huruma anaeleza mambo ya mbinguni ambayo ni ya kisasa yaliyosemwa na Mwokozi. Anaponya wagonjwa halafu akiwa kama Kristo, asema kuwa amebadili Sabato kuwa Jumapili. Anasema kuwa wale watunzao sabato ya Jumamosi wanalikufuru jina lake. Hili ni danganyo kuu katika madanganyo yake. Maelfu ya watu wanaamini uchawi huo na kusema “uwezo huu mkuu ni wa Mungu” Matendo 8:10.

Watu wa Mungu hawapotoshwi

Lakini watu wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya huyu kristo bandia hayalingani na Maandiko. Mibaraka yake ameitoa kwa waabudu mnyama na sanamu yake, watu ambao watamwagiwa ghadhabu ya Mungu isiyo na huruma, kama Biblia isemavyo.

Zaidi ya hayo, shetani hataruhusiwa kuigiza kabisa jinsi Kristo atakavyokuja. Mwokozi amewaonya watu wake kuhusu sehemu hii, ya udanganyifu. Amesema “kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa, na maajabu wapate kuwapoteza, kama yumkini, hata wateule ... Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yuko nyumbani msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu”. Mat. 23:24-27. Soma pia Mathayo 25:31; ufunuo 1:7; 1Thes. 4:16-17. Kuja kwa jinsi hii, hakuna uwezekano wa kukuigiza. Kutaonekana katika ulimwengu mzima.

[305] Wanafunzi wa kweli wa Biblia tu, waliopokea upendo wa kweli ndio watakingwa na madanganyo haya makuu, yatakayoukumba ulimwengu. Ushuhuda wa Biblia pekee ndio utakaompinga mdanganyaji katika hila zake. Je, watu wa Mungu sasa wameimarika katika Neno la Mungu, kwamba hawatatikiswa na kuangukia mbali katika madanganyo? Je, katika matatizo kama hayo wataambatana na Biblia tu?

Kwa vile amri itakavyotolewa na makanisa ya kikristo mahali mahali ili kuwapinga washika sabato, serikali haitawalinda, ila itawaacha kusudi watendwe mabaya na wale wanaotaka kuwatenda vibaya. Ndipo watu wa Mungu watakimbia kutoka mijini na vijijini, na kujikusanya vikundi vikundi, wakiishi mahali pa shida huko nyikani. Wengi watapata makao mapangoni mwa milima, sawa kama wakristo wa mabonde ya Piedmonti. Lakini wengi sana wa mataifa yote na wa kabali zote, watu wakuu na wadogo, matajiri na maskini weusi na weupe watatupwa katika vifungo vibaya sana. Wapenzi wa Mungu watapitia wakati mgumu sana, wakifungwa katika magereza, wakitajwa kuuawa, wakionekana kuwa watakufa katika giza magerezani.

Je, Bwana atawasahau watu wake katika wakati wa dhiki kama hiyo? Je, alimsahau Nuhu mwaminifu au Lutu, Yusufu, Eliya,

Yeremia au Danieli? Ingawa adui zao wawatupe magerezani, hata hivo kuta za magereza haziwezi kuwatenganisha na mbingu, wala kutenga roho zao na Kristo. Malaika watawazuru katika magereza ukiwa penye giza patang'azwa na nuru ya mbinguni kama ile iliyong'ara pale Paulo na Sila walipokuwa wakifungiwa, na kuimba katika mji wa Filipi.

Hukumu za Mungu zitawaangukia wale waliokuwa wakitaka kuangamiza watu wake. Kwa Mungu, kutoa mapigo ni jambo geni. Isaya 28:21. Soma pia Ezekieli 33:11. Bwana ni “mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli. . . mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi” Hata hivyo “hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe” Kutoka 34:6-7; Nahumu 1:3. Taifa ambalo amelivumilia muda mrefu, na limekijaza kikombe cha uovu, mwishowe litakinywea kikombe cha ghadhabu ya Mungu isiyokuwa na huruma.

Kristo amalizapo maombezi yake katika patakatifu pa mbinguni, ghadhabu yake isiyochanganyikana na huruma itawakabili wote waabuduo mnyama, itamwagwa. Mapigo ya Misri yalikuwa sawa na ghadhabu ya Mungu itakayomwagwa ulimwenguni, ila itakuwa kali zaidi. Ghadhabu hii itamwagwa kwa muda mfupi kabla ya ukombozi wa watu wa Mungu. Mwandishi wa Ufunuo asema, “pakawa na jipu baya, bovu, juu ya watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake” “Basi ikawa damu kama damu ya mfu”.

“Na mito, na chemichemi za maji zikawa damu. . . . Malaika akatangaza, wewe u mwenye haki Ee, Bwana. . . Kwa kuwa umehukumu hivi. . . Kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na manabii wako, nawe umewapa wainywe; nao wamestahili” ufunuo 16:2-6, 8-9. Kwa kuwahukumia kifo watu wa Mungu, wamejipatia hatia ya damu yao; kana kwamba wameimwaga kwa mikono yao. Kristo alisema kuhusu Wayahudi wa siku zake, kuwa walikuwa na hatia ya damu ya watakatifu wote, tangu ziku za Habili (Mathayo 23:34-36) maana hata wao wanayo roho ile ile ya uuaji wa manabii.

Pigo litakalofuata litatolewa kwa jua. Jua litapewa uwezo wa kuwaanguza watu kwa joto. Nabii asema kuhusu wakati huo wa kutisha: “maana mavuno ya mashamba yamepotea”“Mizabibu imesinyaa, mtini nao umeiva, nao mkomamanga, na mtende, na mtofaa, naam, miti yote ya mashamba imekauka, maana fu-

raha imekauka katika wanadamu. Jinsi wanyama wanavyougua! Makundi ya ng'ombe wamefadhaika, kwa sababu hawana malisho; naam makundi ya kondoo yamepata mateso. Vijito vya maji vimekauka, na moto umeyateketeza malisho nyikani.” Yel. 1:11-12, 18-20.

Mapigo haya hayatapiga ulimwengu wote, lakini yatakuwa mabaya sana sana kwa wale watakaoyapata. Mapigo yote ya Mungu yaliyotokea kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema, yamekuwa yenye huruma ndani yake. Damu ya Kristo imemkinga mwenye dhambi asipate adhabu inayostahili hali yake. Lakini katika hukumu ya mwisho, mapigo ya adhabu ya Mungu hayatakuwa na huruma. Watu watatafuta kificho cha Mungu waliyemdharau.

Wakati watakaposumbuka kuona dhiki, wakitafuta chakula, watu wa Mungu hawataachwa wapotee. Malaika watawaletea mahitaji yao. “atapewa chakula chake maji yake hayatakoma” “Mimi Bwana nitawasikia, mimi Mungu wa Israeli sitawaacha” Isaya 33:16; 41:17.

Kwa kibinadamu itaonekana kuwa karibuni watu wa Mungu watamwaga damu yao, yaani watauawa, kama wafia dini wengine waliowatangulia. Ni kitambo cha utisho wenye uchungu. Waovu wanashangilia na kusema Je, imani yenu iko wapi. Mbona Mungu hakuwaokoa mikononi mwetu, iwapo kweli ninyi ni watu wake? Lakini watu wa Mungu wanakumbuka Yesu alivyokufa mslabani. Kwa hiyo wanaendelea kushuhudiana na Mungu tu kama Yakobo.

Makundi ya Malaika Walinzi

Malaika wameamuriwa kuwalinda wana wa Mungu wenye kushika Neno lake. Malaika wameona dhiki zao na kusikia maombi yao.

[307] Wanangojea amri ya jemadari Mkuu ili apate kuwaondoa mara moja. Ila lazima wangojee kidogo. Watu wa Mungu lazima wakinywee kikombe na kubatizwa kwa ubatizo. Mathayo 20:20-23; lakini kwa ajili ya wateule wakati wadhiki utafupishwa. Mwisho unakuja upesi kiasi mtu asivyodhani.

Ijapokuwa amri ya kuwaangamiza wasabato imekwisha tangazwa, adui zao mahali pengine watajaribu kuitekeleza. Lakini hakuna awezaye kupenya ngome ya malaika walinzi ili kuwafikia. Wengine watawarukia, lakini silaha zao zitavunjika kama mabua.

Wakrsto wengine watapiganiwa na malaika wenye umbo la binadamu.

Katika vizazi vyote wakaa mbinguni wamekuwa wakijishughulisha na mambo ya wanadamu. Wengine wamekaribishwa kama binadamu, wengine kama wasafiri wameingizwa katika nyumba za watu, wengine katika magereza na kuwafungulia wafungwa wa Bwana. Walikuja kuingirisha jiwe kaburini pa Yesu.

Malaika huzuru mikusanyiko ya waovu, kama waliyozuru Sodoma, ili kuona la kuwatendea hao; kama kuangamizwa. Bwana huzuia maangamizi kwa ajili ya watu wake wachache walio kati ya waovu, na kuingea muda zaidi wa usalama. Wenye dhambi hawana habari kuwa maisha yao yanahifadhiwa na watu wa Mungu wachache walio kati yao, ambao huwaudhi.

Kila mara katika mabaraza ya walimwengu malaika wamekuwa wasemaji. Masikio ya wanadamu yamesikia maombi yao, na midomo ya watu imeyadharau mashauri yao. Malaika hawa wa mbinguni wamethititisha hali ya binadamu ilivyo kwa kweli wamewashinda na kuwakamata malaika waovu wanaowatesa wanadamu, ambao ni wacha Mungu.

Wana wa Mungu wanangojea kwa subira ishara za Mfalme wao anayekuja. Kwa kadiri wanavyokazana na mapambazuko ya milele. Neno likasikika likiwa kama wimbo mtamu, “Kristo yu aja” Sauti ya Kristo ikasikika kutoka katika lango jinsi lilivyokuwa likifunguka “Mimi sasa nipo nanyi. Msiogope. Nimewapigania vita, na kwa jina langu sasa ninyi ni washindaji”.

Mwokozi atatumia msaada wake tunapouhitaji. Wakati taabu ni muhimu sana kwa watu wa Mungu lakini kila mwumini budi aone jinsi imani inavyoleta ahadi za Mungu kutuzungukia. “Waliokombolewa na Bwana, watarudi, watakuja Sayuni wakiimba. Furaha za milele watapata, huzuni na kuugua zitakimbia” isaya 51:11.

Kama damu ya mashahidi wa Kristo ingemwagika wakati huu, uaminifu wao usingaliwaaminishwa watu wengine. Kwa kuwa ugumu wa mioyo yao umeisukumia rehema mbali, wala haitarudi tena. Kama wenye haki wangaliangamizwa na adui zao na kunyamazishwa mwovu angelishangilia. Kristo alikuwa amesema, “Njooi watu wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako, ukafunge mlango nyuma yako ukajifiche kitambo kidogo, mpaka ghadhabu hii itakapopita. Kwa maana tazama, Bwana anakuja kutoka mahali

pake, ili kuwaadhibu wao wakaao duniani kwa sababu ya uovu wao”
Isaya 26:20-21.

Itakuwa fahari ya ukombozi wa watu hao ambao wamengoja kwa uvumilivu kurudi kwake Mwokozi, watu ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima.

Wakati ulinzi wa kibinadamu wa kisheria utakapoondolewa kwa watu wenye kuiheshimu sheria ya Mungu ndipo kutakuwa miondoko kadhaa katika nchi mbalimbali ya kuwaangamiza. Wakati unapokaribia wa kuwaangamiza, kama ilivyoamuriwa, watu wataazimu kuwavamia usiku mmoja ili kuwanyamazisha kabisa.

Watu wa Mungu, wengine wamo magerezani, wengine wamo misituni milimani, wanaendelea kumsihi Mungu awahifadhi. Watu wenye silaha, wakihimizwa na malaika wa shetani, wanajitayarisha kuwaangamizia mbali. Sasa katika muda wa wasiwasi mno, Mungu ataingilia kati. “Mtakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku kama vile mtu aendapo . . . katika mlima wa Bwana, aliye mwamba wa Israeli. Naye Bwana atawafanya watu kusikia sauti yake ya utukufu, naye atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira yake na mwako wa moto ulao, pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu” isaya 30:29-30.

Makundi ya watu waovu yako karibu kuwavamia wana wa Mungu, wakati giza kuu, na kuu kabisa kuliko usiku lilifunika dunia. Kisha upinde wa mvua ukatanda mbinguni na ukaonekana kama upinde huo unawazungushia hawa wana wa Mungu. Kundi la waovu linazubaa. Kusudi lao limesahaulika, sasa wanakodolea macho juu ya ishara ya agano la Mungu, na wanataka wafunikwe wasione mng’aro huo.

Kwa watu wa Mungu sauti ilisikika ikisema, “Tazamameni juu” Wakatazama juu wakauona utukufu wa Mungu na Mwana Kondoo katika kiti cha enzi, kama Stefano alivyoona. Matendo 7:55-56. Walizitambua alama za misumari, ambazo ni alama za kujidhili kwake. Kisha wakasikia neno “nataka hao ulionipa wawe pamoja nami” Yohana 17:24. Sauti ilisikika ikisema, “Wanakuja, wametakaswa, hawana waa lolote, wala uchafu! Wameshika neno la uvumilivu wangu”.

Kwenye usiku wa manane Mungu aonyesha uwezo wake wa ajili ya kuwaokoa watu wake. Jua latokea liking’aa kwa nguvu. Maajabu

na ishara vyafuata. Waovu wakaangalia kwa hofu kuu juu ya mambo hayo, wakati wateule wanaona kuwa hizo ndizo ishara za ukombozi wao. Katikati ya mbingu zilizokasirika, kunatokea nafasi wazi yenye utukufu usioelezeka, ambako sauti ya Mungu inatokea ikinguruma kama maporomoko ya maji, ikisema, “Imekwisha kuwa!” Ufunuo 16:17.

[310] Sauti hiyo hutetemesha mbingu na nchi. Litatokea tetemeko la nchi. “Kubwa, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi, hapakuwa namna ile”. Ufunuo 16:18. Miamba mikubwa ikatupwa huku na huko juu ya nchi. Bahari ikasukasuka kwa fujo na ghasia. Kukasikika sauti ya kilio na mvumo wa tufani kama sauti ya mashetani. Uso wa nchi ukavunjikavunjika. Msingi wake ukaonekana kana kwamba umeng’oka. Bandari kuu zilizofananishwa na Sodomia kwa uchafu na ufisadi wake, zikazamishwa na bahari yenye msukosuko. Babeli mkuu, amekumbukwa mbele za Mungu, ampe kikombe cha ghadhabu ya uchafu wake. Ufunuo 16:19. Mvua ya mawe makubwa inafanya kazi yake ya kuponda watu. Miji mikuu yenye kiburi inaangushwa chini. Majumba makubwa, ambamo wakuu na matajiri walifanyia anasa zao yakabomolewa machoni mwao. Magereza yakapasuliwa na watu wa Mungu waliofungiwa huko wakatoka.

“Makaburi yakafunguliwa, na wengi wao waliolala mavumbini... wakaamka, wengine wapate uzima wa milele, na wengine wapate aibu na kudharauliwa milele”

“Na wale waliomchoma Kristo, waliokuwa wakimdhiki na kuchekelea kifo chake cha uchungu mkuu” “na wale waliokuwa wapingaji wakuu wa ukweli, watafufuliwa wapate kuona heshima watakayopewa waaminifu na watiifu wa sheria ya Mungu” Dan. 12:2 Ufu 1:7.

Umeme mkali unametameta ukizunguka nchi, ukiwa kama mwali wa moto. Juu ya ngurumo za ajabu, sauti, za sirisiri na masikitiko zikitangaza ajali ya waovu. Wale waliokuwa wenye majivuno na wapinzani wakuu, wakatili kwa watumishi wa Mungu, sasa wanagwaya kwa hofu. Mashetani wanatetemeka, wakati watu wanaomba msamaha.

Siku ya Bwana

Nabii Isaya asema, “Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuzi-abudu, kwa fuko na popo; ili aingie ndani ya pambo za majabali, na ndani ya tundu za miamba iliyopasuka, mbele ya utisho wa Bwana na utukufu wa enzi yake atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia” Isaya 2:20-21.

Wale waliotoa yote kwa Kristo watakuwa salamini. Mbele ya dunia na katika kifo wamemshuhudia jinsi walivyo waaminifu kwake aliyekufa kwa ajili yao. Nyuso zao, ambazo hapo mbele zilikuwa na wasiwasi, sasa zimejaa kutabasamu na mshangao.

Sauti zao zinaimba wimbo wa ushindi, wakisema, “Mungu ni ngome yetu na nguvu, ni msaada kwenye shida ulio karibu sana. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, ijapopepesuka milima kwa kiburi chake”. Zaburi 46:1-3. [311]

Maneno haya yenye matumaini matakatifu yanapopaa kwa Mungu, utukufu wa mji mtukufu unaonekana wakati malango yanapofunguliwa. Halafu ukaonekana mkono angani ukishikilia mbao mbili za mawe. Hizo ni mbao za amri za Mungu zilizotangazwa huko Sinai. Sasa zinadhihirika kuwa ndizo kipimo katika hukumu. Maneno yake ni dhahiri, rahisi kueleweka kwa wote. Kumbukumbu inaamshwa. Hali ya ushirikina ufedhuli inaondolewa mawazoni.

Haiwezekani kuelekeza hali ya hofu na fadhaa itakayowapata wale waliokanyaga sheria ya Mungu. Waliihalifu sheria ya Mungu ili kupata furaha ya ulimwengu, na wakawafanya wengine pia kuihalifu. Sasa wanahukumiwa na sheria ile ile waliyoidharau. Wanaona kuwa hawana udhuru wote. Watu hao, maadui wa sheria za Mungu sasa wanaona wazi upya juu ya ukweli na wajibu wao. Sasa wanaona kuwa sabato ni muhuri wa Mungu aliye hai. Wanaona, lakini wamechelewa msingi wa mchanga walikuwa wamejenga; lakini wamechelewa. Walikuwa wakipigana na Mungu wakati wakidhani kuwa walikuwa wanamwabudu. Walimu wa dini waliowaongoza watu kwenda ahera, wakati walidhani kuwa wanawapeleka mbinguni. Wenye madaraka kanisani wanao wajibu mzito kiasi gani! Wachungaji wasio wa kweli wana ole mzito kiasi gani.

Mfalme wa Wafalme Atokea

Sauti ya Mungu inasikika ikitangaza siku na saa ya kuja kwake Yesu. Waisraeli wa Mungu wanasimama wakisikiliza. Nyuso zao ziking'aa kwa utukufu wa Mungu. Mara ikaonekana ishara, wingu dogo jeusi likaonekana upande wa mashariki. Ni wingu ambalo linamzunguka Mwokozi. Watu wa Mungu wanalikodolea macho wakiwa kimya kabisa. Wingu linazidi kukaribia. Kumbe ni wingu jeupe kubwa kabisa, kitako chake kinang'aa kwa utukufu mwingi, kama moto uwakao, juu yake kama upinde wa agano ukilizunguka. Sasa huyu ajaye siye “mtu wa huzuni”, bali ni “mshindaji mkuu” Malaika, ambao ni wengi mno wasiohesabika, wanafuatana naye. Ni wengi mno, maelfu elfu mara elfu kumi, elfu mara maelfu. Kila jicho linamwona Mkuu wa uzima. Taji ya utukufu imo kichwani mwake.

[312] Uso wake unang'aa kuliko jua la mchana. Katika vazi na paji la uso wake analo jina limeandikwa, “MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA” Ufunu o19:16.

Mfalme wa wafalme anakuja juu ya wingu, likizungukwa na miale ya moto. Nchi ikatetemeka mbele yake. “Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbigu zilizo juu, na nchi pia awahukumu watu wake” Zab. 50:3-4.

“Na wafalme wa dunia na wakuu, na majemadari na matajiri na wenye nguvu na kila mtumwa na mwungwana, wakajificha katika pango na nchi ya miamba ya milima, wakaiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira ya Mwanakondoo. Kwa maana siku iliyo kuu ya hasira yao imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?” Ufunuo 6:15-17.

Mambo ya mizaha imekoma, midomo ya uongo imenyamzishwa. Hakuna sauti inayosikika sana, ila vilio na maombolezo. Waovu wanaomba wafukiwe ardhini, kuliko kumwona yule waliyemdhikahi na kumchezea. Sauti ile inayopenya mpaka katika masikio ya wafu waijua. Sauti hiyo iliwasihi mara ngapi ili atubu. Ilisikiwa mara nyingi ikiwaita watu kwa kuwasihi kwa rafiki, ndugu na mkombozi. Sauti inakumbusha juu ya maonyo yaliyodharauliwa na miito iliyokataliwa.

Kuna wale waliomdhihaki Kristo wakati wa mateso yake. Alisema, “Tangu sasa mtamwona mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu akija juu ya mawingu ya mbinguni” Mathayo 26:64. Sasa wanamwangalia katika utukufu wake, na bado atamwona tena ameketi mkono wa kulia wa nguvu. Yuko shupavu Herode aliyemcheka. Wako wale waliomvika taji ya miiba kichwani mwake. Wako wote waliomtendea ufedhuli waliomtemea mate wote waliomchoma na misumari wanaoa alama hizo kwa hofu wa kila aina na kumtesa. Wote hao wanatafuta kukimbia wasionekane kwake.

“Makuhani na wakuu wanakumbuka mambo ya kalwari jinsi walivyokuwa wakisema kuwa, aliponya wengine, basi na ajiponye” Mathayo 27:42. Walivyokuwa wakipiga kelele, “Asulubiwe, asulubiwe” “Ni mwana wa Mungu. Wote wanaukimbia uso wake mfalme wa wafalme.”

[313]

Wote waliukataa ukweli, kutakuwa wakati watakapokumbuka, na kutafakari walivyopata nafasi wakazikataa watatetembea ajabu. Katika fadhaa yao watasikia sauti za wenye haki zikisema “Tazama huyu ndiye Mungu wetu. Ndiye tuliyemngoja, naye atatuokoa” Isaya 25:9.

Sauti ya Mwana wa Mungu yawaita wateule ambao wamelala mavumbini. Watu wataisikia sauti yake popote walipolala, nao watatoka wakiwa jeshi kubwa sana, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha. Watatoka katika gereza la kifo wakiwa wamevaa hali ya kutokufa, huku wakisema, “Ku wapi ewe mauti kushinda kwako? Uwapi ewe mauti uchungu wako?” 1 Kor. 15:55.

Wote wanatoka makaburini mwao wakiwa na kimo kile walicokufa nacho. Lakini wote wanatoka na kuwa na hali ya ujana wa milele. Kristo alikuja ili kurudisha kile kilichopotea. Ataibadili miili yetu ya hali ya hafifu ipate kufanana na mwili wake wa utukufu. Miili ya kufa, ambayo ni miharibifu iliyoharibiwa na dhambi, itakuwa kamili kabisa, yenye sura nzuri, na isiyoharibika. Vilema wote na hali ya ugonjwa vitaachwa kaburini. Walikombolewa watakua (Malaki 4:2) wafikie kimo cha ukamilifu wa waliokuwa nao wanadamu kabla hawajaasi. Laana yo yote imeondolewa. Wateule wa Kristo watakuwa na sura ya Bwana wao katika ukailifu wa miili, mawazo na roho.

Wenye haki walio hai wanabadilishwa; kitambo kufumba na kufumbua jicho. Kwa agizo la Mungu wanabadilika na kuvaa kuto-

haribika, halafu wanaungana na wale waliofufuka ili kumlaki Bwana Hewani. Malaika watawakusanya wateule wote kutoka pande nne za nchi, kutoka upande huu mpaka upande mwingine. Mathayo 24:31. Watoto wachanga wanachukuliwa na kupelekwa kwa mama zao Marafiki waliotengwa na kifo sasa wanaungana tena, bila kuachana kamwe, na wote watapanda kwenda katika mji wa Mungu huku wakiimba nyimbo za furaha kuu.

Mpaka Mji Mtakatifu

[314] Watu wote waliokombolewa ambao hesabu yao ni kama mchanga, macho yao wote wanamwangalia Yesu. Kila jicho linautazama utukufu wake ambaye, “Uso wake ulikuwa umeharibika sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wanadamu” Isaya 52:14. Juu ya vichwa vya washindaji, Yesu anaweka taji za utukufu. Kila mtu ana taji yenye jina lake lile jina jipya (Ufunuo 2:17) na andiko lisemalo, “Utakatifu kwa Bwana”. Kila mtu akapewa tuzo ya ushindi, na kinanda au kinubi cha kuimbia, chenye kung’aa sana. Halafu malaika, mwimbaji anapopiga wimbo, kila mtu anashika kinubi chake akiimba kwa ufundi wa ajabu. Kila sauti ikainuliwa kwa sifa za shukrani ikisema, “Kwake yeye atupendaye na kutuoosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele” Ufu. 1:5-6.

Mbele ya jeshi la waliokombolewa uko mji mtakatifu Yesu afungua malango, na mataifa ambao wametunza sheria yake wanaingia ndani. Kisha sauti yake inasikika ikisema, “Njooi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” Mathayo 25:34. Kristo anawapeleka watu walionunuliwa kwa damu yake mbele ya Baba yake na kusema “Mimi niko hapa pamoja na watoto ulionipa” “Wale ulionipa, nime-watunza”. Waebrania 2:13; Yohana 17:12. Wakati huo Baba awatazamapo kundi hili la waliokombolewa, naona sura yake mwenyewe ndani yao. Alama ya dhambi imeondolewa, na sasa ubinadamu na Uungu umeungana.

Furaha ya Mwokozi inazidi anapoona kundi lililokombolewa kutokana na mateso yake. Na wateule hawa watashiriki katika furaha yake. Wanawaona wale waliowahudumia kwa njia ya maombi

yao, kazi yao, na sadaka zao. Furaha yao itazidi wanavyoona jinsi muungano wa kazi ulivyo, yaani huyu akamleta yule na yule akamleta wingine kadhalika.

Adamu Wawili Wakutana

Waliokombolewa walipokaribishwa katika mji wa Mungu, kulikuwa na shangwe kuu, Adamu wawili karibu wakutana. Mwana wa Mungu atampokea baba wa taifa la kibinadamu, ambaye alimwumba, akamtenda dhambi ambazo zilisababisha kusulubishwa kwa Mwokozi, na kupata alama katika mwili wake. Adamu anapoona alama za misumari katika mikono yake, anajitupa chini ya miguu ya Kristo. Mwokozi anamwinua na kumwambia atazame tena bustani ya Edeni, ambayo alifukuzwa kwa siku nyingi.

Maisha ya Adamu yamekuwa ya huzuni nyingi. Kila mara alipoona majani yakinyauka na alipouona mnyama wa sadaka, ili kumpatanisha na Mungu yote hayo yalimkumbusha ubaya wa dhambi. Aliona uchungu wa ajabu, mambo hayo yote yalipotupwa kwake, kwamba ni yeye aliyesababisha, alijuta kabisa. Akafa katika tumaini. Na sasa kwa kuwa alisamehewa, amerudishiwa hali yake ya kwanza. [315]

Akijaa furaha tele, aliuona mti wa uzima uliokuwa chakula chake. Akaona miche na miti ambayo yeye alikuwa akiishughulikia kwa mikono yake. Akaona maua mazuri. Kweli Edeni imerudishwa!

Mwokozi anamwongoza kwenda kwenye mti wa uzima na akaambiwa ale matunda yake. Adamu aliona maelfu ya ukoo wake ambao wamekombolewa. Ndipo akaitupa taji yake miguuni mwa Mwokozi, akamsujudia. Akashika kinubi chake na kuimba kwa shangwe kuu; “Anayestahili, anayestahili ni Mwana Kondoo peke aliyechinjwa”. Ufu. 5:12. Ndipo ukoo wote wa Adamu wakazitupa taji zao miguuni pa Mwokozi wakamwabudu. Wakati Adamu alipoasi malaika waliomboleza, lakini Kristo alipofungua makaburi wakatoka wenye haki huku ilikuwa shangwe kuu. Wakaona kazi ya ukombozi ilivyotimizwa. Ndipo wakaungana na waliokombolewa katika nyimbo za kusifu.

Juu ya bahari ya kioo iliyochanganyika na moto, likasimama jeshi la washindaji, walipata ushindi juu ya mnyama na sanamu yake, na chapa ya jina lake, na hesabu ya jina lake. Watu mia

moja na arobaini na nne elfu waliokombewa kutoka katika watu. Hao waliimba wimbo mpya, wimbo wa Musa na Mwana Kondoo. Ufunuo 15:2-3. Hakuna wengine, ila ni wale mia na arobaini na nne elfu peke yao, ndio waliweza kuimba wimbo huo maana ni wimbo unaohusu mambo yaliyowapata, ambayo wengine hawakuyapitia. “Hawa ndio wamfuatao mwana Kondoo kila mahali aendako” hawa wamebadilishwa kati ya watu hai, ndio malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana Kondoo. Ufunuo 14:4-5.

Wamepitia wakati wa taabu kuu ambayo ilikuwa haijatokea wamevumilia dhiki ya taabu ya Yakobo; walisimama peke yao bila mtetezi wakati wa mapigo saba ya Mungu. “Wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya mwana Kondoo. Katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa”. “Hawataona njaa kamwe, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.

[316] Kwa maana huyo mwana Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza katika chemichemi ya maji ya uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao”. Ufunuo 7:14; 14:5; 7:16-17.

Waliokombolewa Katika Utukufu

Katika vizazi vyote wateule wa Mwokozi wamekuwa wakitembea katika njia nyembamba. Walitakiwa katika tanuru la mateso. Kwa ajili ya Kristo walivumilia chuki masingizio, masengenyo, kujikana, na machungu mengi. Wamejifunza ubaya wa dhambi, nguvu ya dhambi, na hatia ya dhambi, na matokeo ya dhambi. Wameiona katika hali ya kuichukia. Kuifahamu dhabihu ya Mwokozi kwa ajili yao, kumwafanya kuwa wanyenyekevu na wapole. Wamependa sana kwa sababu wamesamehewa mengi Luka 7:47. Kwa kuwa wamekuwa washiriki wa mateso ya Kristo, wamestahili pia kuwa washiriki wa utukufu wake.

Warithi wa Mungu wanatoka mahali hafifu, vijumba vya ovyo, gerezani, mapangoni, milimani, jangwani mwituni. Ni watu wa dhiki tu daima. Waliteswa wengi walilala makaburini katika hali ya dhiki na fedheha, kwa sababu walikataa kusalimu amri kwa shetani. Sasa hawana dhiki tena wala masumbuko. Hivyo sasa wanasimama katika furaha isiyosemekana, na kuvaa mavazi ya

utukufu. Wanavaa taji tukufu, ambayo kamwe havikuvaliwa na mfalme ye yote duniani. Mfalme wa utukufu amefuta machozi yote katika macho yao. Wanaimba tu nyimbo za kusifu safi na tamu. Mbingu inajaa na nyimbo zikisema “wokovu una Mungu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwanakondoo” na wote wanaitikia wakisema “Amina, Baraka, na utukufu, na hekima na shukrani na heshima, na uwezo na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele” ufunuo 7:10-12.

Katika maisha haya tunaweza tu kuanza kufahamu mpango wa wokovu. Kwa akili yetu ndogo tunaweza kuelewa mambo ya aibu na ya utukufu, uzima na mauti, haki na rehema ambayo hukutania msalabani; lakini kwa ajili ya uhafifu wetu tunashindwa kuelewa mambo yayo hayo katika umuhimu wake. Urefu, na upana na kwenda juu na kina cha upendo wa ukombozi tunavifahamu kidogo sana kigizagiza. Mpango wa wokovu hautafahamika kamili hata kama waliokombolewa watafika huko na kuona mambo waziwazi; na kujua kama wanavyojulikana, lakini kwa maisha ya milele na milele, kweli mpya, mpya zitaendelea kufunuliwa kwa watu wenye mawazo ya utambuzi kamili, ambao watakuwa wakishangaa na kujifunza wakati wote. Ijapokuwa masikitiko na magonjwa na uchovu pamoja na majaribu ya dunia vimekwisha, na laana imeondolewa, watu wa Mungu watakuwa na akili timamu ya kujua kwa kweli kila kilichogharimisha wokovu wao.

[317]

Msalaba ndio utakuwa kiini cha elimu ya kujifunza na wimbo wa kuimba milele na milele zote. Katika Kristo mwenye utukufu, watamwona jinsi alivyosulubishwa. Kamwe haitasahauliwa kuwa mkuu wa utukufu mbinguni alijinyenyekeza ili kusudi apate kuwainua walioanguka dhambini. Kwamba alichukua maovu na masikitiko yote, na uso wa Baba yake alificha usimwelekee Yesu, na ole wa ulimwengu mzima ukamkalia mpaka roho yake ikavunjika na kufa. Mwumbaji wa ulimwengu aliacha tukufu wake ili kumwokoza mpotevu. Upendo huu wa Yesu kwa binadamu, kamwe hautasahaulika katika malimwengu yote. Mataifa ya waliookoka watakapomwangalia Mwokozi, na kujua kuwa ufalme wake hauna kikomo, basi wanapaza sauti wakimba: “Anayestahili ni Mwanakondoo, aliyechinjwa akatukomboza kwa damu yake, na kutufanya wana wa Mungu”

Siri ya msalaba inafunua siri zote. Itaonekana wazi kuwa mwenyenzi Mungu mwenye hekima yote asingebuni njia nyingine ya kumwokoa mwanadamu isipokuwa ni hiyo ya kujitoa kwa mwana wake. Matokeo ya kujitoa huku ni kujaza watu katika dunia, ambao waishio milele. Hiyo ndiyo thamani ya roho, ambayo ililipiwa gharama hiyo na Baba aliridhika nayo. Na Kristo aonapo matunda ya kafara yake kuu ataridhika.

Wakati sauti ya Mungu itakapofungulia watu wake, kutakuwa na mwamko wa kutisha kwa wale walioshindwa, katika mapambano haya ya maisha. Wakipofushwa na madanganyo ya shetani, matajiri wakijivuna juu ya wale waliokuwa na mali kama zao. Lakini hawakuwajali maskini, wenye njaa, walio uchi, wala hawakutenda matendo ya haki, huruma na upendo. Sasa vitu vyao vyote wamenyag'anywa wameachwa fukara. Wakaangalia kwa hofu kuu uangamivu wa sanamu zao ambavyo walivifanyia miungu yao. Waliuza roho zao katika furaha na anasa za dunia. Maisha yao yamekuwa katika hali ya ufukara. Mali walizochuma katika maisha yote zimeyeyuka kwa kitambo. Matajiri wanaombeza, kwa ajili ya maangamizi ya majumba yao makubwa. Mtawanyiko wa dhahabu na fedha zao. Wana hofu kuangamia na sanamu zao. Waovu wanaomboleza kwa sababu matokeo yamekuwa hivyo, wala hawakutubu.

Mchungaji aliyeacha ukweli ili apendwe na watu anafahamu sasa kuwa mafundisho yake yalikuwa na mvuto mbaya. Kila mstari ulioandikwa na kila neno lililonenwa ambalo liliwafanya watu watulie katika ngome ya uongo, lilikuwa mbegu iliyopandwa, sasa wanaona mavuno yalivyo. Bwana asema “Ole wao wachungaji wanaoharibu kondoo za malisho yangu, na kuwatwawanya . . . Angalieni nitawapatiliza uovu wa matendo yenu.” “Mnemhuzunisha moyo wenye haki ya uongo, ambaye mimi sikumhuzunisha, na kuitia nguvu mikono ya mtu mbaya hata asigeuke na kuiacha njia yake mbaya” Yeremia 23:1-2; Eze.13:22.

Wachungaji wa watu wao wanaona kuwa, kumbe walikuwa wamemwasi Mwenye sheria zote za haki, yaani Mungu. Walipoiacha sheria, wakafungua njia ya maasi yote, mapaka nchi ikawa ziwa la uharibifu. Lugha haitoshi kuelezea hali ya kutamani waovu waliyo nayo ya kupata uzima. Lakini saa wamepoteza milele, uzima wa milele.

Watu wanashitakiana wao kwa wao kwamba wamekoseshwa mpaka wamepotea, lakini wote wakaelekeza matusi yao ya kuwalaani wachungaji ambao wamewakosesha.

[319] Wachungaji ambao walisema maneno laini (Isaya 30:10) ambayo yaliwafanya watu wajiepushe na sheria ya Mungu. Watainuka na kusema “Tumepotea, na ninyi ndio mliotukosesha” Mikono ile iiyokuwa ikiwasifu na kuwatukuza, sasa inawainukia ipate kuwaangamiza. Kila mahali palijaa mapigano na kumwaga damu!

Mwana wa Mungu pamoja na wenyeji wa mbinguni wamekuwa wakipambana na uovu, huku wakiwamulikia, na kuwavuta watu ili watoke katika njia za uovu na kuelekea nuru ya uzima. Na sasa kila mtu ameamua upande wa kusimama. Waovu waliamua kuungana na shetani ili kushindana na Mungu. Kwa hiyo mapambano si ya shetani peke yake, bali ni wanadamu pia. “Bwana anayo mateto pamoja na mataifa”. Yeremia 25:31.

Malaika wa Mauti

Sasa malaika wa mauti anatoka, katika njozi ya Ezekieli aki-fananishwa na watu wenye silaha za kufisha. “Waueni kabisa, mzee, na kijana na msichana na watoto wachanga na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama, tena anzeni katika patakatifu pangu”. Basi wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba “waliodai kuwa waongozi wa watu” Eze. 9:6. Walinzi wa uongo ndio wa kwanza kuanguka. “Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakao duniani, kwa sababu ya uovu wao, ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunuka tena watu wake waliouawa”. “Mashaka makubwa yatokanayo kwa Bwana yatakuwa kati yao, na kila mmoja wao atakamata mkono wa jirani yake, na mkono wake utainuliwa ili kushindana na mkono wa jirani yake” Isaya 26:21; Zekaria 14:12-13.

Mashindano yao ya kinyama, pamoja na mapigo ya Mungu yasiyochanganywa na huruma, wataanguka waovu, makuhani, wakuu, na watu kwa ujumla. “Na waliouawa na Bwana siku ile watakuwako, toka upande mmoja wa dunia na hata upande wa pili”. Yeremia 25:33.

Katika kurudi kwake Kristo, waovu watauawa kwa mng'aro wa utukufu wake. Kristo anachukua watu wake mpaka katika jiji la Mungu. Nchi inabaki tupu bila wakaaji. "Tazama, Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, aifanya ukiwa, aipindua na kuwatawanya wakao ndani yake... Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; maana Bwana amenena neno hilo... Kwa maana wamezi-asi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketee." Isaya [320] 24:1,3,5-6.

Dunia inaonekana kama jangwa. Miji imeharibiwa na tetemeko la nchi, miti imeng'oka, miamba na mawe makubwa yametawanyika kote. Mashindano makubwa yanaonyesha mahali milima ilipokuwa. Misingi yake imetoweka.

Kifungu cha Shetani

Sasa mambo yanayotokea ni yale yaliyokuwa kivuli chake wakati wa huduma ya mwisho wa siku ya upatanisho. Wakati dhambi za Waisraeli zilipohamishwa kutoka patakatifu kwa njia ya sadaka ya mbuzi, yule mbuzi wa Azazeli aliletwa hai mbele ya Bwana. Kuhani mkuu akiungama dhambi zote za watu wote, ziliwekwa juu ya kichwa cha huyo mbuzi wa Azazeli. Mambo ya Walawi 16:21. Hali kadhalika, kazi ya upatanisho ya Kristo katika patakatifu pa mbinguni, itakapokamilika mbele za Mungu, ndipo jeshi la malaika wote na waliokombolewa wote, ambao dhambi zao zote zitawekwa juu ya Shetani kama juu ya mbuzi wa Azazeli. Sasa atatangazwa kuwa mwenye hatia ya dhambi zote alizowafanya watu wazitende. Kama vile mbuzi wa Azazeli alivyopelekwa porini mahali pasipokuwa na watu, hali kadhalika Shetani naye atafungwa katika dunia hii iliyoharibika ambayo ni ukiwa kabisa.

Baada ya kutaja habari za kurudi kwake Kristo, mwandishi wa ufunuo anaendelea asema, "Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu; akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya

mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchach.” Ufunuo 20:1-3.

“Kuzimu” Kunafananishwa na dunia iliyoharibika na kuvurugika. Yeremia akiangalia siku kuu ya Mungu, alisema “Naliangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru. Naliangalia milima, na tazama, inatetemeka, na milima yote inasogea huko na huko. Nikaangalia, na tazama hapakuwa na mtu hata mmoja na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikaangalia, na tazama shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, miji yake yote imebomoka mbele za Bwana, na mbele za hasira yake”. Yeremia 4:23-26.

[321] Hapo ndipo shetani na malaika zake waovu watakapoishi kwa muda wa miaka 1000. Hataruhusiwa kutoka katika dunia zingine kuwajaribu wenyeji wa huko. Hakuna mtu aliyebaki ambaye atajaribu. Amekatwa kabisa na kazi ya udanganyifu ambayo aliipenda sana.

Nabii Isaya akiangalia siku za kushindwa kwa shetani, alisema, “Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi, jinsi ulivyokatwa kabisa, ewe uliyewaangusha mataifa!... Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu... Nitafanana na yeye aliye juu. Lakini utashushwa mpaka kuzimu, mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, watakushangilia sana wakisema, je huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, huyu ndiye aliyetikisa falme aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake, asiyefungua wafungwa wake waende kwao?” Isaya 14:12-17.

Kwa Muda wa miaka 6,000 shetani amewafunga watu wa Mungu katika gereza lake, lakini Kristo amelivunja na kuwafungulia watu wake. Shetani peke yake na malaika zake waovu wataona matokeo ya dhambi. “Wafalme wa dunia, wote wakilala katika utukufu, kila mmoja nyumba yake mwenyewe (kaburi) Bali wewe ume-tupwa mbali na kaburi lako, kama chipukizi lililochukiza kabisa.... Hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi kwa maana umeharibu nchi yako, umewaua watu wako” Isaya 14:18-20.

Kwa muda wa miaka 1000 Shetani ataangalia matokeo ya uasi wake juu ya Mungu. Maumivu yake yatakuwa machungu sana.

Ameachwa atafakari kazi yake ya uasi na matokeo yake, na kufikiri juu ya adhabu atakayopata kama malipo ya kazi yake.

Katika miaka 1000 baina ya ufufuo wa kwanza na wa pili, ndipo adhabu ya waovu itakatwa. Paulo anataja jambo hilo kama hivi, “Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana” Wenye haki wanatawala kama wafalme na makuhani. Yohana naye asema “Niliona viti vya enzi, wakaketi juu yake, wakapewa hukumu. . . . watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu”. Ufunuo 20:4-6.

Wakati huo wenye haki watauhukumu ulimwengu. 1Kor. 6:2. Wakishirikiana na Kristo, watawahukumu waovu, wakiwakatia hukumu kufuatana na matendo ya kila mtu. Mambo yao yote yatakuwa yameandikwa katika kitabu cha mauti.

[322]

Shetani na malaika zake wanahukumiwa na Kristo na watu wake. Paulo anasema, “Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika?” Yuda asema, “Na malaika wasiolinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu” Yuda 6.

Mwisho wa miaka 1000 ufufuo wa pili utatokea. Waovu watafufuka waje mbele za Mungu wapate kupewa hukumu yao kama ilivyoandikwa. Zaburi 149:9. Hivyo basi mwandishi wa ufunuo asema, “Hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu”. Ufunuo 20:5 Isaya naye asema, “Nao watakusanywa pamoja kama vile wakusanywavyo wafungwa katika shimo, nao watafungwa katika gereza; na baada ya siku nyingi watajiliwa”. Isaya 24:22.

42/Amani ya Milele Mwisho wa Mapambano

Mwisho wa miaka 1000 Kristo anarudi duniani akifuatana na waliokombolewa na jeshi la malaika. Anawaita waovu waliokufa waamke ili wapate malipo yao ya ajali. Wanatokea wengi sana wasiohesabika, kama mchanga wa pwani wakiwa na hali zao za maradhi na kifo. Tofauti kubwa na wale waliofufuliwa mara ya kwanza.

Kila jicho linamwalia Mwana wa Mungu jinsi alivyo mtukufu. Waovu wanapaza sauti kwa umoja wakisema, “Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana”. Mathayo 23:39. Hasemi hivyo kwa upendo, ila tu ukweli wa mambo unawalazimisha kusema hivyo bila kutaka. Jinsi waovu walivyokufa wakiwa na hali ya ukafiri, ndivyo watafufuka wakiwa na hali hiyo. Hakuna nafasi ya kurekebisha tabia zao.

Nabii asema, “Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizietuni Nao mlima wa mizeituni utapasuka katikati yake” Zekaria 14:4. Mji wa Yerusalemu unaposhuka chini, kutoka mbinguni, utatua juu ya mahali palipotayarishwa na Kristo pamoja na watu wake na jeshi la malaika, wanaingia mjini.

Wakati shetani alipofungwa asipate mtu wa kudanganya alikuwa katika hali mbaya sana, lakini sasa aonapo waovu wamefufuka jeshi kubwa, matumaini yake yanamrudia. Anakusudia kuendelea na mapambano tu, wala asisalimu amri. Atalipanga jeshi lake vema, maana wote hao ni waasi kama yeye, wako tayari kufanya kama apendavyo. Hajitaji kuwa yeye ni shetani, bali ajitaja kuwa mtawala wa ulimwengu kihalali. Anatumia hila zake ili kuwahadaa. Kwamba ni yeye mrithi wa ufalme ila ananyang’anywa haki yake kwa dhuluma. Anajidai kuwa yeye ni mkombozi, anao uwezo wa kushinda vita, kwamba uwezo wake ndio umewatoa makaburini. Shetani anawatia nguvu wote walio dhaifu, na kuwachochea kwa bidii ili wakauteke mji wa Mungu. Anaona jeshi kubwa la watu waliofufuka na kusema kuwa yeye kama kiongozi wao atashinda na kutwaa enzi yake.

Katika jeshi hilo yamo majitu ya zamani yaliyoishi kabla ya gharika, majitu makubwa yenye akili na uwezo mwingi kimawazo, ambao walikuwa waasi waliosababisha gharika. Pia kulikuwamo na wafalme na majemadari wakuu ambao siku zao hawakushindwa vita kamwe. Watu hawa hawakubadilika, maana katika kifo hakuna kubadilika. Walipofufuka walikuja na hali yao ile ya vita na ukatili.

[324]

Shambulio la Mwisho Juu ya Mungu

Shetani alishauriana na watu hawa hodari. Wakasema kuwa jeshi lililomo mjini ni dogo, ukilinganisha na lao. Kwa hiyo watalishinda tu. Basi mafundi wanaanza kuunda silaha kwa haraka sana. Majemadari wanapanga majeshi katika vikosi vyao.

Mwisho amri ikatolewa ili kushambulia. Jeshi kubwa mno likianza kwenda kusogelea mji wa Mungu. Ni jeshi kubwa mno halijapata kutokea vizazi vyote, halihesabiki. Anatangulia shetani na wafalme na majemadari wanakuja nyuma. Wakasikia katika dunia iliyobomoka bomoka wakiuelekea mji wa Mungu. Yesu akaagiza milango ya mji ifungwe. Na jeshi la shetani lajiweka tayari kuushambulia

Sasa Kristo akaonekana machoni mwa adui zake. Mbali kule mjini, mahali panapong'aa kwa dhahabu na kuna kiti cha enzi. Juu ya kiti hicho ameketi mwana wa Mungu na kumzunguka wako waliokombolewa, raia zake. Utukufu wa Baba unamzunguka mwanawe. Utukufu wake unang'aa ukipenya mjini mpaka nchi yote ikazungukwa.

Karibu na kiti cha enzi wanaketi watu waliokuwa watumishi mashuhuri wa shetani hapo kwanza, ambao walinyakuliwa kama kinga cha moto, na sasa wanamtumikia Kristo kwa uaminifu sana. Baada ya hao wako wale walioishi katika nchi ya maovu, lakini wakaishi maisha safi bila kuambukizwa na maovu hayo. Watu walioshika sheria ya Mungu wakati watu wengine walipoasi. Na watu mamilioni waliouawa kwa ajili ya Yesu, watu wa vizazi vyote. Halafu ndipo linakuja “jeshi kubwa, ambalo hakuna mtu awezaye kuwahesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha Wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao” Matawi ya mitende ni alama ya ushindi. Mavazi meupe ni alama ya haki ya Kristo, ambayo ni yao sasa.

[325]

Katika kundi hilo lote, hakuna hata mtu anayedai kuwa amepata mambo hayo kwa haki yake na wema wake mwenyewe. Hakuna kitu kisemwacho kuhusu dhiki iliyopatikana duniani. Neno kuu lao ni, “Wokovu una Mungu wetu na mwana kondoo”

Waasi watamkiwa Hukumu

Kutawazwa kwa Kristo kunafanyika mbele ya wakaaji wambinguni na wenyeji wa duniani. Na sasa Kristo akikabidhiwa utukufu na nguvu, akiwa ndiye mfalme wa wafalme, awatamkia waovu ambao wameivunja sheria yake na kuwatesa wafuasi wake. “Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vitabu vile, sawasawa na matendo yao”. Ufunuo 20:11-12.

Macho ya Yesu yalipokuwa yakiwatazama waovu wao waliona kukumbuka kila aina ya dhambi waliyotenda maishani mwao. Wanaona mahali miguu yao ilipoteleza na kuacha njia nyofu. Wanaona majaribu yaliyowavuta na kuwaingiza dhambini kwa ajili ya tamaa. Wanaona jinsi walivyowadharau wajumbe wa Mungu pamoja na ujumbe wao. Ugumu wa ukaidi wa mioyo yao uliwazuia wasitubu, vyote vyaonekana kama vieandikwa kwa herufi za moto.

Juu ya kiti cha enzi msalaba ulifunuliwa. Mfululizo wa maono kama picha ya mfululizo ikionyesha anguko la Adamu, na hatua zilizofuata katika mpango wa wokovu kuzaliwa kwa Mwokozi; maisha ya Mwokozi ya hali ya unyenyekevu na kujidhili, ubatizo wake kaitka mto wa Yordani, kuomba na kuanguka kwake jangwani, majaribu yake, huduma yake na huruma kwa wanadamu, ikionyesha mibaraka ya mbingu, kukesha kwake usiku katika kuomba mlimani, matendo yake mema yasiyo na kifani, matendo ya kihaini na usaliti aliyofanyiwa kufuata wema wake. Kuteseka kwake katika Getsemane akiona mzigo wa dhambi za ulimwengu ukimkalia. Kusalitiwa na kukamatwa kwake na kundi la wauaji usiku wa vitisho akiwa mikononi mwa makutano, mfungwa asiyekaidi ameachwa na wanafunzi wake; katika majumba ya hukumu na kwa wakuu katika jumba

la hukumu la Pilato mbele ya mwoga Herode, kutukanwa, kudhihakiwa, kuteshwa kupita kiasi, na mwisho kusulubishwa msalabani. Yote yanaonekana wazi.

Na sasa mbele ya majeshi yanayotetemeka yanafunuliwa maneno ya mwisho, mteswaji mvumilivu akikanyaga njia ya kwenda kalwari. Mfalme wa mbinguni akifa msalabani waandishi na makuhani huku wakimdhihaki. Mavumilivu yake makali wakati akifa. Giza laifunika dunia wakati akikata roho. [326]

Haya yote yalipoonekana shetani na wafuasi wake hawakuwa na la kusema, wala njia ya kujificha wasiyaone. Kila jambo lilimongona sehemu aliyoifanya. Herode aliyechinja watoto wadogo wa Bethlehemu, Herodias mwenye hatia ya damu ya Yohana Mbatizaji, Pilato mwamuzi dhaifu, majeshi yaliyokuwa pale katika kumdhihaki Mwokozi, makundi ya waliopagawa waliopaza sauti zao na kusema, “Damu yake na iwe juu yetu na watoto wetu”. Wote hao walitafuta kutoroka, wasiweze. Wakati huo waliokombolewa, wakizitupa taji zao miguuni pa Mwokozi na kusema “Alikufa kwa ajili yangu”.

Hapo yuko Nero, mkuu wa ukatili, anawaangalia wale aliowatesa katika hali ya unyama, watu hawa wametukuzwa kwa ajabu. Hata mamaye aliyemtia moyo wa ukatili kwa mfano wa mvuto wake, alikuwako akiyaona mazao ya matunda yake ya uasi uliotetemesha dunia.

Mapapa na wakuu wao wapo hapo, waliokuwa wakijidai kuwa wao ndio mawakili wa Mungu duniani ambao walitumia ukatili kwa wana wa Mungu; ukatili wa kila aina; kufunga watu, kupiga kuchoma moto, na mateso ya namna namna. Mapapa waliojivuna majivuno makuu sana kuliko Mungu kiasi cha kutaka kubadili sheria ya Mungu. Sasa wamechelewa kugundua kuwa mwenyezi Mungu siyo wa kudhihakiwa kiasi hicho. Hawana udhuru wo wote sasa. Waasi wote wanashangaa pale kwa kujua kuwa walikuwa wanashindana na Mungu. Hawana la kujitetea. Tamko linatamkwa juu yao kuwa, watapata kifo cha milele kuwa ndiyo malipo yao. Waovu wanaona kuwa hayo ndiyo matunda ya uasi wao. Kwa hiyo wanapaza sauti kwa umoja wakisema, “Tumepotea mambo haya yote tungaliyapata, kama tungalijali maonyo! Tumebadili, furaha, amani, heshima, na uzima badala yake tumepata uharibifu aibu na kifo. Katika maisha yao walitangaza ‘hatumtaki Yesu atutawale’”.

[327]

Shetani Ashindwa

Wakati waovu wakiangalia kutawazwa kwa mwana wa Mungu, waliona katika mikono yake alishika mbao mbili za amri zake ambazo walizidharau, kumbe ndio sheria ya serikali ya Mungu. Walishuhudia ibada ya waliokombolewa, ndipo waovu walisema, “Ni haki na za kweli njia zako, Ee, Bwana Mungu mwenyenzi” Wanasema hivyo huku wakianguka na kusujudu. Ufu. 15:3.

Shetani alichanganyikiwa kiasi cha kufa ganzi. Aliyekuwa kerubi wa kusitiri, alikumbuka alikojikwaa na kuanguka, kutoka mahali pake pa heshima mbinguni. Alimwona malaika mwingine amesimama karibu na Baba, katika cheo alichokuwa nacho shetani. Akajua kuwa kama angalidumu kuwa mwaminifu angalikuwa na cheo chake.

Alikumbuka jinsi alivyokuwa hapo zamani na heshima yake, amani aliyokuwa nayo. Alijikumbusha kazi yake katika ulimwengu na matokeo yake, kuwa ni chuki tu kati yao na uharibifu wa maisha. Akaona kuwa kilichomo ulimwenguni ni vita na kupinduana siku zote ni fujo na ghasia tu kila mahali. Akatafakari jinsi alivyojitahidi kupinga kazi ya Kristo. Alipoona matunda ya juhudi yake akaona kuwa hakuambulia chochote. Tena na tena katika vita vyake na Kristo amekuwa akishindwa kwa kila hatua, na kuombwa asalimu amri.

Kusudi la uasi wake lilikuwa kuonyesha ufanisi wake zaidi ya serikali ya Mungu. Amewashawishi watu majeshi na majeshi kukubaliana naye katika mipango yake. Kwa muda wa miaka maelfu mkuu wa uovu huyu ameeneza uongo wake pote. Sasa wakati ume-fika ambao tabia halisi ya shetani itadhihirika wazi. Katika juhudi yake ya mwisho ya kumwondoa Kristo, kuangamiza watu wake, na kuuteka mji wa Mungu, mdanganyaji mkuu huyu amejidhihirisha kuwa ni mwongo, wala hana uwezo wa kufaulu lo lote kama alivyo-owaahidia wafuasi wake. Watu waliomfuata wanaona kuwa mambo yote, na mipango yake yote imekuwa bure.

Shetani anaona kuwa uasi wake umemwondoa asifae kukaa mbinguni. Alijizoeza kushindana na Mungu; kwa hiyo uzuri wa mbingu ni fahari ya huko, kwake ingekuwa mateso matupu. Anainama chini na kukubali adhabu inayomstahili.

Kila jambo la udanganyifu katika vita yake limedhihirika wazi, na ukweli umeonekana ulivyo. Matokeo ya kuacha sheria ya Mungu yameonekana yalivyo. Historia ya sheria ya Mungu yenye kumletea kila mtu raha na amani, inasimama kwa wote, ikiwa kama mashahidi wa kushuhudia kuwa Mungu anakusudia kuwaletea viumbe wake furaha daima. Viumbe vyote pia, vyenye kumtii na vilivyoasi, pamoja na shetani vinapaza sauti na kusema “ni za haki na za kweli njia zako, Ee Bwana, mfalme wa watakatifu”

[328]

Wakati umefika ambapo Kristo atatukuzwa kupita majina yote. Kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake ya kuwaleta wana na binti katika utukufu, ilimfanya avumilie msalaba. Anawatazama waliokombolewa wakiwa na sura yake mwenyewe. Anaona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika. Isaya 53:11. Mbele ya waliokombolewa na waovu, anatamka, “Tazameni walionunuliwa kwa damu yangu! Kwa ajili yao niliteseka na kufa”

Mwisho Mbaya wa Waovu

Tabia ya Shetani inabaki ile ile bila kubadilika. Anaendelea na uasi wake tu. Wala hakutaka kusalimu amri kwa mfalme wa uzima. Na katika jeshi lake la watu mamilioni, hakuna mwenye imani naye. Waovu bado wangali na chuki kwa Mungu kama shetani alivyowapandia, walakini wanaona kuwa wameambulia ng’anda. “Kwa sababu umejitukuza kama Mungu tazama basi nitawaleta wageni juu yako, taifa la kutisha nao watavuta panga zao juu ya uzuri wako na hekima yako, nao watakuharibu kung’aa kwako. Watakushusha mpaka shimoni... Nitakuharibu, ewe kerubi wa kustriri, katikati ya mawe ya moto... Nitakutupa chini, nitakulaza mbele ya wafalme ili wakuone... Nitakuleta kwenye makapi katika nchi mbele ya wakuonao... utakuwa utisho, wala hutakuwako tena kabisa”. Ezekiel 28:6-8, 16-19. “Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote Awanyeshe wasio haki mtego, moto na kiberiti na upepo wa hari na liwe fungu la kikombe chao” Isaya 34:2; Zaburi 11:6. Moto unashuka kutoka mbinguni. Nchi inavunjika vunjika. Ndimi za moto zinafumuka kutoka katika mashimo yote ya nchi ambayo yamezibuliwa. Miamba yote itawaka moto. “viumbe vya asili vitaunguzwa na kufumuliwa, nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea” 2Pet. 3:10. Uso wa dunia utayeyuka na kuwa kama fungu la takataka, itafanana kama ni

[329]

ziwa la maji linalotokota, katika moto. “Ni siku ya kisasi cha Bwana mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni” Isaya 34:8

Waovu wanaadhibiwa kwa kadiri ya matendo yao. Shetani hataadhibiwa kwa ajili ya uasi wake tu, bali kwa ajili ya dhambi, alizosababisha watu wa Mungu kufanya pia. Kadhalika ndimi za moto waovu wanateketea na kumalizika kabisa, shina na matawi vyote vinaungua kabisa. Shetani ambaye ndiye shina, na wafuasi wake ndio matawi. Adhabu kamili ya kuvunja sheria imelipwa, madai ya haki yametimizwa. Kazi ya shetani ya uharibifu imekwisha, kwa milele. Sasa viumbe wa Mugu wamekombolewa milele kutokana majaribu yake.

Wakati nchi inapochomwa motoni, wenye haki wanakaa salamini mjini kwa Mungu. Mungu anapokuwa kwa waovu, moto ulao, kwa wenye haki ni ngao. Soma Ufunuo 20:6; Zaburi 84:11.

“Nikaona mbingu mpya na nchi mpya, maana mbingu za kwanza na nchi za kwanza zimekwisha kupita” Ufunuo 21:1. Moto utakaowateketeza waovu, utaitikasa nchi. Kila alama ya laana imefutika kabisa. Moto huo hautawaka milele mbele ya waliokombolewa, ambao ni kama kumbukumbu ya dhambi.

Ukumbusho wa Kusulubiwa

Jambo moja tu litabaki ambalo ni ukumbusho wa ukatili uliosababishwa na dhambi, nalo ni alama ya kusulubishwa kwake mwokozi. Mkombozi wetu ataendelea daima kuwa na makovu ya kusulubiwa kwake alama pekee ya ukatili ulioletwa na dhambi. Milele zote makovu ya kalvari yataendelea kung’aa yakionyesha sifa zake na kutangaza uwezo wake.

Kristo aliwahakikishia wanafunzi wake kuwa anakwenda kuwaandalia makao huko mbingu kwa Baba yake. Lugha ya kibinadamu haitoshi kuelezea zawadi watakazopata wenye haki. Zawadi hizo zitajulikana tu na wale watakaoziona. Mawazo hafifu ya kibinadamu hayawezi kuzielewa.

Katika Biblia urithi wa waliookoka unatwa “nchi” Waebrania 11:14-16. Pale mchungaji wa mbinguni atawaongoza watu wake katika malisho mema na kwenye chemichemi za maji ya uzima.

[330] Huko maji hububujika daima, maji maang’avu kama kioo, na kando yake kuna miti inayotupa matawi yake kwenye njia ya waliookoka.

Uwanda mpana unapandia kwenye vilima maridadi kabisa, na vilele vya milima ya Mungu vyenye kupendeza mno. Katika nyanda nzuri hizo, kando ya maji matulivu ndiko wana wa Mungu ambao wamekuwa wasafiri muda mrefu, watatulia na kufurahia maisha ya milele na milele.

“Watajenga nyumba na kuishi ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga na mwingine akakaa, wala hawatapanda na mwingine akala. Maana kama siku za mti ndivyo zitakuwa siku za watu wangu”. “Nyika na ukame patafurahi, jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi”. “Mbwa wa mwitu atakaa pamoja na mwanakondoo, na chui atalala pamoja na wana mbuzi Na mtoto mdogo atawaongoza. Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu”. Isaya 65:2,22; 35:1, 11:6-9.

Huko hakuna magonjwa. Hakuna kilio wala mazishi yoyote. “Wala mauti hayatakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita”. “Wala hapani mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa; watu wakaa humo watasamehewa uovu wao” Ufunuo 21:4; Isaya 33:24.

Hapo kuna Yerusalemu mpya, mji mkuu wa nchi mpya iliyotakaswa. “Mwanga wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri” “Na mataifa watatembea katika nuru yake, na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake” “Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao” Ufunuo 21:11, 24. 3

Katika mji wa Mungu hakutakuwako na usiku. Ufunuo 22:5 Hapatakuwapo na hali yo yote ya wasiwasi. Tutajisikia katika hali ya utulivu daima. Nuru ya jua inapatilizwa na utukufu, na kutoa nuru safi isiyo na ukali wo wote. Nuru yake inazidi nuru ya jua wakati wa aduhuri. Waliokombolewa watatembea katika nuru kamilifu kabisa.

“Sikuona hekalu ndani yake kwa maana Bwana Mungu Mwenyenzi na Mwana Kondoo ndio hekalu lake”. Ufunuo 21:22. Watu wa Mungu watapata bahati ya kuongea na Mungu na Mwana Kondoo. Tutamwona Mungu uso kwa uso, sio kwa fumbo tena.

[331]

Ushindi wa Pendo la Mungu

Hapo pendo la Mungu alilopanda mwenyewe mioyoni mwa watu litakamilika. Ushirikiano na viumbe vitakatifu, na umoja wa haki usio na kasoro, jamii yote ya mbinguni na ya duniani vitadumisha furaha ya milele iliyo kamili. Waefeso. 3:15. Hapo katika mawazo makamilifu tutaona maajabu ya uwezo wa Mungu wa kuumba, na siri za upendo wa ukombozi. Kila kiungo kitakuwa na kuendelea. Maarifa ya kujifunza hayatakua na kikomo. Mambo makuu ya ajabu yatafikiwa na hali ya juu ya mawazo na vifiko vyote vitafikiwa. Hata hivyo kutakuwa na mambo mengi ya ajabu ya kupekua. Kwa milele na milele kutakuwa na mafunzo yasiyo na mwisho wala hakuna kuchoka.

Hazina zote za Mungu zitafunguliwa kwa wana wa Mungu waliokombolewa. Watatembea dunia nyingine bila kuwa na safari za kuchosha. Wana wa nchi hii wataingia katia ulimwengu wa wasiokuwa na dhambi na kushiriki maajabu ya elimu yao isiyokuwa na kasoro, ambayo wao wamekuwa nayo vizazi kwa vizazi.

Wataangalia utukufu wa uumbaji bila kuwa na kiwi machoni. Na jua, nyota na sayari zote zikikizunguka kiti cha enzi.

Kadiri miaka ya milele inavyokwenda, ndivyo ufunuo wa utukufu wa Mungu na Kristo utakavyofunuliwa kwa ajabu. Kwa kadri watu watakavyojifunza tabia ya Mungu ndivyo watazidi kumwabudu na kumpenda. Kadri Yesu anavyowafunulia siri za ukombozi wa vita kuu kati ya wema na ubaya ulivyoletwa na shetani, ndivyo watakavyozidi kumtukuza na kumtumikia, na kumwambia kwa sauti za watu maelfu mara maelfu makumi, “Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari na vitu vyote vilivyo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na yeye Mwana Kondoo hata milele na milele” Ufunuo 5:13

Mapambano makuu yamekoma. Dhambi na wenye dhambi hakuna tena. Ulimwengu mzima sasa umeshafika. Umoja na ushirikiano ulio kamili kabisa umeenea ulimwenguni. Kutoka kwa Muumbaji hufurika uzima, nuru na furaha na kuenea mahali pote. Tangu kwa kitu kidogo mno mpaka kwa kikubwa kilinganacho na ulimwengu mzima, vitu vyote, vilivyo hai na visivyo hai, katika hali yote, hutangaza kuwa Mungu ni pendo.